# Qur'an Tukufu

SWAHILI

# QUR'AN TUKUFU

*Imefasiriwa Na*
Jumbe Omari Jumbe

GOODWORD BOOKS

Tafsiri hii haina haki miliki.

First published 2023

Goodword Books
A-21, Sector 4, NOIDA-201301, Delhi-NCR, India
Tel. +91 120 4131448, Mob. +91-8588822672
email: info@goodwordbooks.com
www.goodwordbooks.com

CPS International
Centre for Peace and Spirituality International
1, Nizamuddin West Market, New Delhi-110013
Mob. +91-9999944119
email: info@cpsglobal.org
www.cpsglobal.org

Center for Peace and Spirituality, USA
2665 Byberry Road, Bensalem, PA 19020, USA
Mob. 617-960-7156
email: kkaleemuddin@gmail.com
www.cpsusa.net

Printed in India

# YALIYOMO

Utangulizi Wa Wachapishaji 7

Utangulizi Wa Mfasiri 19

1. Sura Al- Fatiha (Sura ya Ufunguzi) 23
2. Sura Al-Baqara (Sura ya 'Kisa cha' Ng'ombe) 23
3. Sura Aal-Imran (Sura ya Familia Imran) 66
4. Sura An-Nisaa (Sura ya Wanawake) 90
5. Sura Al-Maida (Sura ya Meza yenye Chakula) 115
6. Sura Al-An'am (Sura ya Wanyama mifugo) 133
7. Sura Al-A'araf (Sura ya Miinuko) 153
8. Sura Al-Anfal (Sura ya Nyara za Vita) 175
9. Sura At-Tawba (Sura ya Toba –au Bara a-Kinga) 184
10. Sura Yunus (Sura ya Yunus 'Jonah') 201
11. Sura Hud (Sura ya 'Nabii' Hud) 213
12. Sura Yusuf (Sura ya 'Nabii' Yusuf/Joseph) 227
13. Sura Ar Ra'd (Sura ya Radi) 239
14. Sura Ibrahim (Sura ya 'Nabii' Ibrahim/Abraham) 245
15. Sura Al-Hijr (Sura ya Njia ya Majabalini) 251
16. Sura An-Nahl (Sura ya 'Mamlaka ya' Nyuki) 257
17. Sura Bani Israil (Sura ya Wana wa Israeli) 270
18. Surah Al-Kahf (Sura ya 'Waliojificha' Pangoni) 281
19. Sura Maryam (Sura ya Maria 'Mama wa Yesu') 292
20. Sura Twaha (Sura ya Twaha) 299
21. Sura Al-Anbiyaa (Sura ya Manabii) 309
22. Sura Al-Hajj (Sura ya Hijja) 318
23. Sura Al-Mu'minun (Sura ya Waumini) 327
24. Sura An-Nur (Sura ya Mwangaza) 334
25. Sura Al-Furqan (Sura ya Upambanuzi) 343
26. Sura Ash-Shu'araa (Sura ya Washairi) 350
27. Surah An-Naml (Sura ya Sungusungu) 359

28. Sura Al-Qasas (Sura ya Matukio) 367
29. Sura Al-A'nkabut (Sura ya Buibui) 377
30. Sura Ar-Rum (Sura kuhusu 'Dola la' Wazungu) 385
31. Sura Luqman (Sura ya Luqman) 390
32. Sura As-Sajda (Sura ya Sujudi) 395
33. Surah Al-Ahzab (Majeshi Washirika) 397
34. Sura As-Sabaa (Mji wa Saba') 407
35. Surah Al-Fatir (Muumbaji wa Mwanzo) 413
36. Sura Yasin (Sura ya Yasin) 419
37. Sura As-Saffat (Malaika Waliojipanga Safu) 424
38. Sura Swad (Sura ya Swad) 431
39. Sura Azzumar (Sura ya Umati) 438
40. Sura Al-Mu'min (Sura ya Muumini au Ghafir) 447
41. Sura Fussilat (Sura ya Kilichoelezewa kwa upana) 456
42. Sura Ash-Shura (Sura ya Mashauriano) 462
43. Sura Az-Zukhruf (Sura kuhusu Mapambo) 468
44. Sura Ad-Dukhaan (Sura ya moshi) 474
45. Sura Al-Jathiya (Sura ya Kupiga Magoti) 477
46. Sura Al-Ahqaf (Sura ya Njia zilizopinda za Jangwani) 480
47. Sura Muhammad (Sura Muhammad) 485
48. Sura Al-Fat'h (Sura Ya Ushindi) 489
49. Sura Al-Hujurat (Sura ya Vyumbani) 493
50. Sura Qaf (Sura ya Qaf) 496
51. Sura Adh-Dhariyat (Sura ya Upepo Unaotawanya) 499
52. Sura At-Tur (Sura ya Mlima Tur) 502
53. Surah Al-Najm (Sura Ya Nyota) 504
54. Sura Al-Qamar (Sura Ya Mwezi) 507
55. Sura Ar-Rahman (Sura Ar-Rahman) 510
56. Sura Al-Waqia (Sura ya Tukio Muhimu) 513
57. Sura Al-Hadid (Sura ya Chuma) 516
58. Sura Al-Mujadila (Sura Ya (kisa cha) Mwanamke Mwenye Madai 521
59. Sura Al-Hashr (Sura ya Mkusanyiko) 525

60. Sura Al-Mumtahana (Sura ya (mwanamke) Kutathminiwa 528
61. Sura As-Saf (Sura ya (umuhimu wa) kupanga safu vitani 531
62. Sura Al-Jum'a (Sura ya (siku ya) Ijumaa) 533
63. Sura Al-Munafiqun (Sura kuhusu Wanafiki) 534
64. Sura Attaghabun (Sura ya faida na hasara ya pamoja) 536
65. Sura At-Talaq (Sura ya Talaka) 538
66. Surah At-Tahrim (Sura ya Kukataza) 540
67. Sura Al-Mulk (Sura ya Ufalme) 542
68. Sura Al-Qalam (Sura Al-Qalam) 545
69. Sura Al-Haqqa (Sura ya Ukweli Halisia) 547
70. Sura Al-Ma'arij (Sura ya Njia za Kupandia Mbinguni) 549
71. Sura Nuh (Sura ya Nuh/Noah) 551
72. Sura Al-Jinn (Sura ya Ma-jinni) 553
73. Sura Al-Muzzamil (Sura ya Mwenye Kujizongazonga Nguo 555
74. Sura Al-Muddathir (Sura ya Mwenye Kujigubika Shuka) 557
75. Sura Al-Qiyama (Sura Ya Kiyama) 559
76. Sura Al-Insan (Sura ya Mwanadamu) 560
77. Sura Al-Mursalat (Sura Ya Pepo Zitumwazo) 562
78. Sura An-Nabai (Sura ya Habari Kuu) 564
79. Sura An-Nazia'tt (Sura ya 'Malaika' Watoao Roho kwa Nguvu 565
80. Sura A'basa (Sura ya Aliyekunja Uso) 567
81. Sura At-Takwir (Sura ya Kukunjwa Jua) 568
82. Sura Al-Infitar (Sura ya Mbingu Kupasuka) 569
83. Sura Al-Mutaffifin (Sura ya Wapunjaji vipimo) 570
84. Sura Al-Inshiqaq (Sura ya Kuchanika Mbingu) 572
85. Sura Al-Buruj (Sura ya Kitita cha Sayari, Zodiaki) 573
86. Sura At-Twariq (Sura ya Mgeni wa Usiku) 574
87. Sura Al-Aa'la (Sura ya Mtukufu zaidi) 575

88. Sura Al-Ghashiya (Sura ya Tukio Lifunikalo Matukio Yote 576
89. Sura Al-Fajr (Sura Al-Fajr) 577
90. Sura Al-Balad (Sura ya Mji) 578
91. Sura As-Shams (Sura ya Jua) 579
92. Sura Al-Layl (Sura ya Usiku) 579
93. Sura Ad-Dhuha (Sura ya Mwangaza wa Asubuhi) 580
94. Sura Al-Inshirah (Sura ya Kukunjuliwa Kifua) 581
95. Sura At-Tin (Sura ya Tin) 581
96. Surat Al-Alaq (Sura ya Kipande cha damu kining'inizi) 582
97. Sura Al-Qadr (Usiku wa Heshima) 583
98. Sura Al-Bayyina (Sura ya Hoja ya Wazi) 583
99. Sura Al-Zilzal (Sura yaTetemeko la Ardhi) 584
100. Sura Al-A'diyat (Sura ya Farasi Watokao mbio) 585
101. Sura Al-Qari'a (Sura ya (Siku ya) Kelele na Ghasia/Kiyama) 585
102. Sura At-Takathur (Sura ya (wenye) kulimbikiza utajiri) 586
103. Sura Al-A'sr (Sura ya Wakati Kupitia Zama na Zama) 586
104. Sura Al-Humaza (Sura ya m-mbea) 587
105. Sura Al-Fil (Sura ya (kisa cha) Ndovu) 587
106. Sura Quraysh (Sura ya watu wa kabila la Quraysh) 588
107. Sura Al-Mau'n (Sura ya Kuzuia Msaada) 588
108. Sura Al-Kawthar (Sura ya Kheri Nyingi) 589
109. Sura Al-Kafirun (Sura ya Wanamkana Mungu) 589
110. Sura An-Nasr (Sura ya Ushindi) 590
111. Sura Al-Masad (Sura ya Ndifu) 590
112. Sura Al-Ikhlas (Sura ya Uhalisia wa Imani) 591
113. Sura Al-Falaq (Sura ya Mapambazuko) 591
114. Sura An-Nas (Sura ya Wanadamu) 591
References (Vitabu Vya Marejeo) 592

# UTANGULIZI WA WACHAPISHAJI

Quran ni Kitabu kitokacho kwa Mwenyezi Mungu. Kimehifadhiwa kwa ukamilifu kwa wakati wote ujao.

Ingawa hapo awali Qur'an iliandikwa kwa Kiarabu, baadaye imeweza kufahamiwa hata na wale wasiojua Kiarabu, kutokana na juhud za wafasiri. Pamoja na kuwa tafsiri haina uwezo wa kuwakilisha kila kitu kilichomo kwenye Qur'an asilia, hata hivyo tafsiri imesaidia sana kueneza neno hili la Mwenyezi Mungu mbali zaidi ya watu wanaozungumza Kiarabu, kwa wigo mpana zaidi.

Ingawa Quran inaonekana iko katika lugha ya Kiarabu, lakini kwa kweli, iko katika lugha ya maumbile, ambayo ni lugha ambayo Mwenyezi Mungu alizungumza na wanadamu wote moja kwa moja wakati alipowaumba. Mazungumzo haya ya Dhati Tukufu na binadamu yamo ndani ya roho ya kila binadamu. Ndiyo maana Quran inaeleweka na wote - wengine kwa ufahamu wa wazi, na wengine kwa akili ya ufahamu (subconscious). Ukweli huu umeelezewa katika Qur'ani kama 'ufunuo ulio wazi katika mioyo ya wale waliopewa maarifa.' Aya hii inaendelea kusema kwamba 'hakuna anayekataa Ishara zetu isipokuwa walio wahalifu' (29: 49). Hii inamaanisha kuwa Ukweli huu, ulioelezewa na Qur'an, unaofahamiwa na mwanadamu kwa akili yake aliyonayo, ulikuwepo kabla, na aliufahamu katika hatua ya akili ya ufahamu (subconscious level) kabla ya kuzaliwa.

Kwa sababu hiyo basi, Ujumbe wa Quran sio jambo geni kwa mwanadamu. Kwa kweli ni kiasi cha kuweka wazi kwa matamshi na maneno tu, lakini ujumbe wenyewe ni ule ule

wa Mwenyezi Mungu ambao binadamu alikwisha ujua; unaokwenda sambamba na tabia asilia ya binadamu.

Quran inalielezea hili kwa kusema kuwa wale waliozaliwa baadaye walikuwa tayari roho zao zimekwishaumbwa wakati wa kuumbwa kwa Adam, na wakati ule Mwenyezi Mungu alikuwa amezungumza moja kwa moja na roho hizi zote za wanadamu. Tukio hili limetajwa katika Quran: "[Wakumbushe ewe Mtume], wakati Mola wako Mlezi alipotoa watoto kutoka katika migongo ya Wana wa Adam na kuwafanya washuhudie. Akawauliza, ' Je! Mimi sio Mola wenu?' Wakajibu, 'Ndio, tunashuhudia kwamba Wewe ni Mola wetu. Hii ni kwa ajili msije mkasema Siku ya Kiyama, ' Hatukujua hili '(7: 172). Katika aya ifuatayo, Qur'an inataja zaidi mazungumzo hayo ya Mwenyezi Mungu na mwanadamu: 'Hakika Sisi tulizipendekezea mbingu, ardhi na milima kuchukua amana hii, lakini vyote vikakataa kuichukua na vikaiogopa, lakini mwanadamu akajitwika. Hakika yeye daima si mwadilifu, na mjinga!'(33:72). Qur'an imejulikana kwa mwanadamu tangu azali, na si kitu kigeni kabisa. Kwa kweli, Quran ni ufumbuo wa akili ya mwanadamu. Mtu ambaye amehifadhi umbile la tabia asilia ambalo halikuchafuliwa na mwingilio wa mafunzo hasi, anaposoma Qur'an, seli za ubongo wake zilizohifadhi ujumbe asilia wa Mwenyezi Mungu, zinaamshwa upya. Tukizingatia hili, haitakuwa vigumu kufahamu kwamba tafsiri ya Qur'an ni njia muwafaka ya kuifahamu tu. Iwapo yale mazungumzo ya mwanzo ya Mwenyezi Mungu yalikuwa ni Agano Lake la Kwanza, basi Quran ni Agano la Pili. Kila mmoja anashuhudia ukweli wa mwenzake. Ikiwa mtu ana uelewa mdogo, au hajui lugha ya Kiarabu, akasoma tafsiri ya Qur'an

pekee...asifazaike kuwa atashindwa kufahamu Qur'an, kwa sababu dhana ya Qur'an kuwa mwanadamu ndiye mpokeaji wa asili wa neno la Mwenyezi Mungu imethibiti kabisa katika zama hizi za sasa. Sayansi ya Kanuni za Maumbile (Genetic Code) uvumbuzi wa anthropolojia zote zinaunga mkono maoni haya kikamilifu.

*Shabaha Ya Uumbaji Wa Mungu*

Kila kitabu kina lengo. Madhumuni ya Qur'ani ni kumjulisha mwanadamu shabaha ya Uumbaji wa Mungu. Hiyo ni, kumwambia mwanadamu kwanini Mungu aliumba ulimwengu huu; kusudi gani la kumweka mwanadamu duniani; kile kinachotakikana kutoka kwa mwanadamu katika kipindi chake cha maisha kabla ya kifo, na kile atakachokabiliana nacho baada ya kifo.

Mtu huzaliwa kama kiumbe wa milele. Wakati Mungu alimuumba mwanadamu aligawanya muda wa maisha yake katika vipindi viwili, kipindi cha kabla ya kifo, ambacho ni wakati wa majaribio, na kipindi cha baada ya kifo, ambao ni wakati wa kupokea malipo mema au adhabu anayostahili kwa mujibu wa matendo ya mtu wakati wa maisha yake ya duniani.

Hii huchukua sura ya Paradiso ya milele au Jehanamu ya milele pia. Madhumuni ya Quran ni kumfanya mwanadamu atambue ukweli huu. Hii ndio mada ya Kitabu hiki Kitakatifu ambacho hutumika kumwongoza mwanadamu katika safari yake yote kupitia maisha ya hapa hadi maisha ya baadaye. Itakuwa sahihi kusema kwamba mtu anazaliwa akiwa mtafutaji. Maswali haya yafuatayo yako katika akili ya kila mtu: mimi ni nani? Ni nini madhumuni ya maisha yangu?

Na je, nini ukweli wa maisha na kifo? Je, ni siri gani ya kufaulu na kufeli kwa mwanadamu? Nk. Kwa mujibu wa Quran, jibu la maswali haya ni kwamba dunia ni uwanja wa majaribio, na chochote kile mwanadamu anachopewa katika kipindi chake cha kabla ya kifo, yote ni sehemu ya mtihani. Akhera ni mahali ambapo matokeo ya mtihani yatazingatiwa na Mwenyezi Mungu, na kila mtu atapokea aidha malipo maridhia au adhabu, sawa sawa na matendo yake katika ulimwengu huu. Siri ya mafanikio ya mwanadamu katika maisha haya ni kuelewa shabaha ya uumbaji wa Mwenyezi Mungu na kupanga maisha yake ipasavyo.

### *Kitabu Cha Onyo La Mwenyezi Mungu*

Quran ni kitabu cha onyo la Mungu. Mchanganyiko wa mafunzo na mawaidha. Inaweza kuitwa kwa usahihi zaidi, 'kitabu cha hekima'. Quran haifuati mfumo wa kitabu cha darasa za mafundisho. Kwa kweli, wakati msomaji wa kawaida anachukua Quran, inaonekana kwake kuwa ni mkusanyiko wa vipande vipande vya taarifa. Lakini hivi sivyo ilivyo katika uhalisia. Mpangilio huu wa Qur'an hautokani na kasoro yoyote, bali ni kwa kufuata mpango maalum wa Qur'an wa kubakiza umbo lake la asili ili kutimiza kusudi lake la kufikisha ujumbe wa ukweli kwa msomaji ambaye, wakati anapitia-pitia maandiko, huenda akawa na wakati wa kusoma ukurasa mmoja tu, mstari mmoja au kifungu kimoja tu kwa wakati mmoja. Jambo moja muhimu la Quran ni kwamba ni ujumbena ukumbusho wa baraka zilizotolewa na Mhisani Mkuu. La muhimu zaidi kati ya hizi ni sifa za uwezo wa kipekee ambazo Mwenyezi Mungu amempa mwanadamu wakati alipomuumba. Baraka nyingine kubwa ni kwamba

alimleta hapa duniani, sayari ambayo ina kila aina ya mifumo ya msaada kwa faida yake. Madhumuni ya Qur'an ni kuhakikisha kwamba, wakati mwanadamu anafurahia baraka hizi za maumbile, atamuweka Mhisani wake akilini kwa kumkumbuka; lazima atambue hiba nyingi za bure ambazo Muumba wake amemzawadia. Ni kwa kufanya hivyo mtu huyo atazawadiwa kwa kuingia katika Pepo ya milele. Kumpuuza Mfadhili wake, kwa upande mwingine, kutamsababishia mwanadamu moja kwa moja kwenda mahali pabaya pa milele. Kwa kweli Quran ni ukumbusho wa kweli wa jambo hili usioweza kuepukwa.

*Dhati Ya Roho Na Utambuzi Wa Mwenyezi Mungu*

Sifa moja muhimu ya Quran ni kwamba inatupa kanuni za msingi tu. Kutokana na muhimu wake, mara nyingi Qur'an huzirudia rudia kanuni hizo za msingi ili kuzisisitiza. Kinyume chake, yale yasiyo ya msingi, au mambo yanayohusiana na muundo tu, hayo huchukua sehemu ndogo ya maandiko. Huu ndiyo mpango wa Qur'an; kwamba mambo yanayohusu muundo huchukua nafasi ya pili.

Dhana ya Quran ni kuwa kanuni zilizo muhimu zaidi ni zile ambazo ni mwongozo wa kimsingi. Kipengele hiki cha Qur'an kiko dhahiri sana, kiasi kwamba msomaji hawezi kukipita bila ya kushangaa. Ukweli ni kwamba dhati ya roho (internal spirit) ni ya umuhimu mkubwa katika ujenzi wa utambulisho wa Kiislamu. Mara tu dhati ya roho ikitengenezwa, ni rahisi kwa mfumo sahihi kufuatia. Lakini mfumo peke yake hauwezi kamwe kuzaa dhati ya roho. Ndio maana lengo la Quran ni kuanzisha na kuleta mapinduzi ya kielimu ndani ya mwanadamu. Maneno yaliyotumiwa na

Quran kwa mapinduzi haya ya kielimu ni ma'rifah (kutambua ukweli) (5:83). Quran inasisitiza umuhimu wa mwanadamu kugundua mwenyewe ukweli katika kiwango cha utambuzi. Katika kiwango hicho, ndipo mtu hufikia Imani ya kweli ya Mwenyezi Mungu . Endapo hakuna utambuzi wa Mwenyezi Mungu, basi hakuna imani.

*Neno La Mungu*

Unaposoma Qur'an, utaona mara kwa mara imeelezwa kuwa ni neno la Mungu. Huu kwa dhahiri ni ukweli ulio wazi. Lakini unapotazama kwa undani zaidi na kulingana na muktadha huu, kauli hiyo ni taarifa isiyo ya kawaida. Kwa sababu kuna vitabu vingi ulimwenguni ambavyo vinaaminika kuwa vitakatifu. Lakini, isipokuwa kwa Quran, hatupati kitabu chochote cha kidini ambacho kinadai kuwa ni Kitabu kutoka kwa Mungu. Aina hii ya taarifa, inayoonekana kipekee katika Quran, inampa msomaji mahali pa kuanzia. Kwa hiyo, ataisoma kama kitabu cha kipekee, badala ya kama kitabu cha kawaida kilichoandikwa na mwanadamu. Tunakuta mara kwa mara katika Qur'an maneno kama haya : 'Ewe mwanadamu! Huyu ni Mola wako Mlezi anayesema nawe. Sikiza maneno Yake na uyafuate'. Namna hii ya kuzungumza na msomaji ni ya kipekee kabisa, na haipatikani katika kitabu kingine chochote isipokuwa Qur'an pekee. Inamwacha msomaji abakie na hisia ya kudumu. Anahisi Mola wake Mlezi anamzungumza naye moja kwa moja. Hisia hii inamfanya msomaji kuchukua matamshi ya Quran kwa umakini uliokithiri, badala ya kuyachukulia kama taarifa za kila siku katika kitabu cha kawaida. Mtindo wa ukusanyaji wa Quran pia ni wa kipekee.

Vitabu vilivyoandikwa na wanadamu kawaida hupangiliwa kwa mpangilio kutoka A hadi Z, kulingana na mada. Lakini Quran haifuati mpangilio wa aina hii. Kwa mtu wa kawaida huonekana kana kwamba Qur'an haina utaratibu au mpangilio. Lakini kwa hakika ni kitabu chenye mshikamano na mpangilio mzuri mno na bora; wenye mtindo wa kiuandishi wenye shani.

Wakati tunasoma Qur'an, tunahisi mwandishi wake yuko mahali palipo juu sana, na kutoka huko Yeye anaangalia chini akihutubia wanadamu wote, ambao ndiyo anaowajali sana. Anayahutubia makundi makundi mbalimbali ya wanadamu, lakini hotuba hiyo wakati huo huo inawahusu wote.

Jambo moja maalum la Quran ni kwamba wakati wowote msomaji wake anaweza kushauriana na mwandishi wake, akauliza maswali yake na kupokea majibu, kwani mwandishi wa Quran ni Mwenyezi Mungu mwenyewe. Yeye ni Mungu aliye hai. Kama muumba wa mwanadamu, Yeye husikia moja kwa moja na kujibu maombi ya mwanadamu.

### *Mapambano Ya Itikadi Kwa Njia Ya Amani*

Wale ambao wanatambulishwa Qur'ani kwa kupitia vyombo vya habari pekee, kwa jumla wana maoni kwamba Quran ni kitabu cha jihadi. Na jihadi kwao ni jaribio la kufikia lengo la mtu kwa kutumia nguvu na vurugu. Lakini wazo hili linatokana na kutoelewa. Mtu yeyote anayejisomea mwenyewe Quran atatambua mara moja kuwa ujumbe wake hauhusiani kamwe na utumiaji nguvu. Quran, kuanzia mwanzo hadi mwisho, ni kitabu kinachohubiri amani na haikivumilii utumiaji nguvu wa njia yeyote ile. Ni kweli kwamba jihadi ni mojawapo ya mafundisho ya Quran.

Lakini jihadi, ikichukuliwa kwa maana yake sahihi, ni jina la mapambano ya amani, badala ya aina yoyote ya vitendo vya utumiaji nguvu wa kiholela. Dhana ya jihadi katika Qur'an imeelezewa katika aya ifuatayo, 'Pigana jihadi kubwa kwa msaada wa hii Qur'an (25:52)'.

Ni dhahiri kabisa kuwa Qur'an siyo silaha, bali ni kitabu ambacho kinatupa muhtasari wa itikadi ya mapambano ya amani. Mbinu ya mapambano kama hayo, kulingana na Qur'an, ni 'kusema nao neno la kufikia roho zao' (4:63). Kwa hivyo, njia inayotakikana, kulingana na Qur'an, ni ile inayoathiri moyo na akili ya mwanadamu. Inamaanisha kwamba katika kuzihutubia akili za watu, Qur'an inawaridhisha na inawahakikishia ukweli wake. Kwa kifupi, inaleta mapinduzi ya kiakili ndani yao. Hii ndio dhamira ya Qur'an. Na kazi hii inaweza kufanywa tu kwa njia ya hoja za busara. Lengo hili haliwezi kufikiwa kwa njia ya utumiaji nguvu au hatua za kijeshi.

Ni kweli kwamba kuna aya fulani katika Quran, ambazo zinawasilisha maagizo yanayofanana na yafuatayo, 'Waueni popote mtakapowapata' (2: 191). Kuna wale wanaozitaja Aya hizo na kutoa maoni kwamba Uislamu ni dini ya vita, ilhali Aya hizi zinazungumzia tukio au matukio maalum, ambapo Waislamu wamevamiwa na majeshi yaliyoshirikiana, na mara nyingi ni baada ya watu hao kufanya mauaji na kuvunja makubaliano na Waisalamu ya kutopigana vita.

Aya hiyo hapo juu haitoi amri ya jumla ya Uislamu. Ukweli wa mambo ni kwamba Quran haikuteremshwa kama kitabu kamili tulichonacho leo, bali iliteremshwa mara kwa mara na vipande vipande kuzungumzia matukio, mazingira yaliyokuwepo. Hilo lilichukua muda wa miaka 23.

Tukiigawa miaka hiyo 23 kati ya miaka ya amani na miaka ya vita, utaona miaka ya amani ilikuwa miaka 20, wakati ile ambayo kulikuwa na vita ni miaka mitatu pekee.

Ufunuo wa Qur'an katika kipindi hiki cha miaka 20 ya amani ulikuwa ni mafundisho ya amani ; kama unavyofafanuliwa katika Aya zinazohusu utambuzi wa Mungu, ibada, maadili, haki, n.k. Mgawanyiko huu wa amri katika vikundi tofauti ni wa asili na hupatikana katika vitabu vyote vya dini. Kwa mfano, Gita, kitabu kitakatifu cha Wahindu, kinahusu hekima na maadili. Walakini pamoja na hayo kuna mahimizo ya Krishna kwa Arjuna, kumtia moyo kupigana (Bhagavad Gita, 3:30). Hii haimaanishi kwamba waumini wa Gita wanapaswa kupigana vita kila wakati. Mahatma Gandhi, baada ya yote, alipata falsafa yake ya kutokuwa na utumiaji nguvu kutoka kwa Gita huyo huyo. Ushauri wa kupigana vita katika Gita unatumika tu kwa hali za kipekee ambapo hakuna namna ya kuepuka vita. Lakini kwa maisha ya kawaida ya kila siku inatoa amri sawa za amani kama ilivyofahamiwa na Mahatma Gandhi.

Vivyo hivyo, Yesu Kristo alisema, 'Msidhani kwamba nilikuja kuleta amani Duniani. Sikuja kuleta amani, bali upanga. '(Mathayo, 10:34). Haitakuwa sawa kabisa kusema kwamba dini iliyohubiriwa na Yesu Kristo ilikuwa ya vita na utumiaji nguvu, kwani matamshi kama hayo yanahusiana na hali fulani tu. Isipokuwa kwa ujumla, Yesu Kristo alifundisha maadili ya amani, kama vile kujenga tabia nzuri, kupendana, kusaidia maskini na wahitaji, n.k.

Ndivyo ilivyo pia kwa Qur'an. Wakati Mtume Muhammad alipohama kutoka Makka kwenda Madina, makabila yaliyoabudu masanamu yalikuwa na jeuri kwake. Lakini

Mtume daima aliepuka kuwashambulia, na alikuwa na subira,

uvumilivu na mkakati wa kuwakwepa. Walakini katika hali nyingine hakukuwa na chaguo jingine, isipokuwa kujitetea tu. Ndipo ikabidi apigane mara kadhaa. Ni katika hali hizi ndipo ufunuzi wa Aya hizo za vita zilipoteremshwa kuzungumzia hali iliyopo.

Amri hizi, zikiwa maalum kwa hali fulani, hazikuwa za matumizi ya jumla, siku zote. Hazikuwa na maana ya kuwa halali kwa wakati wote. Ndiyo maana hadhi ya kudumu ya Mtume imetajwa kama ‘huruma kwa wanadamu wote.’ (21: 107) Uislamu ni dini ya amani kwa maana kamili ya neno hilo. Quran inaiita njia yake kuwa ‘njia za amani’ (5:16). Inaelezea upatanisho kama ‘sera bora’ (4: 128), na inasema kwamba Mwenyezi Mungu anachukia ‘uharibifu wowote wa amani’ (2: 205). Tunaweza kusema bila ya kutia chumvi kwamba Uislamu na utumiaji nguvu ni vitu viwili tofauti kabisa.

## *Kitabu Kilichofunuliwa*

Quran ni kitabu cha Mwenyezi Mungu kilichofunuliwa kwa Nabii Muhammad kidogo kidogo kwa muda wa miaka 23.

Sehemu ya kwanza ilifunuliwa mnamo 610 AD, wakati Mtume Muhammad alipokuwa akiishi Makka. Baadaye, sehemu tofauti za Qur’an ziliendelea kufunuliwa mara kwa mara, sehemu ya mwisho ilifunuliwa mnamo 632 AD, wakati Mtume alikuwa akiishi Madinah.

Kuna sura 114 katika Quran, ndefu na fupi. Aya zake ni takriban 6600. Ili kukidhi mahitaji ya kisomo, Quran

iligawanywa katika Juzu 30. Juzu hizi ziliwekwa kwa utaratibu maalum kupitia mwongozo wa Malaika Jibril, ambaye Mwenyezi Mungu alimtuma kufikisha ujumbe wa Qur'an kwa Mtume Muhammad (SAAW). Wakati Quran ikifunuliwa katika robo ya kwanza ya karne ya 7, karatasi tayari ilikuwa imegunduliwa. Karatasi hii, iliyojulikana kama papyrus, ilitengenezwa kwa mikono kutokana na nyuzi za mmea fulani uotao kando ya mto. Wakati wowote ule sehemu yoyote ya Qur'an ilipofunuliwa, iliandikwa kwenye papyrus. Wakati wa mchakato huu, watu walihifadhi Aya hizo kwenye kumbukumbu zao. Quran wakati huo ilikuwa ndiyo fasihi pekee ya Kiislam ambayo ilisomwa katika Swala, na pia kusomwa kwa madhumuni ya Da'wah. Kwa njia hii, Quran iliendelea kuhifadhiwa katika nyoyo kwa wakati mmoja na pia kuandikwa. Njia hii ya kuhifadhi iliendelea wakati wa uhai wa Mtume Muhammad.

Khalifa wa tatu, 'Uthman ibn' Affan, alikuwa ameandaa nakala kadhaa. Alizipeleka katika miji tofauti, ambapo zilihifadhiwa katika misikiti mikubwa. Watu hawakusoma tu kutoka kwenye nakala hizi, lakini pia walitoa nakala zaidi. Uandishi wa Quran kwa mikono uliendelea mpaka mashine ya uchapishaji ilipobuniwa na karatasi ikaanza kutengenezwa kwa idadi kubwa, hongera kwa mapinduzi ya viwanda. Kisha, Quran ilianza kuchapishwa. Mbinu za uchapishaji ziliendelea kuboreshwa na kwa hivyo uchapishaji wa Quran pia uliboreshwa. Sasa kuona nakala zilizochapishwa za Quran limekuwa jambo la kawaida sana, kiasi kwamba zinaweza kupatikana katika kila nyumba, msikiti, maktaba na duka la vitabu.

Leo hii mtu yeyote anaweza kupata nakala nzuri ya Quran, popote alipo, katika sehemu yoyote ya ulimwengu.

*Namna Ya Kusoma Qur'an*

Quran inasema, 'Soma Quran taratibu na kwa uwazi.' (73: 4) Hii inamaanisha, soma Quran kwa sauti taratibu, iliyopimwa. Inamaanisha soma ukizingatia kabisa maana ya yaliyomo. Inaposomwa namna hii, kunakuwa na aina ya mungano ya njia mbili kati ya Quran na msomaji wake. Kwa msomaji, Quran ni kana kwamba Mwenyezi Mungu anazungumza naye, na hapo moyo wake unaanza kujibu kwa kila Aya. Pale ambapo neema na baraka za Mwenyezi Mungu zinatajwa, moyo wa msomaji hufurika kwa shukrani. Waama pale ambapo makaripio na adhabu ya Mwenyezi Mungu itajwapo, moyo wake hutetemeka. Na ambapo amri ya Mwenyezi Mungu inatajwa, hisia inajengeka ndani ya msomaji kwamba anapaswa kuwa mtiifu kwa Mola wake kwa kutekeleza agizo hilo.

Maulana Wahiduddin Khan
New Delhi
www.mwkhan.com

# Utangulizi Wa Mfasiri

Bismillahi ar Rahmaani ar Raheem

Kwa wazungumzao Kiswahili kama lugha ya mama au lugha ya kwanza, kama vile wakazi wa pwani ya mwambao wa Afrika Mashariki, hii hawataiita tafsiri, bali wataielezea kuwa ni tarjuma ya Qur'an Tukufu.

Wao wana uwezo wa kutofautisha baina ya tafsiri na tarjuma. Kwamba ya kwanza inamaanisha sherehe, maelezo ya kina au udadavuzi wa maneno ya Qur'an na yanavyofahamiwa na ulama, wakati ile ya pili ni kuweka neno la Kiswahili mukabala wa aya ya Qur'an; bila kuzama katika fahiwa ya aya na jinsi inavyofahamiwa na wanazuoni mbali mbali wa Kiislamu.

Hivyo kuiita kwangu hii 'tafsiri' ni kwa istiara tu, na kuwasaidia wale wanaotumia Kiswahili kama 'lingua franca' ambao ndiyo wengi miongoni mwa wazungumzao Kiswahili.

Huu ni uamuzi wa makusudi, ili tafsiri hii iwe marejeo ya upesi ya maana ya maneno ya Qur'an, na pia kumpa fursa na uhuru msomaji atakaye kuelewa undani wa maana hiyo, aende akatafute kwa mwanazuoni yeyote atayemwamini kwa kumpa maelezo hayo ya ziada.

Sababu nyingine ni kuifanya tafsiri hii iweze kufikiwa na watu wa aina mbali mbali na wenye madhehebu tofauti ya dini, falsafa na hata wale ambao watataka kuisoma kwa udadisi tu.

Shabaha yangu ni kuifanya tafsiri hii iwe rahisi kwa kila mtu, na kuepukana na sera za wana taaluma ya Kiislamu na elimu za Kiarabu, ambao mara nyingi wanakitoa muhanga Kiswahili ili kufuata utaratibu wa nahau na istilahi za lugha ya Kiarabu.

Mimi naamini Kiswahili ni lugha inayojitegemea na ina mfumo wake ambao pindi unapokorofishwa inakuwa vigumu

kwa mzungumzaji wa Kiswahili kufahamu fahiwa, hasa hasa katika zama hizi ambapo wazungumzaji wengi wa Kiswahili hawana upeo mrefu wa msamiati au mawako ya lugha hiyo, na mbinu nyingi za Kiswahili zimepotea.

Utaona kuwa tafsiri hii haina mukabala wake wa Qur'an iliyoandikwa Kiarabu. Hii pia ni kwa kusudi la kuifanya isomwe na kila mtu na iwezekane hata kuwekwa hotelini.

Mtu huenda akauliza, mbona zipo tafsiri nyingi za Qur'an kwa Kiswahili? Kuna haja gani ya tafsiri mpya?

Ni kweli kabisa. Maktaba ya Kiswahili siku hizi ni tajiri sana katika upande huu. Nakumbuka miaka ya sabini wakati tafsiri ya kwanza ya Kiswahili ilipotoka, ya Sheikh Abdullah Saleh Al Farsi, jinsi ilivyokuwa ndiyo marejeo pekee ya sisi maamuma kujua maana ya Qur'an. Si hivyo siku hizi! Leo hii kuna tafsiri si chini ya kumi za Wafasiri mbali mbali wa lugha ya Kiswahili. Kwa mantiki hiyo, ni kweli kuwa isingekuwa na maana sana kuongeza tafsiri nyingine.

Isipokuwa Qur'an si kitabu kama vitabu vingine! Qur'an ina uwezo wa kutoa maana mpya ya aya zake, kadri ufahamu wa watu unavyozidi kuongezeka katika elimu mbali mbali za sayansi au za kiroho.

Mfano mdogo tu ni huu: kwa muda mrefu wafasiri walikuwa wakistaajabu kwamba katika kuzungumzia nyumba ya buibui kuwa ni dhaifu mno, ( Sura Al-ankabut 21: 41), Qur'an ilitumia kiwakilishi nomino (pronoun) cha mwanamke; ingawaje katika lugha ya Kiarabu tamko 'buibui' ni la kiume…

Siku hizi tunajua, baada ya sayansi kugundua, sababu hasa ya kutumia neno la kike ni kwa vile anayejenga nyumba ya buibui si mwingine isipokuwa buibui mwanamke, ambaye yeye pekee ndiye mwenye 'utomvu' wa kujengea!

Tafsiri yangu hii, fauka ya nilivyosema hapo juu, pia nimekusudia kuleta dhana mbadala ya baadhi ya mafahamio

ya Qur'an; kitabu hiki cha ajabu ambacho kila wakati msomaji anapokifunua kwa kukisoma kwa kutadaburi, hugundua kitu kipya.

Mfano mdogo tu ni neno 'Azwaaaj' linalofasiriwa 'wake' kama katika Sura Az Zukhruf aya 70, '(Wataambiwa): ingieni peponi nyie na wake zenu mkifurahia' Tafsiri za Qurtubi, Tabari na Ibn Kathir, zikinukuliwa na tafsiri kadhaa za Kiswahili zimefasiri hivyo. Miye nimeonelea badala ya 'wake' niseme 'wenza'. Kwa vile wote, waume na wake wanaweza kuwa sababu ya wenza wao kuingia peponi, na si waume pekee wanaohutubiwa, isipokuwa tu mara nyingi Qur'an hutumia tamko la kiume kutokana na mazoea ya Waarabu. Zaidi ya hayo, neno lenyewe 'azwaaj' kwa kweli linaweza kumaanisha 'wake au waume' katika Kiarabu. Unaona kwamba kulifasiri "wenza" ni kwenda na wakati, na kutasaidia kudhibiti tuhuma kuwa Uislamu unawapendelea wanaume.

Maendeleo makubwa katika elimu za kompyuta , sayansi, hasa katika kanuni za maumbile (genetic code) na asidi nasaba (DNA), na yaliyogunduliwa kutokana na safari za safina za anga za nje….yametoa upeo mpya wa ufahamu wa aya za Qur'an ambazo hapo nyuma zilikuwa zachukuliwa kufahamisha mambo yaliyojulikana mintarafu ya wigo mfupi wa maisha ya watu.

Ni kwa sababu hizi na nyingine, kuna haja kila mara kufasiri kitabu hiki cha ajabu ili kuendelea kuthibitisha ukweli wake.

Nimejaribu kiasi cha uwezo kwenda na wakati, kama wasemavyo.

Labuda pia nieleze kuwa sisi wafasiri wa zama hizi tuna bahati kubwa kuliko wenzetu waliotutangulia. Hivi sasa, kutokana na maendeleo ya tarakilishi, mfasiri huweza kutazama jinsi aya ilivyoelezewa na wafasiri wengine kumi au zaidi, katika lugha mbali mbali, akachagua rai muwafaka

zaidi. Hayo anaweza kuyafanya kwa dakika chache tu kwa kuperuzi mtandao au mitandao maalum. Kwa mfasiri aliyeishi miaka kumi tu iliyopita, kazi hiyo ingemchukua miezi kadhaa na uwezo mkubwa wa kukusanya vitabu na mijalada mbali mbali!

'Al Kamaalu Li Llahi'. Ndivyo tusemavyo Waislamu, kwamba hakuna asiye na makosa isipokuwa Mwenyezi Mungu pekee. Yeye ndiye mwenye ukamilifu wote. Mapungufu yote utakayoyakuta wewe msomaji ni yangu binafsi. Hivyo nitashukuru sana ukinitumia barua-pepe: tubalayya@gmail.com kunielezea, ili tuweze kusahihisha katika matoleo yajayo.

Itakuwa ni utovu wa kurudisha fadhila kama sitawashukuru wengi walioshiriki hadi kuifanya tafsiri hii iwafikie wasomaji. Miongoni mwa wote ni rafiki yangu kipenzi, hayati Alhajj Hassan Ali Mwalupa, aliyetenga wakati wake kwa kuipitia na kunielekeza katika mengi. Sheikh Hassan pia ni askari bobea (veteran) wa Tarjuma na Tafsiri ya Qur'an.

Bila kumsahau mke wangu mpenzi aliyenivumilia mno wakati mrefu wa kazi hii, bi Fatma K. Ngalaa. Allah ampe kheri za dunia na akhera.

Hatimaye, ni mtu ambaye bila yeye fikra nzima ya tafsiri ya Qur'an isingekuwepo, angalau kwa wakati huu. Huyu ni ndugu Hasanain Jethabhai, aliyekuwa kila mara akifuatilia maendeleo ya tafsiri hii na kuwasiliana na wahisani waliojitolea kuichapisha.

Nawashukuru wote walioniomba, kunihimiza na kuchukua dhima ya kuichapisha tafsiri hii na kuieneza.

Mwenyezi Mungu awajazi ridhaa yake na Mabustani ya neema.

Jumbe Omari Jumbe
Grong, Norway
18 Januari , 2021

1. Sura Al- Fatiha

## SURA YA UFUNGUZI

1 Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

2 Sifa njema zinamstahiki Allah, Mola Mlezi wa viumbe
wote 3 Mwingi wa rehema, mwenye kurehemu 4 Mfalme
wa siku ya malipo 5 Wewe pekee tunaukuabudu, na wewe
pekee tunakuomba msaada…6 Utuongoze njia iliyonyooka
7 Njia ya wale uliowapa neema, na siyo waliokasirikiwa,
wala waliopotea.

2. Sura Al-Baqara

## SURA YA ‘KISA CHA’ NG’OMBE

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 *Alif Laam Miim:* (Mwenyezi Mungu pekee ndiye ajuaye
maana yake; katika hii na nyingine zinazoaza hivi).

2 Hiki ni kitabu kisicho na shaka ndani yake, ni mwongozo
kwa wanaomtii na kumuenzi Mwenyezi Mungu. 3 Wale
wanaoamini (japokuwa) wasiyoyaona kwa macho yao,
hudumu kuswali na wakatoa baadhi ya vile tulivyowapa.
4 Na ni wale wanaoamini ujumbe ulioletwa kwako
(Muhammad), na ulioletwa (kwa mitume wengine) kabla
yako, na wana yakini juu ya Akhera. 5 Hao ndiyo wanaofuata

mwongozo kutoka kwa Mola wao mlezi, na hao ndiyo
waliofaulu.

6 Ama wale waliokana, ni sawa sawa kwao ikiwa
umewaonya au hukuwaonya, hawataamini. 7 Mwenyezi
Mungu amezipiga muhuri nyoyo zao na masikio yao
[wasiamini], na kuna pazia mbele ya macho yao. Na
inawangojea adhabu kubwa.

8. Kuna baadhi ya watu husema, 'tumemwamini Mwenyezi
Mungu na Siku ya mwisho' lakini (ndani ya nyoyo zao) si
waumini. 9. (Hudhani) wanamhadaa Mwenyezi Mungu na
wale walioamini, lakini hawatambui kuwa ni wao wenyewe tu
ndiyo wanaojidanganya. 10. Ndani ya nyoyo zao mna maradhi,
na Mwenyezi Mungu akawazidishia maradhi mengine. Na
Inawangoja adhabu chungu (kwa kutokuwa wakweli na nafsi
zao). 11. Na waambiwapo msifanye uharibifu duniani, wao
husema, 'sisi ni waleta maendeleo'. 12. Kwa hakika wao ndiyo
waharibifu wakubwa ila hawatambui. 13. Wanapoambiwa:basi
kuweni waumini kama watu wengine, husema, 'ati sisi tuamini
kama walivyoamini wale wapumbavu?!' Kwa hakika wao
ndiyo wapumbavu lakini hawajitambui. 14. Na wanapokutana
na wale walioamini husema, 'na sisi pia tumeamini', lakini
wanapokwenda chemba na waovu wenzao huwaambia: 'ah,
sisi kwa kweli tuko pamoja nanyi, sisi twawachezea akili tu
wale.' 15. Mwenyezi Mungu atawarudishia wenyewe mchezo
wao huo, na awaache katika upotofu wao wakitangatanga.
16. Hao ndiyo waliochagua upotofu badala ya uongofu; ila
biashara yao hii haina faida, na wamepoteza dira.

17. Mfano wao ni kama wale waliowasha moto (ili
uwaangazie njia). Ulipoangazia sehemu za kando kando
yao, (ghafla) Mwenyezi Mungu akauzima mwanga wao na

akawaacha katika giza nene, hawaoni. 18. Wasiweze kusikia, wasiweze kusema, wasiweze kuona. Wao hawawezi tena kurudi katika njia (iliyonyooka). 19. Au ni kama (mfano) wa mvua kubwa kutoka mawinguni, yenye kiza kikuu, radi na umeme, wakawa wanatia vidole vyao katika masikio yao kujikinga na miungurumo ya radi wakiogopa kifo. Na Mwenyezi Mungu amewazunguka kwa kuwajua vilivyo hao wanaomkana. 20. (Mwangaza wa) umeme unakaribia kupofua macho yao. Unapowamulika wao huutumia kwa kutembelea, na unapozimika, husimama wima pale walipo. Na laiti Mwenyezi Mungu angependa, angewafanya wasisikie wala wasione. Hakika Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kila kitu.

21. Enyi watu! Mwabuduni Mola wenu Mlezi, aliyewaumba ninyi na wale waliokuwepo kabla yenu, ili muweze kumtii vyema na kumuenzi. 22. Ambaye ameifanya ardhi kuwa kama tandiko kwenu, na mbigu kama paa, na akashusha mvua kutoka mawinguni, na kwa sababu yake akaotesha matunda yakawa ni chakula chenu. Basi msimfanyie Mwennyezi Mungu washirika na hali nyie mnajua (kuwa hanao). 23. Ikiwa mna shaka na yale tuliyomteremshia mja wetu (Muhammad), basi leteni angalau Sura moja inayofanana na (hii) Qur'an, na waiteni mashahidi na wasaidizi wenu badala ya Mwenyezi Mungu, ikiwa ninyi mnasema kweli. 24. Msipofanya - na wala kamwe hamtaweza kufanya- basi uogopeni moto ambao kuni zake ni watu na mawe, ulioandaliwa wale wanaomkana Mwenyezi Mungu. 25. Na wape habari njema wale walioamini na wakafanya mambo mema, kwamba watahodhi Bustani ambazo mito (ya maji, maziwa na asali) hupita chini yake. Kila wanapopewa matunda humo kuwa chakula chao, husema, 'haya ndiyo yale yale tuliyopewa hapo mwanzo',

ilihali wameletewa yakiwa yamefanana. Pia humo watakuwa na wenza walio wasafi na wataishi humo milele.

26. Hakika Mwenyezi Mungu haoni haya kutoa mfano wowote; mbu au zaidi ya mbu. Ama walioamini wataelewa kuwa mfano huo ni kweli kutoka kwa Mola wao Mlezi. Lakini waliomkana Mwenyezi Mungu watasema, 'nini amekusudia Mwenyezi Mungu kwa mfano huu?' Mwenyezi Mungu huwaachia wengi wakapotea kwa mfano huo, na wengi akawaongoza. Lakini hatamwacha yeyote apotee kwa mfano huo isipokuwa wale ambao tayari wametoka kwenye utiifu (wa Mwenyezi Mungu). 27. (Hao ni) Wale wanaovunja ahadi (yao) kwa Mweneyezi Mungu baada ya kuikubali, na wakavunja (udugu) ambao Mwenyezi Mungu ameamrisha uunganishwe na wakafanya maovu duniani. Hao wamejiharibia wenyewe.[1] 28Vipi mnamkana Mwenyezi Mungu ilihali mlikuwa wafu, akawaleta kwenye uhai, kisha atawafanya mfe tena na kisha atawafufua, kisha mrudishwe kwake? 29 Yeye ndiye aliyewaumbia vyote vilivyomo ardhini, tena akakusudia kuumba mbingu na akaziumba kwa ustadi mbingu saba, na Yeye hujua kila kitu.

30. Kumbuka wakati Mola wako Mlezi alipowaambia Malaika, 'Mimi nitamweka naibu wangu duniani'. (Malaika) wakasema, 'utamweka ardhini kiumbe atakayeharibu na kumwaga damu huko, ingawaje sisi tunakutakasa kwa sifa

1. Imani ya Kiislamu ni kuwa binadamu wote, wakiwa katika ulimwengu wa roho, kabla ya kuubwa kuwa watu, walikubali ahadi au agano na Mwenyezi Mungu kuwa Yeye pekee ndiye watakayemkubali kuwa Bwana wao Mlezi. Ni agano hili ndilo linalozungumziwa.

zako na kukutukuza? (Mwenyezi Mungu) Akasema, ‘Hakika mimi najua msiyoyajua’.

31.Na akamfundisha Adam majina ya vitu vyote, kisha akavileta mbele ya Malaika na akasema, ‘niambieni majina ya vitu hivi ikiwa ninyi mnasema kweli’. 32. Wakajibu, ‘utakatifu ni Wako! Hatujui isipokuwa kile ulichotufundisha. Wewe ndiye mwenye kujua zaidi na mwenye hekima kuu’. 33. ( Mwenyezi Mungu) Akasema: ewe Adam! waambie hao majina ya vitu hivyo. Alipokwisha waambia majina ya vitu hivyo, akawaambia, ‘jee, sikuwaambia ninyi kuwa Mimi ninajua siri zote za mbinguni na ardhini, na ninayajua mnayoyaweka wazi na yale mliyokuwa mnayaficha’?.

34. Na wakumbushe watu pale tulipowaambia Malaika ‘inameni kumpa heshima Adam’. Wote waliinama chini isipokuwa Ibilisi. Yeye alikataa kwa majivuno. (tangu hapo) Akawa katika wale waliomkana Mwenyezi Mungu. 35. Ndipo Tukasema, ‘Ewe Adam, kaa wewe na mkeo Peponi. Kuleni humo kwa raha mustarehe (chochote na) popote mpendapo, ila tu msiukaribie mti huu; msije mkawa katika wale waliozidhuru roho zao (kwa kuasi amri hii)’. 36. Lakini Shetani (Ibilisi) akawatia mtegoni na akawatoa katika hali ya neema waliyokuwemo. Tukawaambia, ‘Tokeni humo mkiwa maadui nyie kwa nyie! (tokea sasa) Ardhi ndiyo yatakuwa maskani yenu na mahali pa kustarehe kwa muda’. 37.Kisha Adam akapokea maneno fulani kutoka kwa Mola wake mlezi (ya kumfundisha kuungama, akayasema), akamsamehe. Hakika Yeye ni mwingi wa kusamehe, mwingi wa huruma. 38. Tukasema, ‘Tokeni humo nyote!’. Pindi uongozi utokao kwangu utakapowafikia, wale watakaoufuata uongozi huo, haitakuwa hofu juu yao wala hawatahuzunika. 39.Waama

wale watakaomkana Mwenyezi Mungu na wakaona ishara
zetu ni uongo, hao ndiyo watu wa motoni, watakaa humo
milele.
40. Enyi wana Israeli! Ikumbukeni neema yangu niliyowapa,
na tekelezeni ahadi yangu, nami nitatekeleza ahadi yangu
kwenu, na msiwogope yeyote ila Mimi tu. 41. Na muamini
kile nilichokishusha kinachothibitisha kile mlichonacho,
na msiwe wa mwanzo kukikakana. Wala msitake kubadili
maneno yangu kwa thamani ndogo (ya dunia), na nitiini
na kunienzi Mimi pekee. 42. Wala msichanganye ukweli na
uongo, mkaficha ukweli nanyi mwajua. 43. Na dumisheni
kuswali na toeni zaka; na mrukuu pamoja na wanaorukuu.
44. Hivi (inakuaje) kwamba mnawaamrisha watu kufanya
yaliyo mema na huku mnajisahau nyie wenyewe, hali
mnasoma kitabu! Kweli hamfahamu? 45. Na ombeni msaada
(wa Mwenyezi Mungu) kwa kusubiri na kuswali. Hilo ni
jambo gumu isipokuwa kwa wanyenyekevu… 46. Hao ni wale
ambao wana uhakika wa kukutana na Mola wao Mlezi, na
kwamba watarejea kwake.
47. Enyi wana Israeli! Ikumbukeni neema yangu niliyowapa,
na kwamba Mimi niliwapa kipa umbele juu ya walimwengu
wengine. 48. Na iogopeni siku ambayo nafsi haitoifaa nafsi
nyingine kwa lolote, wala hayatakubaliwa maombezi, wala
haitapokewa fidia ya kuikomboa, na kamwe hawatasaidiwa.
49. Na kumbukeni pale tulipowaokoa kutoka kwa watu wa
Firauni (Pharaoh) waliokuwa wakiwapa adhabu kali kabisa;
kwa kuwachinja wana wenu wa kiume na kuwaacha hai wana
wenu wa kike. Hayo yalikuwa majaribu makubwa kwenu
aliyowajaribu Mola wenu Mlezi. 50. Na pale tulipoipasua
bahari (ya Sham) kwa ajili yenu, tukawaokoa nyie na

tukawazamisha watu wa Firauni na huku nyie mkiangalia. 51.Na pale tulipomuahidi Musa (kwamba tungempa Torati baada ya kufunga) siku arobaini. Lakini baadaye mkamfanya ndama kuwa Mungu wenu, na mkawa watu waovu kabisa. 52.Lakini tukawasamehe baada ya hayo yote, ili mshukuru. 53.Na pale tulipompa Musa kitabu cha kubainisha kweli na batili, ili mpate kuongoka. 54.Na kumbukeni pale Musa alipowaambia watu wake "hakika ninyi mmezidhulumu roho zenu kwa kumfanya ndama kuwa mungu wenu. Kwa hiyo ungamaneni kwa Mola wenu Mwumba, kwa kujiuwa (wale wakosaji). Hilo ni bora kwenu mbele ya Mola wenu Mwumba". Ndipo akawasamehe, kwani Yeye ni mwingi wa msamaha, mwenye huruma nyingi. 55.Na kumbukeni pale mliposema, 'Ewe Musa! Sisi hatutakuamini hadi tumwone Mungu waziwazi'. Ikawaangamizeni radi kutoka mbiguni na huku mnaangalia. 56.Kisha tukawafufueni baada ya kifo chenu, hivi kwamba mpate kushukuru. 57.Tukawafunika kwa kiwingu (ili msiungue kwa joto la jangwani mlipotoka Misri kwenda Syria), tukawashushia Manna na ndege wa Kwale. Kuleni katika hivi vitu vizuri tulivyowaruzuku. Nao hawakutudhulumu sisi(walipopinga amri zetu), isipokuwa wamejidhulumu wenyewe.

58.Na kumbukeni tulipowaambia, ingieni katika mji huu, na kuleni kwa raha mustarehe chochote mkitakacho humo, na ingieni kwa unyenyekevu kwa kupitia lango lake, mseme 'Hittah', (tusamehe makossa yetu). Tutawasamehe makosa yenu na tutawazidishia (mgao) wale wafanyao wema. 59. Lakini waovu wakabadili maneno kinyume cha yale waliyoambiwa (wakasema 'Hintah' lete ngano!), tukawashushia hao waliodhulumu giza kutoka mbinguni

kwa sababu ya utovu wao wa utiifu. 60.Na kumbukeni wakati
Musa alipowaombea maji watu wake . Tukamwambia, lipige
jiwe ( hili) kwa fimbo yako! Mara zikabubujika kutoka
kwenye jiwe hilo chemi chemi kumi na mbili. Kila kabila
likajua mahali pake pa kunywea. (tukawaambia) kuleni,
kunyweni hiyo riziki ya Mwenyezi Mungu, na msiasi na
kufanya uharibifu duniani. 61.Na kumbukeni mlipomwambia
Musa, Ewe Musa! Sisi hatuwezi kuvumilia kula chakula cha
aina moja! Tuombee kwa Mola wako Mlezi atutolee vile
vinavyooteshwa na ardhi: kama mboga, matango, ngano,
adesi na vitunguu. Akasema, hivi kweli mnataka kubadili kile
kilicho bora kwa kilicho duni? Haya, ingieni mjini. Humo
mtapata mvitakavyo. Wakagubikwa na unyonge na shida. Na
wakastahiki hasira ya Mwenyezi Mungu. Hilo ni kwa vile
walikuwa wakikana ishara za Mwenyezi Mungu na wakawa
wanawaua mitume wa Mwenyezi Mungu bila uadilifu, na
hiyo ni kwa vile walivyoasi na kuendelea na uadui.

62.Hakika wale walioamini Qur’an, na Wayahudi,
na Wakristo na Wasaabia…yoyote miongoni mwao
aliyemwamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho na
akafanya mema, watapokea malipo yao kutoka kwa Mola
wao Mlezi, na wala hawatakuwa na hofu wala huzuni.

63.Kumbukeni (enyi Waisraeli) pale tulipokubali Agano
lenu na tukaliinua jabali la Tur juu yenu,( tukawaambieni)
fuateni kwa umadhubuti haya tuliyowapa na daima kumbukeni
yaliyomo, ili mpate kumtii na kumuenzi Mwenyezi Mungu.
64. Lakini mkageuka baada yake. Na lau si fadhila na huruma
za Mwenyezi Mungu kwenu, mngekuwa katika wale
waliopata hasara. 65.Hakika mmejua (yaliyowafika) wale
waliokhalifu amri ya (kutofanya kazi) siku ya Jumamosi.

Tuliwaambia 'geukeni muwe manyani wanyonge'. [66.] Kwa hivyo tukayafanya hayo kuwa onyo kwa waliokuwa katika zama zao na waliokuja baada yao, na fundisho kwa wanaomtii na kumuenzi Mwenyezi Mungu.

[67.] Na pale Musa alipowaambia watu wake: Hakika Mwenyezi Mungu anawaamrisha mumchinje ng'ombe (yeyote yule). Wakasema: Ebo! Unatufanya sisi watu wa mzaha? Akasema: Najikinga kwa Mwenyezi Mungu nisiwe miongoni mwa wasiojua wakisemacho. [68.] Wakasema: 'Tuombee Mola wako Mlezi atufafanulie ni ng'ombe gani huyo?' Akasema: Yeye anasema kwamba ng'ombe huyo si mzee wala si ndama, bali wa rika la kati kati. Haya sasa fanyeni mnavyoamrishwa. [69.] Wakasema: 'Tuombee Mola wako Mlezi atufafanulie rangi yake ni ipi?' Akasema: Yeye anasema ng'ombe huyo ni wa manjano, wa rangi iliyokoza mno, huwapendeza wanaomtazama. [70.] Wakasema: 'Tuombee Mola wako Mlezi atufafanulie ni yupi huyo? Kwetu sisi ng'ombe wote wanafanana, na sisi tunaomba mwongozo, apendapo Mwenyezi Mungu.' [71.] Akasema: 'Yeye anasema kuwa huyo si ng'ombe anayefanyishwa kazi ya kulima ardhi, wala kutilia maji mimea, mwenye afya timamu na wala hana aibu yeyote. Wakasema: 'Sasa umeleta ukweli!'. Wakamchinja (na kumtoa kafara). Lakini walikaribia wasifanye hivyo. [72.]Na kumbukeni mlipomwua mtu kisha mkazozana (nani aliyefanya hivyo). Lakini Mwenyezi Mungu akayafichua mliyokuwa mkiyaficha. [73.] Tukasema: Ipigeni (maiti ya mtu huyo) kwa minofu ya ng'ombe huyo (wa kafara). Na ndiyo kama hivyo Mwenyezi Mungu atawafufua wafu; na anawaonesha ishara zake ili mpate kufahamu.

[74.] Kisha nyoyo zenu zikawa ngumu baada ya hayo,

zikawa kama mwamba wa jiwe, au ngumu zaidi. Kwa vile katika miamba kuna ile inayobubujika maji, na kuna mingine inayopasuka yakatoka maji ndani yake, na mingine huanguka kwa sababu ya kumtii Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu si Mwenye kughafilika na myafanyayo.

75. Je, mna matumaini ya kwamba watawaamini nyie na
ilihali baadhi yao walikuwa wakisikia maneno ya Mwenyezi
Mungu, kisha wanayabadili baada ya kuwa wameyafahamu,
na haku wanajua? 76. Na wanapokutana na wale walioamini
husema: 'nasi tumeamini!'. Na wanapokuwa faragha peke
yao, wao kwa wao, husema: 'mbona mnawaambia yale
Mwenyezi Mungu aliyoyateremsha kwenu, ili wayatumie
katika kuhojiana nanyi mbele ya Mola wenu? Hivi hamjui
(nia yao)'? 77. Hawajui kwamba Mwenyezi Mungu anayajua
wanayoyayafanya siri na wanayoyaweka wazi?

78. Na miongoni mwao wako wasiojua kusoma; hawakijui
Kitabu ila (huona humo) matamanio yao tu. Hawana lolote
isipokuwa kudhani-dhani tu! 79. Ole wao wanaoandika
kitabu kwa mikono yao, kisha wakasema, 'hiki chatoka
kwa Mwenyezi Mungu!'. Ili wachukue thamani duni ya
duniani. Ole wao kwa yale iliyoyaandika mikono yao. Na
ole wao kwa yale wanayoyachuma. 80. Na walisema: 'sisi
moto hautatugusa kamwe isipokuwa kwa siku chache tu'.
Sema: Je, mmepata ahadi kwa Mwenyezi Mungu juu ya
hilo, kwa hivyo Mwenyezi Mungu hatavunja ahadi Yake,
au mnamsingizia Mwenyezi Mungu mambo msiyoyajua?
81 Naam! Anayechuma ubaya, na mabaya yake yakamzonga,
hao ndio watu wa Motoni, humo watadumu. 82 Na wale
walioamini na wakafanya mema, hao ndio watu wa Peponi,
humo watadumu.

83. Na kumbukeni pale tulipofanya Agano na wana wa Israeli: kwamba hamtamwabudu yeyote ila Mwenyezi Mungu, na muwatendee wema wazazi na jamaa na mayatima na maskini; na mseme na watu (wote) vizuri, na mdumu kuswali na mtoe Zaka. Lakini mligeuka isipokuwa wachache tu katika nyinyi, na mkawa mnapuuza.

84. Na kumbukeni tulipofanya Agano nanyi (kuwa) hamtamwaga damu zenu, wala hamtatoana majumbani mwenu, mkakubali, nanyi mnashuhudia. 85. Kisha nyinyi hao hao mnauwana , na mnawatoa baadhi yenu majumbani mwao, mkisaidiana dhidi yao kwa (njia ya) dhambi na uadui. Na wakiwajia kama mateka mnachukua fidia na hali mmekatazwa kukombolewa. Je mnaamini baadhi ya Kitabu na kukataa baadhi nyingine? Basi malipo pekee kwa mwenye kufanya hivyo miongoni mwenu ni fedheha katika maisha ya hapa duniani, na Siku ya Kiyama watapelekwa kwenye adhabu kali. Na Mwenyezi Mungu si Mwenye kughafilika na yale mnayoyafanya. 86. Hao ndio walionunua uhai wa duniani (wa kupita) kwa Akhera (wa kudumu); kwa hivyo hawatapunguziwa adhabu wala hawataokolewa.

87. Na hakika tulimpa Musa (Moses) Kitabu na tukawafuatisha baada yake mitume wengine. Na tukampa Isa (Yesu), mwana wa Maria, hoja zilizo wazi, na tukamtia nguvu kwa Roho Mtakatifu. Kila alipowafikieni mtume na ambayo hamyapendi mlipanda kiburi; wengine mkawakana na wengine mkawaua. 88. Na husema: ‘Nyoyo zetu ni vifuniko!’ (vya kuhifadhia maneno ya Mungu). Bali Mwenyezi Mungu amewalaani kwa kufuru zao; kwa hivyo ni kidogo tu wanayoyaamini.

89. Na kilipowafikia Kitabu kitokacho kwa Mwenyezi

Mungu kinachothibitisha waliyonayo, na hali hapo zamani walikuwa wakiomba ushindi dhidi ya mapagani (wa Kiarabu), lakini yalipowafikia yale waliyoyajua, waliyakataa. Hivyo laana ya Mwenyezi Mungu iko juu ya wasiokuwa na imani ya Mwenyezi Mungu. 90. Kibaya zaidi walichokiuzia roho zao, ni kule kukataa kwao alichokiteremsha Mwenyezi Mungu, kwa sababu tu ya kuona wivu kuwa (iweje) Mwenyezi Mungu amteremshie fadhila zake (mtu) amtakaye katika waja wake! Ndipo wamejitakia wenyewe hasira juu ya hasira. Na wasiomwamini Mwenyezi Mungu watapata mateso ya kudhalilisha.

91. Na wakiambiwa: 'Yaaminini aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu'. Husema: 'Tunaamini yale tuliyoteremshiwa sisi tu', na huyakana yasiyokuwa hayo, na ilihali yote ni ukweli unaothibitisha hayo yao. Waambie: 'mbona mliwaua manabii wa Mwenyezi Mungu hapo zamani ikiwa kweli mlikuwa waumini'? 92. Na Musa aliwajia na hoja zilizo wazi wazi, hata hivyo, mkamgeuza ndama kuwa mungu wenu baada yake, na matendo yenu yakawa maovu kabisa.
93. Na kumbukeni tulipofanya Agano nanyi na tukaliinua jabali la mlima (Sinai) juu yenu: (tukawaambia): 'shikeni kwa madhubuti haya tuliyowapa, na sikieni'. Wakasema: Tumesikia na tumekataa! Wakanyweshwa nyoyoni mwao (imani ya) ndama kwa sababu ya kufuru yao. Sema: Ni kiovu mno hicho kilichowaamrisha imani yenu (kufanya)! Ikiwa kweli mna imani yoyote! 94. Sema: Ikiwa nyumba ya Akhera iliyoko kwa Mwenyezi Mungu ni yenu ninyi tu pasi na watu wengine…. basi si mtamani kufa, ikiwa ninyi mnasema kweli? 95.Na kamwe hawatayatamani mauti, kwa sababu ya yale iliyokwisha yatanguliza mikono yao. Na Mwenyezi

Mungu anawajua vyema watu waovu. [96.] Na Utawaona wao ndiyo wana pupa zaidi ya kutaka kuishi kuliko watu wengine, na hata kuliko mapagani wa Kiarabu. Kila mmoja katika wao anapenda laiti angelipewa umri wa miaka elfu moja! Lakini hilo haliwezi kumwondoshea adhabu; na Mwenyezi Mungu anayaona wanayoyafanya.

[97.] Sema: Yeyot anayemfanyia uadui Jibrili (anajisumbua). Sababu yeye ndiye ameishusha (Qur’an) moyoni mwako kwa ruhusa ya Mwenyezi Mungu, kwa kuthibitisha yale yaliyokuwa kabla yake, na ni uongofu na bishara njema kwa waumini. [98.] Anayemfanyia uadui Mwenyezi Mungu na malaika Wake na mitume Wake na Jibrili na Mikaili, basi Mwenyezi Mungu ni adui wa makafiri. [99.] Na hakika tumekuteremshia Aya zilizo wazi; na hakuna wanaozikataa isipokuwa wapotofu.. [100.] Hivi ati kila wanakubali Agano huwapo kikundi miongoni mwao kikalivunja? Hapana! Wengi wao tu hawaamini. [101.] Na alipowajia Mtume kutoka kwa Mwenyezi Mungu, mwenye kuthibitisha yale waliyo nayo, kundi moja miongoni mwa wale waliopewa Kitabu, lilikitupa Kitabu hicho cha Mwenyezi Mungu nyuma ya migongo yao, kana kwamba hawajui.

[102.] Wakafuata yale waliyoyafichua mashetani (kwa uongo) juu ya nguvu na uweza wa Suleiman (Solomon). Wala Suleiman hakumkana Mwenyezi Mungu, bali mashetani ndio waliomkana; kwa kuwafundisha watu uchawi na yaliyoteremshwa kwa Malaika wawili, Harut na Marut, katika (mji wa) Babylon. Lakini wawili hawa hawakumfundisha yeyote mpaka wamwambie:’sisi ni majaribu’. Basi usimkane Mwenyezi Mungu. Wakajifunza kwao mambo ya kumtenganisha mtu na mkewe. Wala hawawezi kumdhuru

mtu kwa uchawi huo ila kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Na wakajifunza yatakayowadhuru wala hayawanufaishi. Na kwa hakika wanajua kwamba anayenunua uchawi hatakuwa na fungu lolote la furaha huko Akhera. Na hakika ni kiovu mno hicho walichobadilishana na roho zao, laiti wangejua.
103. Na lau wangeamini na kujikinga na uovu, basi malipo yatokayo kwa Mwenyezi Mungu yangekuwa bora kwao, laiti wangelijua.

104. Enyi walioamini! Msiseme (maneno ndumi la kuwili, kama) ‘Raa’ina’ bali semeni (maneno yenye maana nyoofu, kama) ‘Undhurnaa’. Na sikieni! Kwa wale wanaomkana Mwenyezi Mungu inawangojea adhabu chungu.[2]
105 Waliomkana Mwenyezi Mungu miongoni mwa watu wa Kitabu na mapagani wa Kiarabu, hawapendi mteremshiwe kheri yeyote kutoka kwa Mola wenu. Ilihali Mwenyezi Mungu humchangua ampendaye kumpa rehema zake. Na Mwenyezi Mungu ana hazina kubwa ya rehema.
106 Aya yoyote tunayoifuta (hukumu yake) au kuisahaulisha, tunaleta iliyo bora kuliko hiyo, au iliyo mfano wake. Hujui kwamba Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kila kitu?
107 Hujui kwamba Mwenyezi Mungu ni Wake Yeye Ufalme wa mbingu na ardhi? Nanyi hamna mlizi wala msaidizi asiyekuwa Mwenyezi Mungu?
108 Au mnataka kumwuliza Mtume wenu kama alivyoulizwa Musa zamani? Na anayebadilisha imani kwa ukafiri, basi hakika amepotea njia iliyo sawa.

2. Maneno yote mawili yana maana ‘tupe muda tufahamu’ lakini la kwanza pia lina maana ‘mchunga mbuzi wetu’ Wanafiki walikuwa wakimkejeli Mtume kwa kutumia neno la kwanza na kukusudia maana ya pili. Waumini wakaamriwa watumie neno ‘Undhurna’ pekee, lisilo na undumi kuwili! -Mfasiri).

109 Wengi miongoni mwa watu wa Kitabu wanatamani lau wangewarudisha ninyi muwe makafiri baada ya kuamini kwenu, kwa sababu ya wivu uliyo katika nyoyo zao baada ya wao kujua ukweli. Basi sameheni na mwachilie mbali mpaka Mwenyezi Mungu atapoleta amri Yake. Hakika Mwenyezi Mungu Ni Muweza wa kila kitu. 110 Na dumisheni Swala na toeni Zaka, na kheri yoyote mtakayoitangulizia nafsi zenu, mtaikuta kwa Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuyaona mnayoyafanya. 111 Na walisema: Hataingia Peponi isipokuwa Myahudi au Mkristo. Hayo ni mapenzi yao tu. Waambie: ‘Leteni ushahidi wenu kama nyinyi mnasema kweli’. 112 Ni kweli! Kwamba yeyote anayemkusudia Mwenyezi Mungu pekee kwa ibada yake, naye akawa mtenda mema, basi ana malipo yake kwa Mola wake Mlezi, wala haitakuwa hofu juu yao wala hawatahuzunika.

113. Mayahudi husema: Wakristo hawana chochote! Na Wakristo nao husema, Mayahudi hawana lolote! Na ilihali (wanadai) wanasoma Kitabu (hicho hicho). Na vivi hivi ndivyo wale wasiojua kitu wasemavyo mfano wa kauli yao hii. Basi Mwenyezi Mungu atahukumu baina yao Siku ya Kiyama katika yale waliyokuwa wakitofautiana.. 114. Ni nani dhalimu mkubwa kuliko yule anayezuia misikiti ya Mwenyezi Mungu kutajwa jina Lake humo, na akapania kuibomoa? Hao haitafaa waingie humo ila wakiwa wana hofu. Duniani watapata fedheha na Akhera wana adhabu kubwa. 115. Na Mashariki na Magharibi ni ya Mwenyezi Mungu, basi kokote mnakoelekea, huko Mwenyezi Mungu yupo. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuenea pote, Mwenye kujua. 116. Na wanasema: Mwenyezi Mungu ati ana

mwana! Ametakasika na hilo! Bali vyote viliyomo mbinguni na ardhini ni Vyake. Vyote vinamtii Yeye. [117.] Mbunifu wa mbingu na ardhi; na anapotaka jambo, huliambia tu: 'Iwe! Na likawa'.

[118.] Na wale wasiojua chochote walisema: Si Mwenyezi Mungu mwenyewe angetuambia sisi (kuwa wewe ni Mtume) au kwa nini haitujii ishara (tuitakayo) ? Mfano wa maneno yao haya ndiyo hivyo hivyo walivyosema waliokuwa duniani kabla yao. Dhamira zao zimefanana. Hakika sisi tumeweka wazi ishara kwa watu wenye yakini. [119.] Hakika sisi tumekutuma kwa ukweli, uwe mwenye kutoa habari njema na mwonyaji, wala hutaulizwa kuhusu watu wa motoni. [120.] Kamwe hawatakukubali si Mayahudi wala Wakristo mpaka ufuate dini yao. Sema: Hakika uongofu wa Mwenyezi Mungu ndio uongofu wa kweli.. Na kama ukifuata mapenzi yao baada ya elimu iliokufikia, basi hutapata mlinzi wala msaidizi yoyote dhidi ya Mwenyezi Mungu. [121.] Wale tuliowapa Kitabu wakakisoma kama inavyostahiki kukisoma, hao ndio wanaokiamini. Na wanaokikataa, basi hao ndio wenye hasara.

[122.] Enyi wana wa Israeli! Kumbukeni neema Yangu niliyowaneemesha, na hakika nimewapendeleeni ( kuwapa ujumbe wangu kwanza) juu ya wengine wote. [123.] Na ogopeni siku ambayo mtu hatakuwa na muda na mtu mwingine kwa jambo lolote, wala hakitakubaliwa kwake kikomboleo, wala hayatamfaa maombi, wala hawatanusuriwa. [124.] Na (kumbuka pale) Mola wako Mlezi alipomjaribu Ibrahim (Abraham) kwa kumpa amri fulani, naye akazitimiza. Akamwambia: Nimekufanya kiongozi wa watu. Akajibu: Na katika kizazi

changu (pia)? Akasema: ahadi yaangu haitawafikia wafanyao uovu..

[125.] Na (pale) tulipoifanya ile Nyumba (Al-Kaaba) iwe mahali pa kuendewa na watu na mahali pa amani. Na pafanyeni alipokuwa akisimama Ibrahim kuwa mahali pa kuswalia. Na tuliagana na Ibrahim na Ismail kuwa: ‘Itakaseni Nyumba Yangu kwa ajili ya wanaoizunguka kwa kutufu na wenye kujitenga huko kwa ibada, na wanaoinama na kusujudi’. [126.] Na (pale) Ibrahim aliposema: Ewe Mola wangu Mlezi! Ufanye huu uwe mji wa amani, uwaruzuku watu wake matunda, wale tu wanaomwamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho miongoni mwao. Mwenyezi Mungu akasema: ‘Na hata mwenye kukana pia! Nitamstarehesha kidogo tu, kisha nitamsukumiza katika adhabu ya Moto; napo ni mahali pabaya kabisa pa kufikia!’.

[127.] Na (kumbukeni pale) Ibrahim na Ismail waliponyanyua misingi ya ile Nyumba wakaomba: Ewe Mola wetu Mlezi! Tukubalie (kazi hii yetu), hakika wewe ndiye Msikizi, Mjuzi. [128.] Ewe Mola wetu Mlezi! Utufanye tuwe wanyenyekevu Kwako, na pia miongoni mwa kizazi chetu wawe umma mnyenyekevu kwako. Na utufundishe ibada zetu na utukubalie toba zetu. Hakika Wewe ndiye Mwingi wa kukubali toba, Mwingi wa huruma. [129.] Ewe Mola wetu Mlezi! Waletee Mtume anayetokana na wao, awasomee Aya Zako, na kuwafundisha Kitabu na hekima na awatakase. Hakika Wewe ndiye Mwenye nguvu Mwenye hekima.

[130.] Na ni nani atajitenga na dini ya Ibrahim isipokuwa anayetaka kujitia katika upumbavu tu! Hakika Sisi tulimteuwa na kumtakasa hapa duniani, naye huko Akhera atakuwa miongoni mwa watu wema. [131.] (Pale) Mola wake

Mlezi alipomwambia (Ibrahim): ‘Salimu amri kwa matakwa
yangu (Silimu)!’ Akasema: Nimesalimu amri kwa Mola wa
walimwengu wote. 132. Na Ibrahim akawausia haya wanawe,
na (pia) Yakobo (Jacob): ‘Enyi wanangu! Hakika Mwenyezi
Mungu amewachagulia dini hii; msitoke duniani isipokuwa
nyie ni Waislamu’. 133. Je, mlikuwapo yalipomfika Yakobo
mauti? Pale alipowauliza wanawe: Mtaabudu nini baada
yangu? Wakasema: Tutamwabudu Mola wako na Mola wa
baba zako, Ibrahim na Ismail na Is-hak; Mungu mmoja tu, na
sisi tunajisalimisha Kwake. 134. Hao ni watu waliokwishapita.
Watavuna waliyoyachuma, nanyi mtavuna mtakayoyachuma,
wala hamtaulizwa waliyokuwa wakiyafanya.

135 Na wanasema: ‘kuweni Mayahudi au Wakristo
ndiyo mtaongoka!’. Sema: bali (tunashika) dini ya Ibrahim
mwongofu, wala hakuwa katika wale wanaomshirikisha
Mwenyezi Mungu na wengine. 136 Semeni: Tumemwamini
Mwenyezi Mungu na yale tuliyoteremshiwa sisi, na yale
yaliyoteremshwa kwa Ibrahim na Ismail na Is-hak na
Yakobo na wajukuu zake, na waliyopewa Musa (Moses)
na Isa (Yesu) na (pia) yale waliyopewa Manabii (wengine)
kutoka kwa Mola wao Mlezi; hatumbagui yeyote katika
wao, na sisi tumejisalimisha Kwake. 137 Basi wakiamini
kama mnavyoamini nyinyi, watakuwa wameongoka. Na
wakirudi nyuma, basi wao ndiyo watakuwa wamejitenga.
Basi Mwenyezi Mungu atakutoshea (shari yao). Na yeye
ndiye Msikizi, Mjuzi. 138 (Dini hii) ndiyo unadhifu wa
kiroho (ubatizo) anaoukubali Mwenyezi Mungu. Ni nani
mtoaji mzuri wa unadhifu wa kiroho kuliko Allah? Na sisi
tunamwabudu Yeye. 139 Waambie: ‘Je mnahojiana nasi juu ya
Mwenyezi Mungu, na hali Yeye ndiye Mola wetu Mlezi na

ndiye Mola wenu Mlezi? Na sisi tutawajibika kwa matendo yetu, nanyi pia mtawajibika kwa matendo yenu. Na sisi tunamtakasia Yeye tu (imani yetu)? [140] Au mnasema kuwa Ibrahim na Ismail na Is-hak na Yakobo na wajukuu (zake) walikuwa Mayahudi au Wakristo? Sema: Je, ninyi mnajua zaidi au Mwenyezi Mungu? Na ni nani dhalimu mkubwa kuliko yule afichaye ushahidi alio nao utokao kwa Mwenyezi Mungu? Na Mwenyezi Mungu si Mwenye kughafilika na hayo mnayoyafanya. [141] Hao ni watu waliokwishapita. Watavuna waliyoyachuma (hapa duniani) nanyi mtavuna mtakayoyachuma. Wala kamwe hamtaulizwa waliyokuwa wakiyafanya.

[142.] Watu wapumbavu watasema: Kitu gani kilichowafanya wageuke kuacha kibla chao (Jerusalem) walichokuwa wakielekea? Waambie: Mashariki na Magharibi vyote ni milki ya Mwenyezi Mungu. Humwongoza amtakaye kwenye njia iliyonyooka. [143.] Kwa ajili hiyo ndipo tumewafanya ninyi kuwa umma wa wastani, ili muwe mashahidi juu ya watu wote, na Mtume awe shahidi juu yenu. Na hatukukifanya kile Kibla ulichokuwa unakielekea isipokuwa kwa kumjaribu yule aliyekuwa akimfuata Mtume, kumpambanua na yule atakayegeuka na kurudi nyuma. Na kwa hakika Jambo hilo lilikuwa gumu isipokuwa kwa wale ambao Mwenyezi Mungu aliwaongoza. Na Mwenyezi Mungu kamwe si Mwenye kuifanya imani yenu kuwa si chochote. Hakika Mwenyezi Mungu, ni Mpole mno kwa watu, Mwenye kuwaonea huruma mno.

[144.] Kwa hakika tunakuona unavyogeuza geuza uso wako kuelekea mbinguni (kutaka maelekezo); basi tutakuelekeza Kibla ukipendacho. Haya! Elekeza uso wako upande wa

Msikiti Mtukufu (Kaaba). Na popote mlipo, geuzeni nyuso zenu upande huo. Na hakika wale waliopewa Kitabu wanajua kwamba huo ndiyo ukweli utokao kwa Mola wao Mlezi; na Mwenyezi Mungu si Mwenye kughafilika na yale wanayoyafanya. 145. Na hao waliopewa Kitabu hata ukiwaletea hoja za kila namna, hawatafuata Kibla chako; wala wewe si mwenye kufuata Kibla chao, wala baadhi yao si wenye kufuata Kibla cha wengine. Na kama utafuata mapenzi yao baada ya elimu iliyokufikia, basi utakuwa miongoni mwa madhalimu. 146. Wale tuliowapa Kitabu wanayajua haya kama wanavyowajua watoto wao. Na hakika kundi katika wao wanauficha ukweli na hali wanajua. 147. (Huu ni) ukweli kutoka kwa Mola wako Mlezi. Basi usiwe miongoni mwa wanaotia shaka.

148. Na kila dini ina upande wanakoelekea wafuasi wake. Basi fanyeni haraka kufanya mema (kuelekea Ka'ba). Popote mtakapokuwa, Mwenyezi Mungu atawaleta nyote pamoja. Hakika Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kila kitu. 149. Na popote uendapo elekeza uso wako upande wa Msikiti Mtukufu; na huo ndiyo ukweli utokao kwa Mola wako Mlezi. Na Mwenyezi Mungu si Mwenye kughafilika na yale mnayoyatenda. 150. Popote uendapo elekeza uso wako upande wa Msikiti Mtukufu. Na popote mlipo elekezeni nyuso zenu upande huo; ili watu wasiwe na sababu ya kuzozana nanyi, isipokuwa wale wapenda shari miongoni mwao; hao msiwaogope, niogopeni Mimi, ili niwatimizie neema Zangu na ili mpate kuongoka. 151. Kama tulivyomleta Mtume kwenu anayetokana na nyinyi wenyewe, anayewasomea Aya Zetu na kuwatakasa na kuwafundisha Kitabu na Hekima na

kuwafundisha mliyokuwa hamyajui. [152.] Basi nikumbukeni nitawakumbuka, na nishukuruni wala msinikane.

[153.] Enyi walioamini! Jisaidieni kwa kusubiri na kuswali. Hakika Mwenyezi Mungu yuko pamoja na wanaosubiri. [154.] Wala msiseme kwamba wale wanaouawa katika njia ya Mwenyezi Mungu ni maiti, bali wako hai lakini nyinyi hamtambui. [155.] Na hakika tutawatia katika msukosuko wa hofu na njaa na upungufu wa mali na watu na matunda. Na wape bishara njema wanaosubiri. [156.] Ambao ukiwapata msiba, husema: ‘Hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu, na Kwake tutarejea’. [157.] Hao watapokea Baraka na huruma zitokazo kwa Mola wao Mlezi, na hao ndio wenye kuongoka.

[158.] Hakika (vilima vya) Swafaa na Mar-wa ni katika ishara za Mwenyezi Mungu. Basi anayehiji Nyumba hiyo au akafanya Umra, si vibaya kwake akavizunguuka. Na anayefanya kheri, basi Mwenyezi Mungu ni Mwenye shukrani, Mjuzi. [159.] Hakika wale wanaoficha tuliyoyateremsha, nazo ni hoja zilizo wazi na uwongofu, baada ya Sisi kuziweka wazi kwa watu ndani ya Kitabu, hao anawalaani Mwenyezi Mungu, na wanawalaani kila wanaolaani. [160.] Ila wale waliotubu na kujirekebisha na wakafafanua wazi ukweli (waliokuwa wakiuficha), hao nitapokea toba yao, na Mimi ni Mwingi wa kupokea toba, Mwenye huruma nyingi. [161.] Hakika wale waliokufuru, na wakafa hali ni makafiri, hao wana laana ya Mwenyezi Mungu na ya Malaika na ya watu wote. [162.] Watadumu humo. Hhawatapunguziwa adhabu wala hawatapewa muda wa kupumzika.

[163.] Na Mungu wenu ni Mungu Mmoja tu, hakuna mungu isipokuwa Yeye, Mwingi wa huruma, Mwenye kurehemu. [164.] Hakika katika kuumbwa mbingu na ardhi, na kubadilika

kwa usiku na mchana, na vyombo ambavyo hupita baharini (na bidhaa) ziwafaazo watu, na mvua anayoishusha Mwenyezi Mungu kutoka mawinguni, na kwa mvua hiyo akaipa uhai ardhi baada ya kufa kwake, na akaeneza humo kila aina ya wanyama, na mabadiliko ya pepo, na mawingu yanayoamrishwa kupita baina ya mbingu na ardhi, ni ishara kwa watu wenye akili.

[165.] Na katika watu wapo wale wanaojitengenezea waungu wemgine wasiokuwa Mwenyezi Mungu, wanawapenda kama mapenzi ya Mwenyezi Mungu. Lakini wale walioamini wanampenda Mwenyezi Mungu zaidi. Na laiti waliodhulumu (nafsi zao) wangejua watakapoiona adhabu, kwamba nguvu zote ni za Mwenyezi Mungu, na kwamba Mwenyezi Mungu ni Mkali wa kuadhibu…..(Uff. Wasingefanya hivyo) [166.] Siku waliofuatwa watakapowakana wale waliowafuata, baada ya kwishaiona adhabu na ukavunjika uhusiano wao wote.
[167.] Wale waliofuata watasema: Laiti kama tungepata fursa moja tu! Nasi tukawakataa kama walivyotukataa. Hivi ndivyo Mwenyezi Mungu atakavyowaonesha vitendo vyao kuwa majuto kwao; wala hawatakuwa wenye kutoka Motoni.

[168.] Enyi watu! Kuleni vilivyomo ardhini halali, vizuri. Na msifuate nyayo za Shetani. Hakika yeye kwenu ni adui aliye dhahiri. [169.] Hakika yeye anawaamrisha maovu na machafu, na mumsingizie Mwenyezi Mungu mambo msiyoyajua.
[170.] Na wanapoambiwa: Fuateni aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu; husema: Bali tutafuata yale tuliyowakuta nayo baba zetu. Je, hata kama baba zao walikuwa hawafahamu chochote wala hawakuongoka? [171.] Na mfano wa wale waliokufuru, ni kama mfano wa anayempigia kelele asiyesikia ikawa wito na sauti tu. Ni viziwi, mabubu, vipofu; kwa hivyo hawafahamu.

[172.] Enyi walioamini! Kuleni vizuri tulivyowaruzuku, na mumshukuru Mwenyezi Mungu ikiwa kweli mnamwabudu Yeye tu. [173.] Hakika amewaharamishia tu mzoga na damu, na nyama ya nguruwe, na kilichotajwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu wakati wa kuchinja. Lakini aliyefikwa na dharura (akala) si kwa kuasi wala kupita kiasi, yeye hana dhambi. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye maghufira, Mwenye kurehemu. [174.] Hakika wale wafichao aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu katika Kitabu na wakanunua kwacho thamani ndogo (ya dunia), hao hawali matumboni mwao isipokuwa Moto: wala Mwenyezi Mungu hatawasemesha Siku ya Kiyama, wala hatawatakasa; na wao wana adhabu chungu. [175.] Hao ndio walionunua upotofu badala ya uwongofu, na adhabu badala ya msamaha. Je, wana ujasiri gani hao wa kuvumilia Moto? [176.] Hayo ni kwa sababu Mwenyezi Mungu ameteremsha Kitabu kwa haki, na wale waliohitilafiana katika Kitabu (hiki) wamo katika upinzani ulio mbali na haki.

[177.] Wema, siyo tu kuelekeza nyuso zenu upande wa mashariki na magharibi, lakini wema ni wa anayemwamini Mwenyezi Mungu, na Siku ya Mwisho, na Malaika, na Kitabu na Manabii; na akatoa mali, ingawaje ana haja nayo, kuwapa jamaa zake na mayatima na masikini na walio safarini, na waombao, na katika ukombozi wa watumwa; na akadumisha Swala na akatoa Zaka; na watekelezao ahadi zao wanapoahidi, na wanaokuwa na subira katika shida na dhiki na katika wakati wa vita. Hao ndio waliosadikisha na ndio wanaomtii na kumuenzi Mwenyezi Mungu.

[178.] Enyi walioamini! Mmepewa ruhusa ya kulipiza kisasi kwa waliouawa; muungwana kwa muungwana, na

mtumwa kwa mtumwa, na mwanamke kwa mwanamke.
Na anayesamehewa chochote na ndugu ya aliyeuawa, basi
afuatishe kwa matakwa yanayokubalika (Diya), naye amlipe
bila usumbufu. Huko ni kupunguziwa na huruma kutoka
kwa Mola wenu Mlezi. Na atayekiuka mipaka baada ya
hayo, basi ana adhabu iumizayo. 179. Katika kulipiza kisasi
kuna kulinda maisha yenu, enyi wenye akili, ili msalimike.
180. Hukumu imetolewa kwenu kuwa mmoja wenu
anapofikwa na mauti, kama akiacha mali yeyote, (anaweza)
kufanya wosia kwa wazazi wawili na jamaa wa karibu kwa
kiasi kinachokubalika, hii ikiwa ni haki kwa wale wanaomtii
na kumuenzi Mwenyezi Mungu. 181. Na atakayeubadilisha
(wosia huo) baada ya kuusikia, basi dhambi yake ni juu
ya wale watakaoubadilisha. Hakika Mwenyezi Mungu ni
Mwenye kusikia, Mjuzi. 182. Na mwenye kuhofia muusiaji
kwenda kombo au (kufanya) dhambi, akasuluhisha baina
yao, basi hatakuwa na kosa. Hakika Mwenyezi Mungu ni
Mwingi wa maghufira, Mwenye kurehemu.

183. Enyi walioamini! Ni wajibu kwenu kufunga, kama
kulivyowajibishwa kwa wale waliokuwa kabla yenu, ili mpate
kumtii na kumuenzi Mwenyezi Mungu. 184. Siku maalum
za kuhesabika. Na atakayekuwa mgonjwa katika ninyi, au
akiwa safarini, basi atimize idadi katika siku nyingine. Na
wale wanaoweza kufunga lakini kwa kujikalifisha, watoe
fidia kwa kumlisha maskini mmoja. Lakini atakayejitolea
zaidi kwa hiari yake, hiyo ni bora kwake. Na kufunga ni bora
kwenu, ikiwa mnajua. 185. Mwezi wa Ramadhani ndiyo ambao
imeteremshwa katika mwezi huu Qur'an, kuwa mwongozo
kwa watu na hoja zilizo wazi za mwongozo na upambanuzi.
Hivyo atakayeushuhudia mwezi miongoni mwenu (akiwa

kwake), basi aufunge. Ama akiwa mgonjwa au safarini, basi atimize idadi katika siku nyingine. Mwenyezi Mungu anawatakia wepesi wala hawatakii uzito, na mkamilishe idadi hiyo, na mumtukuze Mwenyezi Mungu kwa kuwa amewaongoza, na ili mpate kushukuru.

186. Na waja Wangu watakapokuuliza habari Yangu, Mimi niko karibu. Naitikia maombi ya mwombaji anaponiomba. Basi nawaniitike Mimi na waniamini Mimi ili wapate kuongoka. 187. Mmehalalishiwa usiku wa saumu kujamiiana na wake zenu. Wao ni vazi lenu na nyinyi ni vazi lao. Mwenyezi Mungu anajua kuwa mlikuwa mkizifanyia khiyana nafsi zenu, kwa hivyo amewatakabalia toba yenu na amewasamehe. Basi sasa ingilianeni nao na tafuteni (kwao) alichowaandikia Mwenyezi Mungu. Na kuleni na kunyweni mpaka uwabainikie uzi mweupe wa Alfajiri kutoka uzi wa kiza cha usiku. Kisha timizeni Swaumu mpaka usiku. Na wala msiingiliane nao na hali mko katika itikafu misikitini. Hiyo ni mipaka ya Mwenyezi Mungu, msiikaribie. Namna hii Mwenyezi Mungu anabainisha aya Zake kwa watu ili wapate kujifunza kudhibiti nafsi zao. 188. Wala msitumie mali zenu baina yenu kwa njia ya batili na mkazipeleka kwa mahakimu ili mpate kula sehemu ya mali ya watu kwa dhambi, na hali mnajua.

189. Wanakuuliza kuhusu miezi inavyoandama. Sema: Hiyo ni vipimo vya nyakati kwa ajili ya watu na kwa Hijja. Wema si kuingia majumbani kwa (kupitia) nyuma. Bali wema ni (wa) yule amchaye Mungu. Na ingieni majumbani kupitia milangoni, na mtiini na muenzini Mwenyezi Mungu ili mpate kufaulu. 190. Na piganeni katika njia ya Mwenyezi Mungu dhidi ya wale wanaowapiga, wala msianze uchokozi.

Hakika Mwenyezi Mungu hawapendi wachokozi. 191. Na
wauweni popote muwapatapo, na wafurusheni popote
walipowafurusha nyie; kwani fitina ni mbaya zaidi kuliko
kuua. Wala msipigane nao karibu na Msikiti Mtukufu mpaka
wapigane nanyi huko. Wakipigana na nyinyi, basi waueni.
Namna hii ndivyo yalivyo malipo ya wanaomkana Mungu.
192. Lakini wakikoma, basi hakika Mwenyezi Mungu ni
Mwingi wa maghufira, Mwenye kurehemu. 193. Na piganeni
nao mpaka kusiwe na uasi na machafuko, na dini iwe ya
Mwenyezi Mungu peke Yake. Na wakikoma, basi usiweko
uadui ila kwa wanaofanya ukandamizaji.

194. Mwezi Mtukufu kwa mwezi Mtukufu, na vitu vitukufu
vimewekewa kisasi. Basi anayewashambulia, nanyi mlipizeni
kwa kadiri ya alivyowashambulia. Lakini mwogopeni
Mwenyezi Mungu na jueni kwamba Mwenyezi Mungu yuko
pamoja na wanaomtii na kumuenzi (Yeye). 195. Na toeni mali
zenu katika njia ya Mwenyezi Mungu wala msijitie wenyewe
katika maafa. Fanyeni mambo mazuri. Hakika Mwenyezi
Mungu huwapenda wafanyao mazuri.

196. Na timizeni Hijja na umra kwa ajili ya Mwenyezi
Mungu. Na kama mkizuiliwa, basi chinjeni wanyama walio
wepesi kupatikana. Wala msinyoe vichwa vyenu mpaka
wanyama hao wafike machinjioni mwao. Na atakayekuwa
mgonjwa katika nyinyi, au ana adha kichwani mwake, basi
atoe fidia kwa kufunga au sadaka au kuchinja mnyama. Na
mtakapokuwa salama, basi mwenye kujistarehesha kwa
kufanya umra, kisha akahiji, achinje mnyama aliye mwepesi
kumpata. Na asiyepata, ni kufunga siku tatu katika Hijja
na siku saba mtakaporudi; hizo ni siku kumi kamili. Hayo
ni kwa yule ambaye watu wake hawako karibu na Msikiti

mtukufu. Na mcheni Mwenyezi Mungu na jueni kwamba Mwenyezi Mungu ni Mkali wa kuadhibu. [197.] Hijja ni miezi maalum. Na anayekusudia kufanya Hijja katika miezi hiyo, asiseme maneno machafu wala asifanye vitendo vichafu wala asibishane katika Hijja. Na kheri yoyote mnayoifanya Mwenyezi Mungu anaijua. Na chukueni masurufu, na hakika masurufu bora ni kumcha Mungu; na nicheni Mimi, enyi wenye akili.

[198.] Si vibaya kwenu kutafuta riziki ya Mola wenu Mlezi (mkiwa katika Hijja). Na mtakapomiminika kutoka Arafa, mtajeni Mwenyezi Mungu katika Mash’aril-Haram: Na mkumbukeni kama alivyowaongoza, ijapokuwa zamani mlikuwa miongoni mwa waliopotea. [199.] Kisha mtembee kwa haraka kutoka mahali wanapomiminikaa watu (wote), na mumwombe Mwenyezi Mungu maghufira; hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kughufiria, Mwenye kurehemu. [200.] Na mkishatimiza ibada zenu, basi mtajeni Mwenyezi Mungu kama mlivyokuwa mkiwataja baba zenu; bali mtajeni zaidi. Na wapo baadhi ya watu wasemao: Ewe Mola wetu Mlezi, tupe hapa duniani! Na ilihali huko Akhera hawana fungu lolote. [201.] Na katika wao wapo wale wasemao: Mola wetu Mlezi! Utupe mema hapa duniani na mema huko Akhera, na utukinge na adhabu ya moto. [202.] Hao ndio wenye fungu katika waliyoyachuma, na Mwenyezi Mungu ni mwepesi wa kutoa hukumu. [203.] Na Mtajeni Mwenyezi Mungu katika siku zinazohisabiwa. Na mwenye kufanya haraka (kurudi nyumbani) katika siku mbili, hana dhambi; na mwenye kukawia pia hapati dhambi, kwa wanaomcha Mungu, Na mcheni Mwenyezi Mungu, na jueni kwamba nyinyi mtakusanywa kwake.

204. Na katika watu kuna ambaye kauli yake inakupendeza katika maisha ya duniani, naye humtaka Mwenyezi Mungu awe shahidi kwa yaliyo moyoni mwake, na hali yeye ni hasimu mkubwa kabisa. 205. Lakini anapokupa mgongo tu hufanya bidii kufanya uharibifu duniani, na huangamiza mimea na viumbe, na Mwenyezi Mungu hapendi uaribifu.
206. Na anapoambiwa: Mtii na umuenzi Mwenyezi Mungu, hupandwa na kiburi afanye dhambi. Basi Jahannam inamtosha, nayo ni makao mabaya mno. 207. Na katika watu yuko anayejitolea uhai wake ili apate radhi ya Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu ni Mpole mno kwa waja.

208. Enyi walioamini! Ingieni katika Uislamu kikamilifu, wala msifuate nyayo za Shetani. Kwa hakika yeye kwenu ni adui aliye wazi. 209. Na kama mkiteleza (mkarudi nyuma) baada ya kuwafikia hoja zilizo wazi, basi jueni kwamba Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mwingi wa hekima.
210. Je, wanangojea hadi hapo Mwenyezi Mungu awajie katika mihimili ya mawingu akiwa na Malaika, ndipo iwe jambo hili limetatuliwa? Basi ni kwa Mwenyezi Mungu pekee ndiko masuala yote hurudishwa ( kwa uamuzi).
211. Waulize wana wa Israeli ni ishara ngapi wazi wazi tulizowapa? Na anayezibadilisha neema za Mwenyezi Mungu baada ya kumfikia, basi hakika Mwenyezi Mungu ni Mkali wa kuadhibu. 212. Maisha ya hapa duniani huwavutia wale waliomkana Mwenyezi Mungu, hivi kwamba huwafanyia kejeli wale walioamini. Lakini wenye kumtii na kumuenzi Mungu watakuwa juu yao Siku ya Kiyama. Na Mwenyezi Mungu humruzuku amtakaye bila kipimo.

213. Watu wote walikuwa taifa moja. Kisha Mwenyezi Mungu akapeleka Manabii kutoa bishara njema na kuonya.

Na pamoja nao akawateremshia kitabu kinachoshikamana na ukweli ili kitoe hukumu baina ya watu katika yale wanayotofautiana. Na hawakutofautiana wale waliopewa kitabu hicho isipokuwa baada ya kuwafikia hoja zilizo wazi, kwa sababu ya huki na wivu baina yao. Ndipo Mwenyezi Mungu, kwa ridhaa yake, akawaongoza walio amini kweye ukweli katika yale mambo waliyotofautiana. Na Mwenyezi Mungu humwongoza amtakaye kwenye njia iliyonyooka.
214. Au mnadhani kuwa mtaingia Peponi na ilihali hayajawakuta kama yaliyowakuta wale waliopita kabla yenu? Wao walipatwa na shida na madhara, wakasukwasukwa hadi Mtume na waumini waliokuwa pamoja naye wakauliza: Lini nusura ya Mwenyezi Mungu itatufikia? Ndiyo! Nusura ya Mwenyezi Mungu (siku zote) iko karibu.

215. Wanakuuliza watoe nini? Sema: kitu chochote kizuri mtakachotoa, iwe kwa ajili ya wazazi wawili na ndugu wa karibu na mayatima na masikini na walio safarini. Na kitu chochote kizuri mnachokifanya Mwenyezi Mungu anakijua.
216. Mmeamuriwa kupigana vita, na jambo hilo hamlipendi. Lakini huenda mkachukia kitu kikawa ni kizuri kwenu. Na huenda mkapenda kitu kikawa kibaya kwenu. Na Mwenyezi Mungu anajua na nyie hamjui.

217. Wanakuuliza juu ya kupigana (vita) katika mwezi Mtukufu. Sema: Kupigana vita katika wakati huo ni dhambi kubwa. Lakini kuzuilia watu wasiende katika njia ya Mwenyezi Mungu na kumkana, na kuwazuia wasiingie Msikiti Mtukufu, na kuwatoa waliomo humo….(haya) ni dhambi kubwa zaidi mbele ya Mwenyezi Mungu. Na machafuko, uasi, ni mbaya zaidi kuliko kuua. Wala hawataacha kupigana nanyi mpaka wawatoeni katika dini yenu, kama wakiweza.

Na yeyote katika nyinyi atakayeikana Dini yake, akafa akiwa kafiri, basi hao yameporomoka (malipo ya) amali zao hapa duniani na Akhera. Na hao ndio watu wa Motoni, humo watakaa milele. [218.] Hakika wale walioamini na wale waliohama na wakapigania njia ya Mwenyezi Mungu, hao ndio wanaotaraji rehema ya Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kughufiria, Mwenye kurehemu.

[219.] Wanakuuliza kuhusu ulevi na kamari. Sema: Katika hivyo kuna dhambi kubwa na pia manufaa kwa watu. Lakini dhambi zake ni kubwa zaidi kuliko manufaa yake. Na wanakuuliza watoe nini? Sema: Vilivyozidi mahitaji yenu. Namna hii Mwenyezi Mungu anawabainishia Aya (zake) mpate kufikiria… [220.] Katika mambo ya duniani na ya Akhera. Na wanakuuliza kuhusu mayatima. Sema: Kuwatengenezea mambo yao ndiyo vizuri. Laa kama mkichanganyika nao (kuchanganya mali zenu na zao kwa kuzikuza), basi ni ndugu zenu. Na Mwenyezi Mungu anamjua mtu (mwenye nia) mbaya na mleta maendeleo. Na laiti kama Mwenyezi Mungu angelitaka, angewafanyia vigumu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mwenye hekima.

[221.] Wala msiwaoe wanawake mapagani mpaka wakubali imani. Na mjakazi muumini ni bora kuliko mapagani, hata akiwapendeza. Wala msiwaoze (binti zenu) wanaume mapagani mpaka waamini. Na mtumwa muumini ni bora kuliko mpagani, hata akiwapendeza. Hao wanawavutia kwenye Moto, na Mwenyezi Mungu anawavutia kwenye Pepo na maghufira, kwa ridhaa Yake. Naye hubainisha Aya Zake kwa watu ili wapate kukumbuka. [222.] Wanakuuliza kuhusu hedhi. Waambie: ni uchafu. Basi jitengeni na wanawake wakati wa hedhi, wala msiwajamii mpaka wajitakase.

Wakisha jitakasa basi waendeeni kwa namna, wakati au mahali kama alivyowaamrisha Mwenyezi Mungu.. Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wanaotubia na huwapenda wanaojitakasa. [223.] Wake zenu ni mashamba yenu. Basi yaendeeni mashamba yenu mpendavyo. Lakini jifanyieni mambo mazuri kabla ya hapo, na mumtii na kumuenzi Mwenyezi Mungu na jueni kwamba mtakutana naye, na wabashirie wenye kuamini.

[224.] Wala msilifanye jina la Mwenyezi Mungu katika viapo vyenu kuwa ni kisingizio cha kutofanya mema na kumtii na kumuenzi Mwenyezi Mungu na kusuluhisha kati ya watu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia, Mjuzi. [225.] Mwenyezi Mungu hatawafanya muwajibike kwa sababu ya viapo vyenu vya upuuzi. Lakini atawawajibisha kwa (viapo) vilivyonuiwa na nyoyo zenu. . Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa maghufira, Mpole. [226.] Kwa wale ambao wanaapa kutowajamii wake zao, wangojee miezi minne. Endapo watarejea (uhusiano wa kawaida), basi Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa maghufira, Mwenye kurehemu. [227.] Lakini kama wameazimia kuachana, basi Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia, Mjuzi. [228.] Na wanawake waliopewa talaka wangojee mpaka zipite tohara tatu (au hedhi). Wala si halali kwao kuficha alichokiumba Mwenyezi Mungu katika matumbo yao, endapo (kweli) wanamwamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho. Na waume zao wana haki zaidi ya kuwarejesha (kwenye ndoa) katika muda huo, kama wakitaka kufanya suluhu. Na wanaume wana wajibu na haki kwa wake zao, kama ambavyo wake wana wajibu na haki kwa waume zao, kwa mujibu wa desturi, lakini wanaume wanawazidi kidogo wanawake (kwa majukumu

na madaraka). Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mwenye hekima.

229. Talaka ni mara mbili; kisha ni kuishi pamoja kwa
wema au kuachana kwa hisani. Wala si halali kwenu
kuchukua chochote katika mlivyowapa wake zenu, isipokuwa
wakiogopa (wote wawili) kwamba hawataweza kuhifadhi
mipaka ya Mwenyezi Mungu. Basi mkiogopa kwamba
hawataweza kuhifadhi mipaka ya Mwenyezi Mungu,
itakuwa hapana ubaya kwao ikiwa mwanamke (atatoa
kitu) kwa kujikomboa (kutoka ndoa). Hii ndiyo mipaka ya
Mwenyezi Mungu; basi msiipetuke. Na watakaoipetuka
mipaka ya Mwenyezi Mungu, basi hao ndio madhalimu.
230. Na kama mume amemwacha mkewe kabisa (kwa kumpa
talaka tatu)/ basi si halali tena kwa mume huyo baada
ya hapo mpaka aolewe na mume mwingine. Na (mume
wa pili) akimwacha, basi hapo si vibaya kwao kurejeana
wakiona kuwa watahifadhi mipaka ya Mwenyezi Mungu.
Na hii ndiyo mipaka ya Mwenyezi Mungu anayoibainisha
kwa watu wajuao. 231. Na mtakapowapa wanawake talaka,
wakatimiza muda wao (wa kukaa eda), basi warejeeni
kwa wema au waacheni kwa wema. Wala msiwarejee kwa
kunuia kuwadhuru ili mfanye uadui. Na atakayefanya hivyo,
amejidhulumu mwenyewe.. Wala msizifanyie mzaha Aya
za Mwenyezi Mungu. Na kumbukeni neema ya Mwenyezi
Mungu juu yenu, na Kitabu alichowateremshia na hekima, ili
awaonye kwa kupitia Kitabu hicho. Na mtiini na mumuenzi
Mwenyezi Mungu, na jueni kwamba Mwenyezi Mungu ni
Mjuzi wa kila kitu.

232. Na mtakapowapa wanawake talaka na wakatimiza
muda wao, msiwazuie kuolewa na waume zao (waliowaacha),

ikiwa wamepatana kwa wema. Hayo anaonywa nayo yule, miongoni mwenu, anayemwamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho. Hivyo ni vizuri sana kwenu na safi zaidi. Na Mwenyezi Mungu anajua, na ninyi hamjui. [233.] Na mama wazazi wawanyonyeshe watoto wao miaka miwili kamili, kwa yule apendaye kukamilisha muda wa kunyonyesha. Na ni jukumu la baba aliyezaliwa mtoto kuwalisha akina mama wazazi na kuwavisha kulingana na desturi. Wala halazimishwi mtu isipokuwa kwa kadri ya uwezo wake. Mama asitiwe taabuni kwa ajili ya mwanawe, wala baba mvyelewa kwa ajili ya mwanawe. Na ni juu ya mrithi (wa baba) majukumu mfano wa yale ya baba mzazi. Na kama wote wawili wakitaka kumwachisha ziwa kwa ridhaa yao na (baada ya) kushauriana, basi si vibaya kwao. Na kama mkitaka kuwapatia watoto wenu mama (wengine) wa kuwanyoyesha, basi haitakuwa vibaya kwenu kama mkiwalipa mlichowaahidi kwa desturi. Na mtiini na muenzini Mwenyezi Mungu na jueni kwamba Mwenyezi Mungu anayaona mnayoyafanya.

[234.] Na wanaofikwa na mauti miongoni mwenu na kuacha wake, (inapasa) wake hao wangoje wao wenyewe miezi minne na siku kumi. Na wanapotimiza muda wao (wa eda), hakuna lawama kwenu kwa yale wanayojifanyia wenyewe kwa kadri inavyokubalika katika desturi. Na Mwenyezi Mungu ana habari za mnayoyafanya. [235.] Wala si vibaya kwenu kuonesha ishara za kukusudia kuwaposa wanawake (walio katika eda), au kutia azma katika nyoyo zenu. Mwenyezi Mungu anajua kwamba ninyi mtawafikiria. Lakini msiwaahidi kisiri-siri; isipokuwa mseme nao tu maneno yaliyoruhusiwa katika sheria. Wala msiazimie kufunga nao ndoa mpaka muda wa eda ulioamriwa ufike mwisho wake. Na jueni ya kwamba

Mwenyezi Mungu anayajua yaliyomo katika nyoyo zenu, basi jihadharini naye. Na jueni kwamba Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa maghufira, Mpole. [236.] Si vibaya kwenu kuwapa talaka wanawake ambao bado hamjawajamii au hamjafikia makubaliano juu ya mahari. Lakini wapeni zawadi ya kuwaliwaza; tajiri kwa kadiri awezavyo na maskini kadiri awezavyo. Kipoza moyo kitachoendana na desturi. Huo ni wajibu (wa kibinadamu) kwa wafanyao mambo mema. [237.] Na kama mkiwapa talaka kabla ya kuwajamii na mkawa mmekwisha patana mahari, basi (mtatoa) nusu ya hayo mahari mliyopatana. Isipokuwa kama wanawake wenyewe wanasamehe (nusu yao), au anasamehe (nusu yake) yule mume ambaye fundo la ndoa liko mikononi mwake. Na kusamehe (kwa mwanamume) ndio karibu zaidi na utiifu na kumuenzi Mwenyezi Mungu. Wala msisahau hisani baina yenu; hakika Mwenyezi Mungu anayaona mnayoyafanya.

[238.] Chungeni sana Swala, na hasa Swala ya katikati. Na simameni kwa unyenyekevu mnapo mwabudu Mwenyezi Mungu. [239.] Na kama mkiwa na hofu, basi swalini mkiwa mnatembea au mkiwa mmepanda. Na mtakapokuwa katika amani, basi mkumbukeni Mwenyezi Mungu kama alivyowafunza yale mliyokuwa hamyajui. [240.] Na wale wanaonyemelewa na mauti miongoni mwenu na watawaacha wake, basi na waache wosia kwa ajili ya wake zao wa kupata masurufu ya mwaka mzima, na marufuku kutolewa nyumbani. Lakini wakiondoka wenyewe, basi si vibaya kwenu kwa yale waliyojifanyia kwa hiari yao yanayokubalika katika desturi. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mwenye hekima. [241.] Na wanawake waliopewa talaka wapewe cha kuwaliwaza kulingana na desturi; huo ni wajibu (wa kibinadamu) kwa

wenye kumtii na kumuenzi Mwenyezi Mungu. [242.] Namna hiyo Mwenyezi Mungu anawabainishia Aya Zake ili mpate kufahamu.

[243.] Je, hukufikiria juu ya wale walioacha nyumba zao kwa maelfu, kwa kuogopa mauti? Mwenyezi Mungu akawaambia: Kufeni! Kisha akawafufua. Kwa hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye fadhila juu ya watu, lakini watu wengi hawashukuru. [244.] Na piganeni katika njia ya Mwenyezi Mungu, na jueni kwamba Mwenyezi Mungu ni Msikizi, Mjuzi. [245.] Ni nani atakayemkopesha Mwenyezi Mungu mkopo mzuri, ili amzidishie ziada nyingi nyingi? Mwenyezi Mungu hutoa kwa uchache na kwa ukunjufu, na Kwake mtarejeshwa.

[246.] Je, hukufikiria kisa cha machifu wa wana wa Israeli baada ya (kufa) Musa, pale walipomwambia Nabii wao: 'tuteulie mfalme nasi tutapigana katika njia ya Mwenyezi Mungu'. (Mtume wao) akasema: Je, haiyumkini kuwa huenda msipigane pindi kupigana kutakapofanywa kuwa lazima kwenu? Wakasema: 'Itakuwaje tusipigane katika njia ya Mwenyezi Mungu na hali sisi tumefukuzwa kutoka kwenye miji yetu sisi na watoto wetu'? Lakini walipolazimishwa kupigana, wakageuka isipokuwa wachache miongoni mwao. Na Mwenyezi Mungu anawajua wafanyao mabaya. [247.] Na Nabii wao akawaambia: 'Hakika Mwenyezi Mungu amewachagulia Talut (Saul) kuwa mfalme wenu'. Wakasema: 'Vipi yeye awe na madaraka juu yetu, na hali sisi tunastahiki zaidi madaraka kuliko yeye! Na yeye hata hakupewa utajiri mkubwa'? Akasema: 'hakika Mwenyezi Mungu amemteua yeye juu yenu na amemzidishia upana wa elimu na mwili'. Na Mwenyezi Mungu humpa madaraka yake amtakaye. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuwaenezea wote hisani zake,

Mjuzi. [248.] Na Nabii wao akawaambia: alama kuu ya ufalme wake ni kuwajia nyie lile kasha (la Agano, the Ark of the Covenant), ambalo ndani yake mna (dhamana ya) usalama kutoka kwa Mola wenu Mlezi na mabaki ya walivyoviacha familia ya Musa (Moses) na familia ya Harun (Aaron). Litabebwa na Malaika. Hakika katika hayo mna dalili kwenu ikiwa ninyi ni wenye kuamini.

[249] Basi Talut (Saul) aliposonga mbele na jeshi lake, aliwaambia: Mwenyezi Mungu atawapa mtihani wa mto wa maji; yeyote atakayekunywa maji ya mto huo si mtu wangu na asiyekunywa ni wangu, isipokuwa atakayeteka kifumba kimoja tu kwa mkono wake (huyo hatahesabika amekunywa). Wote wakanywa maji ya mto huo isipokuwa wachache tu katika wao. Basi walipovuka, yeye na wale walioamini pamoja naye (baadhi yao) wakasema: 'sisi hatuna nguvu leo dhidi ya Jalut (Goliath) na Jeshi lake'. Ama wale wenye yakini ya kukutana na Mola wao walisema: 'hivi majeshi mangapi madogo yameweza kuyashinda majeshi makubwa kwa idhini ya Mwenyezi Mungu?' Na Mwenyezi Mungu yuko pamoja na wenye subira. [250] Na walipotoka kupambana na Jalut (Goliath) na jeshi lake waliomba: 'Ewe Mola wetu Mlezi, utumiminie subira na uifanye imara miguu yetu na utusaidie tuwashinde watu wanaokukana'. [251] Basi wakawashinda wale kwa idhini ya Mwenyezi Mungu; na Daud (David) akamwua Jalut (Goliath), na Mwenyezi Mungu akampa yeye ufalme na hekima na akamfundisha alichokipenda. Na laiti Mwenyezi Mungu asingewazuia watu kwa (kuwatumia) watu wengine, dunia ingeharibika; lakini Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa fadhila juu ya viumbe vyote.

[252.] Hizi ni Aya za Mwenyezi Mungu, tunakusomea

kwa ukweli; na hakika wewe ni miongoni mwa Mitume. [253.] Hao Mitume, baadhi yao tumewapendelea zaidi kuliko wengine. Kati yao kuna ambaye Mwenyezi Mungu alisema naye; na wengine akawapandisha vyeo. Na tukampa Isa mwana wa Maryam (Yesu mwana Maria) dalili zilizo wazi na tukamsapoti kwa Roho Mtakatifu (Jibril). Na laiti Mwenyezi Mungu angetaka, vizazi vilivyofuatia baada yao visingepigana wao kwa wao, hata baada ya kuwafikia dalili zilizo wazi. Lakini walitofautiana; kuna katika wao aliyeamini na kuna aliyekana. Na laiti Mwenyezi Mungu angependa wasingepigana, lakini Mwenyezi Mungu hufanya analolipenda.

[254.] Enyi walioamini! Toeni baadhi ya vile tulivyowapa, kabla haijafika siku ambayo hapatakuwa na biashara wala urafiki wala uombezi. Na makafiri ndio madhalimu. [255.] Allah. Hapana mola isipokuwa Yeye pekee. Yu hai, msimamizi wa kila kitu. Hasinzii wala hashikwi na usingizi. Ni Vyake vilivyomo mbinguni na ardhini. Ni nani huyo awezaye kumwombea mwingine msamaha mbele Yake bila ya idhini Yake? Anayajua yajayo mbele yao na yaliyokwisha pita. Lakini wao hawajui chochote miongi mwa vilivyomo katika ujuzi Wake ila kile alichokitaka (wakijue). Ufalme Wake wa Enzi umeenea mbinguni na ardhini, wala hakumchoshi Yeye kuzilinda hizo. Na Yeye ndiye aliye na madaraka ya juu zaidi, Mkuu wa wote na vyote. [256.] Hapana kulazimishana katika dini hii. Uongofu umekwisha pambanuka na vile vile upotofu. Basi atakayemkana shetani akamwamini Mwenyezi Mungu, hakika huyo ameshikilia kamba madhubuti isiyokatika. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia, Mjuzi. [257.] Mwenyezi Mungu ni rafiki wa karibu wa wale walioamwamini; huwatoa

kutoka giza nene na kuwaingiza katika mwangaza. Lakini walio kufuru, marafiki zao ni mashetani; huwatoa wao kwenye mwangaza na kuwaingiza katika giza nene. Hao ndio watu wa motoni, watadumu humo.

258. Je, hukufikiria (kisa cha) yule aliyebishanana na Ibrahim (Abraham) kuhusu Mungu wa Ibrahim, kwa sababu (tu) Mwenyezi Mungu alimpa mtu huyo cheo? Pale Ibrahim alipomwambia: ‘Mungu wangu mimi ni yule ambaye hutoa uhai na mauti’. Yule akasema: ‘Mimi pia natoa uhai na mauti!’. Ibrahim akasema: ‘Mwenyezi Mungu hulifanya jua lichomoze upande wa mashariki, hebu basi wewe lifanye lichomoze magharibi!’. Akafedheheka yule aliyemkana Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu hawaongozi watu wasio waadilifu.

259. Au kama yule mtu aliyepita kwenye kijiji kilichobakia magofu matupu, paa za nyumba zake zimeangukiana. Akauliza: ‘Atawezaje Mwenyezi Mungu kukirudisha kijiji hiki kwenye uhai baada ya kutoweka kabisa? Mwenyezi Mungu akamfanya afe kwa miaka mia, kisha akamfufua. Akamwuliza: ‘Umekaa hapa muda gani?’ Akasema: ‘(Labda) nimekaa siku moja au sehemu ya siku’. Akamwabia: ‘Bali umekaa miaka mia. Hebu angalia chakula chako na kinywaji chako, havikuharibika. Halafu mwangalie punda wako! Na ili tukufanye wewe uwe ni kielelezo kwa watu… iangalie hii mifupa yake jinsi tunavyoikusanya na tunavyoivisha nyama. Ilipomwingia akilini, alisema: ‘Sasa natambua kwamba Mwenyezi Mungu ni Mwenye uwezo juu ya kila jambo’.
260. Na pale Ibrahim aliposema: ‘Mola wangu Mlezi! Nioneshe vipi unawaleta kwenye uhai waliokufa?’ (Mwenyezi Mungu) akamwuliza: ‘Je, bado hujaamini?’ Akasema: ‘La hasha! Ni

kwa ajili tu moyo wangu utulie'. Akamwambia: 'Chukua ndege wanne, ukawafuge wakuzoee. kisha (baada ya kuwachinja), uweke juu ya kila kilima kipande cha viwiliwili vyao. Kisha waite… watakujia mbio. Ndipo ujue kwamba Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu kubwa, Mwenye hekima.

261. Mfano wa wale wanaotoa mali zao kwa ajili ya Mwenyezi Mungu ni kama mfano wa punje moja ya mmea iliyochipuza mashuke saba; katika kila shuke mna punje mia. Na Mwenyezi Mungu humzidishia maradufu amtakaye, na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kueneza hisani zake kwa wote, Mjuzi. 262. Wale wanaotoa mali zao katika njia ya Mwenyezi Mungu kisha wasifuatishie kile walikichotoa na masimango wala udhia, wao wana ujira wao kwa Mola wao, wala hawatakuwa na hofu, wala hawatahuzunika. 263. Kauli njema na kusamehe ni bora kuliko sadaka inayofuatishiwa na udhia na Mwenyezi Mungu ni Mkwasi, Mpole. 264. Enyi walioamini! Msizitoe thamani sadaka zenu kwa masimango na maudhi; kama vile yule anayetoa mali yake kwa kuwaonesha watu, wala hamwamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho. Mfano wake ni kama mfano wa jiwe kubwa laini juu yake pana mchanga, mvua kubwa ikalinyeshea na ikaliacha tupu. Hawana uwezo wa kuhifadhi chochote katika walivyovichuma. Na Mwenyezi Mungu hawaongozi watu makafiri.

265. Na mfano wa wale wanaotoa mali zao kwa kutaka radhi ya Mwenyezi Mungu na kujidhaminia (malipo) kwa nafsi zao, ni kama mfano wa bustani iliyo mahali pa juu, ikafikiwa na mvua kubwa ikatoa mazao yake maradufu. Na kama si mvua kubwa iliyoifikia, basi hata manyunyu

(hutosha). Na Mwenyezi Mungu anayaona mnayotenda. 266. Hivi yupo mmoja wenu angependa kuwa na kitalu cha mitende na mizabibu ambacho mito hupita chini yake, akawa anavuna matunda ya kila msimu …. uzee ukamfika, na huku ana watoto wasiojiweza….ndipo kishambuliwe na kimbunga chenye moto kiungue? Hivi ndivyo anavyowabainishia Mwenyezi Mungu Aya ili mpate kufikiria.

267. Enyi walioamini! Toeni katika vizuri mlivyovichuma na katika vile tulivyowatolea ardhini; wala msikusudie kutoa vilivyo vibaya, hali nyinyi wenyewe msingevipokea isipokuwa kwa kuvifumbia macho. Basi jueni kwamba Mwenyezi Mungu ni Mkwasi, Mwenye kusifiwa. 268. Shetani anawatia hofu ya ufukara na anawaamrisha machafu (kama ubakhili) ; na Mwenyezi Mungu anawaahidi msamaha utokao kwake na neema, na Mwenyezi Mungu kawaenezea wote neema zake, Mjuzi. 269. Humpa hekima amtakaye. Na aliyetunukiwa hekima hakika amepewa neema nyingi. Na hawakumbuki (hilo) ila wanaofahamu.

270. Na chochote mtoacho, au nadhiri mnayoweka, basi Mwenyezi Mungu anakijua. Na madhalimu hawana wa kuwasaidia. 271. Mkitoa sadaka zenu wazi wazi, ni sawa. Lakini mkizitoa kwa siri na kuwapa mafukara, hivyo ni bora zaidi kwenu na hilo litawaondoshea baadhi ya maovu yenu; na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa mnayoyafanya. 272. Si juu yako wewe (Muhammad) kuwafanya wafuate mwongozo, lakini Mwenyezi Mungu ndiye humwongoza amtakaye. Na chochote kizuri mkitoacho hiyo ni kwa manufaa yenu wenyewe. Wala msitoe ila kwa kutaka radhi ya Mwenyezi Mungu. Na mali yoyote mnayoitoa mtalipwa kwa ukamilifu wala hamtadhulumiwa. 273. (Sadaka) wapewe mafukara

ambao wamezuiwa kwa sababu ya jambo la Mwenyezi Mungu, wasiweze kwenda huku na huko duniani (kutafuta riziki). Asiyewajua hali zao atawadhania kuwa ni matajiri kwa sababu ya kujizuia (kuomba). Utawafahamu kwa alama zao; hawaombi watu kwa kuwang'ang'ania. Na mali yoyote mnayoitoa, kwa hakika Mwenyezi Mungu anaijua. 274. Wale watoao mali zao usiku na mchana, kwa siri na kwa wazi wazi, wana ujira wao kwa Mola wao; wala haitakuwepo hofu juu yao wala wao hawatahuzunika.

275. Wale wala riba hawatainuka (Siku ya kufufuliwa) ila kama ainukavyo aliyezugwa na shetani kwa wazimu. Hivyo ni kwa sababu wanasema kuwa biashara ni kama riba, na ilihali Mwenyezi Mungu ameruhusu biashara na amekataza riba. Basi aliyefikiwa na onyo kutoka kwa Mola wake Mlezi akakoma, basi yake ni yaliyokwishapita, na suala lake liko kwa Mwenyezi Mungu. Ama waliorudia, hao ndio watu wa motoni; humo watadumu. 276. Mwenyezi Mungu huiondolea baraka riba na huzizidishia sadaka. Na Mwenyezi Mungu hampendi kila asiye na shukrani, mwovu. 277. Hakika wale walioamini wakatenda mema na wakadumu Kuswali na wakatoa Zaka, wao watapata ujira wao kwa Mola wao Mlezi, wala haitakuwepo hofu juu yao wala hawatahuzunika.

278. Enyi walioamini! Mwogopeni Mwenyezi Mungu na sameheni riba zenu zilizosalia, ikiwa mmeamini. 279. Na kama hamtafanya, basi pokeeni ilani ya vita kutoka kwa Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Lakini mkitubu, basi stahiki yenu ni rasilimali zenu pekee, (kwa namna hiyo) hamdhulumu wala hamdhulumiwi. 280. Na iwapo (mdaiwa) yuko katika hali ngumu, basi (mdai) angoje mpaka imuwie wepesi kulipa. Waama mkiligeuza deni kuwa sadaka, hiyo ni bora kwenu,

kama mngejua. 281. Na iogopeni siku ambayo mtarudishwa
kwa Mwenyezi Mungu, kisha kila nafsi ilipwe iliyoyachuma
bila ya wao kudhulumiwa.
282. Enyi walioamini! Mnapokopeshana deni kwa muda
mliokubaliana, basi liandikeni. Na mwandishi aandike baina
yenu kwa uadilifu. Wala mwandishi asikatae kuandika.
Aandike kama vile alivyomfunza Mwenyezi Mungu.
Acha mdaiwa awe ndiye anayeaandikisha, ila amwogope
Mola wake Mlezi na asipunguze chochote katika deni.
Na kama mdaiwa ana matatizo ya akili au ni dhaifu au
hawezi kuandikisha mwenyewe, basi msimamizi wake
aandikishe kwa uadilifu. Na muwashuhudize mashahidi
wawili wanaume kati yenu. Kama hakuna wanaume wawili,
basi ni mwanamume mmoja na wanawake wawili, katika
wale mnaowaridhia kuwa mashahidi, ili kama mmoja wao
akikosea, mwingine amkumbushe. Na mashahidi wasikatae
waitwapo. Wala msikimwe kuandika deni, liwe dogo au
kubwa, hadi muda wake. Huu ndio uadilifu zaidi mbele
ya Mwenyezi Mungu na imara sana kwa ushahidi, na ina
uwezekano mkubwa zaidi wa kuepusha kutiliana shaka.
Ila ikiwa ni biashara ya mkono kwa mkono mnayopeana,
basi hapo si vibaya kwenu msipoandika. Lakini wekeni
mashahidi mnapouziana. Wala asitiwe matatani mwandishi
wala shahidi. Na mkifanya hivyo, basi hilo ni kosa kwenu.
Na mtiini na mumuenzi Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi
Mungu atawaelimisha. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi
kwa kila kitu. 283. Na kama mkiwa safarini na hamkupata
mwandishi, itatosha kukabidhiana kama rehani. Na kama
mmoja wenu akimwamini mwingine, basi aliyeaminiwa
atekeleze uaminifu wake na amwogope Mwenyezi Mungu,

Mola wake Mlezi. Wala msifiche ushahidi. Na atakayeuficha, basi hakika moyo wake ni wenye kuingia dhambini. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi kwa mnayoyatenda.

284. Ni vya Mwenyezi Mungu vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini. Na kama mkidhihirisha yaliyo katika nafsi zenu, au mkiyaficha, Mwenyezi Mungu atawawajibisha juu ya hayo; kisha amghufirie amtakaye, na amwadhibu amtakaye. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye uweza juu ya kila kitu. 285. Mtume na Waumini, wanaamini yaliyoteremshwa kwake kutoka kwa Mola wake Mlezi. Wote wamemwamini Mwenyezi Mungu na Malaika Wake na Vitabu Vyake na Mitume Wake: Hatutofautishi baina ya yoyote katika Mitume wake. Na (waumini) husema: ,Tumesikia na tumetii. Twaomba maghufira yako ewe Mola wetu Mlezi! Marejeo ni Kwako. 286. Mwenyezi Mungu haikalifishi nafsi yoyote ila kwa kadri ya uwezo wake. Faida ya yale iliyoyachuma ni yake, na hasara iliyoyachuma ni juu yake. (Ombeni) Ewe Mola wetu Mlezi! Usituadhibu tukisahau au tukikosa. Na usitutwike mzigo kama ulioutwika wale waliokuwa kabla yetu. Mola wetu Mlezi! Usitubebeshe tusiyoyaweza na utusamehe na utughufurie na uturehemu wewe ndiye Mola wetu na utunusuru na watu makafiri.

# SURA YA FAMILIA IMRAN

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 *Alif laam mim.*

2 Mwenyezi Mungu, hakuna mola isipokuwa Yeye aliye hai
Mwenye kusimamia kila jambo. 3 Amekuteremshia kitabu
chenye taarifa za kweli, kinachothibitisha yaliyokuwa kabla
yake. Na ameteremsha Torati na Injili… 4 Kabla yake, ili
viwe uongozi kwa watu, na ameteremsha Upambanuzi
(Qur'an). Hakika wale waliozikana Aya za Mwenyezi
Mungu wana adhabu kali, na Mwenyezi Mungu ni Mwenye
nguvu Mwenye kulipiza. 5 Hakika kwake Mwenyezi Mungu
hakifichiki chochote kilichomo ardhini wala kilichomo
mbinguni. 6 Yeye ndiye anayewatia sura matumboni jinsi
anavyotaka. Hakuna Mola isipokuwa Yeye Mwenye nguvu
Mwenye hekima.

7 Yeye ndiye aliyekuteremshia Kitabu ndani yake zimo
Aya zilizo dhahiri (maana yake), ambazo ndizo msingi
wa Kitabu hiki, na nyingine zenye kutatanisha. Ama wale
ambao nyoyoni mwao mna upotofu wanazilenga zile
zinazotatanisha katika kitabu hicho, kwa kutafuta ubishi na
kutaka kuzifafanua (kufanana na malengo yao). Na wala
hajui maana yake halisia isipokuwa Mwenyezi Mungu.
Na waliozama katika elimu husema 'tumeamini kitabu
hiki. (Aya) zote hizi zimetoka kwa Mola wetu Mlezi'. Na
hawaonyeki isipokuwa wenye kufahamu. 8 (Husema) Mola

wetu Mlezi! Usizipotoshe nyoyo zetu baada ya kutuongoza na utupe rehema kutoka kwako. Wewe ndiwe mpaji mkuu. [9] Mola wetu Mlezi! Wewe ndiwe Mwenye kuwakusanya watu katika siku isiyo shaka kutokea kwake. Hakika Mwenyezi Mungu havunji miadi.

[10.] Hakika wale ambao wamekufuru hautawafaa kitu utajiri wao na watoto wao kwa Mwenyezi Mungu; na hao ndio kuni za Moto. [11.] Ni kama (ilivyokuwa) desturi ya watu wa Firauni (Pharaoh) na wale waliokuwa kabla yao; walizichukulia Aya zetu kuwa ni uwongo, ndipo Mwenyezi Mungu akawatia adabu kwa sababu ya dhambi zao; na Mwenyezi Mungu ni Mkali wa kuadhibu. [12] Waambie wale waliokufuru: 'Mtashindwa na mtakusanywa mtiwe kwenye Jahannam; na mahali pabaya zaidi pa kupumzikia ni humo.'. [13] Hakika tayari mmepata ishara tosha katika yale majeshi mawili yalipokutana ( vita vya Badr). Jeshi moja likipigana katika njia ya Mwenyezi Mungu na jingine la makafiri, Wakawa wanawaona Waislamu, kwa macho yao, kuwa (idadi yao) ni mara mbili zaidi kuliko wao. Mwenyezi Mungu humpa nguvu amtakaye kwa ushindi wake. Hakika katika hayo kuna mazingatio kwa wenye busara.

[14.] Watu wamepambiwa kupenda matamanio ya wanawake, watoto na mirundo ya dhahabu na fedha, na farasi wazuri, na mifugo na mashamba. Vitu hivyo ni anasa za maisha ya duniani. Ila kwa Mwenyezi Mungu ndiko kwenye marejeo mazuri. [15.] Sema (Ewe Muhammad): Je, niwaambieni vilivyo bora kuliko hivyo? kwa wale wanaomtii na kumuenzi Mwenyezi Mungu wana bustani kwa Mola wao Mlezi, zipitazo mito chini yake, wataishi humo milele. Na pia (watakuwa na) wenza wasafi na (wapate) radhi ya Mwenyezi

Mungu. Na Mwenyezi Mungu huwaona waja wake. 16. Wale ambao husema: Mola wetu Mlezi! Hakika sisi tumeamini, basi tusamehe madhambi yetu, na utuepushe na adhabu ya moto. 17. Wanaofanya subira na wasema kweli na watiifu na wanaotoa sadaka na wanaoomba maghufira kabla ya Alfajiri…

18. Mwenyezi Mungu na Malaika wake na wenye elimu wanashuhudia kwamba hakuna Mola wa kweli ila Yeye tu, mwenye kuwasimamia (viumbe) kwa uadilifu. Hakuna mola isipokuwa Yeye, Mwenye nguvu Mwenye hekima. 19. Hakika dini mbele ya Mwenyezi Mungu ni Uislamu. Na wale waliopewa Kitabu hawakutofautiana (juu ya hili) isipokuwa baada ya kuwafikia wao ujuzi wa hili; kwa sababu tu ya chuki na uadui baina yao. Na anayezikataa Aya za Mwenyezi Mungu basi Mwenyezi Mungu ni Mwepesi wa kuwajibisha. 20. Na kama wakikubishia, sema: Nimejisalimisha kwa Mwenyezi Mungu, mimi na wanaonifuata. Na waambie wale waliopewa Kitabu na wale wasiopewa, Je, mmesilimu? Kama wakisilimu basi wameongoka; na kama wakikengeuka, basi jukumu lako ni kufikisha ujumbe tu. Na Mwenyezi Mungu huwaona waja (wake). 21. Hakika wale ambao wanazikanusha Ishara za Mwenyezi Mungu na wakawaua manabii pasipo haki na wakawaua wanaoamrisha mambo ya haki, wabashirie adhabu iumizayo. 22. Hao ndio ambao matendo yao (mema) yamepotea bure hapa duniani na Akhera pia, na wala hawana yeyote wa kuwanusuru.

23. Je, huwaoni wale waliopewa sehemu ya Kitabu (Torati na Injili) , wanaitwa kwenye Kitabu cha Mwenyezi Mungu ili wahukumiwe kwa mujibu wake, lakini baadhi yao wanageuka wanakikataa. 24. Hivyo ni kwa sababu wanasema:

'moto hautatugusa sisi isipokuwa kwa siku chache tu!' Yakawadanganya yale waliyokuwa wakiyazua katika dini yao. [25.] Basi itakuwaje tutakapowakusanya kwa siku ambayo hapana shaka kuja kwake, na ilipwe kila nafsi, kwa ukamilifu, kile ilichokichuma bila ya wao kudhulumiwa?. [26.] Sema: Ewe Mola Mwenye kumiliki ufalme wote! Unampa madaraka umtakaye na unamvua madaraka umtakaye, na unamtukuza umtakaye na unamdhalilisha umtakaye. Mambo yote mazuri yako mkononi mwako. Hakika wewe ni Mwenye uwezo juu ya kila kitu. [27.] Huuingiza usiku katika mchana na huuingiza mchana katika usiku na humtoa aliye hai kutoka kwa maiti na humtoa maiti kutoka kwa aliye hai. Na unamruzuku umtakaye bila ya kipimo.

[28.] Waumini wasiwafanye Makafiri kuwa marafiki wa kuwalinda badala ya waumini (wenzao). Na mwenye kufanya hivyo, asitarajie chochote (cha msaada) kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Isipokuwa ikiwa kwa kujilinda na shari zao. Na Mwenyezi Mungu anawahadharisheni (mumwogope) Yeye pekee. Na marejeo yenu ni kwa Mwenyezi Mungu. [29.] Sema: Mkificha yaliyomo nyoyoni mwenu au mkiyaweka wazi, Mwenyezi Mungu anayajua. Na anayajua yaliyomo mbinguni na yaliyomo ardhini. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye uweza juu ya kila kitu. [30.] Siku ambayo kila nafsi itakuta mema iliyoyatenda yameletwa mbele, na vile vile uovu iliyoutenda. Itapenda lau kungekuwa na masafa marefu baina ya uovu huo na yeye. Na Mwenyezi Mungu anawahadharisheni Naye. Na Mwenyezi Mungu ni mpole kwa waja. [31.] Sema (Muhammad): Ikiwa mnampenda Mwenyezi Mungu, basi nifuateni mimi,, Mwenyezi Mungu atawapenda na atawaghufiria madhambi

yenu; na Mwenyezi Mungu ni mwenye kusamehe Mwenye
kurehemu. 32. Sema: Mtiini Mwenyezi Mungu na Mtume.
Wakipa nyongo, basi hakika Mwenyezi Mungu hawapendi
makafiri.

33. Hakika Mwenyezi Mungu alimchagua Adam na Nuh
(Noah) na familia ya Ibrahim na familia ya wa Imran juu
ya walimwengu wote. 34. Ni kizazi cha wao kwa wao na
Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia Mwenye kujua.
35. Pale aliposema mke wa Imran: Mola wangu Mlezi!
Nimekuwekea nadhiri kilicho tumboni mwangu kuwa
wakfu; basi nikubalie, hakika Wewe ndiwe usikiaye uliye
mjuzi. 36. Alipomzaa alisema: Mola wangu Mlezi! Nimemzaa
mwanamke-Na Mwenyezi Mungu anajua sana alichokizaa,
na mwanamume si kama mwanamke-nami nimemwita
Maryam (Maria). Na mimi namwombea ulinzi wako, yeye
na kizazi chake, dhidi ya shetani aliyelaaniwa. 37. Basi
Mola wake akamkubalia kwa kabuli njema na akamkuza
makuzi mema. Na akamfanya Zakaria (Zechariah) awe
mlezi wake. Kila mara Zakaria alipoingia katika chumba
cha ibada alimkuta na chakula. Akamwuliza: Ewe Maryam,
unatoa wapi hiki? Akajibu: Vinatoka kwa Mwenyezi Mungu.
Hakika Mwenyezi Mungu humruzuku amtakaye bila kipimo.
38. Pale pale Zakaria akamwomba Mola wake, akasema: Mola
wangu Mlezi! Nipe kutoka kwako mwana mwema. Hakika
wewe ndiwe usikiaye maombi. 39. Malaika wakamlingania
alipokuwa amesimama katika chumba cha kuswalia, kwamba
Mwenyezi Mungu anakupa habari njema za kuzaliwa Yahya
(John) atakayethibitisha neno litokalo kwa Mwenyezi
Mungu, na (atayekuwa) mtu wa kuheshimiwa, mtawa na
Nabii miongoni mwa watu wema. 40. Zakaria akasema: Mola

wangu Mlezi! Nitapataje mtoto na hali ukongwe umenifikia na mke wangu ni tasa? Akasema: Ndiyo hivyo! Mwenyezi Mungu hufanya apendalo. 41. Akasema: Ewe Mola wangu Mlezi! Nipe ishara. Akasema: ishara yako ni kuwa hutaweza kuzungumza na watu kwa siku tatu, isipokuwa kwa ishara tu. (Ila) umtaje sana Mola wako Mlezi, umtakase wakati wa jioni na asubuhi. 42. Na pindi Malaika waliposema: Ewe Maryam! Hakika Mwenyezi Mungu amekuteua na akakutakasa na akakuteuwa (uwe) juu ya wanawake wa ulimwenguni. 43. Ewe Maryam! Mnyenyekee Mola wako na usujudu na urukuu pamoja na wanaorukuu. 44. Hizi ni habari za ghaibu tunazokufunulia; hukuwepo nao walipokuwa wakitupa mishale yao kuwekeana dau; nani kati yao amlee Maryam? Na hukuwa nao walipokuwa wakizozana..

45. Na pale Malaika waliposema: Ewe Maryam! Hakika Mwenyezi Mungu anakupa habari njema ya Neno litokalo kwake; jina lake ni Masiya (Yesu) mwana wa Maria; atakayeheshimika duniani na akhera na kuwa miongoni mwa waliofanywa kuwa karibu zaidi na Mwenyezi Mungu. 46. Na atazungumza na watu akiwa kwenye mbeleko (mtoto mchanga) na katika utu uzima, na atakuwa miongoni mwa watu wema. 47. Maryam akauliza: Ewe Mola wangu Mlezi! Vipi nitapata mtoto na hali hajanigusa mtu yeyote? (Malaika) akasema: Ndiyo hivyo Mwenyezi Mungu, huumba anachokitaka. Anapohukumu jambo, huliambia tu ‘Iwe!’ likawa. 48. Na Mwenyezi Mungu atamfundisha Kitabu na hekima na Torat na Injili. 49. Na (atamteua kuwa) Mtume kwa wana wa Israil (na ujumbe huu): ‘Mimi nimewajia na Ishara kutoka kwa Mola wenu: kwamba natengeneza kwa udongo mfano wa ndege. Kisha nampulizia na anakuwa

ndege (wa kweli) kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Na pia
nawaponesha waliozaliwa hawaoni na wenye ukoma na
nawafufua waliokufa kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Na
nawaambia mnavyokula na mnavyoweka akiba majumbani
kwenu. Hakika katika haya ipo ishara kwenu mkiwa ni wenye
kuamini. 50. Na (nimekuja) kuthibitisha yale yaliyokuwa
kabla yangu katika Torat. Na ili niwahalalishie baadhi ya
mliyoharamishiwa na nimewajia na ishara kutoka kwa
Mola wenu. Kwa hiyo mcheni Mwenyezi Mungu na mnitii.
51. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mola wangu Mlezi na ni
Mola wenu basi mwabuduni. Hii ndiyo njia iliyonyooka.

52. Isa (Yesu) alipohisi kwao kuwa wanang'ang'ania
kutoamini, alisema: Ni wapi wafuasi wangu kwa
(kumnusuru) Mwenyezi Mungu? Wanafunzi wakasema: Sisi
ni wafuasi wako kwa Mwenyezi Mungu. Tumemwamini
Mwenyezi Mungu nawe shuhudia kuwa sisi ni Waislamu.
53. Mola wetu Mlezi! Tumeyaamini uliyoyateremsha, na
tumemfuata Mtume, basi tuandike pamoja na washuhudiao.
54. Na (wengine) wakapanga njama; na Mwenyezi Mungu
akawalipizia njama yao; na Mwenyezi Mungu ndiye bora
ya wote wenye kutibua njama. 55. Kumbuka pale Mwenyezi
Mungu aliposema: Ewe Isa! Mimi nitakutwaa ukiwa
usingizini na nikuinue kwangu, na nikutakase na wale
waliokataa kuamini. Na nitawafanya wale waliokufuata
wawe juu ya wale waliokataa kuamini, mpaka siku ya
kiyama. Kisha marejeo yenu yatakuwa kwangu, nitahukumu
baina yenu katika yale mliyokuwa mkitofautiana. 56. Ama
wale waliokataa imani, nitawaadhibu adhabu kali katika
dunia na Akhera, na hawana wa kuwanusuru. 57. Na wale
walioamini na wakatenda mema, atawatimizia malipo yao

bila kupungua. Na Mwenyezi Mungu hawapendi wenye kudhulumu. 58. Haya tunayokusomea ni katika Ishara na mawaidha yenye hekima.

59. Hakika mfano wa Isa (Yesu) kwa Mwenyezi Mungu, ni kama mfano wa Adam; alimuumba kutokana na udongo, kisha akamwambia: 'Iwe!', akawa. 60. Huu ni ukweli kutoka kwa Mola wako, basi usiwe miongoni mwa wenye shaka. 61. Na watakaobishana nawe katika jambo hili baada kukufikia elimu hii, waambie: Njooni, tuwaite watoto wetu na watoto wenu, na wanawake wetu na wanawake wenu, na sisi wenyewe na nyie, kisha tuombe kwa unyenyekevu tutake laana ya Mwenyezi Mungu iwashukie waongo. 62. Hakika haya ni masimulizi ya kweli, na hapana mola isipokuwa Mwenyezi Mungu. Na hakika Mwenyezi Mungu ndiye mwenye nguvu mwenye hekima. 63. Na wakikengeuka, basi hakika Mwenyezi Mungu anawaelewa waharibifu.

64. Sema: 'Enyi watu wa Kitabu! Njooni kwenye neno tutakalokubaliana sisi na nyinyi: kwamba tusimwabudu yoyote ila Mwenyezi Mungu, na tusimshirikishe na yeyote; na baadhi yetu isiwafanye wengine kuwa Walezi Wakuu (rabbi) badala ya Mwenyezi Mungu'. Wakikataa, semeni: 'Shuhudieni ya kuwa sisi ni waislamu'. 65. Enyi watu wa Kitabu! Kwa nini mnabishana juu ya Ibrahim (Abraham), na ilihali Torat na Injili havikuteremshwa ila baada yake? Hivi hamuwezi kutafakari? 66. Angalieni! (si) nyinyi ndiyo wale wale mliobishana katika yale mliyokuwa na ujuzi nayo, mbona (sasa) mnabishana katika msiyokuwa na ujuzi nayo? Na Mwenyezi Mungu ndiye ajuaye, na nyinyi hamjui (kitu). 67. Ibrahim hakuwa Myahudi wala Mkristo, lakini alikuwa mnyoofu Mwislamu, wala hakuwa katika washirikina.

68. Hakika watu walio karibu zaidi kwa Ibrahim ni wale
waliomfuata yeye na Mtume huyu na wakaamini (ujumbe
wake). Na Mwenyezi Mungu ndiye rafiki wa karibu wa
waumini. 69. Kikundi katika watu wa Kitabu wangependa
kuwapoteza; lakini hawajipotezi ila wenyewe bila kutambua.
70. Enyi watu wa Kitabu! Mbona mnazikanusha Aya za
Mwenyezi Mungu na hali nyinyi ni mashahidi (wa ukweli
wake)? 71. Enyi watu wa Kitabu! Mbona mnauvisha ukweli
kwa uongo, na mnaficha haki na hali mnajua?

72. Kikundi katika watu wa kitabu kilisema: Yaaminini
yale waliyoteremshiwa Waislamu mwanzo wa siku, kisha
muyakanushe mwisho wa siku; huenda (wao wenyewe)
wakarudi nyuma. 73. (Wakaambiana), Msimwamini ila yule
anayefuata dini yenu tu. Sema: hakika uongozi hasa ni
uongozi wa Mwenyezi Mungu. (Ninyi mwaogopa) kuwa
mtu mwingine atapewa kama mliyopewa nyinyi, au (mtu
huyo) atabishana nanyi mbele ya Mola wenu Mlezi! Sema:
hakika vipawa vyote viko mikononi mwa Mwenyezi Mungu,
humpa amtakaye; na Mwenyezi Mungu huwaenezea wote
neema zake, ni Mjuzi mno. 74. Humchagua kumpa rehema
yake amtakaye. Na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye utajiri
mkubwa. 75. Na Miongoni watu wa Kitabu yuko ambaye
ukimpa akuwekee amana mrundo wa mali atakurudishia.
Na katika wao yuko ambaye ukimpa akutunzie senti moja
hakurudishii, isipokuwa ukimsimamia kumdai. Hivyo ni
kwa kuwa wao wanasema: (Mungu) hatupi sisi dhambi
zozote kwa sababu ya (hawa) wajinga mapagani (gentiles).
Wanamzulia uwongo Mwenyezi Mungu, na hali wanajua.
76. Lakini, ndiyo! Yeyote anayetimiza ahadi yake na akamtii
na kumuenzi Mwenyezi Mungu, basi hakika Mwenyezi

Mungu huwapenda (wote) wanaomtii na kumuenzi (bila kubagua).

77. Hakika wale wanaouza Agano la Mwenyezi Mungu na viapo vyao kwa sababu ya thamani ndogo, hao hawatakuwa na fungu lolote huko Akhera, wala Mwenyezi Mungu hatawasemesha wala hatawatazama siku ya Kiyama, na wala hatawatakasa; nao watapata adhabu iumizayo.
78. Na wapo miongoni mwao wanaopinduapindua ndimi zao (wanaposoma) Kitabu ili mdhanie kuwa hayo yanatoka Kitabuni, lakini hayatoki Kitabuni. Na wanasema: Haya yametoka kwa Mwenyezi Mungu, na hali hayakutoka kwa Mwenyezi Mungu; na wanasema uwongo juu ya Mwenyezi Mungu na hali wanajua.
79. Haiwezekani kwa mtu aliyepewa na Mwenyezi Mungu Kitabu na hekima na Unabii, kisha awaambie watu: 'Kuweni waja wangu mniabudu mimi badala ya Mwenyezi Mungu. Lakini (atawaambia): kuweni wanazuoni watiifu kwa Mwenyezi Mungu, kwa kuwa ninyi mnafundisha Kitabu na kwa vile mnakisoma.
80. Wala hatawaamrisha nyinyi kuwafanya malaika na manabii kuwa miungu. Hivi atawaamrisha kumkana Mwenyezi Mungu baada ya kuwa nyinyi Waislamu?

81. Na (kumbukeni watu wa Kiabu) pale Mwenyezi Mungu alipochukua Agano la manabii (kwamba): Kitabu chochote na hekima nitakazowapa, kisha akawajia mtume mwenye kuthibitisha yale mliyo nayo… ni juu yenu kumwamini na kumsaidia. Akawauliza: Je, mmekubali na mtashika agizo langu juu ya hayo? Wakasema: Tumekubali! Akasema: basi shuhudieni, na mimi ni pamoja nanyi katika mashahidi.
82. Na atakayegeuka baada ya hayo, basi hao ndio mafasiki.
83. Je, wanataka dini isiyokuwa ya Mwenyezi Mungu na

hali waliomo mbinguni na ardhini wanamtii yeye, wapende wasipende, na kwake yeye watarejeshwa? 84. Sema: tumemwamini Mwenyezi Mungu na yale tuliyoteremshiwa sisi na yale aliyoteremshiwa Ibrahim (Abraham), Ismail (Ishmael), Is-haq (Isaac) na Yakobo (Jacob) na kizazi chao, na aliyopewa Musa (Moses) na Isa (Yesu) na manabii wengine kutoka kwa Mola wao; hatubagui baina yao hata mmoja na sisi ni wenye kujisalimisha kwake. 85. Na mwenye kutaka usiyokuwa Uislam kuwa dini (yake), kamwe haitakubaliwa kwake. Naye huko Akhera ni miongoni mwa wenye kupata hasara. 86. Vipi atawaongoza Mwenyezi Mungu watu waliokufuru baada kuamini kwao, na wakashuhudia kwamba mtume ni wa kweli na zikawafikia hoja zilizo wazi? Na Mwenyezi Mungu hawaongozi watu waovu. 87. Hao malipo yao ni kustahiki laana ya Mwenyezi Mungu na ya malaika, na ya watu wote. 88. Humo watakaa milele. Hawatapunguziwa adhabu wala hawatapewa nafasi ya kupumzika. 89. Isipokuwa wale ambao wametubia baada ya hayo, na wakajirekebisha. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa maghufira Mwenye huruma. 90. Hakika wale ambao wamekufuru baada ya kuamini, kisha wakazidi kukufuru, haitatakabaliwa toba yao; na hao ndio waliopotea. 91. Hakika wale waliokufuru na wakafa wakiwa makafiri, haitakubaliwa kutoka kwa yeyote hata dhahabu ya ujazo wa dunia nzima lau angetaka kuitoa kama fidia. Hao watapata adhabu iumizayo wala hawatakuwa na wa kuwasaidia.

92. Hamtapata wema mpaka mtoe katika vile mnavyovipenda; na chochote mnachokitoa, basi hakika Mwenyezi Mungu anakijua. 93. Vyakula vyote viliruhusiwa kwa wana wa Israil kabla ya kuteremshwa Torat, isipokuwa

kile ambacho Israili (Yakobo) amekipiga marufuku juu ya nafsi yake. Sema: Leteni Torat muisome mkiwa ninyi ni wakweli. [94.] Basi wenye kumzulia uongo Mwenyezi Mungu baada ya hayo, hao ndio wanaokana ukweli. [95.] Sema: Mwenyezi Mungu amesema kweli. Kwa hiyo fuateni dini ya Ibrahim aliye mnyoofu; wala hakuwa katika washirikina [96.] Hakika nyumba ya kwanza waliyowekewa watu (kwa ajili ya ibada) ni ile iliyoko Makka yenye kubarikiwa na mwongozo kwa viumbe. [97.] Ndani yake mna ishara zilizo wazi (kama) mahali aliposimama Ibrahim. Na mwenye kuingia humo huwa katika amani; Na ni haki ya Mwenyezi Mungu juu ya watu kuhiji nyumba hiyo kwa mwenye kuweza njia ya kuiendea. Na atakayekana, basi Mwenyezi Mungu si muhitaji wa viumbe. [98.] Sema: Enyi watu wa Kitabu! Kwa nini mnazikanusha Aya za Mwenyezi Mungu na hali Mwenyezi Mungu ni shahidi juu ya myafanyayo? [99.] Sema: Enyi watu wa Kitabu! Kwa nini mnamzuilia na njia ya Mwenyezi Mungu mtu aliyeamini, mkaitafutia (kuipindisha) kona kona, na nyinyi mnashuhudia? Na Mwenyezi Mungu si mwenye kughafilika na muyatendayo.

[100.] Enyi walioamini! Mkiwatii baadhi ya waliopewa Kitabu watawarudisha kuwa makafiri baada ya kuamini kwenu. [101.] Na vipi mnakufuru na nyinyi mnasomewa Aya za Mwenyezi Mungu na Mtume wake yupo kati yenu? Na mwenye kushikamana na Mwenyezi Mungu basi ameongozwa katika njia iliyonyooka. [102.] Enyi walioamini! Mtiini na mumuenzi Mwenyezi Mungu ipasavyo, wala msife ila ninyi ni waislamu. [103.] Na Shikamaneni na kamba ya Mwenyezi Mungu nyote wala msifarakane; na kumbukeni neema ya Mwenyezi Mungu juu yenu mlipokuwa maadui,

naye akaziunganisha nyoyo zenu (kwa mapenzi), na mkawa
ndugu kutokana na neema. Na mlikuwa ukingoni mwa shimo
la moto naye akawaokoa nalo. Hivyo ndivyo Mwenyezi
Mungu anavyozibainisha Aya Zake ili mpate kuongoka.
104. Na liwepo miongoni mwenu kundi lenye kulingania
kwenye kheri, na kuamrisha mema na kukataza maovu.
Na hao ndio wenye kufaulu. 105. Wala msiwe kama wale
waliogawanyika wakatofautiana baada ya kuwajia wao dalili
zilizo wazi; na hao ndio wenye adhabu kubwa. 106. Siku
ambayo nyuso zitang'aa na nyuso (nyingine) zitasawijika. Na
ama ambao nyuso zao zitasawijika, (wataambiwa): 'Mbona
mlikufuru baada ya nyie kuamini? Basi onjeni adhabu kwa
sababu ya yale mliyokuwa mkiyakanusha'. 107. Na ama ambao
nyuso zao zitang'aa, watakuwa katika rehema ya Mwenyezi
Mungu. Wao humo watadumu. 108. Hizo ni Aya za Mwenyezi
Mungu, tunakusomea wewe kwa ukweli; na Mwenyezi
Mungu hataki kuwadhulumu viumbe. 109. Ni vya Mwenyezi
Mungu vilivyomo ardhini na vilivyomo mbinguni; na kwa
Mwenyezi Mungu hurejeshwa mambo yote.
110. Ninyi ni umma bora zaidi uliowahi kutokea (uwe
mfano) kwa wanadamu. Mnaamrisha mema na mnakataza
maovu na mnamwamini Mwenyezi Mungu. Na lau watu wa
Kitabu wangeliamini ingekuwa kheri kwao. Wapo miongoni
mwao waumini; lakini wengi wao ni wakaidi, waovu.
111. Kamwe hawataweza kuwadhuruni isipokuwa kuwafanyia
maudhi tu. Na endapo watapigana nanyi watakupeni migongo
(watakimbia), kisha hawatasaidiwa. 112. Wamehukumiwa (na
Mwenyezi Mungu) kuwa wanyonge popote wanapopatikana.
Isipokuwa wakiwa chini ya mkataba (wa kulindwa) kutoka
kwa Mwenyezi Mungu na kulindwa na watu (Waislamu).

Na wamejitakia wenyewe hasira ya Mwenyezi Mungu, na wamehukumiwa (laana ya) kutangatanga. Hivyo ni kwa sababu walikuwa wakizikanusha ishara za Mwenyezi Mungu na kuwaua mitume (wa Mwenyezi Mungu) kinyume na sheria. (Wanafanya) hayo kwa vile wao ni waasi na watu ambao daima wanapetuka mipaka (ya Mwenyezi Mungu).

113. Sio wote wanalingana: katika watu wa Kitabu wako wale walio na msimamo; husoma Aya za Mwenyezi Mungu nyakati za usiku huku wakiinama (kuswali)...
114. Wanamwamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho na wanaamrisha mema na wanakataza mabaya na wanafanya hima hima mambo mema na hao ndio miongoni mwa watu wema. 115. Kheri yoyote watakayoifanya haitakataliwa. Na Mwenyezi Mungu anawajua wenye kimtii na kumuenzi.
116. Hakika wale ambao wamemkana Mwenyezi Mungu, hautawafaa kitu utajiri wao wala watoto wao mbele ya Mwenyezi Mungu, na wao ndio watu wa motoni, humo watakaa milele. 117. Mfano wa wanavyovitoa wao katika maisha haya ya dunia ni kama mfano wa upepo wenye umande wa barafu, ukafika kwenye shamba la watu waovu, ukaliangamiza. Na Mwenyezi Mungu hakuwadhulumu, lakini wanajidhulumu wenyewe.

118. Enyi walioamini! Msiwafanye marafiki wenu wandani watu wasiokuwa katika nyinyi. Hawatashindwa kuwakorofisha. Wanapenda mpate shida. Imekwisha dhihiri chuki yao katika vinywa vyao, Na wayafichayo nyoyoni mwao ni makubwa zaidi. Tumewabainishia ishara ikiwa nyie mtazitia akilini. 119. Ahaa! Nyie ndio mnaowapenda wao, lakini wao hawakupendeni japokuwa nyie mnaviamini vitabu vyote! Na wakikutana nanyi husema: ‘Tumeamini!,

Ama wanapokuwa peke yao huuma vidole dhidi yenu kwa hasira. Sema: ‘Kufeni na hasira zenu! Hakika Mwenyezi Mungu ni mjuzi wa yaliyo nyoyoni. [120.] Liwapatapo jambo jema huwakasirisha. Na liwafikapo jambo baya hulifurahia. Na ninyi mkisubiri na mkajizuia, basi hila zao hazitawadhuru nyie chochote! Hakika Mwenyezi Mungu ni mwenye kuyazunguka wayatendayo.

[121.] Kumbuka (Ewe Muhammad) pale uliporauka asubuhi ukaiacha familia yako, kwenda kuwaandaa Wislamu kwenye vituo vyao, tayari kwa vita (vya Uhud)….Na Mwenyezi Mungu ni mwenye kusikia, Mjuzi. [122.] Pale makundi mawili miongoni mwenu yalipokaribia kuingiwa woga, na hali Mwenyezi Mungu ndiye Mlinzi wao! Ni Mwenyezi Mungu peke yake ndiyo waumini wamtegemee. [123.] Hakika Mwenyezi Mungu aliwanusuru katika vita vya Badr hali nyinyi mlikuwa wanyonge (wachache). Basi mtiini na mumuenzi Mwenyezi Mungu ili mpate kumshukuru. [124.] Pale ulipowaambia waumini: Je, haiwatosheni kwamba Mola wenu Mlezi atawasaidia kwa malaika elfu tatu watakaoteremshwa. [125.] Hasa! Kama mkisubiri na mkamtii na kumuenzi Mwenyezi Mungu, hata kama maadui watawajia ghafla, Mola wenu Mlezi atawaletea malaika elfu tano wanaoshambulia kwa nguvu. [126.] Na Mwenyezi Mungu hakufanya haya isipokuwa iwe bishara njema kwenu na ili nyoyo zenu zitulie. Na hapana nusura ila itokayo kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, Mwenye hekima [127.] Hivyo ni ili alipangue kundi muhimu la (makamanda wa) jeshi la Makafiri, au awakatishe tamaa warejee nyuma mikono mitupu. [128.] Wewe huna uamuzi wowote katika hili: aidha awasamehe au awaadhibu….wao ni watenda mabaya. [129.] Na ni vya Mwenyezi Mungu vyote

vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini. Humsamehe amtakaye na humwadhibu amtakaye. Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa maghufira Mwenye kurehemu.

130. Enyi walioamini! Msile riba ziada juu ya ziada (aidha ziada ya asilimia moja au asilimia nyingi). Na mcheni Mwenyezi Mungu ili mpate kufaulu. 131. Na uogopeni moto ambao umeandaliwa wanaomkana Mwenyezi Mungu. 132. Na mtiini Mwenyezi Mungu na Mtume ili mpate kuhurumiwa. 133. Na harakisheni kuomba maghufira kwa Mola wenu na pepo ambayo upana wake ni (kama wa) mbingu zote na ardhi, imeandaliwa wenye kumcha Mungu. 134. Ambao hutoa katika (njia ya Allah) wakati wa raha na shida na wazuiao hasira (zao) na wanaowasamehe binadamu wenzao. Na Mwenyezi Mungu huwapenda wafanyao hisani. 135. Na ambao wakifanya jambo ovu au wakidhulumu nafsi zao humkumbuka Mwenyezi Mungu na kuomba msamaha kwa dhambi zao. Na nani anayesamehe dhambi isipokuwa Mwenyezi Mungu? Na wasiwe wakaidi wakaendelea na waliyoyafanya hali wanajua. 136. Hao malipo yao ni msamaha utokao kwa Mola wao Mlezi, na mabustani ambayo mito ya maji hububujika chini yake. Humo ni wenye kukaa milele. Ni ujira mwema ulioje kwa wale wanaoyafanyia kazi (amali) haya. 137. Kabla yenu zilipita aina chungu nzima za staili za maisha. Basi tembeeni duniani muone ulikuwaje mwisho wa wale waliosema haya ni uwongo! 138. Haya ni maelezo mepesi kwa watu, ni mwongozo na ilani kwa wamchao Mwenyezi Mungu.

139. Wala msijione wanyonge wala msihuzunike, kwani nyinyi ndio mlio juu ikiwa nyinyi ni waumini wa kweli. 140. Ikiwa mmepata majeraha, basi hao jamaa wengine pia

wamepata majeraha mfano wa yenu. Na siku za namna hii tunawaletea watu kwa zamu, ili Mwenyezi Mungu apate kuwatambulisha walioamini kwa dhati miongoni mwenu, na ili awateuwe watakaokufa mashahidi (katika vita) miongoni mwenu. Na Mwenyezi Mungu hawapendi wakandamizaji. [141.] Na pia, ili Mwenyezi Mungu awatakase wale walioamini kwa dhati na awaangamize makafiri. [142.] Je, mwadhani mtaingia peponi na hali Mwenyezi Mungu bado hajawatambua (hajawajaribu) wale waliopigana kwa ushupavu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu miongoni mwenu, na kuwatambua wale waliovumilia? [143.] Kwa hakika mlikuwa mkitamani mauti kabla ya kukutana nayo. Sasa mmeyaona (mbele yenu) na huku mnayatazama (kwa macho yenu).

[144.] Muhammad hakuwa (mwengine) ila Mtume. Kabla yake wamepita mitume wengine. Je, akifa au akiuawa mtageuka mrudi nyuma? Na atakayerudi nyuma hatamdhuru kitu Mwenyezi Mungu na Mwenyezi Mungu atawalipa wenye kushukuru. [145.] Na haiwezekani nafsi yeyote kufa ila kwa idhini ya Mwenyezi Mungu, kwa mujibu wa ilivyoandikwa ajali yake. Na anayetaka malipo ya dunia tutampa humo humo na anayetaka malipo ya akhera tutampa huko; na tutawalipa wenye kushukuru. [146.] Ni manabii wangapi walipigana wakiandamana nao wasomi wengi wa dini. Hawakuyumba kutokana na (majanga) yaliyowasibu katika njia ya Mwenyezi Mungu, wala hawakuhisi unyonge, wala hawakujisalimisha. Na Mwenyezi Mungu anawapenda wanaosubiri. [147.] Wala haikuwa kauli yao ila tu kusema: ‘Ewe Mola wetu Mlezi! Tughufirie dhambi zetu na chochote tulichokifanya kilichopita mipaka ya wajibu wetu, na ifanye miguu yetu iwe imara, na utunusuru juu ya watu makafiri.

[148.] Mwenyezi Mungu akawapa malipo ya duniani na malipo bora ya akhera na Mwenyezi Mungu anawapenda watendao mazuri.

[149.] Enyi walioamini! Mkiwatii ambao wamekufuru watawarudisha nyuma, na hapo mtageuka kuwa wenye kupata hasara. [150.] Bali Mwenyezi Mungu ndiye Mlinzi wenu, naye ndiye bora zaidi kuliko walinzi wote. [151.] Tutatia hofu katika nyoyo za ambao wamekufuru kwa sababu ya kumshirikisha Mwenyezi Mungu na kile ambacho hakukiteremshia uthibitisho wowote; na makazi yao ni motoni, maskani mabaya mno kwa watendao maovu. [152.] Na hakika Mwenyezi Mungu aliwatimizia ahadi yake mlipokuwa mkiwaua maadui kwa idhini yake, hadi mlipolegea na na kuanza kuzozana juu ya amri (ya Mtume) na mkaasi baada ya (Mwenyezi Mungu) kuwaonesha vile mnavyovipenda (nyara za vita). Miongoni mwenu kuna anayependa zaidi dunia, na kuna miongoni mwenu apendaye Akhera. Kisha akawafanya msishughulike na maadui, ili awajaribuni. Sasa amekwisha wasamehe. Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa hisani kwa waumini. [153.] Na kumbukeni pale mlipokuwa (mnakimbia) na kupanda kilimani, hamumsikilizi yeyote, na huku Mtume akiwaita nyuma yenu. Ndipo Mwenyezi Mungu akawapa majonzi juu ya majonzi, ili (awafunze) msisisikite juu ya mlivyovikosa (nyara za vita) wala yaliyowafika. Na Mwenyezi Mungu ana habari za mnayoyatenda.

[154.] Kisha baada ya majonzi akawateremshia utulivu; usingizi uliofunika kundi katika nyinyi. Na kundi jingine wasiwasi ukazitawala nyoyo zao, wakawa wanamshuku vibaya Mwenyezi Mungu kutokana na ujinga wao. Wakasema: ‘Je sisi tungeweza kufanya chochote katika

jambo hili? Waambie: hasa! Jambo lote hili linamhusu Mwenyezi Mungu. (Watu hao) huficha katika nyoyo zao mambo wasiyokuonesha wazi. Wanasema: ‘Kama tungekuwa na uwezo wa kufanya chochote katika jambo hili tusingeuawa bure hapa!’ Waambie: ‘hata kama mngelibaki majumbani mwenu, wangetoka wale walioandikiwa kufa kwa kuuawa, wakaenda mahali pao pa kuangukia wafe. (Haya yote yametokea)Ili Mwenyezi Mungu ayajaribu yaliyomo vifuani mwenu na ayasafishe yaliyomo nyoyoni mwenu. Na Mwenyezi Mungu anayajua yaliyomo vifuani. 155. Hakika wale waliokimbia miongoni mwenu siku yalipokutana majeshi mawili, Shetani ndiye aliyewatelezesha kwa sababu ya baadhi ya makosa waliyoyafanya. Basi Mwenyezi Mungu amekwisha wasamehe. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa Maghufira, Mpole.

156. Enyi walioamini! Msiwe kama wale waliokufuru na wakasema kuhusu ndugu zao waliposafiri katika nchi au walipokuwa vitani: ‘laiti wangekuwa kwetu wasingekufa wala wasingeuawa’. Hilo Mwenyezi Mungu analifanya liwe sababu ya majuto katika nyoyo zao. Na Mwenyezi Mungu ndiye anayesababisha uhai na anayesababisha mauti, na Mwenyezi Mungu anaona mnayoyafanya. 157. Na kama mkiuawa katika njia ya Mwenyezi Mungu au mkifa, basi maghufira na rehema kutoka kwa Mwenyezi Mungu ni bora kuliko yale wanayoyakusanya. 158. Na kama mkifa au mkiuawa, nyote mtakusanywa kwa Mwenyezi Mungu. 159. Ni Kwa sababu ya rehema itokayo kwa Mwenyezi Mungu, (ewe Muhammad) ndiyo ukawa mpole kwao. Laiti ungelikuwa jeuri,fedhuli, mwenye moyo wa ukatili, wangekukimbia. Basi wasamehe na uwaombee maghufira na ushauriane nao

katika mambo. Lakini utakapochukua uamuzi, mtegemee Mwenyezi Mungu tu. Hakika Mwenyezi Mungu anawapenda wanaomtegemea Yeye. 160. Mwenyezi Mungu akitaka kuwanusuru, hapana wa kuwashinda. Na kama akiwatupa basi ni nani mwingine atakayewanusuru nyie badala yake? Na waumini wa dhati wamtegemee Mwenyezi Mungu pekee.

161. Haiwezekani kwa Nabii yeyote kufanya khiyana (katika ugavi wa ngawira). Na yeyote anayefanya hiyana, atayaleta yale aliyoyafanyia hiyana Siku ya Kiyama, kisha italipwa kila nafsi iliyoyachuma, wala hawatadhulumiwa. 162. Je, hivi anayefuatia yanayo mridhisha Mwenyezi Mungu atakuwa sawa na yule aliyejitakia mwenyewe hasira za Mwenyezi Mungu na makazi yake yakawa ni Jahannam? Hapo ni mahali pabaya pa kurejea. 163. Wao ni daraja tofauti mbele ya Mwenyezi Mungu na Mwenyezi Mungu ni mwenye kuyaona yale wanayoyafanya. 164. Hakika Mwenyezi Mungu amewaneemesha waumini kwa kuwaletea Mtume miongoni mwao, anayewasomea Aya zake na anayewatakasa na kuwafundisha Kitabu na hekima. Ingawaje hapo nyuma walikuwa katika upotofu wa dhahiri.

165. Hivi inakuwaje nyie lilipowafika janga (siku ya vita vya Uhud), ambalo ninyi tayari mmewatia maadui zenu mara mbili mfano wake (katika vita vya Badr), mnauliza: limetoka wapi hili? Waambie, hilo linatoka kwenu wenyewe. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye uwezo juu ya kila kitu. 166. Na yaliyowasibu siku yaliopambana majeshi mawili ni kwa idhini ya Mwenyezi Mungu, ili awajaribu waumini. 167. Na ili awatambulishe waliokuwa wanafiki. Walipoambiwa ‘Njooni mpigane kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, au (angalau) fanyeni doria, Walisema,’Lau tungejua

kupigana tungewafuata'. Wao siku ile walikuwa karibu mno na ukafiri kuliko imani. Wanasema kwa midomo yao yale yasiyokuwa nyoyoni mwao. Na Mwenyezi Mungu anayajua vizuri wanayoyaficha. 168. Wale waliosema kuhusu ndugu zao (waliouawa) na huku wao wenyewe wamejikalia majumbani:'Kama wangetusikiza wasingeuawa!'. Sema: 'Ziepusheni nafsi zenu na kifo basi, ikiwa mnasema kweli'.

169. Na usifikirie kabisa kuwa wale waliouawa katika njia ya Mwenyezi Mungu wamekufa, bali wako hai mbele ya Mola wao Mlezi wakipokea ruzuku zao. 170. Wakifurahia aliyowapa Mwenyezi Mungu katika hisani zake, na wakipokea habari nzuri nzuri juu ya wale ambao (watakuwa mashahidi) baada yao, lakini bado hawajajiunga nao: ya kwamba haitakuwa hofu juu yao wala hawatahuzunika.
171. Wanashangilia neema na fadhila za Mwenyezi Mungu, na kwamba Mwenyezi Mungu hapotezi malipo ya waumini.
172. Wale waliomwitikia Mwenyezi Mungu na Mtume (hata) baada ya majeraha yaliyowapata; kwa waliofanya wema na wakajikinga na mabaya wana ujira mkubwa. 173. Wale ambao watu (wanafiki) waliwaambia: 'Kwa kweli jeshi kubwa limekusanyika kuwaangamiza nyie, waogopeni!' Lakini hayo hayakuwaongezea isipokuwa imani, wakasema: 'Mwenyezi Mungu pekee anatutosha, na bora ya mwenye kutegemewa ni Yeye'. 174. Basi wakarejea wakiwa na neema ya Mwenyezi Mungu na fadhila yake, hakuna baya lililowagusa, na wakafuata yanayomridhisha Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu ni mwenye hazina isiyo kipimo. 175. Hakika huyo ni shetani tu, anawatia hofu marafiki zake, basi msiwaogope na niogopeni Mimi, ikiwa nyinyi ni waumini.

176. Wala wasikuhuzunishe wale wanaokimbilia ukafiri.

Hakika wao hawatamdhuru kitu Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu anapanga asiwape fungu lolote huko akhera. Nao wana adhabu kubwa. 177. Hakika wale wanaonunua ukafiri kwa (kuuza) imani, hawatamdhuru kitu Mwenyezi Mungu na wana adhabu iumizayo. 178. Wala wasidhanie kabisa wale waliokufuru kwamba huu muda mrefu tunaowapa (wa ku-injoy) ni kheri kwao. Hakika tunawarefushia muda ili waendelee tu na dhambi zao. Na inawangojea adhabu yenye kudhalilisha. 179. Haiwezekani kwa Mwenyezi Mungu kuwaacha waumini katika hali mliyo nayo, hadi awapambanue wabaya na wema. Na wala haiwi kwa Mwenyezi Mungu kuwajulisheni mambo ya ghaibu. Lakini Mwenyezi Mungu humteua amtakaye katika mitume yake. Basi mwaminini Mwenyezi Mungu na mitume Wake. Na kama mtaamini na kumtii na kumuenzi Mwenyezi Mungu, basi mtakuwa na ujira mkubwa.

180. Na wasidhanie kabisa wale ambao wanavifanyia ubakhili vile alivyowapa Mwenyezi Mungu katika hazina yake, kuwa hilo ni jambo jema kwao, bali ni baya kwao. Watafungwa kongwa (shingoni) na hivyo wanavyovifanyia ubakhili hapo Siku ya Kiyama. Ni wa Mwenyezi Mungu urithi wa mbingu na ardhi; na Mwenyezi Mungu ana habari ya mnayoyatenda. 181. Mwenyezi Mungu amekwishasikia kauli ya wale (Mayahudi) waliosema: Mwenyezi Mungu ni fukara na sisi ni matajiri. Tutayasajili yale waliyoyasema; na pia kuwaua kwao Mitume kinyume na sheria; na tutawaambia (siku ya Kiyama): onjeni adhabu ya kuungua. 182. Hayo ni kwa sababu ya yale (maovu) yaliyotangulizwa na mikono yenu na kwamba Mwenyezi Mungu si dhalimu kwa waja. 183. Waliosema: Hakika Mwenyezi Mungu amekubali ahadi

yetu kuwa hatutamwamini mtume yeyote mpaka atuletee
kafara litaloteketezwa na moto (utokao mbinguni), Sema:
Mbona walikwisha kujieni mitume wengi kabla yangu kwa
hoja zilizo waziwazi na pamoja na hivyo mnavyosema…
kwa nini basi mliwaua, kama nyie ni wakweli? 184. Kama
wakisema wewe ni mwongo, basi hakika waliambiwa kuwa
waongo mitume kabla yako waliokuja na hoja waziwazi na
maagizo yaliyoandikwa na kitabu chenye mwanga. 185. Kila
roho itaonja mauti. Na kwa hakika mtalipwa ujira wenu
kamili hapo Siku ya Kiyama. Basi atakaye epushwa mbali na
moto akaingizwa peponi, hakika huyo amefaulu. Na maisha
ya dunia si kitu ila ni starehe ya udanganyifu.

186 Kwa hakika mtapata misukosuko katika mali zenu na
nyie wenyewe. Na mtasikia udhia mwingi kutoka kwa wale
waliopewa Kitabu kabla yenu na kutoka kwa mapagani wa
Kiarabu. Na mkisubiri na mkimtii na kumuenzi Mwenyezi
Mungu, kwa kweli hilo ndiyo azimio la ujasiri katika mambo.
187 Na (wakumbushe ewe Muhammad) pale Mwenyezi
Mungu alipochukua Agano na wale waliopewa Kitabu kuwa:
'lazima mkifafanue kwa watu wala hamtokificha'. Lakini
wakakitupa nyuma ya migongo yao na wakakibadilisha kwa
thamani ndogo (ya dunia). Basi ni kiovu walichokinunua.
188 Usiwadhanie kabisa wale ambao wanafurahia (maovu)
waliyoyafanya na wakapenda kusifiwa kwa wasiyoyafanya
- usiwadhanie kabisa kuwa wataokoka na adhabu, na wao
wana adhabu iumizayo. 189 Na ufalme wa mbinguni na
ardhini ni wa Mwenyezi Mungu na Mwenyezi Mungu ni
mwenye uwezo juu ya kila kitu.

190. Hakika katika kuumbwa mbingu na ardhi na kupishana
kwa usiku na mchana, ziko ishara (za kuwepo Mwenyezi

Mungu) kwa wenye kufahamu. 191. Ambao humtaja
Mwenyezi Mungu katika hali ya kusimama, kukaa na kulala,
na wanatafakari kuumbwa mbingu na ardhi, (wakijisemea)
'Mola wetu Mlezi! Hukuviumba hivi bure. Umetukuka na
hilo! Basi utuepushe na adhabu ya moto. 192. Mola wetu Mlezi!
Hakika utakayemwingiza motoni utakuwa umemwaibisha.
Na hawatakuwepo wa kuwaokoa madhalimu. 193. Mola
wetu Mlezi! Hakika sisi tumemsikia mwenye kulingania
anayelingania kwenye imani kwamba: 'mwaminini Mola
wenu Mlezi!' nasi tukaamini. Mola wetu Mlezi! Tusamehe
madhambi yetu na utufutie makosa yetu na utujaalie tufe
pamoja na watu wema. 194. Mola wetu Mlezi! Na utupe
uliyotuahidi kwa kupitia mitume yako, wala usitufedheheshe
Siku ya Kiyama. Hakika wewe huvunji ahadi.

195. Ndipo Mola wao Mlezi akawajibu kwamba: 'Kamwe
mimi sitaruhusu ipotee amali ya yeyote miongoni mwenu,
awe mwanamume au mwanamke, kwani nyie ni nyinyi kwa
nyinyi. Basi wale waliohama na waliotolewa kwa nguvu
makwao, wakapata maudhi kwa ajili yangu, wakapigana
na wakauawa, bila shaka nitawafutia makosa yao na
nitawaingiza katika mabustani ambayo hupita mito ya maji
chini yake. Ndiyo malipo yanayotoka kwa Mwenyezi
Mungu; na kwa Mwenyezi Mungu kuna malipo mema.
196. Kusikuhadae kabisa kurandaranda nchini kwa wale ambao
wamekufuru; 197. Ni starehe ndogo tu. Kisha makazi yao ni
Jahannam; ni mahali pabaya mno pa kupumzikia. 198. Lakini
wale wanaomtii na kumuenzi Mola wao Mlezi watakuwa na
mabustani ambayo mito ya maji hupita chini yake. Watakaa
humo milele. Ndiyo mahali pa kufikia walipoandaliwa na
Mwenyezi Mungu. Na vilivyoko kwa Mwenyezi Mungu ni

vizuri sana kwa watu wema. 199. Na hakika miongoni mwa watu wa Kitabu wako wale wanaomwamini Mwenyezi Mungu na yaliyoteremshwa kwenu na yaliyoteremshwa kwao, kwa kumnyenyekea Mwenyezi Mungu. Hawaziuzi Aya za Mwenyezi Mungu kwa thamani duni (ya dunia). Hao wana ujira wao kwa Mola wao Mlezi. Hakika Mwenyezi Mungu ni mwepesi wa kuhukumu. 200. Enyi walioamini! Fanyeni subira na mvumilie na kuweni macho, na mtiini na mumuenzi Mwenyezi Mungu ili mpate kufaulu.

4. Sura An-Nisaa

# SURA YA WANAWAKE

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 Enyi watu! Mcheni Mola wenu ambaye amewaumba nyie kutokana na mtu mmoja, na akamuumba mkewe kutokana na mtu huyo huyo. Na akasambaza wanaume wengi na wanawake kutokana na watu hao wawili. Na mtiini na mmuenzi Mwenyezi Mungu ambaye kupitia kwake nyinyi mnaombana haki zenu. Na pia mtii na kuwaheshimu wazazi, ndugu na jamaa. Hakika Mwenyezi Mungu daima ni mkaguzi juu yenu. 2 Na wapeni mayatima mali zao wala msibadilishe kibaya kwa kizuri. Wala msile mali zao (kwa kuzichanganya) pamoja na mali zenu; hakika hiyo daima ni dhambi kubwa sana. 3 Na kama mkihofia kutowafanyia uadilifu mayatima, basi oeni mnaowapenda katika wanawake, wawili wawili na watatu watatu na wanne wane. Na mkihofia kuwa hamuwezi kufanya uadilifu (baina yao), basi oeni mmoja tu, au yule

(mateka mwanamke) ambaye mikono yenu ya kuume imemmiliki. Hilo liko karibu zaidi na kuwazuia nyie msiende kinyume cha uadilifu. [4] Na wapeni wanawake mahari yao kama zawadi. Kama wakiwaachia wenyewe katika hayo mahari, kwa ridhaa yao, basi chukueni kwa kutosheka na kuonesha shukurani.

[5] Wala msiwaachie watovu wa akili mali zenu ambazo Mwenyezi Mungu amewajaalia kuwa sababu ya kukimu maisha yenu. Lakini walisheni na wavisheni kwa mali hiyo, na muwaambie maneno mazuri. [6] Na wajaribuni mayatima mpaka wafikie umri wa kuoa. Mkiwaona wana weledi, basi wapeni mali zao. Wala msizile kwa kuzifuja na kwa pupa kwa (kuhofia) watakuja kuwa watu wazima (waihodhi mali yao). Aliye tajiri ajizue kabisa (kutumia mali hiyo). Ama fukara atumie kwa kiasi kinachokubalika. Na mtakapowakabidhi mali zao, basi leteni mashahidi watakaowashuhudia; na Mwenyezi Mungu anatosha kuwa Mhasibu. [7] Wanaume wana fungu katika mali waliyoiacha wazazi wawili na ndugu wa karibu. Na wanawake pia wana fungu katika walichoacha wazazi wawili na ndugu wa karibu, kiwe kidogo au kingi - fungu la lazima, lililokadiriwa. [8] Na wakati wa kugawanya wakahudhuria ndugu (wengine) wa karibu na (au) mayatima na maskini, basi wapeni nao kitu katika hiyo na waambieni maneno mazuri. [9] Na waache wale ambao (wanagawa mali hizo) wawe na hofu ile ile ambayo wangewahofia watoto wao wanyonge lau wangewaacha nyuma yao. Basi na wamwogope Mwenyezi Mungu na waseme kauli iliyo sawa. [10] Hakika wale wanaokula mali ya yatima kwa dhuluma, hapana shaka wanakula moto matumboni mwao; na wataingia katika moto uwakao.

11. Mwenyezi Mungu anawapa mwongozo juu ya watoto
wenu (katika mirathi, kuwa); fungu la mtoto mwanamume
ni kama fungu la watoto wawili wa kike. Wakiwa binti
wawili au zaidi, basi watapata theluthi mbili za alichokiacha
(marehemu), na akiwa ni mmoja, basi atapata nusu. Na
wazazi wake wawili kila mmoja atapata sehemu ya sita ya
urathi akiwa (marehemu) ana mtoto. Akiwa hana mtoto, na
akarithiwa na wazazi wake wawili (pekee), basi mama yake
atapata theluthi moja. Ama akiwa anao ndugu, basi mama yake
atapata sehemu ya sita ya mirathi. (Hayo ni) baada ya kutoa
za wosia wa marehemu au deni (lake). Baba zenu na watoto
wenu hamjui ni yupi katika wao aliye karibu zaidi kwenu kwa
manufaa. (Mafungu haya) yamekadiriwa na kuwajibishwa
na Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu daima
ni Mjuzi, Mwingi wa hekima. 12. Nanyi mtapata nusu ya
walichokiacha wake zenu ikiwa hawana watoto. Ikiwa wana
watoto, basi mtapata robo ya walichokiacha, baada ya kutoa
za wosia waliyousia au deni. Na wao (wake) watapata robo
ya mlichokiacha ikiwa hamna mtoto. Ikiwa mna mtoto, basi
watapata sehemu ya nane ya mlichokiacha, baada ya kutoa
za wosia mliyousia au kulipa deni. Ikiwa mwanamume au
mwanamke anayerithiwa hana mtoto wala wazazi, lakini ana
ndugu wa kiume au wa kike, basi kila mmoja katika wao
atapata sehemu ya sita ya mirathi. Ama wakiwa wengi zaidi
ya mmoja, basi watashirikiana katika theluthi, baada ya kutoa
za wosia uliousiwa au kulipa deni, bila ya yeyote kukosa
haki yake. Haya ndiyo maelekezo yatokayo kwa Mwenyezi
Mungu; na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi, Mpole. 13. Hiyo ni
mipaka ya Mwenyezi Mungu. Na mwenye kumtii Mwenyezi
Mungu na Mtume wake, atamwingiza katika mabustani

ambayo mito ya maji hupita chini yake, watakaa humo milele. Na huko ndiko kufuzu kukubwa. 14. Na mwenye kumwasi Mwenyezi Mungu na Mtume wake na akapetuka mipaka yake, atamtia katika moto, ni mwenye kudumu humo, na atapata adhabu idhalilishayo.

15. Na ambao hufanya ufuska miongoni mwa wake zenu, leteni mashahidi wane miongoni mwenu (waume) kushuhudia dhidi yao. Wakileta ushahidi ( wa kukoa manza), wazuilieni wake hao majumbani mpaka wafikwe na mauti au Mwenyezi Mungu awafanyie njia nyingine. 16. Na wanaume wawili ambao hufanya uchafu katika ninyi, waadhibuni. Na wakitubu na wakajirekebisha, basi achaneni nao. Hakika Mwenyezi Mungu ni mwingi wa kukubali toba mwenye kurehemu. 17. Hakika toba ikubaliwayo na Mwenyezi Mungu ni ya wale tu wafanyao uovu kwa kutojua kisha wakatubia haraka. Hao ndio ambao Mwenyezi Mungu huwakubalia toba zao na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi; na Mwenye hekima. 18. Lakini msamaha hawapewi wale ambao hufanya maovu mpaka mmoja wao akafikiwa na mauti akasema: ‘sasa mimi nimetubia’. Wala ambao hufa wakiwa makafiri; hao tumewaandalia adhabu iumizayo.

19. Enyi ambao wameamini! Si halali kwenu kuwarithi wanawake kwa nguvu; wala msiwafanyie ukatili (waondoke) ili muwapokonye baadhi ya vitu mlivyowapa. Isipokuwa watakapofanya ufuska ulio wazi (ndio mnaweza kuchukua baadhi ya mahari mliyowapa). Na kaeni nao kwa wema. Na kama mkiwachukia, basi huenda mkachukia kitu na Mwenyezi Mungu akaleta kheri nyingi kupitia kwake. 20. Lakini mkitaka kumbadilisha mke mlete mwingine mahali pake; basi hata mkiwa mmempa yule mmoja wao (mliemwacha) mali

nyingi, kamwe msichukue katika mlichowapa kitu chochote. Hivi yumkinije mkichukue kwa dhuluma na kwa dhambi ya wazi?
21. Mtaichukuaje? Na ilihali mmeingiliana ndani na hao wanawake na wakachukua kutoka kwenu ahadi kubwa?
22. Wala msiwaoe wanawake walioolewa na baba zenu, ila zile ndoa ambazo tayari zilikwishafanyika huko nyuma (kabla ya Uislamu/kusilimu). Hakika hilo lilikuwa ni ufuska, la kuchukiza (kwa Allah) na ilikuwa desturi mbaya.

23. Mmeharamishiwa (kuwaoa) mama zenu na mabinti zenu na dada zenu na shangazi zenu na mama wadogo zenu na wapwa wa kike, na mama zenu waliowanyonyesha na dada zenu wa kunyonya, na mama-wakwe, na binti zenu wa kambo walio katika himaya yenu ambao wamezaliwa na wake zenu mliowajamii. Mkiwa hamkuwajamii hapana vibaya kwenu. Na (waliokuwa) wake wa watoto wenu waliotoka katika migongo yenu, na (pia imeharamishwa) kuoa dada wawili, isipokuwa kwa yaliyokwishafanyika. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa maghufira Mwenye kurehemu.
24. Na pia (mmeharamishiwa) wanawake walio katika ndoa, isipokuwa wale wanawake (mateka) waliomilikiwa na mikono yenu ya kuume. Ndiyo Sharia ya Mwenyezi Mungu kwenu. Na mmehalalishiwa wasiokuwa hao (kwa sharti), muwachumbie kwa mali zenu kwa kuwaoa kihalali bila kufanya zina. Basi kwa chochote mlichojifurahisha nacho kutoka kwao, wapeni mahari yao yaliyo lazimu. Wala hapana ubaya kwenu kwa kiasi mtakachokubaliana zaidi ya wajibu. Hakika Mwenyezi Mungu daima ni Mjuzi, Mwingi wa hekima.
25. Na asiyeweza miongoni mwenu kupata mali ya kuoa wanawake waungwana waumini, basi (na aoe) katika wasichana wenu walioamini wanaomilikiwa na mikono yenu

ya kuume (mateka); na Mwenyezi Mungu anajua sana imani yenu. Nyinyi (mlioamini) ni wenyewe kwa wenyewe. Basi waoeni kwa idhini ya wamiliki wao na muwape mahari yao kwa mujibu wa ada. Wawe ni wenye kujistahi si waasherati wala si mahawara. Watakapoolewa kisha wakafanya ufuska, adhabu yao itakuwa ni nusu ya adhabu iliyowekwa kwa wanawake waungwana. Ruhusa hii ni kwa yule miongoni mwenu anayehofu kufanya dhambi. Na mkisubiri ni bora kwenu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa maghufira Mwenye kurehemu.

26. Mwenyezi Mungu anataka kuwabainishia na kuwaongoza mwendo wa waliokuwa kabla yenu na awatakabalie toba. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi Mwenye hekima. 27. Na Mwenyezi Mungu anataka kuwatakabalia toba, na wale ambao hufuata matamanio wanataka mkengeuke mkengeuko mkubwa. 28. Mwenyezi Mungu anataka kuwafanyia wepesi, kwani mwanadamu ameumbwa dhaifu.

29. Enyi ambao wameamini! Msiliane mali zenu wenyewe kwa wenyewe kwa jia za batili; isipokuwa itakapokuwa ni biashara kwa kuridhiana wenyewe. Wala msijiue. Hakika Mwenyezi Mungu ni mwenye rehema kwenu. 30. Na atakayefanya hilo kwa uadui na dhulma, tutamtia motoni. Na hilo kwa Mwenyezu Mungu ni jepesi. 31. Mkiyaepuka (madhambi) makubwa mnayokatazwa, basi tutawafutia makosa yenu (madogo) na tutawaingiza mahali pazuri. 32. Wala msitamani alichowafadhili Mwenyezi Mungu baadhi yenu kuliko baadhi nyingine. Wanaume wamekadiriwa sehemu katika wanavyovichuma, na wanawake pia wamekadiriwa sehemu katika wanavyovichuma. Na mwombeni Mwenyezi Mungu fadhila zake. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa

kila kitu. [33.] Na wote nyie tumewafanya muwe warithi wa vile walivyoviacha wazazi (wenu) wawili na jamaa wa karibu, na wale ambao mmekula nao yaini za udugu.…wapeni fungu lao. Hakika Mwenyezi Mungu ni shahidi wa kila kitu.

[34.] Wanaume ni wasimamizi wa wanawake, kwa sababu ya kuwa Mwenyezi Mungu amewapa fadhila zaidi baadhi ya binadamu juu ya wengine, na kwa sababu ya mali zao walizozitoa. Basi wanawake wema ni wale wenye kutii na kuchunga vile Mwenyezi Mungu alivyoamuru wavichunge, hata wakati wa kutokuwepo (waume zao). Na wale ambao mnawahofia utovu wa utiifu, (kwanza) wapeni nasaha, kisha muwahame katika vitanda, hatimaye (ikishindikana) muwachape. Watakapowatii, msiwatafutie visingizio vingine. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mtukufu, Mkubwa. [35.] Na endapo (nyinyi) mkihofia mfarakano baina yao, basi pelekeni mwamuzi kutoka upande wa mume na mwamuzi kutoka upande wa mke. Kama kweli wote wawili wanataka kusuluhisha, Hakika Mwenyezi Mungu atawawezesha, Kwa kweli Mwenyezi Mungu ni Mjuzi, Mwenye habari.

[36.] Na mwabuduni Mwenyezi Mungu wala msimshirikishe na chochote, na watendeeni wema wazazi wawili na jamaa zenu na mayatima na maskini na jirani wa karibu na jirani wa mbali, na mwenzako wa ubavuni, na mpita njia na (watumwa/ wajakazi) waliomilikiwa na mikono yenu ya kulia. Hakika Mwenyezi Mungu hawapendi wenye kiburi, wenye majivuno. [37.] Ambao wao wenyewe ni mabakhili na huwaamuru watu wawe mabakhili, na wakaficha vile alivyowapa Mwenyezi Mungu katika fadhila zake. Na tumewaandalia wanaokana neema adhabu yenye kudhalilisha. [38.] Na halkadhalika wale wanaotumia mali zao kwa kuonesha watu, wala wasimwamini

Mwenyezi Mungu wala siku ya mwisho. Na ambaye shetani amemfanya ndiye rafiki yake, basi mwovu wa rafiki ni yeye! 39. Na ingewadhuru nini lau wao wangemwamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho na wakatoa katika alivyowaruzuku Mwenyezi Mungu? Na Mwenyezi Mungu daima anawajua hao. 40. Hakika Mwenyezi Mungu hadhulumu (hata chenye) uzani wa chembe. Na liwapo (jambo) ni jema hulizidisha maradufu na akaongezea kutoka Kwake malipo makubwa.

41. Basi itakuwaje pindi tutakapoleta kutoka kila umma shahidi na tukakuleta (wewe) kuwa shahidi juu ya hawa? 42. Siku hiyo waliokataa kuamini na wakamwasi Mtume watatamani ardhi ifanywe sawa nao (wao pia wawe ardhi), wala hawawezi kumficha Mwenyezi Mungu mazungumzo (yao) yeyote. 43. Enyi walioamini! Msikaribie Swala hali mmelewa mpaka mjue myasemayo. Wala (msiikaribie) mkiwa na janaba - isipokuwa wapita njia- mpaka muoge. Na muwapo wagonjwa au mkiwa safarini, au akawa mmoja wenu ametoka chooni au mkawagusa wanawake (kwa kuwajamii), kisha msipate maji, basi pateni mchanga ulio tohara; mzipake (kwao) nyuso zenu na mikono yenu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe Mwingi wa maghufira.

44. Je, huwaoni wale ambao wamepewa sehemu ya Kitabu Kitakatifu, hununua upotevu (kwa kubadilishana na Kitabu) na wanataka nyie pia mpotee njia? 45. Na Mwenyezi Mungu anawajua sana maadui zenu; na Mwenyezi Mungu anatosha kuwa Rafiki, na Mwenyezi Mungu anatosha kuwa msaidizi. 46. Baadhi ya Mayahudi kuna ambao hugeuza maneno kutoka mahala pake, na husema: 'tumesikia na tumeasi' na 'sikia lakini usisikiwe' na (husema) 'Ra'ina' kwa kupondoa ndimi zao ili kuitukana dini. Na lau kama wao wangesema: 'tumesikia na

tumetii' na 'tuvumilie hadi tuelewe' ingelikuwa heri kwao
na sawa zaidi. Lakini Mwenyezi Mungu amewaalani kwa
kufuru zao, basi hawaamini ila wachache tu.[3]

47 Enyi waliopewa Kitabu! Aminini tuliyoyateremsha
yenye kusadikisha mliyo nayo, kabla hatujazigeuza nyuso
tukazipeleka kisogoni, au tukawalaani kama tulivyowalaani
watu wa Sabato (Jumamosi). Na amri ya Mwenyezi Mungu ni
lazima iwe ni yenye kufanywa. 48 Hakika Mwenyezi Mungu
hasamehi (dhambi ya) kufanyiwa mshirika, lakini husamehe
yasiyokuwa hayo kwa amtakaye. Na mwenye kumshirikisha
Mwenyezi Mungu hakika amezusha dhambi kubwa. 49 Je,
huwaoni wale ambao hudai utakatifu? Bali Mwenyezi Mungu
humtakasa amtakaye, nao hawatadhulumiwa hata (kadri) ya
kijiuzi kilicho katikati ya kokwa ya tende. 50 Tazama jinsi
wamzuliavyo Mwenyezi Mungu uongo, na latosha hilo kuwa
ni dhambi iliyo wazi.

51. Je, huwaoni wale ambao wamepewa sehemu ya Kitabu;
wanaamini uchawi na shetani, na husema juu ya wale walio
kufuru kuwa wao wameongoka zaidi katika njia ya haki kuliko
walioamini? 52. Hao ndio waliolaaniwa na Mwenyezi Mungu.
Na ambaye Mwenyezi Mungu amemlaani, hutampatia
wa kumsaidia. 53. Au wao wana fungu katika ufalme wa
Mungu? Basi hapo wasingewapa watu hata kitobwe cha
kokwa ya tende! 54. Au wanawahusudu watu kwa alichowapa
Mwenyezi Mungu katika fadhila yake? Mbona tuliwapa
watoto wa Ibrahim Kitabu na hekima, na tukawapa pia ufalme
mkubwa? 55. Miongoni mwao kuna wale walioamini Kitabu
(walichopewa), na katika wao kuna ambao hawakukijali. Hata

3. Rejea maelezo marefu katika Sura ya al Baqara Aya 104 - Mfasiri

hivyo Jahannam inatosha kuwa moto mkali wa kuwaunguza. 56. Hakika wale ambao wamezikanusha Ishara zetu tutawatia motoni. Kila zitakapoiva ngozi zao, tutawabadilishia ngozi nyingine ili waonje adhabu ya Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu Mwenye hekima. 57. Na ambao wameamini na wakatenda mena, tutawaingiza katika Mabustani ambayo hupita mito ya maji chini yake. Wataishi milele humo; na humo watakuwa na wenza waliotakaswa na tutawaweka chini ya vivuli vya daima.

58. Hakika Mwenyezi Mungu anawaamrisha kurudisha amana kwa wenyewe. Na mtakapohukumu baina ya watu mhukumu kwa haki na uadilifu. Bila shaka mawaidha anayowapeni Mwenyezi Mungu ni mazuri mno. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia ni Mwenye kuona. 59. Enyi walioamini! Mtiini Mwenyezi Mungu na mtiini Mtume na wenye mamlaka miongoni mwenu. Na kama mkitofautiana katika jambo lolote, basi lirudisheni kwa Mwenyezi Mungu na Mtume wake; ikiwa mnamwamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho. Hivyo ndiyo vizuri na itakuwa na matokeo bora zaidi. 60. Je, huwaoni wale wanaodai kuwa wao wanaamini uliyoteremshiwa wewe na yalioteremshwa kabla yako, wanataka kwenda kuhukumiana kwa shetani na hali wameamrishwa wamkatae. Na Shetani anataka kuwapoteza upotevu wa mbali. 61. Na wakiambiwa njooni kwenye yale aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu na (njooni) kwa Mtume, utawaona wanafiki wanakuhepa mbali nawe kabisaa! 62. Lakini inakuwaje wanapopatwa na maafa kwa sababu ya yale iliyotanguliza mikono yao? Hapo tena watakujia wakiapa ‘Wallahi hatukukusudia isipokuwa wema na mapatano’. 63. Hao ni ambao Mwenyezi Mungu anayajua

yaliyo katika nyoyo zao. Basi achana nao na wape nasaha tu
na waambie maneno yatakayokita katika nyoyo zao.

64. Na hatukumtuma Mtume yeyote isipokuwa atiiwe
kwa amri ya Mwenyezi Mungu. Na laiti pindi walipokosa
kuzitendea haki nafsi wangekujia wakaomba maghufira kwa
Mwenyezi Mungu na wakaombewa maghufira na Mtume,
wangelimkuta Mwenyezi Mungu ni mwenye kutakabali
toba mwenye kurehemu. 65. Naapa kwa Mola wako Mlezi!
Hawataamini mpaka wakufanye wewe hakimu wao katika
yale wanayohitalifiana, kisha wasione dhiki katika nyoyo zao
kwa uliyohukumu na wanyenyekee kabisa kabisa. 66. Na lau
tungewalazimisha kuwa jiueni au tokeni majumbani mwenu,
wasingelifanya hilo isipokuwa wachache katika wao. Na
lau kama wangefanya yale waliyoagizwa, ingelikuwa kheri
kwao na uthibisho wa nguvu zaidi. 67. Na hapo tungewapa
malipo makubwa kutoka kwetu. 68. Na tungewaongoza njia
iliyonyooka. 69. Na wenye kumtii Mwenyezi Mungu na
Mtume, basi hao (watakuwa) pamoja na wale aliowaneemesha
Mwenyezi Mungu miongoni mwa Manabii na wasadikishaji
na mashahidi na watu wema.Ah! Ni uzuri ulioje kuwa pamoja
na watu hao!. 70. Hiyo ni fadhila itokayo kwa Mwenyezi
Mungu. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kutosha.

71. Enyi walioamini! Chukueni tahadhari! Mtoke vikundi
vikundi au tokeni nyote pamoja. 72. Na hakika katika nyinyi
kuna ambaye hukaa nyuma. Uwafikapo msiba husema:
Mwenyezi Mungu amenineemesha kwa vile sikuwa nao!
73. Na iwafikiapo fadhila itokayo kwa Mwenyezi Mungu,
husema - kana kwamba hapakuwa na mapenzi baina yenu
na yeye - laiti ningelikuwa pamoja nao nikapata mafanikio
makubwa! 74. Na wapigane katika njia ya Mwenyezi Mungu

ambao wanauza maisha ya duniani kwa kupata ya Akhera. Na mwenye kupigana katika njia ya Mwenyezi Mungu, akauawa au akashinda, tutampa ujira mkubwa. 75. Na mna nini hampigani katika njia ya Mwenyezi Mungu na kwa ajili ya wale wanaoonewa miongoni mwa wanaume na wanawake na watoto ambao husema: Ewe Mola wetu Mlezi! Tutoe katika mji huu ambao watu wake ni madhalimu, na utupatie mlinzi kutoka kwako, na utupatie wa kutusaidia. 76. Wale walioamini wanapigana katika njia ya Mwenyezi Mungu, na waliokufuru, wanapigana katika njia ya shetani. Basi piganeni na marafiki wa shetani; hakika hila ya shetani ni dhaifu.

77. Je, huwaoni wale ambao wameambiwa: 'zuieni mikono yenu (msipigane), badala yake msimamishe Swala na mtoe Zaka'. Lakini walipolazimishwa kupigana, mara kundi moja katika wao likawa linawaogopa watu kama kumwogopa Mwenyezi Mungu au kwa hofu kubwa zaidi. Wakasema: 'Ewe Mola wetu Mlezi! Kwa nini umetuamrisha kupigana? Laiti ungetucheleweshea kwa muda mchache! Waambie, starehe ya duniani ni chache, na Akhera ni bora kwa wenye kumcha Mwenyezi Mungu. Na wala hamtadhulumiwa hata (kadri) ya uzi wa kokwa ya tende. 78. Popote mtakapokuwa yatawafika mauti na hata mkiwa katika ngome madhubuti. Na likiwafikia zuri wao husema: Hili linatokana na Mwenyezi Mungu. Na likiwafika baya husema: Hili linatokana na wewe. Sema: Yote yanatoka kwa Mwenyezi Mungu. Basi wana nini watu hao hata hawakaribii kufahamu maneno? 79. Jema likufikalo linatokana na Mwenyezi Mungu, na ovu likufikalo linatokana na wewe mwenyewe. Na tumekupeleka

kwa watu kuwa ni mjumbe, na Mwenyezi Mungu ni shahidi
wa kutosha.
80. Mwenye kumtii Mtume ndio amemtii Mwenyezi Mungu;
na mwenye kukataa, basi hatukukupeleka kuwa mlinzi juu
yao. 81. Na wanasema: 'Tunatii,' Lakini wanapotoka kwako
kundi moja katika wao huenda njama usiku, kinyume na
unayowaambia. Na Mwenyezi Mungu anaziandika njama
zao. Basi achana nao na mtegemee Mwenyezi Mungu;
na Mwenyezi Mungu ni mtegemewa wa kutosha. 82. Je,
hawaizingatii Qur'an? Lau kama ingelitoka kwa asiyekuwa
Mwenyezi Mungu, bila shaka wangelikuta ndani yake tofauti
nyingi. 83. Ikiwajia habari ya amani au ya hofu huitangaza.
Na lau wangeirejesha kwa Mtume na kwa wenye mamlaka
katika wao, wale wanaochunguza wangelijua. Na lau si
fadhila ya Mwenyezi Mungu juu yenu na rehema Yake
mngemfuata shetani isipokuwa wachache tu.
84. Basi pigana katika njia ya Mwenyezi Mungu. Hubebi
jukumu isipokuwa (la) nafsi yako pekee. Na watie mori
waumini. Huenda Mwenyezi Mungu akazuia mashambulizi
ya wale waliokufuru. Na Mwenyezi Mungu ni mkakamavu
Zaidi katika kushambulia na mkali wa kuadhibu 85. Mwenye
kupendekeza jambo jema, naye hupata sehemu katika hilo,
na mwenye kupendekeza jambo baya, pia hupata hisa katika
hilo; na Mwenyezi Mungu ni Mwenye uwezo juu ya kila kitu.
86. Na mnapoamkiwa kwa maamkuzi yeyote, basi itikieni
kwa yaliyo bora au mrejeshe hayo hayo. Hakika Mwenyezi
Mungu ni Mwenye kuhisabu kila jambo. 87. Mwenyezi
Mungu, hapana Mola ila Yeye. Kwa yakini atawakusanya
Siku ya Kiyama. Halina shaka hilo. Na ni maneno yapi ya
kweli zaidi kuliko ya Mwenyezi Mungu?

88. Imekuwaje nyinyi mmekuwa makundi mawili katika (habari ya) wanafiki, na hali Mwenyezi Mungu amewapindua kwa yale waliyoyachuma? Je, mnataka kumwongoza ambaye Mwenyezi Mungu amempoteza? Na ambaye Mwenyezi Mungu amempoteza, hutampatia njia. 89. Wanapenda laiti nyinyi mngekufuru kama walivyokufuru wao mkawa sawasawa. Basi msifanye katika wao marafiki mpaka wahame katika njia ya Mwenyezi Mungu. Wakikataa wakamateni na muwaue popote muwakutapo, wala msifanye katika wao rafiki wala msaidizi. 90. Ila wale wanaoungana na kundi ambalo baina yenu na wao mna ahadi, au wakawajia hali vifua vyao vina dhiki kupigana nanyi au kupigana na watu wao. Na laiti Mwenyezi Mungu angetaka, angewasaliti juu yenu wakapigana nanyi. Basi wakijitenga na wasipigane nanyi na wakawapa amani, Mwenyezi Mungu hakuwapa njia ya kupigana nao. 91. Wengine mtawakuta wanataka wapate amani kwenu na wapate amani kutoka kwa watu wao. Kila wakirejeshwa kwenye vita hudidimizwa humo. Wasipojitenga nanyi na wakawapa amani na wakazuia mikono yao, hao wakamateni muwaue popote mtakapowapata. Na hao ndiyo ambao tumewapeni hoja zilizo wazi (za kupigana) dhidi yao.

92. Kamwe haikubaliki kwa Mwislamu kumwua Mwislamu mwenziwe isipokuwa ikiwa kwa kukosea. Na mwenye kumwua Mwislamu kwa kukosea, basi amwache huru mtumwa muumini na atoe fidia kwa watu wake ila watakapoifanya sadaka. Akiwa (aliyeuawa) ni jamaa wa maadui zenu, lakini yeye ni Mwislamu, basi (itatosha) kumwacha huru mtumwa muumini. Na ikiwa ni katika watu ambao baina yenu nyinyi na wao mna mapatano, basi ni fidia kwa watu wake na kumwacha huru mtumwa muumini. Na

ambaye hakupata basi ni kufunga miezi miwili mfululizo, ( hiyo ikiwa ni) kutubia kwa Mwenyezi Mungu; na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi Mwenye hekima. 93. Na mwenye kumwua Mwislamu kwa kukusudia, basi malipo yake ni Jahannam, ni mwenye kudumu humo; na Mwenyezi Mungu amemghadhibikia na amemlaani na amemwandalia adhabu kubwa.

94. Enyi walioamini! Mtakaposafiri katika njia ya Mwenyezi Mungu, basi fanyeni uchunguzi kabla. Wala msimwambie mwenye kuwapa Salaam: 'wewe si Mwislamu'. Mnataka mafao ya duniani? Kwa Mwenyezi Mungu kuna nyara nyingi! Hivi ndivyo mlivyokuwa nyinyi hapo nyuma, lakini Mwenyezi Mungu akawaneemesha. Basi hakikisheni; hakika Mwenyezi Mungu ni mjuzi wa mnayoyatenda. 95. Hawalingani Waislamu (wanaochagua) kubaki nyuma (kulinda) hali hawana ugonjwa wowote, na wale wanaopigana katika njia ya Mwenyezi Mungu kwa mali zao na roho zao. Mwenyezi Mungu amewapendelea kwa daraja zaidi, wale wapiganao katika njia ya Mwenyezi Mungu kwa mali zao na roho zao kuliko wale waliobaki nyuma. Mwenyezi Mungu amewaahidi wote hao Pepo. Na Mwenyezi Mungu amewapendelea wenye kupigana Jihadi kwa malipo makubwa kuliko waliobaki nyuma. 96. Daraja mbali mbali kutoka Kwake, na maghufira na rehema. Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa maghufira Mwenye kurehemu.

97. Hakika wale ambao Malaika wametwaa roho zao wakiwa wamezidhulumu nafsi zao wenyewe, (Malaika) watawauliza: 'Mlikuwa na tatizo gani nyie?' Watasema: Tulikuwa tunaonewa duniani!. Watawauliza: 'Kwani ardhi ya Mwenyezi Mungu haikuwa pana mkahamia humo?' Basi

hao makazi yao ni Jahannam; nayo ni marejeo mabaya. [98.] Isipokuwa wale wanyonge (kweli) katika wanaume na wanawake na watoto (ambao) hawawezi kufanya hila yoyote wala hawawezi kujua njia. [99.] Basi hakika hao Mwenyezi Mungu atawasamehe; na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe, Mwingi wa maghufira. [100.] Na mwenye kuhama katika njia ya Mwenyezi Mungu atapata sehemu nyingi duniani pana za kukikimbilia. Na anayetoka nyumbani kwake kuhamia kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake, kisha yakamfika mauti njiani, basi malipo yake yamethibiti kwa Mwenyezi Mungu; na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa maghufira Mwenye kurehemu.

[101.] Na mnaposafiri katika ardhi, si vibaya kwenu kama mkifupisha Swala, ikiwa mnaogopa kuwa wale waliokufuru watawaletea maudhi. Hakika makafiri ni maadui wenu walio wazi. [102.] Na utakapokuwa pamoja nao, ukawaswalisha, basi kundi moja miongoni mwao wasimame pamoja nawe na wachukue silaha zao. Wakimaliza kusujudi na warejee nyuma, kisha lije kundi jingine ambalo halijaswali, waswali pamoja na wewe nao wachukue hadhari yao na silaha zao. Waliokufuru wanapenda kama nyie mwasahau silaha zenu na vifaa vyenu, wawavamie vamio la ghafla. Wala hapana vibaya kwenu ikiwa mnaona udhia kwa sababu ya mvua au mkiwa wagonjwa, kuweka silaha zenu kando. Hakika Mwenyezi Mungu amewaandalia makafiri adhabu ya kudhalilisha. [103.] Mtakapomaliza Swala, basi mtajeni Mwenyezi Mungu mkiwa mmesimama na mmekaa na mnapojinyoosha chini. Mtakapopata amani, basi simamisheni Swala. Hakika Swala kwa waumini ni faradhi iliyowekewa wakati maalum. [104.] Wala msifanye ajizi katika kuwasaka hao watu. Ikiwa

mnaumia basi na wao wanaumia kama mnavyoumia nyinyi. Na nyinyi mwataraji kwa Mwenyezi Mungu ambayo wao hawayataraji. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi Mwenye hekima.

105. Hakika tumekuteremshia Kitabu kwa haki ili upate kuhukumu baina ya watu kwa alivyokufahamisha Mwenyezi Mungu; wala usiwe mtetezi wa wenye kufanya khiyana.
106. Na mwombe maghufira Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa maghufira Mwenye
kurehemu. 107. Wala usiwatetee wale ambao wamezihini nafsi zao. Hakika Mwenyezi Mungu hampendi aliye haini
mwenye dhambi. 108. Wanaweza kuyaficha (maovu yao) kwa watu, lakini hawawezi kuyaficha kwa Mwenyezi Mungu. Yeye yuko pamoja nao pale wanapokula njama usiku kwa maneno asiyoyapenda. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuyajua vyema wanayoyatenda.

109. Hivi nyinyi mnawatetea hawa katika uhai wa duniani, nani atakayewatetea kwa Mwenyezi Mungu siku ya Kiyama,
au ni nani atakayekuwa wakili wao? 110. Na mwenye kutenda uovu au akadhulumu nafsi yake, kisha akaomba maghufira kwa Mwenyezi Mungu, atamkuta Mwenyezi
Mungu ni Mwingi wa maghufira Mwenye kurehemu. 111. Na mwenye kuchuma dhambi, basi anajichumia mwenyewe.
Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi Mwenye hekima. 112. Na mwenye kutenda kosa au dhambi, kisha akamsingizia asiye hatia, basi hakika amejitwika dhuluma na dhambi iliyo wazi.
113. Na lau si fadhila ya Mwenyezi Mungu juu yako na rehema Yake, lingedhamiria kundi katika wao kukupotosha; wala hawazipotoshi ila nafsi zao; wala hawatakudhuru kwa lolote. Na Mwenyezi Mungu amekuteremshia Kitabu na hekima na

amekufunza uliyokuwa huyajui. Na fadhila ya Mwenyezi Mungu juu yako ni kubwa.

[114.] Hakuna kheri katika mengi wanayoshauriana kwa siri, isipokuwa anayeamrisha kutoa sadaka au wema au kusuluhisha watu. Na mwenye kufanya hayo kwa kutaka radhi ya Mwenyezi Mungu, basi tutampa ujira mkubwa. [115.] Na mwenye kumpinga Mtume baada ya kumdhihirikia yeye uongofu, na akafuata njia isiyokuwa ya waumini, tutamwelekeza alikoelekea na tumtamwingiza katika Jahannam. Hayo ndio marejeo mabaya.

[116.] Hakika Mwenyezi Mungu hasamehi kufanyiwa mshirika, lakini husamehe yasiyokuwa hayo kwa amtakaye. Na anayemshirikisha Mwenyezi Mungu, basi hakika amepotea upotofu ulio mbali. [117.] Wao hawawaombi asiyekuwa Yeye isipokuwa (miungu) wanawake. Kwa kweli hawamwabudu isipokuwa Shetani aliyeasi. [118.] Mwenyezi Mungu amemlaani, naye akasema: kwa hakika nitachukua katika waja wako fungu maalum. [119.] Kwa hakika nitawapoteza na nitawatia tamaa. Na nitawaamrisha, watayakata masikio ya wanyama na nitawaamrisha wabadili maumbile ya Mwenyezi Mungu. Na mwenye kumfanya shetani kuwa mlinzi wake badala ya Mwenyezi Mungu basi amehasirika hasara ya waziwazi. [120.] Anawaahidi na kuwatia tamaa; na shetani hawaahidi isipokuwa udanganyifu. [121.] Hao makazi yao ni moto wa Jahannam wala hawatapata pa kuukimbia. [122.] Na wale walioamini na wakatenda mema, tutawatia katika pepo ambazo hupita mito chini yake, watakaa humo milele. Ndiyo ahadi ya Mwenyezi Mungu. Na ni nani mkweli zaidi kwa usemi kuliko Mwenyezi Mungu?

[123.] Si kwa matamanio yenu wala matamanio ya watu

wa Kitabu! Yeyote anayefanya uovu atalipwa uovu. Wala hatajipatia mlinzi wala msaidizi zaidi ya Mwenyezi Mungu. 124. Mwenye kufanya mema - mwanamume au mwanamke - hali ya kuwa ni mwenye kumwamini Mwenyezi Mungu, basi hao wataingia peponi wala hawatadhulumiwa hata (kadri ya) kitobwe cha kokwa ya tende. 125. Ni nani mwenye dini nzuri kuliko yule aliyejisalimisha yeye wote kwa Mwenyezi Mungu, akafanya mazuri, na akafuata dini ya Ibrahim mnyoofu? Na Mwenyezi Mungu amemfanya Ibrahim kuwa rafiki mwandani. 126. Na ni vya Mwenyezi Mungu vilivyo mbinguni na vilivyo ardhini; na Mwenyezi Mungu ni mwenye kukizunguuka kila kitu.

127. Wanakuuliza maelezo ya kidini (fatwa) juu ya wanawake. Waambie, Mwenyezi Mungu ndiye atakeyewapa maelezo hayo juu yao, na pia mnayosomewa humu kitabuni kuhusu mayatima wanawake, ambao hamuwapi (haki zao) walizoandikiwa, na mkapenda kuwaoa, na walio dhaifu katika watoto. Na muwasimamie mayatima kwa uadilifu. Na kheri yoyote muitendayo basi Mwenyezi Mungu anaijua. 128. Ikiwa mke atahofia ukatili wa mumewe au kutelekezwa, basi hapana vibaya kwao wakipatana (kumaliza tatizo hilo) kwa suluhu. Na suluhu ni bora, ingawaje nyoyo zimewekewa mbele uchoyo. Na mkifanya wema na mkajidhibiti nafsi, basi Mwenyezi Mungu ni mjuzi wa myatendayo. 129 Wala hamtaweza kufanya uadilifu baina ya wake zenu hata mkikamia. Lakini msimpendelee mmoja kabisa kabisa, mkamwacha (mwingine) kama aliyetundikwa (hewani). Na mkisikilizana na mkadhibiti nafsi, basi Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa maghufira Mwenye kurehemu. 130 Na endapo watatengana, Mwenyezi Mungu atamtosheleza kila mmoja

kwa utajiri wake ulio tele. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye utajiri, Mwenye hekima.

131. Ni vya Mwenyezi Mungu vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini. Na hakika tuliwaamrisha waliopewa Kitabu kabla yenu na nyinyi pia, kwamba mtiini Mwenyezi Mungu. Na kama mkikufuru….mbona ni vya Mwenyezi Mungu vyote vilivyomo mbinguni na ardhini. Na Mwenyezi Mungu ni mkwasi mwenye kusifiwa. 132. Na ni vya Mwenyezi Mungu vilivyo mbinguni na vilivyo ardhini, na Mwenyezi Mungu anatosha kuwa mlinzi. 133. Endapo atataka atawaondolea mbali, enyi watu, alete wengine. Na Mwenyezi Mungu ni muweza wa hilo. 134. Anayetaka malipo ya duniani, basi yako kwa Mwenyezi Mungu malipo ya dunia na Akhera na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia Mwenye kuona.

135. Enyi walioamini! Kuweni wenye kusimama imara kwa haki na usawa, mtoao ushahid kwa ajili ya Mwenyezi Mungu; hata ikiwa dhidi yenu wenyewe, au wazazi wenu au ndugu. Iwe ni (dhidi ya) tajiri au fukara, Mwenyezi Mungu anawastahiki zaidi (kuwalinda). Basi msifuate mapenzi (ya moyo) mkapindisha haki. Endapo mtapotosha haki au mkaacha kuitoa…Mwenyezi Mungu ana habari ya myatendayo.

136 Enyi walioamini! Mwaminini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake na Kitabu ambacho amemteremshia Mtume Wake na Kitabu alichokiteremsha kabla. Na mwenye kumkakataa Mwenyezi Mungu na Malaika Wake na vitabu Vyake na siku ya mwisho, basi huyo amepotea upotevu ulio mbali. 137 Hakika wale walioamini kisha wakakufuru kisha wakaamini kisha wakakufuru kisha wakazidi kukufuru, kamwe Mwenyezi Mungu si mwenye kuwaghufiria wala

kuwaongoza njia. [138] Wabashirie wanafiki kuwa wana adhabu iumizayo, [139] ambao huwafanya makafiri ndio marafiki badala ya waumini. Je wanataka kwao utukufu? Basi hakika utukufu wote ni wa Mwenyezi Mungu.

[140.] Na amekwisha wateremshia katika Kitabu hiki kwamba mtakaposikia Aya za Mwenyezi Mungu zinakanushwa na zinadharauliwa, msikae pamoja nao mpaka waingie katika mazungumzo mengine. (Vinginevyo) nyinyi mtakuwa kama wao. Hakika Mwenyezi Mungu atawakusanya wanafiki na makafiri wote katika Jahannam. [141.] Ambao wanawangojea-ngojea. Mpatapo ushindi kutoka kwa Mwenyezi Mungu, husema: Si tulikuwa pamoja nanyi? Na ikiwa ni makafiri ndiyo walioshinda, huwaambia (makafiri) "Si sisi tulikuwa na nguvu zaidi yenu kuwashinda, lakini tukawakingeni na Waumini? Mwenyezi Mungu atahukumu baina yenu Siku ya Kiyama na Mwenyezi Mungu hatawapa makafiri njia ya kuwashinda waumini.

[142.] Wanafiki (wanadhani) wanamzunguka Mwenyezi Mungu, na hali Yeye ndiye Mwenye kuwazunguka. Na wanapoinuka kwenda kuswali, huinuka kwa uvivu. Wanajionyesha kwa watu na wala hawamtaji Mwenyezi Mungu ila kidogo tu. [143.] Ni vizabizabina baina ya huku na huko; huku hawako na huku hawako. Na ambaye Mwenyezi Mungu amempoteza huwezi kumpatia njia. [144.] Enyi walioamini! Msiwafanye makafiri kuwa marafiki badala ya waumini. Je, mnataka kumfanya Mwenyezi Mungu awe na hoja dhahiri dhidi yenu? [145.] Hakika wanafiki watakuwa katika tabaka ya chini zaidi motoni. Hutakuta kwa ajili yao msaidizi. [146.] Ila wale waliotubu na wakarekebisha (mwendo wao) na wakashikamana na Mwenyezi Mungu na

wakamtakasia Mwenyezi Mungu dini yao, basi hao watakuwa pamoja na waumini na Mwenyezi Mungu atawapa waumini malipo makubwa. [147.] Mwenyezi Mungu ana haja gani ya kuwaadhibu kama mtashukuru na mtaamini? Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye shukrani Mjuzi

[148.] Mwenyezi Mungu hapendi maneno machafu yatangazwe, isipokuwa kwa mtu aliyedhulumiwa. Na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kusikia, Mjuzi. [149.] Mkidhihirisha kheri au mkiificha au mkisamehe maovu, basi hakika Mwenyezi Mungu ndiye Mwingi wa kusamehe, Mwenye uweza. [150.] Hakika wale ambao humkana Mwenyezi Mungu na Mitume wake na wanataka kubagua baina ya Mwenyezi Mungu na mitume Wake kwa kusema : wengine tunawaamini na wengine tunawakataa, na (wale) wanaotaka kuchukua njia ya katikati ya hizo mbili… [151.] Hao ndio makafiri kweli kweli, na tumewaandalia makafiri adhabu idhalilishayo. [152.] Na wale ambao wamemwamini Mwenyezi Mungu na Mitume Wake wala wasibague baina ya yeyote katika wao, hao Atawapa ujira wao. Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa maghufira, Mwenye kurehemu.

[153.] Watu wa Kitabu wanakutaka uwateremshie Kitabu kutoka mbinguni. Walimwomba Musa makubwa kuliko hayo. Walimwambia; ‘Tuoneshe Mwenyezi Mungu waziwazi’. Wakaangamizwa na radi kwa sababu ya dhuluma yao. Wakamfanya ndama (kuwa Mungu) hata baada ya kuwafikia hoja. Hata hivyo tukawasamehe hayo. Na tukampa Musa hoja zilizo wazi. [154.] Na Tukanyanyua mlima juu yao kwa kufanya agano nao. Na tukawaambia: Ingilieni mlangoni kwa unyenyekevu. Na tukawaambia msivunje miiko ya siku ya Sabato. Na tukachukua ahadi madhubuti nao.

155. Kwa sababu ya kuvunja kwao ahadi yao, na kuzikufuru Ishara za Mwenyezi Mungu, na kuua manabii pasipo haki, na kusema kwao nyoyo zetu zimefumbwa; bali Mwenyezi Mungu amezipiga muhuri kwa kufuru yao. Basi hawataamini ila kichache tu. 156. Na kwa kufuru yao na kwa kumsingizia Maryam uwongo mzito. 157. Na kwa kusema kwao: Sisi tumemwua Masih Isa mwana wa Maryam, Mtume wa Mwenyezi Mungu. Na hawakumwua wala hawakumsulubu, lakini alifananishwa kwao. Na hakika wale waliohitalifiana katika haya wamo katika shaka nayo; hawana ujuzi, ila kufuata dhana tu. Wala hawakumwua kwa yakini. 158. Bali Mwenyezi Mungu alimwinua daraja mbele yake, na Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mwenye hekima.

159. Na hawi miongon mwa watu wa Kitabu isipokuwa atamwamini kabla ya kufa. Na Siku ya Kiyama atakuwa shahidi juu yao. 160. Basi kwa dhuluma yao Mayahudi tuliwaharamishia vitu vizuri walivyohalalishiwa, na kwa sababu ya kuwazuia kwao watu wengi na njia ya Mwenyezi Mungu. 161. Na kuchukua kwao riba nao wao wamekatazwa, na kula kwao mali za watu kwa batili. Na tumewaandalia makafiri adhabu yenye uchungu. 162. Lakini waliobobea katika elimu miongoni mwao na waumini, wanaamini uliyoteremshiwa na yaliyoteremshwa kabla yako. Na wenye kusimamisha Swala na wenye kutoa Zaka na wenye kumwamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho hao tutawapa ujira mkubwa.

163. Hakika sisi tumekuletea Ufunuo kama tulivyompelekea Ufunuo Nuh na Manabii baada yake. Na tukampelekea Ufunuo Ibrahim na Ismail na Is-haq na Yaqub na wajukuu na Isa na Ayyub na Yunus na Harun na Suleiman; na Daud

tukampa Zaburi. [164.] Na mitume tuliokusimulia kabla na mitume ambao hatukukusimulia. Na Mwenyezi Mungu alimsemesha Musa kwa maneno. [165.] (Ni) Mitume wabashiri, waonyaji, ili watu wasiwe na hoja juu ya Mwenyezi Mungu baada ya kuletewa mitume. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu Mwenye hekima.

[166.] Lakini Mwenyezi Mungu anayashuhudia aliyokuteremshia. Ameya- teremsha kwa elimu Yake na Malaika (pia) wanashuhudia. Na Mwenyezi Mungu anatosha kuwa shahidi. [167.] Hakika wale waliokufuru na kuzuilia (watu) njia ya Mwenyezi Mungu, wamepotea kabisa. [168.] Hakika wale waliokufuru na kudhulumu, Mwenyezi Mungu hawi mwenye kuwasamehe watu hao wala kuwaongoza njia. [169.] Isipokuwa njia ya Jahannam, humo watadumu milele. Na hayo kwa Mwenyezi Mungu ni mepesi. [170.] Enyi watu! Amewajieni Mtume kwa haki kutoka kwa Mola Wenu, basi aminini (itakuwa) kheri kwenu. Na kama mtakataa, basi hakika ni vya Mwenyezi Mungu vyote vilivyomo mbinguni na ardhini, na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi Mwenye hekima.

[171.] Enyi watu wa Kitabu! Msipite kiasi katika dini yenu, wala msiseme juu ya Mwenyezi Mungu ila yaliyo haki. Masih Isa bin Maryam ni Mtume wa Mwenyezi Mungu na neno lake tu alilompelekea Maryam, na ni roho iliyotoka Kwake. Basi mwaminini Mwenyezi Mungu na mitume Wake; wala msiseme ‘Utatu’. Komeni! Itakuwa kheri kwenu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mungu Mmoja tu. Ametukuka Yeye na kuwa na mwana. Ni Vyake vilivyo mbinguni na vilivyo ardhini; na Mwenyezi Mungu anatosha kuwa mlinzi. [172.] Masih hataona unyonge kuwa mtumwa wa Mwenyezi

Mungu wala (hawataona) Malaika wenye kukurubishwa. Na watakaoona unyonge utumwa wa Mwenyezi Mungu na kutakabari, basi atawakusanya wote Kwake. [173.] Ama wale ambao wameamini na wakatenda mema, atawalipa ujira wao sawa, na atawazidishia kwa fadhila Yake. Na ama wale walioona unyonge na wakafanya kiburi, basi atawaadhibu adhabu iliyo chungu; wala hawatopata kiongozi wala wa kuwasaidia. [174.] Enyi watu! Imewafikia hoja kutoka kwa Mola Wenu na tumewateremshia nuru iliyo wazi.

[175.] Ama wale waliomwamini Mwenyezi Mungu na wakashikamana Naye, basi atawaingiza katika rehema itokayo Kwake na fadhila, na atawaongoza Kwake kwenye njia iliyonyooka. [176.] Wanakuuliza hukumu. Sema: Mwenyezi Mungu anawapa hukumu juu ya mkiwa (asiye mwana). Iwapo mtu amekufa hali hana mtoto na anaye ndugu wa kike tu, basi (huyo dada) atapata nusu ya alichokiacha. Naye (kaka) atamrithi nduguye wa kike akiwa hana mtoto. Wakiwa ndugu wa kike wawili basi watapata theluthi mbili za alichokiacha (kaka yao). Na wakiwa ni ndugu wa kiume na wa kike, basi fungu la mwanamume ni kama fungu la wanawake wawili. Mwenyezi Mungu anawabainishia ili msipotee; na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu.

5. Sura Al-Maida

# SURA YA MEZA YENYE CHAKULA

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 Enyi walioamini! Tekelezeni mikataba na makubaliano
(mliyoingia). Mmehalalishiwa wanyama wenye kwato,
isipokuwa wale mnaotajiwa. Lakini msihalalishe kuwinda
mkiwa katika katika Hijja. Hakika Mwenyezi Mungu
anahukumu apendavyo. 2 Enyi walioamini! Msivunje
heshima ya alama za Mwenyezi Mungu wala mwezi mtukufu,
wala wanyama wa kuchinja, wala vigingi vyao, wala za
wale wakusudiao kwenda kwenye Nyumba Tukufu kutafuta
fadhila za Mwenyezi Mungu na radhi. Na mkishatoka
kwenye Ihramu, basi (ruhusa) windeni. Na wala chuki za
watu waliowazuia kufika Msikiti mtukufu, zisiwapelekee
kuwafanyia uadui. Na saidianeni katika wema na kumcha
Mungu, wala msisaidiane katika dhambi na uadui. Na mcheni
Mwenyezi Mungu; hakika Mwenyezi Mungu ni mkali wa
kuadhibu.

3 Mmeharamishiwa nyamafu na damu na nyama ya
nguruwe, na (mnyama ambaye) damu yake imemwagwa kwa
kutajwa (jina) la asiyekuwa Mwenyezi Mungu, na aliyekufa
kwa kunyongwa, na aliyekufa kwa kupigwa, na aliyekufa
kwa kuanguka, na kwa kuchomwa pembe, na aliyeliwa na
mnyama mwitu, ila mkidiriki kumchinja, na aliyechinjiwa
mizimu. Aidha (ni haramu) kugawa (nyama,vitu kwa
matokeo ya) bahati nasibu. Hayo yote ni ufasiki. Leo
waliokufuru wamekata tamaa na dini yenu, basi msiwaogope

na niogopeni Mimi. Leo nimewakamilishia dini yenu na
kuwatimizia neema Yangu na nimeridhia Uislamu kuwa dini
yenu. Lakini ambaye hana budi kwa sababu ya njaa, pasi
na kuelekea kwenye dhambi, hakika Mwenyezi Mungu ni
Mwingi wa maghufira Mwenye kurehemu.[4]
4. Wanakuuliza wamehalalishiwa nini. Sema
mmehalalishiwa vilivyo vizuri na safi. Na mlichowafunza
wanyama wakali (kama mbwa) kukiwinda, kama
ambavyo Mwenyezi Mungu amewafunza. Basi kuleni
walichowakamatia na tajeni jina la Mwenyezi Mungu
(mnapokichinja). Na mcheni Mwenyezi Mungu; hakika
Mwenyezi Mungu ni Mwepesi wa kuhisabu. 5. Leo
mmehalalishiwa vilivyo vizuri na safi, na chakula cha wale
waliopewa Kitabu ni halali kwenu, na chakula chenu ni halali
kwao. Na wanawake wenye kujichunga katika waumini na
wanawake wenye kujichunga katika wale waliopewa Kitabu
kabla yenu, mtakapowapa mahari yao, mkafunga ndoa bila
ya kufanya uzinzi wala kuwafanya mahawara. Na mwenye
kukataa kuamini hakika amali zake zimepomoka na yeye
huko Akhera atakuwa miongoni mwa wenye kupata hasara.
6. Enyi walioamini! Mnaposimama kwa ajili ya Swala,
basi osheni nyuso zenu na mikono yenu mpaka viiko, na
mpake vichwa vyenu na (muoshe) miguu yenu mpaka
kwenye nguyu. Na mkiwa na janaba basi ogeni, na mkiwa
wagonjwa au mumo safarini au akawa mmoja wenu ametoka
chooni au mkagusana na wanawake, kisha msipate maji, basi
tayamamuni kwa mchanga ulio tohara, mpake nyuso zenu

4. Aya kwa ujumla wake inakataza aina zozote za kupata faida, matokeo kwa kubahatisha: ku bet, kupiga ramli, bahati nasibu nk- Mfasiri.

na mikono yenu. Mwenyezi Mungu hapendi kuwatia katika taabu lakini anataka kuwatakasa na kutimiza neema Yake juu yenu ili mpate kushukuru.

7. Na kumbukeni neema ya Mwenyezi Mungu juu yenu na ahadi Yake aliyoifungamanisha nanyi, pale mliposema: 'Tumesikia na tumetii'. Na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa yaliyomo vifuani.
8. Enyi walioamini! Kuweni wasimamizi madhubuti kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, muwe mkitoa ushahidi kwa uadilifu. Wala kuchukiana na watu kusiwapelekee kutofanya uadilifu. Fanyeni uadilifu, hivyo ndiyo kuwa karibu mno na ucha Mungu. Na Mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika
Mwenyezi Mungu ana habari za mnayoyatenda.
9. Mwenyezi Mungu amewaahidi wale walioamini na wakafanya mema
kuwa watapata maghufira na malipo makubwa.
10. Na wale waliokufuru na kuzikadhibisha Ishara Zetu, hao ndio watu wa
motoni.
11. Enyi walioamini! Kumbukeni neema za Mwenyezi Mungu juu yenu, walipoazimia watu kuwanyooshea mikono yao, akaizuia mikono yao kuwafikia. Na mcheni Mwenyezi Mungu. Na waumini wamtegemee Mwenyezi Mungu.

12. Na hakika Mwenyezi Mungu alifanya agano na wana wa Israil, na tukateua wakuu kumi na wawili miongoni mwao. Na Mwenyezi Mungu akasema: Kwa yakini Mimi niko pamoja nanyi, kama mkisimamisha Swala na mkatoa Zaka na mkaamini mitume Yangu na mkawasaidia na mkamkopesha Mwenyezi Mungu mkopo mzuri; ha kika nitawafutia maovu yenu na nitawaingiza katika mabustani ambayo hupita mito chini yake. Basi yeyote atakayekufuru baada ya hayo hakika
amepotea njia iliyo sawa.
13. Basi kwa sababu ya kuvunja kwao agano lao, tuliwalaani na tukazifanya nyoyo zao

kuwa ngumu. Wanageuza maneno kutoka mahali mwake na wamesahau sehemu (kubwa) ya ujumbe waliopelekewa. Na utaendelea kugundua hiyana yao, isipokuwa wachache tu miongoni mwao. Basi wasamehe na uwaache. Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wafanyao wema.

14. Na kwa wale waliojiita 'Wakristo' pia tulifanya nao agano, lakini wakasahau sehemu (kubwa) ya ujumbe waliopelekewa. Hivyo tukawawashia uadui na chuki baina yao hadi siku ya Kiyama. Na punde hivi Mwenyezi Mungu atawaonesha nini walichokuwa wakikifanya.

15. Enyi watu wa Kitabu! Amekwishawafikieni Mtume Wetu, anayewafichulia mengi mliyokuwa mkiyaficha katika Kitabu, na anaachilia mbali mengi. Hakika imekwisha wafikia nuru kutoka kwa Mwenyezi Mungu na Kitabu kinachobainisha.
16. Mwenyezi Mungu huwaongoza kwacho wenye kutaka radhi Yake kwenye njia za amani na huwatoa kutoka gizani kuwapeleka kwenya nuru kwa amri Yake, na huwaongoza katika njia iliyonyooka.
17. Hakika wamekufuru wale waliosema: Mwenyezi Mungu ndiye Masih bin Maryam! Sema: Ni nani anamiliki chochote mbele ya Mwenyezi Mungu kama akitaka kumwangamiza Masih bin Maryam na mama yake na waliomo ardhini wote? Na ni wa Mwenyezi Mungu ufalme wa mbingu na vilivyomo baina yake. Huumba atakavyo. Na Mwenyezi Mungu ni Muweza juu ya kila kitu.

18. Mayahudi na Wakristo wanasema: 'Sisi ni watoto wa Mwenyezi Mungu na vipenzi vyake'. Sema: Basi kwa nini anawaadhibu kwa ajili ya dhambi zenu? Bali nyinyi ni watu (tu) katika aliowaumba. Humghufiria amtakaye na humwadhibu amtakaye. Na ni wa Mwenyezi Mungu

ufalme wa mbingu na ardhi na vilivyomo baina yake; na marejeo ni Kwake. [19.] Enyi watu wa Kitabu! Hakika amewafikia Mtume Wetu anayewawekea wazi (ujumbe wa Allah), baada ya kipindi cha kusita (kuja) Mitume; ili msije mkasema hakutufikia sisi mtoaji bishara wala mwonyaji; basi amekwishawafikia mtoaji bishara na mwonyaji na Mwenyezi Mungu ni Muweza juu ya kila kitu.

[20.] Na (kumbuka) pale Musa alipowaambia watu wake: Enyi watu wangu! Kumbukeni neema za Mwenyezi Mungu zilizo juu yenu, vile alivyowafanya manabii kati yenu, na akawafanya watawala, na akawapa ambayo hakuwapa wowote katika walimwengu. [21.] Enyi watu wangu! Ingieni katika ardhi takatifu ambayo Mwenyezi Mungu amewaandikia. Wala msirudi nyuma msije mkawa wenye kuhasirika. [22.] Wakasema: Ewe Musa! Huko wako majitu majabari. Nasi hatutaingia huko mpaka watoke. Wakitoka huko ndiyo nasi tutaingia. [23.] Wakasema watu wawili, miongoni mwa wale wanaomwogopa (Mwenyezi Mungu), ambao Mwenyezi Mungu amewaneemesha: ‘Waingilieni kwa mlangoni! Mkishaingia hapo, ushindi ni wenu! Lakini mtegemeeni Mwenyezi Mungu ikiwa nyinyi ni waumini’. [24.] Wakasema: Ewe Musa! Sisi hatutaingia huko kamwe maadamu mijitu hiyo iko huko. Nenda wewe na Mola Wako Mlezi mkapigane! Sisi tutabakia hapa hapa.

[25.] Akasema (Musa): Ewe Mola Wangu Mlezi! Miye sina madaraka ila juu yangu mwenyewe na (huyu) ndugu yangu (Harun). Basi tutenge na watu hawa waasi. [26.] (Mwenyezi Mungu) akasema: ‘Basi wameharamishiwa ardhi hiyo kwa miaka arubaini, watakuwa wakitangatanga ardhini. Basi usiwasikitikie watu waasi.

27. Na wasomee habari za wana wawili wa Adam kwa
ukweli. Pale walipotoa Sadaka, ikakubaliwa ya mmoja
wao, na isikubaliwe ile ya mwingine. (yule asiyekubali)
akamwambia (nduguye): Nitakuua! Akamjibu: 'Hakika
Mwenyezi Mungu hupokea sadaka za Wacha Mungu tu'.
28. 'Kama utaninyooshea mkono kuniua, mimi sitakunyooshea
mkono wangu kukuua. Hakika mimi namwogopa Mola Mlezi
wa walimwengu'. 29. Mimi nitaacha ubebe dhambi zangu
pamoja na dhambi zako; na kwa hivyo utakuwa miongoni
mwa watu wa motoni. Na hayo ndio malipo ya madhalimu.

30 Basi nafsi yake ikampelekea kumwua ndugu yake,
akamwua; na akawa miongoni mwa wenye kuhasirika.
31 Hapo Mwenyezi Mungu akamtuma kunguru anayefukua
ardhi, ili amwoneshe jinsi ya kusitiri mwili wa nduguye.
Akasema: 'Ole wangu! Nimeshindwa kuwa kama kunguru
huyu nikamsitiri ndugu yangu?' Basi akawa miongoni mwa
wenye kujuta.

32. Kwa ajili ya hilo tukatoa agizo kwa wana wa Israil
ya kwamba yeyote atakayemwua mtu bila ya huyo kuua
mtu au kufanya uovu katika nchi… basi ni kama amewaua
watu wote. Na mwenye kumwokoa mtu na mauti ni kama
amewaokoa watu wote duniani. Hakika waliwafikia wao
mitume wetu kwa hoja zilizo wazi; kisha wengi katika wao
baada ya haya wakawa waharibifu katika ardhi. 33. Hakika
malipo ya wale wanaompiga vita Mwenyezi Mungu na
Mtume wake na kufanya uharibifu katika ardhi, ni kuuawa
au kusulubiwa au kukatwa mikono yao na miguu yao kwa
kutofautiana; au kuhamishwa katika nchi. Hii ndiyo hizaya
yao katika dunia, na huko Akhera watapata adhabu kubwa.
34. Isipokuwa wale waliotubu kabla hamjawatia nguvuni.

Hapo jueni kuwa Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa maghufira, Mwenye kurehemu.

35. Enyi walioamini! Mcheni Mwenyezi Mungu na tafuteni njia ya kumfikia mfanye juhudi katika njia Yake' ili mpate kufaulu. 36. Hakika wale waliokufuru lau wangekuwa na yote yaliyomo duniani, na mengine kama hayo, ili wayatoe fidia ya kuepukana na adhabu ya siku ya Kiyama, yasingelipokelewa kutoka kwao; na wanayo adhabu iumizayo 37. Watataka watoke motoni, lakini hawatatoka humo, na wanayo wao adhabu inayodumu. 38. Na mwizi mwanamume na mwizi mwanamke, ikateni mikono yao. Hayo ni malipo ya yale waliyoyachuma, ikiwa ndiyo adhabu itokayo kwa Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu Mwenye hekima. 39. Mwenye kutubia baada ya uhalifu alioufanya na akajirekebisha, basi hakika Mwenyezi Mungu atapokea toba yake. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa maghufira Mwenye kurehemu. 40. Je, hujui kuwa Mwenyezi Mungu ana ufalme wa mbingu na ardhi? Humwaadhibu amtakaye na humsamehe amtakaye. Na Mwenyezi Mungu ni Muweza juu ya kila kitu.

41. Ewe Mtume! Wasikuhuzunishe wafanyao haraka kukufuru (ikiwa) miongoni mwa wale wasemao kwa vinywa vyao 'tumeamini' hali nyoyo zao hazikuamini, au miongoni mwa Mayahudi, watu wasikiao uwongo wowote. Wanawasikiza watu wengine ambao hata hawajafika kwako. Wanayageuza maneno kutoka mahali mwake; wanasema: 'Mkipewa haya yashikeni, na msipopewa haya tahadharini'. Na ambaye Mwenyezi Mungu anataka kumjaribu, wewe huna madaraka yeyote naye mbele ya Mwenyezi Mungu. Hao ndio ambao Mwenyezi Mungu hataki kuzitakasa nyoyo

zao; wana hizaya duniani, na Akhera watakuwa na adhabu kubwa.

42. Wasikilizao sana uwongo, walao sana (vya) haramu. Basi wakikujia, hukumu baina yao au achana nao. Na ukiachana nao, hawatakudhuru kwa chochote. Na ukiwahukumu basi hukumu baina yao kwa uadilifu; hakika Mwenyezi Mungu anapenda waadilifu. 43. Watakufanyaje hakimu nao wanayo Torat yenye hukumu za Mwenyezi Mungu? Kisha baada ya hayo wanakataa. Kwa sababu hao si wenye kuamini.

44. Hakika tuliteremsha Torati (kwa Musa) ndani yake mna mwongozo na mwangaza. Kwa kutumia sheria za Torat, Manabii waliojisalimisha kwa Mwenyezi Mungu, watawa (Rabbi) na wanazuoni, waliwahukumu Mayahudi, kwa vile ni wao ndio walioaminiwa kukilinda Kitabu cha Mwenyezi Mungu. Nao wakawa mashahidi juu yake. Kwa hiyo, msiwaogope watu bali niogopeni Mimi. Wala msibadilishe Aya Zangu kwa thamani duni (dunia). Na wasiohukumu kwa (mujibu wa) yale aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu, hao ndiyo waliokana. 45. Na tuliwapa maagizo humo ndani (ya Torat) kwamba (kutoa) roho iwe kwa roho na jicho kwa jicho na pua kwa pua na sikio kwa sikio na jino kwa jino na majeraha yana kisasi (cha kadri yake). Lakini atakayesamehe, basi itakuwa kafara kwake. Na wasiohukumu kwa mujibu wa alivyoteremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndio madhalimu. 46. Na katika nyayo zao tukamtuma Isa bin Maryam kuja kuyasadikisha yaliyokuwa kabla yake katika Torat, na tukampa Injili (Gospel), ndani yake mna mwongozo na nuru, na isadikishayo yaliyo kabla yake katika Torat, na ni mwongozo na mawaidha kwa wenye kumcha Mungu. 47. Acha watu wa Injili wahukumu kwa mujibu wa

aliyoteremsha Mwenyezi Mungu. Na wasiohukumu kwa mujibu wa alivyoteremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndio waasi.

48. Na tumekuteremshia wewe Kitabu hiki kwa haki; kinachothibitisha vitabu vilivyokuwa kabla yake na kinachovihifadhi (kwa kuboresha sheria zilizomo). Basi hukumu baina yao kwa mujibu wa aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu, wala usifuate matamanio yao kwa kuacha haki iliyokufikia. Na kila (Umma) katika nyinyi, tumeujalia sharia yake na njia yake. Na kama Mwenyezi Mungu angelitaka, angeliwafanya nyote muwe umma mmoja, lakini ni ili awajaribuni katika vile alivyowapa. Basi shindaneni katika mambo ya kheri. Marejeo yenu nyote ni kwa Mwenyezi Mungu; Naye atawaambia yale mliyokuwa mkitofautiana.

49. Na hukumu baina yao kwa mujibu wa alivyoteremsha Mwenyezi Mungu, wala usifuate mapenzi yao. Nawe jihadhari nao wasije wakakutia kwenye fitna ukaacha baadhi ya yale aliyokuteremshia Mwenyezi Mungu. Na kama wakikengeuka, basi jua kwamba Mwenyezi Mungu anataka kuwasibu kwa baadhi ya dhambi zao. Na hakika watu wengi hupenda uasi.
50. Je, wanataka hukumu za kijahiliya? Na ni nani aliye mzuri zaidi kwa kuhukumu kuliko Mwenyezi Mungu, kwa watu wenye yakini?

51. Enyi walioamini! Msiwafanye Mayahudi na Wakristo kuwa rafiki zenu (wa kuwalinda). Wao kwa wao ndiyo marafiki. Na yule miongoni mwenu atakayewafanya urafiki nao, basi huyo ni katika wao. Hakika Mwenyezi Mungu hawaongozi watu madhalimu.
52. Utawaona wale wenye maradhi nyoyoni mwao wanakimbilia kwao wakisema: ‘Tunaogopa yasitusibu majanga’. Huenda Mwenyezi Mungu

akaleta ushindi au jambo jingine litokalo Kwake, wakawa
wenye kujuta kwa yale waliyoyaficha nyoyoni. 53. Na
watasema walioamini: Hivi hawa ndio wale walioapa kwa
jina la Mwenyezi Mungu ukomo wa viapo vyao, kwamba wao
wako pamoja nanyi? Zimepomoka amali zao na wamekuwa
wenye hasara.
54. Enyi walioamini! Atakayeiacha dini yake miongoni
mwenu, basi Mwenyezi Mungu atakujawaleta watu
anaowapenda nao wanampenda. Wanyenyekevu kwa
waumini, wenye nguvu juu ya makafiri, wanapigania njia ya
Mwenyezi Mungu, wala hawaogopi lawama ya anayelaumu.
Hiyo ni fadhila ya Mwenyezi Mungu humpa amtakaye.
Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye wasaa, Mwenye kujua.
55. Hakika marafiki zenu (wa kweli kabisa) ni Mwenyezi Mungu
na Mtume Wake na wale walioamini, ambao husimamisha
Swala na hutoa Zaka (hata) wakiwa wameinama kuswali.
56. Na anayemfanya rafiki Mwenyezi Mungu na Mtume Wake
na wale walioamini, basi kundi (hilo) la Mwenyezi Mungu
ndio watakaoshinda.
57. Enyi walioamini! Msiwafanye marafiki wale
walioifanyia kejeli na mchezo dini yenu miongoni mwa
wale waliopewa Kitabu kabla yenu na makafiri. Na
mcheni Mwenyezi Mungu kama nyinyi ni waumini. 58. Na
mnapoadhinia Swala, wao wanaifanyia mzaha na mchezo.
Hayo ni kwa sababu wao ni watu wasiokuwa na ufahamu.
59. Sema: Enyi watu wa Kitabu! Hivi si mnatuchukia kwa kuwa
tumemwamini Mwenyezi Mungu na yale yaliyoteremshwa
zamani na kwa kwamba wengi wenu ni wapotofu? 60. Sema:
Je, niwaambie yule mwenye malipo mabaya Zaidi kuliko
haya mbele ya Mwenyezi Mungu? Ni yule ambaye Mwenyezi

Mungu amemlaani na kumkasirikia na akawafanya miongoni mwao manyani na nguruwe na akamwabudu Shetani. Hao ndio wenye mahali pabaya na wamepotea zaidi njia iliyo sawa.

61. Na wanapowajia husema: 'Tumeamini', ilhali wao wameingia na ukafiri wao na wametoka nao. Na Mwenyezi Mungu anayajua sana wanayoyaficha. 62. Na utawaona wengi katika wao wanakimbilia kwenye dhambi na uadui na ulaji wao vya haramu. Bila shaka wayatendayo ni mabaya mno. 63. Mbona Makuhani wao (Rabbi) na maulama wao wa sheria hawawakatazi maneno yao ya dhambi na ulaji wao vya haramu? Hakika wayatendayo ni mabaya kabisa.

64. Wayahudi wanasema: 'Mkono wa Mwenyezi Mungu umefumba.' Mikono yao ndiyo iliyofumba, na wamelaaniwa kwa waliyoyasema. (Hapana), Bali mikono Yake imefumbuliwa, hutoa apendavyo. Bila shaka yale yaliyoteremshwa kwako kutoka kwa Mola Wako Mlezi, yatawazidisha wengi miongoni mwao jeuri na uasi. Na tumewatilia uadui na chuki baina yao hadi Siku ya Kiyama. Kila mara wanapowasha moto wa vita Mwenyezi Mungu anauzima. Na wanajitahidi kuleta uharibifu katika ardhi. Na Mwenyezi Mungu hawapendi waharibifu.

65. Na lau kwamba watu wa Kitabu wangeliamini na wakamcha Mungu, tungeliwafutia makosa yao na kuwaingiza katika bustani (pepo) zenye neema. 66. Na lau wangeliishika Torat na Injil na yale yaliyoteremshwa kwao kutoka kwa Mola Wao Mlezi, wangelikula vya juu yao na vya chini ya miguu yao. Miongoni mwao wako watu walio sawa na wengi wao wanayoyafanya ni mabaya.

67. Ewe Mtume! Fikisha uliyoteremshiwa kutoka kwa

Mola Wako Mlezi. Na kama hutafanya, basi hukufikisha ujumbe Wake. Mwenyezi Mungu atakulinda na watu. Hakika Mwenyezi Mungu hawaongozi watu makafiri.

68. Sema: Enyi watu wa Kitabu! Hamna chenu, hadi muishike Torat na Injili na yaliyoteremshwa kwenu kutoka kwa Mola Wenu. Kwa hakika yaliyoteremshwa kwako kutoka kwa Mola Wako yatawazidisha wengi katika wao ujeuri na uasi. Basi usiwasikitikie watu makafiri. 69. Hakika wale walioamini (Quran) na Mayahudi na Wasabia na Wakristo, watakao mwamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho na wakafanya amali njema, basi wao hawatakuwa na hofu wala hawatahuzunika.

70. Hakika tulifanya agano na Wana wa Israil na tukawapelekea Mitume. Kila alipowajia Mtume pamoja na wasiyapenda, baadhi walimkana na baadhi walimwua. 71. Na wakadhani kuwa hakutakuwa na matatizo (hawataadhibiwa), basi wakajifanya vipofu na viziwi. Kisha Mwenyezi Mungu akawatakabalia toba; kisha tena wengi katika wao wakajifanya vipofu na viziwi; na Mwenyezi Mungu anayaona wanayoyatenda.

72. Kwa hakika wamekufuru wale waliosema Mwenyezi Mungu ni Masih mwana wa Maryam. Na ilhali Masih aliwaambia: ‘Enyi wana wa Israil! Mwabuduni Mwenyezi Mungu Mola Wangu na Mola Wenu Mlezi; kwani anayemshirikisha Mwenyezi Mungu, hakika Mwenyezi Mungu amemharamishia (kuingia) pepo na makazi yake ni motoni. Na watenda maovu hawatakuwa na wa kuwanusuru. 73. Kwa hakika wamekufuru wale waliosema, Mwenyezi Mungu ni wa tatu katika Utatu (trinity); ilhali hakuna Mungu ila Mungu Mmoja tu. Na kama hawataacha hayo wayasemayo,

kwa hakika itawapata, wale waliokufuru miongoni mwao, adhabu iumizayo. [74.] Je, hawatubu kwa Mwenyezi Mungu na kumwomba maghufira? Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa maghufira Mwenye kurehemu. [75.] Masih mwana wa Maryam hakuwa mwingine isipokuwa Mtume. Wamepita kabla yake Mitume wengi, na mama yake ni mkweli. Wote wawili walikuwa wakila chakula. Angalia jinsi tunavyowafafanulia Aya, kisha angalia jinsi wanavyogeuzwa (na haki). [76.] Sema: Je, mtaabudu badala ya Mwenyezi Mungu, kitu ambacho hakiwezi kuwadhuru wala kuwanufaisha? Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia, Mwenye kujua.

[77.] Sema: Enyi watu wa Kitabu! Msivuke mipaka katika dini yenu bila ukweli wowote, wala msifuate matamanio ya watu waliokwishapotea tangu zamani; na wakawapoteza wengi, na wenyewe wakapotea njia iliyo sawa.

[78.] Walilaaniwa wale waliokufuru miongoni mwa wana wa Israil kwa ulimi wa Daud na wa Isa mwana wa Maryam. Hayo ni kwa sababu waliasi, nao walikuwa wakivuka mipaka. [79.] Walikuwa hawakatazani mambo mabaya waliyokuwa wakiyafanya. Hakika ni maovu waliyokuwa wakiyafanya. [80.]Utawaona wengi katika wao wanawafanya marafiki wale waliokufuru. Kwa hakika ni maovu yaliyotangulizwa na nafsi zao; ya kwamba Mwenyezi Mungu amewakasirikia na watadumu katika adhabu. [81.] Na lau wangelikuwa wanamwamini Mwenyezi Mungu na Nabii na yale yaliyoteremshwa kwake, wasingeliwafanya hao kuwa marafiki, lakini wengi katika wao ni wapotofu.

[82.] Hakika utawakuta walio maadui zaidi kuliko watu wote kwa Waislamu ni Mayahudi na Washirikina. Na utawakuta walio karibu zaidi kwa mapenzi kwa Waislamu ni wale

waliosema: Sisi ni Wakristo. Hayo ni kwa sababu wapo
miongoni mwao makasisi na watawa na hao hawana kiburi.
83. Na wanaposikia yaliyoteremshwa kwa Mtume, utaona
macho yao yanamiminika machozi kwa sababu ya ukweli
walioutambua; wanasema: Mola wetu Mlezi, tumeamini!
Basi tuandike sisi pamoja na wanaoshuhudia. 84. Na kwa nini
tusimwamini Mwenyezi Mungu na ukweli uliotujia, na hali
tunatumai Mola atuingize Peponi pamoja na watu wema?
85. Basi Mwenyezi Mungu atawalipa, kwa yale waliyosema,
Bustani ambazo hupita chini yake mito. Humo watakaa
milele. Na hayo ndiyo malipo ya wafanyao mema. 86. Na
wale waliokufuru na kuzikanusha Aya zetu, hao ndio watu
wa motoni.

87. Enyi walioamini! Msiharamishe vizuri
alivyowahalalishia Mwenyezi Mungu. Wala msivuke mipaka.
Hakika Mwenyezi Mungu hawapendi wanaopetuka mipaka.
88. Na kuleni katika vile alivyowaruzuku Mwenyezi Mungu
vilivyo halali na vizuri; na mcheni Mwenyezi Mungu ambaye
nyinyi mnamwamini. 89. Mwenyezi Mungu hatawaadhibu kwa
viapo vyenu vya upuuzi; lakini atawaadhibu kwa mlivyoapa
kwa kukusudia. Basi kafara lake ni kuwalisha masikini kumi
kwa wastani wa mnavyowalisha watu wenu, au kuwavisha,
au kumwacha huru mtumwa. Na asiyeweza kupata (hayo),
basi afunge siku tatu. Hayo ndiyo kafara la viapo vyenu.
Na vichungeni viapo vyenu. Namna hii Mwenyezi Mungu
anawabainisha Aya zake ili mpate kushukuru.

90. Enyi walioamini! Hakika vileo na kamari na (kuabudu)
mizimu na bahati nasibu ni uchafu katika kazi ya Shetani.
Basi jiepusheni navyo, ili mpate kufaulu. 91. Hakika Shetani
anataka kuwaingizia uadui na bughudha baina yenu kwa ulevi

na kamari na kuwazuia nyie na kumkumbuka Mwenyezi Mungu na kuswali. Basi je, mtakoma? 92. Na mtiini Mwenyezi Mungu na mtiini Mtume na tahadharini (na maovu). Na mkikengeuka basi jueni kuwa ni juu ya mtume wetu kufikisha tu (ujumbe) ulio wazi. 93. Hakuna dhambi juu ya wale walioamini na wakatenda mema kwa sababu ya walivyovila (kabla ya kuharamishwa), maadamu wamejichunga na maovu, wakaamini na wakatenda mema, tena wakamcha Mungu na wakaamini, tena wakamcha Mungu na wakafanya mazuri. Na Mwenyezi Mungu huwapenda wafanyao mazuri.

94. Enyi walioamini! Hakika Mwenyezi Mungu atawajaribu kidogo kwa wanyama wa mawindo mnaowafikia kwa mikono yenu na mikuki yenu. Ili Mwenyezi Mungu amjaribu nani anayemwogopa Yeye pamoja nakuwa hamwoni machoni. Basi atakayevuka mipaka baada ya hayo, atapata adhabu iumizayo. 95. Enyi walioamini! Msiue wanyama pori nanyi mkiwa mmehirimia Hijja. Na miongoni mwenu atakayemuua kwa kusudi, basi malipo (yake) yatakuwa (kuchinja mnyama) aliye mfano wa aliyemwua katika mifugo, kama watavyohukumu waadilifu wawili miongoni mwenu. Mnyama apelekwe Al-Kaaba (kama sadaka); au kutoa kafara kwa kuwalisha masikini; au badala ya hayo ni kufunga; ili aonje ubaya wa jambo lake. Mwenyezi Mungu amekwisha yasamehe yaliyopita; na atakayerudia, Mwenyezi Mungu atampa adhabu. Na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye nguvu Mwenye kuadhibu.

96. Mmehalalishiwa kuvua wanyama wa baharini na kuwala, kwa manufaa yenu na kwa wasafiri. Na mmeharamishiwa mawindo ya nchi kavu maadamu mko katika Ihram. Na mcheni Mwenyezi Mungu ambaye kwake mtakusanywa.

[97.] Mwenyezi Mungu amefanya Al-Kaaba nyumba tukufu, kuwa ni hifadhi ya amani kwa watu, na pia miezi mitukufu na wanyama wa kuchinja na vigwe. Hayo ni kwa sababu mjue kuwa Mwenyezi Mungu anayajua yaliyomo mbinguni na yaliyomo ardhini na kwamba Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu. [98.] Jueni kwamba Mwenyezi Mungu ni mkali wa kuadhibu na kwamba Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa maghufira, Mwenye kurehemu. [99.] Haimlazimu Mtume ila kufikisha (ujumbe) tu. Na Mwenyezi Mungu anajua mnayoyadhihirisha na mnayoyaficha. [100.] Sema: Havifanani kibaya na kizuri, hata ukikupendeza wingi wa vibaya. Basi mcheni Mwenyezi Mungu enyi wenye akili ili mpate kufaulu.

[101.] Enyi walioamini! Msiulize mambo ambayo yakiwekwa wazi yatawachukiza. Na mnapoyauliza wakati inapoteremshwa Qur'an mtawekewa wazi. Mwenyezi Mungu ameyasamehe hayo; na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa maghufira Mpole. [102.] Waliyauliza watu waliokuwa kabla yenu kisha wakawa wenye kuyakataa. [103.] Si Mwenyezi Mungu ndiye aliyeweka (imani za Kipagani, kama) Bahira wala Saiba, Waswila, wala Hami, isipokuwa wale waliokufuru ndiyo waliokuja na uzushi wa uongo dhidi ya Mwenyezi Mungu. Na wengi wao hawana busara.[5] [104] Wanapoambiwa njooni kwenye yale aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu na njooni kwa Mtume, husema: Yanatutosha yale tuliyowakuta nayo babu zetu. Hivi hata kama baba zao walikuwa hawajui kitu wala hawakuongoka? [105] Enyi walioamini! Jalini nafsi

5. Mapagani wa Kiarabu walikuwa wana imani kuwa aina hizo za ngamia aidha watolewe kafara (ngamia aliyezaa mapacha), au waachiwe wasifanyishwe kazi (ngamia waliozaa watoto kumi) nk - Mfasiri.

zenu. Hawawadhuru waliopotea ikiwa ninyi mmeongoka. Marejeo yenu nyote ni kwa Mwenyezi Mungu; atawaambia yale mliyokuwa mkiyatenda.

106 Enyi walioamini! Yanapomfika mauti mmoja wenu, wakati wa kuusia, wawepo mashahidi wawili kati ya jamaa zenu walio waadilifu. Au wengine wasio kuwa jamaa zenu endapo mko safarini na msiba wa mauti ukawafikia. Mtawazuia wawili hao baada ya swala, na waape kwa Mwenyezi Mungu mkiwa na shaka (kwa kusema): 'Hatutapokea thamani yeyote kwa kufanya hivi hata kama (mfaidika) ni ndugu yetu wa karibu, na wala hatufichi ushahidi wa Mwenyezi Mungu, hakika hapo tutakuwa miongoni mwa wenye dhambi. 107. Ikigundulika kuwa wawili hao wana makosa (ya udanganyifu), basi wawili wengineo kutokana na warithi wenye kudai haki washike mahali pa wa mwanzo. Nao waape kwa Mwenyezi Mungu kuwa : 'Ushahidi wetu ni wa kweli zaidi kuliko wa wale; na sisi hatukuvuka mipaka (ya ukweli), kwani hapo tutakuwa miongoni mwa watenda uovu. 108. Hiyo inaelekea zaidi ya kwamba watatoa ushahidi ulio sawa au wataogopa visije vikaletwa viapo vingine baada ya viapo vyao. Na mcheni Mwenyezi Mungu na msikie. Na hakika Mwenyezi Mungu hawaongoi wapotofu.

109. Siku ambayo Mwenyezi Mungu atawakusanya Mitume awaambie, 'mlijibiwa nini'? Watasema: Hatujui, hakika wewe ndiwe mjuzi sana wa ghaibu. 110. Ndipo Mwenyezi Mungu atasema: 'Ewe Isa mwana wa Maryam! Kumbuka neema Yangu juu yako na juu ya mama yako. Nilipokutia nguvu kwa Roho Mtakatifu, ukazungumza na watu ukiwa kwenye mbeleko na ukiwa mkongwe, na nilivyokufundisha Kitabu na hekima na Torat na Injili, na ulipotengeneza kwa udongo

kama umbo la ndege kwa idhini Yangu, kisha ukapuliza likawa ndege kwa idhini Yangu, na ulipowaponyesha vipofu na wenye mbalanga kwa idhini Yangu, na ulipowafufua wafu kwa idhini Yangu, na nilipokuhami na wana wa Israil ulipowafikia na hoja zilizo wazi, wakasema wale waliokufuru miongoni mwao: Haya si chochote ila ni uchawi tu.

111. Na nilipowapelekea ufunuzi wanafunzi (wako) kwamba 'Niaminini mimi na Mtume wangu', wakasema: 'Tumeamini na ushuhudie kuwa sisi ni wanyenyekevu'.
112. Na pale Wanafunzi waliposema: 'Ewe Isa bin Mariyam! Je, Mola Wako anaweza kututeremshia chakula kutoka mbinguni'? Isa akasema: 'Mcheni Mwenyezi Mungu ikiwa nyinyi ni waumini'. 113. Wakasema: 'Tunataka kula chakula hicho na ili zitulie nyoyo zetu na tujue ya kuwa umetuambia kweli, na tuwe miongoni mwa wanaoshuhudia'. 114. Akasema Isa bin Maryam: 'Ewe Mwenyezi Mungu Mola wetu Mlezi! Tuteremshie chakula kutoka mbinguni, ili kiwe sikukuu kwa ajili ya wa mwanzo wetu na wa mwisho wetu, na kiwe ishara itokayo Kwako. Basi uturuzuku, kwani Wewe ni Mbora wa wanaoruzuku'. 115. Mwenyezi Mungu akasema: 'Hakika Mimi nitawateremshia, lakini atakayekufuru baada ya hapo kati yenu, basi nitamwadhibu adhabu ambayo sijamwadhibu yeyote katika walimwengu'.

116. Na pale Mwenyezi Mungu atakaposema: 'Ewe Isa bin Maryam! Ati wewe uliwaambia watu: Nifanyeni mimi na mama yangu kuwa ni miungu badala ya Mwenyezi Mungu'? Isa atasema: 'Subhaanak' Wewe umetakasika! Hainifalii mimi kusema ambayo si haki yangu. Ikiwa niliyasema basi bila shaka umekwishayajua. Wewe unayajua yaliyo ndani ya nafsi yangu, wala mimi siyajui yaliyomo katika nafsi

Yako; hakika wewe ndiye mjuzi zaidi wa yaliyofichikana.
[117.] 'Sikuwaambia isipokuwa yale uliyoniamrisha: kwamba mwabuduni Mwenyezi Mungu, Mola Wangu na Mola Wenu. Na mimi nilikuwa shahidi juu yao nilipokuwa nao na uliponifisha ukawa Wewe ndiye Mwangalizi juu yao; na Wewe ni shahidi juu a kila kitu'.
[118.] Ukiwaadhibu basi hao ni waja Wako. Na ukiwasamehe basi Wewe ndiye Mwenye nguvu Mwenye hekima.

[119.] Mwenyezi Mungu atasema: 'Hii ndiyo siku ambayo wasemao kweli utawafaa ukweli wao. Wao watapata bustani ambazo hupita mito chini yake; humo watadumu milele. Awe radhi nao Mwenyezi Mungu na wao wawe radhi Naye; huko ndiko kufuzu kukubwa.
[120.] Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye ufalme wa mbingu na ardhi na vilivyomo; Naye ni Mweza wa kila kitu.

## 6. Sura Al-An'am

# SURA YA WANANYAMA MIFUGO

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

[1] Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu aliyeumba mbingu na ardhi na akafanya giza na mwangaza. Tena baada ya haya wale waliokufuru wanamlinganisha Mola wao Mlezi (na wengine).
[2] Yeye ndiye aliyewaumba nyinyi kwa udongo; kisha akawahukumia muda maalum. Na kuna muda mwingine maalum Kwake. Tena baada ya haya nyinyi mnatia shaka.
[3] Na Yeye ndiye Mwenyezi Mungu mbinguni na ardhini; anaijua siri yenu na dhahiri yenu, na anayajua

mnayoyachuma. 4 Na haiwafikii ishara yoyote katika ishara
za Mola wao ila huwa wanaipa nyongo. 5 Wameukana
ukweli pale ulipowajia. Basi punde hivi zitawajia habari za
yale waliyokuwa wakiyafanyia mzaha. 6 Je hawaoni vizazi
vingapi tuliviangamiza kabla yao? Tuliwawezesha katika
ardhi namna ambayo hatukuwawezesha nyie; tukawapelekea
mvua nyingi; na tukaifanya mito inapita chini yao. Mwishowe
tuliwaangamiza kwa dhambi zao, na tukaanzisha baada yao
kizazi kingine.

7 Na lau tungelikushushia kitabu chenye karatasi,
wakakigusa kwa mikono yao hasa, wanaomkana Mungu
(hata hivyo) wangesema: ‘Hiki si chochote ila uchawi
wa wazi wazi’. 8 Wanasema: Mbona hakuteremshiwa
Malaika? Kama tungeliteremsha Malaika, jambo hili
lingekuwa tayari limemalizwa na wasingelipewa nafasi.
9 Na kama tungemfanya Malaika, ingebidi tumfanye (kama)
binadamu, na hapo tungewaongezea kuchanganyikiwa juu
ya kuchanganyikiwa waliko nako hivi sasa. 10 Na hakika
mitume waliokuwepo kabla yako walifanyiwa kejeli,
lakini waliowafanyia kejeli wakaja wakazungukwa na yale
waliyoyafanyia kejeli. 11 Sema: Tembeeni katika ardhi, kisha
muone ulikuwaje mwisho wa wale waliokadhibisha?

12. Sema: Ni vya nani vilivyomo ardhini na mbinguni?
Useme ni vya Mwenyezi Mungu. Amejilazimisha
kuwahurumia (viumbe). Hakika atawakusanya Siku ya
Kiyama, isiyo na shaka. Ni wale waliozipoteza roho zao
ndiyo hawaamini (hivyo). 13. Ni vyake vilivyotulia katika
usiku na mchana; naye ndiye asikiaye na ajuaye. 14. Sema:
Je, nimfanye Mola asiyekuwa Mwenyezi Mungu; Muumba
wa mbingu na ardhi, naye ndiye anayelisha, wala halishwi?

Sema: Hakika mimi nimeamrishwa niwe wa mwanzo katika wenye kusilimu. 'Na wala kabisa usiwe katika washirikina'.
15. Sema: Hakika mimi ninaogopa adhabu ya siku kubwa ikiwa nitamwasi Mola wangu. 16. Atakayeepushwa nayo siku hiyo, hakika (Mwenyezi Mungu) amemwonea huruma, na huko ndiko kufuzu kuliko wazi.

17. Na kama Mwenyezi Mungu akikugusa kwa shida, hakuna wa kuiondoa ila Yeye. Na akikugusa kwa kheri, basi Yeye ndiye Mwenye uweza juu ya kila kitu. 18. Naye ndiye mwenye nguvu juu ya waja wake; naye ndiye Mwenye hekima Mjuzi wa yote. 19. Sema: Ni kitu gani ushahidi wake ni mkubwa zaidi? Sema: 'Mwenyezi Mungu'. Yeye ndiye shahidi baina yangu na baina yenu. Na nimefunuliwa Qur'an hii ili niwaonye nyinyi na kila inayemfikia. Je, kweli nyinyi mnashuhudia kwamba wako waungu wengine pamoja na Mwenyezi Mungu? Sema: Mimi sishuhudii. Sema: Yeye ni Mungu mmoja tu, na hakika mimi ni mbali na hayo mnayoyashirikisha.

20. Wale tuliowapa Kitabu wanaajua haya kama wanavyowajua wana wao. Wale ambao wamezitia hasarani nafsi zao hawaamini. 21. Na ni nani dhalimu zaidi kuliko yule amzuliaye Mwenyezi Mungu uwongo, au azikadhibishaye Ishara Zake? Hakika madhalimu hawatafaulu. 22. Na siku tutakapowakusanya pamoja wote, kisha tutawaaambia wale walioshirikisha: Wako wapi washirikishwa wenu mliokuwa mnadai? 23. Kisha hautakuwa ujanja wao ila kusema: Wallahi, Mola wetu Mlezi! Hatukuwa washirikina!. 24. Angalia jinsi wanavyojisemea uwongo wenyewe; na yamepotea waliyokuwa wakiyazua.

25. Na miongoni mwao wako wanaokusikiliza; na tumezitia

pazia nyoyo zao wasije kuyafahamu; na mna uziwi masikioni
mwao; na wakiona kila Ishara hawaiamini. Hata wakikujia
kujadaliana nawe wanasema waliokufuru: Hizi si chochote
isipokuwa ni ngano za watu wa kale. 26. Nao wanawazuia watu,
na wao wenyewe wanajitenga nayo. Lakini hawaangamizi
isipokuwa nafsi zao na wala hawatambui. 27. Na lau ungeona
wanaposimamishwa mbele ya moto wakawa wanasema:
Laiti tungerudishwa (duniani) tusingekadhibisha Aya za
Mola wetu Mlezi, bali tukawa miongoni mwa walioamini.
28. Bali (sasa) yamewadhihirikia waliyokuwa wakiyaficha
zamani. Na kama wangerudishwa, bila shaka wangeyarudia
yale yale waliyokatazwa, na hakika wao ni waongo.

29. Na wanasema: Hakuna maisha (mengine) isipokuwa
maisha yetu ya hapa duniani, na wala sisi hatutafufuliwa.
30. Na lau ungeliona watavyosimamishwa mbele ya Mola
wao Mlezi, Awaulize: Je, haya si kweli? Watasema: Kwani?
Tunaapa kwa Mola wetu Mlezi, ni kweli. Mwenyezi Mungu
atasema: ‘Basi onjeni adhabu kwa sababu ya yale mliyokuwa
mkiyakana.

31. Hakika wamehasirika wale waliokana kukutana na
Mwenyezi Mungu, na wamefuzu wale waliomwamini,
mpaka kinapowajia Kiyama ghafla watasema: ‘Oo! Majuto
yetu juu ya yale tuliyoyapuuza! Nao watabeba mizigo yao
migongoni mwao. Ehee! Ni mabaya mno wanayoyabeba.
32. Na maisha ya dunia si kitu ila mchezo na upuzi; na hakika
nyumba ya akhera ni bora zaidi kwa wenye takua. Basi je
hamtii akili?

33. Hakika tunajua kwamba yanakuhuzunisha yale
wanayoyasema. Basi hakika hao hawakukadhibishi wewe,
lakini madhalimu wanakataa Ishara za Mwenyezi Mungu.

34. Na hakika walikadhibishwa Mitume kabla yako,
wakavumilia juu ya kukadhibishwa na kuudhiwa, mpaka
ikawafikia nusura yetu. Na hakuna wa kubadilisha maneno
ya Mwenyezi Mungu. Na bila shaka zimekujia baadhi ya
habari za Mitume hao. 35. Na ikiwa ni makubwa kwako huku
kukataa kwao, basi kama unaweza kutafuta njia ya chini
kwa chini ardhini, au ngazi kwendea mbinguni uwaletee
ishara. Na lau Mwenyezi Mungu angelitaka, angewakusanya
hao kwenye uongofu. Basi usiwe miongoni mwa wajinga.
36. Hakika watakaokubali ni wale tu wanaosikia (ukweli).
Na wafu Mwenyezi Mungu atawafufua kisha watarejeshwa
Kwake.

37. Na husema: Kwa nini hakuteremshiwa Ishara kutoka
kwa Mola Wake? Sema: Hakika Mwenyezi Mungu ni
Mwenye uwezo wa kuteremsha ishara yoyote, lakini wengi
wao hawajui. 38. Na hakuna mnyama katika ardhi wala
ndege arukaye kwa mbawa zake, ila ni umma kama nyinyi.
Hatukupuuza Kitabuni kitu chochote. Kisha watakusanywa
kwa Mola Wao. 39. Na wale waliokanusha Ishara Zetu ni
viziwi na mabubu walio gizani. Mwenyezi Mungu humpoteza
amtakaye na humweka katika njia iliyonyooka amtakaye.

40. Sema: Hebu jifikirieni kama ikiwajia adhabu ya
Mwenyezi Mungu au kikiwajia Kiyama, hivi mtamwomba
asiyekuwa Mwenyezi Mungu, ikiwa nyinyi ni wakweli?
41. Bali Yeye tu ndiye mtakayemuomba. Atawaondolea
mnayomuomba akitaka, na mtawasahau mnaowashirikisha.

42. Kwa hakika tulipeleka (Mitume) kwa mataifa yaliyoishi
kabla yako; tukawatia katika shida na dhiki ili wajifunze
kunyenyekea. 43. Mbona adhabu Yetu ilipowafikia hakuwa
wanyenyekevu? Lakini nyoyo zao zilikuwa ngumu na shetani

akawapambia waliyokuwa wakiyafanya. 44. Basi waliposahau
onyo walilopewa, tuliwafungulia milango ya kila kitu
(kizuri). Mpaka walipokuwa wanafurahia walivyopewa,
ghafla tuliwakamata na mara wakawa wenye kukata tamaa.
45. Ikakatwa mizizi ya watu waliodhulumu; na sifa njema ni
za Mwenyezi Mungu Mola Mlezi wa viumbe vyote.

46. Sema: Mwaonaje kama Mwenyezi Mungu akiwaondolea
kusikia kwenu na kuona kwenu na akaziziba nyoyo zenu,
ni nani Mungu mwingine isipokuwa Mwenyezi Mungu
awezaye kuwarudishia tena? Tazama jinsi tunavyozieleza
Aya kwa njia mbali mbali, kisha wao wanapuuza. 47. Sema:
Mwaonaje ikiwafikia adhabu ya Mwenyezi Mungu kwa
ghafla (bila onyo) au wazi wazi (kwa kutangulia onyo),
nani wataangamizwa isipokuwa watu waliodhulumu?
48. Na hatuwatumi Mitume ila ni wabashiri na waonyaji.
Basi wenye kuamini na wakafanya wema, haitakuwa hofu
juu yao wala hawatahuzunika. 49. Na wale waliokadhibisha
Ishara Zetu itawagusa adhabu kwa sababu ya walivyokuwa
wakipotoka. 50. Sema: Siwaambii kuwa ninazo hazina za
Mwenyezi Mungu, wala sijui ghaibu; wala siwambii mimi ni
Malaika. Mimi sifuati ila ninayofunuliwa. Sema: Je, kipofu
na mwenye kuona wako sawa? Hivi hamfikiri?

51. Na waonye kwayo wale wanaoogopa kwamba
watakusanywa kwa Mola wao. Hawana mlinzi wala
mwombezi isipokuwa Yeye ili wapate kumcha Mungu.
52. Wala usiwafukuze wale wanaomwomba Mola Wao
asubuhi na jioni kwa kutaka radhi Yake; si juu yako hisabu
yao hata kidogo, wala hisabu yako si juu yao hata kidogo,
kwamba uwafukuze na uwe miongoni mwa madhalimu.
53. Na namna hii tumewajaribu wao kwa wao ili waseme: Je,

hao ndio ambao Mwenyezi Mungu amewafadhili miongoni
mwetu? Kwani Mwenyezi Mungu hawajui wanaoshukuru?
54. Na wanapokujia wale wanaoamini Ishara Zetu waambie:
Amani iwe juu yenu (Assalam alaykum), Mola Wenu Mlezi
amejiwajibisha mwenyewe awe na huruma; ya kwamba
atakayefanya miongoni mwenu uovu kwa ujinga, kisha
akatubu baada yake na akajirekebisha, basi Yeye ni Mwingi
wa maghufira Mwenye kurehemu. 55. Namna hii tunazieleza
Ishara na ili njia ya wakosefu ibainike.
56. Sema: Nimekatazwa kuwaabudu wale mnaowaomba
badala ya Mwenyezi Mungu. Sema: Sifuati mpendavyo
nyie, maana hapo nitapotea na sitakuwa miongoni mwa
walioongoka. 57. Sema: Hakika mimi ninayo dalili wazi
itokayo kwa Mola Wangu, nanyi mmeikadhibisha. Mimi sina
hayo mnayoyahimiza yaje. Hapana hukumu ila ya Mwenyezi
Mungu. Anasimulia yaliyo kweli; naye ni Mbora wa
wanaohukumu. 58. Sema: Lau ningelikuwa nayo mnayotaka
yaje haraka, lingekwishakatwa shauri hili baina yangu na
nyie. Na Mwenyezi Mungu anawajua zaidi madhalimu.
59. Na ziko kwake funguo za ghaibu; hakuna azijuaye ila
Yeye; anajua kilichomo nchi kavu na kilichomo baharini. Na
halidondoki jani lolote ila analijua, wala punje katika giza
la ardhi, wala kinyevu wala kikavu, ila kimo katika Kitabu
kinachobainisha.
60. Naye ndiye anayewafisha usiku; na anakijua
mlichokifanya mchana, kisha huwafufua wakati wa mchana
ili muda uliowekwa utimizwe. Kisha Kwake Yeye ndiyo
marejeo yenu; kisha awaambie mliyokuwa mkiyafanya.
61. Naye ndiye Mwenye nguvu za kushinda juu ya waja
Wake. Na huwapelekea waangalizi; hata mmoja wenu

yakimjia mauti wajumbe wetu humfisha nao hawazembei.
62. Kisha watarudishwa kwa Mwenyezi Mungu, Mola wao
wa haki. Hakika hukumu ni Yake; naye ni mwepesi kuliko
wote wanaohisabu.

63. Sema: Ni nani anayewaokoa katika giza la nchi kavu
na baharini? Mnamwomba kwa unyenyekevu na kwa sauti
ndogo: kama akituokoa na haya, hakika tutakuwa miongoni
mwa wanaoshukuru. 64. Sema: Mwenyezi Mungu huwaokoa
katika hayo na katika kila shida; kisha nyinyi mnamshirikisha.
65. Sema: Yeye ndiye awezaye kuwaletea adhabu kutoka juu
yenu au kutoka chini ya miguu yenu; au awavuruge (muwe)
makundi, na awaonjeshe baadhi yenu jeuri ya wenzao.
Tazama jinsi tunavyozieleza Ishara kwa njia mbali mbali
ili wapate kufahamu. 66. Lakini watu wako wanayakanusha
haya, nayo ni kweli. Sema: Mimi sikuwakilishwa juu yenu.
67. Kila ujumbe una wakati wake, na punde mtajua.

68. Na unapowaona wanaziingilia Aya Zetu kwa
mazungumzo ya upuuzi, basi jitenge nao mpaka waingie katika
mazugumzo mengine. Na kama shetani akikusahaulisha, basi
usikae, baada ya kukumbuka, pamoja na watu madhalimu.
69. Wala wanaomcha Mungu hawana jukumu lolote kwao,
lakini ni kukumbusha tu, ili wajiepushe. 70. Na waache wale
wanaoifanya dini yao kuwa mchezo na upuuzi na yakawahadaa
maisha ya duniani. Lakini wakumbushe huu (ukweli): isije
nafsi ikafungwa kwa sababu ya yale iliyoyatenda. Haina
mlinzi wala mwombezi isipokuwa Mwenyezi Mungu. Na
hata ikatoa fidia ya kila namna haitapokelewa. Hao ndio
waliofungwa kwa sababu ya yale waliyoyachuma. Watapata
kinywaji cha maji ya moto mno, na adhabu chungu kwa
sababu ya waliyokuwa wakiyakanusha.

71. Sema: Je, tumwombe asiyekuwa Mwenyezi Mungu,
kitu mbacho hakitunufaishi wala kutudhuru, na turudishwe
nyuma baada ya Mwenyezi Mungu kutuongoza? Kama
yule ambaye mashetani wamemfanya mwendawazimu
akawa anatangatanga duniani? Anao marafiki wanaomwita
aje kwenye njia nzuri: ‘Njoo nasi!’ (lakini haendi). Sema:
Mwongozo hasa ni mwongozo wa Mwenyezi Mungu; na
tumeamrishwa tusilimu kwa Mwenyezi Mungu, Mola wa
viumbe vyote. 72. Na dumisheni Swala na mcheni Yeye;
naye ndiye ambaye Kwake mtakusanywa. 73. Naye ndiye
aliyeziumba mbingu na ardhi kwa (uwiano wa) kweli. Na
siku anayosema ‘iwe!’ basi huwa. Kauli Yake ni kweli. Na
ufalme ni Wake siku hiyo itakapopulizwa tarumbeta. Mjuzi
wa ghaibu na yanayoonekana. Naye ndiye Mwenye hekima
Mwenye habari. 74. Na pindi Ibrahim alipomwambia baba
yake Azar: ‘Unawafanya masanamu kuwa miungu? Hakika
ninakuona wewe na watu wako mko katika upotofu ulio wazi
wazi’.

75. Na ndipo tukamwonyesha Ibrahim ufalme wa
mbingu na ardhi ili awe katika wenye yakini. 76. Usiku
ulipomwingilia akaona nyota akasema, Huyu ndiye Mola
wangu Mlezi!. Ilipotua akasema: sipendi wanaotua. 77. Na
alipouona mwezi unachomoza akasema: Huyu ndiye Mola
wangu Mlezi! Ulipotua akasema: Asiponiongoza Mola
Wangu Mlezi, hakika nitakuwa katika watu wapotevu. 78. Na
alipoliona jua linachomoza alisema: Huyu ndiye Mola wangu
Mlezi! Huyu ni mkubwa kuliko wote! Lilipotua, akasema:
‘Enyi watu! Mimi simo katika hayo mnayoyashirikisha’.
79. Mimi nimeuelekeza uso wangu kwa yule aliyeziumba
mbingu na ardhi, nikiachana na dini zote nyingine, tena

mimi si katika mapagani. 80. Na watu wake wakamhoji.
Akasema: Je, mnanihoji juu ya Mwenyezi Mungu na hali
Yeye ameniongoza? Wala siogopi wale mnaowashirikisha
naye; isipokuwa Mola Wangu Mlezi akitaka kitu (ndipo
kitatokea). Mola Wangu ana wasaa wa kujua kila kitu. Kwa
nini hamjikosoi? 81. Nitaogopaje hao mnaowashirikisha ilhali
nyie hamwogopi kumshirikisha Mwenyezi Mungu na kitu
ambacho hakuwapa ruhusa yeyote? Basi kundi gani katika
mawili haya linastahiki kupata amani kama nyinyi mnajua?
82. Wale walioamini na hawakuchanganya imani yao na
maovu, hao ndio watakaopata amani na ndio walioongoka.
83. Na hiyo ndiyo hoja Yetu tuliyompa Ibrahim kuhojiana na
watu wake. Tunamuinua vyeo yule tumtakaye. Hakika Mola
Wako ndiye Mwenye hekima, Mjuzi. 84. Na tukamtunukia
Ibrahim (Abraham) Is-haq (Isaac) na Yakub (Jacob); kila
mmoja tulimuongoza. Na Nuh (Noah) tulimwongoza zamani.
Na katika kizazi chake Daud (David) na Suleiman (Solomon)
na Ayyub (Job) na Yusuf (Josef) na Musa (Moses) na Harun
(Aaron). Na kama hivyo tunawalipa wafanyao mema.

85. Na Zakariya (Zechariah) na Yahya (John) na Isa (Jesus)
na Ilyas (Elias) , wote ni katika wema. 86. Na Ismail na Al-
Yasa (Elisha) na Yunus (Jonas) na Lut (Lot); na kila mmoja
tulimpa upendeleo juu ya walimwengu wote. 87. Na kutokana
na baba zao na vizazi vyao na ndugu zao. Na tukawachagua
na kuwaongoza katika njia iliyonyooka. 88. Huo ni uongozi
wa Mwenyezi Mungu. Kwa huo humwongoza amtakaye
katika waja Wake. Na kama wangelishirikisha bila shaka
yangeliporomoka kwao yale waliyokuwa wakiyatenda.
89. Hao ndio tuliowapa Kitabu na utawala na utume. Kama
hawa wakiyakataa hayo, basi tumekwisha yawakilisha

Kwa watu wasioyakataa. [90.] Hao ndio ambao Mwenyezi Mungu amewaongoza, basi fuata mwongozo wao. Sema: Siwaombi ujira juu ya haya. Hayakuwa haya ila mawaidha kwa walimwengu wote. [91.] Na hawakumheshimu Mwenyezi Mungu inavyopasa kumheshimu, waliposema: Mwenyezi Mungu hakumteremshia mwanadamu chochote! Sema: nani aliyekileta Kitabu alichokuja nacho Musa chenye nuru na mwongozo kwa watu; mlichokifanya kurasa-kurasa. Baadhi yake mkazionesha lakini nyingi mkazificha. Na mkafunzwa mliyokuwa hamyajui ninyi wala baba zenu? Sema: Ni Mwenyezi Mungu! Kisha waache waendelee na porojo zao.

[92.] Na hiki ni Kitabu tulichokiteremsha, kilichobarikiwa, chenye kusadikisha yale yaliyokitangulia. Na ili uwaonye watu wa Makka (Ummul qura) na walio viungani mwake. Na wale wanaoamini Akhera, wanakiamini hiki; nao huzihifadhi Swala zao. [93.] Na ni nani awezaye kuwa mwovu zaidi kuliko yule anayemzulia uwongo Mwenyezi Mungu, au asemaye nimeletewa Wahyi na hali hakuletewa wahyi wowote, na asemaye (nami) nitateremsha kama vile alivyoviteremsha Mwenyezi Mungu? Na lau ungewaona waovu wanapotapatapa wakati wa kukata roho, huku Malaika wamewanyooshea mikono (wakiwaamuru). 'Zitoeni roho zenu!'Leo mtalipwa adhabu ya kufedhehesha kwa sababu ya yale mliyokuwa mkiyasema juu ya Mwenyezi Mungu yasiyokuwa haki, na mlikuwa mkizifanyia kiburi Aya Zake.

[94.] Hakika mmetujia hali ya kuwa ninyi ni wapweke kama tulivyowaumba mara ya kwanza; na mmeviacha (vyoote) tulivyowapa nyuma yenu. Na hatuwaoni waombezi wenu pamoja nanyi, ambao mlidai kuwa ni washirika (wa Mwenyezi Mungu). Kwa hakika yamekatika mahusiano

baina yenu, na yamewapotea mliyokuwa mkidai. 95. Hakika
Mwenyezi Mungu ndiye mpasuaji mbegu na kokwa
(zikachipua). Humtoa aliye hai kutoka maiti na ni mtoaji wa
maiti kutoka aliye hai. Huyo ndiye Mwenyezi Mungu . Vipi
mnageuzwa (na ukweli)?

96. Ndiye mpambazuaji wa asubuhi; ameufanya usiku
kuwa mapumziko na utulivu, na jua na mwezi (kwenda) kwa
hesabu. Huo ndiyo mpangilio wa Mwenye nguvu, Mjuzi.
97. Na Yeye ndiye aliyewawekea nyota ili mwongozeke
kwazo katika giza la bara na baharini. Hakika tumezifafanua
ishara kwa watu wanaojua. 98. Na Yeye ndiye aliyewaanzisha
nyinyi kutokana na mtu mmoja. Hapa ni mahali pa kufikia
na kundokea. Hakika tumezifafanua Aya zetu kwa watu
wanaojua.

99. Naye ndiye aliyeteremsha maji kutoka mawinguni na
kwayo tukatoa mimea ya kila aina. Baadhi yake tukatoa
mimea ya majani ambayo ndani yake tunatoa punje
zilizopandana. Na katika mitende yakatoka kwenye makole
yake mashada yaliyoinama, na bustani za mizabibu na
mizaituni na makomamanga; yanayofanana na yasiyofanana.
Angalieni matunda yake yanapozaa na kuiva! Hakika katika
hayo kuna ishara nyingi (za kumtambua Mungu) kwa watu
wanaotaka kuamini. 100. Na bado wakamfanyia Mwenyezi
Mungu washirika majinni; na hali Yeye ndiye aliyewaumba
(hao). Na wakamsingizia, bila ya kuelewa, kuwa ana wana
wa kike na wa kiume. Ametakasika na ametukuka na hayo
wanayombandikiza. 101. Yeye ndiye Mbunifu wa mbingu
na ardhi. Inakuwaje awe na mwana na hakuwa na mke?
Ameumba vitu vyote. Naye ana Ujuzi kamili wa kila kitu.
102. Huyo ndiye Mwenyezi Mungu Mola Wenu Mlezi hakuna

Mola (mwingine) isipokuwa Yeye; Muumba wa kila kitu. Kwa hivyo mwabuduni Yeye. Na Yeye ni mtegemewa wa kila kitu. 103. Macho hayamfikii Yeye; bali Yeye huyafikia macho. Naye ni Mpole Mwenye habari. 104. Hakika zimewajia hoja wazi za kuwafungua macho kutoka kwa Mola Wenu. Basi atakayefungua macho ni kwa faida yake mwenyewe, na atakayejifanya kipofu ni hasara yake mwenyewe. Nami (Muhhammad) sipo hapa kufuatilia kila mlitendalo. 105. Na ndiyo hivi tunazieleza Aya kwa njia mbali mbali, wakwambie ‘umesoma’. Na ili tuyabainishe kwa watu wanaojua.

106. Fuata uliyopewa wahyi kutoka kwa Mola Wako. Hakuna Mola (mwingine) isipokuwa Yeye, na achana na washirikina. 107. Na kama Mwenyezi Mungu angetaka wasingeshirikisha. Na hatukukufanya uwe dikteta juu yao, wala kuwa wewe ndiye mtunzaji wa mambo yao. 108. Wala msiwatukane wale wanaoomba asiyekuwa Mwenyezi Mungu, wasije wakamtukana Mwenyezi Mungu kwa jeuri bila ya kujua. Namna hiyo tumelipambia kila taifa vitendo vyao. Kisha marejeo yao yatakuwa kwa Mola Wao Mlezi, naye atawaambia yale waliyokuwa wakiyatenda. 109. Na waliapa kwa Mwenyezi Mungu kwa ukomo wa viapo vyao, kuwa ikiwafikia ishara bila shaka wataiamini. Hakika ishara ziko kwa Mwenyezi Mungu tu. Na ni kitu gani kitakachowatambulisha ya kuwa zitakapowafikia hawataamini?

110. Na tutazigeuza nyoyo zao na macho yao kama walivyokuwa hawakuamini mara ya kwanza. Na tutawaacha katika upotevu wao wakimangamanga. 111. Na lau kama tungewateremshia Malaika, na wafu wakazungumza nao, na tukawakusanyia kila kitu ana kwa ana, wasingeliamini

ila atake Mwenyezi Mungu. Lakini wengi wao wamo ujingani. 112. Na kama hivyo tumemfanyia kila Nabii adui, mashetani watu na majini. Baadhi yao wanawapa wenzao maneno ya kupambapamba ili kuwahadaa.Na kama Mola Wako angelitaka wasingeliyafanya hivyo. Basi waache na wanayoyatunga. 113. Na acha nyoyo za wale wasioamini akhera zifurahie (uzushi) huo na wao wauridhie na wachume (kutokana na uzushi huo) yale watakayoweza kuyachuma. 114. Je, nimtafute hakimu asiyekuwa Mwenyezi Mungu na hali Yeye ndiye aliyewateremshia Kitabu kinachofafanua? Na wale tuliowapa Kitabu wanajua kwamba kimeteremshwa na Mola Wako kwa haki. Basi usiwe miongoni mwa wanaotia shaka.

115. Na limetimia neno la Mola Wako kwa ukweli na uadilifu; hakuna wa kubadilisha neno Lake. Na Yeye ni Msikizi, Mjuzi. 116. Na ukiwatii wengi katika waliomo ardhini watakupoteza na njia ya Mwenyezi Mungu. Hawafuati ila dhana na hawakuwa ila wenye kuzua tu. 117. Hakika Mola Wako anawajua vyema wanaopotea njia Yake na anawajua sana wanaoongoka. 118. Basi kuleni katika (wanyama, ndege) waliosomewa jina la Mwenyezi Mungu, ikiwa nyinyi mnaziamini ishara Zake.

119. Mna nini hamli katika wale waliosomewa jina la Mwenyezi Mungu; na ilhali amewafafanulia aliyowaharamishia, isipokuwa vile msivyokuwa na budi navyo? Na hakika wengi wanawapoteza (wengine) kwa kufuata uchu wao bila ya kujua (haram na halal). Hakika Mola Wako anawajua vyema wanaovuka mipaka. 120. Na acheni dhambi zilizo dhahiri na zilizofichika. Hakika wale wanaochuma dhambi watalipwa yale waliyokuwa wakiyachuma. 121. Wala

msile wale wasiosomewa jina la Mwenyezi Mungu, kwani hilo ni upotofu. Na hakika mashetani wanawafunza marafiki zao kubishana nanyi. Na kama mkiwatii, hakika mtakuwa mapagani. [122.] Je, aliyekuwa maiti kisha tukamhuisha na tukampa nuru, inakwenda naye mbele za watu, mfano wake ni kama yule aliye gizani asiyeweza kutoka humo? Namna hiyo wamepambiwa makafiri waliyokuwa wakiyafanya.

[123.] Na kama hivyo, katika kila mji tumeweka wakubwa wa waovu (kuwa viongozi wao) wafanye vitimbi humo; wala hawamfanyii vitimbi yeyote isipokuwa wanajifanyia wenyewe, lakini hawatambui. [124.] Na zinapowafikia ishara husema: Hatutaaamini mpaka tupewe sawa na yale waliyopewa Mitume wa Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu ndiye Mjuzi zaidi wa kujua mahali anapoweka ujumbe Wake. Yatawafika wale waovu madhila yatokayo kwa Mwenyezi Mungu na adhabu kali kwa sababu ya vitimbi walivyokuwa wakivifanya. [125.] Basi yule ambaye Mwenyezi Mungu anataka kumwongoza hukunjua kifua chake kwenye Uislam; na yule anayetaka apotee hufanya kifua chake kina dhiki kimebana, kana kwamba anakwea mbinguni. Kama hivi anajaalia Mwenyezi Mungu adhabu juu ya wale wasioamini.

[126.] Na huu (Uislamu) ndio njia ya Mola Wako Mlezi iliyonyooka. Hakika tumezipambanua Ishara kwa watu wenye kukumbuka. [127.] Watapata nyumba ya amani kwa Mola Wao naye ndiye rafiki yao, kwa sababu ya yale waliyokuwa wakiyatenda. [128.] Na siku atakapowakusanya wote, (awaambie): Enyi jamii ya majinni! Hakika nyinyi mmewakamata wanadamu wengi mno! Na marafiki zao katika wanadamu waseme:'Mola Wetu Mlezi! Tulinufaishana sisi na wao, na tumefikia muda wetu uliotuwekea'. Atasema:

'Moto ndio makazi yenu, mtadumu humo, isipokuwa pale
apendavyo Mwenyezi Mungu'. Hakika Mola Wako ndiye
Mwenye hekima, Mjuzi.
129. Na kama hivi tunawafanya waovu wapendane wao
kwa wao, kwa sababu ya yale waliyokuwa wakiyachuma.
130. Enyi makundi ya majini na watu! Je, hawakuwafikia
Mitume miongoni mwenu kuwasomea Aya Zangu
na kuwaonya kukutana na siku yenu hii? Watasema:
Tumeshuhudia juu ya nafsi zetu. Na yaliwadanganya maisha
ya dunia; nao watajishuhudia wenyewe kwamba wao
walikuwa Makafiri. 131. Hayo ni kwa sababu ya kuwa Mola
Wako hakuwa ni Mwenye kuiangamiza miji kwa dhuluma
na hali wenyewe wameghafilika. 132. Na wote wana daraja
mbali mbali kutokana na yale waliyoyatenda. Na Mola Wako
si Mwenye kughafilika na yale wanayoyatenda.
133 Na Mola Wako ndiye Mkwasi, Mwenye rehema.
Akipenda atawaaondoa ninyi na kuweka wengine awapendao
baada yenu; kama alivyowaanzisha kutokana na kizazi
cha watu wengine. 134 Hakika mnayoahidiwa yatafika tu;
wala hamtaweza (kuepuka). 135 Sema: Enyi watu wangu!
Fanyeni vile muwezavyo; na mimi nafanya. Mtakuja jua ni
nani atakuwa na makazi mema mwishoni. Hakika waovu
hawafaulu. 136 Na wamemwekea Mwenyezi Mungu sehemu
katika mimea na wanyama aliowaumba! Wakasema, 'hii ni
sehemu ya Mungu' wanadai, 'na hii ni sehemu ya waungu
wetu!' Vile vya miungu wao (ati) havifiki kwa Mwenyezi
Mungu, na vya Mwenyezi Mungu (ati) huwafikia miungu
yao! Ni uovu kabisa hivyo wanayoyahukumu.
137. Ndiyo hivyo basi hao wanaowashirikisha
wamewapambia washirikina wengi kuwauwa watoto wao

wenyewe. Ili wawaangamize na wawafanye wachanganyikiwe katika dini yao. Laiti Mwenyezi Mungu angependa wasingalifanya hayo. Basi waache na wanayoyazua. 138. Na husema: 'Wanyama hawa na mimea hii ni mwiko, hawatokula ila wale tuwatakao sisi tu' kama wanavyodai. Na 'Wanyama hawa imekatazwa kuwapanda', na 'hawa, wasitaje jina la Mwenyezi Mungu (wakati wa kuchinja)'. Wanamzulia uwongo Mwenyezi Mungu. Atawalipa kwa sababu ya uzushi wao.

139. Na husema: 'Kilichomo matumboni mwa wanyama hawa ni kwa ajili ya waume tu na kimekatazwa kwa wanawake wetu' Lakini ikiwa kesha kufa tumboni, hugawana wote. Punde atawaadhibu kwa tendo la kumnasibishia Mwenyezi Mungu imani hizo za kipagani. Hakika Yeye ni Mwenye hekima, Mjuzi. 140 Hakika wamehasirika wale waliowaua watoto wao kwa upumbavu bila ya elimu, na wakaharamisha alivyowaruzuku Mwenyezi Mungu, kwa kumzulia Mwenyezi Mungu. Hakika wamepotea wala hawakuwa wenye kuongoka. 141 Naye ndiye aliyeumba bustani zenye kutambaa juu ya chanja, na zisizo tambaa. Na mitende, na mimea yenye mazao mbali mbali, na mizaituni na mikomamanga; inayofanana na isiyofanana. Kuleni matunda yake inapozaa, na toeni haki yake siku ya kuvuna. Wala msifanye ufujaji; hakika Yeye hawapendi wafujaji.

142. Na katika wanyama amewaumbieni wabebao mizigo na watoao sufu. Kuleni katika wale aliowaruzuku Mwenyezi Mungu, na msifuate nyayo za Shetani, kwani yeye ni adui wenu mkuu. 143. (Hebu chukua) wanyama wafugwao wanane katika jozi nne: kondoo wawili (dume na jike) na mbuzi wawili (kadhalika). Sema, je, (Mwenyezi Mungu) amekataza

(yupi kati yao?) wale madume wawili au majike wawili? Au ni watoto waliyomo katika matumbo ya wale majike wawili? Niambieni kwa utaalamu, ikiwa (madai yenu) ni ya ukweli.

144. Na jozi ya ngamia na jozi ya ng'ombe. Sema, je ameharamisha madume mawili au majike mawili? Au waliyo matumboni mwa majike mawili? Au nyinyi mlikuwepo wakati Mwenyezi Mungu alipowaamuru haya? Basi ni nani anayefanya makosa makubwa zaidi yule anayemzulia Mwenyezi Mungu uwongo, ili awapoteze watu bila ya elimu yeyote? Hakika Mwenyezi Mungu hawaongozi waovu.
145. Sema: Sioni katika yale niliyofunuliwa mimi nyama yeyote iliyoharamishwa kwa mlaji kuila, isipokuwa iwapo ni mzoga au damu iliyomwagwa, au nyama ya nguruwe. Hivyo ni uchafu. Au (akiwa) amechinjwa kwa njia ya upotofu kwa kutajiwa jina la asiyekuwa Mwenyezi Mungu (wakati wa kuchinja). Lakini aliyefikwa na dharura, siyo kwa kukusudia kuasi wala (kula) kupita kiasi, basi Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa maghufira, Mwenye kurehemu.
146 . Na kwa wale walio Mayahudi tuliharamisha kila mnyama/ndege mwenye kucha. Na katika ng'ombe na mbuzi na kondoo tuliwaharamishia shahamu yao; isipokuwa yale iliyobeba migongo yao, au matumbo, au iliyogandamana na mifupa. Tuliwalipa hivyo kwa sababu ya uasi wao. Na hakika sisi ndio wakweli.

147. Wakikukadhibisha, basi sema: Mola Wenu ana rehema iliyoenea, na wala adhabu Yake haizuiliwi kwa watu waovu.
148. Watasema Mapagani: 'Lau Mwenyezi Mungu angependa tusingelimshirikisha na mwingine; sisi wala baba zetu; wala tusingekataza chochote. Namna hii hii ndivyo walikadhibisha waliokuwa kabla yao mpaka wakaonja adhabu Yetu. Sema,

Je, mnayo elimu mtutolee? Nyinyi hamfuati ila dhana tu, na wala hamsemi ila uwongo tu.

149. Sema: Basi Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye hoja komesha. Na kama angelitaka angeliwaongoza nyote.
150. Sema: Leteni mashahidi wenu wanaoweza kushuhudia kuwa Mwenyezi Mungu ameharamisha haya. Wakitoa ushahidi, basi wewe usishuhudie pamoja nao. Wala usifuate matamanio ya wale waliozikadhibisha Ishara Zetu na wale wasioamini Akhera, na ambao humlinganisha Mola Wao na
wengine. 151. Sema: Njooni niwasomee aliyowaharamishia Mola Wenu: Kwamba msimshirikishe na chohote. Na wazazi wenu wafanyieni wema. Wala msiwaue watoto wenu kwa sababu ya umaskini; sisi tunawaruzuku nyinyi na wao. Wala msikurubie mambo machafu, yaliyodhihirika na yaliyofichika; wala msiue nafsi ambayo Mwenyezi Mungu ameharamisha (kuuawa), ila kwa njia ya haki na sharia. Hayo amewausia Mwenyezi Mungu ili myatie akilini.

152. Wala msiikaribie mali ya yatima isipokuwa kwa njia bora zaidi (kwa kuizidisha); mpaka afikie utu uzima. Na kamilisheni vipimo vya ujazo na uzani kwa uadilifu. Hatuikalifishi nafsi ila kwa uweza wake. Na msemapo semeni kwa haki na uadilifu hata kama ni kwa ndugu wa karibu. Na tekelezeni ahadi ya Mwenyezi Mungu. Haya amewausia ili mkumbuke

153. Na kwa hakika hii ndiyo njia yangu iliyonyooka, basi ifuateni wala msifuate njia nyingine, zikawatenga mbali na njia Yake (Mwenyezi Mungu). Hayo amewausia
ili muwe wacha mungu. 154. Kisha tulimpa Musa Kitabu, kwa kumtimizia (neema) yule aliyefanya wema; (kitabu)

kinachoelezea kwa urefu kila kitu, na mwongozo na rehema
ili wapate kuamini kukutana na Mola Wao.
155. Na hiki ni Kitabu tulichokiteremsha kilichobarikiwa.
Basi kifuateni na mcheni Mungu ili mrehemiwe. 156. Msije
mkasema Kitabu kimeteremshwa kwa mataifa mawili tu
kabla yetu, na sisi tulikuwa hatuna habari na waliyokuwa
wakiyasoma. 157. Au mkasema: Lau tungeteremshiwa
Kitabu bila shaka tungekuwa waongofu zaidi kuliko wao.
Sasa imewafikia hoja ya wazi kutoka kwa Mola Wenu, na
uwongofu na rehema. Basi ni nani dhalimu mkubwa kuliko
anayezikadhibisha Aya za Mwenyezi Mungu na akajitenga
nazo? Tutawalipa wale wanaojitenga na Aya zetu adhabu
mbaya kwa sababu ya kule kujitenga kwao. 158. Je, wanangoja
jingine ila wawajie Malaika au awajie Mola Wako Mlezi
au ziwafikie baadhi ya Ishara za Mola Wako Mlezi? Siku
zitakapofika baadhi ya Ishara za Mola Wako Mlezi, siku hiyo
haitamfaa mtu imani yake kama hakuwa alikwisha amini, au
hakufanya mema katika imani yake. Sema: Ngojeni, sisi pia
tunangoja. 159. Hakika wale walioigawa dini yao na wakawa
makundi makundi, huna uhusiano nao wowote. Hakika
shauri lao liko kwa Mwenyezi Mungu tu; kisha atawaambia
yale waliyokuwa wakiyafanya.
160. Afanyae wema atalipwa mfano wake mara kumi, na
afanyaye ubaya hatalipwa isipokuwa mfano wake tu, nao
hawatadhulumiwa. 161. Sema: Kwa hakika miye Mola Wangu
ameniongoza katika njia iliyonyooka, dini yenye msimamo;
ndiyo dini ya Ibrahim mnyoofu. Wala hakuwa miongoni
mwa washirikina.
162. Sema: Hakika Swala yangu na ibada zangu na
uhai wangu na mauti yangu, ni kwa ajili ya Mwenyezi

Mungu Mola wa walimwengu. 163. Hana mshirika. Na
hayo ndiyo niliyoamrishwa, na mimi ni wa mwanzo wa
wale wananaosalimu amri Kwake. 164. Sema: Je, nimtafute
asiyekuwa Mwenyezi Mungu awe ndiye mungu mlezi na
ilhali Mwenyezi Mungu ndiye Mlezi wa kila kitu? Na wala
haijichumii nafsi yoyote (dhambi) isipokuwa yajichumia
yenyewe tu, na wala mbebaji hatabeba mzigo wa mwingine.
Kisha marejeo yenu ni kwa Mola Wenu, naye atawaambia
yale mliyokuwa mkikinzana. 165. Naye ndiye aliyewafanya
nyie kuwa manaibu wake hapa duniani, na akawainua
baadhi yenu juu ya wengine kwa vyeo, ili awajaribu katika
alivyowapa. Hakika Mola Wako ni mwepesi wa kuadhibu; na
hakika Yeye ni Mwingi wa maghufira, Mwenye kurehemu.

## 7. Sura Al-A'araf

## SURA YA MIINUKO

Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa huruma,
Mwenye kurehemu.

1 *Alif Lam Mim Swad*.

2 Kitabu kilichoteremshwa kwako. Basi usiwe na dhiki kifuani
mwako kwa ajili yake, ili uweze kuonya kwacho na kiwe ni
ukumbusho kwa wanaoamini. 3 Fuateni mliyoteremshiwa
kutoka kwa Mola Wenu Mlezi; wala msifuate wasimamizi
wengine badala Yake. Ni machache mno mnayoyakumbuka.
4 Ni miji mingapi tuliiangamiza?! Iliwafikia adhabu Yetu
usiku au wakiwa wamepumzika (kulala) mchana. 5 Basi
hakikuwa kilio chao, ilipowafikia adhabu Yetu, isipokuwa

kusema tu: Hakika sisi tulikuwa waovu. 6 Kwa hakika
tutawauliza wale waliopelekewa (Mitume) na pia kwa hakika
tutawauliza (Mitume) waliopelekwa. 7 Tena kwa hakika
tutawasimulia kwa ujuzi, wala hatukuwa mbali. 8 Na kipimo
siku hiyo kitakuwa ni ukweli na haki. Basi ambao uzani wao
utakuwa mzito, hao ndio wenye kufaulu. 9 Na ambao uzani
wao utakuwa hafifu, basi hao ndio waliozitia hasara nafsi zao
kwa sababu ya kuzidhulumu Ishara Zetu.

10 Na hakika tumewamakinisha katika ardhi na
tukawawekea humo mahitaji ya maisha. Ni shukrani ndogo
mnazotoa. 11 Na hakika tuliwaumba, kisha tukawatia sura,
kisha tukawaambia Malaika: inameni kwa kumheshimu
Adam. Basi wakainama wote isipokuwa Iblisi hakuwa
miongoni mwa waliosujudu. 12 Akasema (Mwenyezi
mungu): Nini kilichokuzuia usisujudi nilipokuamrisha?
Akasema:’ Mimi ni bora kuliko yeye, umeniumba kwa moto
naye umemuumba kwa udongo. 13 Akasema: Basi shuka
kutoka huko, haikufai kufanya kiburi humo. Basi toka!
Hakika wewe ni miongoni mwa walio duni. 14 Akasema:
Nipe muda mpaka siku watakapofufuliwa. 15 Akasema
(Mwenyezi mungu): Utakuwa katika waliopewa muda.
16 Akasema: Kwa kuwa umenihukumia upotofu, basi hakika
nitawavizia katika njia Yako iliyonyooka. 17 Kisha hakika
nitawazukia kwa mbele yao na nyuma yao na kuumeni kwao
na kushotoni kwao; wala hutawakuta wengi wao ni wenye
kushukuru. 18 Akasema: Toka humo! Nawe umefedheheka
na umekwisha fukuzwa. Atakayekufuata miongoni mwao,
hakika nitaijaza Jahannam kwa nyinyi nyote.

19. Na wewe Adam! Kaa wewe na mkeo katika Bustani
(Pepo); na kuleni humo maridhawa popote mpendapo,

wala msiukaribie mti huu, msije mkawa miongoni mwa waliodhulumu (nafsi zao). 20. Basi shetani aliwatia wasiwasi ili kuwafichulia tupu zao walizofichiwa. Na akasema: Mola Wenu Mlezi hakuwakataza mti huu isipokuwa (kwa sababu) msije mkawa Malaika au kuwa miongoni mwa wanaoishi milele. 21. Na akawaapia: Kwa hakika mimi ni miongoni mwa watoa nasaha kwenu.

22. Basi akawateka kwa hadaa. Walipouonja mti ule, tupu zao ziliwafichukia, wakaanza kujibandika majani ya kwenye Bustani (Pepo). Na Mola Wao akawaita: Je, sikuwakataza mti huo na kuwaambia kwamba shetani ni adui yenu wa dhahiri? 23. Wakasema: Mola Wetu Mlezi! Tumezidhulumu nafsi zetu; na kama hutatusamehe na kutuonea huruma tutakuwa miongoni mwa waliohasirika. 24. Akasema: tokeni! (hali ni ) maadui nyinyi kwa nyinyi; na duniani ndiyo yatakuwa makao yenu na starehe yenu kwa muda. 25. Akasema: Mtaishi humo na mtafia humo na kutoka humo mtafufuliwa.

26. Enyi wanadamu! Hakika tumewateremshia vazi lifichalo uchi wenu na kwa kujipamba. Lakini vazi la ucha Mungu ndiyo bora Zaidi. Hiyo ni katika Ishara za Mwenyezi Mungu ili wapate kukumbuka. 27. Enyi wanadamu! Shetani asiwatie katika fitina, kama alivyowatoa wazazi wenu katika Bustani (Pepo), akawavua nguo zao kuwaonyesha tupu zao. Hakika yeye na kabila lake anawaona na nyinyi hamuwaoni. Hakika tumewajaalia mashetani kuwa marafiki wa wasio amini.

28. Na wanapofanya machafu husema: Tumewakuta nayo baba zetu, na Mwenyezi Mungu ametuamrisha hayo. Sema: Hakika Mwenyezi Mungu haamrishi machafu; je, mnasema juu ya Mwenyezi Mungu msiyoyajua? 29. Sema: Mola Wangu

ameamrisha uadilifu, na mumuelekezee nyuso zenu kila
mnaposujudi, na muombeni Yeye tu kwa kumsafia dini. Kama
alivyowaumba kwanza ndivyo mtarudi. 30. Hali ya kuwa
kundi moja ameliongoa, na kundi jingine limethibitikiwa na
upotofu. Hakika wao waliwafanya mashetani kuwa watawala
wao badala ya Mwenyezi Mungu. Na wanadhani kwamba
wao wameongoka.

31. Enyi Wanadamu! Vaeni nguo zenu nzuri kila mahali
pa ibada, na kuleni na kunyweni wala msifanye ufujaji ,
hakika Yeye hawapendi wafanyao ufujaji. 32. Sema: Ni nani
aliyekataza (vitu) vizuri alivyovitoa Mwenyezi Mungu
kwa waja Wake, na pia vilivyo vizuri katika riziki? Sema:
Hivyo ni kwa wale walioamini katika maisha ya duniani,
ni vyao wao pekee siku ya Kiyama. Namna hii tunazieleza
Ishara kwa watu wajuao. 33. Hakika Mola Wangu amekataza
mambo machafu yaliyo wazi na yaliyofichika. Na dhambi,
na uasi bila ya haki. Na kumshirikisha Mwenyezi Mungu na
ambacho hakukiteremshia uthibitisho wowote. Na kumzulia
Mwenyezi Mungu msiyoyajua.

34. Kila umma una muda, utakapofika muda wao
hawatakawia (hata) saa moja wala hawatatangulia. 35. Enyi:
Wanadamu! Watakapowafikia Mitume kutoka miongoni
mwenu, wakawaeleza Aya Zangu, basi watakaomcha Mungu
na wakarekebisha mwenendo wao, haitakuwa hofu juu
yao wala hawatahuzunika. 36. Na wale watakaokadhibisha
Aya zetu na kuzifanyia kiburi, hao ndio watu wa motoni,
watadumu humo. 37. Basi ni nani dhalimu zaidi kuliko yule
amzuliaye Mwenyezi Mungu uwongo, au anayezikadhibisha
Aya Zake? Hao ndio litawafikia fungu lao waliloandikiwa,
mpaka watakapowafikia watumishi wetu (Malaika), kuwatoa

roho, watawauliza: Wako wapi mliokuwa mkiwaabudu badala ya Mwenyezi Mungu? Watasema wametupotea. Na watajishuhudia wenyewe kwamba wao walikuwa makafiri.

[38.] (Mwenyezi Mungu) Atasema: 'Ingieni motoni pamoja na mataifa yaliyopita kabla yenu, majini na watu'. Kila utakapoingia umma utalaani wenzao. Mpaka watakapokusanyika wote humo, wa mwisho watawasemea wa mwanzo wao: 'Mola wetu Mlezi! Hao ndio waliotupoteza. Basi uwape adhabu ya moto maradufu. (Mwenyezi Mungu) Atasema: 'Itakuwa maradufu kwenu nyote, lakini hamjui tu'. [39.] Na wa mwanzo watawaambia wa mwisho wao; 'Na nyie pia hamkuwa na ubora wowote kuliko sisi. Basi onjeni adhabu kwa sababu ya yale mliyokuwa mkiyachuma'.

[40.] Hakika wale waliozikanusha Aya zetu na kuzifanyia kiburi, hawatafunguliwa milango ya mbinguni; wala hawataingia Peponi hadi hapo dakawa (Kamba nene ya kufungia meli bandarini) itakapoweza kupita kwenye tundu ya sindano. Na hivi ndivyo tunavyowalipa wakosefu. [41.] Jahanamu itakuwa kitanda chao, na juu yao shuka za moto za kujifunika. Na hivi ndivyo tunavyowalipa madhalimu. [42.] Na wale walioamini na wakatenda mema; hatumkalifishi mtu yeyote ila kwa kadri ya uwezo wake; hao ndio watu wa Peponi, watadumu humo. [43.] Na tutaondoa chuki vifuani mwao; chini yao itapita mito. Na watasema: Sifa njema zote zinamstahiki Mwenyezi Mungu ambaye ametuongoza kwenye haya; na hatukuwa wenye kuongoka (wenyewe) kama asingetuongoza Mwenyezi Mungu; hakika Mitume wa Mola Wetu walileta ukweli na haki. Na watasikia mwenye kunadi: 'hii ndiyo Pepo mliyorithishwa kwa sababu ya yale mliyokuwa mkiyafanya'.

44. Na watu wa Peponi watawaita watu wa Motoni, kwamba
sisi tumekuta aliyotuahidi Mola Wetu ni kweli. Je, nanyi pia
mmekuta aliyowaahidi Mola Wenu kuwa kweli? Watasema,
ndio. Basi mtangazaji atatangazia, ‘Laana ya Mwenyezi
Mungu iwafike watu waovu’, 45. Ambao walikuwa wakizuia
njia ya Mwenyezi Mungu, na wakataka kuipotosha; nao
hawaiamini Akhera.

46. Na baina ya makundi mawili hayo litakuwepo pazia;
na juu ya miinuko watakuwako watu watakaowajua wote
kwa alama zao. Na wao watawaita watu wa Peponi: ‘Salaam
Alaykum’-Amani iwe kwenu! Wao bado hawajaingia humo
lakini wana matumaini. 47. Na yanapogeuzwa macho yao
kuelekea kwa watu wa Motoni, watasema: ‘Mola Wetu
Mlezi!’ Usituweke pamoja na watu waliodhulumu. 48. Na
watu walio kwenye miinuko watawaita watu wanaowajua
kwa alama zao, waseme: “Makundi yenu hayakuwafaa kitu,
wala mlivyokuwa mkijivunia!’. 49. Je, hawa siyo wale wale
mliokuwa mkiwaapia kwamba Mwenyezi Mungu hatawapa
rehema? Ingieni Peponi, hakuna hofu juu yenu wala
hamtahuzunika.

50. Watu wa Motoni watawaita watu wa Peponi:
‘Tumiminieni maji au chochote katika alivyowapa Mwenyezi
Mungu!’ Nao watawajibu: ‘Mwenyezi Mungu amevikataza
hivyo kwa makafiri’. 51. Wale ambao waliifanya dini yao
kuwa upuuzi na mchezo na yakawahadaa maisha ya dunia.
Basi leo sisi tunawasahau kama walivyosahau kukutana na
siku yao hii na kwa sababu walikuwa wakizikataa Aya Zetu.

52. Na hakika tumewaletea Kitabu tulichokipambanua
kwa ujuzi, ambacho ni mwongozo na rehema kwa watu
wanaoamini. 53. Je, lipo wanalolingojea isipokuwa mwisho

wake?. Siku utakapofika mwisho wa matukio, hapo watasema wale ambao hapo nyuma waliisahau: ‘Kweli!, Mitume wa Mola Wetu walileta haki! Hivi tunao waombezi watuombee; au turudishwe tena (duniani) tukafanye yasiyokuwa yale tuliyokuwa tukiyafanya?’ Hakika wamezitia hasarani nafsi zao na yamewapotea waliyokuwa wakiyazua.

54. Hakika Mola Wenu Mlezi ni Mwenyezi Mungu aliyeziumba mbingu na ardhi katika (kiasi cha ) siku sita. Utawala wake upo thabiti juu ya Kiti cha Enzi. Huufunika usiku kwa mchana, ufuatiao upesi upesi. Na jua na mwezi na nyota zinatumika kwa amri Yake. Fahamuni! Kuumba na amri ni Vyake. Ametukuka Mwenyezi Mungu Mola wa walimwengu wote. 55. Mwombeni Mola Wenu kwa unyenyekevu na kwa siri. Hakika Yeye hawapendi wapetukao mipaka. 56. Wala msifanye uharibifu katika ardhi baada ya kutengenea kwake; na mwombeni kwa kuogopa na kwa kutumai. Hakika rehema ya Mwenyezi Mungu iko karibu na wanaofanya mema.

57. Na Yeye ndiye azipelekaye pepo (zivumazo) kuwa bishara njema kabla ya kufika rehema Yake. Hata zinapobeba mawingu mazito tunayasukuma mpaka kwenye ardhi iliyokauka, kisha tunateremsha hapo maji; kwayo tukatoa kila matunda. Kama hivi tutawafufua wafu ili mpate kukumbuka. 58. Na ardhi nzuri hutoa mimea yake kwa idhini ya Mola Wake. Na mbaya haitoi ila kwa taabu. Namna hii tunazipambanua Aya kwa watu wanaoshukuru.

59. Hakika tulimtuma Nuh (Noah) kwa watu wake. Akasema: Enyi watu wangu! Mwabuduni Mwenyezi Mungu, hamna Mungu mwingine zaidi Yake. Hakika mimi ninawahofia na adhabu ya siku iliyo kuu. 60. Wakasema

wakuu wa watu wake: Hakika sisi tunakuona wewe umo
katika upotofu ulio wazi 61. Akasema: Enyi watu wangu!
Mimi simo katika upotevu, lakini mimi ni Mtume nitokaye
kwa Mola wa walimwengu wote. 62. Nawafikishia ujumbe
wa Mola Wangu na nawanasihi; na ninajua kwa Mwenyezi
Mungu msiyoyajua. 63. Je, mnastaajabu kuwafikia mawaidha
kutoka kwa Mola Wenu kupitia mtu anayetokana na nyinyi, ili
awaonyeni na ili mumche Mungu na ili mpate kurehemiwa?
64. Basi walimkadhibisha; nasi tukamwokoa yeye na
waliokuwa pamoja naye katika jahazi, na tukawazamisha
waliozikadhibisha ishara Zetu. Hakika wao walikuwa watu
vipofu.

65. Na kwa Adi (tulimpeleka) ndugu yao Hud, akasema:
Enyi watu wangu! Mwabuduni Mwenyezi Mungu. Nyinyi
hamna Mungu mwingine zaidi Yake. Hivi hamumchi?
66. Wakasema wakuu waliokufuru katika watu wake: Sisi
tunakuona umo katika upumbavu na tunakudhania ni
miongoni mwa waongo. 67. Akasema: Enyi watu wangu!
Mimi sina upumbavu wowote, bali mimi ni Mtume nitokaye
kwa Mola wa walimwengu. 68. Nawafikishia ujumbe wa
Mola Wangu, na mimi kwenu ni mtoa nasaha, mwaminifu.
69. Je, mnastaajabu kuwafikia ujumbe kutoka kwa Mola
Wenu Mlezi kupitia mtu anayetokana na nyie wa kuwaonya?
Na kumbukeni jinsi alivyowafanya nyie kuwa warithi baada
ya watu wa Nuh, na akawazidisha nguvu katika maumbile.
Hivyo kumbukeni neema za Mwenyezi Mungu ili mpate
kufaulu.

70. Wakasema: Je, umetujia ili tumwabudu Mungu mmoja
pekee tuviache walivyokuwa wakiviabudu baba zetu?
Basi tuletee unayotuahidi ukiwa ni katika wasemao kweli.

[71.] Akasema: Bila shaka adhabu na ghadhabu zimekwisha washukia kutoka kwa Mola Wenu. Hivi mnabishana nami juu ya majina mliyoyabuni nyinyi na baba zenu, ambayo Mwenyezi Mungu hakuteremsha dalili yoyote kuyahusu? Basi ngojeni; mimi pia ni pamoja nanyi katika wangojao. [72.] Basi tukamwokoa yeye na waliokuwa pamoja naye kwa rehema Zetu na tukakata mizizi ya wale waliokadhibisha Aya Zetu, na hawakuwa wenye kuamini.

[73.] Na kwa Thamud (tulimpeleka) ndugu yao Swaleh. Akasema: Enyi watu wangu! Mwabuduni Mwenyezi Mungu, nyinyi hamna Mungu mwingine zaidi Yake. Hakika umekwisha wafikieni ushahidi ulio wazi kutoka kwa Mola Wenu Mlezi. Huyu hapa ngamia (jike) wa Mwenyezi Mungu. Kwenu awe ni ishara. Mwacheni ale katika ardhi ya Mwenyezi Mungu, na msimdhuru, isije ikawaangamiza adhabu chungu ya Mwenyezi Mungu. [74.] Na kumbukeni alipowafanya warithi baada ya Ad na akawafanyia makazi (mazuri) katika ardhi; mkajenga majumba ya fahari katika nyanda zake na mkachonga majumba katika majabali. Basi zikumbukeni neema za Mwenyezi Mungu, wala msifanye ufisadi katika ardhi. [75.] Wakasema waheshimiwa waliojaa kiburi katika watu wake, kuwaambia wananchi wanyonge walioamini kati yao: Hivi nyinyi mnajua kuwa Swaleh ametumwa na Mola Wake?! Wakajibu, ndiyo sisi tunayaamini yale aliyotumwa kwa ajili yake. [76.] Wale wenye kiburi wakasema: ‘Basi sisi hatuyakubali hayo mnayoyaamini’. [77.] Wakamkata miguu na kumwua yule ngamia jike na wakaasi amri ya Mola Wao Mlezi na wakasema: ‘Wee Swaleh! Haya, tuletee unayotuahidi ikiwa wewe kweli ni miongoni mwa Mitume’. [78.] Wakapigwa ghafla kwa tetemeko la ardhi! Asubuhi kulipokucha wakawa

wamelala kubong'oka majumbani mwao,( wamekufa)!
79. Basi Swaleh akawaacha na kusema: Enyi watu wangu!
Kwa hakika nimewafikishia ujumbe wa Mola Wangu na
nikawanasihi, lakini (nyinyi) hampendi wenye nasaha.
80. Na Lut (Lot) alipowaambia watu wake: Je, mnafanya
uchafu ambao hajawatangulia yeyote kwa uchafu huo katika
walimwengu? 81. Hakika nyinyi mnawaendea wanaume kwa
matamanio badala ya wanawake! Bali nyinyi ni watu wafujaji.
82. Na halikuwa jibu la watu wake isipokuwa kuambizana:
'Watoeni mjini mwenu, maana hao (eti) ni watu wasafi'.
83. Tukamwokoa yeye na jamaa zake, isipokuwa mkewe
alikuwa miongoni mwa waliobakia. 84. Na tukawamiminia
mvua, basi tazama jinsi ulivyokuwa mwisho wa waovu.
85. Na kwa wa Madyan (tulimpeleka) ndugu yao Shuaib
akasema: Enyi watu wangu! Mwabuduni Mwenyezi Mungu,
nyinyi hamna Mungu mwingine zaidi Yake. Hakika umewajia
ushahidi ulio wazi kutoka kwa Mola Wenu. Basi kamilisheni
kipimo na mizani wala msiwapunje watu vitu vyao, wala
msifanye uharibifu katika ardhi baada ya kutengenea kwake.
Hayo ndiyo bora kwenu ikiwa nyinyi mmeamini. 86. Wala
msikae katika kila njia huku mkiwatisha watu na kuwazuia
njia ya Mwenyezi Mungu wale wenye kumwamini, na
mkataka njia ya Mungu iende kombo. Na kumbukeni
mlipokuwa wachache Akawafanya wengi, na tazameni
jinsi ulivyokuwa mwisho wa watenda maovu. 87. Na kama
liko kundi miongoni mwenu lililoamini yale niliyotumwa
kwayo, na kundi (jingine) halikuamini, basi subirini mpaka
Mwenyezi Mungu ahukumu baina yetu; Naye ndiye mbora
wa wenye kuhukumu.
88. Machifu waliojaa kiburi katika kaumu yake wakasema:

Ewe Shuaib! Tutakutoa wewe na wale walioamini pamoja nawe katika mji wetu , au mrejee katika utamaduni wetu. Akasema: Je, hata kama tunauchukia? 89. Hakika tutakuwa tumemzulia Mwenyezi Mungu uongo, ikiwa tutarudi katika mila yenu baada ya kutuokoa nayo Mwenyezi Mungu. Wala haiwi kwetu kuirudia mpaka akipenda Mwenyezi Mola Wetu Mlezi. Ujuzi wa Mola Wetu umeenea katika kila kitu. Kwa Mwenyezi Mungu tunategemea. Ewe Mola Wetu Mlezi! Hukumu baina yetu na baina ya kaumu yetu kwa haki, Nawe ndiwe bora ya wenye kuhukumu. 90. Na wakuu waliokufuru katika kaumu yake wakasema: Kama nyinyi mkimfuata Shuaib, hapo hakika mtakuwa wenye hasara. 91. Wakapigwa na tetemeko la ardhi, wakaamkia majumbani mwao wakiwa wamelala chini kwa kubong'oka. 92. Wale waliomkadhibisha Shuaib wakawa kana kwamba hawakuwako. Wale waliomkadhibisha Shuaib ndiyo waliokuwa wenye hasara. 93. Basi (Shuaib) akaachana nao na akasema: Enyi watu wangu! Kwa hakika nimewafikishia ujumbe wa Mola Wangu Mlezi na nikawanasihi, basi vipi nihuzunike juu ya watu makafiri.

94. Na hatukumtuma Nabii yeyote kwenye mji, isipokuwa (kwanza) tunawapa watu wa mji huo shida na dhiki ili wapate kunyenyekea. 95. Kisha hubadilisha mahali pa shida kuwa ustawi, hadi idadi yao ikaongezeka na waseme: 'Shida na raha hizo ziliwafika baba zetu (zamani)'. Ghafla tukawawajibisha kwa makosa wakiwa hawatambui. 96. Na laiti watu wa mijini wangeliamini na kumcha Mungu, kwa hakika tungewafungulia baraka kutoka mbinguni na ardhini. Lakini walikadhibisha, kwa hiyo tukawawajibisha kwa sababu ya yale waliyokuwa wakiyachuma. 97. Je, watu

wa miji wameaminisha ya kuwa adhabu Yetu haitawafikia
usiku, hali wamelala? 98. Au watu wa miji wameaminisha
kuwa adhabu Yetu haitawafikia mchana, hali wanacheza?
99. Je, wamejiaminisha na vituko vya Mwenyezi Mungu?
Hawaaminishi vituko vya Mwenyezi Mungu ila watu ambao
hatima yao ni kuharibikiwa.

100. Je, hawazingatii hawa ambao wanarithi ardhi baada
ya watu wake (kuangamizwa) kuwa kama tukipenda na wao
tutawaadhibu kwa dhambi zao, na tukapiga muhuri juu ya
nyoyo zao wakawa hawasikii? 101. Miji hiyo tunayokusimulia
baadhi ya habari zake, waliwajia Mitume wao na Ishara zilizo
waziwazi, lakini wasingeamini yale waliyokwisha yakataa
huko nyuma. Namna hii ndivyo Mwenyezi Mungu anazipiga
muhuri nyoyo za makafiri. 102. Na hatukuona kwa wengi wao
kutimiza ahadi yoyote. Na hakika tuliwakuta wengi wao ni
wapenda uasi.

103. Kisha baada yao tukamtuma Musa na Ishara Zetu kwa
Firauni na wakuu wake, lakini wakazikanusha. Basi tazama
jinsi ulivyokuwa mwisho wa waharibifu. 104. Akasema Musa:
Ewe Firauni! Hakika mimi ni Mtume nitokaye kwa Mola
wa walimwengu. 105. Yanipasa nisiseme juu ya Mwenyezi
Mungu ukweli tu; nimewajia na dalili wazi itokayo kwa
Mola Wenu. Hebu waache wana wa Israel waende nami.
106. Firauni akasema:' Ikiwa umekuja na Ishara, basi ilete
ukiwa ni miongoni mwa wasemao kweli'. 107. Basi akaitupa
chini fimbo yake, lo! Ghafla ikawa joka lionekanalo wazi
wazi. 108. Na akautoa mkono wake, mara ukatoa mwanga
kwa watazamao. 109. Wakuu wa watu wa Firauni wakasema:
Hakika huyu ni mchawi stadi. 110. Anataka kuwatoa katika
ardhi yenu. Basi mnatoa shauri gani? 111. Wakasema: Mwache

hapa kidogo yeye na ndugu yake, na uwatume wakusanyao watu mijini. [112.] Wakuletee kila mchawi, mjuzi.

[113.] Wakaja wachawi wa Firauni, wakasema: Bila shaka tutalipwa ikiwa tutashinda! [114.] Firauni akasema: Ndio. Nanyi hakika mtakuwa miongoni mwa walio karibu nami. [115.] Wachawi wakasema: ‘Ewe Musa, utatupa wewe au tutupe sisi (kwanza)? [116.] Akasema: Tupeni (kwanza)! Walipotupa, waliyazuga macho ya watu na wakawaogopesha. Wakawa wameleta uchawi mkubwa..[117.] Tukampelekea wahyi Musa kwamba tupa fimbo yako chini! Mara ikavimeza walivyovibuni. [118.] Ukweli ukasimama na yakabatilika waliyokuwa wakiyatenda. [119.] Hapo wakashindwa, wakageuka wakawa wanyonge. [120.] Wachawi wale wakapomoka huku wakisujudi. [121.] Wakasema: Tumemwamini Mola Mlezi wa viumbe wote. [122.] Mola wa Musa (Moses) na Harun (Aaron).

[123.] Firauni akasema: Ebo! Mmemwamini kabla sijawapa ruhusa? Hizi ni njama tu mlizozipanga hapa mjini ili muwatoe wenye mji. Lakini punde hivi mtanitambua! [124.] Kwa kweli nitawakata mikono yenu na miguu yenu kwa kupishana: wa kuume kwa wa kushoto, kisha nitawatundika juu nyote! [125.] Wachawi wakasema: ‘Sisi ni wenye kurejea kwa Mola Wetu’. [126.] Na wewe hutulipizii kisasi ila kwa sababu tumeamini ishara za Mola Wetu zilipotujia. Ewe Mola wetu Mlezi! Tumiminie subira na ututoe roho hali ya kuwa sisi ni Waislamu.

[127.] Hapo machifu wa watu wa Firauni wakasema: ‘Kweli, utamwacha Musa na watu wake walete uharibifu nchini na wakuache wewe na miungu yako?’ Firauni akasema: ‘Tutawauwa watoto wao wa kiume na tutawaacha hai wanawake wao. Na hakika Sisi ni Wenye nguvu juu yao’.

128. Musa akawaambia watu wake: 'Ombeni msaada kwa Mwenyezi Mungu na subirini. Ardhi ni ya Mwenyezi Mungu atamrithisha amtakaye katika waja Wake na mwisho mwema ni wa wenye kumcha Mungu'. 129. Wakasema: 'Tumeudhiwa kabla hujatujia na baada ya kutujia'. Musa akawajibu: 'Pengine Mola Wenu Mlezi atamwangamiza adui yenu na kuwafanya nyie warithi katika ardhi, aone jinsi mtakavyofanya.'

130. Na hakika tuliwaadhibu watu wa Firauni kwa miaka ya (ukame) na kwa kupungukiwa na mazao, ili wapate kukumbuka. 131 Ulipowajia (msimu) mzuri, husema, "sisi ndiyo tuliohusika na hii' Ama ulipowajia (msimu) mbaya walimtwisha mkosi huo Musa na walio pamoja naye. Ehee! Hakika mkosi huo ni wao wenyewe, mbele ya Mwenyezi Mungu, lakini wengi wao hawajui. 132. Na wakasema: Hata ukituletea ishara yoyote kuturoga hatutakuamini.

133. Basi tukawapelekea tufani na nzige na chawa na vyura na damu, kuwa ni ishara mbalimbali, lakini wakatakabari na wakawa watu wakosefu. 134. Kila mara adhabu inapowafikia walisema: 'Tafadhali Musa (Moses)! Tuombee kwa Mola Wako Mlezi kama alivyokuahidi, ukituondolea adhabu hii bila shaka tutakuamini na hakika tutawaacha wana wa Israil waende nawe. 135. Lakini tulipowaondolea adhabu mpaka muda maalum ambao walipaswa kuutimiza, walivunja ahadi yao.

136 Mwishowe tuliwalipizia kisasi na tukawazamisha baharini kwa sababu walizikadhibisha Ishara Zetu na wakaghafilika nazo 137. Tukawarithisha ardhi watu waliokuwaa wakifanywa wanyonge mashariki na magharibi ya nchi hiyo tuliyoibariki. Na ahadi njema ya Mola Wako

Mlezi (ikawa) imetimia kwa wana wa Israeli, kwa sababu walikuwa na subira; na tukayabomolea mbali yale (majumba na miundo-mbinu) aliyoijenga Firauni na kaumu yake na yale waliyokuwa wakiyasimamisha kwa fahari kuu.

138. Na tukawavusha bahari wana wa Israil, wakafika kwa watu waliokuwa wakiabudu masanamu yao. Wakasema: Ewe Musa! Hebu nasi tutengenezee mungu kama hawa walivyo na miungu. Musa akasema: ‘Hakika ninyi ni watu wajinga kabisa!’. 139. Hakika waliyonayo hawa yatawaangamiza, na ni bure waliyokuwa wakiyafanya. 140. Akasema: Je, niwatafutie mungu badala ya Mwenyezi Mungu, hali Yeye amewapa fadhila nyingi zaidi kuliko walimwengu wote? 141. Na pindi tulipowaokoa kutoka kwa watu wa Firaun waliowapa adhabu za kikatili kabisa; wakiwaua watoto wenu wa kiume na kuwaacha hai wanawake wenu. Na katika hayo ulikuwa mtihani mkubwa uliotokea kwa Mola Wenu.

142 Na tulimwahidi Musa nyusiku thelathini na tukaziongezea kwa nyingine kumi; ndipo ikatimia miadi ya Mola Wake Mlezi ya nyusiku arobaini (za communion). Na Musa (Moses) akamwambia nduguye Harun (Aaron,kabla ya kwenda mlimani): ‘Shika mahali pangu katika watu wangu na urekebishe, usiusifuate njia ya wanaotaka kuharibu’. 143 Na alipofika Musa kwenye miadi yetu na Mola Wake Mlezi akamsemesha, alisema: ‘Mola Wangu Mlezi! ‘Nioneshe nikutazame’. Akasema: ‘Hutaniona, lakini tazama huu mlima. Kama ukitulia mahali pake ndipo utaniona’. Basi Mola Wake Mlezi alipojionyesha kwenye mlima, aliufanya upasuke, na Musa akaanguka chini amezimia. Alipozinduka akasema: ‘Kutakasika ni Kwako! Natubia Kwako na mimi ni wa mwanzo wa wanaoamini’.

144. Akasema: 'Ewe Musa! Mimi nimekuteua uende kwa watu na ujumbe Wangu na maneno yangu (niliyozungumza nawe). Chukua niliyokupa na uwe miongoni mwa wanaoshukuru'. 145. Na tukamwandikia katika mbao kila kitu, mawaidha na ufafanuzi wa kila jambo. (Tukamwambia) 'Yashike kwa uthabiti, na waamrishe watu wako wayashike kwa namna nzuri zaidi. Punde nitawaonesha makao ya wapotofu. 146. Nitawatenga na Ishara Zangu wale wanaofanya kiburi katika ardhi pasipo haki, na wakiona kila Ishara hawaiamini; na wakiona njia ya uongofu hawaishiki kuwa ndiyo njia; lakini wakiona njia ya upotofu wanaishika kuwa ndiyo njia. Hayo ni kwa sababu wao wamezikadhibisha Ishara Zetu na wameghafilika nazo. 147. Na wale waliozikadhibisha ishara Zetu na mkutano wa Akhera, amali zao zimeporomoka; kwani watalipwa isipokuwa yale waliyokuwa wakiyatenda?

148. Na baada ya kuondoka kwake, watu wa Musa (Moses), kutokana na mapambo yao walimtengeneza (kinyago cha) ndama mwenye kiwiliwili kilichotoa mlio. Je, hawakuona kwamba huyo hasemi nao wala hawaongozi njia? Walimfanya na wakawa wenye kudhulumu. 149. Walipojuta na wakaona kwamba wamekwishapotea walisema: 'Kama Mola Wetu Mlezi hatatuonea huruma na kutusamehe, bila shaka tutakuwa miongoni mwa waliopata hasara. 150. Aliporudi Musa kwa watu wake naye ameghadhibika na kuhuzunika. Akasema: 'Ni uovu ulioje mlionifanyia nyuma yangu! Hivi mmeharakisha iwajie hukumu ya Mola wenu Mlezi? Na akazibwaga chini zile mbao na akamkamata (nywele za) kichwa ndugu yake akamvuta kwake. Harun akamwambia: 'Ewe mtoto wa mama yangu! Watu hawa wamenidharau na wakakaribia kuniua. Usiwafanye maadui wafurahie matatizo

yangu, na wala usinichanganye mimi na watu hawa waasi'.
151. Musa akaomba: 'Mola Wangu Mlezi! Nisamehe mimi na
ndugu yangu na utuingize katika huruma Yako na Wewe ni
Mwenye kuhurumia kushinda wote wenye kuhurumia'.

152. Hakika wale walioabudu ndama, itawapata ghadhabu
kutoka kwa Mola Wao na madhila katika maisha ya
duniani. Na hivyo ndivyo tunavyowalipa wazushi. 153. Na
wale waliotenda maovu, kisha wakatubia baada yake na
wakaamini, hakika Mola Wako baada ya hayo ni Mwingi wa
maghufira Mwenye kurehemu.

154. Na ilipomtulia Musa ile ghadhabu, aliziokota zile
mbao; na katika maandiko yake mna uongozi na rehema kwa
wanaomwogopa Mola Wao. 155. Na Musa akachagua watu
sabini katika watu wake kwa miadi Yetu. Walipokumbwa
na tetemeko akasema: 'Mola Wangu Mlezi! Lau ungetaka
ungeliwaangamiza wao na mimi tangu zamani. Unatuangamiza
kwa sababu ya yale waliyoyafanya wapumbavu katika sisi?
Haya si chochote bali mtihani utokao kwako; ili umwache
apotee umtakaye kwa sababu yake na umwongoze umtakaye.
Wewe ndiye kiongozi wetu. Basi tughufurie na uturehemu.
Nawe Ndiye bora wa kughufiria. 156. Na utuandikie mema
katika dunia hii na akhera. Sisi tunarejea Kwako. (Mwenyezi
Mungu) akasema: Adhabu Yangu nitamsibu nayo nimtakaye;
na rehema Yangu imeenea kila kitu, lakini nitaiwajibisha
hasa kwa wale wanaomcha Mungu, na wanaotoa Zaka na
wanaoziamini Aya Zetu, 157. Ambao wanamfuata Nabii asiye
Myahudi, ambaye wanamkuta ameandikwa kwao katika Torat
na Injili. Anayewaamrisha mema na kuwakataza maovu.
Na anawahalalishia vizuri na kuwaharamishia vibaya, na
kuwaondolea mizigo yao na minyororo iliyokuwa juu yao.

Basi wale waliomwamini na wakamheshimu na wakamsaidia
na wakafuata nuru iliyoteremshwa pamoja naye, hao ndio
wenye kufaulu.
158. Sema: Enyi watu! Hakika mimi ni Mtume wa
Mwenyezi Mungu kwenu nyinyi nyote. (Mungu) ambaye
ni Wake ufalme wa mbingu na ardhi, hapana Mola ila
Yeye, Ndiye ahuyishaye na ndiye afishaye, basi mwaminini
Mwenyezi Mungu na Mtume Wake asiye Myahudi, ambaye
humwamini Mwenyezi Mungu na maneno Yake. Na mfuateni
ili mpate kuongoka. 159. Na katika watu wa Musa lipo kundi
linalowaongoza watu kwa ukweli, na wanafanya uadilifu
kutokana na ukweli.
160. Na tukawagawa katika koo kumi na mbili (za)
makabila mbali mbali. Na tukampa ufunuo Musa (Moses)
pale walipomuomba maji watu wake, kuwa lipige jiwe
kwa fimbo yako. Mara zikabubujika chemichemi kumi na
mbili, na kila watu wakajua mahali pao pa kunywea. Na
tukawafunika kivuli kwa mawingu na tukawateremshia Mana
(mkate utiao nguvu) na ndege wa aina ya Kwale. Kuleni
katika vizuri tulivyowaruzuku. Wala hawakutudhulumu,
bali wamejidhulumu wenyewe. 161. Na walipoambiwa kaeni
katika mji huu na kuleni humo maridhawa popote mpendapo
na ingieni katika mlango (wake) kwa kunyenyekea na
semeni: 'Tusamehe'. Tutawasamehe makosa yenu na
tutawazidishia wale wafanyao mazuri. 162. Lakini wapenda
uasi wakabadilisha kauli isiyokuwa ile waliyoambiwa. Na
ndipo tukateremsha juu ya hao waasi adhabu kubwa kutoka
mbinguni kwa vile walivyokuwa wakiasi.
163. Na waulize habari za mji uliokuwa kando ya bahari
walipokuwa wakivunja (amri ya kupumzika) Sabato. Siku

yao ya mapumziko, Samaki wao walikuwa wakiwajia wazi wazi wakinyanyua vichwa juu ya maji. Lakini siku isiyo ya mapumziko hawakuwajia. Kama hivyo tulitaka tuwajaribu kwa sababu walikuwa watu wapendao uasi. 164. Na pale kikundi katika wao waliposema: ‘Kwa nini mnawaonya watu ambao tangu hapo Mwenyezi Mungu atawaangamiza au atawaadhibu adhabu kali?’(Wahubiri) Wakajibu: Ili kutimiza wajibu wetu mbele ya Mola Wenu Mlezi, na (pia) huenda wakamtii na kumuenzi.

165. Basi walipoyasahau waliyokumbushwa tuliwaokoa waliokuwa wakikataza maovu, na tukawawajibisha walio dhulumu kwa adhabu kali, kwa sababu walikuwa wakipenda uasi. 166. Walipoasi waliyokatazwa kwa ukaidi wao tuliwaambia ‘kuweni manyani wa kudharauliwa’.

167. Na alipotangaza Mola Wako (kwamba) hakika atawaleta watu ambao watawaadhibu kwa adhabu mbaya mpaka siku ya Kiyama. Hakika Mola Wako ni mwepesi wa kuadhibu na hakika Yeye ni Mwingi wa maghufira, Mwenye kurehemu. 168. Na tukawatenga katika ardhi makundi makundi; miongoni mwao wako walio wema na wengine kinyume cha hivyo. Na tukawajaribu kwa mema na mabaya, ili wapate kurejea.

169. Na kikafuatia baada yao kizazi (kibaya) kilichorithi Kitabu. Wakachagua anasa za maisha haya ya dunia wakisema, ‘Tutasamehewa kila kitu!’ Na ikiwajia tena anasa kama hiyo, wataichukua pia. Je, hawakuchukua ahadi katika Kitabu kuwa hawatasema juu ya Mwenyezi Mungu ila kweli tupu, na si wanasoma yaliyomo humo?! Basi nyumba ya Akhera ni bora kwa wale wenye kumcha Mungu. Hivi kweli hamfahamu?! 170. Na wale wanaoshikamana na

Kitabu na wakasimamisha Swala, hakika Sisi hatupotezi
ujira wa wanaorekebisha’. 171. Na tulipouinua mlima ukawa
juu yao mithili ya kiwingu kilichowafunika na wakadhani
utawaangukia. Tukawaambia: Shikeni kwa imara yale
tuliyowapa na yakumbukeni yaliyomo ndani yake ili mpate
kumcha Mungu.

172. Na kumbuka (Muhammad) pale Mola Wako Mlezi
alipokitoa kizazi cha Adam kutoka katika migongo ya baba
zao na akaja kuzishuhudisha roho zao ; ‘Hivi Mimi si Mola
Wenu Mlezi?’ Wakasema: ‘Kulikoni! Tunashuhudia’. “Msije
mkasema siku ya Kiyama kuwa sisi tulikuwa tumeghafilika
na haya”. 173. “Au mkasema, baba zetu ndio walioshirikisha
kabla yetu, nasi tulikuwa kizazi chao baada yao. Sasa,
utatuangamiza kwa waliyofanya wapotofu?” 174. Na kama
hivyo tunazipambanua Ishara, kwa kutaraji kuwa watarejea.

175. Na wasomee habari za yule tuliyempa Aya Zetu, naye
akajivua nazo. Na shetani akamwandama akawa miongoni
mwa waliopotea. 176. Na kama tungelitaka tungelimuinua
kwazo, lakini yeye akashikilia ulimwengu na kufuata
mapenzi yake. Mfano wake ni kama wa mbwa, ukimhujumu
hutweta na ukimwacha pia hutweta. Huo ni mfano wa watu
waliozikadhibisha Aya Zetu. Basi simulia visa, huenda
wakatafakari. 177. Huu ni mfano mwovu kabisa wa watu
wanaokadhibisha Aya Zetu na wakajidhulumu nafsi zao.
178. Amwongozaye Mwenyezi Mungu huyo ndiye aongokaye,
na ampotezaye basi hao ndio watakaopata hasara.

179. Hakika tumeiumba Jahannam kwa ajili ya majini
wengi na watu. Wana nyonyo, lakini hawafahamu kwazo,
na wana macho, lakini hawaoni kwayo, na wana masikio,
lakini hawasikii kwayo. Hao ni kama wanyama bali wao ni

wapotevu Zaidi. Hao ndio walioghafilika. 180. Na Mwenyezi Mungu ana majina mazuri, basi mwombeni kwayo. Na achaneni na wale wanaoingiza ulahidi katika majina Yake, watalipwa waliyokuwa wakiyatenda. 181. Na miongoni mwa tuliowaumba wako watu wanaoongoza (wengine) kwa ukweli na kwa misingi yake wanatenda haki. 182. Na wale waliokadhibisha Aya Zetu, tutawavuta kidogo kidogo kwa namna wasiyoijua. 183. Nami nitawapa muda, hakika mpango Wangu ni madhubuti.

184. Je, hawafikiri? Huyu mwenzao hana wazimu! Yeye si kitu kingine isipokuwa ni mwonyaji aliye wazi. 185. Hivi hawatazami ufalme wa mbingu na ardhi na alivyoviumba Mwenyezi Mungu, na kuwa pengine ajali yao imekwisha karibia? Basi ni mazungumzo gani baada ya haya watakayoyaamini? 186. Ambaye Mwenyezi Mungu amemwacha apotee hana wa kumwongoza; na atawaacha katika upotofu wao wakihangaika. 187. Wanauliza hiyo saa (ya mwisho, Kiyama) itatokea lini? Sema: Ujuzi wake uko kwa Mola Wangu Mlezi. Hakuna wa kuifichua kwa wakati wake isipokuwa Yeye tu. Ni jambo zito mbinguni na ardhini. Hakitawajia isipokuwa kwa ghafla tu. Wanakuuliza kana kwamba wewe una pupa nacho! Sema: Ujuzi wake uko kwa Mwenyezi Mungu tu, lakini watu wengi hawalijui hili. 188. Sema: Miye sijimilikii mwenyewe manufaa wala madhara ila apendavyo Mwenyezi Mungu. Na lau kama ningelijua ghaibu ningelijizidishia mema mengi wala ovu lisingenigusa. Mimi si chochote ila ni mwonyaji na mtoaji bishara njema kwa watu wanaoamini.

189. Yeye ndiye aliyewaumba kutokana na nafsi moja, na katika hiyo hiyo akamwumba mkewe ili apate kukaa naye kwa

utulivu. Anapomjamii hubeba mzigo mwepesi, anatembea nao. Anapokuwa mja mzito, wote wawili wanamwomba Mola Wao Mlezi, kama ukitupa mwana mwema tutakuwa miongoni mwa wanaoshukuru. 190. Lakini alipowapa mwana mwema walimfanyia washirika katika kile kile alichowapa. Mwenyezi Mungu ametukuka na hao wanaowashirikisha. 191 Hivi! Wanawafanya washirika wa Mwenyezi Mungu wale ambao hawaumbi kitu, bali wao wanaoumbwa? 192. Wala hawawezi kuwasaidia wala kujisaidia wenyewe. 193. Na kama mkiwaita kwenye uwongofu hawatawafuata; ni sawa ikiwa mtawaita au mtanyamaza. 194 Hakika hao mnaowaabudu badala ya Mwenyezi Mungu ni waja mfano wenu. Hebu waombeni nao wawaitikie ikiwa nyinyi mnasema kweli.

195. Je, wao wanayo miguu ya kutembelea? Au wanayo mikono ya kushikia? Au wanayo macho ya kuonea? Au wanayo masikio ya kusikizia? Sema: Waiteni hao mnaowashirikisha kisha pamoja nifanyieni njama zenu, wala msinipe muda. 196. Hakika Mlinzi wangu ni Mwenyezi Mungu aliyeteremsha Kitabu Naye ndiye awalindaye wafanyao mema. 197. Na wale mnaowaabudu badala Yake hawawezi kuwasaidia wala kujisaidia wenyewe. 198. Na kama mkiwaita kwenye uongofu hawatasikia. Na unawaona wanakutizama, nao hawaoni.

199. Shikamana na kusamehe na amrisha mema na achana na wajinga. 200. Na kama wasi wasi wa shtani utakusumbua, jikinge kwa Mwenyezi Mungu; hakika Yeye ndiye asikiaye na ajuaye. 201. Hakika wale wamchao Mungu zinapowagusa pepesi za Shetani huzinduka, mara wanaona njia. 202. Lakini ndugu zao (Shetani) wanawavuta ndani kabisa katika upotofu na kamwe hawalegezi tena (juhudi zao).

203. Na usipowaletea Aya (waitakayo), husema: Kwa nini

hukuibuni? Sema: Hakika nafuata yale tu yanayofunuliwa kwangu na Mola Wangu Mlezi. Hii (Quran) ni busara zitokazo kwa Mola Wenu Mlezi na ni uwongofu na rehema kwa watu wanaoamini. [204.] Na isomwapo Qur'an isikilizeni na mnyamae ili mpate kuonewa huruma. [205.] Na mtaje Mola Wako nafsini mwako kwa unyenyekevu na heshima na bila ya kupiga kelele, asubuhi na jioni. Wala usiwe miongoni mwa walioghafilika. [206.] Hakika wale waliopo kwa Mola Wako hawajivuni wakaacha kumwabudu na wanamtakasa na wanamsujudia.

## 8. Sura Al-Anfal

# SURA YA NYARA ZA VITA

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

[1] Wanakuuliza juu ya nyara. Sema nyara ni za Mwenyezi
Mungu na Mtume. Basi mcheni Mwenyezi Mungu na
msuluhishe mambo baina yenu, na mtiini Mwenyezi Mungu
na Mtume Wake ikiwa nyinyi ni waumini. [2] Hakika waumini
ni wale ambao atajwapo Mwenyezi Mungu nyoyo zao hujaa
hofu, na wanaposomewa Aya Zake huwazidisha imani, na
wanamtegemea Mola Wao. [3] Ambao wanasimamisha Swala
na wanatoa katika vile tulivyowaruzuku. [4] Hao kweli ndio
waumini; wao wana vyeo kwa Mola Wao, na maghufira na
riziki bora.

[5] Kama vile alivyokuamuru Mola Wako kutoka nyumbani
kwako kwa ukweli, ingawaje kundi moja la waumini
linachukia hilo. [6] Wanajadiliana nawe kwa jambo hilo la

haki baada ya kuwa dhahiri. Kana kwamba wanasukumwa
katika mauti na huku wanaona. 7 Na pale alipowaahidi moja
ya makundi mawili kuwa ni lenu; nanyi mkapenda lile lisilo
na silaha ndio liwe lenu. Lakini Mwenyezi Mungu anataka
kuihakikisha haki kwa maneno Yake na kuikata mizizi ya
makafiri. 8 Ili kuihakikisha haki na kuivunja batili; ijapokuwa
watachukia wafanyao makosa.

9. Mlipokuwa mkimwomba msaada Mola Wenu, naye
akawajibu kuwa: kwa yakini Mimi nitawasaidia kwa Malaika
elfu moja wanaofuatana mfululizo. 10. Na Mwenyezi Mungu
hakuyafanya haya ila kuwa bishara njema, na ili nyoyo zenu
zitue kwayo. Na hakuna msaada ila utokao kwa Mwenyezi
Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu,
Mwenye hekima. 11. Kumbuka alipowafunikeni kwa usingizi
kuwapa utulivu utokao kwake, na akawateremshia maji kutoka
mawinguni ili awasafishe kwayo na kuwaondolea uchafu wa
shetani na kuzikazanisha nyoyo zenu na kuitia nguvu miguu
yenu. 12. Kumbuka pale Mola Wako alipowafunulia Malaika
(ujumbe huu): ‘Hakika Mimi niko pamoja nanyi, basi
watieni nguvu wale walioamini; nitatia woga katika nyoyo za
makafiri, basi wakateni juu ya shingo na wakateni ncha zote
za vidole vyao. 13. Hayo ni kwa kuwa wamemwasi Mwenyezi
Mungu na Mtume Wake. Na mwenye kumwasi Mwenyezi
Mungu na Mtume Wake, basi hakika Mwenyezi Mungu ni
mkali wa kuadhibu. 14. Ndiyo hivyo! Basi onjeni! Na hakika
makafiri wana adhabu ya moto.

15. Enyi walioamini! Mnapokutana vitani na wale
waliokufuru, basi msiwageuzie migongo. 16. Na
atakayewageuzia mgongo wake siku hiyo, isipokuwa kwa
mbinu za vita au kuungana na kikosi, hakika amestahiki

ghadhabu ya Mwenyezi Mungu; na makazi yake ni Jahannam, napo ni mwishilio muovu.

17. Hamkuwaua nyinyi, lakini Mwenyezi Mungu ndiye aliyewaua, na hukutupa wewe ulipotupa, lakini Mwenyezi Mungu ndiye aliyetupa. Na ili awajaribu waumini majaribu mazuri. Hakika Mweyezi Mungu ni Msikizi, Mjuzi. 18. Ndiyo hivyo! Na hakika Mwenyezi Mungu ndiye adhoofishaye vitimbi vya makafiri. 19. Kama mnataka ushindi, basi ushindi umekwishawajia, na kama mkiacha (kutenda mabaya) basi itakuwa kheri kwenu; na kama mtarudia (kushambulia) Sisi pia tutarudia (kuwanusuru); na jeshi lenu (pekee) halitawafaa chochote, hata likiwa kubwa. Na kwa hakika Mwenyezi Mungu yuko pamoja na waumini.

20. Enyi walioamini! Mtiini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, wala msijiepushe naye hali mnasikia (maneno yake) 21. Wala msiwe kama wale wanaosema: 'Tumesikia! Na kumbe hawasikii'. 22. Hakika wanyama waovu mbele ya Mwenyezi Mungu ni viziwi, mabubu ambao hawatumii akili zao. 23. Na kama Mwenyezi Mungu angelijua wema wowote kwao, angeliwasikilizisha; na kama angeliwasikilizisha, wangeligeuka wakapuuza.

24. Enyi walioamini! Mwitikieni Mwenyezi Mungu na Mtume anapowaita kwenye lile litakalowapa uhai. Na jueni kuwa Mwenyezi Mungu huingia kati ya mtu na moyo wake, na kwamba mtakusanywa Kwake. 25. Na ogopeni balaa ambalo halitawafikia waovu miongoni mwenu pekee. Na jueni kuwa Mwenyezi Mungu ni mkali wa kuadhibu.

26. Na kumbukeni mlipokuwa wachache, mkionekana wadhaifu katika nchi; mkawa mnaogopa watu wasiwanyakue; akawapa makao na akawatia nguvu kwa nusura Yake

na akawapa riziki njema ili mpate kushukuru. 27. Enyi
walioamini! Msimfanyie hiyana Mwenyezi Mungu na
Mtume na mkahini amana zenu na hali mnajua. 28. Na jueni
kwamba mali zenu na watoto wenu ni mtihani (mliopewa).
Na hakika kwa Mwenyezi Mungu yapo malipo makubwa.
29. Enyi walioamini! Mkimcha Mwenyezi Mungu
atawapeni upambanuzi, na atawafutia makosa yenu na
atawasamehe; na Mwenyezi Mungu ni Mwenye fadhila
kuu. 30. Na pale walipokupangia njama wale waliokufuru
ili wakufunge au wakuue au wakutoe mjini. Na wakapanga
hila zao na Mwenyezi Mungu naye akapanga. Na Mwenyezi
Mungu ndiye mbora wa mipango.
31. Na wanaposomewa Aya Zetu, husema:
'Tumekwishasikia. Kama tungependa tungelisema kama
haya; haya si chochote ila ni ngano tu za watu wa kale.
32. Na pale waliposema: 'Ewe Mwenyezi Mungu! Ikiwa hii ni
kweli itokayo kwako, basi tunyeshee mawe kutoka mbinguni
au tuletee adhabu yeyote iumizayo. 33. Na Mwenyezi Mungu
hakuwa ni Mwenye kuwaadhibu maadamu wewe umo
pamoja nao, wala hakuwa Mwenyezi Mungu ni Mwenye
kuwaadhibu hali wanaomba msamaha. 34. Hivi wana jambo
gani hata Mwenyezi Mungu asiwaadhibu, ilhali wanazuilia
watu na Msikiti Mtakatifu na wao si walinzi wake? Bali
walinzi wake si wengine ila wacha Mungu pekee, lakini
wengi wao hawajui. 35. Na haikuwa ibada yao kwenye hiyo
Nyumba isipokuwa kupiga mbinja na makofi tu! Basi onjeni
adhabu kwa sababu ya yale mliyokuwa mkikufuru.
36. Hakika wale waliokufuru hutoa mali zao ili kuzuilia njia
ya Mwenyezi Mungu. Basi watazitoa, kisha zitakuwa majuto
juu yao, na watashindwa hivyo hivyo. Na wale waliokufuru

watakusanywa kwenye Jahanamu. [37.] Ili Mwenyezi Mungu apate kuwapambanua walio wabaya na walio wazuri na kuwaweka wabaya juu ya wabaya wengine na kuwarundika wote pamoja na kuwatupa katika Jahanamu. Hao ndio waliohasirika.

[38.] Waambie wale waliokufuru, kama watakoma, watasamehewa yaliyopita; na wakirudia basi imekwishapita desturi ya watu wa zamani. [39.] Na piganeni nao mpaka kusiwe na fitna na dini yote iwe kwa ajili ya Mwenyezi Mungu; wakikoma, basi hakika Mwenyezi Mungu anayaona wanayotenda. [40.] Na wakigeuka, basi jueni kuwa Mwenyezi Mungu ndiye Mola Wenu, ni Mola mwema na msaidizi mwema.

[41.] Na jueni kwamba chochote mkipatacho kama nyara, basi sehemu ya tano yake (khums) ni ya Mwenyezi Mungu na Mtume na jamaa na mayatima na masikini na msafiri, ikiwa nyinyi kweli mmemwamini Mwenyezi Mungu na yale tuliyoteremsha kwa mja wetu siku ya upambanuzi, siku yalipokutana majeshi mawili. Na Mwenyezi Mungu ni Muweza juu ya kila kitu.

[42.] Kumbuka mlipokuwa kwenye ng'ambo ya karibu ya bonde, na wao wakawa g'ambo ya mbali; na msafara (magari ya farasi wa vita) upo chini yenu; kiasi kwamba hata mngeliagana (kukutana) mngelihitalifiana katika miadi. Lakini (mkakutana) ili Mwenyezi Mungu alitimize jambo lililokuwa lifanyike; aangamie (aliyepangiwa) kuangamia huku akiwa amepata hoja iliyo dhahiri, na awe hai (aliyepangiwa) kuwa hai kwa hoja dhahiri. Na hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia mwenye kujua. [43.] Kumbuka pale alipokuonesha katika usingizi wako kuwa

wao ni wachache. Na lau angelikuonesha kuwa wao ni wengi mngelivunjika moyo na mngelizozana katika jambo hilo, lakini Mwenyezi Mungu kakuvueni. Hakika Yeye ni Mjuzi wa yaliyo vifuani. 44. Na mlipokutana akawaonesha machoni mwenu kuwa ni wachache, na akawafanya nyinyi kuwa wachache machoni mwao ili Mwenyezi Mungu alitimize jambo lililokuwa lifanyike. Na kwa Mwenyezi Mungu hurejeshwa mambo yote.

45. Enyi walioamini! Mnapokutana na jeshi, basi kueni imara, na mumkumbuke Mwenyezi Mungu sana ili mpate kufaulu. 46. Na mtiini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake wala msizozane, msije mkavunjika moyo na zikapotea nguvu zenu, na subirini; Hakika Mwenyezi Mungu yuko pamoja na wanaosubiri. 47. Wala msiwe kama wale waliotoka majumbani mwao kwa fahari na kujionyesha kwa watu, na kuzuilia njia ya Mwenyezi Mungu; na Mwenyezi Mungu ameyazunguka wanayoyafanya.

48. Na pale shetani alipowapambia vitendo vyao, na kusema: ‘Leo hakuna mtu wa kuwashinda nyie, wakati mimi nikiwa mlinzi wenu’. Lakini yalipokutana majeshi mawili, alirudi nyuma na kusema: ‘Mimi siko pamoja nanyi, mimi naona msiyoyaona, mimi namwogopa Mwenyezi Mungu!’ Na Mwenyezi Mungu ni mkali wa kuadhibu. 49. Na kumbuka pale wanafiki na wale wenye maradhi nyoyoni mwao waliposema: ‘Hawa dini yao imewadadanganya’. Na mwenye kumtegemea Mwenyezi Mungu, basi hakika Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye nguvu Mwenye hekima.

50. Na laiti ungeliwaona Malaika wanapowafisha wale waliokufuru wakipiga nyuso zao na migongo yao na (kuwaambia) hebu onjeni adhabu ya moto unaowaka.

[51.] Hayo ni kwa sababu ya yale yaliyokwishatangulizwa na mikono yenu. Na hakika Mwenyezi Mungu si mwenye kuwadhulumu waja. [52.] Ni kama ada ya watu wa Firaun na wale waliokuwa kabla yao; walizikana Ishara za Mwenyezi Mungu, kwa hiyo Mwenyezi Mungu akawaadhibu kwa sababu ya makosa yao. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mkali wa kuadhibu. [53.] Hiyo ni kwa sababu Mwenyezi Mungu habadilishi kabisa neema alizowaneemesha watu, mpaka wao wabadilishe yaliyomo nafsini mwao. Na hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia, Mwenye kujua. [54.] Ni kama hali ya watu wa Firaun na wale waliokuwa kabla yao; walizikadhibisha Ishara za Mola Wao, kwa hiyo tukawaangamiza kwa sababu ya dhambi zao, na tukawazamisha majini watu wa Firaun. Na wote walikuwa wakandamizaji, wakeukaji wa haki za bindamu.

[55.] Hakika wanyama waovu kabisa mbele ya Mwenyezi Mungu ni wale wanaokufuru, wao hawataamini. [56.] Hao ni wale ambao umefikiana nao mapatano kisha wanavunja ahadi yao kila mara; wala hawaogopi. [57.] Basi utakapokuwa na uluwa juu yao katika vita, watawanye na wale walio nyuma yao, ili wapate kufahamu. [58.] Na kama ukihofia uhaini kutoka kwa kundi lolote (la makafiri) basi yatupilie mbali mapatano yao, muwe sawa (katika kuyavunja). Hakika Mwenyezi Mungu hawapendi wahaini.

[59.] Wala wale waliokufuru wasifikirie kwamba wao wame (wa) tangulia (Waislamu); kwa hakika wao hawatashinda. [60.] Na waandalieni nguvu kadri muwezavyo na kwa farasi waliofungwa tayari-tayari, kwa kuwaingiza hofu adui wa Mwenyezi Mungu na adui yenu, na wengineo msiowajua nyinyi, Mwenyezi Mungu anawajua. Na chochote

mtakachotoa katika njia ya Mwenyezi Mungu, mtarudishiwa,
wala nyinyi hamtadhulumiwa. 61. Na kama wakipondokea
kwenye amani, nawe ipondokee, na mtegemee Mwenyezi
Mungu. Hakika Yeye ni Mwenye kusikia Mwenye kujua.
62. Na kama wakitaka kukuhadaa, basi Mwenyezi Mungu
atakutoshelezea. Yeye ndiye aliyekupa nguvu kwa msaada
Wake na kwa waumini. 63. Na akaziunganisha nyoyo zao;
hata kama ungelitoa yote yaliyomo ardhini usingeweza
kuziunganisha nyoyo yao, lakini Mwenyezi Mungu
amewaunganisha. Hakika Yeye ndiye Mwenye nguvu,
Mwenye hekima.

64. Ewe Mtume! Mwenyezi Mungu anakutosha, wewe
na waumini wanaokufuata. 65. Ewe Nabii! Wahimize
waumini waende vitani; wakiwepo miongoni mwenu ishirini
wenye subira, watashinda mia mbili; na kama wakiwa mia
moja miongoni mwenu, watawashinda elfu moja katika
waliokufuru; maana hao ni watu wasiofahamu. 66. Sasa
Mwenyezi Mungu amewahafifishia na anajua kuwa kuna
udhaifu miongoni mwenu. Kwa hiyo, wakiwa mia moja
miongoni mwenu wenye subira watawashinda mia mbili, na
kama wakiwa elfu moja miongoni mwenu watawashinda elfu
mbili kwa idhini ya Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu
yuko pamoja na wanaosubiri.

67. Haimfalii Nabii yoyote kuwa na mateka mpaka awe
ameshinda sawasawa katika ardhi. Mnataka vitu vya dunia,
na hali Mwenyezi Mungu anataka Akhera. Na Mwenyezi
Mungu ni Mwenye nguvu Mwenye hekima. 68. Lau si kuwa
hukumu kutoka kwa Mwenyezi Mungu ilikwishatangulia
(kuwa hawaadhibu watu kwa kutojua), bila shaka
ingeliwapata ninyi adhabu kubwa kwa hivyo mlivyovitwaa.

69. Basi kuleni katika vile mlivyoteka, ni halali na vizuri; na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa maghufira Mwenye kurehemu.

70. Ewe Nabii! Waambie wale mateka waliomo mikononi mwenu: Kama Mwenyezi Mungu akijua kheri yoyote nyoyoni mwenu, basi atawapa bora kuliko vilivyochukuliwa kwenu na atawasamehe. Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa maghufira, Mwenye kurehemu. 71. Na kama wanataka kukufanyia uhaini, basi walikwishamfanyia uhaini Mwenyezi Mungu hapo nyuma, na akakupa ushindi juu yao. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi, Mwenye hekima.

72. Hakika wale walioamini na wakahama na wakapigania dini ya Mwenyezi Mungu kwa mali zao na nafsi zao; na wale waliowapokea (wahamiaji) na kuwasaidia, hao ndio wanaolindana wao kwa wao. Na wale walioamini lakini wasihame, nyinyi hamna wajibu wa ulinzi wao hata kidogo, mpaka wahame. Lakini wakiwaomba msaada katika dini, basi ni juu yenu kuwasaidia, isipokuwa ikiwa dhidi ya watu ambao yapo mapatano baina yenu na wao (ya kutopigana). Na Mwenyezi Mungu anayaona mnayoyatenda. 73. Na wale waliokufuru wanalindana wenyewe kwa wenyewe. Msipofanya hivi (kulindana nyie kwa nyie) kutakuwa na machafuko na uasi duniani na uharibifu mkubwa.

74. Na wale walioamini wakahama na kupigana jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu na wale waliopokea wahamiaji na kuwasaidia, hao ndio waumini wa kweli; watapata maghufira na riziki njema. 75. Na wale waotakaomini baadaye na wakahamia na wakapigania jihadi pamoja nanyi, basi hao ni miongoni mwenu. Na ndugu wa nasaba wanastahikiana

zaidi wenyewe kwa wenyewe katika Kitabu cha Mwenyezi
Mungu, hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu.

9. Sura At-Tawba

## SURA YA TOBA –AU BARA A-KINGA

1 (Hili ni tangazo la) Kujitoa Mwenyezi Mungu na Mtume
Wake (na dhima ya ahadi) kwa wale mlioahidiana nao
miongoni mwa Mapagani wa Kiarabu. 2 Basi tembeeni
katika nchi miezi minne (mpendavyo); lakini jueni kwamba
nyinyi hamuwezi kumshinda Mwenyezi Mungu, na kwamba
Mwenyezi Mungu atawatia aibu wale wanaomkana. 3 Na ni
tangazo litokalo kwa Mwenyezi Mungu na Mtume Wake
kwa watu wote siku ya Hijja kubwa ya kwamba Mwenyezi
Mungu amejitoa na (jukumu lolote kwa) Mapagani, na pia
Mtume Wake. Basi kama mkitubu ndiyo kheri kwenu, na
kama mkikengeuka, basi jueni kwamba nyinyi hamuwezi
kumshinda Mwenyezi Mungu, na wabashirie waliokufuru
adhabu iumizayo. 4 Isipokuwa wale mlioahidiana nao
miongoni mwa mapagani, kisha wasiwasaliti kwa kuvunja
kipengee chochote cha makubaliano, wala wasimsaidie
yeyote dhidi yenu, basi watimizieni ahadi yao mpaka muda
wao. Hakika Mwenyezi Mungu anawapenda wenye kumcha.

5 Na iishapo miezi mitukufu, piganeni na waueni
washirikina popote mtakapowakuta, na wakamateni na
muwazingire na wavizieni katika kila njia. Lakini wakitubu na
wakadumisha swala na wakatoa zaka, basi waachieni wende
zao. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa maghufira
Mwenye kurehemu. 6 Na kama yeyote katika mapagani

akikutaka hifadhi, mhifadhi ili apate kusikia maneno ya
Mwenyezi Mungu, kisha mfikishe mahali pake pa usalama.
Hayo ni kwa kuwa wao ni watu wasiojua.

7 Itakuwaje Mapagani wawe na ahadi na Mwenyezi
Mungu na Mtume Wake, isipokuwa tu wale mlioahidiana
mbele ya Msikiti Mtakatifu? Basi maadamu wanakwenda
na nyinyi sawa, nanyi nendeni nao sawa. Hakika Mwenyezi
Mungu anawapenda wenye kumcha. 8 Itakuwaje, na ilhali
wao wakiwashinda hawataheshimu mahusiano ya udugu
wala ahadi? Wanawafurahisha kwa midomo yao tu, hali
nyoyo zao zinakataa; na wengi wao ni waovu. 9 Wamenunua
Ishara za Mwenyezi Mungu kwa thamani ndogo (dunia),
kwa hiyo wakazuilia watu na njia Yake. Hakika ni mabaya
waliyokuwa wakiyafanya. 10 Hawaheshimu kwa Muislamu
uhusiano wa udugu wala ahadi; na hao ndio warukao mipaka.
11 Lakini wakitubu na wakadumisha Swala na wakatoa Zaka,
hao ni ndugu zenu katika dini na tunazifafanua Aya kwa watu
wanaojua

12. Na kama wakivunja viapo vyao baada ya kuahidi kwao
na wakatukana dini yenu, basi piganeni na viongozi wa ukafiri.
Hakika hao hawana viapo (vya kweli); huenda kwa (kufanya
hivyo) wakaacha. 13. Je, hamtapigana na watu waliovunja
viapo vyao na wakala njama ya kumfukuza Mtume, nao ndio
waliowaanzeni mara ya kwanza? Je, mnawaogopa? Basi
Mwenyezi Mungu anastahiki zaidi mumuogope ikiwa ninyi
ni waumini. 14. Piganeni nao, Mwenyezi Mungu awaadhibu
kwa mikono yenu, na awafedheheshe, na awanusuru
muwashinde na aipoze hasira ya watu walio waumini.
15. Na aondoe ghadhabu ya nyoyo zao. Na Mwenyezi Mungu

humkubalia toba amtakaye, na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi,
Mwenye hekima.
16. Je, mlidhani kuwa mtaachwa tu kabla Mwenyezi
Mungu hajawabainisha wale waliopigana jihadi miongoni
mwenu, ambao hawakumfanya rafiki mwandani asiyekuwa
Mwenyezi Mungu na Mtume Wake na waumini? Mwenyezi
Mungu ana habari za mnayoyafanya.
17. Haiwi kwa Mapagani kuwa ndio waimarishe Misikiti
ya Mwenyezi Mungu, hali wanajishuhudia wenyewe ukafiri.
Hao vitendo vyao vimeporomoka, na watadumu katika moto.
18. Wanaoimarisha misikiti ya Mwenyezi Mungu ni wale tu
wanaomwamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho na
wakadumisha swala na wakatoa zaka na wasimwogope yeyote
isipokuwa Mwenyezi Mungu. Basi hao huenda wakawa
miongoni mwa waliongoka. 19. Je, mnafanya kuwanywesha
maji mahujaji na kuimarisha Msikiti Mtakatifu ni sawa na
yule aliyemwamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho
na akapigana jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu?
Hawawi sawa mbele ya Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi
Mungu hawaongozi watu madhalimu. 20. Wale walioamini
na wakahama na wakapigana jihadi katika njia ya Mwenyezi
Mungu, kwa mali zao na roho zao, wao wana cheo kikukbwa
mbele ya Mwenyezi Mungu, na hao ndio wenye kufuzu.
21. Mola Wao anawapa habari njema za (kupata) huruma na
ridhaa zitokazo Kwake na mabustani ambayo watapata ndani
yake neema zitakazodumu. 22. Watakaa humo milele. Hakika
kwa Mwenyezi Mungu kuna malipo makubwa.
23. Enyi walioamini! Msiwafanye baba zenu na ndugu
zenu kuwa vipenzi vyenu ikiwa wanapenda zaidi ukafiri
kuliko imani. Na atakayewafanya vipenzi katika nyinyi

basi hao ndio madhalimu. 24. Sema, ikiwa baba zenu, na wana wenu, na ndugu zenu, na wake zenu, na jamaa zenu, na mali mlizozichuma, na biashara mnazohofia kuharibika, na majumba mnayoyapenda, hivyo mnavipenda zaidi kuliko Mwenyezi Mungu na Mtume Wake na jihadi katika njia Yake….. basi ngojeni mpaka Mwenyezi Mungu alete hukumu Yake, na Mwenyezi Mungu hawaongozi watu mafasiki.

25. Hakika Mwenyezi Mungu amewanusuru nyie katika viwanja vingi vya vita, na siku ya (vita vya) Hunain wakati wingi wenu ulipowafurisha vichwa, ila haukuwafaa chochote. Ardhi ikawawia finyu ingawaje ni pana; kisha mkageuka nyuma kukimbia. 26. Kisha Mwenyezi Mungu akateremsha utulivu Wake juu ya Mtume Wake na juu ya waumini, na akawateremshia majeshi ambayo hamkuyaona, na akawaadhibu wale waliokufuru. Na hayo ndiyo malipo ya makafiri 27. Kisha baada ya haya Mwenyezi Mungu atamkubalia toba amtakaye. Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa maghufira, Mwenye kurehemu. 28. Enyi walioamini! Hakika Mapagani ni wachafu, kwa hivyo wasiukaribie Msikiti Mtakitifu baada ya mwaka wao huu. Na kama mkihofia umasikini, basi hivi karibuni Mwenyezi Mungu atawatajirisha kwa fadhila Yake akitaka. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi Mwenye hekima.

29. Piganeni na wale wasiomwamini Mwenyezi Mungu wala siku ya mwisho wala hawaharamishi aliyoharamisha Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, wala hawashiki dini ya haki, miongoni mwa waliopewa Kitabu, mpaka watoe kodi kwa hiari yao wakiwa watiifu. 30. Mayahudi wanasema, Uzayr (Ezra) ni mwana wa Mungu; na Wakristo wanasema Issa (Yesu) ni mwana wa Mungu. Hiyo ndiyo kauli yao kwa

vinywa vyao. Wanaiga maneno ya wale waliokufuru zamani.
Mwenyezi Mungu awalaani! Lo! Wanajidanganya vipi hawa!
31. Wamewafanya makuhani wao na watawa wao kuwa
miungu badala ya Mwenyezi Mungu, na pia Masih (Masiah)
mwana wa Maryam. Wala hawakuamrishwa isipokuwa
wamwambudu Mungu mmoja tu hakuna Mungu ila Yeye
Ametakata na wanayomshirikisha nayo.
32. Wanataka kuizima nuru ya Mwenyezi Mungu kwa
vinywa vyao. Na Mwenyezi Mungu anakataa ila aitimize
nuru Yake, ijapokuwa mapagani watachukia. 33. Yeye ndiye
aliyemtuma Mtume Wake kwa uongofu na dini ya haki ili
ipate kushinda dini zote, ijapokwa washirikina wamechukia.
34. Enyi walioamini! Hakika wengi katika wachungaji
na watawa wanakula mali za watu kwa batili na kuwazuilia
watu na njia ya Mwenyezi Mungu. Na wale walimbikizao
dhahabu na fedha na hawazitumii katika njia ya Mwenyezi
Mungu, basi wabashirie adhabu iumizayo. 35. Siku (fedha na
dhahabu zao) zitakapofuliwa katika moto wa Jahannam, na
zikachapwa kwenye mapaji ya nyuso zao na mbavu zao na
migongo yao (wakiambiwa)'Hizi ndizo mlizojilimbikizia.
Haya, onjeni vile mlivyokuwa mkivilimbikiza'..
36. Hakika idadi ya miezi kwa Mwenyezi Mungu ni
miezi kumi na miwili katika Kitabu cha Mwenyezi Mungu
(tangu) siku alipoumba mbingu na ardhi. Katika hiyo iko
(miezi) mine mitakatifu. Hiyo ndiyo dini iliyo sawa. Basi
msidhulumu nafsi zenu katika miezi hiyo. Na piganeni na
Mapagani wote, kama wanavyopigana nanyi wote; na jueni
kuwa Mwenyezi Mungu yuko pamoja na wamchao. 37. Hakika
kuakhirisha (miezi iliyokatazwa) ni nyongeza ya ukafiri,
kwa tendo hilo hupotezwa zaidi wale walio kufuru. Mwaka

mmoja wanauruhusu na mwaka mwingine wanaukataza, ili wafanye sawa idadi ya ile (miezi) ambayo Mwenyezi Mungu amekataza (vita). (Kwa kufanya hivyo) huhalalisha aliyoharamisha Mwenyezi Mungu. Wamepambiwa matendo yao mabaya wayaone mazuri. Na Mwenyezi Mungu hawaongozi watu wanaomkana.

38. Enyi walioamnini! Mna nini mnapoambiwa nendeni katika njia ya Mwenyezi Mungu mnang'ang'ania mno dunia? Je, mnaridhika zaidi na maisha ya duniani kuliko ya Akhera? Lakini starehe za maisha ya dunia kulinganisha na Akhera ni chache tu. 39. Kama hamwendi atawaadhibu kwa adhabu iumizayo na atawaleta watu wengine badala yenu, na hamtamdhuru chochote; Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye uwezo juu ya kila kitu. 40. Kama hamtamsaidia, basi Mwenyezi Mungu alikwisha mnusuru; pale waliokufuru walipomtoa nyumbani, akiwa hana mwingine ila mwenzake mmoja tu na wao wawili wakiwa ndani ya pango, akamwambia mwenziwe 'Usihuzunike, hakika Mwenyezi Mungu yuko pamoja nasi'. Mwenyezi Mungu akamteremshia utulivu Wake, na akamwunga mkono kwa kwa majeshi msiyoyaona. Na akalifanya neno la wale waliokufuru kuwa chini, na neno la Mwenyezi Mungu ndilo la juu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu Mwenye hekima.

41. Tokeni kweda kwenye jihadi mkiwa (na silaha) nyepesi au nzito, mkapigane jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu kwa mali zenu na roho zenu. Hilo ni kheri kwenu mkiwa mnajua. 42. Lau ingekuwa ni ushindi bila jasho, na safari yenyewe ni fupi, bila shaka wote hao (wanafiki) wangekufuata. Lakini imekuwa ndefu kwao na kuwalemea. Wataapa kwa Mwenyezi Mungu, 'lau tungeliweza bila shaka

tungelitoka pamoja nanyi’. Wanaziangamiza nafsi zao tu, kwani Mwenyezi Mungu anajua kuwa ni waongo.

43. Mwenyezi Mungu amekusamehe. Kwa nini umewapa ruhusa kabla ya kubainika kwako wanaosema kweli na ukawajua waongo. 44. Hawatakuomba ruhusa wale ambao wanamwamini kweli Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho, ya kutokwenda kupigana jihadi kwa mali zao na roho zao. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuwajua wenye kumcha.
45. Hakika wanaokuomba ruhusa ni wale tu wasiomwamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho, na wenye shaka katika nyoyo zao; kwa hiyo wanasitasita katika shaka yao hiyo. 46. Lau wangelitaka kutoka (kwenda vitani), bila shaka wangelifanya maandalizi. Lakini Mwenyezi Mungu alichukia wao kutoka, kwa hiyo akawazuia na ndiyo wakaambiwa: ‘Kaeni pamoja na wakaao.’

47. Lau wangelitoka pamoja nanyi wasingewazidisha isipokuwa utovu wa nidhamu, na wangelikwenda huku na huko kati yenu kuwachochea uasi. Na miongoni mwenu wako ambao wangewasikiliza. Na Mwenyezi Mungu anawajua watu wabaya. 48. Tangu hapo walikwishakula njama ya kufanya uasi na wakakupindulia pindulia mambo, mpaka ukweli ukafika, ilani ya Mwenyezi Mungu ikawa wazi na wao wakawa wamechukia.

49. Na miongoni mwao kuna anayesema: Niruhusu wala usinitie katika fitina. Hakika wamekwishatumbukia katika fitina. Na hakika Jahannam imewazunguka makafiri.
50. Linapokupata jambo zuri linawachukiza, na ukikusibu msiba husema: ‘sisi tulikwishachukua tahadhari tayari’ wanageuka kwenda zao wakiwa wamefurahi. 51. Sema halitatusibu isipokuwa lile alilotuandikia Mwenyezi Mungu.

Yeye ni Mola Wetu. Na kwa Mwenyezi Mungu pekee ndio waumini waweke mategemeo yao. 52. Sema: hivi mnangojea litupate lolote isipokuwa moja kati ya mazuri mawili: (kuuawa au kupata ushindi)? Na sisi tunawangojea Mwenyezi Mungu awafikishie adhabu itokayo Kwake au kwa kupitia kwenye mikono yetu. Basi ngojeeni nasi tunangoja pamoja nanyi.

53. Sema: Toeni mkipenda msipende, hakitakubaliwa kitu chochote kutoka kwenu. Hakika nyinyi mmekuwa watu wabaya, waasi. 54. Na hakikuwazuia kukubaliwa michango yao kitu chochote isipokuwa ni kule kuwa wamemkana Mwenyezi Mungu na Mtume Wake. Wala hawaji kwenye swala isipokuwa katika hali ya uvivu, wala hawatoi michango yao ila huku wamechukia. 55. Kamwe zisikuvutie mali zao wala watoto wao. Hakika Mwenyezi Mungu anataka tu kuwaadhibu kwayo katika maisha ya dunia, na roho zao zitoke na hali wao ni makafiri. 56. Na wanaapa kwa Mwenyezi Mungu kwamba wao ni katika nyinyi, na wala wao si katika nyinyi. Lakini wao ni watu wanaoogopa (kujulikana). 57. Lau wangelipata pa kukimbilia au mapango au mahali pa kuingia wangeligeukia huko kwa kasi sana.

58. Na miongoni mwao wako wanaokulaumu katika (kugawa) sadaka. Wanapopewa katika hizo huridhika, na wasipopewa katika hizo hukasirika. 59. Na lau wangeliridhia kile alichowapa Mwenyezi Mungu na Mtume Wake na wakasema: ‘Mwenyezi Mungu anatutosheleza, Mwenyezi Mungu atatupa katika fadhila Zake, na Mtume Wake pia. Sisi twaelekeza kwa Mwenyezi Mungu matarajio yetu’ (Hii ingekuwa bora kwao). 60. Wa kupewa sadaka ni mafukara na masikini na wafanyao kazi ya kuzikusanya na kuzigawa, na wanaotiwa nguvu nyoyo zao (kwa Uislamu), na kwa

kuwakomboa watumwa na wenye madeni na katika njia ya Mwenyezi Mungu na wasafiri. Huu ni wajibu uliofaradhiwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua, Mwenye hekima.

61. Na miongoni mwao wako wanaomuudhi Mtume na kusema: 'Yeye asikiza kila kitu tu'. Sema: Anasikiliza yaliyo mema tu kutoka kwenu. Anamwamini Mwenyezi Mungu, na ana imani na waumini; na ni rehema kwa wale wanaoamini miongoni mwenu. Na wale wanaomuudhi Mtume wa
Mwenyezi Mungu wana adhabu iumizayo. 62. Wanawaapia
Mwenyezi Mungu ili wawaridhishe na hali Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, ndiye mwenye haki zaidi ya kumridhisha,
ikiwa wao ni waumini. 63. Je, Hawajui kuwa anayeshindana
na Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, basi huyo atapata moto wa Jahanam adumu humo? Hiyo ni hizaya kubwa.

64. Wanaogopa wanafiki isije ikateremshwa sura kwa ajili yao itakayowatajia yaliyomo nyoyoni mwao. Sema: Fanyeni mzaha tu, hakika Mwenyezi Mungu atayatoa mnayoyaogopa.
65. Na ukiwauliza watasema: 'Sisi tulikuwa tukipiga porojo na kucheza tu'. Sema: Je, mlikuwa mkimfanyia mzaha
Mwenyezi Mungu na Aya Zake na Mtume Wake? 66. Msitoe
udhuru, mmekwisha kufuru baada ya kuamini kwenu. Tukisamehe kundi moja miongoni mwenu tutaliadhibu kundi jingine kwa vile wao walikuwa wakosefu.

67. Wanafiki wanaume na wanafiki wanawake ni hali moja. Wanaamrisha maovu na kukataza mema na wanafumba mikono yao. Wamemsahau Mwenyezi Mungu na Yeye
amewasahau. Hakika wanafiki ndio mafasiki. 68. Amewaahidi
Mwenyezi Mungu wanafiki wanaume na wanafiki wanawake na makafiri moto wa Jahanam hali ya kudumu humo. Ni

tosha yao. Na Mwenyezi Mungu amewalaani. Na wana wao adhabu ya kudumu. 69. Ni kama wale waliokuwa kabla yenu; walikuwa na nguvu zaidi kuliko nyinyi, na mali nyingi zaidi na watoto. Basi walistarehea fungu lao, na nyinyi mwastarehea fungu lenu, kama walivyostarehea fungu lao wale waliokuwa kabla yenu na mkazama (katika batili) kama walivyozama. Hao zimeporomoka amali zao katika dunia na Akhera, na hao ndio waliopata hasara. 70. Je, hazikuwafikia habari za wale walio kuwa kabla yao, watu wa Nuh (Noah) na Ad na Thamud na kaumu ya Ibrahim na watu wa Midian na miji iliyopinduliwa juu chini? Basi Mwenyezi Mungu hakuwa ni mwenye kuwadhulumu, lakini wao walikuwa wakijidhulumu wenyewe.

71. Na waumini wanaume na waumini wanawake ni marafiki wao kwa wao; huamrishana mema na kukatatazana maovu, na husimamisha swala, na hutoa zaka, na humtii Mwenyezi Mungu na Mtume Wake. Hao Mwenyezi Mungu atawarehemu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu Mwenye hekima. 72. Amewaahidi Mwenyezi Mungu waumini wanaume na waumini wanawake bustani (Pepo) ambazo hupita mito chini yake; hali ya kudumu humo na maskani mema katika mabustani ya milele. Na radhi za Mwenyezi Mungu ndiyo (neema) kubwa zaidi. Huko ndiko kufuzu kukubwa.

73. Ewe Mtume! Pambana na makafiri na wanafiki na uwawekee ngumu. Na makazi yao ni Jahanamu, nayo ni marejeo mabaya. 74. Wanaapa kwa Mwenyezi Mungu, hawakusema. Na hakika wamekwishasema neno la kufuru, na wakakufuru baada ya kusilimu kwao, wakajihimu kufanya wasiyoyaweza kuyafikia. Na hawakuchukia ila

kuwa Mwenyezi Mungu na Mtume Wake amewatajirisha
katika fadhila Zake. Wakitubia, itakuwa heri kwao; na kama
wakikengeuka, Mwenyezi Mungu atawaadhibu adhabu
iumizayo duniani na Akhera. Hawana kiongozi katika ardhi
wala msaidizi.
75. Na miongoni mwao wapo waliomwahidi Mwenyezi
Mungu (kwa kusema): ‘Akitupa katika fadhila yake, bila
shaka tutatoa sadaka na hakika tutakuwa miongoni mwa
watendao wema’. 76. Lakini alipowapa katika fadhila
yake, waliifanyia ubakhili wakageuka na huku wakipuuza.
77. Basi akawalipa unafiki kuutia nyoyoni mwao mpaka siku
watakapokutana Naye, kwa sababu ya kumhalifu Mwenyezi
Mungu yale waliyomwahidi na kwa sababu ya kusema kwao
uwongo. 78. Je, hawajui kwamba Mwenyezi Mungu anajua
siri zao na minong’ono yao, na kwamba Mwenyezi Mungu
ndiye ajuaye sana mambo ya ghaibu?
79. Wale wanaowabeza waumini wanaotoa sadaka nyingi,
na (hata) wale wasio nacho cha kutoa ila kadri ya juhudi
yao, basi huwakejeli. Mwenyezi Mungu atawafanyia kejeli
nao, na wana adhabu iumizayo. 80. Waombee msamaha
au usiwombee. Hata ukiwaombea msamaha mara sabini,
Mwenyezi Mungu hatawasamehe. Hayo ni kwa sababu
wao wamemkufuru Mwenyezi Mungu na Mtume Wake; na
Mwenyezi Mungu hawaongozi watu waovu.
81. Walifurahi walioachwa nyuma kwa kule kubakia kwao
nyuma ya Mtume wa Mwenyezi Mungu. Na walichukia
kupigana jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu kwa
mali zao na roho zao. Wakaambiana: ‘Msitoke nje wakati
wa joto!’. Sema: Moto wa Jahanamu una joto kali zaidi
lau wangelifahamu. 82. Basi (waache) wacheke kidogo.

Watalia sana. Hayo yatakuwa malipo ya (uovu) waliokuwa wakiufanya. 83. Basi Mwenyezi Mungu akikurudisha kwenye kundi miongoni mwao, na wakakutaka idhini ya kutoka (nawe), sema: 'Hamtatoka pamoja nami tena milele, wala hamtapigana na adui pamoja nami. Hakika nyinyi mliridhia kukaa nyumbani mara ya kwanza, basi kaeni pamoja na watakaobaki nyuma'. 84. Wala usimswalie kamwe yeyote miongoni mwao akifa, wala usisimame kaburini kwake. Hakika wao wamemkataa Mwenyezi Mungu na Mtume Wake na wakafa wakiwa ni mafasiki.

85. Wala zisikubabaishe mali zao na watoto wao. Hakika Mwenyezi Mungu anataka kuwaadhibu kwa sababu yake katika dunia na zitoke roho zao wakiwa ni waovu. 86. Na inapoteremeshwa Sura, kuwa mwaminini Mwenyezi Mungu na piganeni jihadi pamoja na Mtume Wake, wanakuomba ruhusa, wale wenye nguvu na uwezo miongoni mwao, na kusema: tuache tuwe pamoja na wanaobaki nyumbani. 87. Wamechagua kuwa pamoja na wanaobaki nyuma, Na nyoyo zao zimepigwa muhuri kwa hiyo hawafahamu. 88. Lakini Mtume na wale walioamini pamoja naye walipigana jihadi kwa mali zao na roho zao. Na hao ndio wenye kheri; na hao ndio wenye kufaulu. 89. Mwenyezi Mungu amewaandalia bustani ambazo hupita mito ya maji chini yake, watakaa humo daima. Huko ndiko kufuzu kukubwa.

90. Na walikuja wenye kudai kuwa na udhuru miongoni mwa mabedui ili wapewe ruhusa. Lakini wale waliomsingizia uwongo Mwenyezi Mungu na Mtume walijikalia tu (bila kuomba ruhusa. Itawafika wale waliokufuru miongoni mwao adhabu iumizayo. 91. Hapana lawama juu ya walio dhaifu, wala juu ya wagonjwa, wala wasiokuwa na mali ya kutumia,

maadam wamemsafishia nia Mwenyezi Mungu na Mtume Wake. Hakuna sababu (ya kuwalaumu) wanaofanya wema; na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa msamaha, Mwenye kurehemu. 92. Wala hakuna lawama juu ya wale waliokujia ili uwachukue, ukasema: sina cha kuwabebea. Wakarudi huku macho yao yanamiminika machozi kwa huzuni ya kutopata cha kugharamia. 93. Lakini lawama ni juu ya wale wanaokuomba ruhusa (ya kutokwenda vitani) na hali wao ni matajiri. Wameridhika tu kuwa pamoja na wanaobaki nyumbani. Na Mwenyezi Mungu amepiga muhuri juu ya nyoyo zao; kwa hivyo hawajui.

94. Watawatolea (visingizio na) nyudhuru kadhaa mnaporudi kutoka vitani. Sema, msitoe visingizio. Sisi hatuwaamini. Mwenyezi Mungu amekwishatueleza habari zenu. Na Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, watavifuatilia vitendo vyenu. Kisha mtarudishwa kwa Mjuzi wa ghaibu na yaliyo dhahiri ili awaambie mliyokuwa mkiyatenda.
95. Watawaapia kwa jina la Mwenyezi Mungu mtakaporudi kwao (kutoka vita ya Tabuk) ili muachane nao. Basi achaneni nao. Hakika wao ni machukizo, na makazi yao ni Jahanamu. Hayo ni malipo ya yale waliyokuwa wakiyachuma.
96. Wanawaapieni ili muwe radhi nao. Kama mkiwa radhi nao, basi hakika Mwenyezi Mungu hatakuwa radhi na wahaini.

97. Mabedui wamewazidi sana (watu wa mjini) katika kufuru na unafiki. Na wameelekea zaidi kutojua mipaka ya yale aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu juu ya Mtume. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi, Mwenye hekima. 98. Miongoni mwa mabedui wako wanaochukulia kuwa wanavyovitoa ni kutozwa faini, na wanangoja mambo yawageukieni. Wao

ndiyo mambo yatawageukia kuwa mabaya. Na Mwenyezi Mungu ni Msikizi, Mjuzi.

[99.] Miongoni mwa mabedui wako wanaomwamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho, na wanaamini kuwa wanavyovitoa ndivyo vitavyowaweka karibu na Mwenyezi Mungu na (kupata) dua za Mtume. Naam! Ni kweli hivyo vitawaweka karibu. Mwenyezi Mungu atawaingiza katika rehema Yake. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa maghufira, Mwenye kurehemu.

[100] Na waliotangulia mwanzoni miongoni mwa Wahamiaji na Waliowapokea (Muhajirun na Ansar) , na wale waliowafuata kwa wema, Mwenyezi Mungu yuko radhi nao na wao wako radhi Naye, na amewaandalia Bustani ambazo hupita mito ya maji chini yake, watakaa humo milele. Huko ndiko kufuzu kukubwa. [101] Na miongoni mwa mabedui walio pambizoni mwenu wamo wanafiki, na katika wenyeji wa Madina pia wako waliobobea katika unafiki. Wewe huwajui, Sisi tunawajua. Tutawaadhibu mara mbili, kisha watarudishwa kwenye adhabu kubwa.

[102.] Na wengine wamekiri dhambi zao; wakachanganya vitendo vyema na vingine viovu. Huenda Mwenyezi Mungu akapokea toba zao. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa maghufira, Mwenye kurehemu. [103.] Twaa sadaka katika mali zao uwasafishe na uwatakase kwayo. Na uwaombee huruma. Hakika maombi yako ni utulivu kwao. Na Mwenyezi Mungu ni Msikizi, Mjuzi. [104.] Je, hawajui kwamba Mwenyezi Mungu ndiye anayekubali toba ya waja Wake na kuzipokea sadaka. Na kwamba Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kukubali toba, Mwenye kurehemu? [105.] Na sema: Tendeni vitendo. Mwenyezi Mungu na Mtume Wake na waumini

wataviona vitendo vyenu, kisha mrudishwe kwa Mjuzi
wa visivyoonekana na vinavyoonekana, Naye awaambie
mliyokuwa mkiyatenda. 106. Na wapo wengine wanangojea
amri ya Mwenyezi Mungu; ama atawaadhibu au awasamehe.
Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi, Mwenye hekima.
107. Na (kuna) wale waliojenga msikiti kwa ajili ya
kuleta madhara na kufuru na kuwatenganisha Waislamu,
na (kuwa) mahali pa kumngojea yule aliyempiga vita
Mwenyezi Mungu na Mtume hapo nyuma. Na bila shaka
wanaapa kwamba 'hatukukusudia isipokuwa wema tu'.
Mwenyezi Mungu anashuhudia kuwa wao ni waongo.
108. Usisimame ndani ya msikiti huo kabisa. Msikiti uliojengwa
juu ya misingi ya kumcha Mungu tangu siku ya mwanzo,
unastahiki zaidi wewe usimame ndani yake. Humo mna watu
wanaopenda kujitakasa; na Mwenyezi Mungu anawapenda
wanaojitakasa. 109. Je, aliyeweka msingi wa jengo lake juu
ya kumcha Mwenyezi Mungu na kutaka radhi (zake) ni bora,
au aliyeweka msingi wa jengo lake ukingoni mwa shimo
linalomomonyoka, na likaporomoka pamoja naye katika
moto wa Jahannam? Na Mwenyezi Mungu hawaongozi watu
madhalimu. 110. Jengo lao hilo walilolijenga litaendelea kuwa
ni sababu ya kuwa na shaka nyoyoni mwao, hadi hapo nyoyo
zao zitakapokatika vipande vipande (kufa). Na Mwenyezi
Mungu ni Mjuzi, Mwenye hekima.
111. Hakika Mwenyezi Mungu amenunua kwa Waumini
roho zao na mali zao kwamba wao wapate Pepo: hupigana
katika njia ya Mwenyezi Mungu;wakaua na kuuawa. Hiyo
ndiyo ahadi ya kweli aliyowapa waumini katika Torati, Injili na
Qur'an. Na ni nani atekelezaye zaidi ahadi kuliko Mwenyezi
Mungu? Basi furahini kwa biashara yenu mliyofanya naye.

Na huko ndiko kufuzu kukubwa. [112.] (Waumini wa kweli ni) Wanaotubia, wanaoabudu, wanaohangaika kusafiri (kutafuta elimu) wanaorukuu, wanaosujudu, wanaoamrisha mema na wanaokataza maovu na wanaohifadhi mipaka ya Mwenyezi Mungu. Na wape bishara njema Waumini

[113.] Haifai kwa Nabii na wale walioamini kuwatakia msamaha mapagani, hata kama ni jamaa zao, baada ya kutambua kuwa wao ni watu wa motoni. [114.] Ibrahim hakumwombea msamaha baba yake isipokuwa kwa sababu alimwahidi baba yake kuwa angemwombea msamaha. Lakini alipogundua kuwa yeye ni adui wa Mwenyezi Mungu, alijiepusha naye. Hakika Ibrahim alikuwa mpole sana na mnyenyekevu. [115.] Mwenyezi Mungu hawaachi watu wapotee baada ya kwisha kuwaongoza; mpaka awabainishie ya kujiepusha nayo. Hakika Mwenyezi Mungu anajua kila kitu. [116.] Hakika Mwenyezi Mungu ni Wake ufalme wa mbingu na ardhi, huhuisha na hufisha; nanyi hamna kiongozi wala msaidizi isipokuwa Mwenyezi Mungu.

[117.] Hakika Mwenyezi Mungu amekwisha msamehe Mtume na wahamiaji na wenyeji (Ansar) waliomfuata katika saa ya dhiki, pale zilipokaribia nyoyo za baadhi yao kugeuka. Kisha akawakubalia toba yao. Hakika Yeye kwao ni Mpole, Mwenye kurehemu. [118.] Na pia (amewasamehe) wale watatu walioachwa nyuma, mpaka wakaiona dunia ni finyu, ingawaje ni kunjufu. Na wakaona dhiki kubwa. Wakajua kuwa hapana pa kukimbilia isipokuwa kwa Mwenyezi Mungu pekee. Kisha akawaelekea (kwa rehema yake) ili wapate kutubu. Hakika Mwenyezi Mungu ndiye Mwingi wa kukubali toba Mwenye kurehemu.

[119.] Enyi walioamini! Mcheni Mwenyezi Mungu na

kuweni pamoja na wakweli. 120. Haifai kwa watu wa Madina na mabedui walio pembeni mwao kubakia nyuma wasitoke na Mtume wa Mwenyezi Mungu, au kupendelea uhai wao zaidi kuliko wa Mtume. Hiyo ni kwa sababu hakiwapati kiu wala taabu wala njaa katika njia ya Mwenyezi Mungu, wala hawakanyagi mahali panapowachukiza makafiri, wala hawapatwi na majeraha kutoka kwa adui, isipokuwa huandikiwa kuwa ni amali njema. Hakika Mwenyezi Mungu haupotezi ujira wa watendao mazuri. 121. Wala hawatoi chochote cha kujikimu, kidogo au kikubwa, wala hawavuki bonde lolote ila huandikiwa (malipo) ili Mwenyezi Mungu aje awalipe bora zaidi ya mema waliyokuwa wakiyatenda.

122. Wala haifai kwa waumini kutoka wote (kupigana) . Laiti kingetoka katika kila jeshi kikundi kimoja kwenda kujifunza dini, ili waje wawaonye wenzao watakaporejea, ili wapate kujihadhari.

123. Enyi walioamini! Piganeni na wale makafiri walio karibu yenu na waonje ushupavu wenu; na jueni kuwa Mwenyezi Mungu yuko pamoja na wenye kumcha. 124. Na inapoteremshwa Sura, wapo miongoni mwao wasemao, ‘Ni nani miongoni mwenu Sura hii imemzidishia imani? Wale walioamini huwazidishia imani, nao hufurahia. 125. Ama wale wenye maradhi katika nyoyo zao, huwazidishia shaka juu ya shaka waliyonayo, na watakufa wakiwa makafiri. 126. Je, hawaoni kwamba wao hujaribiwa kila mwaka (kwa njaa na maradhi) mara moja au mara mbili? Kisha hawatubu wala hawakumbuki? 127. Na inapoteremshwa Sura wanatazamana wenyewe kwa wenyewe (wakiulizana): ‘Je, kuna yeyote anayewaona’? Kisha hugeuka. Mwenyezi

Mungu amezigeuza nyoyo zao kwa kuwa wao ni watu wasiofahamu.

128. Hakika amewajia Mtume kutoka miongoni mwenu wenyewe. Yanamhuzunisha yanayowataabisha, anawahangaikia (nyinyi) sana, kwa waumini ni mpole, mwenye huruma. 129. Basi wakigeuka, sema: 'Mwenyezi Mungu tosha!, hakuna Mola ila Yeye tu. Mimi namtegemea Yeye, na Yeye ndiye Bwana wa Kiti cha madaraka na enzi.

10. Sura Yunus

# SURA YA YUNUS 'JONAH'

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema, Mwenye kurehemu.

1 *Alif Lam Raa.*

Hizi ni Aya za Kitabu chenye hekima. 2 Hivi imekuwa ajabu kwa watu, kwamba tumemfunulia ujumbe mmoja wao, kuwa uwaonye watu na uwape bishara wale walioamini kwamba wana cheo kikubwa cha heshima mbele ya Mola Wao? (Lakini) makafiri wakasema: 'Hakika huyu ni mchawi wa wazi'.

3 Hakika Mola Wenu ni Mwenyezi Mungu ambaye ameumba mbingu na ardhi katika (kipimo cha) siku sita, na akajiimarisha katika ufalme wake, akiendesha mambo yote. Hakuna mwombezi ila baada ya idhini Yake. Huyo ndiye Mwenyezi Mungu, Mola Wenu, mwabuduni. Hivi hamwonyeki? 4 Kwake ndiyo marejeo yenu nyote. Hii ni ahadi ya Mwenyezi Mungu ya kweli. Hakika Yeye

ndiye alieanzisha uumbaji kisha ataurejesha, ili awalipe kwa uadilifu wale walioamini na wakafanya mema. Na waliokufuru, watapata kinywaji kinachochemka na adhabu chungu kwa kuwa walikuwa wakikufuru.

5. Yeye ndiye aliyefanya jua kuwa ni mwanga na mwezi kuwa ni nuru, na akaupimia vituo ili mjue idadi ya miaka na hisabu. Mwenyezi Mungu hakuviumba hivyo isipokuwa ili ukweli (uwe wazi). Anazipambanua Aya kwa watu wanaojua. 6. Hakika katika kuhitalifiana usiku na mchana na alivyoviumba Mwenyezi Mungu katika mbingu na ardhi, kuna ishara kwa watu wamchao. 7. Hakika wale wasiotaraji kukutana Nasi na wakawa radhi na maisha ya duniani na wakatosheka nayo, na wale walioghafilika na Ishara Zetu... 8. Hao makazi yao ni motoni kwa sababu ya yale waliyokuwa wakiyachuma. 9. Hakika wale walioamini na wakatenda mema, Mola Wao Mlezi atawaongoza kwa sababu ya imani yao. Itapita mito ya maji chini yao katika Mabustani yenye neema. 10. Wito wao humo utakuwa: 'Subhaanak Allahumma- Umetakasika ewe Mwenyezi Mungu!' Na maamkuzi yao ni 'Salaam' na mwisho wa wito wao ni: 'Alhamdulillahi Rabbi al Alamiin- Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu Mola Mlezi wa walimwengu wote.'

11. Na laiti Mwenyezi Mungu angewaharakishia watu kuwaletea adhabu (kutokana na matendo yao), kama wao wanavyoharakishia kupata kheri, hakika wangekwishatimiziwa muda wao (wa kuishi). Lakini tunawaacha wale wasiotaraji kukutana Nasi wakihangaika katika upotevu wao. 12. Na mtu apatapo shida hutuomba (katika hali zote), akiwa kaegemea kwa ubavu wake, au akiwa ameketi au amesimama. Lakini tunapomwondolea

shida yake, huendelea kana kwamba hakuwahi kutuomba tumwondolee shida iliyompata. Ndiyo hivi matendo ya wale wakiukao mipaka wamepambiwa wayaone mazuri mbele ya macho yao.

13. Hakika tumekwisha waangamiza watu waliokuwa kabla yenu walipodhulumu; na waliwajia Mitume wao kwa hoja zilizo wazi, lakini hawakuwa wenye kuamini. Namna hii tunawalipa watu wakosefu.
14. Kisha tukawafanya nyie kuwa warithi wa ardhi baada yao, ili tuone jinsi mtakavyotenda.

15. Na wanaposomewa Aya Zetu zilizo wazi, wale wasiotaraji kukutana Nasi husema: 'Lete Qur'ani isiyokuwa hii, au ibadilishe'. Sema: Haiwezekani kwangu kuibadilisha jinsi nitakavyo mimi. Mimi sifuati ila niliyopewa ufunuzi; hakika mimi naogopa, nikimwasi Mola Wangu Mlezi, adhabu ya siku hiyo kubwa.
16. Sema: lau Mwenyezi Mungu angetaka nisingewasomea hiyo wala nisingewajulisha. Nilikwishakaa nanyi umri mrefu kabla yake. Kwa nini hamfahamu hili?
17. Basi ni nani aliye dhalimu zaidi kuliko yule amzuliaye Mwenyezi Mungu uwongo au akadhibishaye Aya Zake? Hakika wakosefu hawafaulu.

18. Na wanaabudu wasiowadhuru wala kuwanufaisha badala ya Mwenyezi Mungu. Na wanasema: Hawa ndio waombezi wetu kwa Mwenyezi Mungu. Sema: Je, mnamwambia Mwenyezi Mungu asiyoyajua katika mbingu wala katika ardhi? Ametakasika na ametukuka na hao wanaomshirikisha Naye.
19. Watu wote walikuwa umma wa dini moja tu, kisha wakahitalifiana. Na lau si neno lililokwishatangulia kutokana na Mola Wako Mlezi (kuwa malipo yasubiri siku ya Kiyama) bila shaka hukumu ingekwishatolewa baina yao katika hayo wanayokhitalifiana.

20. Na wanasema: Kwa nini hakuteremshiwa ishara kutoka
kwa Mola Wake Mlezi? Sema hakika ajuaye ghaibu ni
Mwenyezi Mungu pekee, basi ngojeni na mimi niko pamoja
nanyi katika kungojea. 21. Na tunapowaonjesha binadamu
neema baada ya shida kuwagusa, huanza kuzipangia njama
ishara zetu. Sema, Mwenyezi Mungu ni mwepesi zaidi
wa kupanga njama. Hakika wajumbe Wetu wanayaandika
mnayoyapanga.

22. Yeye ndiye anayewawezesha ninyi kutembea
katika nchi kavu na baharini. Hata mnapokuwa ndani ya
majahazi na yakawa yanakwenda nao kwa upepo mzuri na
wakaufurahia…, mara upepo mkali ukawazukia, yakawajia
mawimbi kutoka kila upande na wakajikuta wamezingirwa….
hapo humwomba Mwenyezi Mungu kwa kumtakasia
nia (kwamba) ukituokoa na haya kwa hakika tutatakuwa
miongoni mwa wanaoshukuru. 23. Lakini alipowaokoa, mara
wanafanya tena maovu duniani kwa jeuri tu. Enyi watu! Jeuri
yenu itawarudia nyinyi wenyewe tu. Hii ni starehe ya maisha
ya dunia tu, kisha marejeo yenu ni Kwetu, ndipo tuwaambie
mliyokuwa mkiyatenda.

24. Hakika mfano wa maisha ya duniani ni kama mfano wa maji tuliyoyateremsha kutoka mawinguni, kisha yakachanganyika na mimea ya ardhi wanayokula watu na wanyama. Mpaka ardhi ilipokamilisha uzuri wake na ikapambika, na wenyewe wakadhani kuwa wana nguvu zote juu yake…Hapo amri Yetu ikaifikia usiku au mchana , tukaifanya imefyekwa kana kwamba jana haikuwepo. Namna hii tunazipambanua Aya kwa watu wenye kufikiri.

25. Na wito wa Mwenyezi Mungu ni kuelekea Nyumba ya Amani. Na humwongoza amtakaye kwenye njia iliyonyooka.

[26.] Kwa wafanyao wema (malipo yao) ni wema na zaidi. Si giza wala udhalili utazifunika nyuso zao. Hao ndio watu wa Peponi; hao humo wataishi milele [27.] Na wale waliochuma maovu, malipo ya uovu ni mfano wake. Na udhalili utawafunika. Hawatakuwa na wa kuwakinga na Mwenyezi Mungu. Kana kwamba nyuso zao zimefunikwa na vipande cha usiku wenye giza. Hao ndio watu wa motoni hao humo wataishi milele.

[28.] Na siku tutakapowakusanya nyote, kisha tuwaambie wale walioshirikisha: 'Simameni sehemu yenu nyinyi na washirika wenu!' kisha tutawatenganisha. Na hao waliokuwa wakiwashirikisha na Mwenyezi Mungu watasema: 'ninyi hamkuwa mkituabudu sisi'. [29.] Mwenyezi Mungu anatosha kuwa shahidi baina yetu na nyinyi. Hakika sisi tulikuwa hatuna habari na ibada yenu. [30.] Huko kila mtu atajua aliyoyatanguliza, na watarudishwa kwa Mwenyezi Mungu, Mola Wao wa kweli, na uwongo wote waliokuwa wakiubuni utawatoweka.

[31.] Sema: Ni nani anayewaruzuku kutoka mbinguni na ardhini? Au ni nani anayemiliki kusikia na kuona? Na ni nani amtoaye hai kutoka maiti na akamtoa maiti kutoka aliye hai? Na ni nani anayesimamia mambo yote? Watasema, 'ni Mwenyezi Mungu'! Sema, : 'kwa nini hamumtii na kumuenzi basi?' [32.] Basi huyo ndiye Mweyezi Mungu Mlezi Wenu. Ni nini tena baada ya haki isipokuwa upotevu? Vipi tena mnageuzwa (kumwacha Yeye)? [33.] Kama hivyo basi ndivyo Neno la Mola wako lilivyothibiti kuwa kweli dhidi ya wale walioasi, kwamba hawatoamini.

[34.] Sema: Je, miongoni mwa miungu yenu ya upagani yuko anayeanzisha kuumba (kiumbe) kisha akakakakirejesha tena?

Sema: Mwenyezi Mungu tu ndiye anayeanzisha kiumbe kisha
akakirejesha. Iweje mnadanganywa? 35. Sema: Je, hivi yupo
katika miungu yenu ya upagani anayetoa mwongozo kufikia
ukweli? Sema: Mwenyezi Mungu pekee ndiye aongozaye
kwenye ukweli. Je, anayestahiki kufuatwa ni yule aongozaye
kwenye ukweli au ni yule asiyeongoza isipokuwa aongozwe
yeye? Mna nini nyinyi! Mnahukumuje?! 36. Na wengi wao
hawafuati isipokuwa kudhania dhania tu. Lakini dhana haifai
kitu mbele ya ukweli. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa
wanayoyatenda.

37. Na haiwezekani kuwa hii Qur’an imetungwa,
haitoki kwa Mwenyezi Mungu. Isipokuwa inathibitisha
yaliyotangulia na ni ufafanuzi wa Kitabu kisicho shaka
ndani yake, kutoka kwa Mola Mlezi wa viumbe vyote.
38. Je, wanasema ameizusha? Waambie: Hebu leteni Sura moja
mfano wake na mumwite (awasaidie) yeyote mnayeweza
kumwita, asiyekuwa Mwenyezi Mungu, ikiwa nyinyi ni
wakweli. 39. Bali wamekanusha yale ambayo hawakuyaelewa
barabara, hata kabla haujawajia ufafanuzi wake. Kadhalika
walikanusha waliokuwa kabla yao hivyo hivyo. Basi angalia
jinsi ulivyokuwa mwisho wa madhalimu hao.

40. Na miongoni mwao wapo wanaoamni hii Quran,
na miongoni mwao wapo wasio iamini. Na Mola Wako
anawajua sana wafanyao uharibifu. 41. Na kama wakikuambia
wewe ni mwongo, waambie: matendo yangu ni yangu na
yenu ni yenu. Ninyi hamna jukumu kwa niyafanyayo, na
mimi sina jukumu kwa myafanyayo. 42. Na miongoni mwao
wapo (wanaojifanya) wanakusikiliza. Je, wewe unaweza
kuwafanya viziwi wasikie ingawa hawana ufahamu?
43. Na miongoni mwao wapo wanaokutazama. Je, wewe

unaweza kuwaongoza vipofu ingawa hawaoni? 44. Hakika Mwenyezi Mungu hawadhulumu watu chochote, lakini watu wanajidhulumu wenyewe.

45. Na siku atakapowakusanya, itakuwa kana kwamba hawakukaa (makaburini) isipokuwa saa moja tu ya mchana. Watatambuana. Hakika wamehasirika waliokanusha kukutana na Mwenyezi Mungu, wala hawakuwa wenye kuongoka. 46. Ikiwa tutakuonyesha baadhi ya tunayowaahidi au tutakufisha (kabla yake), kwa vyovyote vile marejeo yao ni Kwetu tu. Kisha Mwenyezi Mungu ni shahidi wa wanayoyafanya.

47. Na kila umma una Mtume. Alipowafikia Mtume wao walihukumiwa baina yao kwa uadilifu; nao hawakudhulumiwa.

48. Na wanasema: Ni lini ahadi hii (ya Kiyama), ikiwa ninyi mnasema kweli? 49. Sema: Similiki nafsi yangu madhara wala manufaa yeyote, isipokuwa apendavyo Mwenyezi Mungu. Kila umma una muda wake. Unapofikia muda wao hawakawii hata saa moja wala hawatangulii. 50. Sema: Mwaonaje ikiwafikia adhabu yake usiku au mchana. Kitu gani hasa katika adhabu wanachokifanyia haraka hao wahalifu? 51. Je, hatimaye ikishatokea ndiyo mtaiamini? Ebo! Hivi sasa? Na nyie mlikuwa mkiihimiza (ije)? 52. Kisha waliodhulumu wataambiwa: Onjeni adhabu ya kudumu. Kwani mtalipwa tu yale yale mliyokuwa mkiyachuma.

53. Na wanakuuliza: Je, ni kweli hayo? Sema: 'Ndiyo! Naapa kwa Mola Wangu Mlezi hiyo ni kweli tupu! Na nyie hamtaweza kuponyoka. 54. Na lau kama kila mtu/jinni aliyedhulumu anamiliki kila kilichomo duniani, angevitoa vyote kujikombolea. Na watakapoiona adhabu wataficha

majuto; na patahukumiwa baina yao kwa uadilifu; nao hawatadhulumiwa. 55. Ndiyo! Hakika vyote vilivyomo mbinguni na ardhini ni vya Mwenyezi Mungu. Ndiyo! Hakika ahadi ya Mwenyezi Mungu ni kweli, lakini wengi wao hawajui. 56. Yeye ndiye anayefufua na anayefisha, na Kwake mtarudishwa.

57. Enyi watu! Hakika yamewafikia mawaidha kutoka kwa Mola Wenu, na (dawa) ya kuponesha yaliyomo katika nyoyo zenu, na mwongozo na huruma kwa waumini. 58. Sema: Kwa fadhila ya Mwenyezi Mungu na huruma Yake, basi na wafurahie. Hayo ni bora kuliko (utajiri) wanaolimbikiza. 59. Sema: Hivi mnaonaje zile riziki alizowateremshia Mwenyezi Mungu, kisha mkafanya katika hizo nyingine haramu na nyingine halali? Waulize: Je, Mwenyezi Mungu amewaruhusu, au mnamzulia Mwenyezi Mungu uwongo? 60. Wanafikiria nini wale wanaomtungia uwongo Mwenyezi Mungu juu ya siku ya Kiyama? Hakika Mwenyezi Mungu ana fadhila juu ya watu, lakini wengi wao hawashukuru.

61. Na huwi katika jambo lolote lile, na husomi sehemu yeyote ile ya Qur’an, na wala (nyie wanadamu) hamfanyi kitendo chochote kile...isipokuwa Sisi huwa mashahidi juu yenu mnaposhughulika nacho. Na hakifichiki chochote, hata chenye uzito wa chembe, kwa Mola Wako Mlezi, kiwe katika ardhi au mbinguni, wala kidogo kuliko hicho wala kikubwa, isipokuwa kimo katika Kitabu kinachobainisha. 62. Naam! Jueni kuwa vipenzi wa Mwenyezi Mungu hawatakuwa na hofu wala wao hawatahuzuniki. 63. (Hao ni) ambao wameamini na wakawa wanamtii na kumuenzi Mwenyezi Mungu. 64. Wao wana bishara nzuri katika maisha ya dunia na katika Akhera. Hakuna mabadiliko katika maneno ya

Mwenyezi Mungu. Huko ndiko kufuzu kukubwa. [65.] Wala yasikuhuzunishe maneno yao. Hakika enzi na utukufu wote ni wa Mwenyezi Mungu. Yeye ndiye Mwenye kusikia, Mjuzi, [66.] Jueni kuwa ni wa Mwenyezi Mungu wote waliomo mbinguni na waliomo ardhini. Na wale wanaomwomba asiyekuwa Mwenyezi Mungu hawawafuati washirika wowote wa Mungu. Wanachokifuata ni dhana tu, na hawasemi isipokuwa uwongo. [67.] Yeye ndiye aliyewafanyia usiku ili mpate utulivu ndani yake, na mchana wa kuonea (vitu). Hakika katika haya kuna Ishara kwa watu wanaosikia.

[68.] Wanasema: Mwenyezi Mungu amejifanyia mwana! Subhaanah! Ametakasika na hilo! Yeye ni Mkwasi, anayejitosheleza. Vyote vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini ni vyake. Nyinyi hamna uthibitisho wa hayo myasemayo. Je, mnasema juu ya Mwenyezi Mungu msiyoyajua? [69.] Sema: Hakika wale ambao wanamzulia Mwenyezi Mungu uwongo hawatafaulu. [70.] Starehe fupi tu ya duniani. Kisha marejeo yao ni Kwetu, ndipo tutawaonjesha adhabu kali, kwa sababu walikuwa wakikufuru.

[71.] Na wasomee habari ya Nuh (Noah). Pale alipowaambia watu wake: Enyi watu wangu! Ikiwa kukaa kwangu nanyi na kuwakumbusha Ishara za Mwenyezi Mungu ni jambo zito kwenu…. miye namtegemea Mwenyezi Mungu. Basi na nyie pataneni na washirika wenu juu ya mpango wenu. Tena mpango wenu usiwe siri wala wa kutatanisha. Kisha pitisheni hukumu yenu dhidi yangu, wala msinikawize. [72.] Lakini mkijirudia, basi mimi siwaombi ujira wowote. Ujira wangu uko kwa Mwenyezi Mungu pekee. Na nimeamrishwa niwe miongoni mwa Waislamu. [73.] Wakamkana. Tukamwokoa na waliokuwa naye katika jahazi, na tukawafanya wao

ndio waliobakia na tukawazamisha ndani ya maji wale waliozikanusha Ishara Zetu. Basi angalia vipi ulikuwa mwisho wa wale walioonywa (lakini hawakuonyeka).

74. Kisha baada yake tukawatuma Mitume kwa watu wao. Nao wakawajia kwa Ishara zilizo wazi. lakini hawakuwa ni wenye kuamini yale waliyokwisha yakanusha hapo nyuma. Ndio kama hivyo tunapiga muhuri juu ya nyoyo za wapetukao mipaka.

75. Kisha tukampeleka baada ya hao Musa (Moses) na Harun (Aaron) kwa Firaun (Pharaoh) na wapambe wake, kwa ishara Zetu. Wakafanya kiburi, nao walikuwa watu waovu.
76. Ulipowafikia Ukweli kutoka Kwetu walisema: 'huu ni uchawi ulio wazi'. 77. Musa akawaambia: 'Mnasema hivi juu ya Ukweli uliowafikia? Uchawi ni (kama) hivi? Na wachawi hawafanikiwi'! 78. Wakasema: Je, umetujia ili utuachishe yale tuliyowakuta nayo baba zetu, ili ukubwa uwe wenu nyinyi wawili katika nchi hii? Wala sisi kamwe hatuwaamini wawili ninyi!

79. Kisha Firaun (Pharaoh) akasema: 'Hebu nileteeni kila mchawi aliyebobea'. 80. Walipokuja wale wachawi, Musa (Moses) akawaambia: 'Tupeni mnavyotaka kutupa!'.
81. Walipotupa, Musa (Moses) akasema: 'Mliyoleta ni uchawi. Hakika Mwenyezi Mungu ataupoza. Hakika Mwenyezi Mungu hafanikishi vitendo vya watakao uharibifu. 82. Na Mwenyezi Mungu huthibitisha Ukweli kwa maneno yake, hata wachukie waovu!.

83. Basi hawakumwamini Musa, isipokuwa baadhi ya vijana wadogo katika watu wake, kwa sababu ya kumwogopa Firaun (Pharaoh) na wapambe wao, asije akawatia msuko suko. Na hakika Firaun (Pharaoh) alikuwa jeuri katika ardhi,

na kwa hakika yeye alikuwa miongoni mwa waliopetuka mipaka. 84. Na Musa akasema: Enyi watu wangu! Ikiwa nyinyi mmemwamini Mwenyezi Mungu, basi mtegemeeni Yeye, ikiwa nyinyi ni Waislamu. 85. Wakasema: Tunamtegemea Mwenyezi Mungu. Ewe Mola Wetu! Usitufanye wenye kutiwa misukosuko na watu madhalimu. 86. Na utuokoe kwa rehema Yako na watu makafiri.

87. Na tukampa wahyi Musa (Moses) na Harun (Aaron): 'watengezeeni watu wenu majumba Misri. Na mzifanye nyumba zenu ndiyo sehemu za ibada. Na simamisheni Swala. Na wape bishara waumini.

88. Na Musa akasema: Mola Wetu Mlezi! Hakika Wewe umempa Firaun (Pharaoh) na wapambe wake mapambo na mali nyingi katika maisha ya dunia. Mola Wetu Mlezi! Hivyo wanawapoteza watu na njia Yako. Mola Wetu Mlezi! Ziangamize mali zao. Na zifunge nyoyo zao, wasiamini mpaka waione adhabu chungu.

89. Mwenyezi Mungu akasema: 'maombi yenu yamekubaliwa. Basi muwe na msimamo wala msifuate njia ya wale wasiojua'.

90. Na tukawavusha bahari wana wa Israeli, na Firaun (Pharaoh) na askari wake wakawafuatia kwa kiburi na uadui, mpaka alipokaribia kuzama, akasema: 'Sasa ninaamini kwamba hakuna Mola isipokuwa yule wanayemwamini wana wa Israel nami ni miongoni mwa wanaonyenyekea'. 91. Ebo, hivi sasa? Na hali uliasi kabla yake na ukawa miongoni mwa wafanyao uharibifu?. 92. Basi leo tutakuokoa kwa mwili wako ili uwe ishara kwa ajili ya wajao baada yako. Na hakika watu wengi wameghafilika na Ishara Zetu.

93. Na hakika tuliwaandalia wana wa Israeli makazi mema

na tukawaruzuku vitu vizuri. Nao hawakuhitalifiana mpaka ilipowafikia elimu. Hakika Mola Wako Mlezi atahukumu baina yao siku ya Kiyama katika yale waliyokuwa wakihitalifiana.

94 Ukiwa na shaka juu ya tuliyokuteremshia, basi waulize wale wasomao Kitabu kabla yako. Ukweli umekwishakufikia kutoka kwa Mola Wako Mlezi, kwa hivyo usiwe miongoni mwa wafanyao shaka. 95 Na kabisa usiwe miongoni mwa wanaokadhibisha Ishara za Mwenyezi Mungu, usije ukawa miongoni mwa wenye hasara.

96. Hakika wale ambao Neno la Mola Wako Mlezi (la adhabu) limekwishawathibitikia, hawataamini. 97. Hata ikiwajia kila aina ya Ishara, mpaka waione adhabu iumizayo. 98. Kwa nini usiweko mji ulioamini na imani yake ikawafaa, isipokuwa kaumu ya Yunus (Jonah)? Walipoamini tuliwaondolea adhabu ya fedheha katika maisha ya dunia na tukawastarehesha kwa muda.

99. Lau angetaka Mola Wako Mlezi, wangeamini wote waliomo ardhini. Basi hivi wewe utawalazimisha watu wawe Waumini? 100. Na hakuna nafsi inayoweza kuamini isipokuwa kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Na hujaalia shaka kwa wale ambao hawatumii akili.

101. Sema, tazameni yapi yaliyomo mbinguni na yaliyomo ardhini? Dalili na maonyo hayawasaidii watu wasioamini. 102. Basi je, wanangojea lolote jingine isipokuwa mfano wa yaliyotokea siku za watu waliopita kabla yao? Sema, basi ngojeni, mimi pia ni pamoja nanyi katika wanaongojea. 103. Kisha Sisi huwaokoa Mitume Wetu na wale walioamini, Ndio kama hivyo inatustahiki Sisi kuwaokoa Waumini.

104. Sema, Enyi watu! Ikiwa mnayo shaka katika dini

yangu, basi mimi siwaabudu wale mnaowaabudu badala ya Mwenyezi Mungu, lakini ninamwabudu ambaye anawafisha, na nimeamrishwa niwe miongoni mwa wenye kuamini. 105. Na kwamba elekeza uso wako kwenye dini iliyonyooka, wala usiwe miongoni mwa mapagani. 106. Wala usiwaombe wasiokuwa Mwenyezi Mungu ambao hawakunufaishi wala kukudhuru. Ukifanya hivyo, basi wewe utakuwa miongoni mwa madhalimu. 107. Kama Mwenyezi Mungu akikugusisha madhara yeyote, hakuna wa kuyaondoa isipokuwa Yeye tu. Na kama akikutakia kheri, basi hakuna awezaye kurudisha fadhila Yake. Huifikisha kwa amtakaye katika waja Wake, Naye ni Mwingi wa maghufira Mwenye kurehemu.

108. Sema, Enyi watu! Ukweli umekwishawafikia kutoka kwa Mola Wenu. Basi anayeongoka hakika anaongoka kwa faida ya nafsi yake, na anayepotea anapotea kwa hasara ya nafsi yake. Na mimi si wa kuwachunga nyie. 109. Na wewe (Muhammad) ufuate yale yanayofunuliwa kwako, na vumilia mpaka Mwenyezi Mungu ahukumu, na Yeye ndiye bora wa mahakimu.

## 11. Sura Hud

# SURA YA ‘NABII’ HUD

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 *Alif lam raa.*

Hiki ni Kitabu chenye Aya zilizopangwa kwa jumla, kisha zikafafanuliwa kwa upana, kitokacho kwa Mwenye

hekima, Mjuzi wa yote. 2 (Hufunza) Kwamba msimwabudu isipokuwa Mwenyezi Mungu. Hakika mimi nimetumwa kutoka kwake kuja kuwaonya, na kutoa khabari njema. 3 Na tena (kufundisha kuwa) mumwombe msamaha Mola Wenu Mlezi, kisha mtubie Kwake. Atawastarehesha starehe nzuri mpaka muda uliokadiriwa, na atampa kila anayestahiki fadhila, fadhila Yake. Laa kama mtageuka kurudi nyuma, basi mimi nawahofia adhabu ya siku kubwa. 4 Marejeo yenu ni kwa Mwenyezi Mungu, naye ni Mwenye uwezo juu ya kila kitu.

5 Ebo! Ati wanavifunika (vilivyomo katika) vifua vyao, ili wamfiche Mwenyezi Mungu! Ah! Hata wanapojigubika maguo yao, Yeye anajua wanayoyaficha na wanayoyatangaza. Hakika Yeye ni Mjuzi wa yaliyomo vifuani. 6 Na hakuna mnyama yoyote ardhini isipokuwa riziki yake iko kwa Mwenyezi Mungu. Hujua makao yake na mapitio yake. Yote yamo katika Kitabu kinachobainisha.

7. Naye ndiye aliyeumba mbingu na ardhi katika (kipimo cha) siku sita, wakati huo Jaha ya mamlaka yake ilikuwa juu ya maji (chanzo cha viumbe wote). Ili awajaribu ni nani miongoni mwenu mzuri zaidi wa vitendo? Na kama ukiwaambia, 'hakika nyinyi mtafufuliwa baada ya kufa', bila shaka waliomkana Mwenyzi Mungu watasema: 'hiyo haitakuwa kitu kingine ila uchawi ulio wazi'. 8. Na kama tukiwacheleweshea adhabu mpaka muda uliokadiriwa, watasema: 'nini kinachoizuia kuja sasa'? Ah! Siku itakapowajia haitaondolewa kwao; na watazungukwa gubi gubi na yale waliyokuwa wakiyafanyia kejeli.

9. Na pindi tunapomwonjesha mwandamu huruma kutoka kwetu kisha tumwondolee....Lo! Anakuwa mwenye kukata

tamaa na humkana Mwenyezi Mungu hasa! [10.] Na kama tukimwonjesha neema baada ya shida iliyompata, husema: ' Ah, sasa shida zote zimeniondokea'! Hapo hufurahi mno akijigamba! [11.] Isipokuwa wale waliosubiri na wakatenda mema, hao watapata msamaha na ujira mkubwa.

[12.] Huenda wewe (Muhammad) ukahisi uache baadhi ya yale yanayofunuliwa kwako katika Wahyi, na kifua chako kikaona dhiki kwamba wanasema, 'mbona hakushushiwa hazina, au akaja Malaika pamoja naye? Wewe ni muonyaji tu. Mwenyezi Mungu ndiye Mlinzi na Mpangaji wa kila kitu. [13.] Au wanasema ameizua? Sema: basi leteni Sura kumi zilizozuliwa mfano wa hii na mwiteni yeyote mnayeweza kumwita asiyekuwa Mwenyezi Mungu, ikiwa mnasema kweli. [14.] Na wasipowaitikia, basi jueni ya kwamba imeteremshwa kwa ujuzi wa Mwenyezi Mungu, na kwamba hapana Mola isipokuwa Yeye. Je, nyinyi ni Waislamu?

[15.] Wanaotaka maisha ya dunia na anasa zake, tutawalipa kamili humo humo (ujira wa) vitendo vyao na humo hawatapunjwa. [16.] Hao ndio ambao katika Akhera hawatakuwa na kitu isipokuwa moto, (vile) yamekwisha haribika waliyoyafanya duniani na yamepotea bure yale waliyokuwa wakiyatenda.

[17.] Je, hivi mtu aliye na dalili wazi (Quran) itokayo kwa Mola Wake, na akafundishwa na shahidi atokaye Kwake, kama ilivyokuwa kabla yake, Kitabu cha Musa kilichokuwa mwongozo na huruma…. (ni muongo?) Hao wanakiamini. Na atakayekikana miongoni mwa vikundi, moto ndio utakuwa mahali pa ahadi (ya kukutana).Basi usiwe na shaka nayo. Hakika hiyo ni haki itokayo kwa Mola wako. Lakini watu wengi hawaamini.

18. Ni nani anayekosea zaidi kuliko yule amzuliaye
Mwenyezi Mungu uongo. Hao watahudhurishwa mbele
ya Mola Wao Mlezi. Na mashahidi watasema: ‘Hawa
ndio waliomzulia Mola Wao Mlezi uwongo. Basi laana ya
Mwenyezi Mungu iwe juu ya madhalimu. 19. Ambao wanazuia
njia ya Mwenyezi Mungu na wanataka ipotoke na wanaikataa
Akhera. 20. Hao hawataweza kuponyoka katika ardhi na wala
hawana walinzi badala ya Mwenyezi Mungu. Watazidishiwa
adhabu maradufu. Hawakuwa wakiweza kusikia wala
hawakuwa wakiona. 21. Hao ndio ambao wamezitia hasara
nafsi zao, na yamepotea waliyokuwa wakiyazua. 22. Bila
shaka hao ndio wenye hasara zaidi katika Akhera.

23. Hakika wale walioamini na wakafanya matendo mema
na wakamnyenyekea Mola Wao, hao ndio watu wa Peponi,
wao watadumu humo. 24. Mfano wa makundi mawili ni kama
kipofu na kiziwi, na anayeona na anayesikia. Je, hawa wawili
wanaweza kuwa sawa? Je, hampati mawaidha?

25. Hakika tulimtuma Nuh kwa watu wake (awaambie):
Hakika mimi kwenu ni muonyaji abainishaye. 26. Ya kwamba
msiabudu isipokuwa Mwenyezi Mungu. Hakika mimi
nawahofia na adhabu ya Siku iumizayo. 27. Wakasema wakuu
wa wale waliokufuru katika kaumu yake: ‘Hatukuoni wewe
ni chochote ila mtu sawa nasi. Wala hatuoni wamekufuata
isipokuwa wale watu duni kwetu, wasiokomaa kimawazo.
Wala hatuwaoni nyie ni bora kuliko sisi; bali tunawaona
kuwa mu waongo.

28. Akasema: Enyi watu wangu! Mwaonaje ikiwa
ninayo hoja iliyo wazi itokayo kwa Mola Wangu Mlezi, na
amenipa rehema (ya Utume) kutoka Kwake, lakini ikawa
vigumu kwenu kuitambua, Je, tuwalazimishe na hali nyinyi

mnaichukia? [29.] Na enyi watu wangu! Siwaombi mali kwa hili. Mimi Sina ujira ila kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Na mimi sitawafukuza wale (watu wa hali ya chini) walioamini, hakika wao watakutana na Mola Wao Mlezi. Lakini mimi nawaona nyinyi ni watu msiojua (yatakayowafika). [30.] Na enyi watu wangu! Ni nani atakayenisaidia kwa Mwenyezi Mungu nikiwafukuza hawa? Hivi hamfikiri? [31.] Wala sidai kuwa nina hazina za Mwenyezi Mungu; wala kuwa mimi ninajua mambo ya ghaibu; wala sidai kuwa mimi ni Malaika. Wala siwasemi wale ambao yanawadharau macho yenu, kuwa Mwenyezi Mungu hatawapa kheri. Mwenyezi Mungu anayajua yaliyo katika nafsi zao. Hapo bila shaka nitakuwa miongoni mwa madhalimu.

[32.] Wakasema: Ewe Nuh (Noah)! Umehojiana nasi mno kupita kiasi, haya basi tuletee unayotuahidi ukiwa wewe ni miongoni mwa wakweli. [33.] Akasema: 'Hayo Mwenyezi Mungu atawaletea akipenda na wala nyinyi hamuwezi kumshinda'. [34.] Wala nasaha yangu haitawafaa kitu nikitaka kuwapa nasaha, ikiwa Mwenyezi Mungu anataka kuwaacha mpotee. Yeye ndiye Mola Wenu Mlezi; na Kwake mtarejeshwa.

[35.] Au wanasema ameizusha? Sema: ikiwa nimeizua, basi kosa hilo ni juu yangu, na mimi pia sihusiki na makosa yenu myatendayo.

[36.] Ndipo Nuh akaletewa ufunuo kuwa 'hataamini katika watu wako isipokuwa yule ambaye tayari amekwishaamini. Usisikitike kwa waliyokuwa wakiyatenda'. [37.] Na unda jahazi kwa msaada na maelekezo katika ufunuo Wetu, wala usinizungumzie kuhusu wale waliodhulumu, hakika wao watagharikishwa. [38.] Na akawa anaunda jahazi na kila

wakipita wakuu wa kaumu yake wakawa wakimkejeli. Akasema: Ikiwa nyinyi mnatukejeli, hakika nasi tutawakejeli, kama mnavyotukejeli. 39. Mtakujajuwa ni nani itakayemfika adhabu ya kudhalilisha na itakaye mshukia adhabu ya kudumu.

40. Hata ilipokuja amri Yetu na chemchemi za ardhi zikafoka maji, tulimwambia (Nuh) 'Pakia ndani ya jahazi wawili wawili, dume na jike kutoka kila aina, na pia familia yako, isipokuwa wale ambao imekwishawapitia hukumu, pia wachukue wale walioamini' Na hawakuamini pamoja naye isipokuwa wachache tu. 41. Na pandeni humo kwa (kusema) 'Bismillah, kwenda kwake na kusimama kwake'. Hakika Mola Wangu ni Mwingi wa maghufira, Mwenye kurehemu. 42. Ikawa inakwenda nao katika mawimbi (makubwa) kama milima. Na Nuh (Noah) akamwita mwanawe (Kanaan) naye alikuwa mbali: 'Ewe mwanangu! Panda pamoja nasi wala usiwe pamoja na makafiri'. 43. Akasema: 'Nitakimbilia mlimani unilinde na maji'. Nuh akamjibu:: 'Leo hapana wa kulindwa na hukumu ya Mwenyezi Mungu, isipokuwa yule aliyemwonea huruma!' Hapo wimbi likawatenganisha, akawa miongoni mwa waliogharikishwa. 44. Na ikatolewa amri:'Ewe ardhi! meza maji yako na ewe mawingu! Jizuie!. Na maji yakadidimia chini, na hukumu ikawa imepitishwa, na Jahazi likasimama juu ya (mlima ) Judi. Na ikasemwa (na Malaika): 'wapotelee mbali watu waovu'!

45. Na Nuh akamwomba (tena) Mola Wake Mlezi akisema: 'Ewe Mola Wangu Mlezi! Hakika mwanangu ni katika watu wangu, na hakika ahadi Yako ni kweli na Wewe ni hakimu bora wa mahakimu wote'. 46. (Mwenyezi Mungu) akamjibu: 'Ewe Nuh! Yeye si katika watu wako; mwendo

wake si mwema. Usiniombe jambo usilo na ujuzi nalo. Mimi
nakuonya usije ukawa katika wa wajinga'. 47. Nuh akasema:
'Ewe Mola Wangu Mlezi! Hakika mimi ninajikinga Kwako
kukuomba nisilo na ujuzi nalo. Na kama hutanisamehe na
kunionea huruma nitakuwa katika waliohasirika'.

48. Amri ikatolewa: 'Ewe Nuh! Shuka kwa Amani
itokayo Kwetu na baraka nyingi juu yako na juu ya umma
watakaotokana na hawa walio pamoja nawe. Na (kutakuwepo)
mataifa mengine tutakaowapa starehe (kidogo) kisha wapewe
adhabu chungu itokayo Kwetu. 49. Hizo ni habari za ghaibu
tunazokupa ufunuo. Hukuwa ukizijua wewe wala watu wako
kabla ya hii. Basi subiri. Hakika mwisho (mwema) ni wa
wacha Mungu.

50. Na kwa A'ad (tulimpeleka) ndugu yao Hud, akasema:
'Enyi watu wangu! Mwabuduni Mwenyezi Mungu pekee!
Nyinyi hamna Mungu mwingine isipokuwa Yeye tu. Ninyi
si chochote ila wazushi (wa miungu wengine). 51. Enyi watu
wangu! Siwaombi ujira juu ya haya. Ujira wangu si kutoka
kwa yeyote ila Yule aliyeniumba tu. Mbona hamtumii akili
zenu? 52. Enyi watu wangu! Muombeni maghufira Mola
Wenu kisha mtubie Kwake, atawaletea mawingu yenye mvua
tele na atawazidishia nguvu juu ya nguvu zenu mlizonazo.
Basi msigeuke kuwa waovu.

53. Wakasema: 'Ewe Hud! Hujatuletea dalili yoyote. Na
sisi hatuiachi miungu yetu kwa kauli yako tu, nasi kamwe
hatukuamini. 54. Hatuna la kusema isipokuwa (huenda)
baadhi ya miungu yetu imekurushia kitu kibaya. Akasema
Hud:'Hakika mimi ninamshuhudisha Mwenyezi Mungu, na
nyinyi shuhudieni kwamba niko mbali na hao mnaowafanya
washirika wake.... 55. mkamwacha Yeye. Basi nyote ninyi

nifanyieni njama (kuniua), wala msinipe muhula' [56.] Hakika mimi nimemtegemea Mwenyezi Mungu, Mola Wangu Mlezi na Mola Wenu. Hakuna yeyote atembeaye juu ya mgongo wa ardhi isipokuwa Yeye ndiye mwenye kuukamata utosi wake (mwenye mamlaka kamili naye). Hakika Mola Wangu yuko juu ya njia iliyonyooka.

[57.] Wakirudi nyuma, basi mimi nimekwishawafikishia niliyotumwa kwenu. Na Mola Wangu atawaleta watu wengine badala ya nyinyi; wala hamumdhuru kitu. Hakika Mola Wangu ni Mwenye kuhifadhi kila kitu. [58.] Ilipofika amri yetu tulimwokoa Hud na walioamini pamoja naye, kwa rehema itokayo Kwetu na tukawaokoa na adhabu nzito. [59.] Na hao ndio akina Aa'd, walikanusha Ishara za Mola Wao Mlezi na wakawaasi mitume Wake na wakafuata amri ya kila jabari mwenye inadi. [60.] Na wakafuatishiwa laana katika dunia hii na Siku ya Kiyama. Basi tambueni! Hakika Aa'd walimkufuru Mola Wao Mlezi. Ndiyo! Wamepotelea mbali kina A'ad, watu wa Hud, kutoka uso wa dunia.

[61.] Na kwa Thamud (tulimpeleka) ndugu yao Swaleh. Akasema: Enyi watu wangu! Mwabuduni Mwenyezi Mungu! Nyinyi hamna Mungu mwingine isipokuwa Yeye. Yeye ndiye aliyewaumba nyie kutokana na ardhi na akawawezesha muifanye iwe koloni lenu. Basi muuombeni maghufira Mola Wenu kisha mtubie Kwake. Hakika Mola Wangu yuko karibu Mwenye kuitikia. [62.] Wakasema: 'Ewe Swaleh! Ulikuwa ukitarajiwa kuwa na mambo mazuri kwetu kabla ya haya. Hivi unatukataza kuabudu waliyokuwa wakiyaabudu mababa zetu? Kwa kweli sisi tuna shaka na wasiwasi kwa haya unayotuitia'. [63.] Akasema: Enyi watu wangu! Mwaonaje ikiwa nina hoja iliyo wazi itokayo kwa Mola Wangu Mlezi

na akanipa rehema (ya utume) kutoka Kwake, basi ni nani atakayeninusuru kwa Mwenyezi Mungu kama nikimwasi? Ninyi hamtanizidishia isipokuwa hasara tu.

64. Enyi watu wangu! Huyu ngamia wa Mwenyezi Mungu, ni ishara kwenu, basi mwacheni ajilie kwenye ardhi ya Mwenyezi Mungu; wala msimdhuru, isije ikawaangamiza adhabu iliyo karibu. 65. Wakamkata miguu yule ngamia jike. Hapo (Swaleh) akawaambia: ‘Stareheni katika mji wenu kwa siku tatu tu. Hiyo ni ahadi isiyo ya uongo.’. 66. Ilipotolewa hukumu Yetu tulimwokoa Swaleh na walioamini pamoja naye, kwa rehema itokayo Kwetu kutokana na fedheha ya siku hiyo. Hakika Mola Wako ni Mwenye nguvu, Mwenye kushinda. 67. Na mpasuko wa sauti kubwa ukawaangamiza wale waliodhulumu, wakapambaukiwa wamelala kifudifudi (maiti) katika majumba yao. 68. Kana kwamba hawakuwemo humo. Ndiyo! Hakika Thamud walimkufuru Mola Wao Mlezi. Zingatieni! Jinsi Thamud walivyopotelea mbali.

69. Na wajumbe Wetu (Malaika) walimjia Ibrahim (Abraham) na bishara njema. Wakasema: Salaam! Naye akajibu: Salaam! Na hakukaa muda, mara akaleta ndama aliyeokwa. 70. Alipoona mikono hawainyooshi kwenye ile nyama, aliwatilia shaka, na akawahofia. Wakamwambia: Usiogope! Hakika sisi tumetumwa kwa watu wa Lut (Lot). 71. Na mkewe alikuwa kasimama wima, akacheka. Tukampa bishara ya (kumzaa) Is-haq (Isaac) na baada ya Is-haq, na Ayub (Jacob). 72. Akasema: Uwii, Miye?! Nizae? Na mimi ni mkongwe na huyu mume wangu ni mzee? Hakika hili ni jambo la ajabu kabisa! 73. Wakasema: Unastaajabu amri ya Mwenyezi Mungu? Rehema ya Mwenyezi Mungu na baraka

Zake ziko juu yenu watu wa nyumba hii. Hakika Yeye ni Mwenye kusifiwa, Mwenye kutukuzwa.

74. Basi hofu ilipomwondokea Ibrahim na ikawa ile bishara ameipokea, alianza kutusihi (Malaika) juu ya watu wa Lut.
75. Hakika Ibrahim (alikuwa) mpole, mnyenyekevu na mwepesi wa kurejea (kwa Mungu). 76. Ewe Ibrahim (Abraham)! Achana na haya! Hakika hukumu ya Mola Wako imekwishapita, na hakika wao itawafika adhabu isiyoweza kurudishwa.

77. Na pale wajumbe Wetu walipofika kwa Lot, aliwahuzunikia na akaona hana nguvu ya kuwahami. Akasema: 'Hii ni siku ngumu'. 78. Hapo watu Lut wakamjia mbio mbio. Na kabla ya hapo walikuwa wakifanya maovu (hayo ya kulawiti). Lut akawaambia: 'Enyi watu wangu! Hawa binti zangu wao ni wasafi zaidi kwenu! Mcheni Mwenyezi Mungu. Wala msinifedheheshe mbele ya wageni wangu. Hivi hakuna hata mtu mmoja mnyoofu miongoni mwenu? 79. Wakasema: 'Si umekwishajua hatuna haja na binti zako? Wee unajua fika sisi tunataka nini'!

80. Akasema: 'Laiti ningelikuwa na nguvu juu yenu au nikamtegemea mtu mwenye nguvu'! 81. (Wale wageni) wakasema: Ewe Lut! Sisi ni wajumbe wa Mola Wako Mlezi. (Hawa) hawawezi kukudhuru. Wewe ondoka pamoja na familia yako huku bado usiku ungalipo, wala yeyote katika nyinyi asigeuke kutazama nyuma. Isipokuwa mkeo. Yeye yatamfika yatakayowafika hao. Ahadi yao ni kesho asubuhi. Si asubuhi iko karibu? 82 Basi ilipofika hukumu Yetu, tuliigeuza (miji yao) juu kukawa chini. Na tukawateremshia mvua ya mawe ya udongo mkavu uliookwa motoni, yaliyotawanyika tabaka baada ya tabaka. 83 Kila jiwe lilitiwa alama na Mola

Wako Mlezi (ya jina la mlengwa). Na nchi hizo za madhalimu
hao haziko mbali (na Makka).
84. Na kwa Watu wa Madyan (tulimpeleka) ndugu yao
Shuaib. Akasema: Enyi watu wangu! Mwabuduni Mwenyezi
Mungu, hamna Mungu mwingine zaidi Yake. Wala
msipunguze kipimo na mizani. Mimi nawatakia nyie kheri
tu lakini nawahofia na adhabu ya siku ambayo itawazunguka
ninyi nyote. 85. Enyi watu wangu! Timizeni kipimo na mizani
kwa uadilifu na msidokoe vitu vya watu kwa (udanganyifu);
wala msieneze uharibifu katika ardhi mkaleta vurugu.
86. Alivyowabakizia Mwenyezi Mungu ndiyo bora kwenu,
ikiwa nyinyi ni waumini; wala mimi sio mtu wa kuwachunga.
87. Wakasema: Ewe Shuaib! Ni hizi Swala zako ndizo
zinakuamuru sisi tuache walivyokuwa wakiviabudu mababu
zetu au kufanya tupendavyo katika mali zetu? Hakika wewe
ndiwe mpole, mwongofu!
88. Akasema: Enyi watu wangu! Mwaonaje ikiwa nina dalili
iliyo wazi itokayo kwa Mola Wangu Mlezi na ameniruzuku
riziki njema itokayo Kwake? Wala sitaki kutofautiana nanyi
(halafu) nifanye yale yale ninayowakataza. Mimi sitaki ila
kutengeneza (hali yenu) kiasi cha uwezo wangu. Na mafanikio
yangu (katika hili) hayatapatikana ila kwa kuwezeshwa na
Mwenyezi Mungu pekee; Kwake Yeye ninategemea na
Kwake naelekea. 89. Na enyi watu wangu! Kupinga kwangu
vitendo vyenu kusiwe sababu ya nyie kufanya maovu, yasije
yakawafika mfano wa yaliyowafika watu wa Nuh (Noah)
au watu wa Hud au watu wa Swaleh. Na watu Lot hawako
mbali sana nanyi! 90. Na muombeni maghufira Mola Wenu
kisha mtubie Kwake. Hakika Mola Wangu Mlezi ni Mwenye
huruma nyingi, Mwenye upendo.

91. Wakasema: Ewe Shuaib! Mengi ya hayo unayoyasema hatuyafahamu! Nasi twakuona wewe mnyonge kwetu. Na laiti si jamaa zako, bila shaka tungekupiga mawe. Wala wewe huna heshima yeyote kwetu. 92. Akasema: Enyi watu wangu! Kwani jamaa zangu wana heshima zaidi kwenu kuliko Mwenyezi Mungu? Na Yeye mmemuweka nyuma ya migongo yenu? Hakika Mola Wangu ni Mwenye kuyazunguka yote mnayoyatenda. 93. Enyi watu wangu! Fanyeni muwezavyo, na mimi ninafanya (wajibu wangu). Karibuni mtajua ni nani itakayemfika adhabu itakayomfedhehesha na nani aliye mwongo. Na ngojeni nami ninangoja pamoja nanyi.

94. Ilipofika hukumu Yetu tulimwokoa Shuaib na walioamini pamoja naye, kwa rehema itokayo Kwetu. Na mlipuko wa sauti kubwa ukawaangamiza wale waliotenda mabaya. Kulipopambazuka, walikuwa wamelala kifudifudi katika majumba yao (wamekufa). 95. Kana kwamba hawakuwemo humo. Ndiyo! (watu wa) Madyan wamepotelea mbali; kama walivyopotelea mbali (watu wa) Thamud.

96. Na hakika tulimtuma Musa (Moses) pamoja na Ishara Zetu na madaraka ya wazi, 97. Kwa Firaun (Pharaoh) na machifu wake, lakini wao walifuata amri ya Firaun, na amri ya Firaun haikuwa ya mwongozo mzuri. 98. Siku ya Kiyama atawatangulia watu wake na atawaingiza motoni. Ni ubaya ulioje wa mahali wanapoongozwa kuingia! 99. Na wamefuatishiwa laana katika (dunia ) hii na siku ya Kiyama. Ni kibaya mno watakachopewa.

100. Hizo ni habari za miji tunazokusimulia. Mingine bado ipo na mingine imetokomea mbali. 101. Nasi hatukuwadhulumu, lakini wao wamejidhulumu wenyewe. Na miungu yao waliyokuwa wakiiabudu badala ya Mwenyezi

Mungu, haikuwafaa kitu ilipofika hukumu ya Mola Wako Mlezi, na haikuwazidishia isipokuwa maangamizi.

102 Na kama hivyo, ndivyo inavyokuwa Mola wako anapoitia nguvuni miji inapokuwa imefanya makosa. Hakika adhabu inakuwa chungu na kali. 103 Hakika katika visa hivi kuna mafundisho kwa yule anayeogopa adhabu ya Akhera. Hiyo ndiyo siku ambayo watu watakusanywa na hiyo ndiyo siku ya kutolewa ushahidi. 104 Na hatutaicheleweshа isipokuwa tu kwa muda uliokadiriwa. 105 Siku itakapofika, nafsi yoyote haitazungumza ila kwa kwa idhini Yake. Miongoni mwao (waliokusanywa) kutakuwa na waovu na wengine ni wema.

106. Ama wale waovu watakuwa motoni, humo wataambulia kukoroma na kulia, 107. Watadumu humo muda wa kudumu mbingu na ardhi, isipokuwa apendavyo Mola Wako. Hakika Mola Wako hufanya atakavyo. 108. Ama wale wema watakuwa Peponi watadumu humo muda wa kudumu mbingu na ardhi, isipokuwa apendavyo Mola Wako. Ni kipawa kisicho na ukomo. 109. Usiwe na shaka yeyote juu ya wanavyoviabudu hawa: wanaabudu vile vile walivyokuwa wakiviabudu babu zao zamani. Na hakika sisi tutawatimizia fungu lao bila kupunguzwa.

110. Na hakika tulimpa Musa (Moses) Kitabu, zikazuka khitilafu ndani yake. Na lau kama si neno lililokwisha tangulia kutoka kwa Mola Wako Mlezi, bila shaka ingekwisha pitishwa hukumu baina yao. Na hakika wao wamo katika shaka inayowahangaisha. 111. Na kwa uhakika kabisa, Mola Wako Mlezi atamlipa kila mmoja wao malipo kamili ya vitendo vyao. Hakika Yeye ana habari za wanayoyatenda.

112. Basi simama sawa sawa kama ulivyoamrishwa wewe

na yule anayeelekea (kwa Mwenyezi Mungu) pamoja nawe wala msikiuke mipaka. Hakika Yeye anayaona mnayoyafanya. 113. Wala msiwategemee wafanyao maovu, usije moto ukawagusa. Na nyinyi hamna walinzi asiyekuwa Mwenyezi Mungu wala hamtasaidiwa. 114. Na simamisha Swala katika sehemu mbili za mchana na nyakati za usiku zilizo karibu na mchana. Hakika mema huondoa maovu. Huu ni ukumbusho kwa wanaokumbuka. 115. Na subiri, kwani hakika Mwenyezi Mungu hapotezi ujira wa wanaofanya mazuri.

116. Basi mbona hawakuwamo katika watu wa karne kabla yenu wenye busara, wakakataza uovu katika ardhi, isipokuakuwa wachache tu kati yao tuliowaokoa? Na wale madhalimu wakafuata starehe zao wakawa wakosefu. 117. Na hakuwa Mola Wako wa kuangamiza miji kwa dhulma na hali watu wake ni watenda mema.

118. Na lau Mola Wako Mlezi angetaka, angewafanya watu wote kuwa taifa moja. Lakini wataendelea kutofautiana. 119. Isipokuwa wale ambao Mola Wako amewaonea huruma. Na kwa hiyo (huruma) ndiyo Mwenyezi Mungu amewaumba. Na litatimia neno la Mola Wako: ‘kwa hakika nitaijaza Jahannam majini na watu kwa pamoja’.

120. Na yote haya tunayokusimulia katika habari za mitume ni kwa kuupa nguvu moyo wako. Na katika (simulizi) hizi umekujia ukweli na mawaidha na ukumbusho kwa wenye kuamini. 121. Na waambie wale wasioamini: Fanyeni muwezavyo, nasi (pia) tunafanya (wajibu wetu). 122. Na ngojeni, hakika sisi tunangoja. 123. Na ni vya Mwenyezi Mungu vyote vilivyofichikana katika ardhi na mbingu. Na mambo yote yatarejeshwa Kwake. Basi mwabudu Yeye na

umtegemee Yeye pekee. Na Mola Wako Mlezi si Mwenye kughafilika na mnayoyafanya.

12. Sura Yusuf

## SURA YA 'NABII' YUSUF/JOSEPH

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 *Alif lam ra.*

Hizo ni Aya za Kitabu kinachobainisha wazi. 2 Hakika Sisi
Tumeiteremsha Qur'an kwa lugha ya kiarabu ili mpate
kutambua. 3 Sisi tunakusimulia visa vizuri sana kwa yale
tunayokufunulia katika hii Qur'an. Ingawaje wewe kabla ya
hii Qur'an ulikuwa miongoni mwa wale wasioelimika.

4 Kumbuka wakati Yusuf (Joseph) alipomwambia baba
yake (Yakobo): Ewe baba yangu! Mimi nimeota ndoto kuwa
nyota kumi na moja, jua na mwezi vinanisujudia mimi.
5 Akasema: mwanagu! Usiwasimulie ndugu zako ndoto yako
hii, wasije wakakufanyia njama. Hakika Shetani ni adui aliye
dhahiri kwa mtu. 6 Na kadhalika Mola Wako Mlezi atakuteua
na atakufundisha tafsiri ya mambo, na atatimiza neema
Yake juu yako na juu ya ukoo wa Ayyub (Yakobo); kama
alivyowatimizia hapo zamani baba zako Ibrahim (Abraham)
na Isaac. Hakika Mola Wako ni Mjuzi, Mwenye hekima.

7. Kwa hakika katika Yusuf na ndugu zake kuna ishara
kwa wanaotafuta ukweli. 8. Pale waliposema: 'Inakuaje
Yusuf na nduguye wanapendwa zaidi na baba yetu kuliko
sisi na hali sisi ni kundi imara. Hakika baba yetu yumo

katika upotevu dhahiri’. [9.] Mwueni Yusuf au mtupeni kwenye nchi isiyojulikana, hivyo kwamba upendo wa baba yenu uwe kwenu pekee. Na baada ya hapo muwe watu wema. [10.] Akasema msemaji wao: msimwue Yusuf . Lakini mtumbukizeni kisimani chini kabisa, ataokotwa na baadhi ya wasafiri. Endapo mnataka kufanya.

[11.] Wakamwambia (baba yao): baba! Mbona wewe hutuamini juu ya Yusuf na hali sisi kwa dhati ni wenye kumtakia mema? [12.] Mwache aje nasi kesho, afurahi na acheze, na sisi tutamwangalia. [13.] (Ayyub, baba) Akasema: ‘Kwa kweli nitajihisi upweke mkienda naye na (pia) nahofia asije akaliwa na mbwa mwitu na nyie mkiwa mmemsahau’. [14.] Wakasema: Ikiwa mbwa mwitu atamla, nasi ni kundi kubwa imara, si bora tufe sisi kwanza!

[15.] Basi walipoondoka naye na wote wakawa wamekubaliana wamtumbukize chini katika kisima, tulimpa (Yusuf) wahyi (kwamba) bila shaka (siku moja) utakuja wakumbusha jambo lao hili na hali wao hawakutambui. [16.] Hatimaye wakamjia baba yao usiku, wakilia. [17.] Wakasema: ‘Ewe baba yetu! Sisi tulikwenda kushindana mbio na tukamwacha Yusuf na vitu vyetu, akaliwa na mbwa mwitu. Lakini wewe hutatuamini, ijapokuwa tunasema kweli. [18.] Wakawa wameipaka kanzu yake damu ya uongo. (Baba akasema) ‘Bali nafsi zenu zimewashawishi kutenda jambo fulani. Lakini subira ni njema. Na Mwenyezi Mungu ndiye wa kuombwa msaada kwa haya mnayoyasimulia’.

[19.] Ukaja msafara. Wakamtuma mteka maji wao. Akatumbukiza ndoo yake, akapiga keleke: ‘furahini! Furahini! Huyu hapa mtoto wa kiume! Wakamficha awe bidhaa. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa wanayoyafanya.

[20] (Hatimaye) Wakamwuza kwa thamani duni, vipesa kidogo vya kuhisabiwa. Wala hawakuwa na haja naye.

[21] Na yule aliyemnunua kutoka Misri alimwambia mkewe: Mtayarishie mahali pazuri pa kukaa, huenda akatufaa au tukamfaya mtoto wetu. Na kwa namna hiyo ndivyo tulivyomweka Yusuf katika nchi hiyo, ili tumfundishe jinsi ya kufasiri hekaya na matukio. Na Mwenyezi Mungu ndiye mshindi katika jambo lake, lakini watu wengi hawajui. [22] Na alipofikia utu uzima, tulimpa madaraka na elimu. Na hivyo ndivyo tunavyowalipa watendao mema.

[23] Mama mwenye nyumba aliyokuwemo (Zulekha), akamtongoza (Yusuf) bila yeye kutaka. Akafunga milango kisha akamwambia: 'hebu njoo!' Akamjibu: 'audhubillah!- Najikinga kwa Mwenyezi Mungu'. Kwa kweli yeye bosi wangu (mumeo) amenitunza vizuri. Hakika wafanyao ubaya hawawezi kufaulu. [24] Kwa hakika yule (mama wa nyumba) alimkusudia Yusuf kwa matamanio, na yeye pia angemtamani, kama asingeona ishara ya Mola Wake Mlezi. Basi hivyo ndivyo ilivyokuwa, ili tumwepushie uovu na uchafu. Hakika yeye ni katika waja Wetu waliotakaswa.

[25] Wote wawili wakakimbilia mlangoni na yule mwanamke akairarua kanzu yake (Yusuf) kwa nyuma. Pale mlangoni wakakutana na mumewe. (Mama mwenye nyumba) akasema: 'Nini malipo (yafaayo) kwa mwenye kutaka kumfanyia maovu mkeo, isipokuwa kufungwa gerezani au kupewa adhabu chungu?'. [26] Akasema (Yusuf): 'Yeye ndiye aliyenitongoza bila ya mimi kumtaka. Na mtu aliyeona hayo, aliyekuwa katika jamaa za mke (akasema): 'ikiwa kanzu yake imechanwa mbele, basi (mama mwenye nyumba) amesema kweli, na yeye (Yusuf) ni katika waongo.

27. Na ikiwa kanzu yake imechanwa nyuma basi mwanamke
ni mwongo na yeye (Yusuf) ni katika wakweli. 28. Basi
mume alipoona kanzu imechanwa nyuma, akasema: Hii ni
katika hila zenu (nyie wanawake). Kweli hila zenu ni kubwa.
29. Yusuf! Wee achana nayo haya. Na wewe mwanamke omba
msamaha kwa dhambi zako, hakika wewe ni miongoni mwa
wakosaji.

30. Wanawake wa mjini wakakawa wananong'onezana: 'Ati
mke wa (mheshimiwa) Aziz anamtongoza mtumishi wake,
naye wala hamtaki! Amelewa kwa mahaba yake! Sisi kweli
twamuona kwa dhahiri ametetereka mno!'. 31. Aliposikia
kusengenya kwao, aliwaita na akawawekea matakia ya
kukalia, na akampa kila mmoja wao kisu. Akamwambia
Yusuf: 'Jitokeze mbele yao! Walipomwona wakastaajabu
kuwa kitu adhimu kabisa, na (kwa mshangao) wakajikata
mikono (vidole) vyao, wakitahamaki: 'Hasha lillahi! Huyu
si mwanadamu! Huyu si mwingine bali Malaika mtukufu!
32. Akawaambia: ehee, huyu ndiye mliyekuwa mkinilaumu
juu yake. Na kweli nilimtongoza bila yeye kuridhia,
akakataa. Na asipofanya ninayomwamrisha basi hapana
shaka atafungwa gerezani na atakuwa miongoni mwa watu
duni. 33. Yusuf akajisemea: Ewe Mola Wangu Mlezi! Jela
ni bora zaidi kwangu kuliko haya wanayonitaka nifanye.
Na kama hutaniondolea vitimbi vyao nitawaitika na
nitakuwa miongoni mwa wajinga. 34. Basi Mola Wake Mlezi
akamwitika na akamuondoshea vitimbi vyao; hakika Yeye ni
Msikizi, Mjuzi.

35. Kisha ikawadhihirikia baada ya kuona ishara ya kuwa
(ni bora) wamfunge kwa muda. 36. Wakaingia gerezani
pamoja naye vijana wawili. Mmoja wao akasema: Hakika

mimi nimejiona (katika ndoto) nakamua mvinyo. Mwingine akasema: mimi nimejiona nimebeba mkate juu ya kichwa changu na ndege wanaudonoa wakiula. Hebu tuambie tafsiri yake; kwani sisi tunakuona wewe ni katika watu wema.

37. (Yusuf) akawaambia:: Hata kabla ya nyie kuletewa chakula chenu, mimi nitaweza kuwaambia aina ya chakula hicho. Haya ni katika aliyonifundisha Mola Wangu Mlezi. Kwa vile mimi nimeachana na dini ya watu wasiomwamini Mwenyezi Mungu na wakawa wanakanusha Akhera.
38. Na nikafuata dini ya baba zangu Ibrahim (Abraham) na Is-haq (Isaac) na Ayyub (Yakobo). Sisi kamwe hatushirikishi chochote na Mwenyezi Mungu. Hiyo ni katika neema ya Mwenyezi Mungu juu yetu na juu ya watu. Lakini watu wengi hawashukuru.
39. Enyi wafungwa wenzangu! Je, miungu wengi wanaotofautiana ni bora au (bora) ni Mwenyezi Mungu mmoja Mwenye nguvu zisizoshindika?
40. Kinyume chake, nyie hamuabudu chochote isipokuwa majina tu mliyoyapanga wenyewe na baba zenu. Mwenyezi Mungu hakuyateremsha uthibitisho wowote juu yake. Hukumu si ya yeyote isipokuwa ya Mwenyezi Mungu tu. Ameamrisha msimwabudu yoyote isipokuwa Yeye tu. Hiyo ndiyo dini iliyonyooka, lakini watu wengi hawajui.

41. Enyi wafungwa wenzangui! Ama mmoja wenu, yeye atamnywesha bosi wake mvinyo. Na ama yule mwingine yeye atasulubiwa, kisha ndege watakula kutoka kwenye kichwa chake. Uamuzi wa mahakama juu ya jambo hili mlilokuwa mkiuliza, umekwishapitishwa.
42. Kisha akamwambia yule aliyetabiri kuwa ataokoka katika wawili wale: 'basi unitaje kwa bosi wako!'. Lakini shetani akamsahaulisha kumtaja

kwa bosi wake, na Yusuf akaendelea kukaa gerezani miaka kadhaa mingine.

43. Kisha (Siku moja) mfalme akasema; 'Mimi nimeota kuwa ng'ombe saba walionona wanaliwa na ng'ombe saba waliokonda; na mashuke saba mabichi ya mimea, na mengine makavu.... Enyi machifu wangu! Niambieni maana ya ndoto yangu, ikiwa nyinyi mnaweza kutabiri ndoto.
44. Wakasema: 'Ni ndoto tu zilizoparaganyika. Sisi si wajuzi wa kutabiri ndoto'. 45. Yule mfungwa aliyeachiwa katika wale wawili akakumbuka baada ya kupita muda, akasema: 'Mimi nitawaambia tafsiri yake, basi nileteeni….

46. Yusuf ! Ewe mkweli! Tuelezee nini maana ya ng'ombe saba wanene kuliwa na ng'ombe saba waliokonda na mashuke saba mabichi ya mimea na mengine yaliyokauka, ili nirejee kwa watu wapate kujua'. 47. Akasema: 'Mtalima miaka saba mfululizo. Mtakachovuna kiacheni katika mashuke yake, isipokuwa kidogo tu mtakachokula'. 48. 'Kisha itakuja baadaye miaka saba ya ukame imalize mazao yote mliyojiwekea, isipokuwa kidogo mtakachokuwa mmekihifadhi'. 49. Kisha baada ya hapo utakuja mwaka ambao watu watapata mvua nyingi na watakamua (mvinyo na mafuta).

50. Mfalme akasema: 'Nileteeni mtu huyo! Mjumbe alipomjia Yusuf alimwambia: 'Rejea kwa bosi wako na umwulize habari ya wale wanawake waliojikata vidole. Hakika Mola Wangu Mlezi anajua vizuri hila zao'.
51. (Mfalme) akawauliza: 'Mlikuwa na jambo gani nyinyi mlipomtongoza Yusuf naye hataki'? Wakasema: 'Mungu atulinde! Sisi hatukujua ubaya wowote kutoka kwake'. Hapo mke wa (mheshimiwa) Aziz akasema: 'Sasa haki imedhihiri!

Mimi ndiye niliyemtongoza dhidi ya matakwa ya nafsi yake, na hakika yeye ni katika wakweli.

52. Hayo ni apate kujua kuwa mimi sikumfanyia khiyana alipokuwa hayupo. Na kwamba Mwenyezi Mungu haziongozi hila za mahaini. 53. Na mimi sijitoi katika lawama. Kwa sababu nafsi ndiyo iamrishayo mno uovu, isipokuwa ile ambayo Mola Wangu Mlezi ameionea huruma. Hakika Mola Wangu Mlezi ni Mwingi wa maghufira, Mwingi wa huruma.

54. Ndipo mfalme akasema: ‘Mleteni awe msaidizi wangu muhtasi’. Basi alipozungumza naye alimwambia: ‘Hakika wewe leo kwetu ni mwenye heshima, mwenye kuaminika’. 55. Akasema (Yusuf): Nifanye mweka hazina za nchi. Nitazihifadhi, vile najua umuhimu wake. 56. Na hivyo ndivyo tulivyompa cheo Yusuf katika nchi hiyo; akae humo popote apendapo. Tunamfikishia rehema Zetu tumtakaye, wala hatupotezi ujira wa wafanyao mazuri. 57. Na ujira wa Akhera ni bora kwa wale walioamini na wakamcha Mungu.

58. Wakaja ndugu zake Yusuf wakaingia kwake. Yeye akawajua lakini wao hawakumjua. 59. Alipowakamilishia mahitaji yao aliwaambia: ‘Nileteeni ndugu yenu kwa baba yenu. Je hamuoni kuwa mimi ninatimiza kipimo na kwamba mimi ni bora ya wakaribishao?’ 60. Msiponiletea basi hampati kipimo chochote kwangu wala msinisogelee. 61. Wakasema: ‘Tutamrai baba yake, na hakika sisi tutafanya’.

62. Yusuf akawaambia watumishi wake: Tieni bidhaa zao (walizozileta kubadilishana) katika mizigo yao, wakazione tu baada ya kurudi kwa jamaa zao, ili warejee tena. 63. Basi waliporudi kwa baba yao, walisema: Ewe baba yetu! Tumenyimwa kupimiwa chakula zaidi, shuruti umpeleke ndugu yetu pamoja nasi ili tupate kupimiwa na kwa hakika

sisi tutamlinda. 64. (Ayyub Akasema): Je niwaamini kwa huyu, kama nilivyowaamini kwa nduguye zamani? Lakini Mwenyezi Mungu ndiye bora wa kulinda, na ndiye mwenye huruma nyingi zaidi kuliko wote wale wenye huruma.

65. Walipofungua mizigo yao wakakuta wamerudishiwa bidhaa zao. (Wakasema): Ewe baba yetu! Tutake nini zaidi! Hizi bidhaa zetu tumerudishiwa. Tutaleta chakula zaidi kwa ajili ya jamaa zetu na tutamlinda ndugu yetu na tutaongeza shehena ya ngamia. Hiki ni kipimo kidogo.
66. Akasema: Sitamwacha aje nanyi mpaka muape kwa Mwenyezi Mungu kwamba lazima mtamrudisha kwangu, ila ikiwa nyie wenyewe mmezungukwa. Basi walipompa ahadi yao, alisema: Mwenyezi Mungu ndiye mtegemewa kwa tuyasemayo.

67. Akasema: Enyi wanangu! Msiingie kupitia mlango mmoja, bali ingieni kwa milango mbalimbali. Wala mimi siwassaidii kwa chochote mbele ya Mwenyezi Mungu; hukumu haiko ila kwa Mwenyezi Mungu tu, juu yake Yeye naweka mategemeo yangu na juu yake Yeye wategemee wanaotegemea. 68. Walipoingia kama alivyowaamrisha baba yao, haikuwafaa kitu kwa Mwenyezi Mungu; isipokuwa ni haja tu iliyo katika nafsi ya Ayyub aliyoitimiza. Na hakika yeye ana elimu kwa tulivyomfundisha, lakini watu wengi hawajui.

69. Walipoingia kwa Yusuf alimkumbatia ndugu yake (Benjamin) akamwambia, ‘mimi ni nduguyo! Usihuzunike kwa yale waliyoyafanya’. 70. Alipokwisha watengenezea mahitaji yao akaweka kikombe cha kunywea katika mzigo wa ndugu yake. Kisha mnadi akanadi: ‘Enyi watu wa msafara! nyinyi ni wezi’. 71. Wakawauliza huku wamewaelekea:

'kwani mmepoteza nini? 72. Wakasema: 'Tumepoteza kopo la mfalme na atakayelileta atapata shehena nzima ya ngamia na mimi ni mdhamini'. 73. Wakasema: 'Wallahi mnajua vyema kwamba sisi hatukuja kufanya ubaya katika nchi hii, wala sisi si wezi!' 74. (Wamisri) Wakasema: 'Basi malipo yake yawe nini, ikiwa nyie ni waongo?' 75. Wakasema: 'Malipo yake ni yule ambaye kopo hilo litakutwa katika mzigo wake, huyo ndiye atakuwa malipo yake. Hivi ndivyo tunavyowaadhibu wahalifu'' 76. Basi akaanza na mizigo yao kabla ya mzigo wa ndugu yake; kisha akakitoa katika mzigo wa ndugu yake. Hivyo ndivyo tulivyompa ujanja Yusuf; asingeweza kumchukua ndugu yake katika himaya ya mfalme, isipokuwa kwa mapenzi ya Mwenyezi Mungu. Tunawapandisha vyeo tuwatakao. Na juu ya kila mwenye elimu,Yeye ni Mjuzi zaidi.

77. Wakasema: 'Kama ameiba, basi ndugu yake pia aliiba hapo zamani! Lakini Yusuf aliyaweka siri moyoni mwake wala hakuwaonesha; akasema (moyoni): 'Nyinyi ndiyo mko katika hali mbaya zaidi; na Mwenyezi Mungu anajua zaidi ukweli wa mnayoyaelezea'. 78. Wakasema: Ewe mheshimiwa! Huyu anaye baba mzee sana. Kwa hiyo mchukue mmoja wetu badala yake. Hakika sisi tunakuona wewe ni katika watu wema. 79. Akasema: Mwenyezi Mungu apishie mbali! Hatuwezi kumchukua ila yule tuliyekuta mali yetu iko kwake. Kufanya hivyo tutakuwa tumefanya makossa.

80. Walipokata tamaa naye walikwenda kando kunong'ona. Akasema mkubwa wao: Je, hamjui kuwa baba yenu amechukua nanyi ahadi ya kiapo kwa jina la Mwenyezi Mungu? Na kwamba hapo zamani mlizembea wajibu wenu katika (kumlinda) Yusuf ? Mimi kamwe sitaondoka nchi hii mpaka baba yangu aniruhusu au Mwenyezi Mungu

anihukumie; naye ni bora wa mahakimu.
81. Rudini kwa baba yenu, na mwambieni: Ewe baba yetu! Mwanao ameiba, na hatushuhudii isipokuwa kwa yale tu tuyajuayo (kwa kuona), wala sisi hatuwezi kufanya uchunguzi kwa yale tusiyoyaona.
82. Hebu waulize watu wa mji tuliokuwako na msafara tuliokuja nao. Na sisi kwa kweli tunasema kweli.

83. Akasema: Hapana, nyie mmepanga jambo tu! Lakini subira ni njema kwangu. Huenda Mwenyezi Mungu akaniletea wote pamoja. Hakika Yeye ni Mjuzi, Mwenye hekima.
84. Na akajitenga nao, na akasema: Ah, Masikini Yusuf! Na macho yake yakawa meupe kwa huzuni aliyokuwa akiificha.
85. (Wakamwambia) Wallahi huachi kumkumbuka Yusuf wewe mpaka uwe mgonjwa mahututi au mpaka ufariki dunia!
86. Akasema: miye namshitakia Mwenyezi Mungu majonzi yangu na huzuni yangu, na ninajua kwa Mwenyezi Mungu mambo msiyoyajua.
87. Enyi wanangu! Nendeni mkamtafute Yusuf na nduguye wala msikate tamaaa na faraja ya Mwenyezi Mungu. Hakika hawakati tamaa na faraja ya Mwenyezi Mungu isipokuwa watu makafiri.

88. Basi walipoingia kwa Yusuf walisema: Ewe mheshimiwa! Kwa kweli shida na dhiki imetubana sisi na jamaa zetu na tumekuja na mali kidogo. Tafadhali utupimie kipimo kamili na ifanye kama unatupa sadaka; hakika Mwenyezi Mungu huwalipa wanaotoa sadaka.
89. Akasema: Je, mnajua mlivyomtendea Yusuf na ndugu yake, na nyie mkiwa hamjitambui mnachokifanya?
90. Wakasema: Hivi wewe ni Yusuf? Akasema: Ndiyo, mimi ni Yusuf na huyu hapa ni ndugu yangu! Mwenyezi Mungu ametuneemesha. Hakika mwenye kumcha Mungu na akasubiri, Mwenyezi Mungu haupotezi ujira wa wafanyao mazuri.

91. Wakasema: Wallah! Mwenyezi Mungu amekupendelea
wewe juu yetu sisi na sisi tulikuwa tumefanya hatia.
92. (Akawaambia) Leo hamtakaripiwa wala kulaumiwa.
Mwenyezi Mungu atawasamehe, naye ni Mwingi wa huruma
kuliko wote wanaohurumia wengine. 93. Nendeni na kanzu
yangu hii na muirushe usoni mwa baba yangu atarudi kuwa
mwenye kuona, na mje nao jamaa zenu wote wa nyumbani.

94. Na ulipoondoka msafara, baba yao alisema: Hakika
mimi ninasikia harufu ya Yusuf , lau kama hamtanipuuza
(kuwa ni uzee huo). 95. Wakasema: Wallah wewe bado
uko na akili zako zile zile za kuchanganyikiwa!. 96. Pindi
alipowasili yule mtu wa kufikisha zile habari njema, aliirusha
ile kanzu usoni pake, na (Ayub) akarejea kuona. Akasema:
Je, sikuwaambia kuwa mimi ninajua kutoka kwa Mwenyezi
Mungu yale msiyoyajua nyinyi? 97. Wakasema: ‘Ewe baba
yetu! Tuombee maghufira kwa dhambi zetu, hakika sisi
tulikuwa ni wenye hatia’. 98. Akasema: Nitawaombea
msamaha kwa Mola Wangu Mlezi. Hakika Yeye ni Mwingi
wa maghufira, Mwenye kurehemu.

99. Na walipoingia kwa Yusuf aliwakumbatia wazazi wake
na akasema: ‘Ingieni Misr, Inshallah, mtakuwa katika amani’.
100. Na akawapandisha wazazi wake kwenye kiti cha enzi
na wakaporomoka kusujudi mbele yake. Na akasema: Ewe
baba yangu! Hii ndio tafsiri ya ile ndoto yangu ya zamani.
Mwenyezi Mungu ameifanya iwe ya kweli. Na Mwenyezi
Mungu alinifanyia wema kunitoa gerezani, na kuwaleta
nyinyi hapa kutoka jangwani baada ya shetani kuchochea
kati yangu na ndugu zangu. Hakika Mola Wangu ni Mpole
kwa alitakalo. Hakika Yeye ni Mjuzi, Mwenye hekima.

101. Ewe Mola Wangu Mlezi! Hakika umenipa madaraka

na umenifunza tafsiri ya matukio. Ewe Muumba wa mbingu na ardhi, wewe ndiye Mlinzi wangu duniani na Akhera. Nifanye nife hali ya kuwa ni Mwislamu na unikutanishe na watu wema.

102. Hayo ni katika habari za ghaibu tulizokufunulia. Hukuwa pamoja nao walipoazimia shauri lao wakipanga njama. 103. Si watu wengi watakaoamini hata ukijitahidi vipi! 104. Wala wewe huwaombi ujira kwa jambo hili. Hili si zaidi ya kuwa ni ujumbe tu kwa walimwengu.

105. Ni ishara ngapi katika mbingu na ardhi wanazozipita na huku wanazipuuza. 106 Na wengi wao hawamwamini Mwenyezi Mungu bila ya kumfanya ana washirika. 107. Je wanaaminisha kuwa haitawafikia adhabu ya Mwenyezi Mungu ya kuwagubika, au hakitawafikia Kiyama kwa ghafla na hali hawatambui? 108. Sema: Hii ndiyo njia yangu ninalingania kwa Mwenyezi Mungu kwa busara mimi na wanaonifuata. Ametakasika Mwenyezi Mungu! Wala mimi si katika mapagani.

109 Na hatukuwatuma Mitume kabla yako isipokuwa wanaume tuliowapa wahyi miongoni mwa watu wa miji (yenye watu wengi). Je, hawatembei katika ardhi wakaona ulikuwaje mwisho wa wale waliokuwa kabla yao? Na hakika nyumba ya Akhera ni bora kwa wamchao Mwenyezi Mungu. Kwa nini hamfahamu? 110 (Adhabu itazuliwa) Hadi pale Mitume wanapokata tamaa na wakajua kuwa wamekanushwa, hapo ndipo inapowajia nusura Yetu, wakaokolewa tuwatakao. Na adhabu Yetu haitawaacha watu wakosefu.

111. Kwa hakika katika simulizi zao mna mazingatio kwa wenye ufahamu. Si hadithi za kutunga, lakini ni za

kuthibitisha yale ya kabla yake na ni ufafanuzi wa kila kitu, na mwongozo na rehema kwa wanaoamini.

## 13. Sura Ar Ra'd

# SURA YA RADI

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 *Alif Laam Miim Raa.*

Hizi ni Aya za Kitabu hiki; kwamba uliyoteremshiwa
kutoka kwa Mola Wako Mlezi ni kweli, lakini watu wengi
hawaamini. 2 Mwenyezi Mungu ndiye aliyeziinua mbingu
bila ya nguzo zozote mzionazo; na yupo imara katika kiti cha
enzi, na amelifanya Jua na Mwezi kutii utaratibu (Wake). Kila
kimoja kinafuata (mkondo wake) hadi muda ulioanishwa.
Anayapanga mambo, anaelezea kwa kina Aya, hivi kwamba
huenda ninyi mkawa na yakini ya kukutana na Mola wenu.
3 Na Yeye ndiye aliyeitandaza ardhi, na akaweka humo
milima na mito ya maji. Na matunda ya kila aina akayafanya
dume na jike. Na (Yeye) huufanya usiku kuufunika mchana.
Hakika katika hayo ziko ishara kwa watu wanaofikiria.
4 Na katika ardhi mna vitalu tofauti (ingawaje)
vimekaribiana, na zipo bustani za mizabibu na makonde
yaliyopandwa (mtama) na mitende ichipuayo kwenye shina
moja na isiyochipua kwenye shina moja (lakini yote) inatiliwa
maji yale yale. Na huifanya baadhi yake ikawa bora kuliko
mingine (ingawaje) hupata virutubishi (vile vile). Hakika
katika hayo kuna ishara kwa watu wanotumia akili.

5. Na kama ukistaajabu basi cha ajabu ni usemi wao:
'Ati tukishakuwa mchanga, kweli tutakuwa katika umbo
jipya?!' Hao ndio waliomkana Mola Wao Mlezi, na hao ndio
watakaokuwa na minyororo shingoni mwao, na hao ndio
watu wa motoni. Humo watakaa milele.
6. Wanakuharakisha uwaletee mabaya kabla ya mazuri!
Hata kama zimekwishapita kabla yao adhabu za kupigiwa
mifano. Na hakika Mola Wako Mlezi ni Mwingi wa maghufira
kwa watu pamoja na matendo yao mabaya. Na hakika Mola
Wako Mlezi (pia) ni Mkali wa kuadhibu.
7. Na wale waliomkana Mwenyezi Mungu husema: 'Mbona
hakuteremshiwa ishara kutoka kwa Mola Wake Mlezi?.'
Hakika wewe ni mjumbe wa kuonya tu. Na kila watu wana
wa kuwaongoza.
8. Mwenyezi Mungu anajua akibebacho (tumboni) kila
mwanamke. Na kwa muda gani mimba wakati wa mimba
umepungua au umezidi. Na kila kitu Kwake ni kwa kipimo.
9. Mjuzi wa vinavyoonekana na visivyoonekana. Mkuu,
aliyetukuka. 10. Ni sawa anayeficha maneno yake katika ninyi
na anayesema wazi. Na anayejibanza usiku na anayetembea
wazi wazi mchana.
11.(Kila mtu) ana Malaika wanaomfuatia kwa zamu mbele
yake na nyuma yake wanaomlinda kwa amri ya Mwenyezi
Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu habadilishi yaliyoko
kwa watu mpaka wao wabadilishe yaliyo katika nafsi zao.
Na Mwenyezi Mungu akiwatakia watu uovu hakuna cha
kuuzuia. Na wala hawana wa kuwalinda yeyote badala Yake.
12. Yeye ndiye anayewaonesha ninyi umeme, kuingiza
hofu na tamaa, na huyanyanyua mawingu mazito. 13. Na radi
inamtakasa kwa kumsifu na Malaika pia kwa adhama yake.

Naye hupeleka mapigo ya radi yakampata amtakaye. Na wao (huthubutu) kubishana juu (ya kuwepo) Mwenyezi Mungu; (Ingawaje) Yeye nguvu zake ni adhimu (namna hiyo)!

14. Kwake pekee ndio (yaelekezwapo) maombi ya kweli. Na hao wanao omba badala Yake hawajibiwi chochote isipokuwa kama yule anyooshaye mkono wake kwenye mto wa maji ili yafikie kinywa chake! Na maombi ya wasio amini si chochote isipokuwa upotofu.

15. Na vilivyomo mbinguni na ardhini vinamsujudia Mwenyezi Mungu vitake visitake, asubuhi na jioni.
Na pia vivuli vyao. 16. Sema: Ni nani Mola Mlezi wa
mbingu na ardhi? Sema: ni Mwenyezi Mungu. Sema: Je, mnawafanya wengine badala Yake kuwa wa kuwalinda, nao hawajinufaishi wenyewe kwa jema wala baya? Sema: hivi anaweza kuwa sawa kipofu na aonaye? Au hivi huwa sawa giza na mwanga? Au hivi wanamfanyia Mwenyezi Mungu washirika walioumba kama alivyoumba Yeye, ndipo hivyo viumbe (vikawatatiza) kwa vile vimefanana? Sema: Mwenyezi Mungu ndiye Muumba wa kila kitu na Yeye ni Mmoja, Mwenye kushinda.

17. Ameteremsha maji kutoka mawinguni mabonde yakamiminika maji kwa kadri ya vipimo vyake, na mafuriko yakachukua povu liliyokusanyika juu yake. Na katika vile wanavyoyeyusha katika moto kwa kutengeneza mapambo au vyombo, pia kuna ukungu kama huo. Hivi ndivyo Mwenyezi Mungu (kwa mifano) huonesha ukweli na udanganyifu. Waama povu, hili linapotea kama takataka tu. Ama kinachowafaa watu hubakia kwenye ardhi. Hivyo ndivyo Mwenyezi Mungu anavyopiga mifano.

18. Waliomwitikia Mola Wao Mlezi watapata wema; na

wasiomwitikia, hata wangemiliki vilivyomo ardhini vyote na mfano wake, wangevitoa ili wajikomboe. Hao wana hesabu mbaya kabisa na makao yao ni Jahannam, na hapo ni mahali pabaya mno.

19. Je, anayejua kwamba yaliyoteremshwa kutoka kwa Mola Wako Mlezi ni kweli, ni sawa na aliye kipofu? Hakika wanaozingatia ni wenye akili tu. 20. Wale ambao wanatimiza ahadi ya Mwenyezi Mungu wala hawavunji maagano. 21. Na wale ambao huyaunga yale aliyoamrisha Mwenyezi Mungu yaungwe,[6] na humwogopa Mola Wao, na huihofu hisabu mbaya. 22 Na ambao husubiri kwa kutaka radhi ya Mola Wao, na wakasimamisha Swala na wakatoa kwa siri na kwa dhahiri katika baadhi ya tulivyowapa, na wakayaondoa maovu kwa (kufanya) mema. Hao ndio watakaopata malipo ya nyumba (ya milele). 23 Nayo ni Bustani za Milele wataziingia wao na walio wema miongoni mwa baba zao, wake zao na vizazi vyao. Na Malaika wataingia kwao katika kila mlango.... 24 (Wakiwaambia): Assalaam alaykum, (amani iwe juu yenu) kwa sababu ya mlivyosubiri. Ni mema mno malipo ya nyumba ya Akhera.

25. Na wale wanaovunja ahadi ya Mwenyezi Mungu baada ya kuifunga na wanakatilia mbali aliyoamrisha Mwenyezi Mungu yaungwe na wanafanya uovu katika nchi; hao ndio walio na laana na wana nyumba mbaya. 26. Mwenyezi Mungu humkunjulia riziki amtakaye na humkunjia. Wamefurahia maisha ya dunia. Na maisha ya duniani kulinganisha na Akhera si chochote isipokuwa starehe fupi tu..

6. Mfano Imani na matendo, mapenzi ya Mungu na ya watu, kuwaheshimu Mitume wote, udugu, nk...mfasiri)

27. Na wanasema waliokufuru: ‘Kwa nini hakuteremshiwa Ishara kutoka kwa Mola Wake? Sema: Mwenyezi Mungu humwacha apotee amtakaye na humuongoza anayeelekea Kwake… 28. Ni wale ambao wameamini na nyoyo zao zikapata utuvu wanapomtaja Mwenyezi Mungu. Ndiyo! Kwa kumdhukuru Mwenyezi Mungu nyoyo hutulia. 29. Wale ambao wameamini na wakafanya matendo mema, raha ni yao na marejeo mazuri.

30. Ndio kama hivi tumekutuma kwa mataifa ambayo yamekwishapita kabla yake mataifa mengine, ili uwasomee tunayokufunulia kwa wahyi na wao wamemkufuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema. Sema, Yeye ni Mola Wangu Mlezi hakuna Mola mwengine isipokuwa Yeye. Juu Yake nimetegemea na Kwake Yeye ndio marejeo yangu.

31. Na kama ingekuwepo Qura’n ambayo kwayo milima husogezwa, au ardhi hupasuliwa, au waliokufa husemeshwa (pia wasingeamini). Bali amri ni ya Mwenyezi Mungu juu ya vitu vyote. Hivi hawajui wale walioamini kwamba kama Mwenyezi Mungu angependa bila shaka angewaongoza watu wote (kwenye ukweli)? Na waliomkana Mwenyezi Mungu hawataisha kupatwa na mikosi kutokana na maovu waliyoyatenda, au ikawajia karibu na nyumbani kwao, mpaka iwafikie ahadi ya Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu havunji miadi. 32. Na hakika walifanyiwa kejeli Mitume waliokuwa kabla yako, lakini nikawapa muda wale ambao wamekufuru, kisha nikawatia nguvuni! Hivi ilikuwaje adhabu yangu?!

33. Hivi anayesimamia kila nafsi (na kujua) kila inayoyachuma….(ni kama wengine?) Wanamfanyia Mwenyezi Mungu washirika? Sema: ‘haya, watajeni! Au

ndio mnampa habari ya yale asiyoyajua katika ardhi? Au ni kujitapa kwa maneno tu? Hapana, bali wale waliokufuru wamefanywa wapendezewe na njama zao, na wamezuiwa njia. Na ambaye Mwenyezi Mungu amemwacha apotee hana wa kumwongoza. 34. Wanayo adhabu katika maisha ya duniani. Na hakika adhabu ya Akhera ni ngumu zaidi. Na wala hawana wa kuwalinda dhidi ya Mwenyezi Mungu.

35. Mfano wa Pepo waliyoahidiwa wamchao Mwenyezi Mungu, inapita mito ya maji chini yake, matunda yake ni ya daima na pia kivuli chake. Huo ndio mwisho mwema wa wale wamchao Mungu. Na mwisho wa makafiri ni moto.

36. Na wale ambao tumewapa Kitabu wanafurahia uliyoteremshiwa. Na kuna katika koo nyingine wapo wanaokataa baadhi yake. Sema: Nimeamrishwa nimwabudu Mwenyezi Mungu wala nisimshirikishe. Ninalingania kwake Yeye, na marejeo ni Kwake. 37. Na ndio kama hivyo tumeiteremsha Qur’an iwe hukumu (na) kwa lugha ya Kiarabu. Na kama ukifuata mapenzi yao baada ya kukujia elimu hii, hutakuwa na rafiki wala wa kukulinda mbele ya Mwenyezi Mungu. 38. Na hakika tulikwishawatuma mitume kabla yako na tukafanya wawe na wake na watoto. Na haiwezekani kwa Mtume kuleta muujiza isipokuwa kwa ruhusa ya Mwenyezi Mungu. Kila zama zina kitabu chake. 39. Mwenyezi Mungu hufuta na huthibitisha ayatakayo, na Kitabu cha asili kipo Kwake.

40. Endapo tutakuonyesha (katika umri wako) baadhi ya tunayowaahidi au tukakufisha kabla, wewe ni juu yako kufikisha (ujumbe) tu, na juu Yetu ni kuwafanya wawajibike. 41. Hivi hawaoni kwamba kidogo kidogo tunaipunguza nchi yao kwenye (mipaka ya) pembeni mwake (kutoka kwenye

udhibiti wao)? Na Mwenyezi Mungu huhukumu, hapana wa
kupinga hukumu Yake; na Yeye ni mwepesi wa kuwajibisha.
42. Pia walipanga njama waliokuwa kabla yao, lakini
Mwenyezi Mungu ndiye mwenye mipango yote. Anajua
inayoyachumma kila nafsi. Na makafiri watajua ni ya nani
nyumba ya mwisho.
43. Na wale ambao wamekufuru wanasema wewe si
Mtume. Sema: Mwenyezi Mungu anatosha kuwa shahidi
baina yangu na nyinyi na yule mwenye elimu ya Kitabu.

14. Sura Ibrahim

## SURA YA ‘NABII’ IBRAHIM/ABRAHAM

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 *Alif Laam Ra.*

Hiki ni Kitabu tulichokiteremsha kwako ili uwatoe watu
katika dimbwi la giza uwapeleke kwenye nuru, kwa idhini
ya Mola Wao Mlezi, uwafikishe kwenye njia ya (Mwenyezi
Mungu) Mwenye nguvu, Mwenye kustahiki kusifiwa. 2 Ni
Mwenyezi Mungu ambaye ni Vyake vilivyomo mbinguni
na vilivyomo ardhini. Na ole wao wanaomkana Mwenyezi
Mungu kwa adhabu kali. 3 Wale ambao hupendelea zaidi
maisha ya dunia kuliko Akhera na wakawazuia watu
wasifuate njia ya Menyezi Mungu na wakataka kuipotosha,
hao wamepotea kwa masafa ya mbali.
4 Hatukumtuma Mtume yeyote ila kwa lugha ya watu
wake ili apate kuwawekea wazi (ujumbe). Kisha Mwenyezi

Mungu humwacha akapotea yule amtakaye na akamwongoza
amtakaye; na Yeye ni Mwenye nguvu Mwenye hekima.

5. Hakika tulimtuma Musa (Moses) pamoja na miujiza
Yetu, kuwa (nenda) kawatoe watu wako katika dimbwi la
giza uwapeleke kwenye nuru. Na uwafundishe wakumbuke
siku za Mwenyezi Mungu. Hakika katika hayo kuna ishara
kwa kila mwenye kusubiri, mwenye kushukuru.

6. Kumbuka wakati Musa alipowaambia watu wake:
‘kumbukeni neema ya Mwenyezi Mungu juu yenu, pale
alipowaokoa na watu wa Firauni waliowapa nyie adhabu
kali; wakiwachinja watoto wenu wa kiume na wakiwaacha
hai watoto wenu wa kike. Na katika hayo ni mtihani mkubwa
kutoka kwa Mola Wenu. 7. Na pale alipotangaza Mola Wenu
Mlezi: ‘mkishukuru nitawazidishia na mkikufuru basi adhabu
Yangu ni kali’. 8. Na Musa akawaambia: mkikufuru nyinyi na
wote waliomo duniani, hakika Mwenyezi Mungu ni Mkwasi
Mwenye kusifiwa.

9. Je hazikuwafikia habari za walio kabla yenu: watu wa
Nuh (Noah) na A’d na Thamud na walio baada yao? Hakuna
awajuaye ila Mwenyezi Mungu. Waliwajia mitume wao kwa
hoja zilizo wazi. Wakaweka mikono yao kwenye vinywa
vyao, na wakasema: ‘sisi tumeyakataa hayo mliyotumwa
nayo na hakika sisi tuna shaka kubwa juu ya mnayotuitia’.

10. Mitume wao wakasema: Je, hivi kuna shaka yoyote
juu ya Mwenyezi Mungu, Muumba wa mbingu na ardhi?
Anawaita ili apate kuwaghufiria dhambi zenu na anawapa
muhula mpaka muda uliopangwa. Wakasema: Nyinyi
si chochote ila ni watu kama sisi. Mnataka kutuzuia na
walivyokuwa wakiviabudu baba zetu? Haya, tuleteeni
muujiza ulio wazi.

[11.] Mitume wao wakawaambia: Sisi si wengine isipokuwa wanadamu kama nyinyi, lakini Mwenyezi Mungu humneemesha amtakaye katika waja Wake. Sisi hatuwezi kuwaletea muujiza ila kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Na waumini wamtegemee Mwenyezi Mungu pekee. [12.] Na tuna nini hata tusimtegemee Mwenyezi Mungu na hali Yeye ametuongoza kwenye njia yetu? Hakika sisi tutavumilia mnavyotuudhi; na wale wenye mategemeo basi wamtegemee Mwenyezi Mungu pekee.

[13.] Na wale ambao wamekufuru waliwaambia mitume wao: ‘Tutawafukuza katika ardhi yetu au mrudi kwenye dini yetu. Mola Wao Mlezi akawafunulia kwa njia ya wahyi: ‘hakika bila shaka tutawaangamiza madhalimu’. [14.] Nanyi tutawawezesha muishi katika ardhi baada yao. Hayo ni kwa yule anayehofia kusimama mbele ya mahakama Yangu na akahofia makamio yangu.

[15.] Lakini wao wakaomba ushindi (wa haraka). Ndipo akarudi mikono mitupu kila jambazi mkaidi. [16.] Nyuma yake iko Jahannam, na atanyweshwa maji ya usaha uliochanganyika na damu. [17.] Atayagugumia wala hataweza kuyameza. Na yatamjia mauti kutoka kila mahali, naye wala hafi. Na zaidi ya hiyo kuna adhabu nyingine nzito.

[18.] Mfano wa wale ambao wamemkana Mola Wao vitendo vyao ni kama majivu yanayopeperushwa kwa nguvu za upepo katika siku ya kimbunga. Hawana uwezo wa chochote juu ya walichokichuma. Huko ndiko kupotea mbali (na njia nyoofu). [19.] Je, huoni kuwa Mwenyezi Mungu ameziumba mbingu na ardhi juu ya ukweli? Akitaka atawaondoeni na alete viumbe wapya. [20.] Na hilo kwa Mwenyezi Mungu si jamo gumu.

21. Na wote kwa pamoja watahudhuria mbele ya Mwenyezi Mungu. (Waliokuwa) Wanyonge watawaambia wale waliokuwa wajeuri: 'Sisi tulikuwa wafuasi wenu, je mtatupunguzia kidogo katika adhabu ya Mwenyezi Mungu?' Watasema: 'Lau Mwenyezi Mungu angetuongoza nasi tungewaongoza nanyi pia. Ni mamoja kwetu tukasirike au tusubiri (mateso); hatuna pa kukimbilia.

22. Na shetani atasema baada ya hukumu kutolewa: 'Hakika Mwenyezi Mungu aliwaahidi ahadi ya kweli, nami nikawaahidi lakini sikuwatimizia. Na sikuwa na mamlaka yoyote juu yenu, isipokuwa niliwaita tu mkaniitikia. Basi msinilaumu mimi, lakini mjilaumu wenyewe. Sitawapigia kelele wala nyie msinipigie kelele. Mimi nilikwishakataa tangu zamani kitendo chenu cha kunishirikisha mimi na Mwenyezi Mungu. Hakika watenda maovu wana adhabu chungu.

23. Na wale ambao wameamini na wakatenda mema wataingizwa katika mabustani ambayo hupita mito ya maji chini yake. Watakaa humo milele kwa idhini ya Mola wao Mlezi. Maamkuzi yao humo yatakuwa: Salaam!

24. Je, hukuona jinsi Mwenyezi Mungu alivyopiga mfano
wa neno zuri? (Kwamba) ni kama mti mzuri. Mizizi yake
ni imara na matawi yake (hufika) hadi mbinguni. 25. Hutoa
matunda yake kila wakati kwa idhini ya Mola Wake Mlezi.
Na Mwenyezi Mungu huwapigia watu mifano ili wapate
kuonyeka. 26. Na mfano wa neno ovu ni kama mti mbaya
uliong'olewa juu ya ardhi, hauko imara.

27. Mwenyezi Mungu huwaimarisha wale walioamini kwa kuwapa kauli thabiti katika maisha ya dunia na katika

Akhera, na Mwenyezi Mungu huwaacha wapotee wale wenye kudhulumu, na Mwenyezi Mungu hufanya apendavyo.

28. Je, hukuwaona wale waliobadilisha neema ya Mwenyezi Mungu kwa kufuru? Na wakawafikisha watu wao kwenye nyumba ya maangamivu? 29. Nayo ni Jahannam watakayoiingia. Ni mahala pabaya pa kukaa. 30. Na walimfanyia Mwenyezi Mungu washirika ili wawapoteze watu kutoka njia Yake, Sema: Stareheni! Kwani hakika marejeo yenu ni motoni.

31. Waambie waja Wangu walioamini, wasimamishe Swala na watoe kwa siri na kwa wazi wazi, baadhi ya vitu tulivyowaruzuku, kabla ya kuwadia siku isiyokuwa na kujadiliana bei wala urafiki.

32. Mwenyezi Mungu ndiye ambaye ameziumba mbingu na ardhi na akateremsha maji kutoka mawinguni. Na kwayo akatoa matunda kuwa chakula kwenu. Na akawafanyia wepesi majahazi yaweze kupita baharini kwa amri Yake, na akawafanyia wepesi mito ya maji pia. 33. Na akawafanyia wepesi Jua na Mwezi daima vikifuata utaratibu wao ulivyopangiwa. Na akaufanya usiku na mchana uwatumikieni. 34. Na akawapa kila mlichomuomba. Na mkihesabu neema za Mwenyezi Mungu hamuwezi kuzidhibiti. Hakika binadamu ni mwingi wa kuchukia haki mtovu wa shukrani.

35. Kumbuka pale Ibrahim aliposema: Ewe Mola Wangu Mlezi! Ufanye mji huu uwe wa amani na uniepushe mimi na kizazi changu na kuabudu masanamu. 36. Ewe Mola Wangu Mlezi! Hakika hayo (masanamu) yamewapoteza watu wengi. Basi atakayenifuata, huyo ni miongoni mwangu atakayeniasi basi hakika Wewe ni Mwingi wa maghufira, Mwenye kurehemu.

[37.] Ewe Mola Wetu Mlezi! Mimi nimewaleta baadhi ya kizazi changu waje waishi katika wangwa usio na mimea, kwenye nyumba Yako takatifu- ewe Mola Wetu Mlezi- ili wasimamishe Swala. Basi zifanye nyoyo za baadhi ya watu zijawe na mapenzi kwao na uwaruzuku matunda ili wapate kukushukuru.

[38.] Ewe Mola Wetu Mlezi! Hakika wewe unajua tunayoyaficha na tunayoyaweka wazi. Na hapana kitu kinachofichikana mbele ya Mwenyezi Mungu katika ardhi
wala mbingu. [39.] Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu aliyenipa juu ya uzee wangu Ismail na Is-haq (Isaac). Hakika
Mola Wangu ni Mwenye kujibu mno dua. [40.] Ewe Mola Wangu Mlezi! Nijaalie niwe mwenye kusimamisha Swala na katika kizazi changu pia. Ewe Mola Wetu Mlezi! Na uitakabali dua
yangu. [41.] Ewe Mola Wetu Mlezi! Nighufirie mimi na wazazi wangu wawili na waumini siku ya kusimama hisabu.

[42.] Wala usidhani kuwa Mwenyezi Mungu ameghafilika na wanayoyafanya madhalimu. Hakika Yeye anawaakhirisha tu mpaka siku watu watakapokodoa macho (kwa hofu).
[43.] Wakiwa mbioni kwenda mbele, vichwa juu, macho yao hayapepesi na vifua vyao vikikosa pumzi.

[44.] Na waonye watu siku itakapowajia adhabu na waliodhulumu waseme: Ewe Mola Wetu Mlezi! tuakhirishie kwa muda mfupi, tutaitikia wito Wako na tutawafuata mitume. Je, hamkuwa mmeapa huko nyuma kuwa
nyinyi hamtamalizika? [45.] Na mkakaa katika maskani ya wale waliozidhulumu roho zao, na ikawabainikia jinsi
tulivyowafanya na tukawapigia mifano mingi? [46.] Na kwa hakika walifanya hila zao na hila zao zinajulikana mbele

ya Mwenyezi Mungu, ingawaje hila zao haziwezi kutikisa
milima!

47. Basi usifikiri kuwa Mwenyezi Mungu atavunja
ahadi yake kwa mitume Wake. Hakika Mwenyezi Mungu
ni Mwenye kushinda, Mwenye kulipiza kisasi. 48. Siku
itakapobadilishwa ardhi kuwa ardhi nyingine na mbingu
(pia). Nao watahudhuria mbele ya Mwenyezi Mungu
Mmoja, Mwenye nguvu. 49. Utawaona wahalifu siku hiyo
wamefungwa katika minyororo. 50. Nguo zao zitakuwa za
lami na moto utazigubika nyuso zao. 51. Ili Mwenyezi Mungu
ailipe kila roho kwa yale iliyoyachuma. Hakika Mwenyezi
Mungu ni Mwepesi wa kuwajibisha. 52. Hii (Qur'an) ni
ujumbe wazi kwa watu iwaonye na wapate kujua kuwa
hakika Yeye ni Mungu ni Mmoja tu. Acha wenye akili watie
kichwani ilani hii.

## 15. Sura Al-Hijr

## SURA YA NJIA YA MAJABALINI

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 *Alif Lam Raa.*

Hizi ni Aya za Kitabu na za Qur'an inayoweka wazi. 2 Huenda
waliomkana Mwenyezi Mungu wakatamani wangekuwa
Waislamu. 3 Waache hao wastarehe, wafurahie na iwazuge
tamaa; Punde hivi watajua. 4 Na hatukuiangamiza jamii
yeyote ile ya watu isipokuwa kwanza walipewa ilani katika

(muda) ulioainishwa. 5 Jamii yeyote haiwezi kuwa mbele ya
muda wake au kuwa nyuma.

6 Na walisema: Ewe uliyeteremshiwa ujumbe huu!
Kwa kweli wewe ni mwendawazimu. 7 Mbona hutuletei
Malaika ikiwa wewe ni miongoni mwa wasemao kweli?.
8 Hatuwateremshi Malaika ardhini isipokuwa kwa sababu ya
maana. Na (wanaposhuka), hapo tena (waovu) hawatapewa
simile.

9. Hakika Sisi ndio tuliouteremsha ujumbe huu, na hakika
Sisi ndio tuulindao ( dhidi ya kubadilishwa).

10. Na hakika tulikwishawatuma Mitume kabla yako katika
mataifa ya mwanzo. 11. Na hawakuwafikia wao Mtume yeyote
isipokuwa walikuwa wakimfanyia kejeli. 12. Pamoja na
hivyo, tunaupenyeza (ujumbe) ndani ya nyoyo za wakosefu.
13. Hawatauamini, ingawaje mila za watu wa kale zimepita
(ujumbe huu unadumu). 14. Hata kama tungewafungulia lango
kutoka mbinguni wakawa (siku nzima) wanapanda (kwenda
huko)…. 15. Wangesema:'hakika macho yetu yameathiriwa
kwa ulevi; au sisi wenyewe tumerogwa'.

16 Hakika tumeweka katika mbingu vituo (12) vya
sayari, na tumevifanya vipendeze kwa wenye kuangalia.
17 Na tumevilinda na kila shetani aliyelaaniwa. 18 Isipokuwa
asikilizaye kwa kuiba, naye hufuatwa na kijinga cha moto
kinachoonekana.

19 Na ardhi tumeitandaza na tumeweka humo milima
imara na tukaotesha kila aina ya vitu kwa uwiano sahihi.
20 Na tumefanya humo (sababu za) maisha yenu, na ya hata
yule ambaye nyinyi sio mnayempa riziki.

21. Na hakuna kitu chochote isipokuwa akiba yake iko
Kwetu, lakini hatuiteremshi isipokuwa kwa kipimo maalum.

22. Na tukazipeleka pepo kwa kupandishia (mimea) na tukateremsha kutoka mawinguni maji tukawanywesha hayo; wala sio nyinyi myawekayo akiba.

23. Na Sisi ndio tunaotoa uhai na tunaotoa mauti. Ni sisi ndiyo tutabakia baada ya wote kuondoka. 24. Na hakika tunawajua waliokwishatangulia katika nyinyi na hakika tunawajua wanaokuja nyuma. 25. Na hakika Mola Wako ndiye atakayewakusanya. Hakika Yeye ni Mwenye hekima, Mjuzi.

26. Na hakika tulimuumba binadamu kutokana na udongo wa mfinyazi uliotokana na matope meusi yaliyofinyangwa. 27. Na majinni tumewaumba kabla yenu kwa moto wa upepo wa joto kali.

28. Kumbuka pale Mola Wako Mlezi alipowaambia Malaika: 'Hakika mimi nitamwumba mtu kutokana na udongo wa mfinyazi uliotokana na matope meusi yaliyofinyangwa. 29. Basi nitakapomkamilisha na nikampulizia roho Yangu, mwangukieni kumsujudia. 30. Basi Malaika wote kwa pamoja walimsujudia. 31. Isipokuwa Ibilisi alikataa kuwa pamoja na waliosujudu. 32. (Mwenyezi Mungu) akamwuliza: Ewe Iblisi! Una nini hata hukuwa pamoja na waliosujudu? 33. Akasema (Iblisi): Haiwezekani mimi nimsujudie binadamu uliyemwumba kutokana na udongo nyororo kutokana na matope meusi yenye kufinyangwa.

34. Mwenyezi Mungu akamwambia:' Basi toka humu, hakika wewe umefukuzwa' 35. Na hakika itakuandama laana mpaka siku ya malipo. 36. Akasema (Iblisi): Mola Wangu Mlezi! Nipe muda mpaka siku watakapofufuliwa. 37. (Mwenyezi Mungu) akasema: 'Basi wewe ni katika waliopewa muda, 38. Mpaka siku ya wakati maalum'.

39. Akasema (Iblisi): 'Kwa vile umeniacha nifanye makosa,

basi nami nitahakikisha ninanawafanyia (wanadamu)
mabaya wayaone mazuri hapa duniani na nitawapoteza wote.
40. Isipokuwa waja Wako waliotakaswa.

41. Akasema (Mwenyezi Mungu): ‘Hii hapa njia
iliyonyooka ya kufikia Kwangu’. 42. ‘Hakika waja Wangu
hutakuwa na mamlaka nao, isipokuwa wale wapotofu
waliokufuata’. 43. ‘Na hakika Jahannam ndipo mahali pao
walipoahidiwa wote’. 44. Ina milango saba, kila mlango una
sehemu waliyotengewa.

45. Hakika wamchao Mwenyezi Mungu watakuwa katika
bustani na chemchemi za maji safi. 46. (Wataambiwa):
‘Ingieni kwa amani mhisi usalama’. 47. Na tutaondoa chuki
na mifundo iliyokuwamo vifuani mwao wawe ndugu, wakae
juu ya viti wakielekeana. 48. Humo hayatawagusa machovu
wala hawataambiwa watoke. 49. Waambie waja Wangu ya
kwamba Mimi ndiye Mwenye kusamehe, mwingi wa huruma
kwa waja. 50. Na kwamba adhabu Yangu ndiyo adhabu iliyo
chungu.

51. Na wahadithie kuhusu wageni wa Ibrahim (Abraham).
52. Walipoingia kwake wakasema: Salaam!. Akasema:
‘sisi tunawahofia nyie’! 53. Wakasema: ‘Usihofu!. Sisi
tunakubashiria (utapata) kijana mwenye elimu nyingi’.
54. Akasema: Mnanibashiria miye (mtoto) na uzee wangu
huu?! Kwa lipi hasa mnanibashiria? 55. Wakasema: ‘Tunakupa
habari njema za kweli, basi usiwe miongoni mwa wanaokata
tamaa. 56. Akasema: ‘Na ni yupi anayekata tamaa ya huruma
ya Mola Wake Mlezi isipokuwa wale waliopotea!’.

57. Akasema: ‘Nini hasa kusudio lenu, enyi wajumbe’?
58. Wakasema: ‘Hakika sisi tumetumwa kwa watu waliozama
katika dhambi’. 59. ‘Isipokuwa familia ya Lut, hakika

tutawaokoa wote'. 60. 'Ukimwacha mkewe tu, kwani tuna uhakika yeye atakuwa miongoni mwa watakaobaki nyuma'.

61. Hatimaye wajumbe walipofika kwa familia ya Lot. 62. Aliwaambia: '(Yaonekana) Nyinyi ni watu msiojulikana hapa'. 63. Wakasema: 'Bali tumekujia kupitisha yale waliyokuwa wakiyatilia shaka'. 64. 'Na tumekuletea lile lisiloepukika na hakika tunasema kweli'. 65.'Ondoka na familia yako wakati usiku bado ungalipo, nawe ufuate nyuma yao, wala yeyote kati yenu asigeuke nyuma. Na nendeni kule mnakoamriwa'. 66. Na tukamfunulia hukumu hiyo kwamba (hata) wa mwisho wao atakuwa amefyekwa ifikapo asubuhi'.

67. Wakaja watu wa mji ule wakifurahi. 68. Lut akawaambia: 'kwa kweli hawa ni wageni wangu, tafadhalini msinifedheheshe'. 69. 'Na mwogopeni Mwenyezi Mungu, wala msinidhalilishe'. 70 Wakasema: 'Hivi wewe Lut hatukukukataza kuwa usizungumze kwa niaba ya wote?'. 71 Akasema: 'Basi, hawa binti zangu. Ikiwa mwataka mfanye hivyo'.

72. Naapa kwa umri wako (Ewe Muhammad) ! Hakika hao wamo katika ulevi wao wakimangamanga. 73. Sauti ya mpasuko mkubwa ikawaangamiza, jua lilipokuwa likichomoza. 74. Tukaigeuza ardhi juu chini, tukawanyeshea mvua ya mawe ya udongo mkavu. 75. Hakika katika hayo kuna ishara kwa wale wanaofahamu kwa ishara.. 76. Na miji hii ilikuwa katika njia kuu inayopitwa na watu. 77. Hakika katika (kisa) hicho kuna ishara kwa wale wanaoamini.

78. Na watu waliokuwa wakiishi porini hakika pia walifanya maovu. 79. Hivyo tukawaadhibu. Na miji miwili hii ilikuwa kwenye njia kuu, iliyoonekana wazi. 80. Na watu waliokuwa wakiishi kwenye milima ya mawe kadhalika waliwakana

Mitume wao. 81. Na tukawapa ishara Zetu nao wakazipuuza.
82. Walikuwa wakichonga majumba katika majabali
(wakihisi) amani. 83. Lakini tena sauti ya mpasuko mkubwa
ukawaua majira ya asubuhi. 84. Hayakuwafaa (majumba ya
mawe) waliyokuwa wakiyatengeneza kwa ustadi mkubwa.

85. Na hatukuziumba mbingu na ardhi na vilivyomo baina
yake ila kwa lengo (la kutoa) uadilifu. Na hakika saa ya
mwisho (Kiyama) itafika. Basi wasamehe kwa namna nzuri
(bila kinyongo). 86. Hakika Mola Wako ndiye Muumbaji,
Mjuzi wa kila kitu.

87. Na hakika tumekupa Aya saba zinazorudiwa mara kwa
mara, na Qur'an Tukufu vile vile. 88. Usiumize macho yako
kutazama (kwa kutamani) vitu tulivyozistarehesha tabaka
mbalimbali miongoni mwao. Wala usiwahuzunikie bali
inamisha bawa lako (kuwa mnyenyekevu) kwa Waumini.[7]
89 Na sema: Hakika mimi ni mwonyaji niliye wazi
90 Kama tulivyowateremshia (adhabu) wale waliogawa..
(vitabu vitakatifu kwenye mafungu waliyoyakubali na
waliyoyakataa). 91 (Aidha) Ambao wameifanya Qur'an kuwa
vipande vipande (wakafuata wavipendavyo) 92 Naapa kwa
Mola Wako Mlezi tutawauliza wote. 93 Yale waliyokuwa
wakiyatenda.

94. Basi yatangaze uliyoamrishwa na achana na mapagani.
95. Hakika Sisi tunatosha kukukinga na wafanyao kejeli.
96. Hao wanaofanya pamoja na Mwenyezi Mungu yuko mungu
mwingine. Punde hivi watatambua!. 97. Hakika Sisi tunajua
kwamba kifua chako kinaona dhiki kwa yale wanayoyasema

---

7. istiara hii imechukuliwa kwa ndege anayeinamisha bawa lake kwa upole anapowalisha makinda yake.

(dhidi yako). 98. Basi mtakase na mabaya Mola Wako Mlezi
kwa kumhimidi, na uwe miongoni mwa wanaomsujudia.
99. Na mwabudu Mola Wako Mlezi hadi ikujie yakini (mauti).

## 16. Sura An-Nahl

# SURA YA ‘MAMLAKA YA’ NYUKI

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 Amri ya Mwenyezi Mungu itafika, msiifanyie haraka.
Ametakata na kutukuka na wanavyovishirikisha Naye.
2 Huwateremsha Malaika pamoja na ufunuo wa maagizo
Yake kwa anaowapenda katika waja Wake; kwamba
waonyeni (wanadamu na majinni) kuwa hakuna Mola
anayestahiki kuabudiwa isipokuwa Mimi tu, basi nicheni
Mimi. 3 Ameumba mbingu na ardhi kwa shabaha ya kutenda
uadilifu. Ametukuka kuliko vile wanavyovishirikisha Naye.

4 Amemwumba mwanadamu kwa tone la manii,
lakini ghafla akawa mshindani mkubwa!. 5 Na wanyama
amewaumbieni, katika hao mnapata joto na manufaa
mengineyo, na baadhi yake mnawala. 6 Na wanawapa furaha
pale mnapowarudisha jioni na mnapowapeleka malishoni
asubuhi. 7 Na hubeba mizigo kupeleka kwenye miji ambayo
msingeweza kuifikia isipokuwa kwa taabu nyingi kwenu.
Hakika Mola Wenu Mlezi ni mpole sana, mwingi wa huruma.
8 Pia farasi, nyumbu na punda ili muwapande na pia kwa
maonesho. Na anaumba msivyovijua.

9. Na ni juu ya Mwenyezi Mungu kuongoza njia (iliyo

sawa). Lakini kuna nyingine ni kombo. Kama angependa angewaongozeni nyote kwenye njia nyoofu.

10. Yeye ndiye anayewateremshia maji kutoka mawinguni. Kutokana na hayo nyinyi mnapata ya kunywa na ya kuotesha miti ya kulisha wanyama. 11. Kutokana na hiyo huzalisha mimea kwa ajili yenu na mizaituni na mitende na mizabibu na kila aina ya matunda. Hakika katika hayo zipo ishara kwa watu wanaofikiri.

12. Na amewafanyia wepesi usiku na mchana na jua na mwezi na nyota ziwatumikie kwa amri Yake. Hakika katika hayo kuna ishara kwa watu walio na akili. 13. Na hivi anavyoifanya vizaliane juu ya ardhi vya rangi mbali mbali. Hakika katika hayo kuna ishara kwa watu wanaowaidhika.

14. Yeye ndiye aliyeifanya bahari iwatumikie kwa wepesi, ili kutoka humo mpate kula minofu freshi na laini na mtoe humo mapambo mnayovaa. Na utaona merikebu zikikata mawimbi humo, ili mtafute neema Zake, ili huenda ninyi mkashukuru.

15. Na akakita ardhini milima imara ili ardhi isiyumbe nanyi. Na mito ya maji na njia ili muweze kujiongoza (msipotee njia). 16. Na alama nyinginezo. Na kwa nyota wao hutambua njia.

17. Hivi anayeumba ni kama asiyeumba? Kwa nini hamwonyeki? 18. Na mkihisabia neema za Mwenyezi Mungu hamuwezi kuzidhibiti. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa maghufira, Mwingi wa huruma. 19. Na Mwenyezi Mungu anayajua mnayoyafanya siri na mnayoyafanya wazi.

20. Na wale wanaowaomba wasiokuwa Mwenyezi Mungu hawaumbi kitu chochote, bali wao wameumbwa. 21. Ni wafu hawako hai. Na wala hawatambui watafufuliwa lini.

22. Mola Wenu ni Mungu Mmoja tu. Lakini wasioamini Akhera nyoyo zao zinakataa, nao wana kiburi. 23. Hapana shaka kuwa Mwenyezi Mungu anayajua wanayoyafanya siri na wanayofanya wazi. Hakika Mwenyezi Mungu hawapendi wenye kiburi.

24. Wanapoulizwa: Ameteremsha nini Mola Wenu? Hujibu: 'Hekaya za watu wa kale'. 25. Waache wabebe mizigo yao kwa ukamilifu siku ya Kiyama, na sehemu ya mizigo ya wale wasio na elimu ambao wanawapoteza. Angalia! Ni uzito ulioje wa mizigo hiyo wanayoibeba!

26. Wale waliokuwa kabla yao pia walisuka njama (dhidi ya njia ya Mungu). Lakini Mwenyezi Mungu akayabomoa majengo yao toka kwenye misingi, dari zikawaporomokea vichwani, na adhabu ikawajia kutoka upande wasioudhania. 27. Kisha siku ya Kiyama atawafedhehesha na kuwauliza: 'Wako wapi hao washirika Wangu ambao kwa sababu yao mlikuwa mkibishana (na watu wema)?' Hapo waliopewa elimu watasema: Hakika leo fedheha na huzuni vitawakuta waliomkana Mwenyezi Mungu.

28. Nao ni wale ambao Malaika wanatwaa roho zao huku wakiwa bado wanazitendea uovu roho zao. Basi watajisalimisha (wakidai): 'Hatukuwa tukifanya uovu wowote (kwa kujua)'! (Malaika watajibu): Eeeh? Hakika Mwenyezi Mungu anajua sana mliyokuwa mkiyatenda. 29. Ingieni milango ya Jahannam, humo mdumu. Ni maovu mno makazi ya wenye kiburi!

30. Kwa wanaomcha Mwenyezi Mungu, watakapoulizwa:'Mola Wenu Mlezi ameteremsha nini?' Watasema:'Kheri tupu!'. Waliofanya wema katika dunia hii watapata wema. Na nyumba ya Akhera ni bora zaidi. Ni

bora mno nyumba ya wanaomtii na kumuenzi Mwenyezi
Mungu. 31. Bustani za milele wataziingia, hupita chini yake
mito ya maji. Humo watapata kila wakitakacho. Hivi ndivyo
Mwenyezi Mungu awalipavyo wanaomtii na kumuenzi.
32. Wale ambao Malaika hutwaa roho zao katika hali njema,
huwaambia: ‘Salamun alaykum!’ (Amani iwe juu yenu) kwa
yale mliyokuwa mkiyafanya.

33. Je, wanangojea jengine isipokuwa Malaika wawafikie au
iwafikie hukumu ya Mola Wako Mlezi? Hivyo hivyo ndivyo
walivyofanya wale waliokuwa kabla yao. Na Mwenyezi
Mungu hakuwadhulumu. Lakini wamejidhulumu wenyewe.
34. Ndipo yakawafikia (matokeo ya) uovu wa waliyoyafanya
na ikawazingira (hasira ) ya yale waliyokuwa wakiyafanyia
mzaha.

35. Na wale mapagani husema: ‘Kama Mwenyezi Mungu
angependa, tusingeabudu chochote badala Yake, sisi wala
baba zetu, wala tusingeharamisha chochote bila Yeye’.
Hivyo hivyo walifanya waliokuwa kabla yao. Hivi kuna kazi
nyingine juu ya mitume zaidi ya kufikisha (ujumbe) kwa
uwazi.

36. Na kwa hakika tulimtuma Mtume kwa kila taifa
kwamba mwabuduni Mwenyezi Mungu na kaeni mbali na
uovu na mwovu (Shetani). Basi miongoni mwao wapo ambao
Mwenyezi Mungu aliwaongoza, na miongoni mwao wapo
ambao upotovu ulikuwa hauepukiki kwao. Basi tembeeni
katika ardhi muone ulikuwaje mwisho wa wale walioona
haya ni uwongo. 37. Hata ukiwa na pupa ya kuwaongoza,
lakini Mwenyezi Mungu hamuongozi yule aliyeng’ang’ania
kupotea, wala hawatapata wa kuwakoa na hilo.

38. Na wanaapa kwa Mwenyezi Mungu kwa viapo vyao

vya nguvu (kwamba) Mwenyezi Mungu hatawafufua wafu. Kwani! Hii ahadi aliyojitwisha kuitekeleza kwa kweli, lakini watu wengi hawatambui. 39. (Lazima wafufuliwe) Ili awapambanulie wazi yale wanayotofautiana na ili waliomkana Mwenyezi Mungu watambue kwamba wao walikuwa waongo. 40. Kauli Yetu kwa kitu tunachokitaka kiwe, ni kukiambia tu: ‘iwe! Nacho kinakuwa’.

41. Na wale waliohama nyumba zao kwa ajili ya Mwenyezi Mungu baada ya kuonewa, hakika tutawaweka hapa duniani katika makazi mema. Lakini malipo ya Akhera ni makubwa zaidi, lau wangekuwa wanajua. 42. Hao ni wale wanosubiri na wakamtegemea Mola Wao Mlezi.

43. Na hatukutuma kabla yako ila wanaume tuliowapa ufunuo (wahyi). Basi waulizeni walionao ujumbe ikiwa nyinyi hamjui... 44. Ishara hizo zilizokuwa wazi na vitabu. Na tumekutumia wewe (Muhammad) pia ujumbe ili uwabainishie watu yale waliyoteremshiwa, huenda wakafikiria.

45. Hivi wanaosuka njama za uovu wanaamini vipi kwamba Mwenyezi Mungu hatawadidimiza ardhini au haitawajia adhabu kutoka wasipopatarajia? 46. Au hatawatia nguvuni katika nyendo zao na wasiweze kuponyoka? 47. Au awatie mikononi kwa kuwaacha wamalizike kidogo kidogo (kwa uzee na kifo)? Kwani hakika Mola Wenu Mlezi ni Mpole, Mwenye huruma.

48. Hivi hawavioni vitu alivyoviumba Mwenyezi Mungu, vivuli vyake vikielekea kuliani na kushotoni vikimsujudia Mwenyezi Mungu na huku vikinyenyekea mno? 49. Na vinamsujudia Mwenyezi Mungu vyote vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini miongoni mwa wanyama, Malaika...

na havifanyi kiburi. 50. Vyote vinamhofia Mola Wao Mlezi,
mwenye Utukufu juu yao, na hutenda wanavyoamriwa.
51. Na Mwenyezi Mungu amesema: ‘Msiwe na miungu
wawili kuwaabudu. Hakika Yeye ni Mungu Mmoja tu.
Mniogope Mimi pekee’. 52. Ni Vyake vilivyomo mbinguni
na ardhini, na ni kwake tu wajibu (wenu) daima. Je, mtamcha
mwingine asiyekuwa Mwenyezi Mungu?
53. Na neema yoyote mliyo nayo inatoka kwa Mwenyezi
Mungu. Kisha ikiwagusa shida mnamlilia Yeye. 54, Kisha
anapowaondolea shida, kundi moja miongoni mwenu
linamshirikisha Mola Wao. 55. (Wakionesha) kukana neema
tulizowapa. Ili wakufuru tuliyowapa. Basi stareheni. Punde
hivi mtajua. 56. Na wanawapa wasiowajua kamwe (masanamu)
fungu katika tunavyowaruzuku! Wallahi! Hakika mtaulizwa
hayo mliyokuwa mkiyazua.
57. Na wanamfanya Mwenyezi Mungu ati ana mabinti.
Ametakata na hayo! Na kwa wao wenyewe wanajichagulia
wanavyovitamani (watoto wa kiume).. 58. Na mmoja wao
akibashiriwa msichana uso wake unasawijika, naye hujaa
hasira. 59. Anajificha asionekane na watu kwa ubaya wa
aliyobashiriwa! Je, akae naye pamoja na fedheha au amfukie
mchangani. Doh! Ubaya ulioje huo wa wanavyoamua!
60. Kwa wale wasioamini Akhera hupigiwa mfano wa uovu,
lakini kwa Mwenyezi Mungu hupigiwa mfano wa kilele cha
utukufu, na Yeye ni Mwenye nguvu, Mwenye hekima.
61. Lau Mwenyezi Mungu angewaadhibu watu kwa makosa
yao, asingemwacha juu ya mgogo wa ardhi kiumbe yeyote.
Lakini anawaakhirisha mpaka muda uliowekwa. Utakapofika
muda wao hawatakawia hata saa moja wala hawatatangulia.
62. Humpachikia Mwenyezi Mungu (kila) wakichukiacho!

Kisha ndimi zao zaeleza uwongo kwamba wao watapata mazuri tu! Hapana shaka kwamba wanastahiki moto, na watakuwa wa mwanzo kutangulizwa humo.

[63.] Wallahi! Tulituma Mitume kwa mataifa yaliyokuwepo huko nyuma kabla yako. Lakini shetani aliwapambia vitendo vyao. Huyo hivi leo ndiye kipenzi chao. Basi watapata adhabu kali. [64.] Na hatukukuteremshia Kitabu isipokuwa ili uwabainishie yale ambayo wanatofautiana, na ili kiwe mwongozo na rehema kwa watu wanaoamini.

[65.] Na Mwenyezi Mungu ameteremsha maji kutoka mawinguni na kwayo akaipa uhai ardhi baada ya kufa kwake. Hakika katika hayo kuna ishara kwa watu wanaosikia.

[66.] Na kweli nyinyi mnapata mazingatio katika (hawa) wanyama muwafugao. Kutokana na vilivyomo katika matumbo yao, vilivyopo baina ya kinyesi na damu, tunawanywesha maziwa safi, ya ladha murua kwa wanaoyanywa. [67.] Na kutokana na matunda ya mitende na mizabibu mnatengeneza vileo na chakula kizuri. Hakika katika hayo kuna ishara kwa watu wanaotumia akili.

[68.] Na Mola Wako Mlezi akamfunza nyuki kuwa: 'ujenge sega lako katika milima, na katika miti na katika makazi ya watu'. [69.]'Kisha ule kutoka aina zote za matunda na upite kwa uhodari kwenye njia ulizorahisishiwa na Mola wako Mlezi: kitatoka katika matumbo yao kinywaji chenye rangi mbali, ndani yake kuna cha kuwaponya watu. Hakika katika haya kuna ishara kwa watu wanaofikiri'.

[70.] Na Mwenyezi Mungu anawaumba kisha hutwaa uhai wenu. Miongoni mwenu yupo anayerudishwa kwenye umri dhaifu kabisa, hadi akawa hajui kitu chochote baada ya ujuzi

(aliokuwa nao). Hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi, Mwenye
uwezo.

71. Na Mwenyezi Mungu amewapendelea baadhi yenu
kuliko wengine katika riziki. Wale waliopendelewa hawawezi
kuzirudisha riziki zao kwa (watumwa) ambao imewamiliki
mikono yao ya kulia, ili wawe sawa katika riziki hiyo. Basi
je, wanazikataa neema za Mwenyezi Mungu?

72. Na Mwenyezi Mungu amewaumbia wake kutokana
na nyinyi wenyewe. Na akawajaalia kutoka kwa wake zenu
watoto na wajukuu na akawaruzuku vitu vizuri. Ni vipi kuwa
wanaamini upotofu na wanakanusha neema za Mwenyezi
Mungu? 73. Na badala ya Mwenyezi Mungu wanaabudu
wasiokuwa na mamlaka yeyote juu ya riziki zao kutoka
mbinguni na ardhini, wala hawana uwezo wowote. 74. Basi
msizue mifano kwa (kuifananisha na) Mwenyezi Mungu.
Hakika Mwenyezi Mungu anajua na nyinyi hamjui.

75 Mwenyezi Mungu amepiga mfano wa mtumwa mwenye
kumilikiwa, asiyeweza chochote, na mwingine tuliyemruzuku
riziki njema inayotoka Kwetu, naye anatoa katika riziki hiyo
kwa siri na kwa dhahiri. Je, wanalingana? Sifa njema zote ni
za Mwenyezi Mungu; bali wengi wao hawajui.

76. Na Mwenyezi Mungu anapiga mfano wa watu wawili.
Mmoja wao ni bubu hawezi chochote, naye ni mzigo kwa
bwana wake. Popote anapomuelekeza haleti kheri. Je, huyo
anaweza kuwa sawa na yule anayeamrisha uadilifu, naye
yuko juu ya njia iliyonyooka?

77. Mwenyezi Mungu ana siri zote za mbingu na ardhi. Na
uamuzi wa kuleta Kiyama ni kama kupepesa kwa jicho tu au
upesi zaidi. Hakika Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kila
kitu.

78. Na Mwenyezi Mungu amewatoa matumboni mwa mama zenu hamjui kitu. Na akawapa uwezo wa kusikia na kuona na akili na hisia ili mpate kushukuru.

79. Hivi hawawaoni ndege waliowezeshwa katikati ya anga? Hakuna anayewashika huko isipokuwa Mwenyezi Mungu. Hakika katika haya kuna ishara kwa watu wanaoamini.
80. Na ni Mwenyezi Mungu ambaye amewafanyia makazi yenu yawe ni mahali pa amani na utulivu. Na akawafanyia kutokana na ngozi za wanyama wenu nyumba mnazoziona nyepesi siku ya kusafiri kwenu na siku ya kutua kwenu. Na katika sufu zao na manyoya yao na nywele zao mnatengeneza vyombo na vifaa vya kutumia kwa muda.

81. Na Mwenyezi Mungu amewafanyia vivuli katika alivyoviumba na amewafanyia makazi katika milima na amewafanyia nguo za kuwakinga na joto na nguo za kuwakinga na vita vyenu. Ndio hivyo anatimiza neema Zake kwenu ili mpate kutii amri zake (kusilimu).
82. Na kama wakigeuka nyuma, basi lililo juu yako ni kufikisha tu ujumbe ulio wazi.
83. Wanazijua neema za Mwenyezi Mungu kisha wanazikanusha. Na wengi wao ni wakana neema.

84. Siku tutakapomwinua shahidi katika kila umma, kisha hawataruhusiwa wale waliomkana Mwenyezi Mungu wala hawataachiwa kutaka radhi.
85. Na waliodhulumu watakapoiona adhabu hawatapunguziwa wala hawatapewa muda.

86. Na wale walioshirikisha watakapowaona wale waliowashirikisha watasema: 'Mola Wetu Mlezi! Hawa ndio washirika wetu tuliokuwa tukiwaomba badala Yako'. Ndipo na wao watakapowatupia kauli: 'Kwa kweli nyinyi ni waongo'.
87. Na siku hiyo watasalimu amri mbele ya

Mwenyezi Mungu na yatawapotea waliyokuwa wakiyazua.
88. Wale waliomkana Mwenyezi Mungu na wawakazuia watu njia ya Mwenyezi Mungu tutawazidishia adhabu juu ya adhabu kwa walivyokuwa wakieneza ubaya.

89. Na (wakumbushe) siku tutakapomwinua kutoka kila taifa shahidi miongoni mwao kushuhudia dhidi yao, na tukakuleta wewe uwe shahidi juu yao hao. Na tumekuteremshia Kitabu hiki kubainisha kila kitu, na ni mwongozo na bishara njema kwa kwa waliojisalimisha kwa Mwenyezi Mungu (Waislamu).

90. Hakika Mwenyezi Mungu anaamrisha kutenda haki na wema na kuwapa jamaa na anakataza uchafu na uovu na dhulma. Anawaonya ili mpate kuonyeka.

91. Na tekelezeni ahadi ya Mwenyezi Mungu mnapoahidi; wala msivunje viapo baada ya kuvithibitisha, ilhali mmekwishamfanya Mwenyezi Mungu ndiye Mdhamini Wenu. Hakika Mwenyezi Mungu anayajua mnayoyafanya.
92. Wala msiwe kama mwanamke anayefumua msuko wake baada ya kwisha usokota ukawa mgumu. Mnavifanya viapo vyenu kuwa njia ya kudanganyana baina yenu; kwa kuwa taifa moja eti lina nguvu zaidi kuliko jingine (ndipo linachangua). Hakika Mwenyezi Mungu anawajaribu kwayo na hakika atawabainishia siku ya Kiyama yale mliyokuwa mkitofautiana.

93. Na lau Mwenyezi Mungu angetaka bila shaka angewafanyeni taifa moja, lakini humwacha apotee amtakaye na humwongoa anayemtaka. Na hakika mtaulizwa kuhusu yale mliyokuwa mkiyafanya.

94. Wala msivifanye viapo vyenu ni njia ya kudanganyana baina yenu. Usije mguu ukateleza baada ya kuwa imara,

na mkaonja maovu kwa sababu ya kuzuia kwenu njia ya Mwenyezi Mungu na mkastahiki adhabu kubwa. 95. Wala msiuze Agano la Mwenyezi Mungu kwa thamani ndogo (ya dunia). Hakika kilicho kwa Mwenyezi Mungu ndio bora kwenu ikiwa mnajua.

96. Mlivyo navyo vitakwisha na vilivyoko kwa Mwenyezi Mungu ndivyo vitakavyobaki. Na kwa hakika tutawalipa waliosubiri ujira wao kwa mazuri zaidi ya waliyokuwa wakiyafanya. 97. Mwenye kutenda mema, mwanamume au mwanamke, naye akawa ni muumini, tutampa uhai mzuri; na tutawapa ujira wao kwa mazuri zaidi ya waliyokuwa wakiyafanya.

98. Unaposoma Qur'an muombe Mwenyezi Mungu akulinde na shetani aliyefukuzwa. 99. Hakika yeye hana madaraka juu ya walioamini na wakamtegemea Mola Wao. 100. Hakika madaraka yake yako juu ya wale tu wanaomfanya rafiki, na wale wanaoshirikiana naye.

101. Na tunapoibadilisha Aya mahali pa Aya nyingine- na Mwenyezi Mungu anajua anayoteremsha- wao husema: 'wewe ni mzushi'. Bali wengi wao hawajui. 102. Sema: Ameiteremsha Roho Mtakatifu kutoka kwa Mola Wako Mlezi kwa ukweli, ili kuwafanya walioamini waendelee kushikamana na msimamo wao, na kuwa ni mwongozo na bishara njema kwa Waislamu.

103. Na sisi hakika tunajua kwamba wanasema: 'yupo mtu anayemfundisha'. Lakini lugha ya huyo ambaye wanamuashiria kwa ubaya wao ni ya Kiajemi na hii ni lugha ya kiarabu bayana. 104 .Hakika wale ambao hawaziamini Aya za Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu hawaongozi, nao watapata adhabu chungu. 105. Hakika wanaozua uwongo ni

wale tu wasioziamini Aya za Mwenyezi Mungu, na hao ndio waongo.

106. Anayemkana Mwenyezi Mungu baada ya kumwamini- isipokuwa aliyelazimishwa na hali ya kuwa moyo wake umetulia juu ya Imani- lakini aliyekifungulia kifua chake kwa kufuru, basi hao ghadhabu ya Mwenyezi Mungu iko juu yao na watapata adhabu kubwa. 107. Hiyo ni kwa sababu wao wanapendelea maisha ya dunia kuliko ya akhera. Na Mwenyezi Mungu hawaongozi watu makafiri. 108. Hao ndio ambao Mwenyezi Mungu ameziziba nyoyo zao na masikio yao; na hao ndio wenye kughafilika. 109. Hapana shaka kwamba wao ndio wenye kuhasirika Akhera.

110. Kisha hakika Mola Wako kwa wale waliohama baada ya kuteswa kisha wakapigania dini na wakasubiri, bila shaka Mola Wako Mlezi baada ya hayo ni Mwingi wa maghufira kwao, Mwenye kurehemu. 111. Siku ambayo kila nafsi itakuja kujitetea. Na kila nafsi italipwa sawa na yale iliyoyafanya, nao hawatadhulumiwa.

112. Na Mwenyezi Mungu amepiga mfano wa mji uliokuwa na amani na utulivu, riziki yake ikifika hapo kwa wingi kutoka kila mahali. Lakini wakakufuru neema za Mwenyezi Mungu; kwa hiyo Mwenyezi Mungu akauvika mji huo vazi la njaa na hofu kwa sababu ya yale waliyokuwa wakiyafanya. 113. Na alikwishawajia Mtume kutoka miongoni mwao, lakini wakamkadhibisha, basi ikawafikia adhabu wakiwa wanadhulumu.

114. Basi kuleni katika vile alivyowaruzuku Mwenyezi Mungu vilivyo halali na vizuri. Na shukuruni neema ya Mwenyezi Mungu ikiwa mnamwabudu Yeye tu. 115. Hakika amewaharamishia (nyama ya) mzoga na damu na nyama ya

nguruwe na kilichosomewa jina la asiyekuwa Mwenyezi Mungu (wakati wa kuchinja). Basi aliyefikwa na dharura bila kutamani wala kupitisha kiasi, hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa maghufira, Mwenye kurehemu.

116. Wala msiseme uwongo kwa kuropokwa na ndimi zenu: 'hiki ni halali na hiki ni haramu', mkimzulia uwongo Mwenyezi Mungu. Hakika wanaomzulia uwongo Mwenyezi Mungu hawatafanikiwa. 117. Ni starehe ya muda mfupi tu, nao watapata adhabu chungu.

118. Na Mayahudi tuliwaharamishia tuliyokusimulia hapo nyuma. Na hatukuwadhulumu, lakini walijidhulumu wenyewe. 119. Kisha hakika Mola Wako Mlezi, kwa waliotenda uovu kwa kutojua kisha wakatubu baada ya hayo na wakajirekebisha, hakika Mola Wako Mlezi ni Mwingi wa maghufira kwao, Mwenye kuwaonea huruma.

120. Hakika Ibrahim alikuwa ni taifa zima, mnyenyekevu kwa Mwenyezi Mungu, mnyoofu, wala hakuwa katika mapagani. 121. Mwenye kuzishukuru neema Zake, alimteua na akamwongoza kwenye njia iliyonyooka. 122. Na tukampa wema hapa duniani na hakika yeye Akhera atakuwa miongoni mwa watu wema. 123. Kisha tukakufunulia ya kwamba ufuate mila ya Ibrahim mnyoofu na hakuwa katika mapagani.

124. Hakika siku ya Sabato iliwekwa kwa wale waliotofautiana juu yake. Na hakika Mola Wako Mlezi bila shaka atahukumu kati yao siku ya Kiyama katika yale waliyohitalifiana juu yake.

125. Waite kwenye njia ya Mola Wako Mlezi kwa hekima na mawaidha mazuri na ujadiliane nao kwa namna iliyo bora zaidi. Hakika Mola Wako Mlezi ndiye anayemjua

zaidi aliyepotea njia yake na Yeye ndiye anayewajua zaidi walioongoka.

126. Na kama mkilipiza basi lipizeni kama mlivyofanyiwa. Na kama mtakuwa na subira, hakika hivyo ni bora zaidi kwa wanaoweza kusubiri. 127. Fanya subira. Na kusubiri kwako si kwa yeyote ila kwa Mwenyezi Mungu, wala usihuzunike wala usiwe katika dhiki kwa hila wanazozifanya. 128. Hakika Mwenyezi Mungu yuko pamoja na wanaomcha na wale walio wema.

17. Sura Bani Israil

# SURA YA WANA WA ISRAELI

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 Ametakata na mabaya yote ambaye alimpeleka mja wake usiku kutoka Msikiti Mtukufu mpaka Msikiti wa Mbali ambao tumevibariki vilivyo kandoni mwake, ili tumuoneshe baadhi ya ishara Zetu. Hakika Yeye ni Mwenye kusikia, Mwenye kuona.

2 Na tukampa Musa (Moses) Kitabu na tukakifanya ni mwongozo kwa Wana wa Israeli, (tukamwamuru) ‘msimfanye asiyekuwa Mimi kuwa ndiye mnayemtegemea’
3 Enyi kizazi (kilichotokana na wale) tuliowachukua pamoja na Nuh (Noah)! Hakika yeye alikuwa mja mwenye shukrani.

4. Na tuliwapa Wana wa Israel onyo la wazi katika Kitabu hicho, kwamba mtafanya uharibifu ardhini mara mbili, na mtakuwa na kiburi kupita kiasi! 5. Pindi muda wa onyo la mwazo ulipopita, tuliwatumia waja wetu, hodari sana kwa

vita. Hawa waliingia mpaka ndani ya nyumba zenu. Na onyo hili tayari limekwishatekelezwa. [6.] Kisha tukawarudishia nguvu zenu dhidi yao na tukawapa rasilimali na watoto, na tukawafanya muwe wengi mno kwa idadi.

[7.] Mkifanya wema mnajifanyia wenyewe na mkifanya ubaya mnajifanyia (dhidi yenu) wenyewe. Na ulipopita muda wa onyo la mwisho (tuliwaruhusu adui zenu) waziumbue nyuso zenu na waingie katika Hekalu lenu, kama walivyoiingia mara ya kwanza, na wakafanya uharibifu mkubwa kwa kila walichokiteka. [8.] Huenda Mola Wenu Mlezi (bado) akawaonea huruma. Lakini mkirudia (uovu wenu) Nasi tutarudia (adhabu)! Na tumeifanya Jahanam gereza kwa wanaokana Imani ya Mungu.[8]

[9.] Hakika hii Qur'an inaongoza kwenye yaliyonyooka kabisa na inawabashiria waumini ambao wanatenda mema kwamba watapata malipo makubwa. [10.] Na wale wasioamini Akhera tumewaandalia adhabu chungu.

[11.] Maombi ambayo mwanadamu (ingebidi) aombe kheri, yeye huomba shari! Kwa vile binadamu ni mwenye pupa. [12.] Na tumeufanya usiku na mchana kuwa ni ishara mbili. Ishara ya usiku tukaiziba, na tukaifanya ishara ya mchana

---

8. Hapa Mwenyezi Mungu anazungumzia matukio ya kihistoria yaliyowafika Mayahudi. Kuadhibiwa kwao kwa kupelekwa utumwani Misri, kulitokana na kuwakana mitume walioletwa. Onyo la kwanza ni pale Nebuchadnezzar alipowateka na kuwapeleka Babylon. Wakarudi kutoka utumwani Babylon mwaka 520 BC. Walipomkana Nabii Issa, ndipo onyo la pili likatekelezwa na Warumi lililopelekea Wayahudi kutawanyika tena duniani. Aya inasema kuwa walisamehewa hapo nyuma, lakini wakiendela tena na ufisadi na ujeuri, huenda wakaadhibiwa tena- Mfasiri.

ya kuangaza, ili muweze kutafuta neema kutoka Mola Wenu Mlezi, na mpate kujua idadi ya miaka na hesabu. Na kila kitu tumekifafanua kwa kina.

13. Hatima ya kila binadamu tumeifunga katika shingo yake. Na siku ya Kiyama tutamtolea kitabu atakachokikuta kimekunjuliwa. 14. (Ataambiwa) Soma kitabu chako! Nafsi yako (mwenyewe) hii leo inakutosha kukuwajibisha. 15. Anayeongoka hakika anaongoka kwa faida yake mwenyewe. Na anayepotea anapotea kwa hasara yake mwenyewe. Wala habebi mbebaji yeyote mzigo wa mwengine. Wala sisi hatumwadhibu yoyote mpaka tupeleke Mtume.

16. Tunapotaka kuangamiza mji (watu wake). (Kwanza) Hutuma onyo kwa wale waliopewa starehe za maisha katika mji huo, lakini bado wakaendelea kufanya maovu humo. Hapo hukumu huthibiti kwa mji huo, ndipo twaubomoa kabisa. 17. Na vizazi vingapi tumeviangamiza baada ya Nuh (Noah)? Na Mola Wako Mlezi anatosha kuwa ni Mwenye habari na Mwenye kujua dhambi za waja wake.

18. Anayetaka vipitavyo (dunia) tutafanya haraka kumpa hapa hapa tunavyovitaka kwa tunayemtaka; kisha tunamwekea Jahannam; ataiingia humo hali kuwa mwenye kupatwa na aibu, mwenye kukataliwa. 19. Na mwenye kutaka ya (Akhera) na akaihangaikia kweli kweli huku akiwa ni mumini, basi hao jitihada yao itakubaliwa.

20. Wote hao, hawa na (pia) wale, tunawakabidhi bure vipawa vya Mola wako Mlezi, kwani vipawa vya Mola wako Mlezi havikuzuiwa (kwa yeyote). 21. Angalia jinsi tulivyowapa zaidi baadhi yao kuliko wengine. Na Akhera ni yenye daraja kubwa zaidi na neema kubwa zaidi.

22. Usimfanye mungu mwingine pamoja na Mwenyezi
Mungu, usije ukabaki ni mwenye kupata aibu, ulietupiliwa
mbali. 23. Na Mola wako ameamrisha kuwa msimwabudu
yoyote ila Yeye tu, na muwatendee wema wazazi wawili.
Endapo mmoja au wote wawili wanafikia uzeeni, nawe uhai,
basi usiwaambie (hata) akh! Wala usiwakemee. Na zungumza
nao kwa heshima. 24. Na uwainamishie bawa (lako) la
unyenyekevu kwa kuwaonea huruma na useme: ‘Mola wangu
Mlezi! Waonee huruma kama walivyonitunza (kwa mapenzi)
nilipokuwa mtoto.’ 25. Mola wenu ni Mjuzi zaidi wa yaliyo
katika nafsi zenu. Ikiwa nyinyi mtakuwa wema, hakika Yeye
ni Mwenye kughufiria wanaorejea kwake.

26. Na mpe jamaa wa karibu haki yake na maskini na msafiri,
wala usifanye ubadhirifu. 27. Hakika wabadhirifu wamekuwa
ni ndugu wa mashetani, na shetani ni mwenye kumkufuru
mno Mola Wake. 28. Na hata ikibidi kuwapa nyongo kwa
kutaka rehema ya Mola Wako Mlezi unayoitaraji, pia sema
nao maneno laini.

29. Wala usiufanye mkono Wako umefungwa shingoni
mwako, wala usiukunjue wote kabisa, ukabaki mwenye
kulaumiwa, mwenye kuishiwa. 30. Hakika Mola Wako
Mlezi humkunjulia riziki amtakaye na humpimia kwa kiasi
amtakaye. Hakika Yeye kwa waja Wake ni Mwenye habari,
aonaye.

31. Wala msiwaue watoto wenu kwa kuogopa umaskini,
Sisi tunawaruzuku nyinyi na wao. Hakika kuwaua ni hatia
kubwa. 32. Wala msiikurubie zina. Hakika hiyo ni uchafu na
njia mbaya.

33. Wala msiiue nafsi ambayo Mwenyezi Mungu amekataza
(kuiua) isipokuwa kwa (sababu ya) haki. Na aliyeuawa kwa

kudhulumiwa, basi tumempa madaraka mrithi wake (ya kulipiza kisasi au kusamehe), lakini asivuke mpaka katika kuuwa, kwani hakika yeye anasaidiwa (na sheria).

34. Wala msiikaribie mali ya yatima isipokuwa kwa njia bora zaidi (kuizidisha), mpaka afikie kukomaa kwake. Na tekelezeni ahadi. Hakika ahadi itaulizwa (siku ya Kiyama)
. 35. Na timizeni kipimo mnapopima, na pimeni kwa mizani zilizo sawa. Hivyo ni vizuri kwenu, na hatimaye ndiyo yenye faida zaidi.

36. Wala usifuatilie ambalo huna ujuzi nalo. Hakika masikio na macho na moyo, hivyo vyote vitaulizwa. 37. Wala
usitembee katika Ardhi kwa mikogo. Hakika wewe huwezi kuipasua ardhi wala kufikia urefu wa milima. 38. Hayo yote
ubaya wake ni wenye kuchukiza mbele ya Mola Wako.

39. Hayo ni katika hekima alizokupa wahyi Mola Wako Mlezi. Usimfanye mungu mwingine pamoja na Mwenyezi Mungu, usije ukatupwa katika Jahannam ukiwa mwenye kulaumiwa, mwenye kufukuzwa.

40. Je, Mola Wenu amewachagulia watoto wa kiume na Yeye akawafanya Malaika ni mabinti zake? Hakika nyinyi mnasema maneno mazito! 41. Hakika tumebainisha (vitu)
katika hii Qur'an kwa njia mbali mbali ili wapate kuonyeka. Lakini haiwazidishii isipokuwa kujiweka mbali (na haki)
42. Sema lau kama wangelikuwa pamoja Naye miungu mingine kama wasemavyo, basi wangelitafuta njia ya kumfikia Mola Mwenye Kiti cha Enzi. 43. Ametakasika na ametukuka juu
kabisa na hayo wanayoyasema. 44. Mbingu zote saba na ardhi
na vilivyomo ndani yake vinaimba kuutakasa Utukufu wake. Na hakuna kitu chochote ila kinaimba sifa zake, lakini ninyi

hamfahamu namna gani vinautakasa Utukufu wake. Hakika Yeye ni Mpole Mwingi wa maghufira.

45. Na unaposoma Qur'an tunaweka baina yako na ya wale wasioamini Akhera pazia linalowafunika. 46. Na tunaweka mifuniko juu ya nyoyo zao, inayowazuia kuifahamu (Qur'an), na tunaweka kwenye masikio yao uziwi. Na unapomtaja Mola Wako peke Yake katika Qur'an, wao hugeuka nyuma wakaenda zao.

47. Sisi tunajua vyema kabisa sababu wanayosikilizia wanapokusikiliza na wanapokuwa faragha wenyewe. Husema hao waovu: 'nyinyi hamumfuati isipokuwa mtu aliyerogwa'. 48. Tazama jinsi wanavyokupigia mfano. Lakini wamepotea, na kamwe hawawezi kuipata njia.

49. Na wanasema: hivi tutakapokuwa mifupa na mifupa iliyochakaa, je tutafufuliwa na kuwa viumbe wapya? 50. Sema: kuweni hata mawe au chuma. 51. Au umbo lolote mnaloliona kubwa katika akili zenu. Watasema: Ni nani basi atakayeturudisha tena? Sema: Ni huyo aliyewaumba mara ya kwanza! Watakutikisia vichwa vyao. Na watasema: ni lini hilo? Sema: Asaa likawa karibu. 52. (Litakuwa) Siku atakayowaita, nanyi mkamwitikia kwa kumsifu. Na mkadhani kuwa hamkukaa (kaburini) ila muda mchache tu.

53. Waambie waja Wangu waseme maneno mazuri. Kwani shetani huchochea ugomvi baina yao. Hakika shetani ni adui aliye dhahiri kwa mtu.

54. Mola Wenu anawajua vilivyo, akipenda atawaonea huruma na akipenda atawaadhibu. Na wala hatukukutuma ili uwe mfuatiaji wa mambo yao. 55. Na Mola Wako Mlezi anawajua zaidi walio mbinguni na waliomo ardhini. Na

hakika tumewapendelea baadhi ya manabii kuliko wengine;
na tulimpa Daud (David) Zaburi (psalms).
56. Sema: 'Waombeni hao mnaowadhania badala Yake.
Hawawezi kamwe kuwaondolea shida wala kuzibadilisha'.
57. Hao wanawaomba, wao wenyewe wanatafuta njia ya
kujikurubisha kwa Mola Wao Mlezi, hata walio karibu zaidi
(kwake) miongoni mwao. Na wanataraji rehema Zake na
wanaihofu adhabu Yake. Hakika adhabu ya Mola Wako ni ya
kuchukuliwa hadhari. 58. Hakuna (watu wa) mji wowote ila
Sisi tutawaangamiza kabla ya Siku ya Kiyama au tutawapa
adhabu kali. Haya yamekwisha andikwa kwenye Kitabu.
59. Na hapana kinachotuzuia kupeleka miujiza ila ni kuwa
watu wa zamani waliikanusha. Na Wathamudi tuliwapa
ngamia jike ili wafungue macho yao , lakini wakamfanya
vibaya. Nasi hatupeleki ishara ila kwa ajili ya kuhadharisha.
60. Na kumbuka tulipokwambia: 'Hakika Mola Wako
amekwishawazunguka hao watu'. Na hatukuifanya ndoto
tuliyokuonyesha isipokuwa kuwajaribu watu na ni mti
uliolaaniwa (uliotajwa) katika Qur'an. Na tunawahadharisha,
lakini hilo haliwaongezi isipokuwa uasi kupindukia!
61. Na kumbuka pale tulipowaambia Malaika: 'Inameni
kumpa heshima Adam!' Wote wakamwinamia isipokuwa
Iblis, alisema: Je, nimwinamie uliyemwumba kwa udongo?
62. Akasema: Unamwona huyu ambaye umempa heshima
zaidi kuliko mimi? Kama utanipa muda mpaka Siku ya
Kiyama, bila shaka nitakiburuza kizazi chake isipokuwa
wachache tu.
63. Akasema: Ondoka! Atakayekufuata katika wao, basi
Jahannam itakuwa ndio malipo yenu, malipo yenye kutimia.
64. Na wachochee uwawezao katika wao kwa sauti yako, na

wakusanyie jeshi lako la wapanda farasi na wendao kwa miguu na shirikiana nao katika mali na watoto na uwaahidi. Na shetani hatoi ahadi isipokuwa ya udanganyifu. 65. Hakika waja Wangu hasa wewe huna mamlaka juu yao, na Mola Wako anatosha kuwa ni wa kutegemewa.

66. Mola Wenu Mlezi ndiye anayewafanyia majahazi yaende shwari baharini kwa ajili yenu, ili mwende kutafuta neema zake. Hakika Yeye ni Mwenye kuwaonea huruma mno. 67. Na iwagusapo shida baharini, hao mnaowaomba kinyume chake, hupotea (wakawaacha). Anapowaokoa mkafika nchi kavu, mnageuka. Ama mwanadamu huwa mtovu wa shukrani mno!

68. Je, mnajihisi amani kuwa hatawadidimiza chini ya ardhi (muwapo) upande wa nchi kavu, au hatawaletea kimbunga cha kokoto, kisha msipate wa kumtegemea? 69. Au mnajihisi amani kuwa hatawarudisha tena humo (baharini), awapelekee dhoruba ya upepo, awazamishe kwa sababu ya utovu wenu wa shukrani, kisha msipate wa kutufuatilia Sisi juu ya hilo..

70. Hakika tumewapa heshima kuu wanaadamu na tukawabeba nchi kavu na baharini na tukawaruzuku vitu vizuri na tukawapendelea juu ya viumbe wengi tuliowaumba kwa kuwapa neema nyingi.

71 Siku tutakapokiita kila (kikundi cha) watu kwa yule kiongozi wao (waliyekuwa wakimfuata). Basi atakayepewa kitabu chake kwa mkono wake wa kuume, hao watasoma kitabu chao wala hawatadhulumiwa hata (kichache kama) uzi wa kokwa yatende. 72 Lakini aliyekuwa kipofu hapa duniani (kwa kutoiona haki) , basi Akhera atakuwa kipofu na aliyepotea zaidi njia.

73. Na hakika walikaribia kukushawishi uache tuliyokufunulia katika wahyi, ili utuzushie mengine. Na hapo

wangelikufanya rafiki mwandani. 74. Lau hatungekuweka imara, ulikuwa umekaribia kuwaelekea kidogo. 75. Hapo basi, tungelikuonjesha (adhabu) maradufu ya uhai, na (Adhabu) maradufu ya mauti; kisha usingelipata wa kukunusuru nasi.

76. Na lengo lao lilikuwa ni kukutisha uiache ardhi yako ili wakufukuze nchi. Lakini wasingeweza kukaa baada yako ila muda mchache tu. 77. Huo ndiyo mwenendo kwa Mitume tuliowatuma kabla yako. Na wala hutapata mabadiliko katika mwenendo Wetu

78. Simamisha Swala linapopinduka jua mpaka giza la usiku, na Qur'an ya alfajiri; hakika Qur'an ya alfajiri ni yenye kushuhudiwa daima. 79. Na amka usiku kwa ibada, ambayo ni ziada kwako. Punde hivi Mola Wako Mlezi atakuinua kwenye cheo kinachosifika.

80. Na sema: Mola Wangu Mlezi! Niingize kupitia lango la ukweli na heshima, na unitoe kupitia lango la ukweli na heshima. Na unipe madaraka kutoka Kwako yanisaidie. 81. Na sema: Ukweli (sasa) umefika na uwongo umetoweka. Hakika uwongo ni wenye kutoweka.

82. Na tunateremsha katika Qur'an ambayo ni tiba na rehema. Wala haiwazidishii waovu isipokuwa hasara.

83. Na tunapomneemesha mtu hugeuka na kujitenga kando (asije kwetu), na inapomgusa shari hukata tamaa. 84. Sema: kila mtu anafanya kwa namna yake. Na Mola Wenu Mlezi tu ndiye anamjua nani aliyeongoka katika njia.

85. Wanakuuliza kuhusu roho. Sema: roho ni suala la Mola wangu (pekee). Nanyi hamkupewa elimu isipokuwa kidogo tu.

86. Lau tungependa tungeyaondoa hayo tuliyokufunulia kwa Wahyi, kisha usingepata mwakilishi yeyote wa

kulalamikia kesi yako dhidi Yetu. [87.] Isipokuwa huruma kutoka kwa Mola wako Mlezi. Kwani neema zake kwako ni kubwa mno. [88.] Sema: Lau wangekusanyika watu na majinni, ili walete mfano wa hii Qur'an, hawawezi kuleta mfano wake, hata wangesaidiana.

[89.] Na hakika tumewaelezea watu hii Qur'an kwa (kuwatolea) mifano mbali mbali. Lakini watu wengi wamekataa isipokuwa kukanusha tu. [90.] Na walisema: Hatutakuamini mpaka utuchimbulie chemchemi za maji katika ardhi hii. [91.] Au uwe na kitalu cha mitende na mizabibu na ukipitishie mito ya maji kati yake inayomiminika. [92.] Au utuangushie mbingu vipande vipande juu yetu, kama ulivyodai, au utuletee Mwenyezi Mungu na Malaika ana kwa ana. [93.] Au uwe na nyumba iliyopambwa kwa dhahabu au upande mbinguni (kwa ngazi). Na hata hivyo hatutaamini kupanda kwako huko mpaka ututeremshie Kitabu tukisome! Sema: ametakasika Mola Wangu Mlezi! Kwani mimi ni nani, isipokuwa ni mwanadamu, Mtume.

[94.] Kwani ni nini kilichowazuia watu kuamini pale ulipowajia mwongozo isipokuwa kusema: "Inakuwaje Mwenyezi Mungu apeleke mwanadamu (kama sisi) awe Mtume (wake)? [95.] Sema: Lau duniani wangekuwepo Malaika wanaotembea kwa utulivu na amani, bila shaka tungewateremshia Malaika kuwa Mtume wao. [96.] Sema: Mwenyezi Mungu anatosha kuwa mshuhuda baina yangu na nyinyi. Hakika Yeye anawajua vyema waja Wake na anawaona.

[97.] Na anayeongozwa na Mwenyezi Mungu ndiye anayeongoka na anayemwacha apotee, basi, hutawapatia wa kuwalinda asiyekuwa Yeye. Na tutawakusanya Siku ya

Kiyama hali ya kukokotwa juu ya nyuso zao, wakiwa vipofu,
mabubu na viziwi. Makazi yao ni Jahannam. Kila moto
ukianza kuzimika tutawazidishia kuuchochea uwake kwa
nguvu. 98. Hayo ni malipo yao kwamba wao walizikataa ishara
Zetu na wakasema: je, tutakapokuwa mifupa iliyochakaa,
tutafufuliwa kuwa umbo jipya?

99. Hawaoni kwamba Mwenyezi Mungu aliyeumba
mbingu na ardhi ni Mwenye uwezo wa kuumba mfano wao?
Na Yeye amewawekea muda usio na shaka yoyote, lakini
wafanya maovu hawataki isipokuwa kukanusha. 100. Sema,
lau mngelikuwa mnamiliki hazina za neema za Mola Wangu
Mlezi, basi mngezizuia kwa wa kuhofia kuzitumia. Kwani
binadamu (daima) ni mchoyo sana.

101. Hakika tulimpa Musa ishara tisa zilizo wazi. Waulize
wana wa Israel pale alipowafikia. Firauni (Pharaoh)
akamwambia: ‘mimi nakuona wewe Musa umerogwa’.
102. Musa akasema: Hakika wewe bila shaka unajua haya
hakuyateremsha isipokuwa Mola Mlezi wa mbingu na
Ardhi, kuwa ushahidi unaoonekana kwa macho. Na miye
nakuona wewe Firauni, umeangamia. 103. Basi Firauni
akataka kuwafukuza kutoka nchini, tukamzamisha yeye na
waliokuwa pamoja naye wote. 104. Na tukawaambia wana
wa Israel baadaye, ‘kaeni katika ardhi. Itakapokuja ahadi ya
Akhera tutawaleta nyote pamoja’.

105. Na kwa ukweli tumeiteremsha (Qur’an) na kwa ukweli
imeteremka. Na hatukukutuma ila uwe mwenye kutoa habari
njema (kwa waumini) na mwenye kuwaonya (wanaokana).
106. Na Qur’an tumeigawanya ili uwasomee watu kwa kituo;
na tumeiteremsha kidogo kidogo.

107. Sema, iaminini au msiiamini. Hakika wale waliopewa

elimu kabla yake, wanaposomewa, huporomoka kifudifudi wakisujudu. . [108.] Wanasema: 'Ametakasika Mola Wetu Mlezi!. Hakika ahadi ya Mola Wetu lazima itimizwe'. [109.] Na huporomoka kifudifudi huku wakilia, na inawazidishia unyenyekevu.

[110.]Sema, mwombeni Mwenyezi Mungu (Allah) au mwombeni Mwingi wa huruma (Rahman), kwa jina lolote mtakalomwita, Yeye ana majina mazuri. Wala usipaze sauti kwa swala yako, wala usiswali kimya kimya, bali fuata njia ya kati kati baina ya (mbili) hizo. [111.]Na sema, sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu ambaye hana mwana wala hana mshirika katika ufalme Wake, wala hahitajii wa kumsaidia kutokana na udhaifu, na mtukuze sana.

## 18. Surah Al-Kahf

## SURA YA 'WALIOJIFICHA' PANGONI

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

[1] Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu ambaye amemteremshia mja Wake Kitabu, ambacho hakuruhusu ndani yake kuwe na upindaji. [2] Kimenyooka sawa sawa, ili kitoe onyo kali kutoka Kwake, na kiwabashirie waumini watendao mema kwamba watapata ujira mzuri [3] Wakae humo milele. [4] Na kiwaonye wale wanaosema Mwenyezi Mungu amezaa mwana. [5] Si wao wala baba zao wana ujuzi wa jambo hili. Ni neno kubwa mno hilo litakalo vinywani mwao; hawasemi ila uongo tu.

[6] Usije ukaidhuru nafsi yako kwa ajili yao kwa kuwasikitikia

kuwa hawaamini ujumbe huu. [7] Hakika tumevifanya vilivyo katika ardhi kuwa ni pambo lake ili tuwajaribu ni nani kati yao mwenye vitendo vizuri zaidi. [8] Na hakika tutavifanya vilivyo juu yake kuwa vumbi, ardhi iliyopatwa na ukame.

[9.] Kwani unadhani kwamba watu wa pango na Maandishi (yaliyopo) walikuwa ni maajabu miongoni mwa ishara Zetu? [10.] Pale vijana walipokimbilia kwenye pango wakasema: 'Mola Wetu Mlezi! Tupe rehema itokayo Kwako na tutengezee jambo letu hili liwe sawa'. [11.] Basi tukayaziba masikio yao pangoni kwa miaka kadhaa wa kadhaa. [12.] Kisha tukawazindua ili tuwajaribu ni lipi kati ya makundi mawili lililohesabu sawa sawa muda waliokaa.

[13.] Sisi tunakusimulia habari zao kwa ukweli. Hakika hao ni vijana waliomwamini Mola Wao Mlezi na tukawazidisha uongofu. [14.] Na tukazitia nguvu nyoyo zao, pale waliposimama wakasema: Mola Wetu Mlezi ni Mola wa mbingu na ardhi. Kamwe hatutamuomba mungu mwingine badala Yake. Tukifanya hivyo, tutakuwa tumetamka neno lililokubuhu kabisa. [15.] Hawa jamaa zetu wamefanya waungu wengine badala Yake. Mbona hawaleti hoja ya wazi yenye mashiko juu ya hao? Ni nani afanyaye makosa makubwa kuliko yule amzuliaye Mwenyezi Mungu uongo?

[16.] (Wakashauriana)' basi mkishajitenga nao na vile wanavyoviabudu badala ya Mwenyezi Mungu, mkimbilie pangoni, Mola Wenu Mlezi atawafungulia rehema Yake na atawafanyia wepesi mambo yenu'.

[17.] Na utaliona jua linapochomoza linaelemea kuumeni mbali na pango lao; na linapokuchwa linawahepa kushotoni na wao wamo wamelala sehemu ya wazi katika pango hilo. Hayo ni katika ishara za Mwenyezi Mungu. Myu

ambaye Mwenyezi Mungu anamuongoza, yeye ndiye kweli aliyeongoka, na anayemwacha apotee hutampatia wa kumlinda amwongoze (njia sawa).

18. Na utawadhania wako macho kumbe wamelala, na tunawageuza-geuza kuume na kushoto, huku mbwa wao akiwa amenyoosha mikono yake mbele kizingitini. Lau ungeliwatokea bila shaka ungegeuka kuwakimbia, ukiwa umejazwa hofu.

19. Na kwa namna hiyo ndivyo tulivyowaamsha wapate kuulizana wao kwa wao. Akauliza msemaji wao: 'Mmekaa muda gani?' Wale wakajibu: 'Tumekaa siku moja au sehemu ya siku'. (Wakasemezana): 'Mola Wenu anajua zaidi muda mliokaa'. Hebu mtumeni mmoja wenu na hizi pesa zenu aende mjini akaangalie chakula gani kinachotufaa zaidi, awaletee chakula kiasi. Na awe mwangalifu, na asimzungumzie yeyote kutuhusu siye. 20. Kwani wao wakiwajua watawapiga mawe au watawarudisha katika utamaduni wao na hamtafanikiwa tena!

21. Na hivi ndivyo tulivyokifanya kisa chao kijulikane kwa watu ili wapate kujua kwamba ahadi ya Mwenyezi Mungu ni kweli na kwamba Kiyama hakina shaka kuja kwake. Kumbuka (pale wenyeji) walipokuwa wakibishana wao kwa wao juu ya jambo hili. Baadhi wakasema, 'jengeni juu yao jengo'. Mola Wao Mlezi anawajua zaidi hao. Wale walioshinda katika jambo hili wakasema: 'bila shaka tutajenga msikiti juu yao'.

22. Watasema, walikuwa watatu na wanne wao ni mbwa wao. Na watasema ni watano na wa sita wao ni mbwa wao, kwa kukisia tu yasiyojulikana. Na watasema ni saba na wa nane wao ni mbwa wao. Sema: 'Mola Wangu Mlezi ndiye anayejua zaidi idadi yao. Hawawajui isipokuwa wachache

tu. Basi usibishane juu yao isipokuwa mjadala katika mambo
yaliyo wazi. Wala usitake kujua maoni ya yeyote katika wao
juu ya vijana hao. 23. Wala kamwe usiseme juu ya jambo
lolote lile: ‘bila shaka nitalifanya hilo kesho’; 24. Isipokuwa
(kwa kuongeza) “inshallah” ‘apendapo Mwenyezi Mungu’.
Na mkumbuke Mola Wako Mlezi pale unaposahahu, na
sema: ‘Asaa Mola Wangu Mlezi akaniongoza hadi karibu
zaidi (na njia nyoofu) kuliko hivi’.

25. Na walikaa katika pango lao miaka mia tatu na
wakazidisha tisa. 26. Sema: Mwenyezi Mungu anajua zaidi
muda waliokaa. Ni Zake pekee siri za mbingu na za ardhi.
Uwazi ulioje wa kuona Kwake, na umadhubuti ulioje wa
usikizi wake! Hawana wa kuwalinda isipokuwa Yeye; wala
hamshirikishi yeyote katika hukumu Yake.

27. Na soma yaliyofunuliwa kwako katika Kitabu cha
Mola Wako Mlezi. Hapana wa kubadilisha maneno Yake.
Wala hutapata makimbilio isipokuwa Kwake. 28. Na ifanye
nafsi yako isubiri pamoja na wanaomuomba Mola Wao Mlezi
asubuhi na jioni, wakitaka radhi Yake; wala macho yako
yasiwaruke hao kwenda kutafuta anasa za maisha ya duniani;
wala usimtii tuliyemghafilisha moyo wake asitukumbuke
kututaja na akafuata matamanio yake, ikawa hali yake
imekiuka mipaka.

29. Na sema, ‘huu ni ukweli utokao kwa Mola Wenu
Mlezi, atakaye aamini na atakaye akanushe’. Hakika
Sisi tumewaandalia wenye kudhulumu moto ambao
Utawazunguka kama hema. Na wakiomba msaada watapewa
maji kama shaba iliyoyeyuka, yanayobabua nyuso. Kinywaji
kibaya kilioje hicho! Na mahali pabaya palioje pa kupumzika!

30. Hakika wale walioamini na wakatenda mema, Sisi

hatupotezi ujira wa anayefanya mazuri [31.] Hao wana Bustani za milele ambazo hupita mito ya maji chini yake. Humo watapambwa kwa bangili za dhahabu, na watavaa nguo za kijani za hariri nyepesi na nzito, huku wakibembea juu ya makochi. Ni malipo bora yalioje na mahali pazuri palioje pa kupumzika!

[32.] Hebu wapigie mfano wa watu wawili: mmoja wao tulimpa vitalu viwili vya mizabibu na tukavizunguushia mitende na kati yake tukaweka mimea ya nafaka. [33.] Hivyo vitalu viwili vikawa vinatoa mazao bila ya kuharibika chochote. Na ndani yake tukapasua mito ya maji. [34.] Mtu huyu alipata mazao mengi. Basi akamwambia mwenzake, huku akibishana naye: ‘Mimi nimekushinda kwa mali na nguvu za watu wangu!’. [35.] Akaingia kitaluni kwake katika hali ya kutoitendea haki roho yake, akasema: ‘Sifikirii hata kidogo kuwa haya yataharibika ’. [36.] ‘Wala sifikirii Kiyama kweli kitatokea. Na hata kama nitarudishwa kwa Mola Wangu Mlezi bila shaka nitakuta huko badali ya vizuri zaidi kuliko hivi!’

[37.] Mwenzake akamwambia katika mabishano naye: Je, unamkana ambaye amekuumba kutokana na udongo, tena kutokana na tone la manii, kisha akakufanya kuwa mtu kamili? [38.] Lakini Yeye Mwenyezi Mungu ndiye Mola Wangu Mlezi, wala si mshirikishi yeyote na Mola wangu Mlezi. [39.] Si ulipokuwa ukiingia katika shamba lako ungesema: ‘Mashaallah! (alitakalo Mwenyezi Mungu huwa), hapana nguvu ila kwa Mwenyezi Mungu? Ikiwa unaniona mimi nina mali na watoto kidogo kuliko wewe…. [40.] Asaa Mola wangu Mlezi akanipa kilicho bora kuliko kitalu chako, na akatuma kwenye kitalu chako radi kutoka mbinguni na kukigeuza

mchanga unaoteleza…. 41. Au maji yake yadidimie usiweze kuyagundua.

42 Ndipo matunda yake yakazungukwa na uharibifu, akabaki akipinduapindua viganja vyake, kwa vile alivyoyagharimia, huku miti ya matunda yake imeanguka juu ya vichanja vyake. Akawa anasema: 'Laiti nisingemshirikisha Mola wangu Mlezi na yeyote!' 43 Wala hakuwa na kundi la kumsadia badala ya Mwenyezi Mungu, wala mwenyewe hakuweza kujisaidia. 44 Huko, ulinzi pekee ni wa Mwenyezi Mungu wa kweli. Yeye ndiye bora kwa malipo na Mwema kwa matokeo ya mwisho.

45. Na wapigie mfano maisha ya hapa duniani. Ni kama maji tuliyoyateremsha kutoka mawinguni yakachanganyika na mimea ya ardhi, kisha (muda mfupi baadaye) mimea hiyo ikawa mashuke yaliyokauka yanapeperushwa na upepo. Na Mwenyezi Mungu ana uwezo juu ya kila kitu. 46. Utajiri na watoto ni pambo la maisha ya dunia. Na mema yanayobakia ndiyo bora kwa Mola Wako Mlezi na kwa malipo na bora kwa matumaini.

47. Na siku (hiyo) tutakapoisawazisha milima na ardhi, ukaiona ardhi iko tupu… kisha tukawakusanya pamoja wala hatutamwacha yeyote katika wao. 48. Na wakaletwa kwa Mola Wako Mlezi wakiwa katika safu. (ikatangazwa); 'Mmetujia kama tulivyowaumba mara ya kwanza (uchi)! Bali mlidhania kuwa hatungetekeleza ng'o kiaga tulichowapa!'.

49. Na (hapo) kitabu kitawekwa ndipo utawaona waovu wakiogopa kwa sababu ya yale yaliyomo ndani. Watasema: Ole wetu! Vipi kitabu hiki! Hakikuacha dogo wala kubwa isipokuwa kimelirikodi? Na watakuta waliyoyafanya yote yameletwa mbele. Na Mola Wako hamdhulumu yoyote.

50. Na pale tulipowaambia Malaika: Msujudieni Adam! Walimsujudia isipokuwa Iblis. Alikuwa miongni mwa majinni akavunja amri ya Mola Wake Mlezi. Je, mnamfanya yeye na kizazi chake kuwa rafiki zenu badala yangu Mimi, hali wao ni adui zenu? Ni ubaya ulioje walivyobadilisha wenye kudhulumu.

51. Sikuwafanya washuhudie kuumbwa kwa mbingu na ardhi wala kuumbwa wao wenyewe. Wala haiwezekani Kwangu Miye kuwafanya wanaowapoteza wengine kuwa wasaidizi wangu.

52. Na siku (Mwenyezi Mungu) atakaposema; "Haya, waiteni hao mliodai kuwa ni washirika wangu! Watawaita lakini hawatawaitikia. Nasi tutawaweka baina yao sehemu
pa maangamizi. 53. Na wahalifu watauona moto na wahofu
kuwa wataanguka humo, na hawatopata namna yoyote ya kuuepuka.

54. Na hakika tumewaeleza watu kwa upana hii Qur'an, kwa aina mbali mbali za mifano. Lakini binadamu, katika
mambo mengi, ni mbishani. 55. Na hapana kilichowazuia watu
kuamini, pale ulipowajia mwongozo, na kuomba maghufira kwa Mola Wao Mlezi; isipokuwa kutaka kwao yawajie yale yale ya watu wa kale, au iwajie adhabu uso kwa uso.

56. Na hatuwatumi Mitume ila wawe watoa bishara njema na waonyaji. Lakini waliokufuru wanabishana kwa hoja za kipuuzi, ili waudhoofishe ukweli. Na wanazifanya ishara
Zangu na yale waliyoonywa kuwa ni mzaha. 57. Na ni nani
dhalimu zaidi kuliko yule anayekumbushwa ishara za Mola Wake Mlezi na akazipuuza na akasahau yaliyotangulizwa na mikono yake? Hakika tumeweka vifuniko juu ya nyoyo zao wasije wakafahamu haya, na tumeweka kwenye masikio yao

uziwi. Na ukiwaita kwenye uongofu hawatakubali kabisa
kuoongoka.

58. Na Mola Wako Mlezi ndiye Mwenye maghufira
na Mwenye rehema, lau angewahukumu sambamba na
wanayoyachuma, bila shaka angewafanyia haraka adhabu.
Lakini wana miadi ambayo hawatapata kimbilio la
kuepukana nayo. 59. Na miji hiyo tuliwaangamiza watu wake
walipofanya madhambi, lakini tuliwawekea miadi (maalum)
ya kuwaangamiza.

60. Na Kumbuka pale Musa alipomwambia kijana wake:
'Sitaacha kusonga mbele mpaka nifike makutano ya bahari
mbili au (hadi) nimalize miaka na miaka katika safari. 61. Basi
wawili hao walipofika makutano ya bahari mbili, walimsahau
samaki wao, naye akashika njia yake kuponyokea baharini.
62. Walipokwishapita alimwambia kijana wake: 'Tuletee
chakula chetu cha mchana. Kwa hakika tumepata machovu
sana katika hii safari yetu.'

63. Akasema: 'wakumbuka pale tulipopumzika penye
jiwe? Basi mimi nilimsahau yule samaki hapo, na hapana
aliyenisahaulisha nisimkumbuke ila ni shetani. Naye
(samaki) akashika njia yake baharini kwa ajabu. 64. Akasema:
Hayo ndiyo tuliyokuwa tunayataka. Basi wakarudi kwa
kufuata njia waliyojia. 65. Wakamkuta mtumishi miongoni
mwa watumishi Wetu tuliyempa rehema kutoka kwetu na
tukamfunza elimu kutoka Kwetu.

66. Musa akamwuliza: 'Naweza nikufuate ili unifunze
katika ule uongofu uliofunzwa?' 67. Yule akasema: 'Hakika
wewe hutaweza kuvumilia kuwa pamoja nami. 68. Na
utawezaje kuvumilia yale usiyoyajua undani wake?' 69. Musa
akasema: 'Inshallah utanigundua kuwa mimi ni mvumilivu

wala sitoasi amri yako'. 70. Akasema: 'Basi ukinifuata, usiniulize chochote mpaka nianze kukueleza'.

71. Basi wawili hao wakaondoka, mpaka walipopanda jahazi (yule) akalitoboa. (Musa) akasema: 'Unalitoboa ili uwazamishe watu wake? Hakika umefanya jambo la ajabu sana!'. 72. (Yule mtu) akasema: 'Je, sikukuambia kuwa wewe hutaweza kuvumilia kuwa pamoja nami?' 73. Akasema: 'Usinigombeshe kwa vile nimesahau, wala usinitwishe mzigo wa kunichosha katika jambo langu. 74. Basi wawili hao wakaondoka, mpaka wakamkuta kijana, (yule) akamwua. Musa akasema: 'Ebo! Unamwua mtu asiye na kosa na wala hakuuwa mtu? Kwa kweli umefanya kitendo cha kutia karaha kisichowahi kutokea!

75. Akasema: 'Sikukwambia kuwa wewe hutaweza kuvumilia kuwa pamoja nami?' 76. Akasema: Nikikuuliza tena kitu baada ya haya usifuatane nami, kwani tayari una udhuru dhidi yangu. 77. Basi wawili hao wakaondoka, mpaka wakawafikia watu wa mji mmoja, wakawaomba watu wa mji wawape chakula, lakini wakakataa kuwakaribisha. Hapo wakakuta ukuta unakaribia kuporomoka, (yule mtu) akausimika. Musa akamwambia: 'Ungeweza kuwatoza malipo kwa kazi hii, kama ungetaka!' 78. Akasema: 'Hii sasa ndiyo kutengana mimi na wewe. Nitakueleza maana ya yale ambayo hukuweza kuvumilia'.

79. Ama lile jahazi lilikuwa ni la maskini wafanyao kazi baharini. Nikataka kulitia kasoro, kwani alikuwa akiwafuata mfalme anayetwaa majahazi yote kwa nguvu.

80. Ama yule kijana wazazi wake walikuwa waumini, tukahofia asije akawachosha kwa uasi na kufuru. 81. Tukataka

Mola Wao Mlezi awabadilishie aliye bora zaidi ya huyo kwa tabia na aliye karibu zaidi kwa (kuwaonea) huruma.

82 Na ama ule ukuta ulikuwa ni wa vijana wawili mayatima mle mjini, na chini yake ilikuwako hazina yao, na baba yao alikuwa mtu mwema. Mola Wako Mlezi akapenda wafikie kukomaa na waje waitoe hazina yao. Ni huruma ya Mola Wako Mlezi. Hayo sikuyatenda kwa amri yangu. Hayo ndiyo maelezo ya ambayo hukuweza kusubiria.

83. Na wanakuuliza kuhusu Dhul-qarnain. Waambie:
nitawasimulia baadhi ya habari zake. 84. Hakika Sisi tulimpa
nguvu na madaraka katika ardhi na tukampa njia ya kila kitu.

85. Basi akafuata moja ya njia. 86. Hata alipofika machweo
ya jua aliona linatua kwenye chemchemi ya maji yenye matope. Na hapo akawakuta watu, tukamwambia: 'Ewe Dhul-qarnain! Ima uwaadhibu hawa au uwatendee kwa wema'.
87. Akasema: Ama atakayefanya maovu, huyo tutamwadhibu na kisha atarudishwa kwa Mola Wake amwadhibu adhabu
ambayo haijawahi kusikiwa. 88. Na ama mwenye kuamini na akatenda mema atastahiki malipo mazuri na tutamwambia lililo jepesi katika amri Yetu.

89. Kisha akafuata njia nyingine. 90. Mpaka alipofika mawio
ya jua aliona linawachomozea watu ambao hatukuwapa sitara
ya kujikinga nalo. 91. (Akawaacha) kama walivyo. Sisi tulijua
habari za yote yaliyo mbele yake.

92. Kisha akafuata njia nyingine. 93. Hata alipofikia
baina ya milima miwili, alikuta nyuma yake watu ambao
takriban hawakuwa wakifahamu neno. 94. Wakasema: Ewe
Dhul-Qarnain! Hakika Gog na Magog wanafanya uharibifu mkubwa hapa nchini. Basi je, tukulipe ujira ili utujengee ngome baina yetu na wao?

[95.] Akasema: Nguvu aliyonipa Mola Wangu Mlezi ni bora zaidi (kuliko malipo). Lakini ninyi nisaidieni kwa nguvu kazi, nitawawekea kizuizi cha kuziba baina yenu na wao. [96.] Nileteeni matofali ya chuma. Hata alipojaza nafasi iliyo kati ya milima miwili, akasema: Pulizeni!. Hata alipokifanya (chekundu kama) moto akasema: Nileteeni shaba niimwage, iyeyuke. [97.] Hawakuweza kuukwea wala hawakuweza kuutoboa. [98.] Akasema: Hii ni rehema itokayo kwa Mola Wangu Mlezi. Itakapofika ahadi ya Mola Wangu Mlezi ataufanya uvunjike vipande viande. Na ahadi ya Mola Wangu ni ya kweli.

[99.] Na siku hiyo tutawaacha wakisongamana wenyewe kwa wenyewe. Na parapanda itapuziwa na wote tutawakusanywa pamoja. [100.]Na siku hiyo tutawaonesha makafiri moto wa Jahannam wauone wazi wazi, umeenea pote. [101.] Wale ambao macho yao yalikuwa ndani ya pazia la kutonikumbuka, na wakawa hawawezi hata kusikia.

[102.] Je wanadhani waliokufuru kuwa watawafanya waja wangu walinzi wao badaa yangu Mimi? Hakika Sisi tumeiandaa Jahannamu iwe ni mashukio ya makafiri.

[103.] Sema je, tuwaambieni wale wanaokula hasara zaidi katika vitendo vyao? [104.] Ambao bidii zao hapa duniani zimepotea bure, nao wanadhani kuwa wanafanya kazi nzuri. [105.] Hao ndio ambao wamezikanusha ishara za Mola wao Mlezi na wamekana kukutana Naye. Ndipo vitendo vyao vimeporomoka; na wala siku ya Kiyama hatutawapa uzito wowote. [106.] Hayo yatakuwa malipo yao, Jahannam, wataingia hmo kwa sababu ya walivyokufuru na wakazifanyia mzaha ishara Zangu na Mitume Wangu.

[107.] Hakika wale walioamini wakatenda mema, mashukio

yao yatakuwa kwenye Pepo za Firdausi. [108.] Watakaa humo daima, hawatataka kubadilisha.

[109.] Sema: Lau bahari ingelikuwa ndio wino wa maneno ya Mola Wangu Mlezi, basi bahari ingemalizika kabla ya kumalizika maneno ya Mola Wangu Mlezi, hata kama tungeleta mfano wake kuongezea.

[110.] Sema: hakika mimi ni binadamu kama nyinyi. Ninafunuliwa wahyi kwamba Mungu Wenu ni Mungu Mmoja tu. Basi mwenye kutarajia kukutana na Mola Wake Mlezi, na atende matendo mema, wala asimshirikishe yeyote katika ibada ya Mola Wake Mlezi.

## 19. Sura Maryam

## SURA YA MARIA 'MAMA WA YESU'

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema, Mwenye kurehemu.

[1] *Kaaf Ha Ya A'yn Swad.*

[2] Huu ni usimulizi wa rehema ya Mola Wako Mlezi kwa
mtumishi Wake Zakaria. [3] Alipomlilia Mola Wake Mlezi
kwa siri. [4] Akisema: 'Mola Wangu Mlezi! Mifupa yangu
imedhoofika, na kichwa kinameremeta kwa mvi. Mola Wangu
Mlezi! Kamwe sijakuwa mkosefu wa baraka nikuombapo
Wewe! [5] Hakika mimi sasa nahofia jamaa zangu baada yangu
(watakachofanya), na mke wangu ni tasa. Basi hebu nipe
mrithi kutoka Kwako... [6] Atakayenirithi mimi na arithi ukoo
wa Ya'qub (Yakobo). Ewe Mola Wangu Mlezi, na mfanye
atayekuridhisha.

7 Ewe Zakaria! Tunakupa habari njema za mtoto wa kiume: jina lake Yahya (John), hatujapata kumpa jina hilo yeyote kabla yake. 8 Akasema: Ewe Mola Wangu Mlezi! Vipi nitakuwa na mwana na ilhali mke wangu ni tasa, na mimi nimekuwa mkongwe kwa uzee?

9. Akasema, ndio hivyo itakavyokuwa. Mola Wako Mlezi amenena ' Hilo ni jepesi Kwangu. Na hakika nilikuumba wewe zamani na hukuwa kitu chochote'. 10. Akasema: 'Mola Wangu Mlezi, Nipe ishara! Akasema: 'ishara yako ni kuwa hutaweza kusema na watu kwa nyusiku tatu, nawe si bubu. 11. Basi (Zakaria) akawatokea watu wake kutoka Mihrab, akawaashiria kuwa 'mtajeni Yeye asubuhi na jioni'.

12. (sauti ikaita): Ewe Yahya! Kikamate kitabu kwa nguvu. Na tulimpa hekima angali mtoto. 13. Na huruma (kwa viumbe wote) itokayo Kwetu na utakatifu na akawa mcha Mungu. 14. Na mwema kwa wazazi wake wala hakuwa jeuri, mkaidi. 15. Na amani iwe juu yake, siku alipozaliwa na siku ya kufa na siku atakapofufuliwa.

16. Na simulia katika Kitabu hicho (kisa cha) Mariyam. Pale alipojitenga na jamaa zake (akaenda) sehemu ya upande wa mashariki. 17. Na akaweka pazia kujikinga nao. Tukampelekea Malaika Wetu, akajifananisha kwake na binadamu sawa sawa. 18. Maryam akamwambia: 'Hakika mimi najilinda kwa Mwenyezi Mungu aniepushe nawe, ukiwa wewe ni mtiifu wa Mungu'. 19. Akasema: 'Kwa kweli mimi ni mjumbe wa Mola Wako Mlezi (nimekuja) kukubashiria zawadi ya Mwana Mtakatifu' 20. Akasema: 'Nitakuwaje na mwana hali hajanigusa mtu yeyote wala mimi si Malaya? 21. Akasema: 'Ndivyo hivyo itakuwa! Mola Wako amesema, 'haya Kwangu

ni mepesi'! Tutamfanya kuwa ni ishara kwa watu, na rehema
itokayo Kwetu. Na hilo ni jambo limekwishapitishwa.

22. Basi akabebа mimba ya mwana, akaondoka nayo
kwenda mahali mbali. 23. Uchungu ukamfanya aende kwenye
shina la mtende; akasema: 'Laiti kama ningelikufa kabla ya
haya nikawa mwenye kusahaulika kabisa'.

24. Pakanadiwa kutoka chini yake kwamba 'usihuzunike!'
Hakika Mola Wako amepatia chini yako kijito cha maji.
25. Na litikise upande wako shina la mtende, utakuangushia
tende freshi, mbivu. 26. Basi kula na kunywa na uburudishe
jicho lako. Na pindi ukimuona mtu yeyote basi sema hakika
mimi nimeweka nadhiri kwa Mwenyezi Mungu ya kufunga.
Hiyo leo sitasema na mtu.

27. Akaenda na mwanawe kwa jamaa zake huku amembeba.
Wakasema: 'Ewe Maryamu! Hakika umekuja na kitu cha
kushangaza kabisa!'. 28. Ewe dada wa Harun (Aaron)! Baba
yako hakuwa mtu muovu wala mama yako hakuwa kahaba.

29. Ndipo akanyoosha kidole kwa yule mtoto. Wakasema:
'Vipi tuseme na mtoto mdogo ambaye bado yuko katika
mbeleko? 30. (Mtoto) akasema: 'Hakika mimi ni mja wa
Mwenyezi Mungu. Amenipa Kitabu na amenifanya Nabii.
31. Na amenifanya mwenye kubarikiwa popote pale niwapo.
Na ameniusia Swala na Zaka muda wa kuwa niko hai.
32. Na kumtendea mema mama yangu. Wala hakunifanya niwe
jeuri, mwovu. 33. Na amani iwe juu yangu, siku niliyozaliwa
na siku nitakayokufa na siku nitakayofufuliwa.

34. Huyo ndiye Isa (Yesu) mwana wa Maryam (Mary),
kauli ya kweli ambayo wanatilia shaka. 35. Haiwezekani kwa
Mwenyezi Mungu kuwa na mwana. 'Kutakasika ni Kwake
na hilo!' Anapopitisha jambo huliambia tu: 'Iwe! Likawa'.

36. Na hakika Mwenyezi Mungu ni Mola Wangu Mlezi na Mola Wenu Mlezi, basi mwabuduni. Hii ndio njia iliyonyooka. 37. Lakini wafuasi wa vikundi mbali mbali wakatofautiana wao kwa wao. Ole wao waliokufuru inapowadia siku hiyo kuu! 38. Kusikia vizuri kulikoje watakavyosikia, na kuona vizuri kulikoje watakakoona siku hiyo watakayotujia! Lakini madhalimu hiileo wako katika upotofu ulio wazi.

39. Na waonye siku ya majuto wakati jambo (hili) litakapoamuliwa. Wao bado wamo katika kughafilika, wala hawaamini! 40. Hakika Sisi tutairithi ardhi, na walio juu yake Kwetu watarejeshwa.

41. Na simulia katika Kitabu hicho (kisa cha) Ibrahim. Hakika yeye alikuwa mkweli mno, Nabii. 42. Pale alipomwambia baba yake: ‘Baba! Kwa nini unaabudu visivyosikia na visivyoona na visivyokufaa na chochote?’ 43. Ewe baba! Hakika imenifikia elimu ambayo haikukufikia wewe. Kwa hiyo nifuate mimi nitakuongoza njia iliyo sawa. 44. ‘Baba! Usimwabudu shetani. Hakika shetani ni muasi kwa Mwenyezi Mungu. 45. ‘Baba! Mimi nakuhofia isikupate adhabu ya Mwenyezi Mungu ukawa rafiki wa shetani’.

46. Akasema:’Hivi wewe Ibrahim unaichukia miungu yangu?’Kama hutakoma, kwa hakika nitakupiga mawe. Na niondokee hapa upotelee mbali! 47. (Ibrahim) akasema: ‘salamun alayka! (Amani iwe juu yako) Nitakuombea msamaha kwa Mola Wangu Mlezi. Hakika Yeye ni mwingi wa huruma kwangu’. 48. Nami najitenga nanyi na hivyo mnavyoviabudu badala ya Mwenyezi Mungu, na ninamuomba Mola Wangu Mlezi. Natumai sitakuwa mtovu wa adabu kwa kumwomba Mola wangu Mlezi (akusamehe).

49. Alipojitenga nao na vile wanavyoviabudu badala ya

Mwenyezi Mungu, tulimruzuku Is-haq (Isaacs) na Ya’qub (Yakobo) na kila mmoja tukamfanya Nabii. [50.] Na tukawapa rehema Zetu, na tukafanya wapewe heshima kubwa juu ya ndimi za wasema kweli.

[51.] Na simulia katika Kitabu hicho (kisa cha) Musa. Hakika yeye alikuwa mteuliwa maalum, na alikuwa Mtume, Nabii. [52.] Na tulimwita upande wa kulia wa mlima (Sinai) na tukamfanya awe karibu zaidi kwa mazungumzo ya siri. [53.] Nasi kwa huruma zetu tukampaye nduguye Harun (Aaron) kuwa Nabii

[54.] Na simulia katika Kitabu hicho (kisa cha) Ismail. Hakika yeye alikuwa mkweli wa ahadi na alikuwa Mtume, Nabii. [55.] Na alikuwa akiwaamrisha watu wake Swala na Zaka na alikuwa mbele ya Mola Wake Mlezi mwenye kuridhiwa. [56.] Na simulia katika Kitabu hicho (kisa cha) Idris. Hakika yeye alikuwa mkweli mno, Nabii. [57.] Na tukamwinua daraja ya juu.

[58.] Hao ndio ambao Mwenyezi Mungu amewaneemesha miongoni mwa manabii katika kizazi cha Adam, na katika wale tuliowachukua (kwenye Jahazi) pamoja na Nuh (Noah) na katika uzao wa Ibrahim na Israel na katika wale tuliowaongoza na kuwateua. Wanaposomewa Aya za Mwenyezi Mungu huporomoka kusujudu na kulia.

[59.] Lakini wakaja baada yao kizazi kingine; hawa walaacha Swala na wakafuata matamanio yao. Basi punde watakabiliana na (malipo ya) upotevu wao. [60.] Isipokuwa waliotubu, wakaamini na wakatenda mema. Hao wataingia Peponi wala hawatadhulumiwa chochote.

[61.] Bustani za milele ambazo Mwenyezi Mungu aliwaahidi watumishi Wake ingawaje hawakuziona. Hakika Yeye ahadi

yake hapana shaka itafika. [62.] Hawatasikia humo upuuzi ila salaam tu na watapata humo chakula chao asubuhi na jioni [63.] Hiyo ndiyo Pepo tutakayowarithisha miongoni mwa waja Wetu waliomtii Mwenyezi Mungu.

[64.] Wala hatutashuka ila kwa amri ya Mola Wako Mlezi. Ni yake Yeye yaliyoko mbele yetu na yaliyoko nyuma yetu na yaliyoko katikati ya hayo. Na Mola Wako Mlezi si mwenye kusahau. [65.] Mola wa mbingu na ardhi na vilivyo baina yake. Basi mwabudu Yeye na endelea kudumu katika subira ya kumwabudu Yeye. Je, unamjua yeyote anayestahiki jina kama lake?

[66.] Na mwanadamu husema: Hivi nitakapokufa, ni kweli nitatolewa niwe hai tena? [67.] Je hakumbuki huyu mtu kwamba tulimuumba kabla, na hali hakuwa chochote? [68.] Basi naapa kwa Mola Wako Mlezi! Hakika tutawakusanya wao pamoja na mashetani. Kisha tutawaleta kandokando ya Jahannam huku wakiwa wamepiga magoti.

[69.] Kisha kwa hakika tutachomoa katika kila kundi wale miongoni mwao waliozidi kumwasi Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema. [70.] Tena hakika sisi tunawajua vizuri wanaostahili zaidi kuchomwa humo. [71.] Hakuna yeyote katika nyinyi isipokuwa atapitia hapo ( Jahannam). Hiyo ni hukumu ya Mola Wako Mlezi, ni lazima itekelezwe. [72.] Lakini tutawaokoa wale waliomtii Mwenyezi Mungu na tutawaacha watenda mabaya humo wakiwa wamepiga magoti.

[73.] Na wanaposomewa Aya Zetu zilizo wazi, wanaomkana Mwenyezi Mungu huwaambia walioamini: lipi katika makundi hayo mawili litakuwa katika sehemu nzuri zaidi, na (litalokuwa) na watu wengi zaidi wa baraza lao? [74.] Na vizazi

vingapi tuliviangamiza kabla yao! Wao walikuwa na vyombo vizuri zaidi na wazuri zaidi kwa kuwatazama?

75. Sema: walio katika upotevu, Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema na awarefushie zaidi (muda) muda wao, hadi waone waliyoahidiwa: ama adhabu ama Kiyama. Hapo ndipo watajua ni nani mwenye nafasi mbaya zaidi na mwenye askari dhaifu zaidi.

76. Na Mwenyezi Mungu huwazidishia uwongofu wale waliokwishaongoka. Na mema yanayoendelea kudumu ni bora malipo yake mbele ya Mola Wako Mlezi na yana marejesho mazuri.

77. Je, umemuona aliyezikana ishara Zetu na akasema: Kwa vyovyote vile mimi nitapewa utajiri na wana!?
78. Kwani yeye amepata habari za ghaibu au amepokea ahadi kwa Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema? 79. Hasha! Tutaandika anayoyasema na tutamrefushia sana muda wa adhabu. 80. Kwetu yatarudi hayo anayoyasema na yeye atatujia akiwa pekee. 81. Na wamefanya miungu mingine badala ya Mwenyezi Mungu ili iwape nguvu na madaraka.
82. La hasha! Watakuja ikataa hiyo ibada yao na watakuwa dhidi yao!

83. Kwani huoni kwamba tumewatuma mashetani kwa makafiri wawachochee kwa mori! 84. Basi usiwafanyie haraka. Sisi tunawahisabia siku zao (chache). 85. Siku tutakayowakusanya wanaomcha Mwenyezi Mungu kuwapeleka kwa Mwezi Mungu, Mwingi wa rehema, wawe wageni wake. 86. Na tukawachunga wahalifu kuwapeleka Jahannam kama ng’ombe wanaopelekwa kunywa maji!
87. Hawatakuwa na mamlaka ya uombezi ila wale waliochukua ahadi kwa Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema

88. Na wanasema (ati) Mwenyezi Mungu amejifanyia
mwana! 89. Hakika mmeleta jambo la kuchukiza mno!.
90. Mbingu zakaribia kutatuka kwa (uzito wa) neno hilo na
na ardhi kupasuka na milima kuanguka vipande vipande.
91. Kwa kudai kwao kuwa Mwenyezi Mungu ana mwana.
92. Haistahili kwa Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
kuwa na mwana. 93. Hakuna yoyote aliyemo mbinguni na
ardhini ila atafika kwa MMwenyezi Mungu, Mwingi wa
rehema, kama mja wake tu. 94. Hakika amewadhibiti sawa
sawa na amewahesabu wote kwa namba. 95. Na kila mmoja
kati yao atamjia siku ya Kiyama akiwa pekee. 96. Hakika wale
ambao wameamini na wakatenda mema Mwenyezi Mungu,
Mwingi wa rehema, atawafanya wapendane.

97. Hakika tumeifanya nyepesi hii Quran, kwa ulimi
wako ili uwafikishie habari njema kwayo, wale wamchao
Mwenyezi Mungu, na uwaonye kwayo watu wabishi 98. Na
vizazi vingapi kabla yao tumeviangamiza! Je, unawaona hata
mmoja katika wao (hivi asa) au unasikia hata minong’ono
yao?

20. Sura Twaha

## SURA YA TWAHA

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 *Twaha.*

2 Hatukukuteremshia Qur’an ili iwe sababu ya wewe kuwa na
shida. 3 Isipokuwa ni mawaidha kwa wenye kumcha (Mungu).

4 Uteremsho utokao kwa aliyeumba ardhi na mbingu zilizo juu. 5 Mwenyezi Mungu amejizatiti (katika utawala) juu ya Kiti cha Enzi. 6 Ni Vyake vilivyo katika mbingu na katika ardhi na vilivyo baina yao na vilivyo chini ya mchanga.

7 Na ukiinua sauti kuzungumza (au usiinue), Yeye hujua siri na yanayofichika zaidi. 8 Mwenyezi Mungu. Hapana Mola ila Yeye. Yeye ndiye mstahiki wa majina mazuri sana.

9. Je kimekufikia kisa cha Musa (Moses)?. 10. Pale alipoona moto, akaiambia familia yake: ngojeni hapa! Mimi nimeona moto, huenda nikawaletea kijinga kutoka huko au nikapata mwongozo (wa njia) huko kwenye moto.

11. Basi alipoufikia akaitwa: ‘Musa!’ 12. Hakika Mimi ndiye Mola Wako Mlezi. Vua viatu vyako; kwani wewe uko katika bonde takatifu la Tuwa. 13. Nami nimekuteua, basi sikiliza unayofunuliwa. 14. Hakika mimi ndiye Mwenyezi Mungu, hapana Mungu isipokuwa Mimi. Basi niabudu Mimi na usimamishe Swala kwa ajili ya kunikumbuka Mimi. 15. Hakika Kiyama kinakuja. Nimeazimia kukificha, ili kila nafsi ije ilipwe kwa (kiasi cha) iliyoyafanya. 16. Kwa hiyo asiku yule asikupoteze mwelekeo mtu asiyekiamini, anayefuata matamanio yake, ukaangamia

17. Na nini hicho kilicho katika mkono wako wa kuume, Musa? 18. Akasema: Hii ni fimbo yangu; ninaiegemea na ninawaangushia majani kondoo wangu; tena inanifaa kwa matumizi mengine. 19. Akasema: ‘Ibwage chini, Musa!’ 20. Akaibwaga. Mara, ikawa nyoka anayetambaa! 21. Akasema: Ichukue wala usihofu! Tutairudisha hali yake ya kwanza 22. Na ufumbe mkono wako kwenye kwapa lako, utatoka wenye (mwanga) mweupe bila ya madhara yoyote (kuunguza). Hiyo ni ishara nyingine. 23. Ili tukuonyeshe

baadhi ya ishara Zetu kubwa. [24.] Nenda kwa Firauni; kwani hakika yeye amepetuka mpaka.

[25.] Akasema: ‘Ewe Mola Wangu Mlezi! Nitanulie kifua changu [26.] Na unifanyie wepesi jambo langu. [27.] Na ulifungue fundo lilo katika ulimi wangu. [28.] Wapate kufahamu kauli yangu. [29.] Na nipe waziri katika watu wangu, [30.] Harun (Aaron) ndugu yangu. [31.] Niongezee nguvu zangu kwa yeye. [32.] Na umshirikishe katika jambo langu. [33.] Ili tukutakase sana, [34.] Na tukukumbuke sana. [35.] Hakika Wewe daima unatuangalia. [36.] Akasema: Hakika umepewa maombi yako ewe Musa.

[37.] Na hakika tulikwisha kufanyia hisani mara nyingine. [38.] Pale tulipommpa mama yako (ujumbe) kwa wahyi. [39.] Kwamba mtupe (mtoto) katika kisanduku, kisha kitupe kisanduku mtoni na mto utambwaga ufukweni. Atamwokota adui Yangu na adui yake. Na nimekutilia mapenzi kutoka Kwangu, ili ulelewe machoni Pangu. [40.] Pale dada yako alipokwenda na akasema: Je, niwajulishe mtu atayeweza kumlea mtoto? Ndipo tukakurujesha kwa mama yako, ili macho yake yaburudike wala asihuzunike. Na ulimwua mtu nasi tukakuokoa na dhiki hiyo. Na tukakujaribu kwa majaribio mengi. Ukakaa miaka kadhaa kwa watu wa Madyan. Kisha ukaja kama ilivyopangwa, ewe Musa

[41.] Na nimekuandaa wewe kwa ajili (ya kazi) Yangu. [42.] Nenda wewe na nduguyo pamoja na ishara Zangu, wala msichoke kunikumbuka. [43.] Nendeni kwa Firauni, hakika yeye amepetuka mipaka. [44.] Mwambieni maneno laini, huenda akakubali ujumbe au akaogopa.

[45.] Wakasema: Ewe Mola Wetu! Sisi tunaohofia asije akapania kufanya ufedhuli juu yetu au akapetuka mipaka

yote. 46. Akasema: msihofu! Hakika Mimi niko pamoja nanyi. Nasikia na ninaona. 47. Basi mwendeeni na mumwambie: 'Hakika sisi ni wajumbe wa Mola Wako Mlezi, waache wana wa Israel waondoke nasi, wala usiwatese. Tumekuletea ishara itokayo kwa Mola Wako Mlezi. Na amani iwe juu ya wanaofuata mwongozo. 48. Hakika tumeteremshiwa wahyi kwamba adhabu itampata anayekadhibisha na akapuuza.

49. Firaun akasema: 'Nani Mola wa wawili nyie, wee Musa? 50. Akasema: Mola Wetu ni yule aliyekipa kila kitu umbo lake kisha akakiongoza. 51. Akasema: 'Nini hali ya vizazi vilivyopita?' 52. Akasema: 'Elimu ya hilo iko kwa Mola wangu Mlezi (imerekodiwa) katika Kitabu. Mola Wangu hafanyi makosa wala hasahau.

53. Ambaye amewafanyia ardhi kuwa tandiko. Na akawapitishia humo njia. Na akateremsha kutoka mawinguni maji. Na kwayo tukazalisha aina mbali mbali za mimea. 54. Kuleni na mchunge wanyama wenu. Hakika katika hayo zipo ishara kwa wanaofahamu. 55. Kutokana na ardhi tumewaumba nyie (wanadamu) na humo tutawarudisha na kutoka humo tutawatoa mara nyingine.

56. Hakika tulimwonesha ishara Zetu zote, lakini alidai ni uwongo na akakataa 57. Akasema: 'Wee Musa! Hivi umekuja kwetu ili ututoe katika nchi yetu kwa uchawi wako?' 58. Basi tutakuletea uchawi kama huo. Hebu weka miadi baina yetu na wewe ambayo hatutaivunja sisi wala wewe, mahali ambapo wote tutakua na nafasi sawa.

59. Akasema: 'Miadi yenu ni siku ya sikukuu na watu wakusanywe kabla ya adhuhuri'. 60. Basi Firauni akaondoka, akaenda akawakusanya washirika wa njama yake, kisha akaja. 61. Musa akawaambia: 'Ole wenu! Msimzushie

Mwenyezi Mungu uwongo, asije akawafutilia mbali mara
moja kwa adhabu. Na hakika mzushi hurudi mikono mitupu.
[62.] Basi wakazozana juu ya jambo lao wenyewe kwa
wenyewe na wakanon'gona kwa siri. [63.] Wakasema: 'Hakika
hawa wawili ni wachawi, wanataka kuwatoa nyie katika nchi
yenu kwa uchawi wao na waondoe utamaduni wenu ulio
bora kabisa. [64.] Kwa hiyo kusanyeni mbinu zenu pamoja,
kisha mje mkijipanga safu kwa mujibu wa vyeo vyenu (vya
kichawi). Na hakika leo atafuzu atakayekuwa juu.
[65.] Wakasema: 'Ewe Musa! Je, utabwaga wewe au
tutakuwa sisi wa kwanza kubwaga ?' [66.] Akasema: 'Hapana,
bwageni nyinyi!' Mara kamba zao na fimbo zao zikaonekana
mbele yake, kwa uchawi wao, kuwa zinatmbaa! [67.] Musa
akaingiwa hofu katika nafsi yake. [68.] Tukamwambia: Usihofu
hakika wewe ndiye utakayeshinda. [69.] Na kibwage hicho
kilicho kuumeni kwako, kitavimeza walivyoviunda. Hakika
walivyoviunda ni hila za mchawi tu, na mchawi hafanikiwi
popote aendapo. [70.] Hapo wachawi wakaporomoka chini
kusujudi. Wakasema: 'Tumemwamini Mola Mlezi wa
Haruna na Musa!
[71.] Firauni akasema: 'Ebo! Mmemwamini kabla sijawapa
ruhusa? Bila shaka huyu ni mkubwa wenu aliyewafundisha
nyie uchawi. Nitawakata mikono yenu na miguu yenu, wa
kuume kwa wa kushoto. Kisha nitawatundika kuwasulubu
kwenye vigogo vya mitende. Na hapo kwa yakini mtajua ni
nani katika sisi ni mkali kwa adhabu na ambaye adhabu yake
ni endelevu?'
[72.] Wakasema: 'Hatutakuchukulia wewe kuwa bora kuliko
ishara waziwazi zilizotujia, na kuliko aliyetuumba. Potelea
mbali, hukumu utakavyohukumu; wewe unahukumu maisha

haya ya duniani tu'. [73.] 'Hakika sisi tumemwamini Mola Wetu Mlezi ili atusamehe makosa yetu na uchawi uliotulazimisha kuufanya. Na Mwenyezi Mungu ndiye Bora na Mwenye kudumu zaidi'.

[74.] Hakika atakayemjia Mola Wake Mlezi naye ni mhalifu, basi kwa hakika stahiki yake ni Jahannam. Hafi humo wala hawi hai. [75.] Na atakayemjia naye ni mumini aliyetenda mema basi hao ndio wenye daraja za juu. [76.] Bustani za milele ambazo hupita mito ya maji chini yake, watabaki humo milele na hayo ni malipo ya mwenye kujitakasa (na shetani).

[77.] Na tulimfunulia Musa kwamba:'Toka usiku na watumishi Wangu na uwapigie (kwa fimbo itoke) njia kavu baharini, usihofu kufikiwa (na Firauni) wala usiogope chochote. [78.] Firauni akawafuata pamoja na majeshi yake. Hapo maji ya bahari yaliwazidi nguvu na yakawafunika kabisa. [79.] Firauni aliwaongoza watu wake kwenye upotevu wala hakuwaongoza sawa sawa.

[80.] Enyi wana wa Israel! Hakika tuliwaokoa na adui yenu! Na tukafanya Agano nanyi upande wa kuume wa mlima (Sinai). Na tukawateremshia Manna na ndege wa Kwale. [81.] Kuleni katika vizuri tulivyowaruzuku, wala msipetuke mipaka katika hayo isije ikawashukia ghadhabu Yangu. Na inayemshukia ghadhabu yangu basi huyo amepotea. [82.] Lakini bila shaka Mimi (pia) ni Mwenye kusamehe kwa anayetubia na akaamini na akatenda mema tena akakubali mwongozo.

[83.] (Musa alipokuwa Mlimani, Mwenyezi Mungu alimwuliza): Ni kipi kilichokuharakisha ukawaacha nyuma watu wako ewe Musa? [84.] Akasema: 'Hao hapo nyuma yangu wananifuatia. Na nimefanya haraka kukujia, Mola Wangu

Mlezi, ili uridhike'. [85.] Akasema: Basi Sisi tumewatia mtihani watu wako ulipokuwa hupo na Samiri amewapoteza.

[86.] Musa akarudi kwa watu wake akiwa na hasira na huzuni. Akasema: Enyi watu wangu! Kwani Mola Wenu hakuwaahidi ahadi nzuri? Je ahadi imerefuka? Au mmetaka iwafikie ghadhabu kutoka kwa Mola Wenu, ndio maana mkavunja ahadi yangu?

[87.] Wakasema: Hatukuvunja ahadi yako kwa hiyari yetu, lakini tulibebeshwa mizigo ya mapambo ya watu wote (dhahabu zao na fedha). Tukaitupa (kwenye moto iyeyuke) na hivyo ndivyo alivyoshauri Samiri. [88.] (Samiri) Akawafulia watu (kutoka kwenye moto) sanamu la ndama, kiwiliwili chenye sauti. Wakasema: Huyu ndiye mungu wenu na mungu wa Musa, lakini Musa alisahau (tu)! [89.] Je, hawakuona kuwa (huyo ndama wa dhahabu) hakuweza kuwarudishia wao jibu, wala hakuweza kuwadhuru wala kuwafaa?.

[90.] Na hakika Harun alikwisha waambia kabla: Enyi watu wangu! Hakika nyinyi mmetiwa mtihani tu kwa kitu hiki. Na kwa hakika Mola Wenu Mlezi ni Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema. Nifuateni na mtii amri yangu. [91.] Wakasema: 'Hatutaacha kumwabudu mpaka hapo Musa atakaporejea'.

[92.] Akasema (Musa): 'Harun! Ni nini kilichokuzuia ulipowaona watu wamepotea? [93.] Kwamba usinifuate? Je, umeasi amri yangu? [94.] (Harun) Akasema: 'Ewe mwana wa mama yangu! Usinivute kwa ndevu zangu, wala kwa (nywele za) kichwa changu. Kwa hakika niliogopa usije ukasema umesababisha mfarakano baina ya Wana wa Israel, na hukuheshimu kauli yangu'.

[95.] (Musa) Akasema: 'Na wewe Samiri nini shauri lako?' [96.] Akasema: Nimeyaona wasiyoyaona wao. Ndipo

nikachukua kifumba cha (vumbi la) unyayo wa Mtume, nikamtupia (ndama wa dhahabu). Hivyo ndivyo nafsi yangu ulivyonituma.’.[9] [97] Akasema (Musa): Basi ondoka hapa! Na kwa hakika (adhabu yako) katika uhai huu utakuwa ukisema: ‘Usiniguse.’ Na hakika una miadi kwako isiyovunjwa. Na mtazame huyo mungu wako uliyeendelea kumwabudu; hakika tutamfua katika moto, kisha tutatawanya tawanya (mabaki yake) baharini. [98] Hakika Mungu Wenu ni Mwenyezi Mungu tu, hapana mungu mwingine isipokuwa Yeye, ujuzi Wake umeenea kila kitu.

[99] Namna hii ndivyo tunavyokusimulia baadhi ya habari za yaliyopita. Na hakika tumekuletea ujumbe kutoka Kwetu. [100] Mwenye kujitenga na ujumbe huo basi hakika siku ya Kiyama atabeba mzigo. [101] Watadumu katika hali hiyo. Ni mzigo muovu kwao kuubeba siku ya Kiyama! [102] Siku itakapopulizwa parapanda na tukawakusanya wahalifu siku hiyo macho yao yakiwa bluu (kwa hofu). [103] Watanong’onezana wao kwa wao:’ Hamkukaa isipokuwa siku kumi tu!’. [104] Sisi tunayajua zaidi watakayoyasema. Pale atakaposema kiongozi wao mwenye uzoefu: ‘Nyinyi hamkukaa isipokuwa siku moja tu’.

[105.] Wanakuuliza kuhusu milima. Sema: Mola Wangu Mlezi ataing’oa aitawanye iwe vumbi’ [106.] Ataiacha ikiwa tambarare iliyosawazika. [107.] Hutaona hapo (mahali pake) mabonde wala miinuko. [108.] Siku hiyo watamfuata anayeita (moja kwa moja) bila kupinda. Sauti zote zitamnyenyekea

9. Rasul hapa huenda ikamaanisha Mtume Musa au Jibril. Yaani Samiri anadai kuwa ameona nguvu za ajabu katika vumbi hilo na alipomtupia ndama yule aliyekuwa akifuliwa motoni, kweli akatoa sauti!- Mfasiri)

Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema. Basi hutasikia ila mnong'ono.

109. Siku hiyo uombezi hautafaa kitu ila wa yule aliyemruhusu Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema na akamridhia kusema. 110. Anayajua yaliyo mbele yao na yaliyo nyuma yao, wala wao hawawezi kumjua Yeye vilivyo. 111. Zitanyenyenyekea nyuso zote kwa Aliye hai milele, Mwenye kujitosheleza kwa kila kitu. Na hakika ataishia patupu mwenye kubeba dhuluma. 112. Na mwenye kutenda mema naye ni mumini, hatahofia dhuluma wala kupunjwa.

113. Namna hiyo tumeiteremsha Qur'an kwa lugha ya kiarabu na tumekariri humo maonyo ili wamche Mungu, au isababishe wao kumkumbuka Allah. 114. Ametukuka Mwenyezi Mungu, Mfalme wa kweli. Wala usiifanyie haraka hii Qur'an kabla haujamalizika wahyi wake. Na sema: Mola Wangu Mlezi! Nizidishie elimu.

115. Na hapo zamani tulimpa ahadi Adam, lakini alisahau wala hatukuona kwake azimio imara. 116 Kumbuka tulipowaambia Malaika: 'Inameni kwa heshima ya Adam'! Wote wakainama isipokuwa Iblisi, alikataa. 117. Tukasema: Ewe Adam! Hakika huyu ni adui yako na wa mkeo. Tahadhari asiwatoe katika Pepo hii, mkaingia katika mateso.

118. Hakika humo (Peponi) hutakuwa na njaa wala hutakuwa uchi. 119. Na hakika wewe hutapata kiu humo wala hutapata joto. 120. Lakini shetani alimtia wasiwasi, akamwambia: 'Ewe Adam! Je, Nikujulishe mti wa kuishi milele na ufalme usiokoma?' 121. Ndipo wakaula wote na uchi wao ukawadhihirikia na wakaanza kujibandika majani ya Pepo. Na Adam akamuasi Mola Wake Mlezi na akakubali

kushawishika. [122.] Kisha Mola Wake Mlezi akamteua na akamkubalia toba yake na akamwongoa.

[123.] Akasema: Ondokeni humu nyote; hali ya kuwa ni maadui nyinyi kwa nyinyi. Na ukiwafikia uongofu kutoka Kwangu, basi atakayefuata uongofu Wangu, hatapotea wala hatataabika. [124.] Na atakayejiepusha na ujumbe Wangu, hakika atapata maisha yenye dhiki. Na tutamfufua siku ya Kiyama hali akiwa kipofu. [125.] Aseme: 'Ewe Mola Wangu! Mbona umenifufua kipofu, nami nilikuwa nikiona'? [126.] Atasema (Mwenyezi Mungu): Ndivyo hivyo hivyo. Zilikufikia ishara Zetu ukazisahau, nawe kadhalika leo unasahauliwa. [127.] Na hivyo ndivyo tutakavyomlipa kila apitishaye kiasi asiamini ishara za Mola Wake Mlezi. Na Hakika adhabu ya Akhera ni kali zaidi na inadumu.

[128.] Je, haikuwabainikia, ni vizazi vingapi tuliviangamiza kabla yao, nao (hivi sasa) wanatembea katika maskani yao. Hakika katika hayo kuna Ishara kwa wenye akili. [129.] Na lau si neno lililokwishatangulia kutoka kwa Mola Wako na muda uliowekwa, bila shaka ingelilazimu kuja adhabu (sasa hivi). [130.] Yavumilie hayo wayasemayo. Na mtakase Mola Wako Mlezi kwa kumsifu kabla ya mawiyo ya jua na kabla ya machweo yake. Na nyakati za usiku pia umtakase, na ncha za mchana, ili upate furaha ya moyo.

[131.] Wala usivikodolee macho tulivyowastarehesha baadhi ya watu miongoni mwao. Anasa za maisha ya dunia hii, tunazowajaribu kupitia hizo.. Na riziki ya Mola Wako Mlezi ni bora na yenye kudumu zaidi. [132.] Na uwaamrishe watu wako kuswali, nawe kuwa makini nayo. Hatukuombi riziki. Sisi tunakuruzuku wewe. Na mwisho mwema ni kwa kumchamungu.

[133.] Na walisema: Kwa nini hakutuletea ishara kutoka kwa Mola Wake? Je, haikuwajia dalili wazi kwa yote yaliyomo katika vitabu vya mwanzo? [134.] Na lau tungewaangamiza kwa adhabu kabla ya hii, wangesema: Ewe Mola Wetu Mlezi! Kwa nini usituletee Mtume tukazifuata Aya Zako kabla hatujadhalilika na kufedheheka? [135.] Sema: Kila mmoja anangoja; basi ngojeni punde mtajua nani walio kwenye njia ya sawa na nani aliyeongoka.

## 21. Sura Al-Anbiyaa

# SURA YA MANABII

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

[1] Imekaribia kwa watu siku yao ya kuhesabiwa lakini wao bado wamo katika kughafilika, wakipuuza. [2] Hauwafikii ujumbe wowote mpya kutoka kwa Mola Wao Mlezi, ila wao huusikiliza huku wanafanya mchezo. [3] Zimeghafilika nyoyo zao. Na wale watenda maovu hunog'ona kwa siri: Ni nani huyu isipokuwa binadamu tu kama nyinyi! Hivi mnaufuata uchawi hali mnaona? [4] Sema: 'Mola Wangu Mlezi anajua yasemwayo mbinguni na ardhini na Yeye ni Mwenye kusikia, Mwenye kujua'.[10]

[5] Lakina wao wanasema: Hizo ni ndoto za ovyo ovyo tu. Hapana, ameizusha! Hapana, huyo ni mshairi!... Mwache atuletee muujiza kama walivyotumiwa (Mitume) wa mwanzo.

10. Katika kisomo cha Basra Qaala (amesema) inakuwa Qul (sema) nami nakubaliana na kisomo hicho. Hakuna tofauti ya maana- Mfasiri

6 Kabla yao hawakuamini watu wa miji tuliyoiangamiza,
wataamini hawa? 7 Na hatukuwatuma kabla yako isipokuwa
wanaume tuliowapa ufunuo (kama wewe). Waulizeni
wenye kumbukumbu, ikiwa nyinyi hamjui. 8 Na kamwe
hatukuwaumba na miili isiyokula chakula, wala hawakuwa
wenye kuishi milele. 9 Hatimaye tukawatimizia ahadi
yetu, tukawaokoa wao na tuliowataka na tukawaangamiza
waliopetuka mipaka.

10. Hakika tumewateremshia Kitabu, ndani yake mna
ujumbe kwa ajili yenu. Inakuaje hamfahamu? 11. Na ni vizazi
vya miji mingapi vilivyofanya maovu tulivyoviteketeza,
na tukaanzisha baada yao watu wengine? 12. Walipohisi
adhabu Yetu inakaribia, mara wakajaribu kukimbia.
13. Msikimbie! Rudini kwenye starehe zenu na maskani zenu,
huenda mkawajibishwa. 14. Wakasema: Ole wetu! Hakika sisi
tulikuwa watenda maovu. 15. Hicho kiliendelea kuwa kilio
chao hadi tukawafanya (kama konde) lililofyekwa, au (moto)
uliozimwa.

16. Na hatukuziumba mbingu na ardhi na vilivyomo baina
yao kwa mchezo. 17. Kama tungelitaka kufanya mchezo
tungejifanyia Sisi wenyewe, ikiwa sisi (kweli) ni wafanyao
mchezo. 18. Bali tunauvurumisha ukweli juu ya uongo,
ukauchana ubongo wake! Mara Uongo ukafa! Na ole wenu
kwa (uongo) mnaotunasibishia Sisi!

19. Ni Vyake vilivyoko mbinguni na ardhini na walioko
mbele Yake hawafanyi kiburi wakaacha kumwabudu,
wala hawachoki. 20. Wanamsabihi usiku na mchana wala
hawanyog'onyei.

21. Au wamepata miungu ardhini wawezao kufufua?
22. Lau wangelikuwemo humo miungu wengine isipokuwa

Mwenyezi Mungu basi mbingu na ardhi zingeharibika. Ametakasika Mwenyezi Mungu, Mola wa arshi, na hayo wanayomnasibishia. 23. Yeye hahojiwi kwa anayoyatenda na wao ndio wahojiwao kwa wayatendayo.

24. Au wamejifanyia miungu wengine badala Yake? Sema, leteni ushahidi wenu! Huu ni ujumbe wa walio nami na ujumbe wa waliokuwa kabla yangu. Lakini wengi wao hawajui ukweli kwa hiyo wanapuuza. 25. Na hatukumtuma kabla yako Mtume yeyote ila tulimfunulia kwa wahyi kwamba hapana Mungu isipokuwa Mimi, basi niabuduni Mimi tu.

26. Na wanasema, Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema ana mwana! Ametakasika na hilo! Bali hao ni waja waliotukuzwa. 27. Hawamtangulii kwa kauli, nao wanafanya kwa amri yake. 28. Anayajua yaliyo mbele yao na yaliyo nyuma yao. Wala hawamuombei yeyote ila yule anayemridhia. Nao wanamnyenyekea kwa kumcha. 29. Na yeyote miongoni mwao atakayesema: 'Mimi ni mungu na siyo Yeye' Huyo malipo yake yatakuwa Jahannam. Hivyo ndivyo tunavyowalipa waovu.

30. Je, hao waliokufuru hawajui kwamba mbingu na ardhi zilikuwa zimeambatana, ndipo tukazibandua? Na tukaumba kutokana na maji kila kilicho hai. Iweje hawaamini?

31. Na tukaweka katika ardhi milima iliyosimama wima ili ardhi isije ikayumba nao. Na tukaweka humo barabara pana ili wapate kuongozeka. 32. Na tukaifanya mbingu kuwa sakafu iliyohifadhiwa, lakini wanazipuuza ishara za vitu hivi. 33 Na Yeye ndiye aliyeumba usiku na mchana na jua na mwezi. Vyote vinaogelea katika njia yao ya mzunguko.

34. Na hatukumfanya binadamu yeyote kabla yako kuishi

milele. Je, ukifa wewe wao wataishi milele 35. Kila roho
itaonja mauti. Na tutawajaribu kwa mtihani wa shari na kheri
na Kwetu mtarejeshwa.
36. Na wale wanaokataa wanapokuona hawakufanyi
wewe ila (kitu) cha mzaha tu, (wanasema): Hivi huyu ndiye
anayewataja (vibaya) miungu wenu? Na wao hutoa matusi
atajwapo Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema.
37. Binadamu ameumbwa kuwa kiumbe wa haraka-haraka.
Hivi karibuni Nitawaonyesha ishara Zangu, msiniharakishe.
38. Na wanasema: Ahadi hii itatokea lini, ikiwa nyinyi
mnasema kweli? 39. Laiti wangejua, wale wanaomkana
Mwenyezi Mungu, wakati hawataweza kuuzuia moto kwenye
nyuso zao au migongo yao, na wala hawapewi msaada.
40. Bali kitawafikia ghafla, na kitawastua na wala hawataweza
kukirudisha wala hawatapewa muda. 41. Na hakika Mitume
wengine kabla yako (pia) walidhihakiwa. Wale waliokuwa
wakifanya dhihaka yakawafika yale yale waliyokuwa
wakiyadhihaki.
42. Sema nani atakayewalinda usiku na mchana dhidi ya
(hasira ya) Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema? Lakini
wao wanapuuza kumkumbuka Mola Wao Mlezi. 43. Au wao
wana miungu watakaoweza kuwakinga Nasi?. Hao hawawezi
kujinusuru wao wenyewe, wala hawatalindwa Nasi.
44. Bali tuliwastarehesha hawa na baba zao mpaka
umri ukawa mrefu kwao. Je, hawaoni kuwa Sisi pole pole
tunalipunguza eneo la ardhi (lililo chini yao) kuanzia
pembezoni mwake? Je, ni wao watakaokuwa washindi?
45. Sema: Hakika mimi ninawaonya kwa mujibu wa Wahyi
(ufunuo). Na viziwi hawasikii wito wanapoonywa. 46. Na
watapoguswa na mpulizo mmoja tu wa adhabu itokayo kwa

Mola Wako Mlezi, watasema: Ole wetu! Hakika tulikuwa watu waovu!

47. Na tutaweka mizani ya uadilifu kwa siku ya Kiyama. Hivyo, hakuna roho yeyote itakayodhulumiwa kitu. Hata ikiwa kama uzani wa chembe ya hardali, tutaileta. Nasi tunatosha kuwa wenye kuhisabu.

48. Na hakika tulimpa Musa (Moses) na Harun (Aaron) vigezo (vya kuhukumu), na mwangaza na ujumbe kwa wamchao Mwenyezi Mungu. 49. Ambao humwogopa Mola Wao Mlezi katika faragha na wanaihofu Siku ya Kiyama. 50. Na huu ni ujumbe uliobarikiwa ulioteremshwa. Hivi mtaukataa?

51. Na hakika tulikwishampa Ibrahim mwongozo wake hapo zamani na tulikuwa tunamjua. 52. Pale alipomwambia baba yake na watu wake: Ni nini haya masanamu mnayoyanga’ng’ania kuyaabudu? 53. Wakasema: Tumewakuta baba zetu wakiyaabudu. 54. Akasema: Hakika nyinyi na baba zenu mmekuwa kwenye upotofu ulio dhahiri.

55. Wakasema: Je, umetujia na maneno ya kweli au wewe ni katika wafanyao mchezo tu? 56. Akasema: Bali Mola Wenu Mlezi ni Mola wa mbingu na ardhi ambaye ndiye aliyeziumba, na mimi ni katika wenye kuyashuhudia hayo. 57. Naapa kwa Mwenyezi Mungu! Nitayafanyia vitimbi masanamu yenu baada ya kunipa mgongo kwenda zenu. 58. Basi akayavunja vipande vipande isipokuwa kubwa lao, ili wao walirudie.

59. Wakasema: Ni nani aliyeyafanya haya kwa miungu wetu? Hakika huyu ni katika waliowakana miungu yetu.. 60. Wakasema: Tumemsikia kijana mmoja akiwataja. Anaitwa Ibrahim. 61. Wakasema: Mleteni mbele ya macho ya watu, wapate kumshuhudia. 62. Wakamwuliza: Je, wewe ndiwe

uliyefanya hivi kwa miungu yetu, Ibrahim? 63. Akasema: Bali
ameyafanya hayo mkubwa wao huyu. Basi waulizeni ikiwa
wanaweza kutamka.

64. Basi wakajirudi nafsi zao. Wakasema: Kwa kweli nyinyi
ndio mlio katika makosa! 65. Hapo tena wakaingiwa na aibu
(wakasemezana):'Wewe unajua fika kwamba (kweli) hawa
hawasemi!' 66. (Ibrahim) akasema: Basi nyinyi mnaabudu
badala ya Mwenyezi Mungu visivyowanufaisha kitu wala
kuwadhuru? 67. Kefule yenu na mnavyoviabudu badala ya
Mwenyezi Mungu! Hamna akili nyie?

68. Wakasema: 'Mchomeni moto! Ili muwalinde miungu
yenu! Ikiwa mtafanya lolote. 69. Tukasema: 'Ewe moto! Kuwa
baridi na salama kwa Ibrahim! 70. Na wakamtakia ubaya,
lakini Sisi tukawafanya wao ndio wenye kupata hasara.

71. Na tukamwokoa yeye na (mpwa wake) Lut (Lot)
tukawaelekeza kwenye ardhi tuliyoibariki kwa walimwengu
wote. 72. Naye tukamruzuku Is-haq (Isaacs) na Yakub (Yakobo)
kama zawadi ya ziada (mjukuu). Na wote tukawajaalia kuwa
watu wema. 73. Na tukawafanya maimamu wakiongoza
kwa amri Yetu. Na tukawafunulia kwa wahyi watende
kheri na wasimamishe Swala na watoe Zaka na walikuwa
wanatuabudu Sisi pekee.

74. Na Lut tukampa hukumu na elimu na tukamwokoa na
ule mji uliokuwa ukifanya maovu. Hakika hao walikuwa
wabaya, mafasiki. 75. Na tukamwingiza katika rehema Yetu.
Hakika yeye ni miongoni mwa walio wema.

76. Na Nuh (Noah) alipotulilia hapo zamani, Nasi
tukamwitikia na tukamwokoa yeye na watu wake kutokana
na shida kubwa. 77. Na tukamnusuru yeye dhidi ya watu

waliozikadhibisha Ishara Zetu. Hakika hao walikuwa watu wabaya. Hivyo tukawazamisha wote katika mafuriko.

78. Na Daud (David) na Suleiman (Solomon) walipotoa hukumu katika (suala la) shamba ambapo watu fulani walilisha kondoo wao shambani hapo wakati wa usiku. Na Sisi tulikuwa Wenye kushuhudia hukumu yao. 79. Tukamfahamisha Suleiman (haki katika suala hilo) na kila mmoja wao tukampa madaraka na elimu. Na tukamfanyia wepesi Daud kuwa milima na ndege vimsifu Mwenyezi Mungu pamoja naye. Sisi ndiyo tuliyafanya yote hayo. 80. Na tukamfundisha kutengeneza mavazi ya vita ili kuwakinga nyie katika vita vitokeavyo baina yenu. Je, mtakuwa wenye kushukuru?

81. Na ni uwezo wetu ndiyo tukamfanyia Suleman upepo mkali wa kimbunga uwe murua uende kwa amri yake kwenye ardhi tuliyoibariki. Na Sisi ndio tunaojua kila kitu. 82. Na katika mashetani kuna wanaompigia mbizi (baharini kuleta mali) na kufanya kazi nyinginezo; nasi tulikuwa walinzi wao.

83. Na Ayyub (Job) pale alipomlilia Mola Wake Mlezi: ‘Hakika mimi nimepatwa na shida kubwa, Nawe ndiye Mwingi wa huruma zaidi ya wote wenye huruma’. 84. Basi tukamwitikia na tukamuondolea shida yake na tukamrudishia familia yake na tukazidisha idadi yao’ hii ikiwa ni huruma kutoka Kwetu, na jambo la kusherehekea kwa wote wale wanaotutumikia Sisi.

85. Na Ismaili na Idrisa na Dhulkifli, wote walikuwa miongoni mwa wanaosubiri. 86. Na tukawaingiza katika rehema Yetu. Hakika wao ni katika watu wema.

87. Na Dhun-Nun alipoondoka hali ameghadhabika na akadhani kuwa hatutakuwa na uwezo juu yake. Hatimaye

akalia katikati ya kiza kikuu: ‘Hapana Mola isipokuwa Wewe! Umetakasika! Hakika mimi nilikuwa miongoni mwa waliokosa!’. [88.] Basi tukamwitikia na tukamwokoa katika dhiki hiyo. Na kama hivyo Sisi tunawaokoa wenye kuamini.

[89.] Na Zakaria alipomlilia Mola Wake: ‘Ewe Mola Wangu Mlezi! Usiniache mpweke (ingawaje) Wewe ndiye bora ya wanaorithi’. [90.] Basi tukamwitikia na tukamruzukuYahya (John) na tukamponesha mkewe. Hakika wao walikuwa wepesi kufanya kheri na wakituomba kwa mapenzi na heshima na walikuwa wakitunyenyekea.

[91] Na (kumbuka yule) mwanamke aliyelinda uchi wake na tukampulizia humo Roho Wetu na tukamfanya yeye na mwanawe kuwa ni ishara kwa walimwengu.

[92.] Na hakika huu umma wenu ni umma mmoja. Na mimi ndiye Mola Wenu. Kwa hivyo niabuduni. [93.] Lakini (vizazi vilivyofuatia) wakavunja jambo lao (umoja), baina ya mtu na mwengine. (Ingawaje) Wote watarejea Kwetu. [94.] Na atendaye mema naye ni mumini, juhudi zake hazitatupiliwa mbali. Nasi tutamwandikia (mazuri).

[95.] Ni marufuku kwa wana-mji tuliuangamiza kuwa hawatarejea tena. [96.] Hadi hapo watu wa Yajuj na Majuj (Gog na Magog) watakapofunguliwa (kutoka kizuizini) wakawa wanasambaa kutoka kila sehemu ya mwinuko. [97.] Hapo miadi ya ukweli itakuwa inakaribia (kutekelezwa). Na hapo ndipo yatakapokodoka macho ya wale waliokufuru. Ole wetu sisi! Hakika tulikuwa tumeghafilika na haya, bali sisi tulikuwa tumekosea!

[98.] Hakika nyinyi na hivyo mnavyoviabudu kinyume cha Mwenyezi Mungu ni kuni za Jahannam. Ninyi mtafika huko. [99.] Lau kweli hawa walikuwa miungu, wasingeingia

motoni. Lakini kila mmoja wao atabaki huko milele.
100. Lao humo ni kulia kwa kwikwi, na wala hawatasikika
chochte. 101. Ama wale ambao rekodi zao nzuri kutoka
kwetu zilikwishatangulia, hao wataepushwa (na maafa
hayo). 102. Hawatasikia hata mvumo mdogo wa Jahannam.
Kile ambacho roho zao zinakipenda ndicho watachokipata
daima. 103. Hicho kitisho kikubwa hakitawatia huzuni. Na
Malaika watawapokea (wakiwaambia): ‘Hii ndiyo siku yenu
mliyokuwa mkiahidiwa’.

104. Siku tutakapozikunja mbingu kama zikunjwavyo
karatasi za vitabu. Kama vile tulivyoanza umbo la mwanzo
tutalirudisha tena. Ni ahadi tuliyojiwekea. Hakika Sisi
tutaitekeleza kwa vitendo. 105.Tulikwishaandika katika
Zaburi (Psalms) baada ya Ujumbe (wa Musa) kuwa hii ardhi
watairithi watumishi wangu walio wema. 106. Hakika katika
haya kuna ujumbe kwa watu wanaomwabudu Mwenyezi
Mungu (kikweli).

107. Na hatukukutuma wewe (Muhammad) ila uwe rehema
kwa viumbe wote. 108. Sema: Hakika yanayonifikia mimi
kwa njia ya ufunuo wa Wahyi ni kuwa ‘Mola wenu ni Mungu
Mmoja tu’. Je, nyinyi ni Waislamu? 109. Kama wakikataa,
basi sema: ‘Mimi nimewatangazia ujumbe sawa sawa.
Lakini sijui kama yako karibu au mbali hayo mliyoahidiwa’.
110. Hakika Yeye anajua kauli ya dhahiri na anajua
mnayoyaficha (moyoni). 111.Wala sijui pengine huu ni
mtihani kwenu na starehe fupi ya dunia hadi hapo. 112. Sema:’
Ewe Mola wangu Mlezi! Hukumu kwa haki. Na Mola Wetu
Mlezi Mwingi wa rehema ndiye aombwaye msaada dhidi ya
mnayomnasibishia.

22. Sura Al-Hajj

# SURA YA HIJJA

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 Enyi watu! Mcheni Mola Wenu Mlezi. Hakika tetemeko la Kiyama ni jambo kuu. 2 Siku mtakapokiona, kila mwenye kunyonyesha atamsahau amnyonyeshae na kila mwenye mimba atabwaga mimba yake. Na utawaona watu wamelewa, na kumbe hawakulewa. Lakini adhabu ya Mwenyezi Mungu ni kali mno. 3 Na miongoni mwa watu kuna anayebishana juu ya Mwenyezi Mungu bila ya ufahamu, na anamfuata kila shetani mwasi. 4 Ilani imetolewa dhidi yake kwamba anayemfanya rafiki huyo, bila shaka atampoteza na atamwongoza katika adhabu ya moto mkali.

5 Enyi watu! Ikiwa mna shaka ya kufufuliwa, basi kwa hakika tuliwaumba kutokana na udongo kisha kutokana na tone la manii kisha kutokana na pande la damu iliyoganda, kisha kutokana na pande la nyama lililokamilika na lisilokamilika. Ili tuwabainishie (uwezo wetu). Na tunakiacha kiendeele kubaki katika matumbo ya kizazi kile tukitakacho, hadi muda uliopangwa. Kisha tunawatoa hali ya kuwa watoto wachanga, kisha mkafikia kukomaa. Na yupo miongoni mwenu ambaye roho yake hutwaliwa (kabla ya uzee) na yupo miongoni mwenu anaerudishwa kwenye umri wa kotojiweza kabisa, hivi kwamba hajui chochote baada ya kuwa alikuwa akijua. Na unaiona ardhi haina uhai, kame. Lakini tunapoyateremsha maji juu yake, hututumuka na kupanda juu, tena humea kila aina ya mimea mizuri. 6 Hayo ni kwa sababu hakika

Mwenyezi Mungu ni kweli, na kwamba hakika Yeye Ndiye Mwenye kuhuisha wafu, na kwamba hakika Yeye ni Muweza wa kila kitu. [7] Na kwamba Kiyama kitakuja hapana shaka juu ya hilo. Na kwamba Mwenyezi Mungu atawafufua walio makaburini.

[8.] Na miongoni mwa watu wapo wanaobishanan juu ya Mwenyezi Mungu bila ya ufahamu wala mwongozo wala Kitabu kitoacho mwangaza. [9.] (Kwa dharau nyingi) hugeuza shingo yake ili awapoteze watu na njia ya Mwenyezi Mungu. Duniani atapata fedheha na siku ya Kiyama tutamuonjesha adhabu ya moto unaounguza. [10.] Hayo ni kwa sababu ya yale yaliyotangulizwa na mikono yako, kwa vile Mwenyezi Mungu si mwenye kuwadhulumu waja wake.

[11.] Na miongoni mwa watu yupo anayemwabudu Mwenyezi Mungu (akingojea) ukingoni. Ikimfika kheri hutulia, na ukimpata msukosuko hujipindua (kwa hasira). Huyo amepoteza dunia na Akhera; hiyo ndiyo hasara iliyo wazi.

[12.] Anaomba, badala ya Mwenyezi Mungu, kile kisichomdhuru wala kumnufaisha. Huko ndiko kupotelea mbali kabisa (na njia). [13.] Anamuomba yule ambaye bila shaka madhara yake yako karibu zaidi kuliko manufaa yake. Ubaya ulioje rafiki kama huyo, na ubaya gani huo mwenza kama huyo! [14.] Hakika Mwenyezi Mungu atawaingiza wale walioamini na wakatenda mema katika bustani ambazo hupita mito ya maji, maziwa, pombe na asali chini yake. Hakika Mwenyezi Mungu hufanya ayatakayo.

[15.] Aliyekuwa anadhani kwamba Mwenyezi Mungu hatamnusuru (Mtume wake) katika dunia na Akhera, hebu na afunge kamba juu ya paa kisha aikate, aone je, hila

yake hiyo itaondoa yale yanayomkasirisha? 16. Na namna
hiyo tumeiteremsha hii Qur'an kuwa ni Aya zilizo wazi, na
kwamba Mwenyezi Mungu humuongoza anayemtaka.

17. Hakika wale ambao wameiamini (Qur'an) na wale
ambao ni Mayahudi na Wasabia na Wakristo na Majus na
mapagani, hakika Mwenyezi Mungu atapitisha hukumu yake
kwa wote siku ya Kiyama. Hakika Mwenyezi Mungu ni
shahidi juu ya kila kitu.

18. Hivi huoni kuwa vinamsujudia Mwenyezi Mungu
vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini? Jua, mwezi,
nyota, milima, miti, wanyama na watu wengi. Na wengi pia
itawastahiki adhabu. Na anayetwezwa na Mwenyezi Mungu
hana wa kumheshimu. Hakika Mwenyezi Mungu hutenda
apendayo.

19. Hii ndiyo hali ya mahasimu wawili waliobishana
juu ya Mola Wao Mlezi: wale waliomkana watashonewa
nguo za moto na yatamiminwa juu ya vichwa vyao maji
yanayochemka. 20. Kwa maji hayo vitayeyushwa vilivyomo
matumboni mwao, na ngozi zao. 21. Na yatakuwako makomeo
ya chuma kwa ajili yao. 22. Kila wanapotaka kutoka humo
kwa sababu ya uchungu watarudishwa humo humo; na
(kuambiwa):'onjeni adhabu ya kuungua'.

23. Ama wale walioamini, wakatenda mema, hakika
Mwenyezi Mungu atawaingiza bustani ambazo hupita mito
ya maji, maziwa na asali chini yake. Watapambwa humo kwa
bangili za dhahabu na lulu na mavazi yao humo ni hariri.
24. Na wataongozwa kwenye maneno mazuri na wataongozwa
kwenye njia ya Mwenye kuhimidiwa.

25. Na wale waliokana na wakawazuia watu kupita njia
ya Mwenyezi Mungu na (wakawazuia na) Msikiti mtakatifu

ambao tumeufanya sawa sawa kwa watu: mwenyeji wa hapo na mgeni. Na yeyote ambaye kusudio lake humo ni kumtusi Mwenyezi Mungu, au kufanya uovu, tutamwonjesha adhabu chungu.

26. Na kumbuka pale tulipomweka Ibrahim kwenye sehemu ya nyumba (Kaaba), kwamba usinishirikishe hapo na yeyote, na isafishe nyumba Yangu kwa ajili ya wanaoizunguka na wanaosimama kwa ibada na wanaorukuu na wanaosujudu

27. Na watangazie watu Hijja; watakujia hali ya kutembea kwa miguu na juu ya aina mali mbali za ngamia waliokonda kwa kutembea kupitia miteremko mikali ya njia za majabalini za mbali. 28. Ili washuhudie manufaa yao na walitaje jina la Mwenyezi Mungu katika siku maalum juu ya wanyama aliowaruzuku. Basi kuleni katika hao na mumlishe mwenye shida aliye fukara. 29. Kisha wajisafishe taka zao, watimize nadhiri zao na waizunguke nyumba kongwe ya kale.

30. Ndivyo hivyo (Hijja). Na atayeitukuza miiko ya Mwenyezi Mungu hilo ni kheri yake mbele ya Mola Wake Mlezi. Na mmehalalishiwa wanyama wa kufugwa (muwapo katika Hijja) ila wale mliosomewa. Basi jiepusheni na uchafu wa (kuabudu) mizimu na mjiepushe na kauli ya uzushi....

31. Kwa kuwa mkweli mwenye kumtakasia imani Mwenyezi Mungu bila ya kumshirikisha na vingine. Na anayemshrikisha Mwenyezi Mungu ni kama kwamba ameporomoka kutoka mbinguni, kisha ndege wakamnyakua au upepo ukamtupa mahala mbali.

32. Ndivyo hivyo hali yake. Na anayezitukuza nembo za Mwenyezi Mungu, basi hiyo ni katika takua ya nyoyo. 33. Katika hao (wanyama) nyinyi mtanufaika nao hadi muda

ulioainishwa. Kisha mahali pake (pa kuchinjiwa) ni karibu na
nyumba kongwe ya kale.
34. Kila umma tumeupangia ibada ya (kutoa) kafara.
Ili walitukuze jina la Mwenyezi Mungu kwa ajili ya
alivyowaruzuku katika wanyama howa. Lakini Mungu Wenu
ni Mungu Mmoja yule yule. Kwa hiyo jisalimisheni Kwake.
Na wabashirie wanyenyekevu... 35. ambao anapotajwa
Mwenyezi Mungu nyoyo zao hujaa hofu ya adhama yake, na
walio na subira kwa yale yaliyowasibu, na wanaosimamisha
Swala, na wanaotoa katika vile tulivyowaruzuku.
36. Na ngamia wa kafara tumewafanya kwenu kuwa ni
miongoni mwa nembo za Mwenyezi Mungu. Ninyi mwapata
mazuri mengi kutoka kwao. Basi litajeni jina la Mwenyezi
Mungu juu yao wanaposimama safu (kwenda kuchinjwa). Na
wanapokuwa chini (wakilalia) ubavu (baada ya kuchinjwa),
kuleni baadhi yake na mlisheni asiyeomba na aombaye.
Ndiyo hivyo tumewafanya hawa (wanyama) wawe rahisi
kwenu kuwatumia, ili mpate kushukuru. 37. Si nyama zao wala
damu zao zinazomfikia Mwenyezi Mungu bali ni uchamungu
wenu ndiyo unaomfikia. Kama hivyo amewafanya hawa
wawe dhalili kwenu ili mumtukuze Mwenyezi Mungu kwa
alivyowaongoza. Na wape habari njema wenye kufanya
mema.
38. Hakika Mwenyezi Mungu huwakinga walioamini.
Hakika Mwenyezi Mungu hampendi kila haini (wa imani)
mtovu wa shukrani. 39. Wameruhusiwa kupigana wale
wanaoshambuliwa kwa vita kwa sababu wameonewa. Na
kwa hakika Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kuwanusuru.
40. Wale ambao wametolewa majumbani mwao pasipo haki,
ila tu kwa kuwa wanasema ‘Mola Wetu Mlezi ni Mwenyezi

Mungu'. Na lau Mwenyezi Mungu asingewakinga watu kwa (kuwatumia) watu wengine, basi zingebomolewa nyumba za Watawa, Makanisa, Mahekalu (Synagogue) na Misikiti, ambazo ndani yake hutajwa jina la Mwenyezi Mungu kwa wingi. Na hakika Mwenyezi Mungu humnusuru yule anayemnusuru Yeye. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mwenye enzi tukufu.

41. (Hao atakaowanusuru) Ni wale ambao tukiwapa madaraka katika ardhi husimamisha Swala na wakatoa Zaka na wakaamrisha mema na wakakataza mabaya. Na kwa Mwenyezi Mungu ndio kikomo cha mambo yote.

42. Wakikukadhibisha, jamii ya Nuh, kina A'd na Thamud pia walikadhibisha kabla yao. 43. Na jamii ya Ibrahim na jamii ya Lut. 44. Na watu wa Madyan, na Musa pia alikadhibishwa. Nikawapa muda makafiri, kisha nikawatia nguvuni. Ubaya wa namna gani jinsi kuwakataa kwangu watu hao kulivyokuwa.

45. Na (wakazi wa) miji kadhaa mingapi tumewateketeza kwa kufanya maovu? Mapaa ya nyumba zao yakaangukiana, visima vyao vikatelekezwa visitumiwe na majumba madhubuti yaliyojengwa kwa ustadi (yakageuka magofu)? 46. Hivi hawatembei katika ardhi ili wapate nyoyo (akili) za kuzingatia na masikio ya kusikilia? Kwa vile hakika si macho yanayopofuka, lakini zinazopofuka ni nyoyo zilizomo vifuani.

47. Wanakuharakisha ulete adhabu na hakika Mwenyezi Mungu hatashindwa kutekeleza ahadi Yake. Na siku moja kwa Mola Wako Mlezi ni kama miaka elfu kwa mnavyohesabu nyie. 48. Ni (wakazi wa) miji mingapi nimewapa muda na hali walikuwa wametenda maovu, kisha nikawati nguvuni? Na Kwangu Mimi pekee ndio marejeo yote.

49. Sema: Enyi watu! Hakika mimi ni muonyaji kwenu niliye
wazi. 50. Wale walioamini na wakatenda mema, watapata
maghufira na riziki zenye ukarimu. 51. Na wanaojitahidi
kuzipinga Aya Zetu hao ndio watu wa motoni

52. Na hatukumtuma kabla yako Mtume wala Nabii
ila anasoma shetani hutumbukiza (neno baya) katika
kisomo chake. Lakini Mwenyezi Mungu huyaondoa
anayoyatumbukiza shetani; kisha Mwenyezi Mungu
huzimakinisha Aya Zake. Mwenyezi Mungu ni Mjuzi,
Mwenye hekima. 53. Ili alifanye lile alilolitumbukiza shetani
kuwa mtihani kwa wale wenye maradhi katika nyoyo zao,
na wale ambao nyoyo zao zimekuwa ngumu. Na hakika
watendao maovu wamo katika utengano ulio mbali (na
ukweli). 54. Na Ili wajue wale ambao wamepewa elimu
kwamba hiyo (Qur'an) ni kweli itokayo kwa Mola Wako
Mlezi, na waiamini. Na ili nyoyo zao ziweze kuinyenyekea.
Na hakika Mwenyezi Mungu ndiye awaongozaye wale
ambao wameamini kwenye njia iliyonyooka.

55. Na wale ambao wamekufuru hawataacha kuwa katika
shaka ya hiyo (Qur'an) mpaka Kiyama kiwafikie ghafla
au iwafikie adhabu ya siku tasa. 56. Ufalme wa enzi wote
siku hiyo ni wa Mwenyezi Mungu. Atatoa hukumu baina
yao. Basi wale ambao wameamini na wakatenda mema,
watakuwa katika Bustani zenye neema. 57. Na wale ambao
wamekufuru na wakazikadhibisha ishara Zetu watapata
adhabu ya kufedhehesha.

58. Na wale ambao wameacha nyumba zao kwa ajili
ya njia ya Mwenyezi Mungu, kisha wakauawa au wakafa,
Mwenyezi Mungu atawaruzuku riziki njema. Na hakika
Mwenyezi Mungu ni Bora wa wanaoruzuku. 59. Kwa hakika

atawaingiza mahali watakapoparidhia. Na hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi, Mpole.

60. Ndivyo hivyo. Na anayelipiza kisasi kiasi kile kile cha majeraha aliyoyapata, kisha akashambuliwa tena, kwa hakika Mwenyezi Mungu atamsaidia. Na hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa msamaha, Mwingi wa maghufira.

61. Hayo ni kwa kuwa Mwenyezi Mungu huuingiza mchana katika usiku na huuingiza usiku katika mchana na kwamba Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia, Mwenye kuona.
62. Hayo ni kwa kuwa Mwenyezi Mungu ndiye Hakika, na kwamba wale wanaowaomba badala Yake ni batili, na hakika Mwenyzi Mungu ndiye aliye juu, Mkubwa.

63. Hivi huoni kwamba Mwenyezi Mungu huteremsha maji kutoka katika mawingu na mara ardhi inakuwa imevalishwa kijani?. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mpole, Mwenye habari.
64. Ni Vyake vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini. Na hakika Mwenyezi Mungu ni Mkwasi, Mwenye kusifiwa.

65. Hivi huoni kwamba Mwenyezi Mungu amevifanya viwatumikie nyinyi vilivyomo ardhini na majahazi yapitayo baharini kwa amri Yake. Na anazizuia mbingu zisianguke juu ya ardhi, isipokuwa kwa idhini Yake. Hakika Mwenyezi Mungu kwa watu ni Mpole, Mwenye huruma tele.
66. Naye ndiye ambaye amewaacheni hai kisha atawatwaa roho zenu, kisha atawarudishia uhai tena. Hakika mwanadamu ni kiumbe mtovu mno wa fadhila.

67. Kila umma tumewapa ibada zao wanazozifuata. Basi wasizozane nawe katika jambo hili. Na lingania kwa Mola Wako Mlezi; hakika wewe uko katika uongofu ulionyooka.
68. Na wakijadiliana nawe, basi sema: Mwenyezi Mungu anajua zaidi mnayoyatenda.
69. Mwenyezi Mungu atatoa

uamuzi kwenu siku ya Kiyama katika hayo mnayotofautiana.
70. Hivi hujui kwamba Mwenyezi Mungu anayajua yaliyomo
mbinguni na ardhini? Hakika hayo yamo katika rekodi zake.
Hilo kwa Mwenyezi Mungu ni jepesi!

71. Na wanaabudu badala ya Mwenyezi Mungu ambavyo
hakuviteremshia ushahidi wowote, na ambavyo hawana
ujuzi navyo. Waovu hawatakuwa na wa kuwasaidia.
72. Na wanaposomewa Aya Zetu zilizo wazi utaona chuki
katika nyuso za waliokufuru; hukaribia kuwavamia wale
wanaowasomea Aya Zetu. Sema: Je, niwaambiye yaliyo
mabaya zaidi kuliko haya? Ni moto wa Mwenyezi Mungu
aliowaahidi waliokufuru. Na ni marejeo mabaya hayo.

73 Enyi watu! Mnapigiwa mfano, usikilizeni: Hakika wale
mnaowaomba kinyume na Mwenyezi Mungu hawawezi
kuumba (hata) nzi, hata wakikusanyika kwa ajili ya hilo.
Na nzi akiwapokonya kitu hawana uwezo wa kukirejesha.
Ni dhaifu mno huyo anayeomba na anayeombwa!
74 Hawakumpa heshima Mwenyezi Mungu kiasi
anavyostahiki. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu,
Mwenye uwezo mkuu.

75. Mwenyezi Mungu huteua wajumbe miongoni mwa
Malaika na miongoni mwa watu. Hakika Mwenyezi Mungu
ni Mwenye kusikia, Mwenye kuona. 76. Anajua yaliyo mbele
yao na yaliyo nyuma yao. Na kwa Mwenyezi Mungu ndiyo
marejeo ya mambo yote.

77. Enyi walioamini! Rukuuni na sujuduni, na mwabuduni
Mola Wenu Mlezi, na fanyeni kheri ili mfaulu. 78. Na
kakamaeni katika njia ya Mwenyezi Mungu kama
inavyostahiki. Yeye ndiye ambaye amewachagua nyie.
Wala hakuwafanyia uzito katika dini. Ni utamaduni wa

baba yenu Ibrahim. Yeye (Allah) aliwaita nyie 'Waislamu' tangu zamani na katika (ujumbe) huu. Ili Mtume awe shahidi juu yenu na nyinyi muwe mashahidi juu ya watu wengine. Basi simamisheni Swala na toeni Zaka na shikamaneni na Mwenyezi Mungu. Yeye ndiye Mlinzi wenu. Mlinzi bora na Msaidizi bora kabisa.

### 23. Sura Al-Mu'minun

## SURA YA WAUMINI

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 Hakika wamefaulu waumini. 2 Ambao ni wanyenyekevu
katika Swala zao. 3 Na ambao hujiepusha na mambo ya
upuuzi. 4 Na ambao kwa kutoa Zaka ni hodari. 5 Na ambao
wanazilinda tupu zao. 6 Isipokuwa kwa wake zao au kwa
(wajakazi) iliyowamiliki mikono yao ya kuume. Kwa hao
hakuna kulaumiwa. 7 Lakini anayetafuta kinyume cha
hayo basi hao ndio wapetukao mipaka. 8 Na wale ambao
wanachunga amana zao na ahadi zao. 9 Na ambao Swala zao
wanazihifadhi. 10 Hao ndio warithi. 11 Watakaorithi (Pepo ya)
Firdausi, wakae humo milele.

12 Na hakika tumemuumba mwanadamu kutokana na
johari ya udongo asilia. 13 Kisha tukamweka akiwa tone la
manii katika makazi madhubuti. 14 Kisha tukaliumba tone
kuwa pande la damu linaloning'inia na tukaliumba pande
hilo la damu kuwa pande la nyama, na pande hilo la nyama
tukaliumba kuwa mifupa na mifupa tukaivika nyama. Basi
ametukuka Mwenyezi Mungu bora wa waumbaji. 15 Kisha

bila shaka nyinyi baada ya hapo mtakufa. 16 Kisha hakika
nyinyi siku ya Kiyama mtafufuliwa.

17. Hakika tumeumba juu yenu tabaka saba. Nasi si ambao
hawajali juu ya walichokiumba. 18. Na tumewateremshia
kutoka mbinguni maji kwa kiasi (cha mahitajio) na
tukayafanya yatulie ardhini. Na hakika sisi tunaweza
kuyaondoa. 19. Kwa maji hayo tukawaoteshea bustani za
mitende na mizabibu, mnapata humo matunda mengi na
katika hayo mnakula. 20. Na mti unaoota katika Mlima Sinai
unaotoa mafuta na ufanywao kitoweo kwa wale wanaoutumia
kwa chakula. 21. Na hakika katika wanyama wafugwao
kuna mazingatio kwenu. Tunawanywesha kutokana na vile
vilivyomo matumboni mwao, na pia mnapata manufaa
mengine chungu nzima kutokana nao, na mnakula nyama
yao. 22. Na juu yao na juu ya merikebu mnabebwa.

23. Na hakika tulimtuma Nuh (Noah) kwa watu wake,
akasema: Enyi watu wangu! Mwabuduni Mwenyezi
Mungu. Hamna mungu asiyekuwa Yeye. Hivi hamumhofii?
24. Machifu waliokufuru wakasema: Huyu si chochote ila ni
mtu tu kama nyinyi, anataka kujipatia ukubwa juu yenu. Na
lau Mwenyezi Mungu angependa, angeteremsha Malaika.
Hatukuyasikia haya kwa mababa zetu wa zamani. 25. Huyo
si lolote isipokuwa mtu mwenye jinni (limtialo wazimu).
Mwacheni tu kidogo.

26. (Nuh) akasema: Mola Wangu! Ninusuru kwa kuwa
wamenikadhibisha. 27. Tukamtumia Wahyi: 'Tengeneza
Jahazi mbele ya macho yetu na kwa mwongozo wetu. Basi
itakapokuja amri Yetu na chemichemi za maji zikafoka, hapo
waingize ndani ya Jahazi kila aina ya viumbe wawili wawili,
dume na jike, na pia familia yako, isipokuwa wale ambao

kauli imekwishatangulia juu yao. Wala usiniambie kitu juu ya watu waovu, kwani bila shaka watagharikishwa (katika mafuriko).

28. Na ukishapanda juu ya jahazi wewe na walio pamoja nawe, sema, 'sifa njema (Alhamdulillah) ni za aliyetuokoa na watu waovu'. 29. Na sema, Mola Wangu Mlezi! 'Niwezeshe nishuke kwa baraka. Wewe ndiye bora wa kutuwezesha kushuka'. 30. Hakika katika hilo kuna ishara kwa wanaadamu (ili wafahamu) na ndiyo maana tunawapa majaribio.

31. Kisha baada yao tukaanzisha kizazi kingine. 32. Tukawapelekea Mtume miongoni mwao (kuwaambia): 'Mwabuduni Mwenyezi Mungu! Hamna Mungu ila Yeye, Kwa nni hamumchi? 33. Machifu katika watu wake waliomkana Mwenyezi Mungu na wakakana (kuwepo) makutano ya huko Akhera, na ambao tuliwadekeza kwa starehe katika maisha ya duniani, wakasema: 'Huyu si lolote ila binadamu kama nyinyi, anakula mnachokila na anakunwa mnachokinwa'. 34. Ninyi mkimtii mtu kama nyie, basi hakika mtakuwa mmepata hasara.

35. Je, anawaahidi ati mtakapokufa na mkawa mchanga na mifupa kwamba mtatolewa tena? 36. Hayawi! Hayawi hayo mnayoahidiwa. 37. Hakuna (maisha mengine) isipokuwa haya maisha yetu ya dunia hii tu; tunakufa na tunaishi. Wala sisi si wenye kufufuliwa kamwe. 38. Huyo si lolote ila ni mtu anayemzushia Mwenyezi Mungu uongo, wala sisi si wanaomwamini.

39. (Mtume) akasema: 'Mola Wangu Mlezi, ninusuru kwa wanavyonisingizia uongo'. 40. Akasema: 'Muda mchache tu ujao watakuwa wanajuta'. 41. Sauti ya mpasuko mkubwa ikawasomba kwa njia ya haki na uadilifu. Tukawafanya

(kama) takataka zinazoelea juu ya maji. Potelea mbali watu waovu!

42. Kisha baada yao tukaleta mataifa mengine. 43. Hapana taifa liwezalo kuitanguliza ajali yake wala kuikawiza. 44. Kisha tukawapeleka mitume Wetu mmoja baada ya mwingine. Kila taifa alipowajia Mtume wao walimkanusha. Tukawafuatanisha hawa baada ya wale (kwa kuwadhibu). Tukawafanya ni hadithi tu za kusimuliwa. Potelea mbali mijitu isiyoamini!

45. Kisha tukamtuma Musa (Moses) na nduguye Harun(Aaron) pamoja na ishara Zetu, na hoja zilizo wazi. 46. Kwenda kwa Firaun (Pharaoh) na machifu wake, lakini wakajivuna na walikuwa watu jeuri mno. 47. Wakasema: hivi tuwaamini watu wawili hawa kama sisi, na ilhali jamaa zao ni watumwa wetu sisi? 48. Wakawasingizia uwongo. Wakawa miongoni mwa walioangamizwa. 49. Na hakika tulimpa Musa Kitabu, ili wapokee mwongozo.

50. Na tukamfanya mwana wa Maryam na mama yake kuwa kuwa ishara. Na tukawapa hifadhi kwenye mwinuko, mahali penye utulivu na chemchemi za maji.

51. Enyi Mitume! Kuleni (tumieni) vitu vyote vilivyo vyema, vizuri na fanyeni mema. Hakika Mimi ni Mjuzi wa mnayoyatenda. 52. Na hakika umma wenu huu ni umma mmoja na Mimi ni Mola Wenu Mlezi, basi niogopeni Mimi.

53. Lakini wao wakatengana katika jambo lao (la umoja) kwenye vikundi mbali mbali. Kila kundi linafurahia waliyo nayo. 54. Basi waache katika kughafilika kwao hadi muda (uliopangwa). 55. Je wanadhania kwa vile tunawapa mali nyingi na watoto, 56. Ndio tunawahimiza wafanye mema? La, hawatambui tu! (hakika shabaha ni kuwajaribu).

57. Hakika wale ambao humwogopa Mola Wao Mlezi,
wakamnyenyekea, 58. Na wale ambao wanaamini Aya za
Mola Wao Mlezi, 59. Na wale ambao hawamshirikishi Mola
Wao Mlezi, 60. Na wale ambao wanatoa walichopewa na hali
nyoyo zao zinaogopa kwamba (siku moja) watarejea kwa
Mola Wao…. 61. Hao ndio wanaoikimbilia kheri na ndio
watakaotangulia kuzifikia. 62. Na hatumlazimishi mtu yeyote,
ila kwa kadri ya uwezo wake. Na tuna Kitabu kisemacho
kweli. Nao hawatadhulumiwa.

63. Bali nyoyo zao zimo katika kughafilika na haya na wana
vitendo vingine watakavyoendelea kuvitenda…. 64. Mpaka
tutakapowatia katika adhabu wale waliodekezwa kwa starehe
za dunia miongoni mwao, hapo ndipo watakapolalamika
65. Msilalamike leo! Hakika nyinyi hamtasaidiwa nasi.
66. Hakika mlikuwa mkisomewa Aya Zangu nanyi mkawa
mnarudi nyuma. 67. Na huku mkiifanyia kiburi Qur'an, na
usiku mkiizungumzia kama ngano za kuchangamsha!

68. Je, hawakuifikiria kwa kina kauli (ya Mwenyezi Mungu)
au yamewafikia (mapya) yasiyowafikia baba zao wa kale?
69. Au hawakumjua Mtume wao ndio maana wanamkataa?
70. Au wanasema ana wazimu? Bali amewajia na ukweli na
wengi wao huchukia ukweli. 71. Na laiti ukweli ungefuata
wapendavyo wao, basi mbingu na ardhi na vilivyomo ndani
yao vingechanganyikiwa na kuharibika. Bali tumewaletea
ujumbe unaowaonya. Nao wanaupinga ujumbe wao.

72. Au unawaomba malipo? Lakini malipo ya Mola Wako
Mlezi ni bora na Yeye ndiye Bora kabisa ya wanaoruzuku.
73. Na hakika wewe unawalingania kwenye njia iliyonyooka.
74. Na hakika wale ambao hawaamini Akhera wanajitenga
nayo

75. Na laiti tungewaonea huruma tukawaondolea shida zote walizo nazo, bila shaka wangeendelea na upotevu wao wakihangaika huku na huko. 76. Na hakika tulikwishawatia adhabu, lakini hawakuelekea kwa Mola wao Mlezi, wala hawakuwa wanyenyekevu. 77. Mpaka tulipowafungulia mlango wa adhabu kali, hapo ndipo wakawa wenye kukata tamaa.

78. Yeye ndiye aliyewabunia usikizi na uoni na nyoyo. Ni kuchache mno kushukuru kwenu! 79. Yeye ndiye aliyewaumba muishi katika ardhi na Kwake mtakusanywa. 80. Yeye ndiye anayehuisha na kufisha na Yeye ndiye mwenye mabadiliko ya usiku na mchana. Je, hamjui?

81. Bali walisema kama walivyosema wa mwanzo. 82. Kwamba je, tukishakufa tukawa mchanga na mifupa ndio tutafufuliwa? 83. Tuliahidiwa haya zamani sisi na baba zetu. Haya si chochote ila visa vya uongo vya watu wa kale.

84. Sema, ni ya nani ardhi na vilivyomo ndani yake, kama nyinyi mnajua? 85. Watasema, ni vya Mwenyzi Mungu. Basi je, hamkumbuki? 86. Sema, ni nani Mola wa mbingu saba na Mola wa Ufalme Adhimu wa Enzi? 87. Watasema, ni vya Mwenyezi Mungu. Sema, je, hamhofii (ghadhabu yake)? 88. Sema, ni nani yaliyo mkononi mwake madaraka ya kila kitu? Na yeye ni Mlinzi wa kila kitu, wala halindwi (na yeyote), kama mnajua? 89. Watasema, ni wa Mwenyezi Mungu. Sema, basi vipi mnadanganyika?

90. Bali tumewaletea ukweli. Na kwa hakika wao ni waongo. 91. Mwenyezi Mungu hakujifanyia mwana, wala hakuna mungu mwingine pamoja naye. Kama wangelikuwepo, basi kila mungu angelitwaa alichokiumba (akenda nacho). Na miungu wengine wangetaka kuwa mabosi juu ya wengine!

Ametakasika Mwenyezi Mungu na hayo wanayomnasibishia. [92.] Mjuzi wa ghaibu na dhahiri. Ametukuka juu ya hayo wanayomshirikisha nayo.

[93.] Sema, Mola Wangu Mlezi! Ikiwa utanionesha yale wanayoonywa dhidi yake... [94.] Basi Ewe Mola Wangu Mlezi! Usiniweke katika (kundi la) hao watu waovu. [95.] Na hakika sisi tuna uwezo wa kukuonesha yale tunayowaahidi.

[96.] Kinga mashambulio yao kwa kufanya mema. Hakika Sisi tunajua zaidi wanayoyasema. [97.] Na sema, Mola Wangu Mlezi! Najikinga Kwako na vishawishi vya Shetani. [98.] Na naomba hifadhi yako, Ewe Mola wangu Mlezi, wasinikaribie.

[99.] Mpaka yanapomfikia mmoja wao mauti, husema: Mola Wangu Mlezi! Nirudishe..... [100.] Ili nikatende mema katika yale niliyokuwa nimeyapuuza! Wapi! Anajisemea tu!. Mbele yao kuna uzio hadi mpaka siku watakapofufuliwa. [101.]Basi itakapopuziwa parapanda, hapo hakutakuwa na udugu baina ya watu siku hiyo, wala hawatajuliana hali. [102.]Basi ambao mizani zao zitakuwa nzito hao ndio wenye kufaulu. [103.]Na wale ambao mizani zao zitakuwa nyepesi, hao ndio waliozitia hasara roho zao na ndani ya Jahannam watakaa milele [104.]Moto utababua nyuso zao, nao humo watakuwa na tabasamu (la meno pekee) baada ya kumomonyoka nyama za midomo yao.

[105.]Je, hazikuwa Aya Zangu mkisomewa na nyinyi mkizikadhibisha? [106.] Watasema: Mola Wetu Mlezi! Tulizidiwa na uovu wetu na tukawa watu tuliopotea. [107.] ‘Mola Wetu Mlezi! Tutoe humu motoni. Na tukirudia tena, basi kweli sisi ni waovu’. [108.]Atasema: ‘Tokomeeni humo, wala msinisemeshe’. [109.] Hakika lilikuwapo kundi katika waja Wangu likisema: ‘Ewe Mola Wetu Mlezi! Tusamehe

na utuonee huruma, na Wewe ndiwe Bora wa wenye kuhurumia' [110.] Lakini ninyi mkawakejeli kiasi kejeli zenu zikawasahaulisha ujumbe wangu, na mkawa mwaendelea kuwacheka. [111.] Hakika Mimi leo nimewalipa hao kwa vile walivyosubiri. Hakika hao ndio wenye kufuzu.

[112.] (Malaika) Atawauliza: Miaka mingapi mlikaa duniani? [113.] Watasema: Tumekaa siku moja au sehemu ya siku, hebu waulize wanaotunza hesabu. [114.] Atasema: Basi hamkukaa isipokuwa muda mchache tu, laiti mngelikuwa mnajua!

[115.]Je, mnadhani kuwa tuliwaumba kwa mchezo tu na kwamba nyinyi hamtarudishwa Kwetu (kuwajibika)? [116.] Ametukuka Mwenyezi Mungu, Mfalme wa Hakika. Hapana Mungu ila Yeye, Mola wa Ufalme wa Enzi ya kuheshimiwa. [117.]Na anayemuomba - pamoja na Mwenyezi Mungu - mungu mwingine, huyo hana madaraka ya kufanya hivyo. Naye hakika atawajibika kwa Mola Wake Mlezi pekee. Wasioamini bila shaka hawatafanikiwa. [118.]Na sema: Mola Wangu Mlezi! Toa msamaha na urehemu nawe ni bora zaidi ya wanaorehemu.

## 24. Sura An-Nur

## SURA YA MWANGAZA

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

[1] Hii ni Sura tuliyoiteremsha na tukafanya ni lazima (hukumu zilizomo) na tukateremsha ndani yake Aya zilizo wazi, ili mpokee maonyo. [2] Mzinifu mwanamke na mzinifu mwanamume mchapeni kila mmoja wao viboko mia. Wala

isiwashike huruma kwa ajili yao katika kutekeleza sheria ya Mwenyezi Mungu, ikiwa nyinyi mnamwamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho. Na lishuhudie adhabu yao kundi la waumini. [3] Mwanamume mzinifu hamwoi ila mwanamke mzinifu au mwanamke mshirikina. Na mwanamke mzinifu haolewi ila na mwanamume mzinifu au mwanamume mshirikina. Na hayo yameharamishwa kwa waumini.

[4] Na wale ambao wanawasingizia wanawake wanaoheshimika kisha wasilete mashahidi wane, basi watandikeni viboko themanini. Na msiwakubalie ushahidi wao tena. Na hao ndio wavunjaji wa sheria. [5] Isipokuwa wale waliotubia baada ya hayo na wakajirekebisha; kwani hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe, Mwingi wa huruma.

[6.] Na wale wanaowasingizia wake zao na wakawa hawana mashahidi ila wao wenyewe tu, basi ushahidi wa mmoja wao utakuwa kushuhudia mara nne kwa kiapo cha Mwenyezi Mungu ya kwamba hakika yeye ni katika wasema kweli. [7.] Na mara ya tano kwamba laana ya Mwenyezi Mungu iwe juu yake ikiwa ni miongoni mwa waongo. [8.] Na mke itamwondokea adhabu kwa kutoa shahada mara nne kwa kiapo cha Mwenyezi Mungu, kwamba huyo mume ni miongoni mwa waongo. [9.] Na mara ya tano kwamba ghadhabu ya Mwenyezi Mungu iwe juu yake, kama huyo mume ni miongoni mwa wasemao kweli. [10.] Na lau kuwa si fadhila za Mwenyezi Mungu juu yenu na rehema Yake, na kwamba Mwenyezi Mungu ni Mwenye kutakabali toba, Mwenye hekima (mngeharibikiwa).

[11.] Hakika wale waliozusha uwongo ni kundi miongoni mwenu. Msiufikirie kuwa ni vibaya kwenu, bali hiyo ni kheri

kwenu. Kila mmoja katika wao atapata aliyoyachuma katika madhambi. Na yule aliyejitwika uongozi wa jambo hilo miongoni mwao atapata adhabu kubwa.

12. Kwa nini waumini wanaume na wanawake walipousikia uwongo huu, wasitie taswira njema katika akili zao na kusema ‘huu ni uwongo ulio wazi?’ 13. Kwa nini hawakuleta mashahidi wane kuthibitisha uzushi huo? Na kwa vile hawakuleta mashahidi, basi hao mbele ya Mwenyezi Mungu ni waongo tu.

14. Na lau si fadhila ya Mwenyezi Mungu juu yenu na rehema Yake katika dunia na Akhera, bila shaka ingewapata adhabu kubwa kwa sababu ya yale mliyojiingiza kikichwa-kichwa. 15. Mlipoyapokea kwa ndimi zenu na mkayasema kwa vinwa vyenu mambo msiyoyajua, mkifikiri hilo ni jambo dogo kumbe ni kubwa kwa Mwenyezi Mungu. 16. Na kwa nini mlipoyasikia msiseme: ‘Haistahili sisi kuzungumza haya; Kutakasika na mabaya ni Kwako Mola wetu!! Huu ni uzushi mkubwa’. 17. Mwenyezi Mungu anawaonya msirudie tena kufanya kama haya, ikiwa nyinyi ni waumini. 18. Na Mwenyezi Mungu anawabainishia Aya na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi, Mwenye hekima.

19. Hakika wale wanaopenda kuona kashfa inazagaa katika jamii ya waumini, watapata adhabu chungu duniani na Akhera. Na Mwenyezi Mungu anajua na nyinyi hamjui. 20. Na lau si fadhila ya Mwenyezi Mungu juu yenu na rehema Yake na kwa kuwa Mwenyezi Mungu ni Mpole, Mwenye kurehemu (mngeharibikiwa kabisa).

21. Enyi walioamini! Msifuate nyayo za shetani. Na atakayefuata nyayo za shetani, basi yeye huamrisha machafu na maovu. Na lau si fadhila ya Mwenyezi Mungu juu yenu

na rehema Yake, asingetakasika miongoni mwenu yoeyote. Lakini Mwenyezi Mungu humtakasa amtakaye na Mwenyezi Mungu ni Msikizi, Mjuzi.

22. Na asithubutu miongoni mwenu (ninyi) wenye vya ziada na uwezo, kula kiapo kuwa hawatowasaidia jamaa zao, maskini na waliohama kwa sababu ya Mwenyezi Mungu. Na wasamehe (yaliyopita) na waachilie mbali. Je, ninyi hampendi Mwenyezi Mungu awasamehe? Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa maghufira, Mwenye kurehemu.

23. Hakika wanaowasingizia wanawake wanaojiheshimu, waliopitiwa kidogo (lakini) waumini, wamelaaniwa duniani na Akhera na watapata adhabu kubwa. 24. Siku ambayo zitawashuhudia ndimi zao na mikono yao na miguu yao kwa waliyokuwa wakiyatenda. 25. Siku hiyo Mwenyezi Mungu atawapa kikamilifu malipo yao ya haki na watajua kwamba hakika Mwenyezi Mungu ndiye Hakika iliyo wazi.

26. Wanawake wachafu wanawastahiki wanaume wachafu, na wanaume wachafu wanastahiki wanawake wachafu. Na wanawake wema wastahiki wanaume wema, kadhalika wanaume wema ni wa wanawake wema. Hao hawataathiriwa na wayasemayo, (kwani) wao watapewa msamaha na riziki ya heshima.

27. Enyi walioamini! Msiingie nyumba zisizo nyumba zenu mpaka muoombe ruhusa na muwatolee salaam wenyewe. Hayo ni bora kwenu. Ili muwe watiifu. 28. Na msipomkuta yoyote humo basi msiingie mpaka mruhusiwe. Na mkiambiwa rudini, basi rudini. Hivyo ni safi zaidi kwenu na Mwenyezi Mungu anajua mnayoyatenda. 29. Si vibaya kwenu kuingia nyumba zisizokaliwa (na watu) ambazo mna

manufaa nazo. Na Mwenyezi Mungu anajua mnayoyadhirisha na mnayoyaficha.

30. Na waambie waumini wanaume wainamishe macho yao na wazilinde tupu zao. Hivyo ni kujitakasa kuliko bora zaidi kwao. Hakika Mwenyezi Mungu ana habari za wanayoyafanya.

31. Na waambie waumini wanawake wainamishe macho yao na wazilinde tupu zao, wala wasioneshe uzuri na mapambo yao, isipokuwa unajiotokeza (kwa kawaida). Na waangushe shungi zao juu ya vifua vyao. Na wasidhihirishe uzuri na mapambo yao ila kwa waume zao, au baba zao, au baba wa waume zao, au watoto wao, au watoto wa waume zao, au kaka zao, au watoto wa kaka zao, au watoto wa dada zao, au wanawake wenzao, au (watumwa wa kiume) iliyowamiliki mikono yao ya kuume, au wafuasi wanaume wasio na matamanio, au watoto wadogo ambao hawajajua uchi wa wanawake. Wala wasipige chini miguu yao ili yajulikane mapambo waliyoyaficha. Na tubuni kwa Mwenyezi Mungu nyote enyi waumini ili mpate kufanikiwa.

32. Na waozeni waseja (mabachela walio huru) miongoni mwenu, na walio wema katika watumwa wenu na wajakazi wenu. Wakiwa mafukara Mwenyezi Mungu atawatosheleza katika fadhila Zake; na Mwenyezi Mungu ni Mpana wa neema, Mwenye kujua. 33. Na wajizuilie na machafu wale wasiopata cha kuolea, mpaka Mwenyezi Mungu awatosheleze katika fadhila Zake. Na wale ambao wanataka kuandika (mkataba wa kutoka utumwani, kwa kujilipia) katika wale ambao imewamiliki mikono yenu ya kuume, basi waandikieni mkataba, kama mkiona kheri kwao. Na wapeni katika mali ya Mwenyezi Mungu aliyowapa. Wala msiwalazimishe

wajakazi wenu kufanya umalaya kwa ajili ya kutafuta pato la maisha, ikiwa wanataka kujichunga. Na atakayewalazimisha basi Mwenyezi Mungu baada ya kulazimishwa kwao huko ni Mwingi wa maghufira, Mwenye kurehemu (wao). 34. Na hakika tumewateremshia Aya zinazobainisha na mifano kutokana na waliopita kabla yenu na mawaidha kwa wenye takua.

35. Mwenyezi Mungu ni Nuru ya mbingu na ardhi. Mfano wa nuru yake (katika moyo wa muumini) ni kama shubaka ndani yake mna taa. Taa hiyo imo katika tungi. Tungi hilo ni kama nyota inayomeremeta, inayowashwa kwa mafuta yanayotokana na mti uliobarikiwa, mzaituni. Si wa mashariki wala magharibi. Yanakurubia mafuta yake kuwaka ingawa hayajaguswa na moto Nuru juu ya nuru. Mwenyezi Mungu humuongoza kwenye nuru Yake amtakaye. Na Mwenyezi Mungu huwapigia watu mifano; na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua kila kitu.

36. (Nuru yake imo) Katika nyumba ambazo Mwenyezi Mungu amezifanya ziinuke katika utukufu wa kutajwa jina lake humo. Humsabihi humo asubuhi na jioni..... 37. Watu ambao hawashughulishwi si na biashara wala bidhaa wakaacha kumsifu Mwenyezi Mungu, na kusimamisha Swala na kutoa Zaka. Wanaihofu siku ambayo nyoyo na macho yatageuka. 38. Ili Mwenyezi Mungu awalipe bora kuliko yale waliyoyatenda, na awazidishie katika fadhila Zake. Na Mwenyezi Mungu humruzuku amtakaye bila ya kipimo.

39. Na waliokufuru vitendo vyao ni kama mazigazi jangwani. Mwenye kiu huyadhania ni maji, hata akiyaendea hakuti chochote; lakini amkute Mwenyezi Mungu hapo amlipe hesabu yake sawasawa. Na Mwenyezi Mungu

ni mwepesi wa kuwajibisha. 40. Au ni kama giza katika bahari kuu, iliyofunikwa na mawimbi juu ya mawimbi na juu yake yapo mawingu - giza juu ya giza. Akiutoa mkono wake anakaribia asiuone. Na ambaye Mwenyezi Mungu hakumjaalia kuwa na nuru, basi hawi na nuru.

41. Hivi huoni kwamba vinamsifu Mwenyezi Mungu vilivyomo mbinguni na ardhini na ndege wakikunjua mbawa zao? Kila mmoja amekwishajua Swala yake na namna ya kumsifu Yeye. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa wayatendayo. 42. Na ni wa Mwenyezi Mungu ufalme wa mbingu na ardhi, na kwa Mwenyezi Mungu ndio marejeo.

43. Je, huoni kwamba Mwenyezi Mungu huyasukuma mawingu taratibu, kisha huyaambatanisha pamoja, kisha huyafanya mrundo? Ukaona mvua ikitokea katikati yake. Na huteremsha kutoka mbinguni, kwenye milima ya mawingu, mvua ya mawe, akamsibu nayo amtakaye na akamwepusha nayo amtakaye. Mmetuko wake wa umeme hukaribia kupofua macho. 44. Mwenyezi Mungu hufanya usiku na mchana ikipokezana. Hakika katika hilo kuna mazingatio kwa wenye busara.

45. Na Mwenyezi Mungu amemuumba kila mnyama kutokana na maji. Kuna yule baina yao yao atembeae kwa tumbo lake, kuna atembeae kwa miguu miwili na kuna atembeae kwa minne. Mwenyezi Mungu huumba atakacho. Hakika Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kila kitu. 46 Hakika tumeteremsha Ishara zinazobainisha. Na Mwenyezi Mungu humuongoza atakaye kwenye njia iliyonyooka.

47. Na (wanafiki) husema tumemwamini Mwenyezi Mungu na Mtume na tumetii. Kisha kikundi katika wao hugeuka baada ya hayo. Wala wao si wenye kuamini. 48. Na

wanapoitwa mbele ya Mwenyezi Mungu na Mtume Wake ili Mtume awatolee hukumu baina yao, kikundi kimoja kinakataa. 49. Na ikiwa haki ni yao wanakuja kwake kwa hamasa. 50. Kwani wana maradhi katika nyoyo zao au wana shaka na Mtume au wanahofia kuwa Mwenyezi Mungu na Mtume wake hawathukumu kwa haki na uadilifu?? Bali wao ndio madhalimu.

51. Haiwi kauli ya waumini wanapoitwa kwa Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, isipokuwa tu ni kusema: 'Tumesikia na tumetii'. Na hao ndio wenye kufaulu. 52. Na wenye kumtii Mwenyezi Mungu na Mtume Wake na wakamwogopa Mwenyezi Mungu na wakamcha, basi hao ndio wenye kufuzu.

53. Na waliapa kwa Mwenyezi Mungu kwa ukomo wa viapo vyao ya kwamba ukiwaamuru, hawatasita kutoka (kwenda vitani). Sema: msiape! Utiifu ndiyo busara zaidi! Hakika Mwenyezi Mungu ana habari za mnayoyatenda. 54. Sema: Mtiini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake. Kama mkikataa kutii, basi Mtume huwajibika kwa wajibu aliobebeshwa pekee, na nyie mnawajibika kwa wajibu mliobebeshwa. Na mkimtii yeye mtaongoka. Na wajibu pekee wa Mtume ni kufikisha (ujumbe) wazi wazi.

55. Mwenyezi Mungu amewaahidi wale ambao wameamini na wakatenda mema kuwa hakika atawafanya makhalifa katika ardhi, kama alivyowafanya waliokuwa kabla yao. Na kwa yakini atawaimarishia dini yao aliyowapendelea na hakika atawabadilishia amani baada ya hofu yao. Wawe wananiabudu, hawanishirikishi. Na mwenye kukufuru baada ya hayo, basi hao ndio waasi.

56. Na simamisheni Swala na toeni Zaka na mtiini Mtume

ili mpate kuhurumiwa. [57.] Usiwadhanie waliokufuru kwamba watashinda (mipango ya Mungu), la. Na makazi yao ni motoni na hakika ni marejeo maovu.

[58.] Enyi walioamini! Na wawaombeni ruhusa- wale ambao imewamiliki mikono yenu ya kuume na wale ambao hawajafikia baleghe miongoni mwenu, mara tatu: kabla ya Swala ya Alfajiri na wakati mnapovua nguo zenu adhuhuri, na baada ya Swala ya Isha. Ni nyakati tatu za faragha kwenu. Si vibaya kwenu wala kwao baada ya nyakati hizi, kuzungukiana nyinyi kwa nyinyi. Hivyo ndivyo Mwenyezi Mungu anavyowabainishia Aya; na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi, Mwenye hekima. [59.] Na watoto wanapofikia kubaleghe basi (pia) na waombe ruhusa, kama walivyoomba ruhusa wa kabla yao. Hivyo ndivyo Mwenyezi Mungu anavyowabainishia Aya Zake, na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi, Mwenye hekima. [60.] Na wanawake wakongwe ambao hawatarajii kuolewa, si vibaya kwao wakipambua nguo zao (za nje) bila ya kujishaua kwa mapambo. Na kama wakijistahi ni bora kwao. Na Mwenyezi Mungu ni Msikizi, Mjuzi.

[61.] Si vibaya kwa kipofu, wala kwa kiwete, wala kwa mgonjwa, wala kwenu nyinyi, mkila kwenye nyumba zenu, au nyumba za baba zenu au nyumba za mama zenu au nyumba za kaka zenu, au nyumba za dada zenu, au nyumba za baba wadogo zenu, au nyumba za shangazi zenu, au nyumba za wajomba wenu, au nyumba za mama wadogo wenu, au za mliowashikia funguo zao au rafiki yenu. Si vibaya kwenu mkila pamoja au mbali mbali. Na mkiingia katika nyumba amkianeni maamkuzi yatokayo kwa Mwenyezi Mungu yenye baraka yaliyo mema (Salaam Alaykum). Hivyo ndivyo

anavyowabainishia Mwenyezi Mungu Aya Zake mpate kutia akilini.

62. Hakika waumini ni wale tu ambao wamemwamini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake na wakiwa pamoja naye kwa jambo linalowahusu wote, hawaondoki mpaka wamtake ruhusa. Hakika wale wanaokuomba ruhusa, hao ndio wanaomwamini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake. Na watakapokuomba ruhusa kwa baadhi ya mambo yao, mruhusu umtakaye miongoni mwao na uwaombee maghufira kwa Mwenyezi Mungu; hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa maghufira, Mwenye kurehemu.

63. Msifanye kumwita Mtume baina yenu kama mnavyoitana nyinyi kwa nyinyi. Hakika Mwenyezi Mungu anawajua miongoni mwenu wale wanaoondoka kwa visingizio. Basi watahadhari wale ambao wanahalifu amri yake, isije ikawapata fitna au ikawapata adhabu chungu.
64. Ndiyo! Hakika ni vya Mwenyezi Mungu vilivyomo mbinguni na ardhini. Hakika Yeye anajua mnayoyakusudia. Na siku watakaporudishwa Kwake atawaeleza waliyoyafanya. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu.

## 25. Sura Al-Furqan

# SURA YA UPAMBANUZI

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 Ametukuka ambaye ameiteremsha Furqani kwa mtumishi
wake, ili iwe onyo kwa walimwengu wote. 2 Ambaye ni
Wake ufalme wa mbingu na ardhi, wala hakujifanyia mwana,

wala hana mshirika katika ufalme, na ameumba kila kitu na
akaviweka katika vipimo maalum. 3 Na wamejifanyia badala
yake miungu wengine, ambayo hawaumbi chochote, bali
wao huumbwa, hawana uwezo wa kujiondolea madhara wala
kujiletea manufaa; wala hawana udhibiti wa mauti wala uhai
wala kufufuka.

4 Na waliokufuru wanasema: ‘Hii (Qur’an) si lolote
isipokuwa uzushi tu aliouzusha yeye na akasaidiwa na watu
wengine. Kwa hakika wao ndiyo walioleta uovu na uzushi.
5 Na wakasema: Hizi ni hadithi za watu wa kale tu! Yeye
amefanya ziandikwe upya, yeye husomewa hizo akaandika
imla, asubuhi na jioni. 6 Sema, ameiteremsha ajuaye siri za
mbinguni na ardhini. Hakika Yeye ni Mwingi wa msamaha,
Mwenye kurehemu.

7. Na wakasema: Mtume gani huyu anayekula chakula na
kwenda kuhemea masokoni! Si angeteremshiwa Malaika
akawa pamoja nao wakionya watu? 8. Au akaangushiwa
hazina, au awe na bustani akawa anakula katika hiyo? Wale
wanaotenda maonu wakasema; ‘Ninyi mwamfuata mtu
aliyerogwa tu!’ 9. Angalia! Aina gani ya mifano wanakupigia!
Wamepotea, wala hawataweza kupata njia.

10. Ametukuka yule ambaye akipenda aweza kukupa
vilivyo bora zaidi kuliko hivyo walivyovitaja. (Akakupa)
mabustani ambayo hupita mito ya maji chini yake na
akakupa majumba ya fahari.. 11. Bali wanakanusha Kiyama..
Na tumemwandalia moto mkali mwenye kukanusha Kiyama.
12. Moto huo unapowaona kutoka mbali watasikia hasira na
mwungurumo wake. 13. Na watakapotupwa humo mahali
palipo finyu, wakiwa wamefungwa pamoja, ndipo hapo
wataomba mauti. 14. (Wataambiwa): ‘Leo msiombe kufa

mara moja bali ombeni kufa mara nyingi!' 15. Sema, je, hayo ni bora au Pepo ya milele, ambayo wameahidiwa wacha Mungu, iwe malipo yao na marejeo? 16. Watapata humo wayatakayo, wakae humo milele. Ni ahadi inayoombwa kwa Mola Wako.

17. Na siku atakapowakusanya wao na hao wanaowaabudu badala ya Mwenyezi Mungu na akawauliza: 'Je, nyinyi mmewapoteza waja Wangu hawa au ni wao wenyewe walipotea njia?' 18. Watasema: 'Subhaanak! (Umetakasika na upungufu!) Hatukustahiki kuwafanya wao watufanye sisi walinzi wao badala yako! Lakini uliwadekeza hao kwa starehe na pia baba zao, hadi wakasahau ujumbe wako na wakawa watu walioharibika kabisa. 19. (Allah atasema): 'Haya, wamekwisha wakana juu ya mnayoyasema. Hivyo hamwezi kujiepushia (adhabu) wala kupata msaada. Na yeyote kati yenu atakayefanya maovu tutamuonjesha adhabu kubwa.

20. Na hatukuwatuma kabla yako mitume, isipokuwa kwa kweli walikuwa wakila chakula na wakienda masokoni. Na tumewafanya badhi yenu wawe majaribio kwa wengine. Je, mtakuwa na subira? Na Mola Wako ni Mwenye kuona.

21. Na wale wasiotarajia kukutana Nasi walisema: Mbona sisi hatuteremshiwi Malaika au tumuone Mola Wetu Mlezi? Hakika wamejikweza kiburi, na wamekosa adabu mno! 22. Siku watakayowaona Malaika, haitakuwa furaha siku hiyo kwa wahalifu, na (malaika) watasema: 'Wekeni kizuizi cha kuwazuia hao!' 23. Kisha tutayageukia matendo yoyote waliyokuwa wakiyatenda (hapa duniani), tuyafanye kama mavumbi yaliyotawanyika. 24. Watu wa Peponi siku hiyo watakuwa katika makazi bora na mapumziko mazuri zaidi.

25. Siku itakapofunguka mbingu yakatoka mawingu na wakateremshwa malaika safu baada ya safu. 26. Ufalme wa haki siku hiyo utakuwa wa Mwenezi Mungu pekee. Na itakuwa siku ngumu kwa makafiri. 27. Na siku hiyo mfanya maovu atauma vidole vyake, akilia:'Laiti ningelishika njia (ya sawa) pamoja na Mtume!' 28.' Oooh ole wangu! Laiti nisingelimfanya fulani kuwa rafiki'. 29. Kwa hakika amenipoteza nisifuate ujumbe baada ya kunijia! Ah! shetani daima ni haini kwa mwanadamu! 30. Na Mtume atasema: 'Ewe Mola Wangu Mlezi! Hakika watu wangu wameifanya hii Qur'an kuwa mahame. 31. Na kama hivi tumemfanyia kila Nabii adui miongoni mwa wafanyao uovu. Na Mola Wako anatosha kuwa Mwenye kuongoza na Mwenye kunusuru.

32. Na wale waliokufuru wanasema: 'Mbona hakushushiwa Qur'an yote mara moja? Ndiyo, imeshushwa hivyo ili tuuimarishe moyo wako kwa namna hiyo, na ndio maana tumekusomea taratibu, hatua kwa hatua. 33. Wala hawatakujia na swali lolote, isipokuwa Nasi tutakuletea (jawabu) la kweli na maelezo mazuri zaidi. 34. Wale watakaokusanywa kwenye Jahannam kwa kuburutwa kifudifudi, hao watakuwa mahali pabaya na ndio wenye kupotea njia sana.

35. Hakika tulimpa Musa (Moses) Kitabu na tukamweka pamoja naye nduguye, Harun (Aaron), kuwa waziri wake. 36. Tukawaambia nendeni kwa watu waliokanusha Ishara Zetu. Basi tuliwaangamiza wale kabisa. 37. Na watu wa Nuh (Noah) walipowakanusha mitume, tuliwagharikisha na tukawafanya kuwa ishara kwa watu. Na tumewaandalia waovu adhabu chungu. 38. Na kina Ad na Thamud na watu wa Rass na vizazi vingi vilivyokuwa baina yao. 39. Na wote tuliwapigia mifano na wote tuliwavunjilia mbali na kuwaangamiza.

40. Na kwa hakika (wasioamini) wamewahi kupita kwenye mji ulionyeshewa mvua ya shari. Jee, hawakuuona? Lakini tu hawatarajii kufufuliwa.

41. Na wanapokuona hawakufanyii isipokuwa kejeli tu : 'ati huyu ndiye Mwenyezi Mungu aliyemtuma kuwa mtume!'
42. Alikuwa karibu mno kutufanya atupoteze tuachane na miungu yetu, kama tusingekazana kuing'ang'ania'. Basi punde hivi watajua watakapoiona adhabu, ni nani aliyepotea njia.

43. Je, umemwona anayefanya uraibu wake kuwa ndio mungu wake? Jee, wewe unaweza kusimamia mambo yake?
44. Au unadhani wengi wao wanasikia na wanaelewa? Hao si lolote ila mithili ya wanayama tu; bali wao wamepotea zaidi njia.

45. Hivi huoni jinsi Mola Wako Mlezi anavyokirefusha kivuli? Angetaka angekifanya kitulie. Kisha tukalifanya jua kuwa lenye kukiongoza.
46. Kisha tunakivutia kwetu na kukikunja kidogo kidogo.
47. Yeye ndiye aliyewafanyia usiku kuwa (kama) vazi na usingizi kuwa mapumziko na akaufanya mchana kuwa ni (kama) kufufuliwa.
48. Naye ndiye anayetuma upepo wa aina mbali mbali kuwa habari njema kabla ya rehema (mvua) Yake. Na tunateremsha kutoka mawinguni maji safi.
49. Ili kwayo tufufue nchi iliyokufa na tuwanyweshe wanyama na watu wengi tuliowaumba.

50. Na hakika tumeyatawanya hayo (maji ya mvua) baina yao ili wapate kushangilia (sifa zetu), lakini watu wengi wamekataa isipokuwa kukana fadhila.
51. Na kama tungetaka tungepeleka katika kila mji muonyaji.
52. Basi usiwatii makafiri na pambana nao kwayo (Qur'an) kwa hima kubwa.

53. Yeye ndiye ameziachia bahari mbili zikutane: hii

inanyweka tamu na hii ni chumvi sana, na akaweka kinga kati
yake na kizuizi kisichovukika. 54. Naye ndiye aliyemuumba
mwanadamu kutokana na maji na akamfanya kuwa na udugu
wa damu na wa ndoa. Na Mola Wako ni Mwenye uwezo.

55. Na wanaabudu wasiowadhuru wala kuwanufaisha
badala ya Mwenyezi Mungu. Na kafiri daima ni msaidizi
(wa shetani) dhidi ya Mola Wake. 56. Na hatukukutuma wewe
isipokuwa uwe mtoa habari njem na muonyaji. 57. Sema:
Siwaombi ujira juu ya huu ujumbe, ila atakaye na ashike njia
(iliyonyooka) iendayo kwa Mola Wake.

58. Na mtegemee aliye hai ambaye hafi na umtukuze kwa
sifa zake. Na yatosha kwake kuwa Yeye ni Mwenye habari
za dhambi za waja Wake. 59. Ambaye ameumba mbingu
na ardhi na vilivyomo humo katika kipimo cha siku sita.
Naye amekunjua Ufalme wake juu ya Kiti cha Enzi.Yeye
ni Arrahman, Mwingi wa rehema! Uliza habari Zake kwa
ajuaye. 60. Na wanapoambiwa msujudieni Mwenyezi Mungu,
Mwingi wa rehema, wanasema: Ni nani huyo Arrahmaan
(Mwingi wa rehema)? Je, tumsujudie unayetuamrisha wewe?
Na hilo huwafanya wazidi kukimbia kuiacha haki.

61. Ametukuka Yule aliyeweka katika mbingu makundi-
nyota (Constellation), na akaweka huko taa na mwezi unaotoa
mwanga. 62. Naye ndiye ambaye ameufanya usiku na mchana
kupokezana, kwa yule anayetaka kumsifu Mwenyezi Mungu
au anayetaka kushukuru.

63. Na waja wa Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema ni
wale wanaotembea ardhini kwa unyenyekevu. Na wajinga
wanapowasemesha, wao hujibu: ‘amani.’ 64. Na wale
wanaokesha kwa ajili ya Mola Wao Mlezi kwa kusujudu
na kusimama. 65. Na wale wanaosema: Mola Wetu Mlezi!

Tuondolee adhabu ya Jahannam, hakika adhabu ya Jahannm ikimkuta mtu haimwachi. [66.] Hakika hiyo Jahannam ni mbaya kuwa kituo na mahali pa kukaa. [67.] Na wale ambao wanapofanya matumizi hawatumii kwa ufujaji wala hawafanyi uchoyo, bali wanatumia katikati. [68.] Na wale ambao hawamwombi mungu mwingine pamoja na Mwenyezi Mungu, wala hawamwui mtu ambaye Mwenyezi Mungu amefanya maisha yake ni matakatifu isipokuwa kwa sababu ya haki, wala hawazini. Na mwenye kuyafanya hayo (siyo tu) atapata madhambi. [69.] Bali Siku ya Kiyama atazidishiwa adhabu na atadumu ndani ya adhabu mwenye akifedheheka. [70.] Isipokuwa aliyetubia na akatenda matendo mema, basi hao Mwenyezi Mungu atayabadilisha maovu yao yawe mema. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe, Mwenye kurehemu. [71.] Na aliyetubu na akafanya mema, basi hakika huyo ametubu kwa Mwenyezi Mungu toba (inayokubaliwa).

[72.] Na wale ambao hawatoi ushahidi wa uzushi, na wanapopita kwenye upuuzi hupita kwa heshima zao. [73.] Na wale ambao wanapokumbushwa Aya za Mola Wao hawajifanyi viziwi nazo na vipofu. [74.] Na wale wanaosema: Mola Wetu Mlezi! Tupe katika wake zetu na watoto watakaoburudisha macho yetu, na utujaalie tuwe viongozi wa wachamungu.

[75.] Hao ndio watakaolipwa makao ya juu kwa walivyosubiri na watakuta huko maamkuzi mema na Amani. [76.] Watadumu humo milele. Ni uzuri uliojeje wa makao hayo na mahli pa kupumzika! [77.] Sema Mola Wangu Mlezi asingeajali ninyi kabisa lau si kwamba kuna (baadhi yenu) wanaoniomba. Lakini nyie (makafiri) mmemkana Yeye. Hivyo, punde itakuwapo (adhabu) isiyo na budi.

## 26. Sura Ash-Shu’araa

# SURA YA WASHAIRI

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

[1] *Twa Sin Mim.*

[2] Hizo ni Aya za Kitabu kinachoweka wazi. [3] Huenda ukasononeka kwa vile hawawi waumini. [4] Kama tungependa tungewashushia ishara kutoka mbinguni, wakakawa wanainamisha shingo zao kuinyenyekea. [5] Na kila unapowajia ujumbe mpya kutoka kwa Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema, huukataa.. [6] Kwa hakika wamekadhibisha (ujumbe), basi zitawafikia khabari za yale waliyokuwa wakiyafanyia mzaha.

[7] Je hawaitazami ardhi, mimea mingapi mizuri na ya kila aina tumeiotesha humo?. [8] Hakika katika hayo kuna ishara, lakini wengi wao hawaamini. [9] Na hakika Mola Wako Mlezi ndiye Yeye Mwenye nguvu, Mwenye kurehemu.

[10.] Kumbuka! Wakati Mola Wako Mlezi alipomwita Musa (Moses) kwamba nenda kwa watu wabaya. [11.] Watu wa Firauni (Pharaoh). Kwa nini hawamhofii Mungu? [12.] Akasema: ‘Mola Wangu Mlezi! Kwa kweli miye nahofia wataniambia ni mwongo!’ [13.] ‘Na pia kifua changu kikawa na dhiki, na ulimi wangu (huenda) usiweze kutamka sawa sawa. Basi mtumie ujumbe Harun (Aaron)’. [14.] ‘Na wana mashtaka ya hatia dhidi yangu, hivyo naogopa wasije wakaniua’.

[15.](Allah) akasema, ‘Katu!’ Nendeni na miujiza Yetu. Hakika Sisi tu pamoja nanyi, tunasikiza’. [16.] Basi mfikieni

Firauni na mwambieni: 'Hakika sisi ni wajumbe wa Mola wa walimwengu wote'. [17.] Ya kwamba waachie wana wa Israel waende nasi. [18.] Firauni akasema: 'Hivi hatukukulea wewe utotoni, ukakaa kwetu katika umri wako miaka mingi?' [19.]'Na ukafanya tendo lako ulilolifanya, na wewe ni katika watovu wa shukrani?'

[20.] Akasema: 'Nililifanya hivyo kwa kukosea.' [21.] Basi nikakimbia kwa vile niliwahofia. Lakini Mola Wangu Mlezi akanitunukia cheo na akanijaalia miongoni mwa mitume. [22.] Na ni neema gani hiyo ya kuninyanyasa nayo wakati wewe umewafanya wana wa Israel kuwa watumwa? [23.] Akasema Firauni: Na ni nani huyo Mola Mlezi wa walimwengu wote? [24.] Akasema: 'Ni Mola wa mbingu na ardhi ikiwa nyinyi mwataka kuwa na uhakika'. [25.] (Firaun) Akawaambia waliomzunguuka: 'Je, mnasikiza?' [26.] (Musa) akasema:'Ni Mola Wenu Mlezi na Mola wa baba zenu wa kwanza'. [27.] Akasema: 'Hakika huyu mtume wenu aliyetumwa kwenu ni mwenda wazimu'. [28.] Akasema: 'Ni Mola Mlezi wa mashariki na magharibi na viliyomo baina yake, ikiwa nyinyi mna hekima'. [29.] Firauni akasema: 'Kama ukimwabudu mungu mwingine asiyekuwa mimi basi bila shaka nitakufunga jela'. [30.] Musa akasema: 'Japo nikuletee kitu cha kubainisha wazi?' [31.] Akasema: 'Kilete basi kama wewe ni katika wakweli'. [32.] Akaitupa fimbo, mara ikawa nyoka, wazi. [33.] Na akautoa mkono wake. Mara ukawa mweupe (wenye kumetameta) kwa watazamao (Nabii Musa alikuwa mweusi). [34.] Firauni akasema kuwaambia wakuu waliomzunguka: 'Hakika huyu ni mchawi, mjuzi'. [35.] Anataka kuwatoa katika ardhi yenu. Sasa, mnatoa shauri gani?

[36.] Wakasema: Mwache kidogo yeye na ndugu yake, na

uwatume wakusanyao watu mijini. 37. Wakuletee kila mchawi
mkubwa, mjuzi. 38. Basi wakakusanywa wachawi kwa
miadi ya siku maalum. 39. Na watu wakaambiwa: Je, (sasa)
mmekwisha kusanyika? 40. Hakika tutawafuata wachawi
wakiwa wao ndio watakaoshinda. 41. Basi walipokuja
wachawi wakamwambia Firauni: Je, tutapata ujira ikiwa
sisi ndiyo washindi? 42. Akasema: Ndio, hapo nanyi hakika
mtakuwa miongoni mwa watu watakaokuwa karibu nami.

43. Musa akawaambia: Bwageni chini vile mnavyotaka
kuvibwaga. 44. Wakatupa kamba zao na fimbo zao na
wakasema: ‘Kwa jaha ya Firauni hakika sisi bila shaka
tumeshinda!’ 45. Musa akabwaga fimbo yake, mara ikameza
(uwongo) walioubuni. 46. Wachawi wakapomoka wakisujudu.
47. Wakasema: Tumemwamini Mola wa Walimwengu.
48. Mola wa Musa na Harun.

49. Akasema (Firauni): Je, mmemwamini huyu kabla
sijawaruhusu? Bila shaka huyu atakuwa ndiye mkubwa
wenu aliyewafundisha uchawi, lakini punde hivi mtatambua.
Nitawakata mikono yenu na miguu yenu kwa kutofautisha,
kisha nitawasulubu nyote. 50. Wakasema: Haidhuru! Hakika
sisi ni wenye kurejea kwa Mola Wetu Mlezi. 51. Hakika sisi
tunatumai Mola Wetu atughufirie makosa yetu kwa kuwa
ndio wa kwanza kuamini.

52. Na tulimpelekea wahyi Musa kwamba ondoka na
waja Wangu wakati wa usiku, kwa hakika mtafuatwa.
53. Basi Firauni akawatuma mjini wapiga mbiu. 54. (Kusema)
Hawa Waisraeli ni kikundi kidogo, 55. Na hawa kwa kweli
wanatuudhi. 56. Na sisi ni wengi tunaochukua tahadhari.
57. Basi tukawatoa katika mabustani na chemichemi. 58. Na

hazina mbali mbali na vyeo vya heshima. [59.] Ndio hivyo! Na tukawarithisha wana wa Israel.

[60.] Kisha wakawafuata lilipochomoza jua. [61.] Wakati makundi mawili hayo yalipoliona jingine, watu wa Musa wakasema: 'Hakika tumepatikana!' [62.] Akasema: Hapana! Hakika Mola Wangu Mlezi yuko pamoja nami, ataniongoza. [63.] Tukamfunulia wahyi Musa tukamwambia: 'Piga bahari kwa fimbo yako'. Ikatengana pande mbili, na kila sehemu ikawa kama mlima mkubwa. [64.] Na tukawaleta hapo wale wengine. [65.] Na tukamwokoa Musa na waliokuwa pamoja naye wote. [66.] Kisha tukawazamisha hao wengine. [67.] Hakika bila shaka katika hayo ipo ishara, lakini wengi wao si wenye kuamini. [68.] Na hakika Mola Wako Mlezi ndiye Mwenye nguvu, Mwenye kurehemu.

[69.] Na wasomee habari za Ibrahim. [70.] Alipomwambia baba yake na watu wake:' Mnaabudu nini?' [71.] Wakasema: Tunaabudu masanamu nasi tutaendelea kuyanyenyekea. [72.] Akasema: Je yanawasikia mnapoyaita? [73.] Au yanawafaa au yanawadhuru? [74.] Wakasema: Bali tumewakuta mababa zetu wakifanya hivyo hivyo.

[75.] Akasema: Je, mmewaona mnaowaabudu? [76.] Nyinyi na baba zenu wa zamani? [77.] Hakika hao ni maadui zangu, siyo Mola Mlezi wa walimwengu wote. [78.] Ambaye ameniumba Naye ananiongoza. [79.] Na ambaye ananilisha na kuninywesha. [80.] Na ninapougua, Yeye huniponya. [81.] Na ambaye atanifisha kisha atanifufua. [82.] Na ambaye Ndiye ninayemtumai kunisamehe makosa yangu siku ya malipo.

[83.] Mola Wangu Mlezi! Nitunukie hekima na uniunganishe na watu wema. [84.] Na unijaalie kutajwa kwa wema na vizazi vijavyo. [85.] Na unijaalie katika warithi wa Pepo ya neema.

86. Na umghufirie baba yangu, kwani alikuwa miongoni mwa
wapotevu. 87. Wala usinifedheheshe siku watakapofufuliwa.
88. Siku ambayo hautafaa utajiri wala wana. 89. Isipokuwa
mwenye kurejea kwa Mwenyezi Mungu na moyo
uliosalimika.

90. Na Pepo itasogezwa kwa wanaomcha Mungu. 91. Na
Jahannam itafunuliwa wazi kwa wapotofu. 92. Wataambiwa,
wako wapi mliokuwa mkiwaabudu, 93. Badala ya Mwenyezi
Mungu? Je, watawasaidia au kujisaidia wenyewe? 94. Basi
watavurumizwa humo kifudifudi wao na wakosefu 95. Na
majeshi ya Ibilisi yote. 96. Watasema, hali ya kuwa wanazozana
humo: 97. Wallah! Hakika tulikuwa katika upotevu ulio wazi.
98. Tulipowafanya nyie kuwa sawa na Mola wa walimwengu
wote. 99. Na hawakutupoteza isipokuwa wakosefu.
100. Basi hatuna waombezi. 101. Wala rafiki wa kweli. 102.
Laiti tungeweza kurejea tena tungekuwa katika waumini.
103. Hakika katika hayo ipo ishara, lakini wengi wao si wenye
kuamini. 104. Na hakika Mola Wako Ndiye Mwenye nguvu
Mwenye kurehemu.

105. Watu wa Nuh (Noah) waliwakadhibisha mitume.
106. Pale ndugu yao Nuh alipowaambia: Hivi hamumhofii
Mwenyezi Mungu? 107. Hakika mimi kwenu ni Mtume
mwaminifu. 108. Basi mcheni Mwenyezi Mungu na mnitii.
109. Na siwaombi malipo kwa hili. Malipo yangu yako
kwa Mola wa walimwengu wote pekee. 110. Basi mcheni
Mwenyezi Mungu na mnitii. 111. Wakasema: Je, tukuamini
na hali wanaokufuata ni watu duni? 112. Akasema: Nayajuaje
waliyokuwa wakiyafanya? 113. Hisabu yao iko kwa Mola
Wangu Mlezi, pekee. Laiti mwatambua. 114. Wala mimi si

mwenye kuwafukuza walioamini. [115.] Mimi si mwingine isipokuwa muonyaji aliye dhahiri.

[116.] Wakasema: Kama hutakoma weye Nuh bila shaka utapigwa mawe. [117.] Akasema: Ewe Mola Wangu Mlezi! Hakika watu wangu wamenikana. [118.] Basi amua baina yangu mimi na wao uamuzi wa wazi. Na uniokoe na walio pamoja nami katika waumini. [119.] Basi tukamuokoa na walio pamoja naye katika jahazi iliyosheheni. [120.] Kisha tukawagharikisha baadaye waliobaki. [121.]Hakika katika hayo kuna ishara, lakini wengi wao si wenye kuamini. [122.] Na hakika Mola Wako Mlezi Ndiye Mwenye nguvu, Mwenye kurehemu.

[123.] Pia A'd waliwakadhibisha Mitume. [124.] Pale ndugu yao Hud alipowaambia: Mbona hamumtii na kumuenzi Mwenyezi Mungu? [125.] Hakika mimi kwenu ni Mtume mwaminifu. [126.] Basi mcheni Mwenyezi Mungu na mnitii. [127.] Na siwaombi malipo kwa hili. Malipo yangu yako kwa Mola wa walimwengu wote, pekee. [128.] Hivi mnajenga mnara juu ya kila muinuko, kwa kujiburudisha tu? [129.] Na mnajijengea majumba kama ngome, kana kwamba mtakaa milele? [130.] Na mnaposhambulia, mnashambulia kwa ujeuri na uadui mkubwa? [131.] Basi mcheni Mwenyezi Mungu na mnitii. [132.] Na mcheni ambaye amewapa mnayoyajua. [133.] Amewapa wanyama wa kufuga na watoto. [134.] Na mabustani na chemichemi za maji. [135.] Hakika ninawahofia na adhabu ya siku kubwa.

[136.] Wakasema: Ni mamoja kwetu umetuonya au usiwe katika wanaotuonya. [137.] Haya si lolote ila ni ada ya watu wa zamani. [138.] Wala hakuna cha kufanya sisi tuadhibiwe. [139.] Basi wakamkataa. Tukawaangamiza wote. Hakika kuna ishara katika hayo, lakini wengi wao si wenye kuamini.

140. Na hakika Mola Wako Ndiye Mwenye nguvu, Mwenye
kurehemu.
141. Thamud waliwakadhibisha mitume. 142. Ndugu
yao Swaleh alipowaambia: Hivi kwa nini hamumhofii
Mwenyezi Mungu? 143. Hakika mimi kwenu ni Mtume
mwaminifu. 144. Basi mcheni Mwenyezi Mungu na mnitii.
145. Na siwaombi malipo kwa hili. Malipo yangu ni mbele
ya Mola wa walimwengu wote, pekee. 146. Hivi mwadhani
mtaachwa katika amani (mkifurahia) hivi mlivyonavyo?
147. Katika mabustani na chemchemi za maji? 148. Na mimea
na mitende yenye makole yalioiva? 149. Na mnachonga
milimani majumba, huku mkistarehe tuu? 150. Mwogopeni
Mwenyezi Mungu na mnitii. 151. Wala msitii amri za
waliopituka mipaka. 152. Ambao wanafanya uharibifu ardhini
wala hawarekebishi..
153. Wakasema: Hakika wewe ni miongoni mwa
waliorogwa tu. 154. Wewe si lolote ila mtu kama sisi. Basi lete
ishara ikiwa wewe ni katika wasemao kweli. 155. Akasema:
Huyu ngamia jike; awe na zamu yake ya kunywa maji, na
nyinyi muwe na zamu yenu ya kunywa katika siku maalum.
156. Wala msimguse kwa ubaya isije ikawashika adhabu ya
siku kubwa. 157. Lakini wakamkata miguu, wakawa wenye
kujuta. 158. Basi ikawapata adhabu. Hakika katika hayo ipo
ishara, lakini wengi wao si wenye kuamini. 159. Na hakika
Mola Wako Mlezi ndiye Mwenye nguvu, Mwenye kurehemu.
160. Watu wa Lut (Lot) nao waliwakadhibisha mitume.
161. Pale ndugu yao Lut alipowaambia : Mbona hamumchi
Mwenyezi Mungu? 162. Hakika mimi kwenu ni Mtume
mwaminifu. 163. Basi mcheni Mwenyezi Mungu na mnitii.
164. Na siwaombi malipo katika hili. Malipo yangu ni kwa

Mola wa walimwengu wote pekee [165.] Hivi katika viumbe wooote mnawaendea wanaume pekee? [166.] Na mnakiacha alichowaumbieni Mola wenu Mlezi katika wake zenu? Bali nyinyi ni watu mnaovuka mipaka.

[167.] Wakasema: Kama hutakoma wee Lut utakuwa miongoni mwa wanaotolewa mjini. [168.] Akasema: Hakika mimi ni katika wanaokichukia hiki kitendo chenu. [169.] Mola Wangu Mlezi! Niokoe na familia yangu na haya wayatendayo. [170.] Basi tukamuokoa na familia yake yote. [171.] Isipokuwa kikongwe katika waliobakia nyuma. [172.] Kisha tukawaangamiza wale wengine. [173.] Na tukawanyeshea mvua (ya mawe), ikawa mvua mbaya iliyoje kwa watu waliokwisha onywa (hawakuonyeka). [174.] Hakika bila shaka katika hayo ipo ishara, lakini wengi wao si wenye kuamini. [175.]Na hakika Mola Wako Ndiye Mwenye nguvu, Mwenye kurehemu.

[176.] Watu wa mwituni pia waliwakadhibisha mitume. [177.] Alipowaambia Shua'yb: Mbona hamumchi Mwenyezi Mungu? [178.] Hakika mimi kwenu ni Mtume mwaminifu. [179.] Basi mcheni Mwenyezi Mungu na mnitii. [180.] Na siwaombi malipo katika hili, malipo yangu yapo kwa Mola wa walimwengu wote, pekee [181.] Timizeni kipimo sawasawa wala msiwe miongoni mwa wanaopunja. [182.] Na pimeni kwa mizani iliyo sawa. [183.] Wala msizuie vitu vya watu ambavyo ni haki yao. Wala msifanye jeuri mkawa mafisadi. [184.] Na mcheni aliyewaumba nyinyi na vizazi vilivyotangulia.

[185.] Wakasema: Hakika wewe ni miongoni mwa waliorogwa tu. [186.] Na wewe si chochote ila mtu kama sisi, na kwa hakika tunakuona ni katika waongo. [187.] Hebu fanya kipande cha mbingu kituangukie, ukiwa wewe ni mkweli. [188.] Akasema: Mola Wangu Mlezi anajua zaidi mnayoyatenda.

189. Wakamkadhibisha. Ikawafika adhabu ya siku ya kivuli
cha giza. Hakika hiyo ilikuwa adhabu ya siku kubwa.
190. Hakika bila shaka katika hayo ipo ishara, lakini wengi
wao si wenye kuamini. 191.Na hakika Mola Wako Ndiye
Mwenye nguvu, Mwenye kurehemu.

192.Na hakika hiyo ni uteremsho wa Mola wa walimwengu
wote. 193. Ameiteremka nayo Roho mwaminifu. 194. Juu
ya moyo wako, ili uwe katika waonyaji. 195. Kwa lugha ya
kiarabu ilio wazi. 196. Na hakika hiyo imeelezewa katika
vitabu vya watu wa kale. 197. Je haikuwa kwao ni ishara
kwamba haya yamejulikana na maulama wa wana wa Israel?

198. Lau tungeiteremsha juu ya mmoja wa wasiokuwa
Waarabu. 199. Na akawasomea wasingekuwa wenye kuiamini.
200. Hata hivyo tumeiingiza katika nyoyo za wakosefu.
201. Hawataiamini mpaka waone adhabu chungu. 202. Basi
itawafikia ghafla na hali hawaitambui. 203. Na watasema: Je
sisi tutapewa muda?

204. Jee, pamoja na hayo wanataka adhabu yetu iwafikie
haraka? 205. Unaonaje, kama tukiwastarehesha (hapa duniani)
kwa miaka michache?. 206. Kisha yawafikie waliyokuwa
wakiahidiwa. 207. Haitawafaa kuwa walikula starehe hapa
duniani! 208. Wala hatukuwaangamiza wana-mji wowote
ila kulikuwa kwanza na waonyaji. 209. Kwa ukumbusho.
Wala sisi siyo wenye kudhulumu. 210. Wala mashetani
hawakuteremka nao ( ujumbe). 211. Hawastahiki wala
hawawezi (kuutengeneza) 212. Hakika wao wametengwa
mbali na kuisikia.

213. Basi usimwombe mungu mwingine pamoja na
Mwenyezi Mungu ukawa miongoni mwa watakaoadhibiwa.
214. Na waonye jamaa zako wa karibu. 215. Na inamisha bawa

lako (waheshimu) kwa wanaokufuata katika waumini. 216.Na ikiwa watakuasi basi sema: Mimi ninajitenga mbali na hayo mnayoyafanya. 217. Na mtegemee Mwenye nguvu, Mwenye kurehemu. 218. Ambaye anakuona unaposimama (kuabudu). 219. Na kugeuka-geuka kwako katika (migongo ya) wale wanaosujudu. 220. Hakika Yeye ni Mwenye kusikia, Mwenye kujua.

221. Je niwaambie ambao mashetani wanawashukia? 222. Wanamshukia kila mwongo mkubwa, mwingi wa dhambi. 223. (Katika masikio yao) wanamimina maneno ya umbea na uvumi. Na wengi ni waongo. 224. Na washairi, wapotofu ndio wanaowafuata. 225. Je huwaoni kwamba wao wanatangatanga katika kila bonde? 226. Na kwamba wao wanasema wasiyoyatenda? 227. Isipokuwa wale walioamini na wakatenda mema na wakamtaja Mwenyezi Mungu kwa wingi, na wakajitetea (pale tu) baada ya kushambuliwa bila haki. Na punde hivi watajua wale watendao maovu, ni mgeuko gani wa hali zao watageuka?

## 27. Surah An-Naml

# SURA YA SUNGUSUNGU

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 *Twa siin.*

Hizi ni Aya za Qur'an na Kitabu kinachoweka wazi. 2 Ni Mwongozo na bishara njema kwa waumini. 3 Wale ambao wanadumisha Swala na wakatoa Zaka na wana yakini na

Akhera. 4 Hakika wale wasioamini Akhera, tumewafanya
wavione vitendo vyao kuwa vizuri, hivyo wanamangamanga
tu (wakiwa wamechanganyikiwa). 5 Hao ndio watakaopata
adhabu mbaya, na wao huko Akhera ni wenye kupata hasara.
6 Na kwa hakika wewe unafunzwa Qur'an kutoka Kwake
Mwenye hekima, Mwenye ujuzi.

7 (Kumbuka) Pale Musa (Moses) alipowaambia watu wa
familia yake, hakika nimeona moto, nitakwenda kuwaletea
habari au kuwaletea kijinga kinachowaka ili mpate kuota
moto. 8 Basi alipoufikia, pakanadiwa: 'wamebarikiwa wale
waliomo katika moto huu na waliopo pembeni mwake, na
ametakasika Mwenyezi Mungu Mola wa walimwengu wote'.

9. Ewe Musa! Hakika Mimi Ndiye Mwenyezi Mungu
Mwenye nguvu, Mwenye hekima. 10. Na hebu ibwage
fimbo yako! Alipoiona inatingishika, kana kama kwamba ni
nyoka, aligeuka kurudi nyuma wala hakungoja. Ewe Musa!
Usihofu! Hakika Mimi hawahofu mbele Yangu Mitume.
11. Ila aliyefanya ubaya kisha akabadilisha wema baada
ya ubaya huo, basi hakika Mimi ni Mwingi wa msamaha,
Mwingi wa huruma. 12. Na ingiza mkono wako katika mfuko
wako utatoka mweupe (unameta) na si kwa maradhi. Hizo
ni miongoni mwa ishara tisa kwa Firauni (Pharaoh) na watu
wake. Hakika wao ni watu waliokubuhu katika maovu.
13. Zilipowafikia ishara Zetu hizo kuwafungua macho,
walisema: 'Huu ni uchawi wazi wazi'. 14. Na wakazikataa
kwa kuasi na majivuno, na hali ya kuwa (ndani ya) nafsi zao
wana yakini nazo. Basi angalia ulikuwaje mwisho wafanyao
uharibifu.

15. Na hakika tulimpa Daud (David) na Suleiman (Solomon)
elimu. na wakasema: Sifa njema zote (alhamdu-lillah) ni

za Mwenyezi Mungu ambaye ametupendelea juu ya wengi katika watumishi Wake waumini. 16. Na Suleiman alimrithi Daud. Akasema (Solomon): ‘Enyi watu! Sisi tumefunzwa wasemavyo ndege. Na tumepewa kila kitu. Hakika hii ni hisani iliyo kubwa’.

17. Na akakusanyiwa Suleiman majeshi yake ya majini na watu na ndege, nayo yakapangwa kwa nidhamu. 18. Hata walipofikia kwenye bonde la Sungusungu (chungu), Sungusungu mmoja akasema: ‘Enyi Sungusungu! Ingieni maskani zenu, asije akawapondaponda Suleiman na jeshi lake na hali wao hawatambui’. 19. (Solomon) akatabasamu akifurahishwa na maneno ya Sungusungu yule. Akasema: ‘Ewe Mola Wangu Mlezi! Niamuru ili niishukuru neema Yako uliyonineemesha mimi na wazazi wangu na nipate kutenda mema unayoyaridhia na uniingize kwa rehema Yako katika kundi la watumishi Wako wema.

20. Na akalikagua (jeshi la) ndege na akasema: ‘Mbona simwoni Goregore, au amekuwa miongoni mwa watoro’? 24. ‘Huyo nitamwadhibu adhabu kali au nitamchinja, au anileteе hoja madhubuti’. 22. Lakini Goregore hakuwa mbali, akasema: ‘Nimezunguka sehemu ambayo bado wewe hujaizunguka, na ndiyo nimeingia sasa hivi kutoka (Saba’i) Sheba na habari za yakini’. 23. Huko nimemkuta mwanamke anayewatawala na amepewa kila kitu na anacho kiti cha enzi kikubwa. 24. Nimemkuta yeye na watu wake wanaliabudu jua badala ya Mwenyezi Mungu; na shetani amewafanya waone matendo yao kuwa ni mazuri, na amewazuia njia, kwa hivyo hawakuongoka. 25. Kwamba hawamsujudii Mwenyezi Mungu ambaye huyatoa yaliyofichikana katika mbingu na ardhi na huyajua mnayoyaficha na mnayoyatangaza.

26. Mwenyezi Mungu, hapana Mola isipokuwa Yeye, Mola
Mlezi wa Arshi tukufu.

27. Akasema Suleiman: ‘Tutatazama, umesema kweli au
wewe ni katika waongo’. 28. Nenda na barua yangu hii na
uwafikishie, kisha waondokee, utazame watarejesha nini.
29.(Malkia) Akasema: ‘Machifu wangu! Nimekabidhiwa
barua hii ipasayo kuheshimiwa’. 30. ‘Imetoka kwa Suleiman,
nayo ni: ‘Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa huruma,
Mwenye kuhurumia……. 31. ‘Kwamba msinifanyie jeuri
na mnijie mkiwa Wanyenyekevu (Kwa dini ya kweli)’.
32. (Malkia) Akasema: ‘Enyi Machifu! Nipeni ushauri katika
jambo langu hili. kwani mimi siamui jambo lolote mpaka
muwepo’. 33. Wakasema: ‘Sisi ni wenye nguvu na wakali wa
vita, na amri ni yako, angalia nini unatuamrisha’. 34. Akasema:
‘Hakika wafalme wanapouingia katika mji huuharibu na
wanawafanya wale watukufu wake kuwa watwana. Na
hivyo ndivyo wafanyavyo’. 35. ‘Nami nitawapelekea zawadi,
ningoje watakayorudi nayo wajumbe wangu’.

36. Ule ujumbe ulipofika kwa Suleiman, aliwaambia:
‘Hivi nyinyi mnataka kunipa utajiri? Aliyonipa Mwenyezi
Mungu ni bora zaidi kuliko aliyowapa nyinyi. Ni ninyi tu
ndiyo mnaofuraha kwa zawadi yenu’. 37. ‘Rejea kwao!
Kwa yakini tutawajia na majeshi wasiyoweza kuyakabili na
hakika tutawatoa humo na hali wao wamekuwa madhalili na
wanyonge’.

38. Akasema (Suleiman): ‘Wapambe wangu! Ni nani kati
yenu atakayeniletea kiti chake cha enzi kabla hawajanijia nao
wamekwisha salimu amri?’. 39. Akasema Afriti, mmoja kati ya
majini: ‘Mimi nitakuletea kabla hujainuka mahala pako. Na
mimi hakika nina uwezo kwa hilo, mwaminifu’. 40. Akasema

mmoja ambaye ana elimu ya Kitabu: 'Mimi nitakuletea kabla ya kupepesa jicho lako!' (Suleiman) alipokiona (kiti) tayari kimewekwa mbele yake, alisema: 'Haya ni katika hisani za Mola wangu Mlezi, ili anijaribu, nitashukuru au nitakufuru. Na mwenye kushukuru kwa hakika anashukuru kwa manufaa yake mwenyewe na mwenye kukufuru kwa hakika Mola Wangu ni Mkwasi, Mkarimu'.

41. Akasema: 'Kigeuzeni hadi asikitambue kiti chake cha enzi, tuone ataongoka au atakuwa miongoni mwa
wasioongoka?' 42. (Yule malkia) alipofika akaambiwa: 'Je kiti chako cha enzi kiko hivi? Akasema: 'Kana kwamba ndicho hicho'. Nasi tulipewa elimu kabla yake na tukawa
Waislamu. 43. Na kile alichokuwa akikiabudu badala ya Mwenyezi Mungu ndicho kilichomzuia (na elimu). Hakika
yeye alikuwa katika kaumu ya makafiri. 44. Akaambiwa Ingia kwenye bambo la kasri. Alipoliona alidhani ni bwawa la maji, akapandisha nguo mpaka kwenye miundi yake. Solomon akamwambia:' 'Hilo ni bambo tu lililosakafiwa kwa vioo! Akasema: 'Mola Wangu Mlezi! Hakika nimeidhulumu nafsi yangu, na najisalimisha pamoja na Suleiman kwa Mola wa walimwengu'.

45. Na kwa Thamud tulimtuma ndugu yao Swaleh kuwaambia mwabuduni Mwenyezi Mungu. Basi mara
wakawa makundi mawili wanagombana. 46. Akasema: Enyi watu wangu! Kwa nini mnataka mfanyiwe haraka ubaya (adhabu) kabla ya wema? Kwa nini hamumwombi Mwenyezi
Mungu msamaha mpate kuhurumiwa? 47. Wakasema: Twaona mkosi utatufika kwa ajili yako na walio nawe! Akasema: mkosi wenu uko kwa Mwenyezi Mungu. Ndiyo, nyie ni watu mnaojaribiwa.

48. Na walikuwamo mjini watu tisa wakifanya uharibifu
katika ardhi wala hawaleti maendeleo. 49. Wakasema: Kuleni
kiapo cha pamoja kwa (jina la ) Mwenyezi Mungu, kwamba
tutafanya shambulio la siri usiku dhidi yake na familia yake.
Kisha tutamwambia mrithi wake (akitaka kulipiza kisasi):
'Aka! Sisi hatukushuhudia mauaji ya ndugu zake, na sisi
hakika twasema kweli'. 50. Na wakapanga mpango wa siri
Nasi tukapanga mpango wetu, na wao hawatambui. 51. Basi
angalia ulivyokuwa mwisho wa mpango wao; kwamba
tuliwaangamiza wao na watu wao wote. 52. Hizo nyumba
zao sasa ni tupu kwa sababu ya walivyofanya maovu.
Hakika katika hayo kuna ishara kwa watu wanaojua. 53. Na
tukawaokoa wale walioamini na waliokuwa na takua.

54. Na (kumbuka) pale Lut (Lot) alipowaambia watu
wake: Je mnafanya uchafu nanyi mnaona (kuwa ni uovu)?
55. Hakika nyinyi mnawaendea wanaume kwa matamanio
badala ya wanawake! Kwa kweli nyinyi ni watu mnaofanya
ujinga. 56. Na halikuwa jibu la watu wake isipokuwa kusema:
'Watoeni mjini mwenu, maana hao ni watu (wanaotaka
kuwa) wasafi na nadhifu!'. 57. Tukamwokoa yeye na familia
yake, isipokuwa mkewe, Tulikwishaamua dhidi yake kuwa
yeye atakuwa miongoni mwa watakaochelewa nyuma.
58. Na tukawamiminia mvua; ni mbaya mno mvua hiyo ya
hao walioonywa. 59. Sema: Alhamdu-lillah (Sifa njema
ni za Mwenyezi Mungu) na amani ishuke juu ya waja
Wake aliowateua. Je Mwenyezi Mungu ni bora au hivyo
wanavyovishirikisha Naye?

60. Au ni nani yule aliyeziumba mbingu na ardhi
na akawateremshia maji kutoka mbinguni na kwayo
Tukaziotesha bustani zenye kupendeza? Nyinyi hamkuwa na

uwezo wa (kusababisha) kuota miti yake. Je, yuko mungu pamoja na Mwenyezi Mungu? Bali hao ni watu wapotofu tu. 61. Au ni nani yule aliyefanya ardhi madhubuti kwa kuishi? Na akaweka ndani yake mito ya maji na akaweka milima juu yake? Na akaweka kizuizi baina ya bahari mbili. Je, yuko mungu pamoja na Mwenyezi Mungu? Lakini wengi wao hawajui.

62. Au ni nani yule anayemjibu aliyeshikika pale anapomwomba na akaiondoa dhiki? Na akawafanya nyinyi ni warithi wa ardhi? Je, yuko mungu pamoja na Mwenyezi Mungu? Ni machache mnayoyazingatia. 63. Au ni nani yule anayewaongoza katika giza totoro la bara na bahari? Na ni nani yule apelekaye aina aina za upepo kuleta habari njema kabla ya rehema yake? Je, yuko mungu pamoja na Mwenyezi Mungu? Ametukuka Mwenyezi Mungu juu ya yale wanayoyashirikisha. 64. Au ni nani yule anayeuanzisha uumbaji kisha akaurudia? Na ni nani anayewaruzuku kutoka mbinguni na ardhini? Je, yuko mungu pamoja na Mwenyezi Mungu? Sema: Leteni hoja zenu kama ninyi ni wakweli.

65. Sema: Hapana katika mbingu na ardhi ajuaye ghaibu isipokuwa Mwenyezi Mungu; wala wao hawawezi kuhisi lini watafufuliwa. 66. Bali elimu yao ni ndogo mno hata kuweza kuifahamu Akhera. La, wao wamo katika shaka nayo. Bali wao ni vipofu nayo. 67. Na waliokana husema:'Tutakapokuwa mchanga, sisi na baba zetu, hivyo kweli tutakujatolewa'. 68. Tulikwisha ahidiwa haya sisi na baba zetu kabla. Haya si lolote ila ngano za watu wa kale. 69. Sema: Tembeeni katika ardhi na tazameni ulikuwaje mwisho wa wakosefu.

70. Wala usiwahuzunikie wala usiwe katika dhiki kwa hila wanazozifanya. 71. Na wanasema: 'Ahadi hii itatokea

lini ikiwa mnasema kweli?’ 72. Sema: Huenda yamekaribia
kuwafikia baadhi ya yale mnayotaka yaje haraka. 73. Na
hakika Mola Wako Mlezi ni Mwingi wa hisani kwa watu,
lakini wengi wao hawashukuru. 74. Na hakika Mola Wako
Mlezi anayajua yale ambayo vifua vyao vinayaficha na yale
wanayoyatangaza. 75. Na hakuna siri yeyote katika mbingu na
ardhi isipokuwa imo katika Kitabu kinachosajili wazi wazi.

76. Hakika hii Qur’an inawafafanulia wana wa wa Israel
mengi katika yale wanayohitilafiana. 77. Nayo hakika ni
mwongozo na rehema kwa waumini. 78. Hakika Mola Wako
Mlezi atahukumu baina yao kwa uamuzi Wake; Naye ni
Mwenye nguvu, Mjuzi. 79. Basi mtegemee Mwenyezi Mungu.
Hakika wewe uko juu ya ukweli ulio wazi kabisa. 80. Wewe
huwezi kuwafanya wafu wasikize wala kuwafanya viziwi
wasikize wanapogeuka na kurudi nyuma. 81. Wala huwezi
kuwaongoza vipofu (wa haki) waache upotevu wao. Huwezi
kuwasikilizisha ila wale wanaoziamini ishara Zetu, basi hao
ndio watiifu.

82. Na itakapofikia kauli kutimizwa dhidi yao, tutawatolea
jinyama kutoka ardhini litakalowasemesha, kwamba watu
walikuwa hawana yakini na ishara Zetu. 83. Na siku ambayo
tutakusanya kutoka kila taifa kundi la watu; wale wanaosema
ishara zetu ni uwongo, tuwagawe kwa mujibu wa vyeo
vyao. 84. Hata watakakuja (mbele ya hukumu), awaulize
(Mwenyezi Mungu): ‘Je, nyinyi mlizikanusha ishara Zangu
pasipo kuzijua vyema, au mlikuwa mkifanya nini’? 85. Na
kauli itatimia dhidi yao kwa vile walivyofanya maovu. Na
hawatasema chochote. 86. Hivi hawaoni kwamba tumeufanya
usiku ili wapumzike na mchana kuwapa wao mwangaza?
Hakika katika hayo kuna ishara kwa watu wenye kuamini.

87. Na siku itakapopuziwa parapanda, watafazaika (kwa hofu) waliomo mbinguni na waliomo ardhini, ila ampendaye Mwenyezi Mungu. Na wote watamjia wakiwa wanyonge.
88. Na unaiona milima unaidhania imetulia hapo hapo, nayo inapita kama yapitavyo mawingu. Huu ndiyo ufundi wa Mwenyezi Mungu aliyetengeneza vizuri kila kitu. Hakika Yeye ana habari za mnayoyatenda.
89. Watakaokuja na wema watapata bora kuliko hayo. Nao watasalimika na mfazaiko wa siku hiyo.
90. Na watakaokuja na uovu, watamwagwa motoni kwa kutangulizwa nyuso zao. Kwani mtalipwa (vingine) isipokuwa yale mliyoyatenda?

91. Hakika nimeamrishwa kumwabudu Mola wa mji huu ambaye ameufanya uwe mtakatifu; na ni Vyake Yeye vitu vyote. Na nimeamrishwa niwe miongoni mwa wenye kunyenyekea.
92. Na kwamba nisome Qur'an. Mwenye kuongoka, basi anaongoka kwa faida yake mwenyewe, na aliyepotea basi sema: 'Mimi ni miongoni mwa waonyaji tu'.
93. Na Sema: Alhamdu lillah (Sifa njema ni za Mwenyezi Mungu) Atawaonesha ishara Zake, mtazijua. Na Mola Wako si Mwenye kughafilika na mnayoyafanya.

## 28. Sura Al-Qasas

## SURA YA MATUKIO

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 *Twa Sin Mim.* Mwenyezi Mungu pekee ndiye ajuaye maana hasa.

2 Hizi ni Aya Za Kitabu kinachoweka mambo wazi.

[3] Tunakusimulia baadhi ya habari za Musa (Moses) na Firauni (Pharaoh) kwa ukweli, kwa ajili ya watu wanaoamini. [4] Hakika Firauni alijivuna mno katika ardhi akawagawa watu wake makundi makundi, huku akilikandamiza kabila moja miongoni mwao; kwa kuwachinja watoto wao wa kiume na kuwaacha hai watoto wao wa kike. Hakika yeye alikuwa katika watu waovu kabisa. [5] Na tukataka kuwapa neema wale waliokandamizwa katika ardhi na kuwafanya wawe ndio viongozi (wa Imani) na kuwafanya wawe warithi. [6] Na kuwapa madaraka katika nchi, na kumwonesha Firauni na Hamana na askari wao yale yale waliyokuwa wakijihadhari nayo.

[7] Na tulimfunulia Wahyi mama yake Musa kuwa 'Mnyonyeshe mwanao. Na utapohofia juu ya maisha yake, basi mtupe mtoni. Wala usihofu wala usiwe na huzuni. Sisi tutamrudisha kwako na tutamfanya miongoni mwa mitume'. [8] Basi wakamwokota watu wa Firauni (na ilipangwa) aje awe adui wao na sababu ya kuwatia huzuni. Hakika Firauni na Hamana na majeshi yao walikuwa wenye makosa. [9] Akasema mke wa Firaun: '(Huyu mwana) ni kiburudisho cha macho kwangu na kwako. Msimwuue! Huenda akatufaa au tumfanye kuwa mtoto wetu'. Na wao hawakuhisi (yatakayotokea).

[10.] Ndipo moyo wa mamake Musa ukahisi ombwe. Akawa anakaribia kufichua (yaliyotokea), laiti tusingeuzaiti moyo wake (kwa iman), ili aendelee kuwa miongoni mwa waumini. [11.] Akamwambia dadake (Musa) hebu mfuatie. Akawa anamwangalia kwa mbali na wao hawahisi. [12.] Na tukamfanya awakatae wanyonyeshaji wote tangu mwanzo. Ndipo (dadake) akawaambia: Je, niwaoneshe watu wa nyumba fulani watakaomlea kwa ajili yenu na watakuwa

wema kwake? 13. Basi tukamrudisha kwa mama yake ili yaburudike macho yake na ajue kwamba ahadi ya Mwenyezi Mungu ni kweli, lakini watu wengi hawajui. 14. Na alipofikia utu uzima barabara, tulimpa hekima na elimu. Na hivyo ndivyo tunavyowalipa watenda mema.

15. Na akaingia mjini wakati wenyeji wake hawakuwa wakiangalia. Akakuta humo watu wawili wanapigana - huyu ni katika kabila lake na mwingine katika maadui zake. Yule wa kabila lake akamtaka msaada kumpiga yule adui yake. Musa akampiga yule ngumi, akamwua. Akasema: Hiki ni kitendo cha shetani; hakika yeye ni adui mpotezaji wa wazi. 16. Akasema: 'Mola Wangu Mlezi! Hakika mimi nimeidhulumu nafsi yangu, nisamehe'. Akamsamehe. Hakika Yeye ni Mwingi wa maghufira, Mwenye kurehemu. 17. Akasema: 'Mola Wangu Mlezi! Kwa jinsi ulivyonipa neema, katu sitakuwa msaidizi wa waovu'.

18. Akapambaukiwa mjini huku akiwa na hofu, akawa anachungulia huku na huko. Mara yule yule aliyemtaka msaada jana, akawa anampigia kelele tena amsaidie! Musa akamwambia: 'Hakika wewe ni mchokozi wa wazi wazi'. 19. Musa alipotaka kumkamata kwa nguvu yule aliye adui yao wote wawili, (yule mtu) akasema: 'Wee Musa! Unataka kuniua kama ulivyomuua mtu jana? Wewe hutaki lolote isipokuwa uwe jambazi hapa nchini, wala hutaki kuwa miongoni mwa wanaorekebisha mambo!' 20. Akaja mtu huku akikimbia kutoka mwisho wa mji, akasema: 'Ewe Musa! Machifu wanapanga njama ya kukuua, hivyo toka humu! Hakika mimi ni katika wanaokupa nasaha'. 21. Basi akatoka mjini akiwa na hofu, akifanya tahadhari. Akasema: 'Mola Wangu Mlezi! Niokoe na watu hawa wabaya'.

22. Alipoelekea upande wa Madyan alisema: ‘Asaa Mola Wangu akaniongoza njia iliyo sawa’. 23. Alipofika kwenye kisima cha Madyan alikuta umati wa watu wakinywesha. Na akakuta nyuma yao wanawake wawili wakiwazuia (wanyama wao). Akasema: ‘Mna nini nyie? Wakasema: ‘Hatuwezi kunywesha mpaka wamalize hao wachungaji, na baba yetu ni mzee sana’. 24. Basi akawanyweshea kisha akarudi kivulini na akasema: ‘Mola Wangu Mlezi! Hakika mimi ni mhitaji wa kheri utakayoniteremshia’. 25. Basi mmoja wa wale wanawake wawili akamjia naye anatembea akiona haya. Akasema: ‘Baba yangu anakuita akulipe ujira wa kutunyweshea. Alipomjia na kumsimulia visa vyake, alisema: usiogope; umekwishaokoka na watu wabaya’. 26. Akasema mmoja katika wale wasichana: ‘Baba yangu! Tafadhali mwajiri huyu. Bora zaidi ya anayefaa kumwajiri ni huyu: ni shupavu, mwaminifu. 27. Akamwambia: ‘Mimi ninataka kukuoza mmoja wa mabinti zangu hawa kwa kunitumikia kwa miaka minane. Ukitimiza miaka kumi ni hiyari yako. Mimi sitaki kukutaabisha. Inshaallah utanikuta miongoni mwa watu wema’. 28. Akasema Musa: ‘Hayo ni makubaliano tayari baina yangu na yako. Muda wowote kati ya miwili nitakaomaliza si vibaya; na Mwenyezi Mungu ni Shahidi juu ya haya tunayoyasema’.

29. Basi Musa alipomaliza muda wake na akasafiri na familia yake, aliona moto upande wa mlima. Akawaambia familia yake: ‘Hebu ngojeni hapa! Mimi nimeona moto, pengine nitawaletea habari kutoka huko, au kijinga cha moto mpate kuota’. 30. Alipoufikia aliitwa kutoka upande wa kulia wa bonde, katika eneo lilobarikiwa, kutoka mtini, kwamba ewe Musa! Hakika Mimi ndiye Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe. 31. Na kwamba, ibwage chini fimbo yako!

Alipoiona inatingishika, kana kwamba ni nyoka, aligeuka kurudi nyuma, wala hakungoja. (Akaambiwa) Ewe Musa! Njoo mbele wala usihofu! Hakika wewe ni miongoni mwa waliosalimika. 32. Na ingiza mkono wako katika mfuko wako utatoka mweupe (ukimeta) bila ugonjwa. Na kusanya pamoja mbawa zako kujikinga na hofu.[11] Basi hizo ni dalili mbili kutoka kwa Mola Wako Mlezi umpelekee Firauni na machifu wake. Hakika wao ni watu waovu.

33. (Musa) akasema: Mola Wangu Mlezi! Hakika mimi nilimwua mtu katika wao, hivyo nahofia wataniua. 34. Na ndugu yangu Harun ni fasaha zaidi katika kuzungumza kuliko mimi, basi mtume aende pamoja nami kama msaidizi, ili waweze kunisadiki. Hakika mimi nahofia wataniona mwongo. 35. Akasema: Tutautia nguvu mkono wako kwa ndugu yako, na tutawapa madaraka, hawataweza kuwagusa. Kwa miujiza yetu hii mtashinda; nyinyi wawili, na watakaowafuata.

36. Basi alipowafikia Musa na ishara Zetu zilizo wazi wazi, walisema: Haya si lolote ila uchawi uliotungwa. Na hatukuyasikia haya kutoka kwa baba zetu wa zamani. 37. Musa akasema: Mola Wangu Mlezi anamjua zaidi nani aliyekuja na mwongozo kutoka kwake na nani atakayekuwa na mwisho mwema katika nyumba ya Akhera. Hakika wenye kudhulumu hawatafanikiwa. 38.Na akasema Firauni: Enyi machifu! Sijui kama mnaye Mungu mwingine asiye mimi. Ewe Haman! Niwashie tanuri la moto, unichomee udongo (wa matofali),

11. Hapa Mwenyezi Mungu anatumia tena picha ya ndege. Ndege anapokuwa na hofu, hufunua mbawa zake tayari kuruka kukimbia hatari. Ama anapohisi amani, hukusanya-kusanya mbawa zake pamoja na kutulia. Musa anaambiwa hapa ‘ajiusanye pamoja ahisi amani, wala asihofie- Mfasiri.

kisha unijengee mnara mrefu, nipande kumchungulia mungu
wa Musa. Kwa upande wangu, nafikiri Musa ni mwongo tu.
39. Na akawa na kiburi nchini yeye na majeshi yake bila
sababu. Na wakadhani kuwa hawatarudishwa Kwetu.
40. Tukamtia nguvuni yeye na majeshi yake na tukawatupa
baharini. Basi hebu angalia ulikuwaje mwisho wa wenye
kudhulumu. 41. Na tukawafanya wao kuwa viongozi waitao
kwenye moto. Na siku ya Kiyama hawatanusuriwa. 42. Na
tukaifanya laana iwafuate hapa duniani. Na siku ya Kiyama
watakuwa miongoni mwa wanaodhereuliwa na kuchukiwa.
43. Na hakika tulimpa Musa Kitabu, baada ya kuangamiza
vizazi vingi huko nyuma, ili kiwafumbue watu macho, na
kiwe mwongozo na rehema, huenda wakakubali kupokea
maonyo.
44. Wala wewe hukuwa upande wa magharibi (wa bonde
la Sinai) tulipompa Musa amri, wala hukuwa miongoni mwa
walioshuhudia. 45. Lakini Sisi tuliumba vizazi vipya wakawa
umri umewawia mrefu kwao (wakasahau). Wala hukuwahi
kuwa mkazi miongoni mwa watu wa Madyan ukiwasomea
Aya Zetu, lakini ni Sisi tuliokuwa tukiwatuma Mitume.
46. Wala hukuwa kando ya mlima (Sinai) tulipomwita. Lakini
ni rehema itokayo kwa Mola Wako Mlezi ili uwaonye watu
wasiofikiwa na muonyaji kabla yako, huenda wakapokea
maonyo. 47. Na lau (hatukutuma wewe kwa Maquraish),
likaja likawapata janga la adhabu kwa sababu ya dhambi
ilizozitanguliza mikono yao, wangesem: ‘Ewe Mola Wetu
Mlezi! Mbona hukutuletea Mtume nasi tukafuata ishara Zako
na tukawa miongoni mwa waumini?’ 48. Lakini sasa umewajia
ukweli kutoka Kwetu wanasema: ‘Mbona hakupewa
kama vile vile avyopewa Musa? Je, kwani hawakuvikataa

alivyopewa Musa huko nyuma? Wakasema: "Ah, ni wachawi wawili tu wanaosaidiana?' Na wakasema: 'Sisi tunawakataa wote?'.

49. Sema: Basi leteni kitabu kinachotoka kwa Mwenyezi Mungu chenye mwongozo mzuri zaidi kuliko viwili hivyo, nikifuate. Ikiwa nyinyi mnasema kweli. 50. Ikiwa hawakuitikii basi jua wanajifuatia mapenzi yao tu. Na ni nani aliyepotea zaidi kuliko yule anayefuata mapenzi yake bila ya mwongozo utokao kwa Mwenyezi Mungu? Hakika Mwenyezi Mungu hawaongozi watu madhalimu. 51. Sasa tumewafikishia neno wao wenyewe ili wapate kupokea maonyo.

52. Wale ambao tuliwapa Kitabu kabla ya hiki wanauamini ujumbe huu. 53. Wanaposomewa husema tunaumini. Hakika hii ni kweli inayotoka kwa Mola Wetu Mlezi. Hakika sisi kabla yake tulikuwa Waislamu (wanyenyekevu). 54. Hao watapewa ujira wao mara mbili kutokana na walivyovumilia na watafuta ubaya kwa (kutenda) wema, na wakawa wanatoa baadhi ya tulivyowaruzuku. 55. Na wanaposikia upuuzi hujitenga nao na husema: Sisi tuna vitendo vyetu na nyinyi mna vitendo vyenu: Salamun alaykum! (Amani juu yenu) Hatutaki kujibizana na wasiojua. 56. Kwa hakika, wewe huwezi kumuongoza umpendae, lakini Mwenyezi Mungu humuongoa amtakaye, Naye Ndiye anayewajua zaidi walioongoka.

57. Na wanasema: 'Tukifuata mwongozo huu pamoja nawe, tutanyakuliwa kutoka kwene ardhi yetu. Je, kwani hatukuwaweka imara katika mahali patakatifu penye amani, ambapo yanaletwa matunda ya kila aina kuwa chakula kitokacho Kwetu? Lakini wengi wao hawajui.

58. Na ni wangapi wakazi wa miji tuliowaangamiza

waliokuwa wakijifaharisha juu ya maisha yao? Hizo sasa nyumba zao hazikukaliwa tena baada yao ila kwa uchache tu. Na Sisi ndio tumekuwa warithi. 59.Na Mola Wako Mlezi haangamizi wana wa miji mpaka ampeleke Mtume katika mji wao muhimu ili awasomee Aya Zetu. Wala hatuiangamizi miji mpaka watu wake wawe madhalimu.

60.Na kitu chochote mlichopewa ni starehe ya maisha ya dunia na anasa yake; na yaliyoko kwa Mwenyezi Mungu ndio bora na yatakayobaki zaidi. Hivi hamfahamu? 61. Je tuliyemwahidi ahadi nzuri naye kwa hakika ataipata, ni kama tuliyemstarehesha kwa starehe za maisha ya duniani, kisha siku ya Kiyama akawa miongoni mwa wanaoletwa (kwenye Jahannam)?

62. Na siku hiyo (Mwenyezi Mungu) atakapowaita akawauliza: Wako wapi wale mliokuwa mkidai kuwa ni washirika Wangu? 63. Wale iliyothibiti adhabu juu yao, watasema: ‘Mola Wetu Mlezi! Hawa ndio tuliowapoteza. Tuliwapoteza kama tulivyopotea sisi. Tunajitenga nao mbele Yako. Hawakuwa wakituabudu sisi.

64.Na itasemwa: Waiteni miungu wenu wa kipagani. Basi watawaita, lakini hawatawaitikia. Na wataiona adhabu mbele yao. (Watatamani) Laiti wangelikuwa wameongoka. 65.Na siku atakapowaita (waovu), akawauliza: ‘Mliwajibu nini Mitume’? 66. Zitawapotea habari zote siku hiyo. Nao hawataweza kuulizana. 67. Ama mwenye kutubu na akaamini na akatenda mema, huyo atakuwa miongoni mwa wenye kufanikiwa.

68. Na Mola Wako Mlezi huumba na huteua atakavyo. (Viumbe) hawana hiyari. Mwenyezi Mungu ametukuka na ametakasika na hao wanaowashirikisha Naye. 69. Na Mola

Wako Mlezi anayajua yote ambayo nyoyo zao nyoyo zao zinayaficha, na wanayoyatangaza. 70. Naye ni Mwenyezi Mungu, hapana mungu isipokuwa Yeye, ni Zake sifa njema, mwanzo na mwisho na hukumu ni Yake na Kwake Yeye mtarejeshwa.

71. Sema: Mwaonaje, kama Mwenyezi Mungu angeufanya usiku ubakie juu yenu milele mpaka siku ya Kiyama, mungu gani asiyekuwa Mwenyezi Mungu angeweza kuwaletea mwangaza? Hamsikii? 72. Sema: Mwaonaje, kama Mwenyezi Mungu angeufanya mchana ubakie moja kwa moja mpaka siku ya Kiyama, mungu gani asiyekuwa Mwenyezi Mungu angeweza kuwaletea usiku mkapumzika humo? Hamwoni? 73. Na katika huruma Zake amewafanyia usiku na mchana mpate kupumzika, na mtafute fadhila Zake na ili mpate kushukuru.

74. Na siku atakapowaita na akasema: Wako wapi mliokuwa mkidai kuwa ni washirika Wangu. 75. Na tutamtoa shahidi katika kila umma na tuseme: Leteni hoja zenu! Hapo watajua kwamba hakika ukweli ni wa Mwenyezi Mungu na yatawapotea yale waliyokuwa wakiyazusha.

76. Hakika Qaruni alikuwa katika watu wa Musa, lakini aliwafanyia utovu wa adabu. Tulimpa hazina ambazo funguo zake ziliwaelemea kundi la watu wenye nguvu. Pale watu wake walipomwambia: Usijigambe! Hakika Mwenyezi Mungu hapendi wanaojigamba. 77. Na utafute kwa (utajiri) aliokupa Mwenyezi Mungu, makazi ya Akhera; wala usisahau fungu lako katika dunia. Na fanya wema kama alivyokufanyia wema Mwenyezi Mungu, wala usitafute kufanya uharibifu katika ardhi; hakika Mwenyezi Mungu hapendi waharibifu.

78. Akasema: ‘Kwa hakika nimepewa mali hizi kwa sababu

ya elimu yangu niliyo nayo’. Je, hakujua kwamba Mwenyezi
Mungu amekwisha angamiza karne zilizokuwa kabla yake,
waliokuwa na nguvu zaidi kuliko yeye na wenye makundi
makubwa zaidi? Na wakosefu hawaulizwi (mara moja)
malipo ya dhambi zao.

79. Basi akatoka kwa watu wake akiwa amevalia mapambo
yake. Wale waliokuwa wanataka maisha ya duniani
wakasema: Laiti tungekuwa tunayo kama aliyopewa Qaruni!
Hakika yeye ni mwenye bahati kubwa. 80. Wale waliopewa
elimu ya mambo, wakasma: ‘Ole wenu! Thawabu za
Mwenyezi Mungu ni bora kwa mwenye kuamini na akatenda
mema’. Na wala hawatapatiwa hizo isipokuwa wenye subira.

81. Tukamdidimiza yeye na nyumba yake ardhini.
Wala hapakuwa na kundi lolote la kumsaidia badala ya
na Mwenyezi Mungu, wala hakuwa katika walioweza
kujitetea. 82. Ama wale waliokuwa jana yake wakitamani
mahala pake, walisema:’ Kumbe Mwenyezi Mungu
humkunjulia riziki amtakaye katika waja Wake, na humbania
amtakaye! Ingekuwa Mwenyezi Mungu hakutufanyia hisani
angelitudidimiza na sisi. Kumbe makafiri hawafanikiwi!

83. Hayo makazi ya Akhera, tunawawekea wale wasiotaka
ubeberu duniani wala ufisadi. Na mwisho mwema ni wa
wanaomcha Mwenyezi Mungu. 84. Atakayetenda mema
atapata malipo bora kuliko hayo. Na atakayetenda uovu,
hawalipwi watendao mabaya ila kwa kadri ya mabaya
waliyokuwa wakiyatenda.

85. Hakika aliyekulazimisha (kuifuata) hii Qur’an, bila
shaka atakurudisha mahali pa Marejeo. Sema: Mola Wangu
Mlezi Ndiye anayemjua zaidi mwenye kuja na mwongozo
na aliyemo katika upotevu ulio dhahiri. 86. Nawe hukuwa

unatarajia kuteremshiwa Kitabu lakini ni rehema ya Mola Wako. Basi usiwe kabisa katika wanaowasaidia wanaomkana Mwenyezi Mungu. [87.] Wala wasikuzuie na Aya za Mwenyezi Mungu baada ya kuteremshiwa. Na lingania kwa Mola Wako Mlezi, na usiwe kabisa miongoni mwa mapagani. [88.] Na usimwombe pamoja na Mwenyezi Mungu mungu mwingine. Hapana Mungu ila Yeye. Kila kitu kitaangamia isipokuwa Dhati Yake. Hukumu ni Yake na Kwake Yeye mtarejeshwa.

## 29. Sura Al-A'nkabut

## SURA YA BUIBUI

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 *Alif Lam Mim.*

2 Je, wanadhani watu wataachwa waseme tumeamini nao
wasijaribiwe? 3 Hakika tuliwajaribu waliokuwa kabla yao.
Hakika Mwenyezi Mungu atawajua wakweli na atawajua
waongo.
4 Au wanaofanya uovu wanadhania wanatushinda?
Hukumu mbaya hiyo wanayoitoa! 5 Mwenye kutaraji
kukutana na Mwenyezi Mungu, hakika miadi ya Mwenyezi
Mungu itafika. Naye ni Mwenye kusikia Mwenye kujua
mno. 6 Na anayejikakamua (kwa hali na mali) basi hakika
anajikakamua kwa manufaa yake mwenyewe. Kwa sababu
Mwenyezi Mungu si mhitaji wa walimwengu. 7 Na wale
ambao wameamini na wakatenda mema, kwa hakika

tutawafutia madhambi yao, na tutawalipa mazuri zaidi ya waliyokuwa wakiyatenda.

8. Na tumemwusia mwanadamu kuwatendea wema wazazi wake wawili. Na wakikushikilia (kwa lazima) unishirikishe Mimi na mambo ambayo huna uwelewa nayo, usiwatii. Kwangu Mimi ndio marejeo yenu, na nitawaambia
mnayoyatenda. 9. Na wale ambao wameamini na wakatenda
memа, kwa hakika tutawaingiza katika suhuba ya wema.

10. Na katika watu kuna wanaosema:'Tumemwamini Mwenyezi Mungu! Lakini wanapopata shida kwa ajili ya (dini ya) Mwenyezi Mungu huchukulia mateso ya watu kana kwamba ni adhabu ya Mwenyezi Mungu. Na itakapokuja nusra kutoka kwa Mola Wako Mlezi lazima watasema: 'Ah, sisi tulikuwa pamoja nanyi'! Kwani Mwenyezi Mungu
hayajui yaliyomo vifuani mwa walimwengu? 11. Hakika
Mwenyezi Mungu anawajua ambao wameamini bara-bara na kwa yakini anawajua wanafiki.

12. Na wale waliomkana Mwenyezi Mungu huwaambia walioamini: 'Fuateni njia yetu na sisi tutayabeba madhambi yenu'. Kamwe wao hawatabeba chochote katika madhambi
yao. Hakika hao ni waongo. 13. Kwa kweli wao wataibeba
mizigo yao wenyewe tu, na mizigo mingine pamoja na mizigo yao. Na kwa hakika wataulizwa siku ya Kiyama juu ya uwongo waliozusha.

14. Na hakika tulimtuma Nuh (Noah) kwa kaumu yake, akakaa nao miaka elfu moja kasoro miaka hamsini (ndiyo iliyokuwa mizuri). Kisha tufani likawachukua huku wakiwa
wao ni wafanya maovu. 15. Tukamwokoa yeye na watu wa
safina na tukaifanya hiyo kuwa ni ishara kwa walimwengu wote.

16. Na Ibrahim (Abraham) pale alipowaambia watu wake:
'Mwabuduni Mwenyezi Mungu na mcheni Yeye tu. Hilo ni
kheri kwenu ikiwa mnajua'. 17. Hakika nyinyi mnaabudu
masanamu kinyume na Mwenyezi Mungu na mnazusha
uwongo. Hakika mnaowaabudu kinyume na Mwenyezi
Mungu hawamilikii riziki yoyote. Ombeni riziki kutoka kwa
Mwenyezi Mungu na mumwabudu na mumshukuru; Kwake
mtarudishwa. 18. Na kama mkikataa (ujumbe) basi mataifa
chungu nzima kabla yenu yalikwishakataa pia. Na si juu ya
Mtume zaidi ya kufikisha ujumbe tu.

19. Hivi hawaoni jinsi Mwenyezi Mungu alivyobuni
uumbaji na kisha anarudia tena? Hakika hilo kwa Mwenyezi
Mungu ni rahisi. 20. Sema: Tembeeni katika ardhi na tazameni
jinsi alivyoanzisha kuumba toka mwanzo, kisha Mwenyezi
Mungu ndiye atakayeumba umbo la baadaye. Hakika
Mwenyezi Mungu ni Muweza juu ya kila kitu. 21. Humwadhibu
amtakaye, na humwonea huruma amtakaye; na Kwake
mtarudishwa. 22. Wala nyinyi si wa ku(tu)shinda, si ardhini,
si mbinguni. Wala hamna isipokuwa Mwenyezi Mungu wa
kuwalinda au kuwasaidia. 23. Na wale ambao wamezikanusha
Ishara za Mwenyezi Mungu na (wakakanusha) kukutana
Naye, hao wamekata tamaa kupata huruma yangu, na hao
ndio watakaopata adhabu chungu.

24. Basi halikuwa jawabu la watu wake isipokuwa
kusema: 'Mwueni huyo au mchomeni moto ! Mwenyezi
Mungu akamwokoa na moto. Hakika katika hilo kuna ishara
kwa watu wanaoamini. 25. Na akasema: Hakika nyinyi
mmeyashika masanamu (kwa ibada) badala ya Mwenyezi
Mungu kutokana na mapenzi baina yenu katika maisha haya
ya duniani. Lakini siku ya Kiyama mtakataana nyinyi kwa

nyinyi na mtalaaniana nyinyi kwa nyinyi. Na makazi yenu ni motoni wala hamtapata wa kuwanusuru. 26. Lut akamwamini (Ibrahim) akasema: ‘Mimi nahama (mji wa Chaldea) kwa ajili ya Mola Wangu Mlezi. Hakika Yeye ni Mwenye utukufu, Mwenye hekima. 27. Na tukamtunukia yeye Is-haq (Isaac) na Ya’qub (Yakobo) na tukajaalia katika kizazi chake Unabii na Kitabu na tukampa malipo yake ya hapa duniani. Naye hakika huko Akhera, bila shaka atakuwa katika (jumuiya ya) watu wema.

28. Na (kumbuka) pale Lut alipowaambia jamaa zake: Hakika nyinyi mnafanya uchafu ambao hajawahi yeyote kuufanya katika walimwengu. 29. Hivi mnawaingilia wanaume na mnakata njia, na katika vilabu vyenu pia mnafanya maovu (hayo)? Basi halikuwa jibu la watu wake isipokuwa kusema: Tuletee adhabu ya Mwenyezi Mungu ikiwa wewe ni katika wakweli.[12] 30 Akasema: Mola Wangu Mlezi! Ninusuru na watu hawa waliobobea katika machafu.

31. Na pale wajumbe Wetu walipomjia Ibrahim na habari njema, wakasema: ‘Kwa kweli sisi tutawaangamiza watu wa mji huu, kwa sababu watu wake wamekubuhu katika matendo mabaya’. 32. Akasema (Ibrahim): ‘Lakini Lut yumo humo mjini’! Wakasema: ‘Sisi tunajua zaidi nani aliyemo humo. Bila shaka tutamwokoa yeye na wafuasi wake, isipokuwa mkewe. Yeye atakuwa miongoni mwa watakaochelewa

12. Wafasiri kadhaa wameona watu wa Lut walikuwa wakifanya makosa hayo matatu kwa pamoja. Isipokuwa viishiria vya Aya vinaonesha walifanya kosa moja la ulawiti. Ila walilifanya wazi wazi kila mahali, wakiwateka wasafiri katika barabara na kuwafanyia umaluuni huo, aidha vilabuni nk. Hivi ndivyo alivyoona Tabari na wengineo. Nimefuata rai hii- Mfasiri.

kutoka'. 33. Na wajumbe wetu walipomfika kwa Lut, alipata simanzi kwa ajili yao na akaona dhiki. Wakasema: 'Usihofu wala usihuzunike. Sisi tutakuokoa wewe na wafuasi wako, isipokuwa mkeo, yeye ni miongoni mwa watakaochelewa kutoka'. 34. 'Hakika sisi tutawateremshia watu wa mji huu adhabu kutoka mbinguni kwa sababu ya ufuska wanaoufanya'. 35. Hakika tumeacha katika mji huo ishara iliyo wazi kwa watu watakaotaka kujua.

36. Na kwa watu wa Madyan (tulimpeleka) ndugu yao Shua'yb, akasema: 'Enyi watu wangu! Mwabuduni Mwenyezi Mungu! Na iogopeni siku ya Mwisho, wala msieneze uchafu duniani kwa nia ya kuleta uharibifu. 37. Wakamwona mwongo. Ndipo tetemeko la ardhi likawapiga, asubuhi yake wakawa wameanguka majumbani mwao kifudifudi.

38. Na kina A'd na Thamud.Na mmekwishaona yaliyojiri katika makazi yao. Na shetani aliwafanya waone matendo yao kuwa mazuri, akawazuia njia (ya Mwenyezi Mungu) ingawaje wao walikuwa wenye maarifa na werevu.

39.Na Qaruni na Firaun na Haman. Na hakika aliwajia Musa na ishara wazi wazi, lakini wakafanya kiburi katika nchi. Na wala hawakuwa ni wenye kutushinda Sisi.. 40. Na kila mmoja tulimtesa kwa dhambi zake. Kuna wale tuliowapelekea kimbunga cha changarawe, na kuna wale walioangamizwa kwa mpasuko (mkubwa); na kuna tuliowadidimiza katika ardhi; na miongoni mwao wapo tuliowagharikisha majini. Wala Mwenyezi Mungu hakuwa Mwenye kuwadhulumu, lakini walikuwa wakijidhulumu wenyewe.

41. Mfano wa wale ambao wamewafanya (wengine) kuwa wa kuwalinda badala ya Mwenyezi Mungu, ni kama mfano wa buibui aliyejijengea nyumba. Na hakika nyumba dhaifu

zaidi kuliko zote ni nyumba ya buibui, lau wangekuwa wanajua. 42. Hakika Mwenyezi Mungu anajua kitu chochote kile wanachokiomba badala Yake. Na Yeye ndiye Mwenye nguvu, Mwenye hekima. 43. Na hiyo ni mifano tunawapigia watu na hawaifahamu ila wenye elimu. 44. Mwenyezi Mungu ameumba mbingu na ardhi kwa (uwiano wa) haki. Hakika katika hayo kuna ishara kwa waumini.

45. Soma yale uliyofunuliwa kwa Wahyi katika Kitabu; na usimamishe Swala, hakika Swala huzuia machafu na maovu. Na hakika kumtaja na kumkumbuka Mwenyezi Mungu ni jambo kubwa kabisa (katika maisha). Na Mwenyezi Mungu anayajua mnayoyafanya.

46. Wala msibishane na watu wa Kitabu isipokuwa kwa njia iliyo nzuri zaidi; isipokuwa wale waliowafanyieni mabaya miongoni mwao. Na semeni: Tumeamini yaliyoteremshwa kwetu na yaliyoteremshwa kwenu. Na Mungu Wetu na Mungu Wenu ni Mmoja, na sisi ni wenye kujisalimisha Kwake.

47. Na kwa hivi tumekuteremshia Kitabu (Qur’an), kwamba wale ambao tumewapa Kitabu (Injili) watakiamini, na miongoni mwa hao (Mapagani wa Kiarabu) pia watakuwepo watakaokiamini. Hawatakata aya Zetu isipokuwa wanaomkana Mwenyezi Mungu. 48. Na wewe hukuwa kabla yake ukisoma kitabu chochote, wala kukiandika kwa mkono wako wa kuume. Ingelikuwa hivyo, hao wasema ovyo wangetia shaka. 49. Bali hiyo (Qur’an) ni ishara zilizo wazi katika vifua vya waliopewa elimu; na hawazikatai ishara Zetu isipokuwa madhalimu.

50. Na wanasema: Mbona hakuteremshiwa miujiza kutoka kwa Mola Wake? Sema: Hakika miujiza ni kutoka Kwake

Mwenyezi Mungu; na mimi kwa hakika ni mwonyaji mwenye kubainisha tu. [51.] Je, kwani hayakuwatosha kwamba tumekuteremshia Kitabu (hiki) wanachosomewa? Hakika katika hiyo kuna rehema na mawaidha kwa watu wanaoataka kuamini. [52.] Sema: Mwenyezi Mungu anatosha kuwa shahidi baina yangu na nyinyi, anajua yaliyomo mbinguni na ardhini. Na wale ambao wameamini upotevu na wakamkana Mwenyezi Mungu, hao ndio waliopata hasara.

[53.] Na wanakuhimiza (iletwe) adhabu; na lau si wakati maalum uliowekwa, basi adhabu ingewajia na hakika ingewatokea ghafla na hali wao hawatambui. [54.] Wanakuhimiza adhabu na hali Jahannam kwa hakika imewazunguka makafiri. [55.] Siku itakapowafunika adhabu hiyo kutoka juu yao na chini ya miguu yao na (sauti) iwaambie: 'Onjeni (matokeo ya) mliyokuwa mkiyatenda.

[56.] Enyi waja Wangu walioamini! Kwa hakika ardhi Yangu ina nafasi pana. Hivyo niabuduni Mimi tu. [57.] Kila nafsi itaonja mauti, kisha mtarudishwa Kwetu. [58.] Na wale ambao wameamini na wakatenda mema, hakika tutawaweka katika maghorofa ya Peponi, ambayo mito ya maji, maziwa, asali, pombe hupita chini yake, wadumu humo. Ni neema iliyoje kwa malipo ya watendaji. [59.] Ambao walisubiri na wakamtegemea Mola Wao Mlezi. [60.] Na ni wanyama wangapi hawabebi chakula chao? Mwenyezi Mungu huwaruzuku wao na nyinyi. Na Yeye ni Msikizi, Mjuzi.

[61.] Na ukiwauliza ni nani aliyeumba mbingu na ardhi na akalifanya jua na mwezi kutii amri yake? Bila shaka watasema ni Mwenyezi Mungu! Sasa vipi wanadanganywa wasifuate ukweli? [62.] Mwenyezi Mungu humkunjulia riziki amtakaye katika waja Wake na humpa mwingine kwa kipimo. Hakika

Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu. 63. Na ukiwauliza ni nani aliyeteremsha maji kutoka mbinguni na akairudishia ardhi uhai baada ya kunyauka? bila shaka watasema ni Mwenyezi Mungu. Sema: Alhamdulillah (sifa njema ni za Mwenyezi Mungu), lakini wengi wao hawafahamu.

64. Na maisha haya ya dunia si chochote ila anasa na mchezo. Na nyumba ya akhera ndiyo maisha hasa. Kama wangekuwa wanajua. 65. Na wapandapo katika jahazi, humwomba Mungu kwa kumtii Yeye pekee. Lakini anapowaokoa wakafika nchi kavu mara wanamshirikisha. 66. Kwa kuyakana kwa dharau tuliyowapa, ili wapate kustarehe. Punde watajua.

67. Hivi hawaoni kwamba tumeifanya sehemu takatifu (kuzunguka Kaaba) kuwa ina Amani, wakati watu wananyakuliwa pambizoni mwake? Je, wanaamini upuuzi lakini wanakataa (kuamini) neema za Mwenyezi Mungu? 68. Na ni nani anayefanya mabaya zaidi kuliko yule anayemzushia Mwenyezi Mungu uwongo; au akadhibishaye ukweli unapomjia? Je, si katika Jahannam ndio yatakuwa makazi ya makafiri? 69. Na wale wanaofanya juhudi kwa ajili Yetu, hakika tutawaongoza kwenye njia Zetu. Na hakika Mwenyezi Mungu yuko pamoja na watu wafanyao wema.

30. Sura Ar-Rum

## SURA KUHUSU ‘DOLA LA’ WAZUNGU

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 *Alif Lam Mim*.

2 Dola la Warumi tayari limeshindwa, 3 Katika nchi iliyo
karibu. Nao baada ya kushindwa watashinda, 4 Katika miaka
michache. Ni uamuzi wa Mwenyzi Mungu kabla na baada
yake. Na siku hiyo waumini watafurahi… 5 Kwa nusra ya
Mwenyezi Mungu. Humnusuru amtakaye; na Yeye ndiye
Mwenye uwezo, Mwenye kurehemu. 6 Ni ahadi ya Mwenyezi
Mungu, Mwenyezi Mungu havunji ahadi Yake, lakini watu
wengi hawajui. 7 Wanajua kilicho dhahiri (tu) katika maisha
ya dunia, lakini wao juu ya akhera hawana utambuzi.

8 Hivi hawafikirii ndani ya akili zao wenyewe, Mwenyezi
Mungu hakuumba mbingu na ardhi na vilivyomo kati yao
isipokuwa kwa haki, na kwa muda maalum? Kwa hakika
watu wengi ni wenye kukataa kuwa watakutana na Mola Wao
Mlezi. 9 Hivi hawatembei katika ardhi wakaona ulivyokuwa
mwisho wa wale waliokuwa kabla yao? Walikuwa wana
nguvu zaidi kuliko wao. Wakailima ardhi na kuistawisha zaidi
kuliko walivyoistawisha wao (mapagani wa kiarabu). Na
mitume wao wakawajia na dalili zilizo wazi (wakawakataa).
Mwenyezi Mungu hakuwa ni Mwenye kuwadhulumu, lakini
walikuwa wakijidhulumu wenyewe. 10 Hatimaye, mwisho
wa ambao walifanya uovu, ni uovu: kukanusha kwao ishara
za Mwenyezi Mungu, na wakawa wanazifanyia dharau.

11. Mwenyezi Mungu ndiye anayebuni uumbaji na kisha
akaurudisha mara nyingine; na kisha mtarejeshwa Kwake.
12. Na siku kitakaposimama Kiyama, wakosefu watakata
tamaa. 13. Wala hawatakuwa na waombezi miongoni mwa
waliokuwa wakiwashirikisha, nao watawakana washirika
wao. 14. Na siku kitakaposimama Kiyama, siku hiyo
watagawanyika. 15. Ama wale ambao wameamini na
wakatenda mema watakuwa katika Bustani wakifurahishwa.
16. Na ama wale ambao wamekufuru na wakazikadhibisha
ishara Zetu na mkutano wa Akhera, basi hao wataletwa mbele
ya adhabu. 17. Basi Utukufu pasi na kushirikiana na yeyote
ni wa Mwenyezi Mungu wakati mnapofikia machweo na
wakati muamkapo asubuhi. 18. Na sifa njema zote maridhawa
ni Zake katika mbingu na ardhi, na mwisho wa Alasiri na
wakati mchana unaanza kutoweka.

19. Hukitoa kilicho hai kutokana na kilichokufa, na hukitoa
kilichokufa kutokana na kilicho hai; na huipa ardhi uhai baada
ya kufa kwake; na kama hivyo, ndivyo mtakavyofufuliwa.
20. Na katika Ishara Zake ni kuwa amewaumba kwa udongo;
kisha mkawa nyinyi watu mliotawanyika kila upande. 21. Na
katika Ishara Zake ni kuwaumbia wake zenu kutokana na
nyinyi wenyewe, ili mpate utulivu kwao. Na amejaalia baina
yenu mapenzi na huruma. Hakika katika haya kuna Ishara
kwa watu wanaofikiri.

22. Na katika Ishara Zake ni kuumba mbingu na ardhi, na
kutofautiana lugha zenu na rangi zenu. Hakika katika hayo
kuna Ishara kwa wenye elimu. 23. Na katika ishara Zake ni
kulala kwenu usiku na mchana, na kutafuta kwenu fadhila
Zake. Hakika katika hayo kuna ishara kwa watu wanaosikia.
24. Na katika Ishara Zake ni kuwaonesha ninyi umeme kwa

kuwatia hofu na kuwatia tamaa, na kuwateremshia maji kutoka mawinguni, na kwayo akaihuisha ardhi baada ya kufa kwake. Hakika katika hayo kuna ishara kwa watu wenye akili.

25. Na katika Ishara Zake ni kuwa mbingu na ardhi zinasimama kwa amri Yake. Kisha atakapowaita wito mmoja, hapo mtatoka ardhini. 26. Ni chake kila kiumbe kilichoko mbinguni na ardhini. Vyote vinamtii. 27. Naye Ndiye anayebuni uumbaji kisha anaurudisha tena. Na jambo hili ni jepesi zaidi Kwake. Naye ndiye mwenye mfano mzuri adhimu zaidi (usiofikirika kabisa kwa viumbe) katika mbingu na ardhi; na Yeye Ndiye Mwenye uwezo, Mwenye hekima.

28. Amewapigia mfano juu yenu wenyewe. Je, wapo katika hao (watumwa) wanaomilikiwa na mikono yenu ya kuume, mnao washirika katika (utajiri) tuliowapa? Mkawa nyie (na wao) mko sawa sawa katika utajiri huo? Mkawa mnawaogopa kama mnavyoogopana nyie (mlio huru)? Kama hivi tunaziweka wazi aya Zetu kwa watu wenye akili. 29. Bali wanaofanya mabaya wanafuata mapenzi ya nafsi zao wenyewe bila kujua. Ni nani atamwongoza ambaye Mwenyezi Mungu amemwacha apotee?

30. Basi uelekeze uso wako sawasawa kwenye dini. Hilo ndilo umbile la Mwenyezi Mungu alilowaumbia watu. Hapana mabadiliko katika uumbaji wa Mwenyezi Mungu. Hiyo ndiyo dini ya kigezo. Lakini watu wengi hawajui. 31. Muwe wenye kurejea Kwake na mcheni, na dumisheni Swala; wala msiwe katika mapagani... 32. Wale ambao wameigawa dini yao na wakawa vikundi, kila kundi hufurahia yao waliyo nayo.

33. Yanapowapata wanadamu matatizo humwomba Mola

Wao Mlezi huku wakirejea Kwake. Ama aanapowaonjesha rehema kutoka Kwake, mara kikundi miongoni mwao humshirikisha Mola Wao Mlezi na vitu vingine.! 34. Kwa kukana (neema) tulizowapa. Basi stareheni, mtakujajua. 35. Au tumewateremshia kiongozi akawa anawaongoza kwenye vile wanavyovishirikisha?

36. Na watu tunapowaonjesha rehema huifurahia, na ukiwasibu uovu kwa sababu ya yale ambayo mikono yao iliyatanguliza, mara hukata tamaa. 37. Je, hawaoni kwamba Mwenyezi Mungu humkunjulia riziki amtakaye na huibana kwa (amatakaye)? Hakika katika hayo kuna ishara kwa watu wanaoamini. 38. Basi mpatie mwenye udugu wa karibu nawe haki yake, na masikini na mpita njia. Hivyo ni vizuri kwa wale wanaotaka radhi ya Mwenyezi Mungu, na hao ndio wenye kufanikiwa. 39. Na zile (mali) mnazozitoa kwa riba ili ziongezeke katika mali za watu, haziongezeki mbele ya Mwenyezi Mungu. Lakini mlichokitoa kama Zaka kwa kutaka radhi ya Mwenyezi Mungu, basi hao ndio wazidishao (malipo yao).

40. Mwenyezi Mungu Ndiye aliyewaumba, kisha akawaruzuku, kisha atawafanya mfe na kisha atawafufua. Je katika mnaowashirikisha yuko awezaye kufanya lolote katika hayo? Ametakasika na ametukuka na hayo wanayomshirikisha nayo. 41. Uharibifu umejitokeza nchi kavu na baharini kwa sababu ya yatendwayo na mikono ya watu. Hivyo kwamba Mwenyezi Mungu (huenda) akawaonjesha sehemu tu ya waliyoyatenda, ili wapate kurudi nyuma (kuacha uharibifu). 42. Sema: Tembeeni katika ardhi na tazameni ulikuwaje mwisho wa wale waliotangulia. Wengi wao walikuwa mapagani.

43. Basi uelekeze uso wako kwenye dini iliyo kigezo kabla ya kufika siku isiyozuilika, inayotoka kwa Mwenyezi Mungu. Siku hiyo watatengana. 44. Anayekufuru basi ukafiri wake utakuwa juu yake, na anayetenda mema basi wanazitengenezea nafsi zao. 45. Ili awalipe walioamini na wakatenda mema katika hisani zake. Hakika Yeye hapendi makafiri.

46. Na katika ishara Zake ni kuzituma pepo ziletazo bishara njema ili awaonjeshe rehema Yake, na ili majahazi yaende kwa amri Yake mtafute baadhi ya fadhila Yake, ili mumshukuru. 47. Na hakika tulikwishawatuma mitume kwa watu wao na wakawajia na hoja zilizo waziwazi. Tukawaadhibu wale waliofanya makossa. Na ilikuwa ni haki juu Yetu kuwanusuru waumini.

48. Mwenyezi Mungu Ndiye anayezituma pepo zikayatimua mawingu. Kisha akayatandaza mbinguni kama apendavyo, na akayafanya mapande mapande, ukaona mvua inatoka ndani yake. Anapowafikishia anaowataka katika waja Wake, mara wanakuwa na furaha. 49. Ingawaje kabla ya kuteremshiwa walikuwa wenye kukata tamaa. 50. Angalia athari za rehema ya Mwenyezi Mungu, jinsi anavyoihuisha ardhi baada ya kufa kwake. Basi hakika huyo, bila shaka, Ndiye Mwenye kuhuisha wafu; na Yeye ni Muweza juu ya kila kitu. 51. Na kama tungetuma upepo wakaona (mimea yao) imegeuka kuwa rangi ya njano, wangeendelea kuwa watovu wa shukrani baada yake. 52. Kwa hakika wewe huwezi kuwafanya wafu wasikie wala kuwafanya viziwi wasikie wito, wanapogeuka na kurudi nyuma. 53. Wala huwezi kuwaongoza vipofu kuachana na upotevu wao. Huwezi kuwafanya wasikilize ila wale wanaoziamini aya Zetu. Hao ndio wanyenyekevu.

54. Mwenyezi Mungu Ndiye ambaye amewaumba katika udhaifu, kisha akajaalia nguvu baada ya udhaifu, kisha akajaalia udhaifu baada ya nguvu na uzee; anaumba atakavyo; Naye Ndiye Mjuzi, Mwenye uwezo. 55. Na siku kitakaposimama Kiyama, wakosefu wataapa kuwa hawakukaa duniani isipokuwa saa moja tu! Hivyo ndivyo walivyokuwa wakijidanganywa. 56. Na waliopewa elimu na Imani watasema: Hakika nyinyi mlikwishakaa kwa amri ya Mwenyezi Mungu hadi siku ya kufufuliwa. Hii basi ndio siku ya kufufuliwa, lakini nyinyi mlikuwa hamjui. 57. Siku hiyo waliofanya dhambi havitawafaa visingizio watakavyovitoa, wala hawatapewa nafasi ya kuungama.

58. Na hakika tulikwishawapigia watu aina mbali mbali za mifano katika hii Qur'an. Lakini ukiwaletea aya yoyote bila shaka wale waliokufuru watasema: Ninyi hamfanyi lolote ila kupiga porojo tu! 59. Hivyo ndivyo Mwenyezi Mungu (anavyofunga na) kupiga muhuri nyoyo za wasiotaka kufahamu. 60. Basi subiri. Hakika ahadi ya Mwenyezi Mungu ni ya kweli. Wala wasikutingishe-tingishe (kujaribu uimara wako) wale wasio na yakini.

## 31. Sura Luqman

# SURA YA LUQMAN

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 *Alif Lam Mim.* Mwenyezi Mungu pekee ndiye ajuae maana hasa.

2 Hizi ni Aya za Kitabu chenye hekima. 3 Ni mwongozo
na rehema kwa wafanyao wema. 4 Ambao wanasimamisha
Swala, wakatoa Zaka na wana yakini na Akhera. 5 Hao ndio
waliopokea uongofu kutoka kwa Mola Wao Mlezina, na hao
ndio wenye kufaulu.

6 Na miongoni mwa watu wapo wanaonunua maneno ya
porojo pasi kujua, ili wawapoteze watu na njia ya Mwenyezi
Mungu, na wanalichukulia hilo kuwa mzaha. Hao watapata
adhabu ya kuwafedhehesha. 7 Na anaposomewa Aya Zetu
huzipa mgongo kwa kiburi, kana kwamba hakuzisikia, na
kana kwamba masikioni mwake mna uziwi. Basi mtangazie
huyo adhabu chungu. 8 Hakika wale ambao wameamini na
wakatenda mema watakuwa na mabustani yenye neema.
9 Wataishi milele humo. Hii ni ahadi ya kweli ya Mwenyezi
Mungu, na Yeye ndiye Mwenye uwezo, Mwenye hekima.

10. Ameumba mbingu bila ya nguzo mnazoziona, na
ameweka katika ardhi milima ili ardhi isiwayumbishe. Na
akatawanya humo ardhini aina mbali mbali za wanyama; na
tukateremsha maji kutoka mawinguni na tukaotesha katika
ardhi mimea mizuri ya kila namna. 11. Huu ndio uumbaji
wa Mwenyezi Mungu. Basi nionesheni wameumba nini hao
wasiokuwa Yeye! Lakini waovu wamo katika upotevu wa
dhahiri.

12. Na hakika tulimpa Luqman hekima tukamwambia:
Mshukuru Mwenyezi Mungu. Na mwenye kumshukuru
Mwenyezi Mungu basi hakika anashukuru kwa manufaa
ya nafsi yake. Na akana neema za Mwenyezi Mungu, basi
Mwenyezi Mungu ni Mkwasi, Msifiwa. 13. Na (kumbuka
pale) Luqman alipomwambia mwanawe akiwa anampa

nasaha: Ewe mwanangu! Usimshirikishe Mwenyezi Mungu na chochote, hakika ushirikishaji ni makosa makubwa.

14. Na tumemwamrisha mwanadamu kuwatendea wema wazazi wake. Mama yake aliibeba mimba yake (akivumilia) uchungu wa uzazi juu ya mwingine; Na (baada ya) miaka miwili ndipo akamwachisha ziwa: nishukuru Mimi na wazazi wako, kwani marudio ni kwangu tu. 15. Na kama wakishikilia lazima unishirikishe Mimi na yale ambayo huna ujuzi nayo, hapo usiwatii, lakini kaa nao kwa wema duniani, na fuata njia ya yule anayegeukia Kwangu. Hatimaye, hakika marejeo yenu ni Kwangu Mimi, Nami nitawaambia mliyokuwa mkiyatenda.

16. Ewe mwanangu! Ikiwa kuna kitu chenye uzito (duni) kama chembe ya haradali, kikawa kimefichwa ndani ya mwamba au (popote) katika mbingu au katika ardhi, Mwenyezi Mungu atakileta. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa vilivyo ndani kabisa, Mwenye habari nanvyo. 17. Ewe mwanangu! Simamisha Swala na uamrishe mema na ukataze mabaya na subiri kwa yanayokusibu, hakika hivyo ndiyo kuwa na azimio katika (kufanya) mambo. 18. Wala usivimbishe shavu lako kwa (kiburi) watu, wala usitembee katika nchi kwa mikogo na maringo. Hakika Mwenyezi Mungu hampendi kila anayejivuna anayejifaharisha. 19. Na kuwa wastani katika hatua zako, uinamishe sauti yako. Hakika sauti inayochukiza zaidi kuzidi zote ni sauti ya punda.

20. Je, hamuoni kwamba Mwenyezi Mungu amevifanya viwatumikie nyinyi vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini na akawajazieni neema Zake za wazi wazi na zilizojificha? Na miongoni mwa watu wapo wanaojadiliana juu ya Mwenyezi Mungu bila ya elimu wala mwongozo

wala Kitabu cha kuwapa mwanga. 21. Na wanapoambiwa: Fuateni aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu; husema: bali sisi tutafuata yale tuliyowakuta nayo baba zetu. Je, hata kama shetani anawaita kwenye adhabu ya moto unaowaka?

22. Na anayeusalimisha uso wake (mwili) kwa Mwenyezi Mungu naye akawa anafanya wema, basi huyo hakika amekamata kishikilio cha kuaminika; na mwisho wa mambo yote ni kwa Mwenyezi Mungu. 23. Na mwenye kukana, kusikuhuzunishe kukana kwake. Marejeo yao ni Kwetu, ndipo tutawaambia yale waliyoyafanya. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa yaliyomo vifuani. 24. Tunawapa starehe ya muda kidogo, kisha tutawasukuma kwenye adhabu ngumu.

25. Na unapowauliza ni nani aliyeumba mbingu na ardhi? Bila shaka watasema ni Mwenyezi Mungu. Sema: Alhamdulillahi! Bali wengi wao hawafahamu. 26. Ni vya Mwenyezi Mungu vyote vilivyomo mbinguni na ardhini. Hakika Mwenyezi Mungu Ndiye Mkwasi, Msifiwa. 27. Na lau miti yote iliyomo ardhini ikawa ni kalamu na bahari (ikawa wino) na bahari saba nyingine zikaiongezea (wino)…. maneno ya Mwenyezi Mungu yasingemalizika (kuandikwa). Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu kubwa, Mwenye hekima.

28. Na kuumbwa kwenu na kufufuliwa kwenu nyote ni kama kumwumba mtu mmoja tu (si lolote!). Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia, Mwenye kuona. 29. Je, huoni kwamba Mwenyezi Mungu huuingiza usiku katika mchana na huuingiza mchana katika usiku. Na amelifanya jua na mwezi kutii (utaratibu wake)? Kila kimoja hufuata mpangilio wake hadi wakati uliowekwa. Na Mwenyezi Mungu ana habari za mnayoyafanya. 30. Hayo ni kwa kuwa Mwenyezi

Mungu Ndiye wa kweli, na kwamba vile wanavyoviomba badala Yake ni uwongo, na hakika Mwenyezi Mungu Ndiye aliye juu, Mkubwa.

31. Je, huoni kwamba majahazi hupita baharini kwa neema za Mwenyezi Mungu, ili awaoneshe ishara Zake? Hakika katika hayo kuna ishara kwa kila mwingi wa subira , mwingi wa shukrani. 32. Na wimbi linapowafunika kama mawingu, humuomba Mwenyezi Mungu kwa kumsafia ibada kabisa. Lakini anapowaokoa wakafika nchi kavu, wapo baadhi yao huwa wastani (kati ya kutenda mema na mabaya). Hakuna anayekanusha ishara zetu isipokuwa kila mhaini mkuu, mtovu kabisa wa shukrani.

33. Enyi watu! Mcheni Mola Wenu Mlezi na iogopeni siku ambayo mzazi hatamfaa mwanawe wala mwana hatamfaa mzaziwe kwa lolote. Hakika ahadi ya Mwenyezi Mungu ni kweli, basi yasiwadanganye maisha ya dunia wala asiwadanganye na Mwenyezi Mungu (Shetani) mdanganyifu. 34. Hakika Mwenyezi Mungu pekee ndiye mwenye ujuzi wa siku ya Kiyama. Na Yeye ndiye huteremsha mvua na anavijua vilivyo ndani ya matumbo ya uzazi. Na haijui nafsi yoyote itachuma nini kesho. Wala nafsi yoyote haijui itakufa katika nchi gani. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi, Mwenye habari.

32. Sura As-Sajda

# SURA YA SUJUDI

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 *Alif Lam Mim.* Mwenyezi Mungu ndiye ajuaye maana hasa.

2 Ni ufunuo wa Kitabu kisicho na shaka ndani yake,
kinachotoka kwa Mola wa walimwengu wote. 3 Au wanasema
amekizusha? Hapana, hicho ni ukweli utokao kwa Mola
Wako Mlezi, ili uwaonye watu wasiofikiwa na mwonyaji
kabla yako. Labda huenda wataongoka.
4 Mwenyezi Mungu Ndiye aliyeziumba mbingu na ardhi
na vilivyomo kati yake katika (kadiri ya) siku sita. Tena
akakunjua utawala wake juu ya Kiti cha Enzi. Ninyi hamna
wa kuwalinda wala mwombezi isipokuwa Yeye. Jee, bado
hamjapokea onyo? 5 Hupanga mambo yote kutoka mbinguni
kwenda ardhini, kisha (hatimaye) mambo yote yanaishia
Kwake. Katika siku ambayo urefu wake ni (kadiri ya) miaka
elfu kwa mnavyohesabu ninyi. 6 Huyo ndiye Mjuzi wa
mambo ya ghaibu na ya dhahiri, Mwenye uwezo, Mwingi
wa huruma. 7 Ambaye ametengeneza vizuri umbo la kila
kitu na akaanzisha kumwumba binadamu kwa udongo.
8 Kisha akajaalia kizazi chake kitokane na asili ya maji
yanayotwezwa. 9 Kisha akamweka kwa vipimo sahihi, na
akampulizia roho Yake. Na amewajaalia kusikia na kuona na
nyoyo. Ni uchache mnavyoshukuru.
10. Na wao husema: Ati tutakapopotea kabisa ardhini,
kweli tutarudishwa kwenye umbo jipya? Bali wao wanakana

kukutana na Mola Wao Mlezi. 11. Sema: atawafisha malaika wa
mauti aliyewakilishwa kwenu; kisha mtarejeshwa kwa Mola
Wenu. 12. Na kama ungewaona wakosefu wanavyoinamisha
vichwa vyao mbele ya Mola Wao, (wakilia) 'Mola
Wetu Mlezi! Tumeona na tumesikia, turejeshe (duniani)
tukatende mema, kwani hakika sisi (sasa) tuna yakini.
13. Na lau tungetaka tungeipa kila roho mwongozo wake,
lakini neno litokalo kwangu ni la kweli: 'Nitaijaza Jahannam
majini na watu kwa pamoja' 14. Basi onjeni (adhabu) kwa
vile mlivyousahau mkutano wa siku yenu hii. Sisi pia
tumewasahauni. Basi onjeni adhabu ya milele kwa yale
mliyokuwa mkiyatenda. 15. Hakika wanaoziamini Aya Zetu
ni wale tu ambao wanapokumbushwa hizo, huporomoka
kusujudu na kumsabihi kwa kumsifu Mola Wao Mlezi, nao
hawafanyi majivuno. 16. Mbavu zao zinaacha vitanda vyao
vya kulalia, ili kumwomba Mola Wao Mlezi kwa hofu na
matumaini, na hutoa katika vile tulivyowaruzuku. 17. Hakuna
mtu yeyote anayejua waliyofichiwa katika mambo mazuri
yanayofurahisha macho (huko Akhera). Hayo ndiyo malipo
kwa yale waliokuwa wakiyatenda.

18. Je, aliye mumin ni sawa na aliye mpotofu? Hawawi
sawa. 19. Ama wale ambao wameamini na wakatenda mema
watakuwa na mabustani mazuri. Ndipo pa kufikia kwa
waliyokuwa wakiyatenda. 20. Na ama wale ambao wamefanya
maovu, basi makazi yao ni motoni; kila wakitaka kutoka
humo watarudishwa humo humo. Na wataambiwa: 'Onjeni
adhabu ya moto ambayo mlikuwa mkiiona ni uwongo.
21. Na kwa hakika tutawaonjesha adhabu ya duniani kabla
ya adhabu kubwa, labda (watatubu na) watarejea. 22. Ni nani
dhalimu mkubwa kuliko yule anayekumbushwa Aya za Mola

Wake Mlezi kisha akazikataa? Hakika Sisi ni Wenye kulipiza kisasi dhidi ya wafanya mabaya.

23. Hakika tulimpa Musa Kitabu basi usiwe na shaka kuwa kitakufikia.[13] Na tukakifanya ni mwongozo kwa wana wa Israel. 24 Na tukawafanya miongoni mwao viongizi wanaoongoza kwa amri Yetu, kwa vile walivyosubiri na wakawa na yakini na Ishara Zetu. 25 Hakika Mola Wako Mlezi Ndiye atakayefafanua baina yao Siku ya Kiyama katika yale waliyotofautiana. 26 Je, haikuwabainikia, ni vizazi vingapi tuliviangamiza kabla yao, nao wanapita katika maskani zao? Hakika katika hayo kuna ishara. Kwa nini hawasikii?

27. Hivi hawaoni kwamba tunayapeleka maji kwenye ardhi kame, kisha kwayo tunaitoa mimea wanayokula wanyama wao na wao wenyewe? Je, hawaoni? 28. Na wanasema: Ni lini basi uamuzi huo utafanywa, ikiwa nyinyi mnasema kweli? 29. Sema: Siku ya uamuzi, wale ambao wamekufuru haitafaa imani yao (wakati huo), wala hawatapewa muda. 30. Basi achana nao na ungojee; hakika wao pia wanangojea.

## 33. Surah Al-Ahzab

# MAJESHI WASHIRIKA

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 Ewe Nabii! Mche Mwenyezi Mungu wala usiwatii makafiri na wanafiki. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi, Mwenye

---

13. 'kitakufikia' Wafasiri wametofautiana ju ya marejeo ya kiwakilishi nomino H. Baadhi wamesema inarejea kwa Musa na wengine kitabu. Nimechagua kitabu kutokana na mnasaba wa maana- mfasiri.

hekima. 2 Na fuata uliyofunuliwa wahyi kutoka kwa Mola
Wako. Hakika Mwenyezi Mungu ana habari za mnayoyatenda.
3 Na mtegemee Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu
anatosha kuwa ni wa kutegemewa.

4 Mwenyezi Mungu hakumfanya mwanamume
yeyote kuwa na nyoyo mbili ndani ya mwili wake. Wala
hakuwafanya wake zenu mnaowalinganisha migongo yao na
migongo ya mama zenu, kuwa ni mama zenu kweli. Wala
hakuwafanya watoto wenu wa kulea kuwa ni wana wenu
hasa. Hiyo ni namna mzungumzavyo kwa vinywa vyenu tu.
Na Mwenyezi Mungu anasema kweli, Naye huongoza njia.
5 Waiteni kwa (majina ya) baba zao. Hiyo ndiyo uadilifu zaidi
mbele ya Mwenyezi Mungu. Kama hamuwajui baba zao basi
ni ndugu zenu katika dini na rafiki zenu au watumishi wenu.
Na hapana dhambi juu yenu kwa yale mliyoyafanya kwa
makosa isipokuwa kwa yale yaliyofanywa na nyoyo zenu
kwa kusudi. Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa maghufira,
Mwenye kurehemu.

6. (Mwito) wa Mtume hauna budi upewe kipa umbele juu
ya wito wa waumini wanapoitana wenyewe kwa wenyewe.
Na wake zake ni mama zao. Na baadhi ya ndugu wa
damu wako karibu zaidi (katika mirathi) kuliko wengine;
zaidi ya (ukaribu wao na) waumini wengine na wale
waliohamia Madina. Hii ni kwa mujibu wa katika sharia ya
Mwenyezi Mungu. Isipokuwa mnapotaka kufanya wema
(kwa kuwaandikia wosia) baadhi ya warithi wenu. Haya
yalikwishasajiliwa Kitabuni.

7. Na (kumbuka) tulipochukua ahadi kwa Miume na
kwako wewe, na kwa Nuh (Noah) na Ibrahim na Isa (Yesu)
mwana wa Maria, na tulichukua kwao ahadi madhubuti.

8. Ili (Mwenyezi Mungu) apate kuwasaili hao wakweli juu ya ukweli walioutunza. Na amewandaalia makafiri adhabu chungu.

9. Enyi walioamini! Zikumbukeni neema za Mwenyezi Mungu zilizo juu yenu; pale yalipowafikia majeshi, tukayapelekea kimbunga na majeshi ambayo hamkuyaona kwa macho. Na Mwenyezi Mungu anayaona mnayoyatenda. 10. Walipowajia kutoka nyanda za juu yenu na kutoka chini yenu; na macho (yenu) yakakodoka na nyoyo zikapanda kooni (kwa hofu), na mkawa mnamdhania Mwenyezi Mungu dhana mbali mbali (za upuuzi). 11. Hapo waumini walijaribiwa na wakatikiswa mtikiso mkali.

12. Na (kumbuka) pale waliposema wanafiki na wale ambao wana maradhi katika nyoyo zao: 'Mwenyezi Mungu na Mtume Wake hawakutuahidi isipokuwa mahoka tu'. 13. Na kundi moja miongoni mwao liliposema: 'Enyi watu wa Yathrib! Hapana kukaa hapa nyinyi, Rudini!. Na kundi jingine miongoni mwao likaomba ruhusa kwa Mtume wakisema: 'Hakika nyumba zetu ziko wazi na hatarini. Wala hazikuwa wazi; lakini hawakutaka kingine isipokuwa kukimbia tu. 14. Na lau wangeingiliwa kwa pande zote za mji, kisha wakashawishiwa wafanye hiana, wangefanya, na wasingesita isipokuwa kwa muda mfupi tu. 15. Na kwa hakika walikuwa wamemwahidi Mwenyezi Mungu kabla, kwamba hawatageuza migongo yao kukimbia. Na ahadi ya Mwenyezi Mungu ni yenye kuulizwa. 16. Sema: Hakutawafaa kukimbia ikiwa mnakimbia kifo au kuuawa. Na hata hivyo hamtastareheshwa (baadaye) ila muda mdogo tu. 17. Sema: Ni nani atakayewalinda na Mwenyezi Mungu akiwatakia uovu

au akiwatakia rehema? Wala hawatapata wa kuwalinda wala msaidizi asiyekuwa Mwenyezi Mungu.

18. Kwa hakika Mwenyezi Mungu anawajua miongoni mwenu wanaowazuia (watu) na wanaowaambia ndugu zao: 'Njooni kwetu!' Wala hawaingii vitani ila kidogo
tu. 19. Wanaonesha ubakhili kwenu (wakati wa kugawana nyara). Ikija hofu utawaona wanakutazama huku macho yao yakizunguka kama la mtu anayehudhuriwa na mauti. Lakini hofu inapoondoka huwaudhini kwa ndimi kali, na huwa makbahili kwa kila kheri. Hao hawakuamini, na Mwenyezi Mungu amezipomosha amali zao. Na hilo kwa Mwenyezi
Mungu ni jepesi. 20. Wanadhani yale majeshi washirika hayajaondoka, na kwamba majeshi hayo yataporudi tena watatamani lau wangelikuwa majangwani na mabedui wakiulizia habari zenu tu. Na lau wangekuwa nanyi wasingepigana ila kidogo tu.

21. Hakika nyinyi mmepata mfano mwema kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (siku ya Badr), kwa yule mwenye kumtarajia Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho, na
akamkumbuka Mwenyezi Mungu kwa wingi. 22. Ama waumini walipoyaona majeshi washirika walisema: 'Haya ndiyo yale aliyotuahidi Mwenyezi Mungu na Mtume Wake. Na amesema kweli Mwenyezi Mungu na Mtume Wake'. Na hilo halikuwazidishia wao isipokuwa Imani
zaidi na utiifu. 23. Miongoni mwa waumini wapo wanaume waliotimiza waliyoahidiana na Mwenyezi Mungu. Baadhi yao wamekwisha kufa, na baadhi bado wanangojea; wala
hawakubadilisha ahadi yao hata kidogo. 24. Ndipo Mwenyezi
Mungu awalipe wakweli kwa ukweli wao, na awaadhibu

wanafiki akipenda, au apokee toba yao. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa maghufira, Mwenye kurehemu.

25. Na Mwenyezi Mungu akawarudisha nyuma makafiri na hasira zao, hawakupata faida yeyote. Na Mwenyezi Mungu akawatosheleza waumini wasiingie vitani. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mwenye uwezo. 26. Na akawashusha wale walioyasaidia (majeshi washirika) katika watu wa Kitabu kutoka katika ngome zao; na akatia hofu katika nyoyo zao. Baadhi yao mkawa mnawaua na wengine mnawateka. 27. Na akawarithisha nyinyi ardhi yao na majumba yao na mali zao na ardhi ambayo hamjaikanyaga. Na Mwenyezi Mungu ni Muweza juu ya kila kitu.

28. Ewe Mtume! Waambie wake zako: Ikiwa nyinyi mnataka maisha ya dunia na anasa yake, basi njooni niwape kitoka nyumba na niwaache mwachano mzuri. 29. Na ikiwa mnamtaka Mwenyezi Mungu na Mtume Wake na nyumba ya Akhera, basi Mwenyezi Mungu amewaandalia watenda mema kati yenu, malipo makubwa. 30. Enyi wake wa Mtume! Yeyote kati yenu atakayefanya uchafu wazi wazi, atazidishiwa adhabu mara mbili. Na hilo kwa Mwenyezi Mungu ni jepesi.

31. Na yeyote katika nyinyi atakayemtii Mwenyezi Mungu na Mtume Wake na akatenda wema, tutampa malipo yake mara mbili, na tutamwandalia riziki yenye heshima. 32. Enyi wake wa Mtume! Nyinyi si kama yeyote katika wanawake wengine kama mkimcha Mungu. Basi msilegeze sauti (zenu), asije akaingia tamaa mwenye maradhi moyoni mwake. Na semeni maneno mema.

33. Na kaeni majumbani mwenu wala msijioneshe mapambo yenu kama vile walivyokuwa wakijionesha zama za kipagani zilizopita. Na simamisheni Swala, na toeni

Zaka, na mtiini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake. Hakika Mwenyezi Mungu anataka kuwaondolea nyie uchafu, enyi watu wa nyumba (ya Mtume), na awatakase kabisa.
34. Na zingatieni mnayofundishwa majumbani mwenu katika Aya za Mwenyezi Mungu na hekima. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mpole, Mjuzi wa khabari.

35. Hakika Waislamu wanaume na Waislamu wanawake, na waumini wanaume na waumini wanawake, na wanaume watiifu na wanawake watiifu, na wanaume wakweli na wanawake wakweli, na wanaume wanaosubiri na wanawake wanaosubiri, na wanaume wanyenyekevu na wanawake wanyenyekevu, na wanaume watoao sadaka na wanawake watoao sadaka wa, na wanaume wanaofunga na wanawake wanaofunga, na wanaume wanachunga tupu zao na wanawake wanachunga tupu, na wanaume wanaomkumbuka Mwenyezi Mungu kwa wingi na wanawake wanaomkumbuka Mwenyezi Mungu kwa wingi - Mwenyezi Mungu amewaandalia msamaha na malipo makubwa.
36. Haistahili kwa muumini mwanamume wala muumini mwanamke, baada ya Mwenyezi Mungu na Mtume Wake kwisha amua jambo, kuwa na chaguo katika jambo hilo. Na yeyote mwenye kumwasi Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, basi amepotea upotevu ulio wazi.

37. Na (kumbuka) pale ulipomwambia yule ambaye Mwenyezi Mungu amemneemsha nawe ukampenda: ‘Shikamana na mkeo na mche Mwenyezi Mungu!’, na ukaficha yaliyo moyoni mwako kwa kuogopa watu, mambo ambayo Mwenyezi Mungu aliyataka ayafichue. Na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye haki zaidi ya kumwogopa. Baada ya Zayd alipomalizana naye tulikuozesha wewe, ili wasione vibaya waumini (hapo baadaye) kuoa wake wa

watoto wao wa kulea watakapokuwa wamekwisha malizana nao (ki-ndoa). Na amri ya Mwenyezi Mungu daima ni yenye kutekelezwa. 38. Hakuna dhambi yeyote kwa Nabii kufanya ambalo amewajibishwa na Mwenyezi Mungu kulifanya. Huo ndio mwendo wa Mwenyezi Mungu kwa waliopita zamani, na amri ya Mwenyezi Mungu ni uamuzi uliokwishapitishwa. 39. (Huo ni mwenendo wa wale) wanaofikisha ujumbe wa Mwenyezi Mungu na wakamwogopa Yeye tu, na wala hawamwogopi yeyote isipokuwa Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu pekee atosha kuwa hakimu wa matendo ya watu. 40. Muhammad si baba wa yeyote katika wanaume wenu, bali ni Mtume wa Mwenyezi Mungu na mwisho (muhuri) wa manabii. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu.

41. Enyi walioamini! Mkumbukeni Mwenyezi Mungu kwa wingi. 42. Na mumtakase na mabaya yote (tasbih) asubuhi na jioni. 43. Yeye Ndiye anayewapa huruma, na pia malaika wake, ili awatoe katika dimbwi la giza kuwatia kwenye mwanga. Naye ni Mwingi wa huruma kwa waumini. 44. Maamkuzi yao siku ya kukutana Naye yatakuwa ni ‘Salaam’. Na amewaandalia malipo yenye heshima.

45. Ewe Nabii! Hakika Sisi tumekutuma uwe shahidi na mfikishaji wa habari njema na mbaya. 46. Na mlinganiaji kwa Mwenyezi Mungu kwa idhini Yake, na taa iangazayo. 47. Wape bishara njema waumini ya kwamba wana fadhila kubwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu. 48. Wala usiwatii makafiri na wanafiki na usijali maudhi yao, na mtegemee Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu anatosha kuwa msimamizi wa mambo yako.

49. Enyi walioamini! Mkiwaoa wanawake waumini kisha

mkawaacha kabla ya kuwagusa, basi hamna eda juu yao mtakayoihesabu. Lakini wapeni cha kuwaliwaza na waacheni waende kwa njia nzuri.

50. Ewe Nabii! Hakika Sisi tumekuhalalishia wake zako ambao umewapa mahari yao, na (wajakazi) uliowamiliki kwa mkono wako wa kuume katika aliokupa Mwenyezi Mungu katika vita, na mabinti wa ami zako, na mabinti wa shangazi zako, na mabinti wa wajomba zako na mabinti wa mama zako wadogo waliohama pamoja nawe, na mwanamke Muislamu akijitoa mwenyewe kwa Nabii, ikiwa Nabii amependa amwoe. Ni halali kwako wewe tu, si kwa waumini wengine. Sisi tunajua tuliyowaamuru wao kuhusu wake zao na wale (wajakazi) waliomilikiwa na mikono yao ya kuume. Ili isiwe dhiki juu yako. Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa maghufira, Mwenye kurehemu.

51. Unaweza kuakhirisha zamu ya umtakae katika wao, na umsogezee umtakaye. Na kama ukimtaka yule uliyemtenga si vibaya kwako. Kufanya hivi kutapelekea yaburudike macho yao, wala wasihuzunike, na wawe radhi juu ya kile unachowapa wao wote. Na Mwenyezi Mungu anajua yaliyomo nyoyoni mwenu. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi,
Mpole.
52. Si halali kwako wanawake (wengine) baada (ya hawa) wala kuwabadilisha kwa wake wengine, ijapo uzuri wao utakupendeza. Isipokuwa (mjakazi) uliyemmiliki kwa mkono wako wa kuume. Na Mwenyezi Mungu ni Mchungaji wa kila kitu.

53. Enyi walioamini! Msiingie nyumba za Mtume ila mkipewa ruhusa ya kwenda kula, sio mngojee kiwive. Lakini mtakapoitwa, basi ingieni. Na mkishakula, tawanyikeni msiweke mazungumzo. Hakika hailo humwuudhi Mtume

naye anawastahi nyinyi kuwaambia. Lakini Mwenyezi Mungu hastahi juu ya ukweli. Na mnapowauliza wake zake jambo lolote, basi waulizeni nyuma ya mapazia. Hivyo ndiyo usafi zaidi kwa nyoyo zenu na nyoyo zao. Haiwafalii nyinyi kumuudhi Nabii wala kuwaoa wake zake baada yake kabisa. Hakika hilo ni kubwa mbele ya Mwenyezi Mungu. 54. Mkidhihirisha chochote au mkikificha, hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu.

55. Hapana ubaya kwao (kuonekana na) baba zao, wala watoto wao, wala kaka zao, wala watoto wa kaka zao, wala watoto wa dada zao, wala wanawake wenzao, wala wale (wajakazi) wanomilikiwa na mikono yao ya kuume. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kushuhudia kila kitu.

56. Hakika Mwenyezi Mungu na malaika Wake wanamtumia rehema Mtume. Enyi walioamini! Mwombeeni rehema na mtakieni amani kwa heshima zote. 57. Hakika wale ambao wanamwudhi Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, Mwenyezi Mungu amewalaani duniani na Akhera, na amewaandalia adhabu ya kufedhehesha. 58. Na wale ambao wanawaudhi waumini wanaume na waumini wanawake pasi na wao kufanya kosa lolote, hakika wamebeba dhuluma na dhambi kubwa.

59. Ewe Nabii! Waambie wake zako na binti zako na wake wa waumini, wajiteremshie nguo zao za nje (kufunika vifua). Kufanya hivyo itakuwa rahisi zaidi kwao kutambulika hivyo wasinyanyaswe kijinsia. Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa maghufira, Mwenye kurehemu. 60. Kama wanafiki na wenye maradhi nyoyoni mwao, na wale wanaoeneza umbea mjini hawataacha, basi kwa yakini tutakupambanisha dhidi yao, kisha hawatakaa humo karibu yako ila muda mchache

tu. 61. Wamelaaniwa. Popote wanapopatikana wakamatwe na wauawe bila huruma. 62. Huu ni mwenendo wa Mwenyezi Mungu uliyokuwepo kwa wale waliopita zamani. Wala hutapata mabadiliko katika mwenendo wa Mwenyezi Mungu.

63. Watu wanakuuliza kuhusu Kiyama. Sema: Ujuzi wake uko kwa Mwenyezi Mungu tu. Na nini kitakachokujulisha? Pengine hicho Kiyama kipo karibu. 64. Hakika Mwenyezi Mungu amewaandalia makafiri moto unaowaka. 65. Watadumu humo milele. Hawatapata wa kuwalinda wala wa kuwanusuru. 66. Siku ambayo nyuso zao zitapinduliwa pinduliwa katika Moto. Watasema: Laiti tungemtii Mwenyezi Mungu na tungemtii Mtume! 67. Na watasema: Mola Wetu Mlezi! Hakika sisi tuliwatii mabosi wetu na wakubwa wetu, wakatupoteza njia. 68. Ewe Mola Wetu Mlezi! Wape hao adhabu maradufu, na walaani laana kubwa.

69 .Enyi walioamini! Msiwe kama wale waliomuudhi Musa, lakini Mwenyezi Mungu akamtakasa na waliyoyasema. Naye alikuwa wa kuheshimika mbele ya Mwenyezi Mungu. 70. Enyi walioamini! Mcheni Mwenyezi Mungu na semeni kauli iliyoelekezwa kwenye ukweli. 71. Atawarekebishia matendo yenu na atawaghufiria dhambi zenu. Na mwenye kumtii Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, hakika amefuzu kufuzu kukubwa.

72. Hakika Sisi tulizipendekezea mbingu, ardhi na milima kushika amana, lakini vyote vikakataa kuishika na vikaiogopa, lakini mwanadamu akajitwika. Hakika yeye daima si mwadilifu, mjinga! 73. (Matokeo yake ni) kwamba Mwenyezi Mungu atawaadhibu wanafiki wanaume na wanafiki wanawake na mapagani wanaume na mapagani wanawake; na awapokelee toba waumini wanaume na

waumini wanawake. Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa maghufira, Mwenye kurehemu.

## 34. Sura As-Sabaa

# MJI WA SABA'

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu ambaye ni Vyake vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini. Na sifa njema ni Zake huko Akhera. Naye ni Mwenye hekima, Mwenye habari zote. 2 Anavijua vyote vinavyoingia ardhini na vinavyotoka humo, na vishukavyo kutoka mbinguni na vinavyopanda huko na Yeye ni Mwingi wa huruma, Mwingi wa maghufira.

3. Na waliokufuru wanasema: Hakitatujia Kiyama. Sema: Ndio! Naapa kwa Mola Wangu Mlezi, kitawafikia. Yeye ni Mjuzi wa ghaibu. Hapana kinachofichika Kwake hata chenye uzito wa chembe, si katika mbingu wala katika ardhi, wala kilicho kidogo kuliko hivyo wala kikubwa zaidi; ila vimo katika Kitabu chenye kuweka wazi. 4. Ili awalipe wale walioamini na wakatenda mema. Hao watapata maghufira na riziki yenye heshima. 5. Na wale ambao wanahangaika kuzipinga aya Zetu wakiona watashinda, hao watapata adhabu mbaya yenye uchungu. 6. Na wale ambao wamepewa elimu wanaona kuwa uliyoteremshiwa kutoka kwa Mola Wako Mlezi ni kweli na huongoza kwenye njia ya Mwenye nguvu, Mwenye kusifiwa.

7. Na wale waliokufuru walisema (kwa mzaha): 'Je, tuwajulisheni mtu anayewaambia mtakapochanwa vipande

vipande (na kuoza), ati (mtarudishwa) muwe katika umbo
jipya? [8.] Yeye amemzushia Mwenyezi Mungu hilo au ana
wazimu? Bali wale ambao hawaamini akhera wamo katika
adhabu (ya hakika) na upotofu ulio mbali (na ukweli). [9.] Je,
hawaoni yaliyo mbele yao na yaliyopita nyuma yao mbinguni
na ardhini? Tungependa tungewadididimiza chini ya ardhi. Au
tungewaangushia vipande vya mbingu juu yao. Hakika katika
hayo kuna ishara kwa kila mja anayetaka kutubia.

[10.] Na kwa hakika tulimpa Daud (David) hisani fadhila
kutoka Kwetu. 'Enyi milima, itikieni pamoja naye sifa za
Mwenyezi Mungu, na pia ndege'. Na tukamlainishia chuma.
[11.] (Tukamwamru): ' utengeneze nguo za chuma pana na
kadiria sawa katika kuunganisha ringi za chuma, na fanyeni
vizuri. Hakika mimi ninayaona mnayoyafanya'.

[12.]Na kwa Suleiman (tulimfanyia) upepo (umtii). Safari
yake ya asubuhi ni mwendo wa mwezi mmoja, na safari yake
ya jioni ni mwendo wa mwezi mmoja. Na tukamyeyushia
chemchemi ya shaba. Na katika majini kuna waliofanya kazi
mbele yake kwa idhini ya Mola Wake Mlezi. Na anayejitenga
na amri Yetu miongoni mwao tunamwonjesha adhabu ya
moto unaowaka. [13.] Wakawa wanamfanyia apendalo; kama
mikuki, masanamu, masinia makubwa kama mahodhi, na
masufuria makubwa yaliyokita mahali pake. Fanyeni kazi
enyi watu wa Daud na mshukuru. Ni wachache katika waja
Wangu wanaoshukuru.

[14.] Tulipomwamulia mauti yake, hapana aliyewajulisha
kifo chake isipokuwa mnyoo wa ardhini aliyekula fimbo
yake. (Mwili wake) ulipoanguka, majinni walitambua laiti
kama wangejua ya ghaibu, wasingekaa katika adhabu ya
kudhalilisha.

[15] Hakika ilikuwa ishara kwa watu wa Saba’i katika maskani yao - bustani mbili, kulia na kushoto. Kuleni katika riziki ya Mola Wenu Mlezi na mumshukuru. Mji mzuri na Mola Mwenye maghufira. [16] Lakini wakaaacha (kumshukuru Mola wao). Basi tukawapelekea mafuriko makubwa (kutoka bwawa Ma’rib lililobomoka 120 AD), na tukawabadilishia bustani zao kwa bustani nyingine mbili zenye matunda machungu, ukwaju na miti michache ya kunazi mwitu.
[17] Hayo tuliwalipa hivyo kwa vile walikataa kushukuru. Na sisi kamwe hatuwalipizii (namna hiyo) isipokuwa watovu wa shukrani.

[18] Na baina yao na miji mingine tuliyoibariki, tuliweka miji iliyo kando ya barabara, na tukaweka humo vituo vya safari katika masafa tuliyoyapima: (Tukawaambia): Nendeni humo usiku na mchana kwa amani. [19] Lakini wakalalamika: ‘Ewe Mola Wetu Mlezi! Ungeweka masafa marefu baina ya (vituo vya) safari zetu’. Na wakawa wanazidhulumu nafsi zao. Basi tukawageuza kuwa masimulizi tu (yaliyobaki) na tukawatawanya (wakawa) vipande vipande. Hakika katika hayo, kuna ishara kwa kila mwenye kudumu kuwa na subira, mwingi wa shukrani.

[20.] Na hakika Ibilisi alithibitisha fikra yake juu yao. Na walimfuata isipokuwa kundi la waumini tu. [21.] Naye hakuwa na mamlaka yoyote juu yao, isipokuwa tulitaka tumjaribu ni nani mwenye kuamini Akhera na nani anayeitilia shaka. Na Mola Wako Mlezi ni Mwenye ulinzi juu ya kila kitu.

[22.] Sema: Waiteni hao mnaodai kuwa (ni miungu) badala ya Mwenyezi Mungu. Hawamiliki hata chembe katika mbingu wala ardhini. Wala hawana ubia wowote (na Mwenyezi Mungu) humo. Wala Mwenyezi Mungu hana msaidizi yeyote

miongoni mwao. [23.] Wala hautafaa uombezi mbele Yake (siku hiyo) ila kwa yule aliyempa idhini. Hadi pale hofu itakapoondolewa kwenye nyoyo zao (siku ya Kiyama) ndipo watauliza: ‘Mola wenu Mlezi amepitisha nini’ Watasema: ‘haki na uadilifu’, Naye Ndiye mtukufu mno, Mkubwa kwa jaha.

[24.] Sema: Ni nani anayewapa riziki yenukutoka mbinguni na ardhini? Sema, ni Mwenyezi Mungu! Kwa hakika, aidha Sisi au nyie ndio watakuwa kwenye uongofu, au upotofu ulio wazi. [25.] Sema: Si nyinyi mtaulizwa juu ya dhambi zetu wala sisi tutaulizwa kwa mnayoyafanya nyie. [26.] Sema: Mola Wetu atatukusanya kisha atatuhukumu kwa haki, Naye Ndiye Hakimu, Mjuzi. [27.] Sema: Nionesheni wale mliowaunganisha Naye kuwa washirika wake. Hakuna! Bali Yeye ni Mwenyezi Mungu, Mwenye nguvu, Mwenye hekima.

[28.] Na hatukukutuma wewe (Muhammad) isipokuwa kwa watu wote, uwe mtoaji bishara njema na muonyaji, lakini watu wengi hawajui. [29.] Na wanasema: Lini itatimia ahadi hii? Ikiwa mnasema kweli? [30.] Sema: Miadi yenu ni ya siku ambayo hamtachelewa nayo (hata) kwa saa moja, wala hamtaitangulia.

[31.] Na waliokufuru wanasema: ‘Hatutaiamini hii Qur’an, wala vitabu vilivyokuja kabla yake. Na kama (siku hiyo) ungewaona waovu huku wamesimamishwa mbele ya Mola Wao Mlezi, wakirushiana maneno! Wanyonge wakiwaambia wale wakubwa wao: ‘Lau si nyinyi hakika sisi tungekuwa waumini’. [32.] Wale waliojiona wakubwa watawaambia wanyonge: ‘Kwani sisi ndio tuliowazuia na uongofu baada ya kuwafikieni? Bali nyinyi wenyewe mlikuwa waovu’. [33.] Na wale wanyonge watawaambia wale waliojifanya wakubwa:

Bali zilikuwa njama zenu, usiku na mchana, mlipokuwa
mkituamrisha tumkufuru Mwenyezi Mungu na tumfanyie
washirika. Wataficha majuto yao watakapoiona adhabu.
Na tutaweka minyororo shingoni mwa wale waliokufuru.
Kwani hivi watu wanalipwa isipokuwa yale waliyokuwa
wakiyatenda?.

34. Kamwe hatukumtuma mwonyaji yeyote kwa wakazi
wa mji, isipokuwa wale waliodekezwa kwa anasa (matajiri)
katika mji huo, walisema: ‘Sisi tunayakataa hayo mliyotumwa
nayo’. 35. Na wakasema: ‘Sisi tuna utajiri mkubwa mno na
watoto wengi. Hatuwezi kuadhibiwa sisi!’ 36. Sema: Hakika
Mola Wangu Mlezi humkunjulia riziki amtakaye na huitoa
kwa kipimo (kwa amtakaye), lakini watu wengi hawajui.
37. Na si mali yenu wala watoto wenu watakaowajongeza
Kwetu muwe karibu nasi kwa daraja, isipokuwa aliyeamini
na akatenda mema. Hao basi watapata malipo maradufu kwa
waliyoyafanya, nao watakuwa salama katika maghorofa.
38. Na wale ambao wanajitahidi kuzipinga ishara Zetu,
wakaona watashinda. hao ndio wataletwa mbele ya adhabu.
39. Sema: Hakika Mola Wangu humkunjulia riziki amtakaye
katika waja Wake na humkunjia. Na chochote mtakachotoa
Yeye atarudisha badala yake. Naye ni Bora wa wanaoruzuku.

40. Na siku atakayowakusanya wote, kisha atawaambia
Malaika: ‘Je, hawa walikuwa wakiwaabudu nyie?’
41. Watasema: ‘ Kutakasika Kwako!’ Wewe Ndiwe kipenzi
chetu, sio hao. Bali walikuwa wakiwaabudu majinni; wengi
wao wakiwaamini hao’. 42. Na leo hii hawataweza wengine
kuwaletea nafuu wengine wala kuwadhuru. Na tutawaambia
wale ambao wamedhulumu: Onjeni adhabu ya Moto
mliokuwa mkiona ni uwongo.

43. Na wanaposomewa Aya Zetu zilizo wazi wanasema:
Huyu si lolote ila mtu anayetaka kuwazuia na walivyokuwa
wakiviabudu mababa zenu. Na wakasema: Haya si lolote
isipokuwa ni uongo uliozushwa. Na wale waliokufuru
walisema juu ya ukweli pale ulipowajia: Huu si lolote
isipokuwa uchawi wa wazi’. 44. Lakini (hao mababa)
hatukuwapa vitabu wavisome, wala hatukuwatumia muonyaji
kabla yako. 45. Na waliokuwa kabla yao walikadhibisha
(ukweli), na (hawa wapagani wa kiarabu) hawakupewa
hata sehemu ya kumi ya tulivyowapa wale. (Wale)
wakawakadhibisha mitume Wangu. Ehe, vipi yalivyokuwa
maangamizo yangu kwa wale?

46. Sema: Mimi ninawanasihini jambo moja tu: kwamba
msimame mbele ya Mwenyezi Mungu, (ikiwezekana) wawili
wawili au mmoja mmoja; kisha mfikiri:’Mwenzenu huyu
hana wazimu’. Yeye si mwingine isipokuwa mwonyaji kwenu
kabla ya kuwafikia adhabu kali. 47. Sema: Mimi sijawaomba
malipo. Huu (ujumbe) ni kwa manufaa yenu. Malipo ni kwa
Mwenyezi Mungu. Naye ni shahidi juu ya kila kitu.

48. Sema: Hakika Mola Wangu Mlezi hutupa (vazi la)
ukweli (kuwafunika watumishi wake). Yeye ni Mjuzi mno
wa yaliyofichikana. 49. Sema: Ukweli umefika. Na uwongo
hauwezi kuanzisha (kuumba) wala haurudishi. 50. Sema:
Ikiwa nimepotea basi nimepotea kwa kuidhuru nafsi yangu
tu. Na ikiwa nimeongoka basi ni kwa sababu Mola wangu
amenifunulia wahyi. Hakika Yeye ni Mwenye kusikia aliye
karibu.

51. Na laiti ungewaona watakapobabaika (kwa hofu) Ah,
lakini hapana tena mahali pa kukimbilia, na watakamatwa
kutoka mahali pa karibu. 52. Na watasema: ‘Sasa tumeiamini

'! Lakini wataipata wapi (imani) kutoka huko mahali mbali
(walipo sasa)? 53. Ilhali walikwishaikataa kabisa (Imani)
huko nyuma, wakawa wanarusha (matusi) dhidi ya (suala
la) ghaibu, kutoka sehemu ya mbali (walipokuwepo). 54. Na
watawekewa kizuizi baina yao na wanayoyatamani. Kama
walivyofanyiwa wenzao zamani. Hakika wao walikuwa
katika shaka ya kutia wasiwasi.

35. Surah Al-Fatir

# MUUMBAJI WA MWANZO

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu Muumba wa
mbingu na ardhi aliyewafanya Malaika kuwa wajumbe wenye
mbawa, mbili mbili, tatu tatu na nne nne. Huzidisha katika
kuumba apendavyo. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye
uweza juu ya kila kitu. 2 Rehema ambayo Mwenyezi Mungu
amewapa watu hakuna wa kuizuia na anayoizuia hakuna
mwingine anayeweza kuipeleka mbele badala Yake. Naye ni
Mwenye nguvu, Mwenye hekima.

3 Enyi watu! Kumbukeni neema za Mwenyezi Mungu juu
yenu. Je, yuko muumba mwingine asiyekuwa Mwenyezi
Mungu anayewapa riziki kutoka mbinguni na ardhini?
Hapana Mola ila Yeye. Vipi mnadanganywa kuacha ukweli?
4 Na kama wakikukadhibisha, basi wamekwisha kadhibishwa
Mitume kabla yako. Na mambo yote yatarudishwa kwa
Mwenyezi Mungu.

5. Enyi watu! Hakika ahadi ya Mwenyezi Mungu ni ya

kweli. Basi yasiwadanganye maisha ya dunia, wala Shetani asiwadanganye juu ya Mwenyezi Mungu. [6.] Hakika Shetani ni adui yenu, basi mfanyeni kuwa ni adui. Yeye analiita kundi lake liwe katika watu wa motoni. [7.] Wale ambao wamekufuru watakuwa katika adhabu kali na wale ambao wameamini watapata maghufira na malipo makubwa.

[8.] Je, yule aliyefanyiwa matendo yake mabaya ayaone kuwa mazuri (ni sawa na aliyeeongoka)? Hakika Mwenyezi Mungu humwacha apotee yule anayemtaka na humwongoa amtakaye. Basi usiache roho yako isononeke mno kwa kuwasikitikia. Hakika Mwenyezi Mungu anayajua mno wanayoyafanya.

[9.] Na Mwenyezi Mungu Ndiye anayezituma aina aina za upepo ziyatimue mawingu, Nasi tukayafikisha kwenye nchi iliyokufa, tukaifufua ardhi baada ya kufa kwake. Ndio kama hivyo kufufuliwa. [10.] Mwenye kutaka ukubwa na madaraka (na amtii Mwenyezi Mungu), kwani ukubwa na madaraka vyote ni vya Mwenyezi Mungu. Kwake hupanda maneno masafi. Na matendo mema huyaenzi. Na wanaopanga njama za maovu watapata adhabu kali, na njama za hao hazitazaa matunda. [11.] Na Mwenyezi Mungu amewaumba kutokana na udongo, kisha kwa tone la manii, kisha akawafanya wawili-wawili. Na habebi mimba mwanamke yeyote wala hazai isipokuwa Yeye hujua. Wala hazidishiwi umri mwenye umri mrefu wala hapunguziwi umri wake, ila liko ndani ya maamuzi (Yake). Hakika hayo kwa Mwenyezi Mungu ni mepesi.

[12.] Na bahari mbili haziwi sawa; hii maji yake ni tamu mno, kinywaji chake kinateremka uzuri kooni, na hii ni chumvi, chungu. (Hata hivyo) Kutokana na aina zote

mbili za maji mnakula nyama freshi, laini. Na mnatoa humo mapambo mnayoyavaa. Na unaona vyombo vikikata maji humo, ili mtafute fadhila Yake na mpate kushukuru. 13. Anauingiza usiku katika mchana na anauingiza mchana katika usiku. Na amefanya Jua na Mwezi yatii amri yake; kila kimoja kinaendelea mpaka muda kiliopangiwa. Huyo Ndiye Mwenyezi Mungu, Mola Wenu Mlezi. Ni wake Ufalme. Na wale mnaowaomba badala Yake wao hawamiliki hata utando wa kokwa ya tende! 14. Mkiwaomba, hawasikii maombi yenu. Na hata wakisikia hawezi kuwajibu. Na siku ya Kiyama watakanusha ushirikina wenu. Na hapana yeyote (enyi wanadamu) atakayekuambia (ukweli) kama akuambiavyo Yule anayejua kila kitu.

15. Enyi watu! Nyinyi ndio wenye haja kwa Mwenyezi Mungu; na Mwenyezi Mungu hahitajii chchote wala yeyote, Yeye ndiye mstahiki wa sifa zote njema. 16. Akitaka atawaondolea mbali na alete viumbe wapya. 17. Na hilo kwa Mwenyezi Mungu si gumu. 18. Na mbebaji (wa dhambi) hatabeba mzigo wa mwingine. Na kama aliyeelemewa akiomba achukuliwe mzigo wake, hautachukuliwa hata kidogo, ingawa ni jamaa yake wa karibu. Hakika (wewe Muhammad) unawaonya wale tu wamchao Mola Wao Mlezi ingawaje hawamwoni kwa macho, na wakadumisha kuswali. Na anayejitakasa, basi anajitakasa kwa ajili ya nafsi yake. Na marejeo ni kwa Mwenyezi Mungu.

19. Na asiyeona na anayeona katu hawawi sawa. 20. Wala giza na nuru. 21. Wala kivuli na joto. 22.Na hawawi sawa walio hai na wafu. Hakika Mwenyezi Mungu humsikilizisha amtakaye. Na wewe huwezi kuwasikilizisha walio makaburini. 23. Hukuwa wewe ila ni mwonyaji. 24. Hakika

Sisi tumekutuma kwa ukweli, uwe mtoaji habari njema
na pia mwonyaji. Na hakuna taifa lolote (huko nyuma) ila
lilipata mwonyaji aliyeishi kati yao. 25. Na kama wakisema
wewe mwongo, basi walikwisha wasingizia uwongo wale
waliokuwa kabla yako. Waliwajia Mitume wao kwa dalili
wazi wazi na kwa vitabu vya mahubiri ya kuogofya na kwa
Kitabu chenye mwangaza. 26. Kisha nikawatia nguvuni wale
waliokufuru; na je, vipi ulikuwa (mwisho) wa kuwakataa
kwangu watu hao?

27. Hivi huoni kuwa Mwenyezi Mungu ameteremsha
kutoka mawinguni maji na kwayo tumetoa matunda yenye
rangi mbali mbali. Na katika milima kuna mistari myeupe
na myekundu ya ming'aro mbali mbali ya rangi, na pia
nyeusi mno. 28. Na katika watu na wanyama na wanyama
wa kufugwa pia rangi zao zinatofautiana. Hakika hasa hasa
wanaomwogopa Mwenyezi Mungu katika waja Wake ni
ulama (wenye elimu). Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye
nguvu, Mwingi wa maghufira.

29. Hakika wale wanaosoma Kitabu cha Mwenyezi Mungu,
na wakadumisha kuswali, na wakatoa kwa siri na kwa uwazi
katika vile tulivyowapa, hao wana matarajio ya kupata (faida
ya) biashara ambayo haitafilisika. 30. Kwani (Mwenyezi
Mungu) atawalipa ujira wao kwa ukamilifu, na atawazidishia
kutokana na fadhila Zake. Hakika Yeye ni Mwingi wa
maghufira, Mwenye shukrani. 31. Na Kitabu tulichokufunulia
wewe kwa Wahyi ni cha kweli, kinachothibitisha
yaliyofunuliwa kabla yake. Hakika Mwenyezi Mungu kwa
waja Wake ni Mwenye habari, Mwenye kuona.

32. Kisha tukawarithisha Kitabu wale ambao tumewachagua
katika waja Wetu. (Lakini) Kati yao yupo anayeidhulumu

nafsi yake, na yupo anayefuata njia ya katikati, na yupo anayetangulia mbele katika mambo ya kheri, kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Hiyo ndiyo fadhila kubwa.[14] 33 Mabustani ya milele watayaingia. Humo watavikwa vikuku vya dhahabu, na lulu, na mavazi yao humo ni hariri. 34 Na watasema: Alhamdulillah kwa ambaye ametuondoloea huzuni (zote). Hakika Mola Wetu ni Mwingi wa maghufira, Mwenye shukrani. 35 Ambaye kwa hisani yake, ametuweka katika nyumba ya milele. Humo haitugusi taabu wala kuchoka.

36. Na wale ambao wamekufuru watakuwa na moto wa Jahannam, hawatakumiwa (muda) wakafa, wala hawatapunguziwa adhabu yake. Hivyo ndivyo tunavyomlipa kila mwenye kuzidi ukafiri. 37. Na humo watapiga kelele: 'Mola Wetu Mlezi! Tutoe humu (turudi duniani) tukafanye mema, sio kama yale tuliyokuwa tukiyafanya. (Watajibiwa): Je, hatukuwapa umri (mrefu) wa kutosha kiasi aliyetaka kusikia maonyo angesikia? Aidha, na hata mwonyaji aliwajia? Basi onjeni (ladha ya matendo yenu)! Na madhalimu hawana wa kuwanusuru.

38. Kwa hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa siri za mbingu na ardhi. Hakika Yeye ni Mjuzi wa yaliyomo vifuani. 39. Yeye Ndiye aliyewafanya nyinyi warithi wa ardhi. Yeyote anayemkana Mwenyezi Mungu, basi (madhara ya) kukana kwake yatamrudia mwenyewe. Wala kufuru za wanaokufuru

---

14. Hapa wanazungumziwa wale waliokabidhiwa jukumu la kuendeleza ujumbe wa mitume. Hawa ndiyo kuna wengine hawakuweza kuchukua majukumu ipasavyo- Mfasiri.

haziwazidishii kwa Mola Wao ila kuchukiwa. Na wala kufuru za makafiri haziwazidishii wao isipokuwa hasara.

40. Sema: mnaona hawa washirika wenu mnaowaomba badala ya Mwenyezi Mungu? Haya nionesheni ni sehemu ipi wameiumba katika ardhi? Au wana ushirika wowote katika mbingu? Au tumewapa kitabu wakapata uthibitisho ulio wazi (kuwa wao pia ni miungu) kutoka katika kitabu hicho? Hapana! Lakini watenda maovu huwa hawaahidiani wao kwa wao isipokuwa kiwi tu. 41. Kwa hakika Mwenyezi Mungu huzuia mbingu na ardhi zisiondoke (zisisimame kufanya kazi). Zikiondoka, hakuna yeyote wa kuzizuia isipokuwa Yeye. Hakika Yeye ni Mpole, Mwingi wa maghufira.

42. Na waliapa kwa upeo wa kiapo chao, kwamba akiwafikia mwonyaji (Mtume) bila ya shaka watafuata uogozi wake zaidi kuliko taifa jingine lolote. Lakini alipowajia mwonyaji hakuwazidishia ila kuikimbia zaidi (haki). 43. Kwa sababu tu ya kutakabari kwao duniani na kula njama za uovu. Na njama za uovu hazimdhuru ila mwenyewe. Hivi hawangojei ila yale yale yaliowapata watu wa kale? Ndiyo, na hutapata mabadiliko katika mwenendo wa Mwenyezi Mungu (alivyoamiliana) na watu wa kale (waliomkana). 44. Je, hawakusafiri katika ardhi wakaona vipi ulikuwa mwisho wa waliokuwa kabla yao, ingawaje walikuwa na nguvu zaidi kuliko wao? Na hakuna kitu kiwezacho kumshinda Mwenyezi Mungu mbinguni wala ardhini. Hakika Yeye ni Mwenye kujua, Mwenye kuweza.

45. Na lau Mwenyezi Mungu angekuwa anawaadhibu watu kwa sababu ya wanayoyafanya, asingebakiza juu ya mgongo wa ardhi kiumbe anayeishi. Lakini anawachelewesha hadi ufike muda uliopangwa. Umalizikapo muda wao, basi hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuwaona waja Wake.

# SURA YA YASIN

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 *Yasin*

2 Naapa kwa Qur'an iliyojaa hekima! 3 Hakika wewe bila shaka ni miongoni mwa waliotumwa. 4 Uko juu ya njia iliyonyooka. 5 Hii imeteremshwa kutoka kwa Mwenye nguvu kuu, Mwenye kurehemu. 6 Ili uwaonye watu ambao baba zao hawakupokea maonyo, kwa hiyo wao (watoto) wameendelea kughafilika.

7 Imekwishathibiti kauli juu ya wengi wao (ya adhabu), kwa hiyo hawaamini aslan. 8 Hakika (ni kama) tumeweka minyororo shingoni mwao, ikawafika videvuni, kwa hiyo vichwa vyao viko juu (hawatazami huku na huko kutafuta ukweli).. 9 Na (kana kwamba) tumeweka kizuizi mbele yao na kizuizi nyuma yao na tumewafunika, kwa hiyo hawaoni. 10 Ni sawa kwao ukiwaonya au usiwaonye, hawataamini. 11 Hakika unamuonya (akaonyeka) yule tu anayefuata ujumbe na akamwogopa (Mwenyezi Mungu) Mwingi wa rehema pamoja na kuwa hamwoni. Basi mbashirie huyo maghufira na ujira wa heshima.

12. Hakika Sisi tunawahuisha wafu na tunayaandika matendo waliyoyafanya na athari za matendo yao. Na kila kitu tumekihifadhi katika daftari linaloweka wazi kabisa.

13. Na wapigie mfano, wenyeji wa mji mmoja, wakati walipowajia (Mitume) waliotumwa. 14. Wakati (kwanza)

tulipowatuma wawili wakawakataa. Tukawaongezea nguvu kwa (mwingine) wa tatu, wakawaambia: ‘Sisi tumetumwa kwenu’. [15.] Wakasema: ‘Nyinyi si lolote ila ni watu kama sisi tu. Na Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema, hakuteremsha kitu chochote. Nyinyi mnasema uwongo tu. [16.] Wakasema: Mola Wetu anajua kwamba sisi tumetumwa kwenu. [17.] Wala si juu yetu ila kufikisha waziwazi (ujumbe). [18.] Wakasema: Hakika sisi tumepatwa na mkosi kwa sababu yenu. Kama hamtakoma basi hakika tutawaua kwa kuwapiga mawe na itawafika adhabu chungu kutoka kwetu. [19.] Wakasema: Mkosi wenu mnao wenyewe. Hivi (Mnaona ni mkosi) kuwa mnaonywa? Bali nyinyi ni watu mnaopetuka mipaka.

[20.] Na akaja mtu mbio kutoka upande wa mbali wa mji akawaambia (wana mji): Ndugu zangu! Wafuateni (Mitume) hawa waliotumwa. [21.] Wafuateni hawa ambao hawakuombeni malipo yeyote na wao wenyewe wamepokea mwongozo.

[22.] Na kwa nini nisimwabudu Yule aliyeniumba na ambaye nyinyi mtarejeshwa Kwake? [23.] Je, niwafanye miungu wengine kuwa miungu ya kweli badala Yake? (ambao) Kama Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema, akinitakia madhara, uombezi wa hao hautanifaa kitu, wala hawataniokoa? [24.] Hapo mimi nitakuwa katika upotofu ulio dhahiri kabisa! [25.] Hakika mimi nimemwamini Mola Wenu Mlezi wa nyie wote, basi nisikilizeni. [26.] Ikasemwa: ‘Ingia Peponi’! Akasema: ‘Laiti watu wangu wangejua’!... [27.] Jinsi Mola Wangu alivyonighufiria na akanifanya katika wanaopewa heshima.

[28.] Na hatukuwateremshia dhidi ya watu wake jeshi lolote kutoka mbinguni baada yake, wala hapakuwa na haja kwetu kuteremsha. [29.] Haikuwa zaidi ya Sauti ya mpasuko mmoja

tu, mara wakawa (kama majivu) yaliyozimika, kimyaa.
30. Ah, ni masikitiko yaliyoje juu ya wanadamu! Hakuna
Mtume anayewajia isipokuwa wanamfanyia kejeli!. 31. Je,
hawaoni vizazi vingapi kabla yao tumeviangamiza? Kwamba
wao hawatarejea kwao? 32. Na kwamba hapana viumbe
wowote ila wataletwa kwetu?

33. Na ishara kwao ni ardhi iliyokufa: tunaipa uhai, tukatoa
ndani yake punje ya nafaka ambazo baadhi wanakula.
34. Na tukatengeneza katika ardhi mabustani ya mitende
na mizabibu, na tukafanya chemchemi zibubujike ndani
yake. 35. Ili kwamba waweze kula (na kufurahia) baadhi ya
matunda (ya uumbaji wake). Na si mikono yao iliyofanya
hivi. Hivi hawana shukrani? 36. Kutakata na mabaya ni kwa
ambaye ameumba viwili-viwili katika vitu vyote ambavyo
ardhi inaviotesha, na kwa wao wenyewe pia, na katika vitu
wasivyovijua.

37. Na ishara (nyingine) kwao ni usiku: kutokana na usiku
tunauvua mchana, mara wako gizani!. 38. Na jua linakwenda
kwa mujibu wa ratiba yake hadi ukomo wake. Hivyo ndiyo
maagizo ya Mwenye nguvu kuu, Mwenye kujua. 39. Na
mwezi tumeupimia vituo vya kupitia, mpaka urudi kuwa
kama karara la mnazi la zamani. 40. Si jua lathubutu kuufikia
mwezi, wala usiku ni wenye kuutangulia mchana. Na kila
kimoja kinaogelea katika uzingo wake maalum (orbit).

41. Na ni Ishara kwao kwamba tulizipakia jinsi zao katika
jahazi iliyosheheni. 42. Na tukawaumbia kutoka mfano wa
jahazi hilo yale wanayokwea (hivi leo). 43.Na kama tukipenda
tunawagharikisha; wala hapatakuwa wa kuwasaidia, wala
hawaokolewi.44. Isipokuwa kwa rehema zitokazo Kwetu, na
kuwafurahisha kwa muda.

45. Na wanapoambiwa:’ kuweni na hofu ya kitakachotokea
mnakokwenda, na kitakachotokea mlikotoka…. ili mpate
kuonewa huruma’ (hawasikii). 46. Na haiwafikii Ishara yoyote
katika Ishara za Mola Wao Mlezi ila wao huwa ni wenye
kuipuuza. 47. Na wanapoambiwa: ‘Toeni katika alivyowapa
Mwenyezi Mungu’. Waliokufuru huwaambia walioamini:’
Hivi tumlishe ambaye Mwenyezi Mungu angetaka
angelimlisha Yeye Mwenyewe? Nyinyi hamumo ila katika
upotofu ulio dhahiri’.

48. Na wanasema: ‘Ahadi hii itatokea lini, ikiwa nyinyi
ni wakweli’? 49. Hawangojei ila Sauti ya mpasuko mmoja
tu. Utakaowapiga kwa ghafla huku wao wakiwa katikati
ya ugomvi wakizozana.. 50. Hawataweza kuandika wosia,
wala hawatarejea tena kwa watu wao. 51. Kisha itapulizwa
Parapanda. Mara wataibuka kutoka makaburini wakikimbilia
kwa Mola Wao Mlezi. 52. Watasema: ‘Ole wetu! Nani
aliyetufufua malaloni petu’? (Sauti itajibu) ‘Haya ndiyo
aliyoyaahidi Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema na
wamesema kweli Mitume’. 53. Haitakuwa ila sauti ya
mpasuko mmoja tu, mara wote wameletwa mbele Yetu!

54. Basi leo hakuna yeyote atakayedhulumiwa kitu
chochote, wala hamtalipwa ila yale mliyokuwa mkiyafanda.
55. Hakika watu wa Peponi leo wako na furaha katika kila
wakifanyacho. 56. Wao na wenzi wao wapo chini ya vivuli
wakibembea juu ya viti vya fahari. 57. Watapata humo kila
aina ya matunda na watapata kila wakitakacho. 58. Salaam!
Ndiyo kauli itokayo kwa Mola Mlezi, mwingi wa huruma.

59. Na jitengeni leo, Owah, enyi wenye madhambi!. 60. Je,
sikuwausia, enyi wanadamu! Kuwa msimwabudu Shetani?
Hakika yeye ni adui dhahiri kwenu? 61. Na ya kwamba

mniabudu Mimi tu? Hii ndiyo Njia iliyonyooka? 62. Na
hakika yeye amewapoteza viumbe wengi miongoni mwenu.
Je, hamkuwa mkifahamu? 63. Hii ndiyo Jahannam mliyokuwa
mkiahidiwa. 64.Ingieni humo hii leo kwa vile mlivyokuwa
mkimkana Mwenyezi Mungu. 65. Leo tunaviziba vinywa
vyao, na izungumze Nasi mikono yao, na itoe ushahidi miguu
yao juu ya yale waliyokuwa wakiyachuma.

66. Na lau tungependa tungeyaondolea mbali macho
yao, wakawa wanaiwania njia. Lakini wangeionaje?
67. Na lau tungelitaka tungewageuza sura (wakaganda) hapo
hapo walipo, basi wasingeweza kurandaranda, wala kurudi
watokako. 68. Na yeyote tunayempa umri mrefu, tunamrejesha
nyuma katika umbile Lake. Hivi hawayafahamu haya?
69. Wala hatukumfundisha mashairi, wala haistahiki awe
mshairi. Huu si jambo jingine bali ni ujumbe na Qur'an
inayoweka wazi. 70. Ili itoe onyo kwa aliye hai, na ithibitike
kauli (ya kuadhibiwa) dhidi ya wanaomkana Mwenyezi
Mungu.

71 Hivi Hawaoni kwamba ni sisi ndiyo tuliowaumbia,
miongoni mwa vitu ambavyo mikono Yetu imeviunda,
wanyama wa kufuga, na wao ndiyo wanaowamiliki? 72 Na
tumewafanya wawatii wao. Baadhi yao wako wanaowapanda,
na baadhi yao wanakula. 73 Na wanapata faida nyingine na
pia maziwa.Kwa nini hawashukuru? 74 (Licha ya hivyo),
wamejifanyia miungu wengine badala ya Mwenyezi Mungu,
ati pengine watawasaidia! 75 Hawataweza kuwasaidia
katu! Bali wao ndio watakuwa askari wa kuwaleta miungu
hiyo (mbele ya mahakama Yetu). 76 Basi isikuhuzunishe
kauli yao. Hakika Sisi tunayajua wanayoyaweka siri na
wanayoyatangaza.

77. Hivi haoni mwanadamu kuwa tumemuumba kutokana
na tone la manii, kisha yeye amekuwa mgomvi (Wetu) wa
dhahiri?! 78. Na akatulinganisha Sisi na yeye, huku akijisahau
kuumbwa kwake, akasema: ‘Ni nani huyo atakayeirudishia
uhai mifupa nayo imemung’unyika? 79. Sema: Atairudishia
uhai Yule Yule aliyeibuni mara ya kwanza. Na Yeye ni Mjuzi
wa kila aina ya uumbaji. 80. Yeye ambaye aliwatolea moto
kutokana na mti mbichi, nanyi mkawa mnauwasha. 81. Kwani
aliyeziumba mbingu na ardhi hawezi kuwaumba mfano
wao? Ndiyo! Anaweza. Naye ndiye Muumbaji Mkuu, Mjuzi.
82. Hakika amri Yake anapotaka kitu ni kukiambia tu: ‘Iwe!’
Na huwa. 83. Basi Ametakata na yote machafu Yule ambaye
Mkononi Mwake umo Ufalme wa kila kitu; na Kwake
mtarejeshwa nyote.

## 37. Sura As-Saffat

## MALAIKA WALIOJIPANGA SAFU

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 Naapa kwa (Malaika) wanaojipanga safu kwa safu,
2 Kisha kwa wenye nguvu kubwa ya kuzuia (maovu), 3 Halafu
kwa wenye kutangaza ujumbe (wa Mwenyezi Mungu),
4 Hakika Mungu Wenu bila ya shaka ni Mmoja tu. 5 Mola
wa mbingu na ardhi na vilivyomo kati yake, na ni Mola wa
mashariki zote.

6. Hakika Sisi tumeipamba mbingu ya karibu kwa uzuri
wa nyota. 7. (kwa uzuri) Na kwa kuilinda na kila shetani
mkaidi. 8. Ili wasijitahidi kusikiliza mkusanyiko mtukufu

(wa Malaika). Lakini wafukuzwe huko kutoka kila upande. [9.] Wakisukumwa nyuma, kwa vile wanatumikia adhabu ya kudumu. [10.] Isipokuwa anayenyakua kitu kidogo, na huyo hufuatiwa na kijinga cha moto mkali (kimondo) kinachong'aa (kimwunguze).

[11.]Hebu waulize maoni yao: Jee, ni wao ndiyo vigumu zaidi kuumba au viumbe (wengine) tuliowaumba? Sisi tumewaumba hao kwa udongo unaonata! [12.] Wewe unashangaa, lakini wao wanafanya mzaha. [13.] Na wanapoonywa hawaonyeki. [14.] Na wanapoona miujiza, wanaigeuza kuwa mzaha. [15.] Na husema: Haya (anayotuonesha Muhammad) si lolote ila uchawi ulio dhahiri. [16.] Ati tukishakufa na tukawa udongo na mifupa ndio kweli tutafufuliwa? [17.] Hata wazee wetu wa kale pia? [18.] Sema: Ndiyo! Na hali mkiwa dhalili.

[19.] Huko (kufufuliwa) ni ukelele mmoja tu! Na hapo ndio wataona! [20.] Watasema: Ole wetu! Hii ndiyo (ile) Siku ya Malipo. [21.] Hii ndiyo Siku ya hukumu mliyokuwa mkiikadhibisha. [22.] Wakusanyeni waliodhulumu (roho zao) na wenzao, na hao waliokuwa wakiwaabudu, [23.] Badala ya Mwenyezi Mungu. Waongozeni kunako njia ya Jahannamu! [24.] Na wasimamisheni (hapo)! Hakika hao wataulizwa (kwanza). [25.] Mna nini nyie? Mbona (sasa) hamsaidiani? [26.] Hapana. Siku hiyo watasalimu amri.

[27.] Watageukiana wao kwa wao kuulizana. [28.] Watawaambia (wakubwa wao): Ninyi ndiyo mliokuwa mkitulazimisha kwa vile mlikuwa na madaraka. [29.] Watajibu: 'La hasha! Nyie wenyewe hamkuwa waumini'. [30.] Wala hatukuwa na madaraka yeyote juu yenu. Nyie mlikuwa watu wakaidi na waasi. [31.] Hivyo maneno ya Mola wetu Mlezi juu yetu yamethibiti kuwa kweli. Sisi bila ya shaka tutaonja (adhabu).

32. Tuliwapoteza kwa sababu sisi wenyewe tulikuwa wapotofu.
33. Hakika wao siku hiyo watakuwa pamoja katika adhabu.
34. Hivyo ndivyo tutakavyowafanya waovu. 35. Wao
walipokuwa wakiambiwa: Hapana Mola ila Mwenyezi
Mungu tu, (La ilaha illa Llahu), wakijivuna. 36. Na
wakisema: Hivi tuiache miungu yetu kwa ajili ya huyu
mshairi mwendawazimu? 37. Bali amekuja na ukweli, na
amewathibitsha Mitume (waliokuwa kabla yake). 38. Hakika
nyinyi bila ya shaka mtaionja adhabu chungu. 39. Wala
hamtalipwa ila mliyokuwa mkiyafanya.

40. Isipokuwa waja wa Mwenyezi Mungu waliotakaswa (na
kuabudu vingine). 41. Hao ndio watakaopata riziki maalum.
42. Matunda, nao wataheshimiwa. 43. Katika Bustani za
neema. 44. Wako juu ya viti wameelekeana. 45. Wakipitishiwa
glasi zenye kinywaji safi. 46. Cheupe, kitamu kwa wanywao.
47. Hakina masimbi, wala hawatapoteza akili kutokana nacho.
48. Pembeni mwao watakuwepo wenza wenye staha, wenye
macho makubwa. 49. Kana kwamba wao ni mayai (laini)
yaliyohifadhika.

50. Ndipo watageukiana wao kwa wao wakiulizana.
51. Aseme msemaji miongoni mwao: ‘Kweli, nilikuwa na rafiki
mimi’! 52. Aliyekuwa akiniuliza: ‘Hivi wewe pia ni katika
wale wanaoamini?.... 53. Ati tukishakufa tukawa mchanga na
mifupa, ndio tutahesabiwa?’ 54. (Sauti) Itasema: ‘mngependa
kuchungulia huko?’ 55. Basi atachungulia amwone katikati
ya Jahannam. 56. Aseme, ‘Wallahi! Ulikaribia kuniangamiza
(miye pia)’! 57. Na lau si neema ya Mola Wangu Mlezi bila
ya shaka ningelikuwa miongoni mwa walioletwa (huko)’.
58. Je, sisi hatutakufa tena? 59. Isipokuwa kile kifo chetu cha
kwanza, wala sisi hatutaadhibiwa? 60. Hakika huku, bila ya

shaka, ndiko kufuzu kukubwa. 61. Kwa mfano wa haya na wafanye wafanyao.

62. Je, kukaribishwa hivi ni bora, au mti wa Zaqum? 63. Hakika Sisi tumeufanya mti huo kuwa mtihani kwa watenda maovu. 64. Hakika huo ni mti unaoota katikati ya Moto. 65. Panda za matunda yake (zinatisha) kama vichwa vya mashetani. 66. Hakika hao watakula katika huo, na wajaze matumbo kwa huo. 67. Kisha juu yake wapewe mchanganyiko wa maji ya moto. 68. Kisha marejeo yao bila ya shaka yatakuwa kwenye Jahannam. 69. Hakika waliwakuta baba zao wamepotea. 70. Na wao wakafanya haraka kufuata nyayo zao. 71. Na walikwishapotea kabla yao wengi katika watu wa zamani. 72. Na tuliwapelekea waonyaji miongoni mwao. 73. Basi tazama jinsi ulivyokuwa mwisho wa wale walioonywa. 74. Isipokuwa waja wa Mwenyezi Mungu waliotakaswa.

75. Na hakika Nuh (Noah) alitulilia, na Sisi ni bora wa waitikaji. 76. Na tulimwokoa yeye na familia yake kutokana na mateso makubwa. 77. Na tuliwajaalia kizazi chake ndiyo waliosalia (duniani). 78. Na tukaacha (baraka hizi) kwa waliokuja baadaye. 79. Amani imshukie Nuh kutoka kwa walimwengu wote! 80. Kwa hakika hivyo ndivyo tunavyowalipa watendao mema. 81. Hakika yeye ni katika waja Wetu walio waumini. 82. Kisha tukawagharikisha wale wengine.

83. Na hakika Ibrahim (Abraham) alikuwa katika waliofuata njia ya Nuh. 84. Pale alipomjia Mola Wake kwa moyo uliosalimika. 85. Alipomwambia baba yake na watu wake: ‘Mnaabudu nini?’ 86. ‘Hivi ni miungu wa uongo ndiyo mnataka (kuwaabudu) badala ya Mwenyezi Mungu?’ 87. ‘Ni ipi fikra yenu juu ya Mola wa walimwengu wote?’

88. Kisha akatupia nyota jicho. 89. Akasema: Hakika
mimi ni mgonjwa (moyoni)! 90. Nao wakamwacha,
wakaondoka. 91. Ndipo (Ibrahim) akaiendea miungu yao
kwa siri. 92. Akaiambia: Mbona hamli? Mna nini hata
hamsemi? 93. Kisha akaigeukia kuipiga kwa mkono wa
kuume. 94. Wakamjia upesi upesi. 95. Akawauliza: ‘Hivi
mnaviabudu vitu mnavyovichonga nyie wenyewe?...
96. Na hali Mwenyezi Mungu Ndiye aliyewaumba nyinyi
na hivi mnavyovitengeneza?’ 97. Wakasema: ‘Mjengeeni
tanuri, kisha mtupeni motoni!’ 98. Basi walitaka kumfanyia
hila, lakini tukawafanya wao ndio wa kufedheheka. 99. Na
(Ibrahim) akasema: ‘Hakika mimi ninakwenda kwa Mola
Wangu atakayeniongoza. 100. Ewe Mola Wangu! Nitunukie
(mwana) atakayekuwa miongoni mwa watenda mema’.
101. Basi tukambashiria mwana aliye mpole.

102. Alipofikia makamo ya (kuweza) kufanya kazi nzito
naye, alimwambia: ‘Ewe mwanangu! Hakika mimi nimeota
usingizini kuwa nakuchinja. Basi angalia, waonaje’?
Akasema: ‘Ewe baba yangu! Tenda unavyoamrishwa.
Utanikuta mimi, Inshallah, katika wanaosubiri’. 103.Basi
wote wawili walipojisalimisha (kwa Mwenyezi ungu),
na akamlaza kwa kuweka paji lake la uso (ardhini),
104. Tulimwita: ‘Ewe Ibrahim’! 105.Umekwishatimiza (ya)
ndoto. Kwa hakika hivyo ndivyo tunavyowalipa watendao
mema. 106. Hakika haya ni majaribio yaliyo dhahiri. 107. Na
tukamkomboa kwa chinjo adhimu. 108. Na tukaacha (baraka
hizi) kwa waliokuja baadaye. 109. Amani kwa Ibrahim
110. Hivyo ndivyo tunavyowalipa watendao mazuri. 111. Hakika
yeye ni katika waja Wetu waumini. 112. Na tukambashiria Is-
haq, Nabii miongoni mwa watu wema. 113. Na tukambarikia

yeye na Is-haq. Na miongoni mwa vizazi vyao yuko mwema na mwenye kudhulumu nafsi yake waziwazi.

114. Na kwa hakika tuliwafanyia hisani Musa na Harun. 115. Na tukawaokoa wao na watu wao kutokana na taabu kubwa. 116. Na tukawanusuru; na wakawa wao ndio washindi. 117. Na tukawapa wawili hao Kitabu kilichoweka wazi. 118. Na tukawaongoza kwenye njia iliyonyooka. 119. Na tukawaachia (baraka hizi) kwa waliokuja baadaye. 120. Amani kwa Musa na Harun. 121. Kwa hakika hivyo ndivyo tunavyowalipa watendao mema. 122. Hakika hao ni katika waja Wetu walio waumini.

123. Na hakika Ilyas alikuwa miongoni mwa Mitume. 124. Alipowaambia watu Wake: Mbona hammwogopi Mungu? 125. Mnamwabudu Baal (mungu-jua) na mnamwacha aliye bora ya waumbaji. 126. Mwenyezi Mungu, Mola Wenu na Mola wa wazee wenu wa zamani? 127. Wakamkadhibisha. Na kwa hakika wataitwa (kwenye adhabu). 128. Isipokuwa waja wa Mwenyezi Mungu waliotakaswa. 129. Na tukamwachia (Baraka hizi) kwa waliokuja baadaye. 130. Amani kwa Elias. 131. Kwa hakika hivyo ndivyo tunavyowalipa watendao mema. 132. Hakika yeye ni katika watumishi Wetu walio waumini.

133. Na hakika Lut ni miongoni mwa Mitume. 134. Tulipomwokoa yeye na familia yake yote. 135. Isipokuwa mwanamke mkongwe katika wale waliobakia nyuma. 136. Kisha tukawaangamiza wale wengine. 137. Na hakika nyinyi mnapita kwenye (zilizokuwa) sehemu zao mchana, 138. Na usiku. Basi je! Hamfahamu?

139. Na hakika Yunus (Jonah) ni miongoni mwa Mitume. 140. Alipotoroka kwa jahazi lililosheheni. 141. Wakapiga kura,

akawa katika walioshindwa. 142. Nyangumi akammeza, akiwa
ametenda jambo la kustahiki lawama. 143. Na lau asingekuwa
katika wanaomtakasa sana (Mwenyezi Mungu) 144. Hakika
angekaa tumboni mwake mpaka siku ya kufufuliwa. 145. Kisha
tulimtupa ufukweni pasipo mimea, hali yu mgonjwa. 146. Na
tukamuoteshea mmea wa mmung'unye. 147. Na tulimtuma
kwa watu elfu mia moja (laki moja) au zaidi. 148. Wakaamini,
na tukawaruhusu wafurahie maisha yao kwa muda (maalum).

149. Basi waulize: Ati Mola Wako Ndiye Mwenye watoto
wa kike, na wao wana watoto wa kiume? 150. Au tumewaumba
Malaika kuwa ni wanawake, na wao wakashuhudia?
151. Hapana! Wao kwa uzushi wao wanasema, 152. Mwenyezi
Mungu amezaa mwana! Na hakika hao ni waongo! 153. Je,
amechagua watoto wa kike kuliko wa kiume? 154. Mna nini?
Vipi mnahukumu? 155. Mbona hamwonyeki? 156. Au mnayo
hoja iliyo wazi? 157. Basi leteni kitabu chenu kama mnasema
kweli.

158. Na wakazusha kuwa majinni na Yeye (Allah)
wana udugu (wa damu)! Ilhali majini wanajua fika kuwa
wataletwa (kwenye kuhukumiwa). 159. Ametakasika
Mwenyezi Mungu na yale wanayomsingizia nayo.
160. Isipokuwa waja wa Mwenyezi Mungu waliotakaswa.
161. Hakika nyinyi na mnaowaabudu, 162. Hamuwezi
kuwapoteza (watu wasimwabudu Mwenyezi Mungu).
163. Isipokuwa yule atakayeingia Motoni. 164. (Wale
waliopangwa katika safu husema,) 'Hakuna yeyote kati yetu
ila ana mahali pake maalum' 165. Na hakika bila ya shaka
sisi ndio wajipangao safu. 166. Na hakika sisi ndio wenye
kusabihi.

167. Na hakika wao walikuwa wakisema: 168. Laiti

tungekuwa na ujumbe kutoka kwa watu waliopita, [169.] Bila shaka tungekuwa waja wa Mwenyezi Mungu waliotakaswa. [170.] Lakini waliikataa. Basi watakujajua. [171.] Na bila ya shaka neno Letu lilikwishatangulia kwa waja Wetu waliotumwa. [172.] Ya kuwa wao bila ya shaka ndio watakaonusuriwa. [173.] Na kwamba jeshi Letu ndilo litakaloshinda. [174.] Basi waache kwa muda. [175.] Na watazame tu (watafika wapi), nao wataona (utafika wapi).

[176.] Je, kweli wanataka adhabu yetu ifike haraka? [177.] Itakaposhuka uwanja ulio karibu yao, hiyo itakuwa asubuhi mbaya kwa waliokwishaonywa. [178.] Na waache kwa muda. [179.] Na watazame tu, nao wataona. [180.] Kutakata na mabaya ni kwa Mola Wako Mlezi, Mola Mwenye enzi, na yale wanayombandikia. [181.] Na amani ishuke kwa Mitume wote. [182.] Na sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu, Mola wa walimwengu wote.

38. Sura Swad

# SURA YA SWAD

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

[1] *Swaad*.

Naapa kwa Qur'an yenye mawaidha (kwamba huu ni ukweli). [2] Lakini waliokufuru wamezama katika majivuno na ushindani. [3] Vizazi vingapi tumeviangamiza kabla yao, na mwishowe walikuwa wakipia kelele (kuomba wahurumiwe), lakini wakati wa kuokolewa ulikwishapita.

4 Na walistaajabu kwamba Mwonyaji amewajia miongoni mwao wenyewe. Na waliomkataa wakasema: ‘Huyu ni mchawi, mwongo’. 5 Amewafanya miungu wote kuwa Mungu Mmoja tu? Hakika hili kweli ni jambo la ajabu. 6 Na viongozi wao wakaondoka haraka huku wakiwaambia (wafuasi): ‘Nendeni zenu na endeleeni kushikamana na miungu wenu. Hili ni jambo lililopangwa (dhidi yenu)’. 7 Mbona hatukusikia (mfano wa) haya kutoka kwa wazee wa siku hizi za mwisho (zilizopita)? Huu ni uzushi tu! 8 Ati nini? Yeye ndiye aliyeteremshiwa ujumbe kati yetu?! Lakini wao kwa kweli wana shaka juu ya ujumbe wangu Mimi (mwenyewe)! Bali hawajaonja adhabu Yangu.

9. Au wao (pekee) ndiyo wanazo hazina za huruma ya Mola Wako Mlezi, Mwenye nguvu, Mpaji bila kipimo? 10. Au wao ndiyo wenye ufalme wa mbingu na ardhi na vilivyomo kati yake? Basi na wapande kwa (kutumia) vifaa vyovyote (wafike huko).. 11. Lakini huko, hata vikosi vya jeshi lao la washirika vitashindwa, vitoke mbio! 12. Kabla yao, wengi walikawakataa (Mitume). Watu wa Nuh (Noah) na A’ad na Firauni (Pharaoh), mwenye (majengo kama) vigingi (Pyramids). 13. Na Thamud na watu wa Lut (Lot) na watu wa Porini. Hayo ndiyo makundi washirika. 14. Wote waliwakataa Mitume; wakastahili adhabu Yangu. 15. Na hawa (wa sasa) hawangojei ila sauti ya mpasuko mmoja tu (utapokuja) hauna kuchelewa. 16. Na wao husema: ‘Mola Wetu Tuletee upesi adhabu yetu (hata) kabla ya Siku ya Hisabu’.

17.Subiri kwa wayasemayo, Na mkumbuke mja Wetu Daud (David). Mwenye nguvu (ya imani). Hakika yeye alikuwa mwingi wa kurejea kwa Mwenyezi Mungu. 18. Ni Sisi ndiyo tuliyoifanya milima ikariri kwa sauti pamoja naye sifa za

Mwenyezi Mungu, jioni na jua lichomozapo. 19. Na pia ndege waliokusanywa makundi; wote walikuwa wanyenyekevu kwake. 20. Na tukautia nguvu ufalme wake. Na tukampa hekima na (uwezo wa) kutoa maamuzi sahihi.

21. Na hivi imekufikia habari ya wagomvi walioparamia ukuta wa chumba binafsi (cha Nabii Daud). 22. Walipomuingilia Daud akaingiwa na hofu kwa ajili yao. Wakamwambia: Usiogope! Sisi ni wagomvi wawili, mmoja wetu amemdhulumu mwenziwe. Basi tuhukumie kwa haki, wala usipendelee. Na utuongoze kwenye njia iliyo sawa.

23. Huyu ni kaka yangu. Yeye ana kondoo majike tisini na tisa, na mimi nina kondoo jike moja. Akaniambia nimpe wangu amfuge (nami sikupenda, lakini) akanishinda kwa maneno (matamu). 24. (Daud) Akasema: Kwa kweli kaka yako amekuonea kwa kumtaka kondoo wako mmoja kuongezea kwenye kondoo wake. Na hakika washirika wengi hudhulumiana wao kwa wao. Isipokuwa walioamini na wakatenda mema. Na hao ni wachache. Daud akaona kuwa tumempa mtihani (na ameshindwa). Basi akamwomba maghufira Mola Wake Mlezi na akaanguka kunyenyekea na kutubia. 25. Ndipo tukamghufiria kwa hayo. Naye kwa hakika ana hadhi ya kuwa karibu Yetu, na ana marejeo mazuri.[15]

26. Ewe Daud! Hakika Sisi tumekufanya uwe naibu (wetu)

---

15. Nini kosa la Daud? Kwa watu wa kawaida Daud amehukumu haki. Lakini kwa watu wa karibu zaidi ya Mola, kule kujiona kwamba hukumu hiyo imetoka kwake bila kumnasibishia Mwenyezi Mungu, ni kosa. Ndipo Daud akatubu baada ya kuzinduka: 'Hasanatul Abraari, Sayyiaatul-Muqarrabeen' Huenda yaliyo mazuri kwa watu wema, yakawa mabaya kwa walio karibu zaidi kwa Mwenyezi Mungu. Na hao waliomjia si watu, bali ni Malaika wa kumpa mtihani!-mfasiri).

hapa duniani. Basi wahukumu watu kwa ukweli na uadilifu, wala usifuate matamanio, yakakupoteza Njia ya Mwenyezi Mungu. Hakika wanaopotea Njia ya Mwenyezi Mungu, watapata adhabu kali kwa sababu ya kusahau kwao Siku ya kuwajibika.

27. Na hatukuziumba mbingu na ardhi na vilivyomo kati yake pasi na lengo lolote. Hiyo ni dhana ya wanaomkana Mwenyezi Mungu. Ole wao walio kufuru juu ya Moto. 28. Hivi tuwachukulie wale walioamini na wakafanya mazuri, kuwa kama waharibifu duniani? Au tuwachukulie wanaomcha Mwenyezi Mungu kuwa kama waovu? 29. Hiki ni Kitabu, tumekuteremshia wewe, kimebarikiwa, ili wazizingatie Aya zake, na wawaidhike wenye akili.

30. Na tulimtunukia Daud (mtoto) Suleiman (Solomon), aliyekuwa mtu mwema sana katika utumishi wetu, daima anarejea kwetu kuungama. 31. (Kumbuka) pale alasiri moja alipohudhuria maonesho ya farasi, wakimya wasimamapo, wepesi wakimbiapo. 32. (Baadaye) akasema (kwa masikitiko): ‘kwa kweli nimependelea zaidi vitu vizuri juu ya kumtaja na kumsifu Mola wangu Mlezi, hadi jua likazama kwenye pazia (la usiku)!’ 33. (Asubuhi akaamuru): ‘Nirudishieni hao’! Akaanza kuwapiga miguu na shingo (kwa upanga wake, kama alama ya kutubu).[16]

---

16. (Haya ndiyo maelezo niliyochagua miongoni mwa tafsiri nyingi za aya hii. Ni maelezo yanaoendana karibu sana na lafudhi la Aya. Kwamba Suleiman alitubia kuona kwamba alipoteza muda mrefu katika uraibu, kuliko kumdhukuru Mwenyezi Mungu: jambo halali kwa watu wa kawaida, lakini si hivyo kwa Mitume walio karibu zaidi kwa Allah.

Wafasiri wengine wanaona maana ya Aya hizi ni kuwa Sulaiman,

[34.] Na hakika tulimtia Suleiman katika mtihani: tukauweka mwili usio na uhai juu ya kiti chake cha ufalme. Lakini akarejea (Kwetu) kwa kutubu.[17] [35] Akasema: Mola Wangu Mlezi! Nisamehe. Na unipe ufalme, asiupate yeyote baada yangu. Hakika Wewe Ndiye Mwingi wa upaji. [36] Basi tukaufanya upepo umtumikie, ukienda pole pole kwa amri yake, popote alipotaka kufika. [37] Na mashetani pia, kila ajengae na apigaye mbizi (kutoa lulu). [38] Na wengine wafungwao pamoja kwenye minyororo (wanapoasi). [39] Hiki ndiyo kipawa chetu kwako. Ukitaka toa (uwape wengine) au zuia. Hakuna swali lolote utaulizwa. [40] Naye kwa hakika ana hadhi ya kuwa karibu (Yetu), na mahali pazuri pa kurejea.

[41.] Na mtaje kwa wema mja Wetu Ayub (Job). Pale alipomlilia Mola wake Mlezi: 'Kwa hakika Shetani amenigusa na kuniachia mavune na mateso' (niondolee). [42.] (Amri ikaja): Ipige ardhi kwa mguu wako! Haya maji baridi ya kuoga na (vile vile) ya kunywa. [43.] Na tukamrudishia familia yake (iliyomtoroka alipougua) na tukazidisha idadi yao; hii ikiwa ni huruma kutoka Kwetu, na ukumbusho kwa watu wenye

---

ingawaje alikuwa mpenda farasi kupita kiasi, hata hivyo mapenzi hayo hayakuwa ya uraibu na unazi, bali alimwona Mwenyezi Mungu kupitia uzuri wa vitu. Mapenzi hayo hayakumzuia kutimiza wajibu wake kwa Mola wake - Mfasiri)

17. Uff. Aya hii pia ni mahali pa tofauti baina ya wafasiri. Wengine wamesema hii inaishiria ile aya ya 14 Surat Saba'. Lakini maelezo yaliyonikinaisha mimi binafsi ni yale ya kuwa aya hii ni majazi (allegory) ya kuwa ufalme wa hapa duniani, hata ungekuwa adhimu namna gani, haudumu, kwani huo ni kama kiwiliwili kisicho na roho. Mtu mwenye hekima hatautegemea ufalme huo na badala yake atarejea kwa Mwenyezi Mungu kumshukuru na kumwomba toba- mfasiri)

kufahamu. 44. (Akaambiwa) Shika kitita cha ukoka mkononi mwako, kisha ndio upige kwacho, wala usivunje kiapo. Hakika tulimkuta Ayub kuwa mwenye subira. Mtu mwema katika utumishi wetu, daima hurejea kwetu kuungama.[18]

45. Na wakumbuke waja Wetu, Ibrahim (Abraham) na Ishaq (Isaac) na Ya'qub (Jacob) waliokuwa na nguvu na busara. 46. Hakika tumewachagua wao kwa jambo maalum: kuhubiri (ujumbe wa) nyumba (ya Akhera). 47. Na hakika wao mbele Yetu ni miongoni mwa walioteuliwa, walio bora kabisa. 48. Na mtaje kwa wema Ismail na Alyasaa (Elisha) na Dhulkifl, na wote hao ni katika walio bora.

49. Haya ni maonyo! Hakika wanaomcha Mwenyezi Mungu wana mahala pazuri pa kurejea. 50. Bustani za milele ambazo milango yake daima iko wazi (kwao). 51. Humo wataegemea matakia, wawe wanaagiza humo matunda ya aina aina na vinywaji. 52. Na kando yao watakuwepo wanawake wenye staha ya macho, (wenzi) wa rika lao. 53. Haya ndiyo mliyoahidiwa kwa Siku ya Hesabu. 54. Hakika hii ndiyo riziki yetu (kwenu) isiyomalizika.

55. Ndio hivi! Lakini kwa wale watenda maovu kupindukia bila ya shaka watafikia mahali pabaya pa

---

18. Uff. Ingawa Ayub alikuwa mvumilivu mno wakati wa mtihani wa maradhi mabaya, ila mkewe hakuwa hivyo. Alimtaka mumewe amkane Mwenyezi Mungu kutokana na mateso aliyompa. Ayub akamjibu, 'hivi anapotupa raha tufurahie na akitujaribu tumchukie?' Yaelekea mkewe aliendelea kumkera kwa maneno hadi akakasirika na kuapa kumchapa. Lakini hatimaye akakumbuka yeye ni mtumishi wa MMungu na haifai kukasirika. Ndiyo hapa anaambiwa kamata kitita cha ukoka tu kiwe ishara ya fimbo uliyoapa kumpigia mkeo, mchape kwa ukoka huo tu, na hivyo hutakuwa umevunja kiapo chako – Mfasiri)

kurejea. 56. Jahannam! Wataingia humo. Malazi mabaya mno
kupindukia. 57. Ndio hivi! Basi na wayaonje maji ya moto
mno, na usaha. 58. Na adhabu nyingine za namna hii, mfano
wake. 59. Hili hapa kundi (jingine) linalosukumana kuingia
pamoja nanyi. Hakuna (maneno ya) kuwakaribisha. Kwa vile
wao wanaingia Motoni. 60. (Wafuasi) Watasema (kuwaambia
viongozi): 'Hata nyie, hakuna makaribisho kwenu! Nyinyi
ndio mliotusababishia haya! Napo ni pahala paovu kabisa'!
61. Waseme: Mola Wetu Mlezi! Aliyetusababishia haya
mzidishie adhabu mara mbili Motoni. 62. Watasema: Mbona
hatuwaoni wale watu ambao tulikuwa tukiwahesabu ni katika
waovu? 63. Je, tulikosea kwa kuwafanyia kejeli au ni macho
yetu yameshindwa kuwaona hapa? 64. Hakika hivyo kwa
kweli ndivyo itavyokuwa kulaumiana kwa watu wa Motoni..

65. Sema: Hakika mimi ni mwonyaji tu; na hapana Mola
ila Mwenyezi Mungu Mmoja, Mwenye kulazimisha,
Asiyeshindika. 66. Mola wa mbingu na ardhi na vilivyomo kati
yake, Mwenye nguvu, Mwingi wa maghufira. 67. Sema: Hii
ni habari kubwa kabisa. 68. Nyinyi mnaipuuza. 69. Sikuwa na
elimu juu ya Wakuu wa juu zaidi walipokuwa wakijadiliana.
70. Sikupewa Wahyi isipokuwa kwamba mimi ni mwonyaji
tu wa wazi.

71. Kumbuka pale Mola Wako alipowaambia Malaika:
Hakika Mimi nitaumba mtu kutokana na udongo. 72. Na
nitakapomkamilisha na nikampulizia roho inayotokana
Nami, basi mwangukieni kwa kumtii. 73. Wakasujudu
Malaika wote pamoja. 74. Isipokuwa Ibilisi alijivuna na
akawa katika makafiri. 75. Akasema: Ewe Iblisi! Kipi
kilichokuzuia kumsujudia yule niliyemuumba kwa Mikono
Yangu? Je! Umejiona mkubwa, au umekuwa (kweli) katika

wakuu? 76. Akasema: Mimi ni bora kuliko yeye. Umeniumba
kwa moto, naye umemuumba kwa udongo. 77. Mwenyezi
Mungu akasema: Ondoka hapa! Kwani wewe umefukuzwa
na kulaaniwa. 78. Na hakika laana Yangu itakuwa juu yako
mpaka Siku ya Malipo.

79. Akasema: Mola Wangu Mlezi! Nipe muda mpaka siku
viumbe watakapofufuliwa. 80. Akasema: Haya. Wewe ni
katika waliopewa muda, 81. Mpaka siku ya wakati maalumu.
82. Akasema: Naapa kwa utukufu Wako, bila ya shaka
nitawapoteza wote. 83. Isipokuwa wale waja Wako miongoni
mwao waliosafishwa. 84. Akasema: Ni haki! Na haki ndiyo
niisemayo: 85. Kwa hakika nitaijaza Jahannamu kwa wewe na
wale wote wenye kukufuata, kila mmoja wao!

86. Sema: Siwaombi ujira juu ya haya, wala mimi si katika
wanaojifanya. 87. Hayakuwa haya ila ni mawaidha kwa
walimwengu wote. 88. Na bila ya shaka mtajua habari zake
baada ya muda.

## 39. Sura Azzumar

## SURA YA UMATI

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye urehemu.

1 Uteremshaji wa Kitabu hiki umetoka kwa Mwenyezi Mungu
(mwenyewe), Mwenye nguvu, Mwenye hekima. 2 Hakika
tumekuteremshia Kitabu hiki kwa kweli. Hivyo mwabudu
Mwenyezi Mungu ukimsafia Yeye Dini. 3 Hivi siyo kwa
Mwenyezi Mungu pekee ndipo ibada ya kweli ielekezwe?
Na wale wanaowafanya wengine kuwa wa kuwalinda

badala Yake, (husema): Sisi hatuwaabudu ila wapate
kutujongeza kwa daraja tuwe karibu ya Mwenyezi Mungu.
Hakika Mwenyezi Mungu atahukumu baina yao katika
wanayotofautiana. Hakika Mwenyezi Mungu hamwongozi
aliye mwongo, Kafiri.

4 Lau kama Mwenyezi Mungu angetaka kujifanyia
mwana, basi bila ya shaka angemchagua amtakaye miongoni
mwa aliowaumba. Ametakasika na hayo! Yeye ni Mmoja,
Mwenye nguvu za kutopingika. 5 Ameumba mbingu na ardhi
kwa (vipimo vya) ukweli. Ameufanya usiku upishane na
mchana na mchana upishane na usiku, Na akalifanya jua na
mwezi kutii (mfumo alioviwekea), kila kimoja kinafuata njia
yake hadi muda uliowekwa. Hivi kweli Huyo sio Mwenye
Nguvu Kuu, anayesamehe tena na tena?

6. Amewaumba nyote kutokana na nafsi moja. Tena
akaumba kutokana na nafsi hiyo mwenzi wake. Na
amewateremshia wanyama-mifugo wanane wa jozi mbili
mbili. Anawatia maumbile ndani ya mifuko ya uzazi ya
mama zenu, umbo baada ya umbo, katika mapazia matatu ya
giza. Huyo Ndiye Mwenyezi Mungu Mola Wenu Mlezi, ni
wake Ufalme wa vitu vyote. Hapana Mola isipokuwa Yeye.
Vipi ninyi mnageuzwa (na ukweli huu)?

7. Mkikana (kuwepo Kwake), basi Mwenyezi Mungu
hahitajii chochote kutoka kwenu. Wala haridhii utovu wa
shukrani kwa waja Wake. Na mkishukuru atawaridhia. Wala
hatabeba mtu yeyote dhambi za (mtu) mwingine. Kisha
marejeo yenu ni kwa Mola Wenu Mlezi. Kisha atawaambia
mliyokuwa mkiyafanya. Hakika Yeye ni Mjuzi wa yaliyomo
katika nyoyo.

8. Na pindi mwanadamu anapofikwa na matatizo humlilia

Mola wake Mlezi akielekea Kwake kwa dhati. Lakini
akimzawadia neema kutoka Kwake, husahau vile alivyokuwa
akimlilia hapo nyuma. Na tena humfanyia Mwenyezi Mungu
washirika, ili awapoteze wengine na njia Yake (Mwenyezi
Mungu). Sema: Furahia kufuru yako kwa muda mchache;
kwani hakika wewe ni miongoni mwa watu wa Motoni. 9. Je,
hivi afanyaye ibada kwa bidii nyakati za usiku, akisujudi na
kusimama wima, akitahadhari juu ya Akhera, na akitarajia
huruma za Mola Wake Mlezi (na asiyefanya hivyo), sema, Je,
wanalingana? Wale ambao wanajua na wale ambao hawajui?
Hakika wanaokubali maonyo ni wale wenye ufahamu pekee.

10. Sema: Enyi waja wangu walioamini! Mcheni Mola
Wenu Mlezi. Wale ambao wamefanya wema katika dunia
hii watapata wema. Na ardhi ya Mwenyezi Mungu ni pana.
Hakika wenye subira watapewa ujira wao bila kipimo.

11. Sema: Hakika mimi nimeamrishwa nimwabudu
Mwenyezi Mungu kwa kumsafia Yeye tu Dini. 12. Na
nimeamrishwa niwe wa mwanzo wa Waislamu. 13. Sema:
Hakika mimi ninahofia adhabu ya Siku Kubwa nikimwasi
Mola Wangu. 14. Sema: Ni Allah tu (Mwenyezi Mungu)
ninamwabudu kwa kumsafia Yeye Dini yangu. 15. Basi nyinyi
abuduni mpendacho badala Yake. Sema: Hakika waliopata
hasara ni wale waliozitia roho zao na jamaa zao katika hasara
hapo Siku ya Kiyama. Ah! Hiyo ndiyo hasara iliyo dhahiri
16. Watakuwa na matabaka ya moto juu yao, na chini yao
pia watakuwa na matabaka mengine (ya moto). Kwa hayo
Mwenyezi Mungu anawaasa waja Wake. Enyi waja Wangu!
Nicheni Mimi.

17. Na wale waliojiepusha na shetani na kumwabudu, na
wakarejea kwa Mwenyezi Mungu, watapata bishara njema.

Basi wabashirie waja Wangu. 18. Ambao husikiliza maneno, wakafuata mazuri yake zaidi. Hao ndio aliowaongoza Mwenyezi Mungu, na hao ndio wenye ufahamu.

19. Je, yule ambaye hukumu ya adhabu imeshapitishwa juu yake,( ni sawa na anayeepuka maovu?) Je, wewe unaweza kumwokoa aliyemo Motoni? 20. Lakini waliomcha Mola Wao Mlezi watapata ghorofa zilizojengwa juu ya ghorofa; chini yake hupita mito. Ndiyo ahadi ya Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu havunji ahadi Yake.

21. Je, Huoni kwamba Mwenyezi Mungu ameteremsha maji kutoka mawinguni. Kisha akayapitisha yakawa chemchemi katika ardhi? Kisha kwa maji hayo akatoa mimea yenye rangi mbali mbali. Kisha akaifanya inyauke ukaiona imekuwa rangi ya manjano, kisha akaifanya iwe mikavu iliyovunjikavunjika. Bila ya shaka katika hayo kuna ukumbusho kwa wenye akili. 22. Je, yule ambaye Mwenyezi Mungu amekikunjua kifua chake kwa Uislamu, na akawa kwenye nuru itokayo kwa Mola Wake Mlezi, (Ni sawa na mwenye moyo mgumu?). Basi ole wao wenye nyoyo ngumu zisizomkumbuka Mwenyezi Mungu! Hao wamo katika upotofu wa dhahiri.

23. Mwenyezi Mungu ameteremsha ujumbe mzuri kabisa, kitabu chenye (aya) mfululizo, zenye kujirudia-rudia. Husisimka kwacho ngozi za wenye kumhofu Mola Wao Mlezi. Kisha ngozi zao na nyoyo zao hulainika kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu. Huo ndio uongofu wa Mwenyezi Mungu, ambao kwao humwongoza amtakaye. Na ambaye Mwenyezi Mungu amemwacha apotee, basi hana wa kumwongoza.

24. Je, Ajilindae kwa uso wake (yeye mwenyewe) na kilele cha adhabu Siku ya Kiyama (ni sawa na asiye)? Na wafanyao

maovu wataambiwa (siku hiyo): Onjeni hayo mliyokuwa
mkiyachuma! 25. Waliokuwa kabla yao (pia) walikataa
(ujumbe), na ikawajia adhabu kutoka upande wasioufikiria.
26. Basi Mwenyezi Mungu akawaonjesha fedheha katika uhai
wa duniani. Na bila ya shaka adhabu ya Akhera ni kubwa
zaidi; laiti wangelijua!

27. Na hakika tumewapigia watu mifano ya kila aina
katika hii Qur'an ili wapate kuonyeka. 28. Qur'an kwa lugha
ya Kiarabu isiyo na upogo, ili huenda wakamcha Mungu.
29. Mwenyezi Mungu amepiga mfano wa mtu anayewatumikia
(mabwana) washirika wanaogombana. Na mtu mwingine
anayemtumikia mtu mmoja pekee, je, wawili hao wako
sawa ukiwafananisha? Alhamdu lillahi! Lakini wengi wao
hawajui. 30. Kwa hakika wewe utakufa, na wao watakufa.
31. Kisha nyinyi Siku ya Kiyama hakika mtagombana mbele
ya Mola Wenu Mlezi.

32 Basi ni nani dhalimu zaidi kuliko yule anayemzulia
uwongo Mwenyezi Mungu, na kuukataa ukweli pale
ulipomjia? Je, siyo katika Jahannamu ndiyo makazi ya
makafiri? 33 Na aliyeleta ukweli na akauthibitisha, hao
ndio wachamungu. 34 Watapata watakachotaka kwa Mola
Wao Mlezi. Hayo ndiyo malipo ya watendao mema. 35 Ili
Mwenyezi Mungu awafutie (hata) uovu wa kupindukia
walioufanya, na awalipe ujira wao kwa wema zaidi ya
waliokuwa wakiufanya.

36. Je, Mwenyezi Mungu si wa kumtoshea mja Wake? Na
ati wanakutishia kwa (miungu) wengine wasiokuwa Yeye!
Na aliyehukumiwa na Mwenyezi Mungu kupotea hana wa
kumwongoza. 37. Na anayeongozwa na Mwenyezi Mungu

hana wa kumpoteza. Je, Mwenyezi Mungu si Mwenye nguvu, mwenye uwezo wa kulipiza?

[38.] Na ukiwauliza: Ni nani aliyeziumba mbingu na ardhi? Bila ya shaka watasema: Mwenyezi Mungu. Sema: Je, Mnawaonaje wale mnaowaomba badala ya Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu akitaka kunidhuru, wao wanaweza kuniondolea madhara yatokayo Kwake? Au akitaka kunirehemu, je, wao wanaweza kuzuia rehema Yake? Sema: Mwenyezi Mungu ananitosha. Kwake wategemee wanaotegemea. [39.] Sema: Enyi watu wangu! Fanyeni muwezavyo, mimi pia nafanya. Basi punde mtajua, [40.] Ni nani itakayemfikia adhabu ya kumfedhehesha, na itakayemshukia adhabu ya kuendelea. [41.] Hakika Sisi tumekuteremshia Kitabu kwa ajili ya watu wote kwa Haki. Basi mwenye kuongoka ni kwa (faida ya) nafsi yake, na mwenye kupotea bila ya shaka anapotea kwa (hasara ya) nafsi yake. Na wewe si msimamizi juu yao.

[42.] Mwenyezi Mungu ndiye ambaye huzifisha roho ziwapo usingizini, na (pia) ambazo hazikufa wakati zikiwa usingizini. Huzizuia zile zilizohukumiwa kufa (zisirudi kwenye uhai) na huziachia zile nyingine (zirudi kwenye mwili) mpaka ufike wakati uliowekwa. Hakika katika hayo bila ya shaka zipo Ishara kwa watu wanaofikiri.

[43.] Au ndio wamejifanyia waombezi badala ya Mwenyezi Mungu? Sema: hata kama hawana mamlaka yeyote wala hawatambui chochote? [44.] Sema: (Mamlaka ya kutoa ruhusa ya) Uombezi wowote anayo Mwenyezi Mungu. Ni Wake ufalme wa mbingu na ardhi. Kisha mtarejeshwa Kwake. [45.] Na pindi anapotajwa Mwenyezi Mungu pekee, nyoyo za wale wasioamini Akhera hujaa chuki na karaha. Ama

watajwapo (waungu) wengine asiye Yeye, hapo hujawa na
furaha. 46. Sema: Ewe Mola wangu! Mwumba wa mbingu
na ardhi, Mjuzi wa yasiyoonekana na yanayoonekana,
Wewe utahukumu baina ya waja Wako katika hayo mambo
waliyokuwa wakitofautiana. 47. Na hata kama wafanya maovu
wangemiliki vyote viliomo duniani na vingine zaidi ya hivyo,
bila ya shaka wangetaka kuvitoa ili wajikomboe na maumivu
ya adhabu ya Siku ya Kiyama. Na yatawadhihirikia kutoka
kwa Mwenyezi Mungu mambo wasiyokuwa wakiyatarajia.
48. Na utawadhihirikia ubaya wa waliyoyachuma, na
yatawazunguka waliyokuwa wakiyafanyia mzaha.

49. Na pindi matatizo yanapomfika mwanadamu hutulilia
sisi! Lakini tunapomzawadia neema zitokazo Kwetu, husema:
Nimepewa hivi kwa sababu ya elimu yangu. Sio! Huo ni
mtihani, lakini wengi wao hawajui 50. Walikwishayasema
hivyo hivyo wale waliokuwa kabla yao. Lakini hayakuwafaa
chochote waliyokuwa wakiyachuma. 51. Basi ukawasibu uovu
wa waliyoyachuma. Na wale wafanyao maovu miongoni
mwa hawa, (pia) utawasibu ubaya wa waliyoyachuma. Nao
si wenye kushinda 52. Je, hawajui kwamba Mwenyezi Mungu
humkunjulia riziki amtakaye na humkunjia (amtakaye)?
Hakika katika haya bila ya shaka zipo Ishara kwa watu
wanaoamini. 53. Sema: Enyi waja wangu waliovuka mpaka
dhidi ya nafsi zao, msikate tamaa juu ya huruma ya Mwenyezi
Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu husamehe dhambi zote.
Hakika Yeye ni Mwingi wa msamaha, Mwingi wa huruma.
54. Na rejeeni kwa Mola Wenu, na jisalimisheni Kwake, kabla
ya kuwajia mauti. Kisha hapo hamtanusuriwa.

55. Na fuateni yaliyo bora zaidi katika yale yaliyoteremshwa
kwenu kutoka kwa Mola Wenu, kabla hayajawajia mauti kwa

ghafla, pasi na kutambua. 56. Asije mtu akasema, Ole wangu!
Kwa kupuuza kwangu wajibu wangu Kwa Mwenyezi Mungu,
kwani nilikuwa miongoni mwa waliokuwa wakifanya mzaha!
57. Au akasema: Ingelikuwa Mwenyezi Mungu ameniongoza,
bila ya shaka ningelikuwa miongoni mwa wachamungu.
58. Au akasema anapoona adhabu: Lau ningepata nafasi
nyingine moja tu (ya kurudi duniani), ningekuwa miongoni
mwa wafanya mazuri. 59. (Atajibiwa) Hasha! Si zilikwishakujia
Ishara Zangu, nawe ukazikanusha, na ukafanya maringo,
na ukawa miongoni mwa wanaomkana Mwenyezi Mungu?
60. Na Siku ya Kiyama utawaona wale ambao wamemsingizia
uwongo Mwenyezi Mungu nyuso zao zimegeuzwa kuwa
nyeusi. Je, si katika Jahannamu makazi ya wenye kiburi?
61. Na Mwenyezi Mungu atawaokoa wenye kujikinga kwa
ajili ya kufuzu kwao. Hapana uovu utakaowagusa, wala
hawatahuzunika.

62. Mwenyezi Mungu Mungu Ndiye Muumba wa kila
kitu; na Yeye Ndiye Mlinzi na Mchungaji wa kila kitu.
63. Yeye ndiye mmiliki wa funguo za mbingu na ardhi. Na
wale ambao wamezikana Ishara za Mwenyezi Mungu, hao
ndio wenye hasara. 64. Sema: Je, Mnaniamrisha nimwabudu
asiyekuwa Mwenyezi Mungu, enyi wajinga? 65. Na kwa
hakika imefunuliwa kwa njia ya Wahyi kwako wewe na kwa
waliokuwa kabla yako kwamba ukimfanyia Allah washirika,
matendo yako (mazuri) yote yataporomoka, na utakuwa
miongoni mwa waliopata hasara. 66. Bali mwabudu Mwenyezi
Mungu tu, na uwe miongoni mwa wenye kushukuru.

67. Na hawakumheshimu Mwenyezi Mungu kadri
unavyostahiki utukufu Wake. Siku hiyo ya Kiyama ardhi
yote itatoshea (mithili ya) kiganjani Mwake tu! Na mbingu

zitakunjwa katika (mithili ya) mkono Wake wa kuume tu. Ametakasika na Ametukuka na wanayomshirikisha nayo.
68. Mara itapulizwa parapanda, wazimie waliomo mbinguni na waliomo ardhini, isipokuwa yule ambaye Mwenyezi Mungu amemtaka. Kisha itapulizwa mara nyengine. Hapo watainuka wawe wanangojea.
69. Na ardhi itang'ara kwa Nuru ya Mola Wake. Na Kitabu kitawekwa (mbele, kifunguliwe). Na wataletwa Manabii na mashahidi, na patahukumiwa baina yao kwa haki, wala hawatadhulumiwa.
70. Na kila nafsi italipwa kwa yale iliyoyafanya, na Yeye anayajua sana wanayoyatenda.

71. Na waliokufuru wataongozwa kwenda kwenye Jahannam makundi kwa makundi. Mpaka watakapoifikia itafunguliwa milango yake, na walinzi wake watawauliza: Kwani ninyi hawakuwajia Mitume miongoni mwenu wakiwasomea Aya za Mola Wenu Mlezi na kuwaonya mkutano wa siku yenu hii? Watasema: Ndio! Lakini tamko la kuadhibiwa makafiri limehakiki kuwa ni kweli.
72. Itasemwa: Ingieni milango ya Jahannamu mkakae milele humo. Ni ubaya ulioje wa makazi ya wenye kiburi.

73. Na waliomcha Mola Wao Mlezi wataongozwa kwenda Peponi makundi makundi. Mpaka watakapoifikia, nayo milango yake imekwisha funguliwa, walinzi wake watawaambia: Salaam Aleykum, mmefanya vizuri! Basi ingieni humu mkae milele.
74. Na (wao) watasema: Alhamdulillah! Sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu ambaye ametutimizia ahadi yake, na akatufanya warithi wa ardhi hii (ya Pepeni) Tunakaa humu katika Pepo kama tupendavyo. Ni uzuri ulioje wa malipo kwa watendao (yaliyo sawa)!
75. Na utawaona Malaika wakizunguka pembeni mwa

Arshi ya Mwenyezi Mungu, wakimsabihi na kumsifu Mola Wao. Na itahukumiwa baina yao kwa uadilifu na (pande zote) patasemwa: Sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu, Mola wa viumbe vyote!

40. Sura Al-Mu'min

## SURA YA MUUMINI AU GHAFIR

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 *Hamim*.

2 Uteremshwaji wa Kitabu hiki ni kutoka kwa Mwenyezi
Mungu Mwenye nguvu, Mwenye kujua. 3 Mwenye kughufiria
dhambi na anayekubali toba, Mkali wa kuadhibu, Mwenye
kufikia popote. Hakuna mungu ila Yeye. Kwake ndiyo
marejeo ya mwisho.

4 Hawabishani katika Ishara za Mwenyezi Mungu ila wale
ambao wamekufuru. Basi kusikudanganye kupita kwao huku
na huko katika nchi kwa kujivuna. 5 Kabla yao watu wa Nuh
(noah) pia walikataa (ishara), halkadhalika washirika (wa
uovu) baada yao. Na jamii zote hizo walipanga njama dhidi
ya Mtume wao, wamkamate. Na walibishana kwa upotovu ili
kuipindua haki. Kwa hivyo niliwatia nguvuni. Basi ilikuwaje
adhabu Yangu! 6 Hivyo ndivyo lilivyothibiti kuwa kweli
neno la Mola Wako Mlezi juu ya waliokana, kwamba wao ni
watu wa Motoni

7. Wale wanaobeba Arshi, na wanaoizunguka, wanamsabihi
kwa kumhimidi Mola Wao Mlezi, na wanamwamini na

wanawaombea msamaha walioamini. Mola Wetu Mlezi!
Umekifikia kila kitu kwa huruma zako na ujuzi. Basi
wasamehe ambao wametubu na wakaifuata Njia Yako, na
waepushe na adhabu ya Jahannamu. 8. Mola Wetu Mlezi!
Na uwaingize katika Bustani za Milele ulizowaahidi wao na
walio wema katika wazee wao na wake zao na watoto wao.
Hakika Wewe ni Mwenye nguvu, Mwenye hekima. 9. Na
waepushe na maovu; kwani umwepushaye na maovu siku
hiyo, hakika umemhurumia. Na huo ndio ushindi mkubwa.

10. Hakika wale waliokufuru wataulizwa kwa sauti ya
kupaa: 'Hivi chuki zenu kwa Mwenyezi Mungu ni kubwa
kuliko chuki zenu dhidi yenu wenyewe?' Vile mlikuwa
mnaitwa kwenye imani, mkakataa. 11. Watasema: Ewe Mola
Wetu! Mara mbili umetufanya tusiwe na uhai na mara mbili
umetufanya tuwe hai, sasa tumetambua makosa yetu. Je, ipo
njia ya kutoka (hapa)? 12. (Watajibiwa) Hii ni kwa sababu
pale alipoombwa Mwenyezi Mungu peke Yake mlikataa.
Lakini aliposhirikishwa na wengine, mkawa mnaamini. (Leo)
Hukumu yote ni ya Mwenyezi Mungu Mtukufu Mkubwa.

13. Yeye Ndiye ambaye anawaonesha Ishara Zake, na
anayewateremshia riziki kutoka mbinguni. Lakini wanaotii
maonyo ni wale tu wanaomgeukia Mwenyezi Mungu.
14. Basi mwombeni Mwenyezi Mungu pekee kwa ukweli na
dhati, wajapochukia makafiri. 15. Yeye ndiye mwenye vyeo
vya juu kushinda, Mwenye Arshi. Humtuma Jibril kwa amri
Yake, kwa amtakaye katika waja Wake, ili yeye awaonye
(viumbe) juu ya Siku ya kukutana. 16. Siku ambayo wote
watakuja mbele. Hakuna kitu chochote kinachowahusu
kitafichikana kwa Mwenyezi Mungu. Ufalme ni wa nani
leo? Ni wa Mwenyezi Mungu Mmoja, Mwenye nguvu,

asiyeshindika. [17.] Leo kila nafsi italipwa kwa iliyoyachuma. Hapana kudhulumiwa siku hiyo. Kwa sababu Mwenyezi Mungu ni Mwepesi wa kuhesabu.

[18.] Na waonye siku hiyo inayozidi kukaribia, wakati nyoyo zitakapofika kooni, zikiwasonga koo. Watenda maovu hawatakuwa na rafiki, wala mwombezi wa kusikilizwa. [19.] Anajua udanganyifu (unaofanywa kwa) macho na ambayo nyoyo zinayaficha. [20.] Na Mwenyezi Mungu atahuhukumu kwa uadilifu. Na wale ambao (binadamu) wanawaomba kinyume Chake, hawataweza kuhukumu aslan. Hakika Mwenyezi Mungu Ndiye Mwenye Kusikia, Mwenye kuona.

[21.] Je, hawatembei katika dunia wakaona vipi ulikuwa mwisho wa waliokuwa kabla yao? Hao walikuwa wamewazidi wao kwa nguvu na mabaki (ya makumbusho) waliyoyaacha katika ardhi. Na Mwenyezi Mungu aliwatia nguvuni kwa sababu ya madhambi yao. Na wala hapakuwa wa kuwalinda dhidi ya Mwenyezi Mungu. [22.] Hayo ni kwa sababu walikuwa wanawajia Mitume wao kwa hoja zilizo wazi, lakini wakawakataa, ndipo Mwenyezi Mungu akawatia nguvuni. Bila ya shaka Yeye ni Mwenye nguvu, Mkali wa kuadhibu.

[23.]Na kwa hakika tulimtuma Musa (Moses) pamoja na Ishara Zetu na uthibitisho ulio wazi. [24.] Kwa Firauni (Pharaoh) na Hamana na Qaruni. Wakasema: Ni mchawi, mwongo mkubwa. [25.] Alipowajia na ukweli kutoka Kwetu, walisema: ‘Waueni watoto wanaume wa wale waliomwamini na waacheni hai wanawake wao. Lakini njama za wanaokana (haziishii) katika chochote ila makosa na kujidanganya.

[26.] Na Firauni akasema: Niachieni nimwue Musa, naye amwite Mola Wake! Hakika mimi nahofia asije kubadilisha

dini yenu, au akasababisha uharibifu kuchipuka katika nchi (hii). 27. Naye Musa akasema: Hakika mimi (tayari) nimemwomba Mola Wangu na Mola Wenu Mlezi anilinde na kila mwenye kiburi asiyeiamini Siku ya Hesabu.

28. Akasema mtu mmoja Muumini katika watu wa Firauni, anayeficha Imani yake: Mtamuuwa mtu kwa sababu tu anasema Mola Wangu ni Allah, wakati amewajia na uthibitisho ulio wazi kutoka kwa Mola wenu Mlezi? Akiwa ni mwongo basi (dhambi ya) uwongo wake itamrudia mwenyewe. Ama akiwa asema kweli, yatawafika baadhi ya hayo anayowaahidi. Hakika Mwenyezi Mungu hamwongozi (mtu) anayepinduka mipaka, mwongo mkubwa. 29. Enyi watu wangu! Leo mna ufalme, mmeshinda katika nchi; basi ni nani atakayetusaidia kutuokoa na adhabu ya Mwenyezi Mungu kama ikitufikia? Firauni akasema: ‘Siwashauri nyie ila jambo ninaloliona mimi’ wala siwaongozi ila kwenye njia ya uwongofu.

30. Yule aliyeamini akasema: Enyi watu wangu! Mimi nawahofia mfano wa (balaa la) Siku ya washirika (katika dhambi). 31. Mfano wa hali ya watu wa Nuh (Noah) na A’di na Thamudi na wale wa baada yao. Na Mwenyezi Mungu hataki kuwadhulumu waja. 32. Na enyi watu wangu! Hakika mimi nawahofia Siku ya mayowe. 33. Siku mtakapogeuka kurudi nyuma kukimbia, hamtakuwa na wa kuwalinda na Mwenyezi Mungu. Na ambaye Mwenyezi Mungu amemwacha apotee, basi huyo hana wa kumwongoa.

34. Na alikwishawajia Yusuf (Joseph) wakati uliopita pamoja na dalili zilizo wazi, lakini nyinyi mliendelea kutilia shaka ya yale aliyowaletea. Hatimaye alipokufa mkasema: Mwenyezi Mungu hataleta tena Mtume baada yake. Ndiyo

hivyo, Mwenyezi Mungu humwacha apotee yule aliyepituka mpaka, mwenye shaka. [35.] (Kama) Hao ambao huzozana juuu ya Aya za Mwenyezi Mungu bila ya ushahidi wowote uliowafikia. Ni jambo linalochukiza mno mbele ya Mwenyezi Mungu na mbele ya walioamini. Hivi ndivyo Mwenyezi Mungu apigavyo muhuri juu ya kila moyo wa jeuri, mtenda maovu asiyejali.

[36.] Na Firauni akasema: Ewe Hamana! Nijengee mnara ili nipate kuzifikia njia. [37.] Njia za mbinguni ili nikamwone Mungu wa Musa. Na kwa hakika mimi namjua kuwa ni mwongo tu. Na ndiyo hivyo Firauni alivyofanyiwa aone matendo yake mabaya kuwa mazuri, na akazuiliwa na njia (sahihi). Na hila za Firauni hazikuishia popote isipokuwa katika maangamizi (yake).

[38.] Na yule aliyeamini akasema: Enyi watu wangu! Nifuateni mimi, nitawaongoza kwenye njia sahihi. [39.] Enyi watu wangu! Hakika maisha haya ya dunia ni starehe yenye kupita tu, na hakika Akhera ndiyo nyumba ya daima. [40.] Mwenye kutenda uovu hatalipwa ila sawa sawa na uovu wake. Na mwenye kutenda wema, akiwa mwanamume au mwanamke, naye ni muumini, basi hao wataingia Peponi, waruzukiwe humo bila ya hesabu. [41.] Na Enyi watu wangu! Inakuaje mimi ninawaita kwenye uwokovu, nanyi mnaniita kwenye Moto? [42.] Mnaniita nimkufuru Mwenyezi Mungu na nimshirikishe na yule ambaye simjui, nami ninawaita kwa Mwenye nguvu, Mwenye kusamehe tena na tena? [43.] Bila ya shaka mnayeniitia nimwabudu, hastahiki maombi si duniani wala Akhera. Na hakika marejeo yetu wote ni kwa Mwenyezi Mungu (wa haki). Na wanaovuka mpaka (katika dhambi) basi hao ndio watu wa Motoni! [44.] Basi muda

mfupi tu mtayakumbuka ninayowaambia. Nami namkabidhi
Mwenyezi Mungu mambo yangu. Hakika Mwenyezi Mungu
ni Mwenye kuwaangalia waja wake.
45. Basi Mwenyezi Mungu akamlinda na kila ubaya wa
hila walizozipanga (dhidi yake). Lakini mzigo mkubwa wa
adhabu itazingira pande zote za watu wa Firauni. 46. (Nayo
ni) Moto wataletwa mbele yake asubuhi na jioni. Na itapofika
Siku ya Kiyama (itanadiwa): ‘Waingizeni watu wa Firauni
katika adhabu kali kabisa’!
47. Na watapohojiana huko Motoni, wanyonge watawaambia
wale wakubwa (wao) wenye majivuno: Hakika sisi tulikuwa
wafuasi wenu, basi je, mnaweza kutuondolea sehemu ya huu
Moto? 48. Wale waliokuwa wakijivuna watasema: Sisi sote
tumo humu humu! Hakika Mwenyezi Mungu ameshahukumu
baina ya waja! 49. Na walio Motoni watawaambia walinzi wa
Jahannamu: ‘Mwombeni Mola Wenu atupunguzie japo siku
moja ya adhabu!. 50. (Walinzi) Watasema: Je, Hawakuwa
wakiwafikia Mitume wenu kwa hoja zilio wazi? Watasema:
Ndio! Watasema: Basi ombeni nyie! Na maombi ya wasio na
Imani si chochote isipokuwa kupoteza muda tu!.
51. Hakika sisi tutawanusuru Mitume wetu na wale ambao
wameamini katika uhai wa duniani na siku wataposimama
mashahidi (mbele yao). 52. Siku ambayo hautawafaa
madhalimu udhuru wao, nao watapata laana, na watapata
makazi mabaya. 53. Na kwa hakika tulimpa Musa uwongofu,
na tukawarithisha Wana wa Israili Kitabu. 54. Ni Uwongofu
na Ujumbe kwa wenye kufahamu. 55. Basi subiri. Hakika
ahadi ya Mwenyezi Mungu ni kweli. Na, omba maghufira
kwa makosa yako na umsabihi Mola Wako kwa kumhimidi
jioni na asubuhi.

56. Hakika wale ambao wanabishana katika Ishara za
Mwenyezi Mungu bila ya dalili yoyote iliyowafika, hawana
vifuani mwao ila kutaka ukubwa tu, na wala hawaufikii. Basi
jikinge kwa Mwenyezi Mungu; hakika Yeye ni Mwenye
kusikia, Mwenye kuona. 57. Bila shaka kuumba mbingu na
ardhi ni (jambo) kubwa zaidi kuliko kuumba watu, lakini
watu wengi hawajui. 58. Na hawalingani kipofu na mwenye
kuona, wala walioamini na wakatenda mazuri na wale
watenda mabaya. Ni kwa uchache mno mnatii maonyo.
59. Hakika Kiyama kitakuja, bila shaka, lakini watu wengi
hawaamini.

60. Na Mola Wenu Mlezi anasema niombeni Nami
nitawaitikia. Hakika wale ambao wanajivuna kufanya
ibada Yangu wataingia Jahannamu wakiwa madhalili.
61. Ni Mwenyezi Mungu ambaye amewafanyia usiku ili
mpate kupumzika, na mchana wa kuonea. Hakika Mwenyezi
Mungu bila ya shaka ni Mwenye hisani nyingi juu ya watu,
lakini watu wengi hawashukuru. 62. Huyo Ndiye Mwenyezi
Mungu Mola Wenu Mlezi, Muumba wa kila kitu. Hapana
mungu ila Yeye. Basi vipi mnadanganywa mkageuka
(kuacha ukweli)? 63. Hivyo ndivyo walivyodanganywa wale
waliokuwa wakizikanusha Aya za Mwenyezi Mungu.

64. Ni Mwenyezi Mungu aliyewafanyia ardhi kuwa ni
pahala pa kukaa, na mbingu kuwa dari. Na akawatia sura,
akazifanya nzuri sura zenu, na akawaruzuku (katika vitu)
vizuri. Huyo Ndiye Mwenyezi Mungu Mola Wenu. Basi
ametukuka Mwenyezi Mungu Mola wa walimwengu wote.
65. Yeye yuko hai - hapana mungu isipokuwa Yeye. Basi
mwabuduni Yeye mkimtakasia ibada (yenu) Yeye tu. Sifa

njema zote ni za Mwenyezi Mungu, Mola wa walimwengu wote.

66. Sema: Hakika nimekatazwa kuwaabudu wale mnaowaomba badala ya Mwenyezi Mungu, kwa vile zimenijia hoja zilizo wazi kutoka kwa Mola Wangu Mlezi. Na nimeamrishwa nisalimu amri (niwe Muislamu) kwa Mola wa walimwengu wote. 67. Yeye Ndiye ambaye amewaumba kwa udongo, kisha kwa tone la manii, kisha kwa pande la damu linaloning’inia, kisha akawatoa nje katika hali ya mtoto mchanga, kisha akawaacha mfikie utu uzima, kisha akawaacha muwe wazee. Na kati yenu wapo wanaokufa kabla, na kisha akawaacha mfikishe muda uliokwishawekwa, ili mpate kujifunza hekima. 68. Yeye Ndiye ambaye hutoa uhai na mauti. Akiamua jambo lolote, husema tu: ‘iwe!’ na huwa.

69. Je, Huwaoni wale ambao wanabishana katika Ishara za Mwenyezi Mungu Wanageuzwa vipi (kinyume cha uhakika)? 70. Ambao wamekataa Kitabu na yale tuliyowatuma nayo Mitume Wetu. Muda mfupi watajua! 71. Zitakapokuwa pingu shingoni mwao na minyororo, huku wanaburuzwa. 72. Katika maji yanayochemka, kisha motoni watachomwa. 73. Tena wataulizwa: Wako wapi (miungu) mliokuwa mkiwashirikisha… 74. Badala ya Allah? Watasema: Wametupotea, bali tangu zamani hatukuwa tukiomba kitu chochote! Hivyo ndivyo Mwenyezi Mungu huwaacha makafiri wapotee. 75. Haya ni kwa sababu mlikuwa mkifurahia vitu vingine vya duniani badala ya ukweli, na kwa sababu mlikuwa mkidharau. 76. Ingieni kwenye milango ya Jahannamu, mkae milele humo. Ubaya ulioje wa makazi hayo ya wenye kiburi!

77. Basi subiri, hakika ahadi ya Mwenyezi Mungu ni kweli. Ima tukuoneshe (ukiwa hai) baadhi ya yale tuliyowaahidi au tukufishe (kabla), (ni mamoja) Kwani marejeo yao wote ni Kwetu tu.

78. Na kwa hakika tuliwatuma Mitume kabla yako. Wengine katika hao tumekusimulia na wengine hatukukusimulia. Na haiwezekani kuwa Mtume alete muujiza wowote isipokuwa kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Endapo amri ya Mwenyezi Mungu imetolewa, (jambo) hilo huwa limeshahukumiwa kwa haki na uadilifu, na hapo huwa wamepata hasara wale wote wanaoshabikia uongo na batili.

79. Mwenyezi Mungu Ndiye ambaye amewafanyia nyie mifugo baadhi yake mnaipanda na baadhi yake mnakula.
80. Na katika hao mna manufaa mengi, na mnapata kwao haja zilizo vifuani mwenu; na mnachukuliwa juu yao na juu ya
majahazi. 81. Na anawaonesha Ishara Zake, basi ni ipi katika Ishara za Mwenyezi Mungu mtaikataa?

82. Je, hawatembei duniani wakaona ulivyokuwa mwisho wa wale waliokuwa kabla yao? Walikuwa wengi kuliko hawa, na waliwazidi kwa nguvu na athari (walizoacha) duniani. Hata hivyo, yote hayo waliyoyafanya hayawafai chochote!
83. Basi walipowajia Mitume wao kwa dalili zilizo wazi walitamba kwa elimu waliyokuwa nayo. Lakini (adhabu)
waliyokuwa wakiifanyia dhihaka ikawadiriki. 84. Walipoiona adhabu Yetu wakasema: Tumemwamini Mwenyezi Mungu peke Yake na tumekataa tuliyokuwa tukimshirikisha naye.
85. Lakini imani yao haikuwa ni yenye kuwafaa wakati ambapo wamekwishaiona adhabu Yetu. Huo ndio mwenendo wa Mwenyezi Mungu uliyopita kwa waja Wake. Na hapo waliokufuru watapata hasara.

## 41. Sura Fussilat

# SURA YA KILICHOELEZEWA KWA UPANA

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 *Ha Mim.*

2 Kimeteremshwa kutoka kwa Mwingi wa rehema, Mwenye
kurehemu. 3 Kitabu kilichofafanuliwa Aya zake kwa urefu.
Qur'an kwa lugha ya Kiarabu kwa watu wanaojua. 4 Inayotoa
habari nzuri na maonyo. Lakini wengi wao wamekataa; kwa
hiyo hawasikii. 5 Na wakasema: Nyoyo zetu zina vifuniko
kwa hayo unayotuitia, na masikio yetu yana uziwi, na baina
yetu na wewe kuna pazia. Basi wewe fanya (utakavyo), nasi
tufanye (tutakavyo).

6 Sema: Mimi ni mtu kama nyinyi; ninayefunuliwa kwa
njia ya Wahyi kwamba Mungu Wenu ni Mungu Mmoja tu.
Basi simameni wima juu ya ukweli, na mumtake maghufira.
Na ole wao wanaomshirikisha (na wengine). 7 Ambao
hawatoi Zaka na wanaoikanusha Akhera. 8 Hakika wale
ambao wameamini na wakatenda mema watakuwa na ujira,
malipo yasiyo kikomo.

9. Sema: Hivi nyinyi mnamkataa aliyeumba ardhi katika
(muda, sawa na) siku mbili, na mnamfanyia washirika?
Huyo Ndiye Mola wa walimwengu wote. 10. Na akaweka
humo milima iliyosimama wima, na akamimina Baraka
zake humo, na akakadiria chakula chao (viumbe), katika
siku nne, kulingana na (mahitajio ya) wanaohitaji (chakula).
11. Kisha akaijumuisha mbingu katika muundo Wake, nayo

ilikuwa (kama) moshi. Akaiambia hiyo na ardhi pia, 'njooni pamoja, kwa hiari au kwa nguvu'! Zikasema: 'Tunakuja (pamoja) kwa utiifu'. 12. Akazikamilisha kuwa mbingu saba, kwa (muda unaolingana na) siku mbili. Na akaipangia kila mbingu mambo yake. Na tukaipamba mbingu ya chini kwa mataa na kwa ulinzi. Hayo ndiyo maamuzi ya Mwenyezi nguvu Mwenye Kujua.

13. Basi wakipuuza, sema: Nawaonyeni adhabu mfano wa adhabu (ya mpasuko wa radi) iliyowapata A'di na Thamudi. 14. Pale walipowajia Mitume kabla yao na baada yao wakiwaambia: 'Msimwabudu ila Mwenyezi Mungu'! Wakasema: Angetaka Mola Wetu Mlezi bila ya shaka angewateremsha Malaika. Sasa siye kwa hakika tunayakataa hayo mliyotumwa nayo.

15. Ama kina A'di walifanya kiburi duniani dhidi ya ukweli wa aina yeyote. Wakasema: Nani aliye na nguvu zaidi kuliko sisi? Kwani hawajui kwamba Mwenyezi Mungu ambaye amewaumba wao ni Mwenye nguvu zaidi kuliko wao? Na wao wakawa wanazikanusha Ishara Zetu! 16. Basi tuliwapelekea upepo wa kimbunga uliondelea katika siku (zote) za janga. Ili tuwaonjeshe adhabu ya kuwaaibisha katika uhai wa duniani, na bila ya shaka adhabu ya Akhera ni ya kuaibisha zaidi. Na hawataweza kusaidiwa. 17. Na ama Thamudi tuliwaongoza, lakini walipendelea zaidi upofu kuliko uwongofu. Basi adhabu ya kustukiza na ya kufedhehesha ikawafyeka, kwa sababu ya yale waliyokuwa wakiyachuma 18. Na tukawaokoa wale ambao wameamini na wakawa wamchamungu.

19. Na siku watakapokusanywa maadui wa Mwenyezi Mungu kupelekwa motoni, wakigawanywa makundi makundi. 20. Mpaka watakapoufikia, yatawatolea ushahidi

masikio yao, na macho yao na ngozi zao juu ya yote waliyokuwa wakiyafanya. [21.]Na wataziuliza ngozi zao: Kwa nini mmetoa ushahidi dhidi yetu? Zitasema: Ametuwezesha kutamka Mwenyezi Mungu ambaye ametamkisha kila kitu! Na Yeye Ndiye aliyewaumba ninyi mara ya kwanza, na Kwake Yeye (ndiyo) mnarejeshwa. [22.] Na hamkuwa mkitaka kujificha kiasi masikio yenu, na macho yenu, na ngozi zenu, visiweze kupata ushahidi dhidi yenu! Lakini mlidhani kwamba Mwenyezi Mungu hayajui mengi katika mliyokuwa mkiyatenda. [23.]Na hiyo dhana yenu mliyokuwa mkimdhania Mola Wenu Mlezi, imewaangamiza, na mmekuwa miongoni mwa waliopata hasara. [24.] Wakisubiri basi moto ndio makazi yao. Na wakiomba radhi hawakubaliwi.

[25.] Na tuliwawekea marafiki wa mfano wao (huko duniani). Hao wakawafanya wavione vizuri vilivyo mbele yao na nyuma yao. Basi hukumu ile ile iliyotolewa kwa mataifa yaliyotangulia kabla yao, miongoni mwa majini na watu, ikathibiti kwao (pia) kuwa ni kweli. Kwa vile walikuwa wamepotea kabisa.

[26.] Na wale wasioamini walisema: Msiisikilize hii Qur'ani, na payukeni ovyo wakati inasomwa, huenda mkashinda. [27.] Kwa hakika tutwaonjesha adhabu kali wale wasioamini, na tutawalipa kwa mabaya ya kupindukia waliyokuwa wakiyafanya. [28.] Hayo ndiyo malipo ya maadui wa Mwenyezi Mungu - Moto! Humo watakuwa na nyumba ya kudumu, ikiwa ni malipo yao kwa sababu walikuwa wakizikataa Ishara Zetu.

[29.]Na wale ambao wamekufuru watasema: Mola Wetu Mlezi! Tuoneshe (aina mbili ya) waliotupoteza, majini na watu, tuwapondeponde kwa miguu yetu, ili wawe chini

(wakidharauliwa na wote). 30. Hakika wale ambao wamesema: Mola Wetu Mezi ni Allah, kisha wakawa na msimamo wa kunyooka, huwashukia Malaika (na kuwaambia): Msiwe na hofu, wala msihuzunike; na furahini kwa Pepo mliyokuwa mkiahidiwa. 31. Sisi ndio walinzi wenu katika maisha ya dunia na katika Akhera. Nanyi mtapata humo (Peponi) kinachotamaniwa na nafsi zenu, na humo mtapata mvitakavyo. 32. Ni mahali pema pa kushukia palipoandaliwa na Mwingi wa Maghufira, Mwenye kurehemu.

33. Na ni nani bora wa maneno kuliko yule anayewaita watu kwa Mwenyezi Mungu na akatenda mema, na akasema: mimi ni katika Waislamu? 34. Mema na maovu hayawi sawa. Zuia uovu kwa lililo jema zaidi. Mara yule ambaye kati yako na yeye pana uadui atakuwa kama rafiki wa karibu. 35. Lakini hawapewi hayo ila wanaosubiri, wala hawapewi ila wenye bahati kubwa. 36. Na kama Shetani akikuchochea kwa uchochezi wowote ule, basi jikinge kwa Mwenyezi Mungu (kwa kusema Audhubillah). Hakika Yeye ni Mwenye kusikia, Mwenye kujua.

37. Na katika Ishara Zake ni usiku na mchana, na jua na mwezi. Msilisujudie jua wala mwezi, bali msujudieni Mwenyezi Mungu aliyeviumba, ikiwa nyinyi mnamwabudu Yeye tu. 38. Na ikiwa watafanya kiburi (haidhuru), kwani hao walioko kwa Mola Wako wanamtakasa Yeye usiku na mchana, na wao hawachoki.

39. Na katika Ishara Zake ni kwamba utaiona ardhi imechoka, lakini tunapoiteremshia maji mara utaiona inatutumka na inaota mimea. Bila ya shaka aliyeirudishia uhai ardhi hiyo Ndiye atayewarudishia uhai waliokufa. Hakika Yeye ni Muweza juu ya kila kitu. 40. Hakika wale ambao

wanaupotoa ukweli uliomo katika Ishara Zetu hawafichikani
kwetu. Je, atakayetupwa Motoni ni bora au atakayekuja hali
amesalimika Siku ya Kiyama? Fanyeni mpendavyo, kwa
hakika Yeye anayaona mnayoyatenda.
41. Hakika wale ambao wameukataa ujumbe pale
ulipowafikia (pia hawafichiki). Na kwa hakika ujumbe huo
ni kitabu chenye (mashiko ya) nguvu. 42. Hakuna uwongo
utaokikaribia kitabu hicho, si mbele yake wala nyuma yake.
Kimeteremshwa na Mwenye hikima, anayestahiki Sifa.
43. Huambiwi ila yale yale waliyoambiwa Mitume wa kabla
yako; kwamba hakika Mola Wako ni mwingi wa kusamehe
na pia Mwenye adhabu chungu.
44. Na kama tungeliifanya Qur’ani ikawa kwa lugha ya
kigeni wangelisema: Kwa nini Aya zake hazikufafanuliwa?
Vipi! Qur’an iwe katika lugha ya kigeni na Mtume mwarabu?
Sema: Hii Qur’ani ni uwongofu na ya kuponyesha kwa
wanaoamini. Na wasioamini wana (ugonjwa wa) kutosikia
katika masikio yao, nayo ni (kama) upofu kwao. (kana
kwamba) Wameitwa kutoka mahali mbali..
45. Na hakika tulimpa Musa Kitabu, lakini pakatokea
hitilafu kuhusu Kitabu hicho. Na lau kuwa halikwishatangulia
neno la Mola wako Mlezi, hitilafu zao zingesawazishwa.
Lakini waliendelea katika kuwa na shaka na wasi wasi juu
ya Kitabu hicho. 46. Atendaye mema basi ni kwa (maslahi
ya) roho yake mwenyewe, na atendaye mabaya ni dhidi ya
roho yake mwenyewe. Na Mola Wako Mlezi si Mwenye
kuwadhulumu waja (wake).
47. Kwake (mwenyezi Mungu) pekee ndiyo hurejewa
kwa kujua (lini) saa ya Kiyama. Na wala matunda hayatoki
katika mafumba yake, na wala mwanamke hachukui mimba,

wala hazai, ila kwa kujua Kwake. Na siku atakayowaita, (akawauliza): 'Wako wapi hao washirika Wangu?' Watasema: Tunakuhakikishia, hakuna yeyote miongoni mwetu anayeshuhudia hilo. 48. Na watawaacha bila msaada wale wote waliokuwa wakiwaomba hapo nyuma, na watagundua kuwa hawana pa kukimbilia.

49. Mwanaadamu hachoki kuomba vitu vizuri. Ama jambo baya linapomfika, mara huvunjika moyo akakata tamaa. 50.Na tukimwonjesha rehema itokayo Kwetu baada ya kumpata madhara, bila ya shaka atasema: Haya ni yangu, mimi nastahiki! Naa sidhani Kiyama kitakuja! Na hata nikirudishwa kwa Mola Wangu bila ya shaka nina mema yangu Kwake! Basi kwa yakini tutawaelezea wale ambao wamekufuru waliyoyatenda, na kwa yakini tutawaonjesha adhabu ngumu.

51. Na tunapomneemesha mwanadamu hugeuka na kujitenga upande wake (badala ya kuja Kwetu). Na mabaya yanapomgusa, huwa na dua ndeeefu! 52. Sema: Mnaonaje! Ikiwa haya (kweli) yanatoka kwa Mwenyezi Mungu, kisha mkayakataa, ni nani aliyepotea zaidi kuliko aliye katika upinzani, mbali kabisa (na haya)?

53. Tutawaonesha Ishara Zetu pambizoni mwa mbingu na katika nafsi zao, mpaka iwabainikie kwamba haya ni kweli. Je, haikutoshi kuwa Mola Wako Mlezi Yeye ni mwenye kushuhudia kila kitu? 54. Ah! Hivi wao wamo katika shaka ya kukutana na Mola Wao?! Ndiyo! Hakika Yeye amekizunguka kila kitu.

42. Sura Ash-Shura

# SURA YA MASHAURIANO

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 *Ha Mim.* 2 *A'yn Siin Qaf.*

3 Hivyo ndivyo Mwenyezi Mungu Mwenye nguvu na
Mwenye hekima anavyokufunulia Wahyi wewe (kama )
kwa waliokuwa kabla yako. 4 Ni vyake vilivyomo mbinguni,
na vilivyomo ardhini. Na Yeye ndiye Mtukufu, Mkuu.
5 Zinakaribia mbingu kutatuka huko juu (Kwa Utukufu
Wake). Na Malaika wakimwadhimisha Mola wao Mlezi kwa
'Subhanallah, Alhamdulillah' huku wakiwaombea msamaha
waliomo duniani. Lo! Hakika Mwenyezi Mungu ndiye
Mwingi wa msamahama, Mwingi wa huruma. 6 Na wale
waliowafanya wengine badala Yake Yeye kuwa ndiyo walinzi
wao, Mwenyezi Mungu anawaona. Na wewe si msimamizi
juu ya matendo yao.

7 Na namna hivi tumekufunulia Qur'an kwa lugha ya
Kiarabu, ili uwaonye watu wa mji mkuu (Makka) na walio
pembezoni mwake. Na uhadharishe juu ya Siku ya Mkutano
ambayo haina shaka (kuwasili). Kundi moja litakuwa Peponi,
na kundi jingine Motoni.

8. Na laiti Mwenyezi Mungu angelipenda angewafanya
nyie wote taifa moja. Lakini humwingiza amtakaye katika
rehema Yake. Na watenda mabaya hawana wa kuwalinda
wala wa kuwanusuru. 9. Nini! Wamewafanya wengine badala
Yake kuwa walinzi wao?! Bali Mwenyezi Mungu Ndiye

Mlinzi hasa. Yeye ndiye anayewapa uhai wafu, na Yeye ni Mwenye uwezo juu ya kila kitu. [10.] Na kitu chochote mtakachohitalifiana ndani yake (Quran), basi uamuzi wa hilo anao Mwenyezi Mungu. Huyo Mwenyezi Mungu ndiye Mola Wangu Mlezi ninayemtegemea na Kwake Yeye narejea.

[11.] Muumba mbingu na ardhi. Amewafanya mke na mume kutokana nanyi wenyewe, na katika mifugo dume na jike. Anawazidisha kwa namna hii. Hakuna chochote kile kama Yeye. Naye ni Mwenye kusikia Mwenye kuona. [12.] Yeye ndiye Mwenye funguo za mbingu na ardhi. Humkunjulia riziki amtakaye, na humpimia amtakaye. Hakika Yeye ni Mjuzi wa kila kitu.

[13.] Amewawekea dini ile ile aliyomuusia Nuh na tuliyokufunulia wewe, na tuliyowausia Ibrahim (Abraham) na Musa (Moses) na Isa (Jesus), kwamba dumisheni dini hii wala msitofautiane juu yake. Yanawawia vigumu Wapagani haya unayowaitia. Mwenyezi Mungu humchagua Kwake amtakaye, Na humwongeza Kwake aelekeaye (kwake).

[14.] Na kamwe hawakutofautana ila baada ya elimu kuwajia, (na ni) kwa sababu ya ubinafsi na wivu ulio baina yao. Na lau isingekuwa tayari imekwishatangulia kauli kutoka kwa Mola Wako Mlezi (kuchelewesha) mpaka muda uliowekwa, basi bila ya shaka hayo yangekwishatatuliwa baina yao. Na hakika walioritbishwa Kitabu baada ya kuwajia wao elimu, wana shaka nacho, inayowakera.

[15.] Kwa sababu hiyo, waite (kwenye Imani). Nawe simama sawa sawa kama ulivyoamriwa, wala usifuate matamanio yao. Na useme: Naamini Kitabu alichokishusha Mwenyezi Mungu, na nimeamriwa kuhukumu kwa haki na uadilifu baina yenu. Mwenyezi Mungu ni Mola Wetu Mlezi, na Mola Wenu

Mlezi. Sisi tuna jukumu kwa vitendo vyetu, nanyi pia mnalo kwa vitendo vyenu. Hakuna ubishani baina yetu na yenu. Na Mwenyezi Mungu atatukusanya pamoja, na marejeo ni Kwake. 16. Na wanaendelea kuhoji juu ya Mwenyezi Mungu baada ya Yeye kukubalika, hoja za watu hao ni batili mbele ya Mola Wao Mlezi, na juu yao ipo ghadhabu, na itakuwa kwao adhabu kali.

17. Ni Mwenyezi Mungu aliyeteremsha Kitabu kwa (ajili ya) ukweli na (kiwe) kipimo (cha matendo). Na nini kitakujulisha pengine Kiyama kipo karibu? 18. Wale wasiokiamini ndiyo watakao kifike haraka. (Lakini) Wale wanaoamini wanatishika nacho, vile wanajua kwamba hicho ni kweli. Lo! Hakika hao wanaobishana juu ya Kiyama wamo katika upotevu ulio mbali kabisa (na uhalisia).

19. Mwenyezi Mungu ni Mpole kwa waja Wake. Humruzuku ampendaye. Naye ni Mwenye nguvu, Mwenye kushinda. 20. Mwenye kutaka mavuno ya Akhera tutamzidishia katika mavuno yake, na mwenye kutaka mavuno ya duniani tutampa katika hayo, lakini huko Akhera hana fungu lolote..

21. Nini! Au wana (waungu) washirika waliowatungia dini bila ya ruhusa ya Mwenyezi Mungu? Na laiti lisingekuwepo tayari tamko la hukumu, basi wangelikatiwa hukumu yao mara moja. Na hakika watenda uovu watapata adhabu chungu. 22. Utawaona watenda maovu wanavyokuwa na hofu kwa sababu ya waliyoyafanya, nayo (adhabu) itawafika tu. Na walioamini na wakatenda mema watakuwamo katika mabustani ya Peponi. Humo watapata wayatakayo kwa Mola Wao Mlezi. Hiyo ndiyo fadhila kubwa. 23. Hayo ndiyo anayowapa habari nzuri Mwenyezi Mungu waja Wake walioamini na wakatenda mema. Sema: mimi siwaombi

malipo yoyote kwa hili, isipokuwa mapenzi kwa ndugu wangu wa karibu. Na anayefanya wema tutamzidishia wema. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa maghufira Mwingi wa shukrani.

[24.]Au wanasema: Amemzulia Mwenyezi Mungu uwongo? Mwenyezi Mungu akingetaka, angepiga muhuri juu ya moyo wako. Na Mwenyezi Mungu anaifuta batili na anaithibitisha Haki kwa maneno Yake. Hakika Yeye anayajua yaliyomo vifuani. [25.] Naye Ndiye anayepokea toba kutoka kwa waja Wake, na anasamehe makosa. Na anayajua mnayoyatenda. [26.] Na anawaitikia walioamini na wakatenda mema, na anawazidishia fadhila Zake. Na makafiri watakuwa na adhabu kali.

[27.] Na lau Mwenyezi Mungu angeliwakunjulia riziki waja Wake, wangefanya maovu kupita mpaka katika dunia, lakini anaiteremsha kwa kipimo akitakacho. Hakika Yeye kwa waja Wake ni Mwenye habari, Mwenye kuona. [28.] Naye Ndiye anayeiteremsha mvua baada ya wao kukata tamaa, na hueneza rehema Yake. Naye ndiye Mwenye kuwalinda, Mstahiki wa sifa zote. [29.] Na katika Ishara Zake ni kuumba mbingu na ardhi, na wanyama aliowaeneza humo. Naye ni Mwenye uwezo wa kuwakusanya apendapo.

[30.] Na msiba wowote unaowapata, hiyo ni kwa sababu ya yaliyofanywa na mikono yenu. Naye anasamehe mengi. [31.] Na nyinyi hamwezi kushinda ardhini. Na hamna wa kuwalinda wala msaidizi kinyume cha Mwenyezi Mungu.

[32.] Na katika Ishara Zake ni vyombo viendavyo na kurudi shwari baharini (virefu kama) kama milima. [33.] Akitaka, anaweza akautuliza upepo vikabaki vimesimama tutwe juu ya mgongo wa bahari. Hakika katika hayo zipo Ishara kwa kila

mwenye kusubiri akashukuru. 34. Au aviangamize kutokana na matendo (mabaya) waliyoyafanya. Naye husamehe mengi. 35. Waache hao wanaohoji ishaa zetu wajue kwamba pahala pa kukimbilia.

36. Basi vvyote mlivyopewa ni starehe ya maisha ya dunia, lakini kilichoko kwa Mwenyezi Mungu ni bora, na cha kudumu zaidi. Hicho ni kwa ajili ya walioamini na wakawa wanamtegemea Mola wao. 37. Wale wanoepuka madhambi makubwa na mambo machafu na wanapokasirika, hata hapo, usamehe. 38 Na wale waliomwitikia Mola Wao Mlezi na wakadumisha Swala. Na mambo yao ni kwa kushauriana baina yao, na wanatoa katika vile tulivyowaruzuku. 39. Na ambao wanapofanyiwa ukandamizaji (hutoa msaada na) hujitetea. 40. Na malipo ya uovu (wa kumjeruhi mtu) ni uovu (wa majeraha) mfano wake. Lakini mwenye kusamehe na akataka maridhiano, basi huyo malipo yake yapo kwa Mwenyezi Mungu. Hakika Yeye hawapendi wenye kufanya mabaya. 41. Na wanaojitetea baada ya kufanyiwa ubaya, hao hapana sababu ya kuwalaumu. 42 Hakika lawama ipo tu kwa wale wanaowafanyia watu ubaya, na wakafanya uhalifu katika ardhi kwa kuvunja haki na uadilifu. Hao watapata adhabu iliyo chungu. 43. Na anayesubiri na akasamehe, hakika hilo ndio azimio la ujasiri katika mambo.

44. Na ambaye Mwenyezi Mungu amemwacha apotee, hatakuwa na wa kumlinda baada yake. Na utawaona waliozama katika kutenda dhambi watakapoiona adhabu wanasema: Je, ipo njia ya kurudi? 45. Na utawaona wanapelekwa kwenye adhabu wakiwa wamenyenyekea kwa unyonge. Wanatazama (huku na huko) wakitupia jicho la kificho. Na walioamini watasema: Hakika waliopata hasara

ni hao waliohasiri nafsi zao na ndugu zao Siku ya Kiyama. Lo! Hakika wafanyao mabaya watakuwa katika adhabu ya kudumu. [46.] Wala hawana wa kuwalinda watakaowanusuru asiyekuwa Mwenyezi Mungu. Na ambaye Mwenyezi Mungu amemepoteza, basi hana njia yoyote.

[47.] Mwitikieni Mola Wenu kabla haijafika siku isiyoepukika itokayo kwa Mwenyezi Mungu. Siku hiyo hamtakuwa na pa kujihifadhi wala hamtakuwa na nafasi ya kupinga. [48.] Na wakipuuza, basi hatukukupeleka kwao ili uwe msimamizi wa matendo yao. Jukumu lako ni kufikisha ujumbe tu. Kwa hakika tunapomwonjesha mtu rehema kutoka Kwetu, huifurahia. Lakini akipatwa na shida kwa sababu ya ilivyotanguliza mikono yao, basi hakika mtu huyu anakana fadhila.

[49.] Ufalme wa mbingu na ardhi ni wa Mwenyezi Mungu; anaumba apendavyo, anamtunukia amtakaye watoto wa kike, na anamtunukia amtakaye watoto wa kiume. [50.] Au huwachanganya wanaume na wanawake, na akamfanya amtakaye tasa. Hakika Yeye ni Mjuzi, Mwenye uweza.

[51.] Na haiwezekani kwa mwanaadamu kwamba Mwenyezi Mungu aseme naye ila kwa kwa njia ya Wahyi (ufunuo), au kwa nyuma ya kizuizi, au kumtuma Mjumbe. Naye humfunulia ayatakayo kwa idhini Yake. Hakika Yeye ni Mtukufu, Mwenye hekima. [52.] Na ndiyo hivyo, tumekupelekea Jibril kwa njia ya ufunuo (Wahyi), kwa amri yetu. Hukuwa unajua Kitabu ni nini wala imani. Lakini tumeifanya (Qur'an) iwe nuru ambayo kwayo tunamwongoza tumtakaye katika waja Wetu. Na hakika wewe unaongoza kwenye njia iliyonyooka. [53.] Njia ya Mwenyezi Mungu ambaye ni Vyake vilivyomo mbinguni na ardhini. Ndiyo! Mambo yote yanarudi kwa Mwenyezi Mungu.

43. Sura Az-Zukhruf

# SURA KUHUSU MAPAMBO

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 *Ha-mim*.

2 Naapa kwa Kitabu kinachobainisha! 3 Hakika tumeifanya
Qur'an kwa lugha ya kiarabu ili mfahamu. 4 Na hakika hiyo
imo katika Mama wa Kitabu kilichoko Kwetu, ni yenye
kutukuzwa, yenye wingi wa hekima.

5 Je, tuache kuwakumbusha kabisa kwa kuwa ninyi ni watu
mliopita mipaka (katika kukanusha)? 6 Na manabii wangapi
tulikwisha watuma kwa watu wa zamani! 7 Na hakuwepo
Nabii yeyote aliyewafikia isipokuwa walimfanyia kejeli.
8 Na tuliwaangamiza waliokuwa na nguvu zaidi yao hao, na
ndiyo vigano vya wa watu wa zamani vimekwishapita.

9. Na ukiwauliza: Nani aliyeumba mbingu na ardhi? Bila
ya shaka watasema: Kaziumba Mwenye nguvu, Mjuzi.
10. Ambaye amewafanyia ardhi kuwa (kama) tandiko, na
akawafanyia ndani yake njia mpate kuongoka. 11. Na ambaye
huteremsha (wakati baada ya wakati) kutoka mbinguni maji
kwa kiasi maalum, na kwa hayo tukaileta kwenye uhai nchi
iliyokufa. Na hivyo ndivyo mtakavyotolewa (kutoka ardhini).
12. Na ambaye ameumba mume na mke katika kila kitu. Na
akawafanyia merikebu na wanyama mnaowapanda. 13. Ili
mkae vizuri migongoni mwao. Kisha mkumbuke neema za
Mola Wenu mnapokaa sawa sawa juu yao hao mnaowapanda
na mseme: ametakasika aliyemfanya huyu atutumikie na

tusingeliweza kufanya haya wenyewe. [14.] Na hakika sisi tutarudi kwa Mola Wetu.

[15.] Hata hivyo, wanampa Yeye sehemu (ya uungu) kwa kushirikiana na baadhi ya waja wake! Kwa hakika mwanadamu ni mtovu wa shukrani waziwazi. [16.] Au amejichukulia watoto wa kike katika vile alivyoviumba, na akawachagulia nyinyi watoto wa kiume? [17] .Na mmoja wao akipewa habari (ya kuzaliwa) yule anayemchukulia kuwa mfano wa Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema (mtoto wa kike), uso wake hugeuka mweusi akawa amejaa hasira moyoni. [18.] Ati anayesetiwa kwa mapambo, akawa katika mabishano hana hoja ya wazi (anaweza kushirikishwa na Mungu)? [19.] Na wakawafanya malaika, ambao ni waja wa Mwenyezi Mungu, ni wanawake! Kwani wameshuhudia kuumbwa kwao? Ushahidi wao utaandikwa na wataulizwa.

[20.] Na husema: Angependa (Mwenyezi Mungu) Mwingi wa Rehema tusingewaabudu hao! Hawajui chochote juu ya hilo (la mapenzi ya Mungu). Hawana ila kusema uwongo tu. [21.] Au tuliwapa Kitabu kabla ya hiki, ndiyo wanakishikilia hicho? [22.] La! Wao (hukariri tu) kusema: ‘Sisi tuliwakuta baba zetu juu ya dini hii nasi twafuata mwongozo wa nyayo zao! [23.] Ndiyo hivyo hivyo, hatukumtuma mwonyaji kabla yako kwenye mji wowote ila mabwanyeye wa mji walisema: ‘sisi tuliwakuta baba zetu katika dini hii nasi twafuata nyayo zao. [24.] Akasema (mwonyaji): Hata nikiwaletea muongozo bora zaidi kuliko mliyowakuta nayo baba zenu? Wakasema: La! Sisi tunayakataa tu hayo mliyotumwa. [25.] Basi tukawalipizia. Angalia ulikuwaje mwisho wa waliokataa (ukweli)!

[26.] Kumbuka pale Ibrahim alipomwambia baba yake na watu wake: Hakika mimi ninajitenga mbali na hivyo

mnavyoviabudu. 27. Isipokuwa yule aliyeniumba, kwani Yeye ataniongoza. 28. Na akalifanya liwe neno lenye kubaki kwa wale waliokuja baada yake, ili waweze kurejea (kwa Mwenyezi Mungu). 29. Basi tukawapa starehe hawa na baba zao mpaka ukweli ukawajia na Mtume aliyeweka wazi (mambo). 30. Na hatimaye ukweli ulipowafikia, wakasema: Huu ni uchawi, na sisi hakika tunaukataa.

31. Na wakasema: Kwa nini hii Qur’an haikuteremshwa kwa mtu mwenye hadhi katika moja ya miji hii miwili? 32. Kwani wao ndio wanaogawa rehema za Mola Wako Mlezi? Sisi ndio tumewagawanyia baina yao maisha yao katika uhai wa duniani, na tukawainua baadhi yao juu ya wengine kwa vyeo, ili baadhi yao wawatumikie wengine. Na rehema za Mwenyezi Mungu ni bora kuliko hivyo wanavyovikusanya. 33. Na lau isingekuwa kwamba watu wote (wangetaka) kuwa aina moja, tungeliwfanya wanaomkufuru (Mwenyezi Mungu) Mwingi wa rehema nyumba zao ziwe na dari za fedha, na ngazi zao pia wanazopandia. 34. Na milango ya nyumba zao na vitanda wanavyoegemea juu yake (vya fedha). 35. Na mapambo. Na hayo yote si chochote ila ni starehe ya maisha ya dunia tu, na Akhera iliyoko kwa Mola Wako Mlezi ni ya wamchao Mungu.

36. Na yeyote anayejitoa kwenye kumtaja (Mwenyezi Mungu) Mwingi wa rehema, tutamwekea Shetani ndiye rafiki yake anayemwandama popote. 37. Na hao (mashetani) huwazuia wao na kufuata njia (ya sawa) lakini wenyewe wanadhani kuwa ni wenye kuongozwa sawa. 38. Hatimaye anapotujia atasema (kwa rafiki shetani); ‘Laiti kati yangu na wewe kungekuwa na umbali wa (kama) mashariki na magharibi! Rafiki mbaya mno wewe!’ 39 Na kwa kuwa

mlikuwa wahalifu, haitawafaa kitu hii leo kwamba nyinyi mnashirikiana katika adhabu.

40. Je, unaweza kumfanya kiziwi asikie, au kumwelekeza kipofu na ambaye tayari yuko ndani ya upotevu wa wazi?
41. Na hata tukikuondoa, Sisi tutalipiza kisasi kwao. 42. Au tukuoneshe tuliyowaahidi. Nasi bila ya shaka tuna uwezo juu yao. 43. Basi wewe yakamate uliyopewa. Hakika wewe uko kwenye Njia iliyonyooka. 44. Na hakika hii (Qur'an) ni ujumbe kwako na kwa watu wako. Na mtakuja ulizwa. 45. Na waulize Mitume wetu tuliowatuma kabla yako: Je, tulifanya miungu mingine iabudiwe badala ya (Mwenyezi Mungu) Mwingi wa rehema?

46. Na hakika tulimtuma Musa kwa Ishara Zetu aende kwa Firauni na machifu wake, na akasema: Hakika mimi ni Mtume wa Mola Mlezi wa walimwengu wote! 47. Lakini alipowajia na Ishara Zetu, wakawa wanazifanyia dhihaka.
48. Na tukawaonesha ishara baada ya ishara, kila moja ni kubwa zaidi ya nyingine. Na tukawatia nguvuni kwa kuwapa adhabu ili warejee. 49. Na wakasema: Ewe mchawi! Tuombee kwa Mola Wako kutokana na alivyokuahidi. Hapo sisi tutakuwa wenye kuongoka. 50. Basi tulipowaondolea adhabu hiyo, mara wakavunja ahadi yao.

51. Na Firauni akajinadi kwa watu wake akisema: Enyi watu wangu! Kwani huu ufalme wa Misri si mali yangu? Na hii mito ipitayo mbele yangu, hamuoni? 52. Je mimi siyo bora kuliko huyu aliye dhalili, wala hawezi kusema vizuri?
53. Angalau basi angevikwa bangili za dhahabu, au akaja akiandamana na Malaika? 54. Basi akawasimanga watu wake, nao wakamtii. Kwa hakika hao walikuwa watu mafasiki.
55. Hatimaye walipotukasirisha tukawalipizia;

tukawagharikisha wote. 56. Tukawafanya watu wa kale na
(wa kutolewa) mfano kwa watu wa vizazi vilivyokuja.
57. Wakati Isa (Yesu) mwana wa Maryam alipotolewa
mfano, Lo! Watu wako walipaaza sauti (za kejeli) kwa
hilo. 58. Wakasema: Si miungu yetu ni bora kuliko huyo?
Hawakutoa mfano huo ila kwa ubishi tu. Hakika hao ni watu
wagomvi! 59. Hakuwa Isa ni kitu kingine isipokuwa mtumishi
(wetu) tuliyemneemesha na kumfanya ni mfano kwa Wana
wa Israili. 60. Na kama tungelipenda tungewafanya Malaika
miongoni mwenu, mkabadilishana urithi wa dunia. 61. Na
kwa hakika huyo (Isa) ni dalili za kukaribia Kiyama. Basi
usitie shaka juu yake (Kiyama), na nifuateni. Hii ndiyo njia
iliyonyooka. 62. Wala asiwazuie Shetani. Hakika yeye ni adui
yenu wa dhahiri.
63. Na alipokuja Isa (Yesu) na dalili zilizo wazi, alisema:
'Nimewaletea hekima, na ili niwafafanulie baadhi ya yale
mnayotofautiana. Hivyo mcheni Mwenyezi Mungu, na
mnitii. 64. Hakika Mwenyezi Mungu ndiye Mola Wangu
Mlezi, na pia Mola Wenu Mlezi. Hivyo mwabuduni Yeye
tu. Hii ndiyo njia iliyonyooka. 65. Lakini vikundi miongoni
mwao wakazozana wao kwa wao. Ole wao walioasi kwa
adhabu ya siku chungu.
66. Je, nini wanangojea isipokuwa Kiyama kiwajie ghafla
na hali wao hawatambui? 67. Siku hiyo marafiki watakuwa
maadui, wao kwa wao, isipokuwa wamchao Mungu. 68. Enyi
waja Wangu! Leo hamtakuwa na khofu, wala hamtahuzunika.
69. Wale ambao waliziamini Ishara Zetu na wakawa Waislamu.
70. Ingieni kwenye Pepo, ninyi na wenza wenu katika hali
ya kufurahishwa. 71. Watapitishiwa sahani na vikombe vya
dhahabu. Na vitakuwamo ambavyo nafsi zinavipenda,

na macho yanavifurahia. Na nyinyi mtakaa humo milele. 72. Na hiyo ndiyo Pepo mliyorithishwa kwa yale mliyokuwa mkiyafanya. 73. Mtapata humo matunda mengi katika hayo mtayala.

74. Hakika wahalifu watakaa milele katika adhabu ya Jahannamu. 75. Hawatapumzishwa na adhabu hiyo, na wao humo watalemewa. 76. Wala Sisi hatukuwadhulumu, bali wao ndio waliokuwa madhalimu. 77. Na watapiga kelele: Ewe Malik! Si atutoe uhai tu Mola Wako?! Atasema: Nyie ni wa kukaa humo humo! 78 Kwa yakini tuliwaletea Haki, lakini wengi katika nyinyi mlikuwa mnaichukia Haki. 79 Au wamekata shauri jambo? Bali ni Sisi ndio tunaopitisha. 80 Au wanadhani kwamba hatusikii siri zao na minong’ono yao? Ndiyo! (Tunasikia). Na wajumbe Wetu wapo karibu nao, wanayaandika.

81. Sema: Ingelikuwa kweli (Mwenyezi Mungu) Mwingi wa rehema ana mwana, basi mimi (pamoja na hivyo) ningelikuwa wa kwanza kumwabudu. 82. Kutakata na mabaya ni kwa Mola wa mbingu na ardhi, Mola wa Arshi, na hayo wanayomsifia. 83. Basi waache wapige porojo, wakicheza, mpaka wakutane na hiyo siku yao wanayoahidiwa.

84. Na Yeye Ndiye Mungu mbinguni, na Ndiye Mungu katika ardhi. Naye Ndiye Mwenye hekima nyingi, Mwenye ujuzi wa yote. 85. Na ametukuka Mwenye ufalme wa mbingu na ardhi na viliyomo kati yake. Na uko Kwake ujuzi wa (wakati wa) Kiyama Na Kwake Yeye mtarudishwa.

86. Wala hao wanaowaomba kinyume chake Yeye, hawana madaraka ya kumwombea (yeyote), isipokuwa anayetoa ushahidi wa kweli tu (ndiye atapewa madaraka). Nao wanamjua. 87. Na ukiwauliza ni nani aliyewaumba?

Bila ya shaka watasema: Mwenyezi Mungu! Vipi basi
wanadanganywa na kuuacha ukweli? 88. Na usemi wake
(mtume) ni: ‘Ewe Mola Wangu Mlezi! Hakika hawa ni watu
wasioamini’. 89. Basi (ewe Mtume) achana nao, uwaambie
kwaheri! Muda mfupi ujao watajua.

## 44. Sura Ad-Dukhaan

# SURA YA MOSHI

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 *Ha Miim.*

2 Naapa kwa Kitabu kinachobainisha! 3 Hakika
tumekiteremsha katika usiku uliobarikiwa. Hakika Sisi ni
waonyaji (dhidi ya mabaya). 4 Katika huo hubainishwa kila
jambo la hekima. 5 Ni amri itokayo Kwetu. Hakika Sisi
(daima) ni Wenye kutuma (ujumbe). 6 Ni rehema itokayo
kwa Mola Wako. Hakika Yeye ni Mwenye kusikia, Mwenye
kujua. 7 Mola wa mbingu na ardhi na vilivyomo kati yake,
ikiwa nyinyi mna yakini. 8 Hakuna mungu ila Yeye; anatoa
uhai na anafisha. Mola Wenu Mlezi na Mola wa baba zenu
wa mwanzo. 9 Lakini wao wamo katika shaka, wanacheza.
10 Basi ingoje siku ambayo mbingu itatoa moshi
utakaoonekana wazi. 11 Utakaowafunika watu. Hii ni adhabu
chungu! 12 (Watalia): ‘Ewe Mola Wetu Mlezi! Tuondolee
adhabu hii. Kwa kweli sisi ni waumini! 13 Ujumbe utawafaa
nini (hivi sasa)? Na hali alikwishawafikia Mtume akiwaelezea
mambo kwa uwazi kabisa? 14 Lakini wakamgeuzia nyuso

zao, wakasema: ‘amefunzwa huyo, mwenda wazimu’.
15 Tutaiondoa adhabu kidogo, (lakini) nyinyi kwa yakini
mtarudia (mambo yenu). 16 Siku moja tutakayowashambulia
shambulio kubwa, (Ndipo) Sisi tutawalipiza mliyofanya.

17 Na hakika kabla yao tuliwajaribu watu wa Firauni, na
aliwafikia Mtume Mtukufu. 18 (Akiwaambia): Nipeni waja
wa Mwenyezi Mungu; kwa hakika mimi kwenu ni Mtume
mwaminifu. 19 Na msijifanye wakubwa kuliko Mwenyezi
Mungu. Hakika mimi ninakuja na madaraka ya wazi (kutoka
kwa Mungu). 20 Nami nimeomba hifadhi kwa Mola Wangu
Mlezi ambaye pia ni Mola Wenu, ili msinidhuru. 21 Na ikiwa
hamniamini, basi (kwa uchache) jitengeni nami.

22. (Lakini wakawa wa shari) Ndipo akamwomba Mola
Wake Mlezi kuwa ‘watu hawa wamejikita katika uovu’.
23. (Akajibiwa) Ondoka utembee na waja Wangu usiku. Kwa
vyovyote mtafuatwa. 24. Na iache bahari (hivyo hivyo) kama
mtaro, hakika wao ni jeshi litakalozamishwa. 25. Ni bustani
ngapi na chemchemi ngapi za maji waliziacha nyuma! 26. Na
mashamba (ya nganu) na majumba ya fahari! 27. Na utajiri
na starehe walizokuwa wakizifurahia! 28. Ndivyo hivyo
(ulivyokuwa mwisho wao) na tukawarithisha vitu hivyo
watu wengine. 29. Si mbingu iliwalilia wala ardhi na hata
hawakupewa muda tena.

30. Na tukawa tumewaokoa wana Israeli katika adhabu
ya kuwadhalilisha. 31. Ya Firauni. Hakika yeye alikuwa
jeuri mno miongoni mwa wenye kupindukia. 32. Na hakika
tuliwachagua (Wana Israel) miongoni mwa watu wengine,
kutokana na ujuzi wetu. 33. Na tukawapa ishara ambazo ndani
yake kuna mtihani wa wazi.

34. Hakika hawa (Maqureish) wanasema: 35. Hakuna

chochote isipokuwa (hiki hiki) kifo chetu cha kwanza, na
wala sisi hatufufuliwi tena! 36. (Au sivyo) Basi warudisheni
mababu zetu, kama mnavyosema ni kweli! 37. Je, wao ni bora
au watu wa Tubba' na waliokuwa kabla yao? Tuliwaangamiza,
kwa sababu walikuwa wafanya madhambi.

38. (Wala) hatukuziumba mbingu na ardhi na vilivyomo
kati yake kwa mchezo. 39. Hatukuviumba isipokuwa kwa
(lengo la) haki. Lakini wengi wao hawajui. 40. Hakika siku ya
Uamuzi ni wakati uliowekwa kwa wote. 41. Siku ambayo rafiki
hatamfaa rafiki yake kwa chochote, wala hawatanusuriwa.
42. Isipokuwa yule ambaye Mwenyezi Mungu atamrehemu.
Hakika Yeye ndiye Mwenye nguvu, Mwenye kurehemu.

43. Hakika Mti wa Zaqqum. 44. Utakuwa ni chakula
cha mwenye dhambi. 45. Kama shaba nyeupe, hutokota
matumboni, 46. Kama kutokota kwa maji ya moto.
47. (Itaamriwa): 'Mkamateni na mburuzeni mpaka katikati
ya Jahannamu!' 48. Kisha mmwagieni juu ya kichwa chake
adhabu ya maji yanayochemka. 49. Onja! Hakika wewe ndiye
mwenye nguvu, mtukufu! 50. Hakika haya ndiyo mliyokuwa
mkiyatilia shaka.

51. Ama wenye kumchamungu watakua katika mahali pa
amani. 52. Katika mabustani na chemchemi. 53. Watavaa hariri
nyepesi na hariri nzito wakiwa uso kwa uso. 54. Ndio kama
hivyo! na tutawaoza wenza wenye macho makubwa, mazuri,
yenye kung'aa. 55. Humo wataweza kuagizia kila aina ya
matunda wakiwa na Amani. 56. Humo hawataonja mauti ila
mauti ile ya kwanza, na atawalinda na adhabu ya Jahannamu.
57. Ni fadhila zitokazo kwa Mola Wako. Huko ndiko kufuzu
kukubwa.

58. Basi tumeifanya nyepesi hii (Qur'an) kwa lugha yako,
ili wapate kuzingatia maonyo. 59. Ngoja tu, na wao watangoja.

## 45. Sura Al-Jathiya

## SURA YA KUPIGA MAGOTI

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 *Ha mim.*

2 Uteremshwaji wa Kitabu hiki umetoka kwa Mwenyezi
Mungu, Mwenye nguvu, Mwenye hikima. 3 Hakika katika
mbingu na ardhi kuna Ishara nyingi (za kuwepo Allah) kwa
wale wanaotaka kuamini. 4 Na katika namna mlivyoumbwa,
na pia katika wanyama aliowatawanya (huku na huko) zimo
ishara kwa watu watakao kupata yakini. 5 Na katika kupishana
kwa usiku na mchana pia, na katika riziki anayoiteremsha
Mwenyezi Mungu kutoka mbinguni, na kwayo akaipa uhai
ardhi baada ya kufa kwake. Na (katika) mabadiliko ya upepo,
ni Ishara kwa watu wanaotaka kufahamu. 6 Hizo ni Ishara
za Mwenyezi Mungu tunakuorodhoshea kwa kweli. Basi ni
ujumbe gani watakaouamini baada ya (kumkana) Mwenyezi
Mungu na Ishara Zake?

7 Ole wake kila mtunga uongo mwenye dhambi!
8 Anayesikia Aya za Mwenyezi Mungu akisomewa, lakini
akawa mkaidi, akijivuna kana kwamba hakuzisikia. Basi
mbashirie adhabu chungu! 9 Na anapojua kitu katika
Aya Zetu hukifanyia dhihaka. Hao ndio watakaokuwa na
adhabu ya kufedhehesha. 10 Mbele yao ipo Jahannamu. Na

waliyoyachuma hayatawafaa kitu, wala wale waliowafanya
wawe walinzi wao badala ya Mwenyezi Mungu. Na watapata
adhabu kubwa. 11 Huu ni mwongozo. Na wale waliozikataa
Ishara za Mola Wao watapata adhabu yenye maumivu
itokanayo na ghadhabu.

12. Mwenyezi Mungu Ndiye aliyeifanya bahari
iwatumikie, ili humo zipite merikebu kwa amri Yake, na ili
mtafute fadhila Yake, na mpate kushukuru. 13. Na amefanya
viwatumikie vilivyomo mbinguni na vilivyo katika ardhi,
vyote kutoka Kwake. Hakika katika hayo zimo Ishara kwa
watu wanaotafakari.

14. Waambie walioamini wawasamehe wale wasiozitarajia
neema za Mwenyezi Mungu. Ni Yeye ndiye (mhusika) wa
kuwalipa watu kwa yale waliyoyatenda. 15. Anayetenda mema
basi anajitendea (Kwa faida yake) mwenyewe, na anyetenda
uovu basi (madhara) ni juu yake; kisha mtarudishwa kwa
Mola Wenu.

16. Na hakika tuliwapa Wana wa Israeli Kitabu na madaraka
na Utume, na tukawaruzuku vitu vizuri, na tukawapa kipa
umbele juu ya walimwengu wegine. 17. Na tukawapa ishara
za wazi katika jambo (la dini). Hawakutofautiana (juu
ya hili) isipokuwa baada ya kuwajia ujuzi, kwa sababu
ya ushindani baina yao. Hakika Mola Wako atahukumu
baina yao Siku ya Kiyama katika waliyokuwa wakizozana.
18. Kisha tukakuweka wewe juu ya njia sahihi ya dini.
Ifuate, wala usifuate matamanio ya wasiojua. 19. Kwa hakika
hao hawatakufaa kitu mbele ya Mwenyezi Mungu. Na
hakika wafanyao mabaya wanalindana wao kwa wao. Ama
Mwenyezi Mungu Yeye ni mlinzi wa wachamungu. 20. Hizi

ni dalili zilizo wazi kwa watu wote, na ni mwongozo, na rehema kwa watu wanye yakini.

[21.] Je, wanadhani wafanyao mabaya kuwa tutawachukulia kama wale walioamini na wakatenda mema, wawe sawa uhai wao na kufa kwao? Ni vibaya mno wanavyohukumu. [22.] Na Mwenyezi Mungu ameziumba mbingu na ardhi kwa lengo la haki. Na ili kila nafsi ilipwe yale iliyoyachuma. Nao hawatadhulumiwa.

[23.] Je, umemwona aliyeufanya uraibu wake kuwa ndiyo mungu wake? Mwenyezi Mungu, kwa vile ajua hivyo, alimwacha apotee, akapiga muhuri katika masikio yake na moyo wake, na akaweka pazia katika macho yake? Basi nani atamwongoza baada ya Mwenyezi Mungu? Hamkumbuki?

[24.] Na walisema: Kuna nini zaidi isipokuwa huhu huu uhai wetu wa hapa duniani? Tunakufa na tunaishi….hakuna chochote kinachosababisha tufe isipokuwa (kupita) wakati tu. Wasemao hivyo, kamwe hawana ujuzi wa hilo, bali hukisia tu. [25.] Na wakisomewa Aya Zetu zilizo wazi hawana hoja ila kusema: Waleteni baba zetu, ikiwa nyinyi ni wakweli. [26.] Sema: Mwenyezi Mungu anawapa uhai, kisha anawafanya mfe, kisha anawakusanya Siku ya Kiyama, haina shaka hiyo, lakini watu wengi hawajui.

[27.] Na ni wa Mwenyezi Mungu ufalme wa mbingu na ardhi. Na siku kitaposimama Kiyama, siku hiyo watakuwa katika hasara wale wanaoeneza uwongo. [28.] Na utauona kila umma umepiga magoti. Kila umma utaitwa kwenye kitabu chake: leo mtalipwa mliyokuwa mkiyatenda. [29.] Hiki kitabu Chetu kinasema juu yenu kwa haki. Hakika Sisi tulikuwa tukiyanukuu yale mliyokuwa mkiyatenda.

[30.] Ama wale walioamini na wakatenda mema, Mola Wao

Mlezi atawaingiza katika rehema Yake. Huko ndiko kufuzu
kulio wazi. 31. Na ama wale waliokufuru: Kwani hamkuwa
mkisomewa Aya Zangu nanyi mkawa na kiburi, na mkawa
watu waovu? 32. Na ilipokuwa ikisemwa kwamba ahadi
ya Mwenyezi Mungu ni kweli, na Kiyama hakina shaka
kutokea….Nyinyi mlikuwa mkisema: ‘hatujui, ni nini
Kiyama hasa, tunadhania ni fikra tu, lakini hatuna uhakika!’

33. Na ubaya wa waliyoyatenda utawadhihirikia, na
yatawazunguka waliyokuwa wakiyafanyia mzaha. 34. Na
itasemwa: Leo tunawasahau kama mlivyosahau mkutano
wa siku yenu hii; na mahali penu ni Motoni, wala hamna
wa kuwanusuru. 35. Hiyo ni kwa sababu nyinyi mlizifanyia
mzaha Aya za Mwenyezi Mungu; na maisha ya dunia
yakawadanganya. Basi leo hawatatolewa humo wala hao
hawatakubaliwa udhuru.

36. Basi sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu, Mola
wa mbingu, na Mola wa ardhi, Mola wa walimwengu wote.
37. Na utukufu ni Wake, mbinguni na katika ardhi, Naye ni
Mwenye nguvu, Mwenye hekima.

## 46. Sura Al-Ahqaf

## SURA YA NJIA ZILIZOPINDA ZA JANGWANI

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 *Ha miim.*

2 Uteremshwaji wa Kitabu hiki umetoka kwa Mwenyezi
Mungu, Mwenye nguvu, Mwenye hikima. 3 Hatukuziumba

mbingu na ardhi na vilivyomo baina yake ila kwa lengo la haki na kwa muda uliowekwa. Na wale waliokufuru wanayapuuza yale wanayoonywa.

4 Sema: Je, mnawaona wale mnaowaomba badala ya Mwenyezi Mungu? Nionesheni wameumba nini katika ardhi; au wana shirika katika mbingu? Nileteeni Kitabu kilichokuwa kabla ya hiki, au mabaki yoyote ya elimu, ikiwa mnasema kweli. 5 Na ni nani mpotofu mkubwa kuliko yule anayeomba asiyekuwa Mwenyezi Mungu, ambaye hatamjibu mpaka Siku ya Kiyama, Na wala hao hawatambui maombi yao? 6 Na hapo watakapokusanywa watu watakuwa maadui zao, na wataikataa ibada yao.

7. Na wanaposomewa Aya Zetu zilizo wazi, wale waliokufuru husema juu ya ukweli unapowajia: 'Huu ni uchawi ulio wazi'. 8. Au wanasema: Ameizua? Sema: Ikiwa nimeizua mimi, basi nyinyi hamwezi kunifaa chochote mbele ya Mwenyezi Mungu. Yeye anajua zaidi hayo mnayoropokwa; anatosha kuwa shahidi baina yangu na nyinyi. Na Yeye ni Mwingi wa Maghufira, Mwenye kurehemu.

9. Sema, mimi si kioja (mpya) miongoni mwa Mitume. Wala sijui nitakavyofanywa mimi wala nyinyi. Mimi nafuata niliyopewa Wahyi tu, wala mimi si chochote ila ni mwonyaji, mwenye kubainisha. 10. Sema: Mwaonaje ikiwa (mafunzo) haya kweli yametoka kwa Mwenyezi Mungu, nanyi mmeyakataa. Na akashuhudia shahidi miongoni mwa Wana wa Israeli juu ya kufanana haya (na mafunzo yaliyopita), naye akaamini na nyie mkakaidi…. (si mtakuwa hatarini)? Hakika Mwenyezi Mungu hawaongozi watu madhalimu.

11. Na waliokataa waliwaambia walioamini: Laiti hili lingekuwa jambo jema, wasingetutangulia sisi

(Kulikumbatia). Na walipokosa kuongoka kwayo wakasema:
Huu ni uzushi wa zamani.
12. Na kabla yake kilikuwapo Kitabu cha Musa,
chenye kuongoza na ishara ya huruma. Na hiki ni Kitabu
kinachothibitisha hicho, kwa lugha ya kiarabu, ili kiwaonye
watenda mabaya, na kiwe ni habari njema kwa watendao
mazuri. 13. Hakika wale waliosema: Mola Wetu ni
Mwenyezi Mungu; kisha wakawa na msimamo usiotetereka,
hawatakuwa na hofu, wala hawatahuzunika. 14. Hao ndio watu
wa Peponi, watakaa mille humo. Ni malipo kwa waliyokuwa
wakiyatenda.
15. Na tumemwamuru mwanadamu awafanyie wema
wazazi wake. Mama yake ameibeba mimba yake kwa
taabu, na akamzaa kwa taabu. Na kubeba mimba kwake
hadi kumwachisha ziwa ni miezi thalathini. Hata anapofika
kukomaa na akafikilia miaka arubaini, husema: Mola Wangu
Mlezi! Niwezeshe nishukuru neema Yako uliyonineemesha
na wazazi wangu, na nipate kutenda mema unayoyaridhia.
Na unitengenezee kizazi changu. Hakika mimi nimetubu
Kwako, na hakika mimi ni miongoni mwa Waislamu. 16. Hao
ndio tunaowatakabalia matendo yao mazuri waliyofanya, na
tunasamehe makosa yao. Watakuwa miongoni mwa watu wa
Peponi. Miadi ya kweli hiyo waliyoahidiwa.
17. Na ambaye amewaambia, wazazi wake Ah! Nanyi!
Hivi mnanitisha kuwa nitafufuliwa, na hali vizazi vingi
vimekwishapita kabla yangu?! Na wazazi wawili wakawa
wanaomba msaada Mwenyezi Mungu (huku wakimkanya
mwana wao): ‘Ole wako! Kuwa na Imani, kwa hakika ahadi
ya Mwenyezi Mungu ni kweli! Na yeye husema: Hayo si
chochote ila ngano za watu wa kale tu. 18. Hao ndio ambao

hukumu ya Mwenyezi Mungu imethibiti kuwa kweli juu yao, kama vile mataifa yaliyokwishapita kabla yao miongoni mwa majini na watu. Hakika hao watakuwa ni katika wale waliopata hasara.

19. Na wote watakuwa na daraja zao tofauti kwa mujibu wa waliyoyatenda, ili Mwenyezi Mungu awalipe (sawa sawa) kwa vitendo vyao bila ya kudhulumiwa. 20. Na siku wale waliokufuru watakapoletwa mbele ya Moto: 'Nyinyi mlikwisha maliza vitu vyenu vizuri katika maisha yenu ya dunia, na mkastarehe navyo. Basi leo mnalipwa adhabu ya fedheha kwa mlivyokuwa na kiburi huko duniani bila sababu, na kwa mlivyokuwa mkifanya maovu.

21. Na mtaje (Hud) wa kabila la Ad. Pale alipowaonya watu wake kwenye vichuguu vya mchanga -na kwa yakini waonyaji wengi walitokea kabla yake na baada yake-- kuwa msimwabudu isipokuwa Mwenyezi Mungu. Hakika mimi ninawahofia na adhabu ya siku iliyo kuu. 22. Wakasema: Je, umetujia ili ututenganishe na miungu yetu? Basi tuletee hiyo (adhabu) unayotuahidi ikiwa wewe ni miongoni mwa wasemao kweli. 23. Akasema: Hakika ujuzi (wa lini itakuja) uko kwa Mwenyezi Mungu tu. Mimi ninawafikishia niliyotumwa, lakini ninawaona kuwa ninyi ni watu mmezama katika ujinga.

24. Basi walipoliona wingu la mvua likipita mbinguni kuelekea kwenye mabonde yao, walisema: Wingu hili litatuletea mvua! Kumbe, hili ni katika yale mliyotaka yawajie haraka: ni upepo ndani yake imo adhabu chungu! 25. Unabomoa kila kitu kwa amri ya Mola Wake Mlezi. Ilipochomoza asubuhi kukawa hakuonekani kitu isipokuwa

(magofu) ya majumba yao tu. Hivyo ndivyo tunavyowalipizia
watu wakosefu.

26. Na hakika tuliwaweka vizuri siyo kama tulivyowaweka
nyie (Maqureish) tukawapa masikio, macho na nyoyo imara,
lakini hayakuwafaa kitu masikio yao, wala macho yao,
wala nyoyo zao, Kwani hao walikuwa wakizikataa Ishara
za Mwenyezi Mungu, na wakazungukwa gubi gubi na yale
waliyokuwa wakiyafanyia utani. 27. Na hakika tuliviangamiza
vijiji vilivyo jirani yenu (Makka) na tukazionesha alama
(ya hilo) kwa njia mbali mbali, ili huenda wakarudi (Kwa
Mwenyezi Mungu). 28. Basi mbona hawakuokolewa na
wale waliowaabudu kama miungu badala ya Mwenyezi
Mungu, ati ndio njia ya kujikaribisha kwa Mwenyzi Mungu?
Bali waliwaacha patupu! Huo ndio uwongo na uzushi wao
waliokuwa wakiuzua.

29. Kumbuka wakati tulipolileta kwako kundi la Majinni
kusikiliza Qur'an. Walipoihudhuria wakaambiana: 'Kaeni
kimya msikilize! Na ilipokwishasomwa, walirejea kwa watu
wao kwenda kuwaonya. 30. Wakasema: Enyi kaumu yetu!
Sisi tumesikia Kitabu kilichoteremshwa baada ya Musa,
kinachosadikisha yaliyokuwa kabla yake, na kinachoongoza
kwenye ukweli na kwenye Njia iliyonyooka. 31. Enyi wau
wetu! Muitikieni Mwenye kulingania kwa Mwenyezi Mungu,
na mumwamini, Mwenyezi Mungu atawasamehe dhambi
zenu, na atawakinga na adhabu chungu. 32. Na asiyemwitikia
mlingania wa Mwenyezi Mungu, hawezi kutibua (mipango
ya Mungu) katika ardhi, wala hatakuwa na wenye kumlinda
asiyekuwa Yeye. Hao wamo katika upotovu ulio dhahiri.

33. Je, hawaoni kwamba Mwenyezi Mungu aliyeumba
mbingu na ardhi-- na hakuchoka kwa kuziumba-- ni Mwenye

uwezo wa kuwafufua wafu? Ndio! Hakika Yeye ni Mwenye
uwezo wa kila kitu. 34. Na siku makafiri watakapoletwa mbele
ya moto (wataulizwa) Je, hii si kweli? Watasema: Kweli!
Tunaapa kwa Mola Wetu Mlezi! (Sauti) Itasema: ‘Basi onjeni
adhabu kwa sababu ya kule kukataa kwenu’.

35. Basi subiri, kama walivyosubiri Mitume wenye
msimamo imara (wa kufikia lengo). Wala usiwahimizie (hao
Maquresh). Siku watakayoyaona waliyoahidiwa, itakuwa
kana kwamba hawakukaa (kaburini) ila saa moja tu mchana.
(Jukumu lako ni) Kufikisha tu! Kwani huangamizwa
mwingine yeyote zaidi ya waovu tu?

47. Sura Muhammad

# SURA MUHAMMAD

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 Wale waliomkana Mungu na wakazuia (watu na) njia ya
Mwenyezi Mungu, atayafanya Mwenyezi Mungu matendo
yao yapotee. 2 Na wale walioamini, na wakatenda mema,
na wakaamini aliyoteremshiwa Muhammad - nayo ni
kweli iliyotoka kwa Mola wao Mlezi- atawafutia maovu
yao na ataitengeneza hali yao. 3 Hayo ni kwa sababu wale
waliokufuru wamefuata upotovu, na walioamini wamefuata
ukweli uliotoka kwa Mola Wao Mlezi. Hivyo ndivyo
Mwenyezi Mungu anavyowafunza watu kwa kuwatolea
mifano.

4 Basi mnapokutana na waliomkana Mwenyezi Mungu
wapigeni shingo, mpaka mkiwadhoofisha wafungeni pingu.

Baada ya hapo (ni wakati wa) kuwafanyia hisani (kwa kuwaacha huru) au wajikomboe, hadi hapo vita vitulie. Ndio hivyo! Na lau angelitaka Mwenyezi Mungu angewashinda Yeye Mwenyewe, lakini hii ni kwa ajili ya awape nyie mtihani nyie kwa nyie. Na waliouawa katika njia ya Mwenyezi Mungu hatazipoteza amali zao. 5 Atawaongoza na awatengezee hali yao. 6 Na atawaingiza katika Pepo aliyowajulisha.

7. Enyi walioamini! Mkimnusuru Mwenyezi Mungu Naye atawanusuru na ataithibitisha miguu yenu. 8. Na waliomkana Mwenyezi Mungu, kwao ni maangamizo, na atayafanya matendo yao yapotee bure. 9. Hayo ni kwa sababu waliyachukia aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu, basi akayafanya matendo yao yawe bila faida yeyote. 10. Je, hawatembei katika ardhi wakaona ulikuwaje mwisho wa waliokuwa kabla yao? Mwenyezi Mungu aliwaangamiza. Na mwisho kama huo unawangoja wanaokana Mwenyezi Mungu. 11. Hayo ni kwa sababu Mwenyezi Mungu ni mwenye kuwalinda walioamini. Na makafiri hawana wa kuwalinda.

12. Hakika Mwenyezi Mungu atawaingiza walioamini na wakatenda mema katika Bustani ambazo hupita mito chini yake. Na waliomkana Mwenye Mungu hujifurahisha na hula kama walavyo wanyama. Na Moto ndio makazi yao. 13. Ni miji mingapi iliyokuwa na nguvu zaidi kuliko mji wako huu uliosababisha ufukuzwe. Tuliwateketeza na wala hawakuwa na wa kuwanusuru.

14. Hivi mtu aliye juu ya (njia) iliyo wazi kutoka kwa Mola Wake Mlezi ni kama mtu ambaye matendo yake mabaya anayaona ya kupendeza na wakafuata mapenzi yao tu? 15. Mfano wa Pepo waliyoahidiwa wenye takuwa ina mito ya maji yasiyoharibika, na mito ya maziwa isiyoharibika ladha

yake, na mito ya mvinyo yenye kuwafurahisha wanywao, na mito ya asali iliyosindikwa. Na wao humo watakuwa na kila namna ya matunda, na msamaha kutoka kwa Mola Wao Mlezi. Je, hao ni waweza kufananishwa na watakaokaa milele motoni, wakinyweshwa maji yanayochemka yatayokata utumbo wao vipande vipande?

16. Na wapo miongoni mwao wanaokusikiliza, mpaka wakiondoka kwako huwauliza waliopewa elimu: Amesema nini sasa hivi? Hao ndio ambao Mwenyezi Mungu amepiga muhuri juu ya nyoyo zao, na wakafuata mapenzi yao.
17. Lakini wale waliokubali uongofu (Mwenyezi Mungu) huwazidishia uongofu zaidi.

18. Kwani wanangojea jingine isipokuwa kiwafikie Kiyama kwa ghafla? Hakika alama zake zimekwishakuja. Na kitapowajia, maonyo wanayoonywa yatawafaa nini?
19. Hivyo jua kwamba hapana Mola ila Mwenyezi Mungu. Na omba maghufira kwa dhambi zako na za waumini wanaume na waumini wanawake. Na Mwenyezi Mungu anajua mahali penu pa kwenda na kurudi na mahali penu pa kukaa.

20. Na wanasema wale ambao wameamini: Kwa nini haiteremshwi Sura (inayotuhusu sisi)? Lakini inapoteremshwa Sura isiyo na utatanishi na vikatajwa ndani yake vita, utawaona wenye maradhi katika nyoyo zao wanakutazama mtazamo wa anayezimia kwa mauti. Kilicho bora zaidi kwao
…. 21. Utiifu na kauli njema. Na jambo likisha amuliwa, ingekuwa bora kwao kuwa wakweli kwa Mwenyezi Mungu.
22. Hivi itarajiwe kwenu kwamba mnapokuwa kwenye madaraka mtafanya uharibifu nchini na mtavunja uhusiano wenu na ndugu zenu? 23. Hao ndio ambao Mwenyezi Mungu amewalaani, na akawatia uziwi, na akawapofoa macho yao.

24. Kwa nini basi hawataki kwa dhati kuifahamu Qur'an, au kuna makufuli juu ya nyoyo zao? 25. Kwa hakika wanaorudi nyuma (kuritadi) baada ya kuwabainikia uwongofu, Shetani ndiye aliyewashawishi na akawajaza (matumaini ya uwongo). 26. Hayo ni kwa sababu waliwaambia wanaochukia aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu: 'Tutawatii katika baadhi ya jambo (hili). Na Mwenyezi Mungu anajua siri zao. 27. Basi itakuwaje Malaika watakakuwa wanachukua roho zao (wakati wa mauti) wakawa wanawapiga nyuso zao na makalio yao? 28. Hayo ni kwa sababu wao waliyafuata yaliyomchukiza Mwenyezi Mungu na wakachukia yanayomridhisha. Kwa hiyo (Mwenyezi Mungu) akafanya matendo yao yasiwe na faida yoyote.

29. Je, ambao wana maradhi nyoyoni mwao wanadhani kwamba Mwenyezi Mungu hataziweka wazi chuki zao? 30. Kama tungetaka tungekuonyesha hao na ungewatambua kwa alama zao. Lakini bila ya shaka utawajua kwa jinsi wanavyozungumza. Na Mwenyezi Mungu anavijua vitendo vyenu.

31. Na bila ya shaka tutawajaribu mpaka tuwajue wenye kukakamaa na kuwa na subira katika nyinyi. Nasi tutaujaribu (ujasiri wenu) unaozungumziwa. 32. Hakika ambao wamekana Mwenyezi Mungu na wakazuia (watu na) njia ya Mwenyezi Mungu na wakapingana na Mtume baada ya kuwabainikia uwongofu, hawatamdhuru Mwenyezi Mungu kwa lolote, na Mweyezi Mungu atayafanya matendo yao yasiwe na faida yeyote.

33. Enyi walioamini! Mtiini Mwenyezi Mungu, na mtiini Mtume; wala msiharibu amali zenu. 34. Hakika ambao wamekufuru na wakazuilia njia ya Mwenyezi Mungu, kisha

wakafa na hali wanamkana Mungu, Mwenyezi Mungu hatawasamehe. 35. Kamwe msiwe wanyonge wa kukata tamaa na kuomba suluhu, ilhali nyie ndio mtakaoshinda. Na Mwenyezi Mungu Yuko pamoja nanyi, Wala hatawanyima malipo ya vitendo vyenu.

36. Hakika uhai wa duniani ni mchezo na pumbao. Na mkiamini na mkajikinga na uovu, atawapa ujira wenu, Wala hawataki (muache) mali zenu. 37. Endapo atawataka (mali) hizo zote, na akawasisitiza, mtakuwa wachoyo, na atatoa undani wa chuki zenu. 38. Lo! Nyinyi ndio mnaitwa mtoe katika njia ya Mwenyezi Mungu, lakini wapo katika nyinyi wanaofanya uchoyo. Na anayefanya uchoyo basi anajifanyia uchoyo huo mwenyewe. Na Mwenyezi Mungu ni Mkwasi, na nyinyi ndio wahitaji. Na mkigeuka atawaleta watu wengine badala yenu, nao hawatakuwa kama nyinyi!

## 48. Sura Al-Fat'h

# SURA YA USHINDI

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye urehemu.

1 Hakika tumekupa wewe ushindi wa dhahiri. 2 Ili Mwenyezi Mungu akusamehe makosa yako, yaliyotangulia na yajayo. Na akutimizie neema Zake, na akuongoze katika njia iliyonyooka. 3 Na ili Mwenyezi Mungu akunusuru nusura yenye nguvu.

4 Yeye Ndiye aliyeteremsha utulivu katika nyoyo za waumini ili wazidi imani juu ya imani yao. Na ni ya Mwenyezi Mungu majeshi ya mbinguni na ardhini, na Mwenyezi

Mungu ni Mwenye ujuzi, Mwenye hikima. 5 Ili awaingize
waumini wanaume na waumini wanawake katika Bustani
ambazo hupita mito chini yake, wakae milele humo, na
awafutie maovu yao. Na huko ndiko kufuzu kukubwa mbele
ya Mwenyezi Mungu. 6 Na awaadhibu wanafiki wanaume na
wanafiki wanawake, na Mapagani wanaume na Mapagani
wanawake, wanaomdhania Mwenyezi Mungu dhana mbaya.
Ubaya utawageukia wao wenyewe, kisha Mwenyezi Mungu
awakasirikie, na awalaani, na awaandalie Jahannamu. Na
hayo ni marudio maovu kabisa. 7 Na Mwenyezi Mungu ana
majeshi ya mbinguni na ardhini. Na Mwenyezi Mungu ni
Mwenye ujuzi, Mwenye hikima.

8. Hakika tumekutuma uwe shahidi na mfikisha habari
njema, na muonyaji. 9. Ili mumwamini Mwenyezi Mungu na
Mtume Wake, na mumsaidie, na mumhishimu, na mumtakase
asubuhi na jioni. 10. Hakika wanaofunga makubaliano nawe,
kwa hakika ndiyo wamefunga makubaliano na Mwenyezi
Mungu. Mkono wa Mwenyezi Mungu uko juu ya mikono
yao. Basi avunjaye ahadi hakika anaivunja kwa kuidhuru
nafsi yake; na anayetekeleza aliyomwahidi Mwenyezi
Mungu, Mwenyezi Mungu atampa ujira mkubwa.

11. Watakuambia mabedui waliobaki nyuma (wasiende
vitani): zimetushughulisha mali zetu na familia zetu, basi
tuombee msamaha. Wanasema kwa ndimi zao yasiyokuwamo
nyoyoni mwao. Sema: Ni nani awezaye kuwasaidia chochote
kwa Mwenyezi Mungu akitaka kuwadhuru au akitaka
kuwanufaisha? Bali Mwenyezi Mungu anazo habari za
mnayoyatenda. 12. Lakini mlidhani kwamba Mtume na
waumini hawatarudi kabisa kwa familia zao. Nyoyo zenu
zikafanywa zilifurahie hili, na mkadhania dhana mbaya, kwa

vile nyinyi ni watu mliopotea katika kupenda mabaya. [13.] Na asiyemwamini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, basi kwa hakika tumewaandalia makafiri Moto mkali. [14.] Na ni wa Mwenyezi Mungu ufalme wa mbingu na ardhi. Humsamehe amtakaye, na humwadhibu amtakaye, na Mwenyezi Mungu ni Mwenye maghufira, Mwenye kurehemu.

[15.] Waliobaki nyuma watasema mnapoondoka kwenda kuchukua ngawira, 'acheni tuwafuate'! Wanataka kubadili maamuzi ya Mwenyezi Mungu. Sema: 'hamtatufuata kamwe'! Mwenyezi Mungu amekwishamua hivi hapo nyuma. Watasema: 'bali nyinyi mnatuonea wivu'! Hapana. Lakini wao hawafahamu isipokuwa kidogo tu (mambo haya).

[16.] Waambie walioachwa nyuma katika mabedui: Mtakujaitwa kwenda kupigana na watu wakali kwa vita; mpigane nao au wasalimu amri. Basi mkimtii, Mwenyezi Mungu atawapa ujira mzuri; na mkigeuka kama mlivyogeuka kwanza, atawaadhibu adhabu chungu. [17.] Kipofu hana lawama, wala kiguru hana lawama, wala mgonjwa hana lawama. Na mwenye kumtii Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, atamwingiza katika Mabustani ambayo hupita mito chini yake. Na atakayegeuka atamwadhibu adhabu chungu.

[18.] Kwa hakika Mwenyezi Mungu amewaridhia waumini walipofunga nawe makubaliano chini ya mti, na alijua yaliyomo nyoyoni mwao. Basi akateremsha utulivu juu yao, na akawalipa kwa kuwapa ushindi wa haraka. [19.] Na (pia) ngawira nyingi watakazozichukua. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mwenye hikima. [20.] Mwenyezi Mungu amewaahidi ngawira nyingi mtakazozipata. Basi amewatangulizia hii, na akaizuia mikono ya watu isiwafikie. Na ili hiyo iwe ni ishara kwa waumini, na ili awaongozeni

njia iliyonyooka. 21. Na nyingine hamjaweza kuzipata, lakini Mwenyezi Mungu amekwishazizingira. Na Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kila kitu.

22. Na lau makafiri wangelipigana nanyi basi bila ya shaka wangeligeuza migongo wakatimka, kisha wasingelipata wa kuwalinda wala wa kuwasaidia. 23. Kama hivi ndiyo mwenendo wa Mwenyezi Mungu (umeidhinishwa na Mungu) tangu zamani. Hutapata mabadiliko katika mwenendo wa Mwenyezi Mungu (aliouidhinisha). 24. Na Yeye Ndiye aliyeizuia mikono yao isiwafikie, na mikono yenu isiwafikie wao, katika bonde la Makka baada ya kuwapa nyie ushindi juu yao. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuyaona myatendayo.

25. Hao ndio waliokufuru na wakawazuia msiingie Msikiti Mtakatifu, na wakawazuilia wanyama wa kafara kufika mahala pao pa kuchinjwa. Na lau si wanaume waumini na wanawake waumini msiowajua, (kuhofiwa) kuwa mngewapondaponda kwa miguu yenu, mkapatikana na makosa ya jinai juu yao bila ya nyinyi kujua….(Mwenyezi Mungu angewaruhusu muingie kwa nguvu. Lakini amewazuia..) Ili amuingize amtakaye katika rehema Yake. Kama wangetengana (wasingechanganyika) bila ya shaka tungeliwaadhibu waliokufuru adhabu chungu kabisa.

26. Pale makafiri walipotia katika nyoyo zao mori, mori wa kijahili, Mwenyezi Mungu akateremsha utulivu juu ya Mtume wake na juu ya waumini, na akawafanya washikamane na moyo wa kujizuia, na wakawa wanastahiki na ndiyo wenyewe (wakafuata amri kwa utiifu). Na wao walikuwa ndio wenye haki nalo na wenye kustahili. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu.

27. Hakika Mwenyezi Mungu amemtimizia Mtume wake

ndoto yake kwa uhakika. Ya kwamba mtaingia Msikiti Mtakatifu, Inshallah, mkiwa na utulivu, na hali mmenyoa vichwa vyenu au mmepunguza nywele. Hamtakuwa na hofu. Alijua msiyoyajua. Zaidi ya hayo, akawapa ushindi wa haraka.

28. Yeye ndiye aliyemtuma Mtume Wake kwa (kufikisha) mwongozo na dini ya kweli, ili aipe ushindi juu ya dini zote. Na Mwenyezi Mungu anatosha kuwa Shahidi.

29. Muhammad ni Mtume wa Mwenyezi Mungu. Na wale walio pamoja naye, wana nguvu mbele ya makafiri, na wanahurumiana wao kwa wao. Utawaona wakirukuu na kusujudu wakitafuta fadhila na radhi za Mwenyezi Mungu. Alama zao ziko katika nyuso zao, kwa athari ya kusujudu. Huu ndio mfano wao katika Torat na mfano wao katika Injili (Gospel) ni kama mmea uliotoa chipukizi lake, kisha ukalitia nguvu, ukawa mnene, ukasimama juu ya shina lake wenyewe, ukawafurahisha wakulima. (Kwa sababu hiyo), makafiri wakajaa hasira dhidi yao. Mwenyezi Mungu amewaahidi walioamini na wakatenda mema katika wao maghufira na ujira mkubwa.

## 49. Sura Al-Hujurat

# SURA YA VYUMBANI

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 Enyi walioamini! Msitangulie mbele ya Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia, Mjuzi.

2 Enyi walioamini! Msinyanyue sauti zenu juu ya sauti ya
Nabii, wala msiseme naye kwa kelele kama mnavyosemezana
nyinyi kwa nyinyi, zisije zikaporomoka (thawabu) za amali
zenu na hali hamtambui. 3 Kwa hakika wale wanaoshusha
sauti zao mbele ya Mtume wa Mwenyezi Mungu, hao ndio
ambao Mwenyezi Mungu amezipa nyoyo zao majaribio ya
uchamungu (zikafaulu). Hao watakuwa na maghufira na ujira
mkubwa. 4 Hakika ambao wanakuita nyuma ya vyumba,
wengi wao hawafahamu. 5 Kama wangengojea mpaka uwajie
nje ingelikuwa vizuri zaidi kwao. Na Mwenyezi Mungu ni
Mwingi wa maghufira, Mwenye kurehemu.

6. Enyi walioamini! Akiwajia mtu mbaya na habari yoyote
hakikisheni kwanza (ukweli wake); msije mkawadhuru watu
bila kujua, mkawa wenye kujuta kwa mliyoyatenda. 7. Na
jueni kuwa yuko kati yenu Mtume wa Mwenyezi Mungu.
Lau angeliwatii katika mambo mengi, bila ya shaka mngepata
matatizo. Lakini Mwenyezi Mungu amewafanya mpende
imani, na akaipamba katika nyoyo zenu, na akawafanya
mchukie ukafiri na upotevu na uasi. Hao ndio walioongoka.
8. Kwa hisani ya Mwenyezi Mungu na neema Zake. Na
Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua, Mwenye hekima.

9. Na endapo makundi mawili ya waumini yanapigana, basi
yapatanisheni. Na likiwa moja la hayo linadhulumu jingine,
basi lipigeni linalodhulumu mpaka lirejee kwenye amri ya
Mwenyezi Mungu. Na likirejea basi yapatanisheni kwa
uadilifu. Na hukumuni kwa haki. Hakika Mwenyezi Mungu
anawapenda wanaohukumu kwa haki. 10 Hakika Waumini tu
ni ndugu, basi patanisheni baina ya ndugu zenu, na mcheni
Mwenyezi Mungu ili mrehemiwe.

11. Enyi walioamini! Wanaume wasiwadharau wanaume

wengine, kwani huenda hao wakawa bora kuliko wao. Wala wanawake wasiwadharau wanawake wengine, huenda wakawa bora kuliko wao. Wala msivunjiane heshima, wala msibezane kwa majina. Hakuna jina baya kama kumwita mtu fasiki baada ya (yeye) kuamini. Na wasio omba msamaha, hao ndiyo wafanya mabaya.

12. Enyi walioamini! Jiepusheni sana na dhana. Hakika katika baadhi ya hali dhana ni dhambi. Wala msifanye ujasusi, wala msisengenyane nyinyi kwa nyinyi. Je, anapenda mmoja wenu kula nyama ya nduguye aliyekufa? Hilo mnalichukia (basi dhana pia muichukie). Na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kukubali toba, Mwenye kurehemu.

13. Enyi watu! Hakika Sisi tumewaumba nyie kutokana na mwanamume mmoja na mwanamke mmoja. Kisha tukawafanya mataifa na makabila, ili mjuane (sio mdharauliane). Hakika mtukufu zaidi kati yenu mbele ya Mwenyezi Mungu ni anayemcha Yeye zaidi yenu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua, Mwenye habari.

14. Mabedui walisema: Tumeamini. Sema: Hamjaamini, lakini semeni: Tumesilimu. Kwani imani haijaingia katika nyoyo zenu. Na mkimtii Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, hatawapunguzia chochote katika amali zenu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa maghufira, Mwenye kurehemu. 15. Hakika Waumini ni wale tu waliomwamini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake tena wasiwe na shaka (baada ya hapo). Na wakapambana kwa hali na mali katika kuendeleza dini ya Mwenyezi Mungu. Hao ndio waumini wa dhati.

16. Sema: ati mnamfundisha Mwenyezi Mungu Dini

yenu? Ilhali Mwenyezi Mungu anayajua yaliyomo mbinguni
na katika ardhi, na Mwenyezi Mungu anajua kila kitu?
17. Wanakusimbulia kuwa wamesilimu! Sema: Msinisimbulie
kwa kusilimu kwenu. Bali Mwenyezi Mungu Ndiye
anayewasimbulia kwa kuwa amewaongoza kwenye imani,
ikiwa nyinyi ni waumini wa dhati. 18. Hakika Mwenyezi
Mungu anajua siri za mbingu na ardhi. Na Mwenyezi Mungu
anayaona mnayoyatenda.

50. Sura Qaf

# SURA YA QAF

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 *Qaf*.

Naapa kwa Qur’an tukufu! 2 Bali wanastaajabu kwamba
amewafikia mwonyaji kutoka miongoni mwao, na wakasema
makafiri: Hili ni jambo la ajabu! 3 Ati tukifa na tukawa
udongo (tutaishi tena)? Hayo ni marejeo yako mbali (na
ufahamu)! 4 Hakika tunajua kiasi gani ardhi itapunguza
katika miili yao. Na tunacho Kitabu kinachohifadhi. 5 Lakini
wanakataa tu ukweli unapowajia. Hivyo wako katika hali ya
kuchanganyikiwa.

6 Hivi hawaangalii mbingu zilizo juu yao, namna
tulivyozijenga na tukazipamba wala hazina nyufa? 7 Na
ardhi tukaitandaza na tukaweka humo milima, na tukaotesha
mimea mizuri (mume na mke) ya kila aina. 8 Yazingatiwe
(kwa kuyaona) na iwe ukumbusho kwa kila mja mwenye

kuelekea (kwa Mwenyezi Mungu). 9 Na tumeteremsha kutoka
mbinguni maji yaliyobarikiwa, na kwa hayo tukaotesha
mabustani na nafaka zivunwazo. 10 Na mitende mirefu yenye
makole yaliyozaa kwa wingi. 11 Ili iwe ni riziki kwa waja
Wangu. Na tukaipa maisha mapya kwayo ardhi iliyokuwa
imekufa. Na Kama hivyo ndivyo utakavyokuwa ufufuo.

12. Kabla yao (Maquresh) walikana (kufufuliwa) watu
wa Nuh (noah) na watu wa Ras na Thamud. 13. Na A'di na
Firauni na ndugu wa Lut. 14. Na watu wa porini na watu wa
Tubbaa'. Wote waliwakataa Mitume, kwa hiyo onyo langu
likatekelezwa. 15. Kwani tulichoka kwa kuumba mara ya
kwanza hata wao wakawa wanatia shaka juu ya umbo jipya.

16. Na hakika tumemuumba mwanadamu nasi tunajua
yanayoitia wasi wasi nafsi yake. Na Sisi tuko karibu naye
kuliko mshipa wa shingo. 17. Wanapopokea wapokeaji
wawili, walioko kuliani na kushotoni. 18. Hatamki neno ila
karibu yake yupo mwangalizi tayari (kurekodi).

19. Na uchungu wa mauti utamletea ukweli (mbele ya macho
yake). 'Hayo ndiyo uliyokuwa ukiyakimbia'! 20. Na itapulizwa
parapanda. Hiyo ndiyo Siku ambayo onyo lilikwisha tolewa
(juu yake). 21. Na atakuja kila mtu akiandamana na (Malaika)
wa kumwongoza na (mwengine) wa kumshuhudia. 22. Kwa
hakika ulikuwa umeghafilika na haya. Leo tumekuondolea
pazia lako, kwa hivyo macho yako hii leo ni makali. 23. Na
mwenzake atasema: Hii hapa (rekodi yake) ninayo tayari!
24. Mtupeni katika Jahannamu kila kafiri mwenye inadi.
25. Aliyezuia kila jambo zuri, akavuka mipaka yote (ya uasi)
na akawa na shaka (juu ya Allah, ujumbe wake). 26. Ambaye
amejitengezea mungu mwengine pamoja na Mwenyezi
Mungu. Basi (nyie wawili) mtupeni katika adhabu kali.

27. Mwenzake atasema: Ee Mola Wetu Mlezi! Sikumpoteza
mimi, bali yeye mwenyewe alikuwa katika upotevu wa
mbali. 28. (Mwenyezi Mungu) atasema: Msigombane mbele
Yangu. Nilikwisha watangulizia onyo langu. 29. Kwangu
haibadilishwi kauli, wala Mimi siwadhulumu waja.
30. Siku tutapoiambia Jahannamu: Je, umejaa? Nayo
iseme Je, kuna zaidi? 31. Na Pepo italetwa karibu kwa wenye
takua, haitakuwa mbali. 32. Haya ndiyo mnayoahidiwa. Kwa
kila mwenye kurejea kwa Mwenyezi Mungu, ajilindae.
33. Mwenye kumwogopa (Mwenyezi Mungu) Mwingi wa
Rehema ingawaje hamwoni kwa macho, na akaja na moyo
ulioelekea (kwake kwa ibada). 34. Ingieni kwa amani.
Hiyo ndiyo siku ya maisha ya milele. 35. Humo watapata
wakitakacho, na Kwetu yako ya ziada.
36. Na vizazi vingapi tuliviangamiza kabla yao (Maqureish)?
Hao walikuwa na nguvu zaidi kuliko wao, wakaenda huku na
huko duniani. Je, walipata pa kukimbilia? 37. Hakika katika
hayo kuna ujumbe kwa mwenye moyo (wa kufahamu) au
akatega sikio naye akashuhudia kwa dhati (ukweli).
38. Na hakika tumeziumba mbingu na ardhi na vilivyomo
kati yake katika (kiasi cha) siku sita; na wala haukutugusa
uchovu. 39. Basi vumilia kwa hayo wayasemayo na msabihi
Mola Wako kabla ya kuchomoza jua na kabla ya kuchwa.
40. Na katika usiku msabihi na baada ya kusujudu.
41 .Na sikiliza siku ataponadi mwenye kunadi kutoka pahala
karibu mno. 42. Siku watakaposikia mpasuko mkubwa kwa
ukweli. Hiyo ndiyo siku ya kufufuliwa kutoka (makaburini).
43. Hakika Sisi tunatoa uhai na mauti, na Kwetu Sisi ndio
marejeo. 44. Siku itapowapasukia ardhi (watu wakatoka)
mbio mbio! Mkusanyo huo Kwetu ni mwepesi.

45. Sisi tunajua sana wayasemayo. Wala wewe si jabari juu
yao. Basi mwonye kwa Qur'an anayeogopa onyo langu!.

51. Sura Adh-Dhariyat

## SURA YA UPEPO UNAOTAWANYA

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 Naapa kwa pepo zinazotawanya (vumbi)! 2 Na zinazobeba
mizigo (ya maji)! 3 Na zinazokwenda kwa wepesi! 4 Na
kwa (Malaika) wanaogawa mambo (mbali mbali)! 5 Hakika
mnayoahidiwa bila ya shaka ni kweli. 6 Na kwa hakika
(hukumu na) malipo bila ya shaka vitatokea. 7 Naapa kwa
mbingu zenye njia (tofauti)! 8 Hakika nyinyi bila ya shaka
mko katika kauli (madhehebu) mbalimbali. 9 Anadanganywa
kukataa ukweli mwenye kudanganywa.

10 Wamelaaniwa wazushi. 11 Ambao wameghafilika
wamo katika kuchanganyikiwa. 12 Wanauliza: Ni lini hiyo
siku ya (hukumu na) malipo? 13 Ni siku watakayojaribiwa
Motoni. 14 (Wakiambiwa): 'Onjeni mtihani wenu! Haya
ndiyo mliyokuwa mkitaka yaharakishwe'. 15 Hakika
wachamungu watakuwa katika mabustani na chemchemi
za maji. 16 Wakipokea (neema) alizowapa Mola Wao Mlezi.
Hakika wao walikuwa kabla ya haya wakifanya mema.
17 Walikuwa wakilala muda mdogo tu usiku, 18 Na kabla ya
alfajiri wakiomba maghufira. 19 Na katika mali zao ipo haki
ya mwenye kuomba na anayejizuia (kuomba).

20. Na katika ardhi zipo Ishara kwa wenye yakini.
21. Na (hata) katika nafsi zenu wenyewe, Je, hamwoni?

22. Na mbinguni ndiko zilipo riziki zenu na yale mnayoahidiwa.
23. Naapa kwa Mola Mlezi wa mbingu na ardhi, hakika haya ni
kweli kama ilivyokuwa (kweli kuwa) nyinyi mnazungumza.

24. Je, imekufikia hadithi ya wageni watukufu wa Ibrahim
? 25. Pale walipoingia kwake wakasema: Salaam! Na yeye
akasema: Salaam! (Akajisemea): 'watu wa ajabu hawa'!.
26. Akaenda kwa familia yake na akaja na ndama aliyenona.
27. Akawakaribisha, akasema: 'Mbona hamli'?
28. (Walipokataa kula) Akahisi woga. Wakamwambia: 'Usiwe
na hofu!' Na wakampa habari nzuri kuwa atapata kijana
mwenye elimu. 29. Mkewe akasogea karibu akihuzunika
na huku akijipiga (paji lake la) uso, akisema: ' (uuuwii!
Mwanamke mkongwe, tasa (azae)!?' 30. Wakasema: 'Ndiyo
hivyo basi! Mola Wako Mlezi amekwishasema. Hakika Yeye
ni Mwenye hekima Mjuzi'.

31. (Ibrahim) Akauliza: basi ujumbe wenu ni nini, enyi
mliotumwa? 32. Wakasema: Hakika sisi tumetumwa kwa
watu wahalifu. 33. Tuwashushie mawe ya udongo mkavu,
34. Yalikwishatiwa alama (kuwalenga wahusika) kutoka kwa
Mola Wako Mlezi, kwa ajili ya waliopituka mipaka. 35. Ndipo
tukawatoa waliokuwa (mjini) humo katika walioamini.
36. Lakini hatukupata huko ila nyumba moja tu yenye
Waislamu! 37. Na tukaacha humo alama kwa wale
wanaoiogopa adhabu chungu.

38. Na katika Musa (Moses), tulipomtuma kwa
Firauni (Pharaoh) na hoja wazi. 39. Lakini alipuuza kwa
sababu ya nguvu zake na akasema: 'Huyu ni mchawi au
mwendawazimu'! 40. Basi tukamtia nguvuni yeye na majeshi
yake na tukawatupa baharini, na yeye ndiye wa kulaumiwa.
41. Na katika A'di tulipowapelekea upepo tasa (usio

mvua). [42.] Haukuacha chochote ulichokipitia ila ulikifanya kilichosagwasagwa. [43.] Na katika Thamudi walipoambiwa: ‘Stareheni kwa muda mdogo tu’! [44.] Lakini wakaasi amri ya Mola Wao Mlezi. Kishindo kikubwa (tetemeko la ardhi) kikawapiga huku wakiangalia. [45.] Hapo hawakuweza tena kusimama wala hawakuwa wenye kujitetea. [46.] Na watu wa Nuh (Noah) kabla ya hapo. Hakika hao walikuwa watu waovu.

[47.] Na mbingu tumezijenga kwa nguvu na uwezo wetu na hakika Sisi bila shaka ndiyo wapanuaji wa eneo (la anga za nje). [48.] Na ardhi tumeitandaza; bora ya watandazaji ni Sisi! [49.] Na katika kila kitu tumeumba dume na jike, ili mzingatie. [50.] Basi kimbilieni kwa Mwenyezi Mungu, hakika mimi nitokae Kwake, ni mwonyaji wenu wa wazi. [51.] Wala msifanye kuwa kuna mungu mwengine pamoja na Allah. Hakika mimi kutoka Kwake ni mwonyaji wenu wa wazi.

[52.] Basi ndio hivyo hivyo, hakuwajia kabla yao Mtume yeyote ila walisema: Huyu ni mchawi au mwendawazimu. [53.] Je, wameambiana juu ya hili? Lakini hawa ni watu waasi tu. [54.] Basi waachilie mbali, wewe hulaumiwi. [55.] Na kumbusha, kwani ukumbusho huwafaa waumini.

[56.] Sikuwaumba majini na watu isipokuwa Waniabudu Mimi. [57.] Sitaki kwao riziki, wala sitaki wanilishe. [58.] Hakika Mwenyezi Mungu Ndiye Mwenye kuruzuku, Mwenye nguvu, Madhubuti. [59.] Hakika watendao maovu wana fungu lao (la adhabu) kama fungu la wenzao (waliopita). Basi waache kuniharakisha. [60.] Ole wao walioikanusha siku yao waliyoahidiwa.

52. Sura At-Tur

# SURA YA MLIMA TUR

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 Naapa kwa Mlima wa Tur (mahali alipopewa Musa
ujumbe)! 2 Na kwa amri iliyorekodiwa, 3 Katika ngozi
iliyokunjuliwa! 4 Na kwa Nyumba isiyoisha wanaoitembelea!
5 Na kwa dari (ya nyumba hiyo) iliyonyanyuliwa! 6 Na
kwa bahari iliyowashwa moto! 7 Hakika adhabu ya Mola
Wako Mlezi hapana shaka itatokea. 8 Hapana wa kuizuia.
9 Siku zitakapotikisika mbingu mtikiso wa kutisha! 10 Na
milima ikawa inakwenda (huku na huko). 11 Ole wao siku
hiyo wasemao huu ni uwongo! 12 Ambao wanacheza katika
mambo ya upuuzi. 13 Siku wataposukumwa kwenye Moto
msukumo wa nguvu. 14 (Wataambiwa) Huu ndio ule Moto
mliokuwa mkiukanusha! 15 Je, ni uchawi huu, au hamuoni
tu? 16 Ingieni ndani! Mvumilie au msivumilie, ni sawa tu.
Nyie mnalipwa mliyokuwa mkiyatenda!

17 Hakika wachamungu watakuwa katika Mabustani na
neema, 18 Wakifurahia yale aliyowapa Mola Wao Mlezi.
Mola Wao amewalinda na adhabu ya moto wa Jahannam.
19 (Wataambiwa) Kuleni na kunyweni kwa raha mstarehe kwa
sababu ya mliyokuwa mkiyatenda. 20 Watakuwa wakiegemea
juu ya viti vya fahari vilivyopangwa safu. Na tutawaoza
wanawake wenye macho makubwa, mazuri, yanayong’aa
(mahurulaini).

21. Na wale walioamini na vizazi vyao vikawafuata
katika Iman, tutawajumuisha na vizazi vyao hivyo, pasi na

kuwapunguzia chochote katika amali zao. Kila mtu atapata
alichokichuma. 22. Na tutawapa matunda na nyama kama
wapendavyo. 23. Watapeana humo bilauri zenye vinywaji
visivyosababisha upuuzi wala dhambi. 24. Wakizungukwa na
watumishi wao (maridadi) kana kwamba ni lulu zilizofichwa
ndani ya chaza. 25. Watakuwa wakielekeana huku wakijuzana,
26. Wakisema, ‘tulipolikuwa duniani (ingawa) baina ya jamaa
zetu, tukiogopa (adhabu hii ya Akhera)’. 27. Kwa sababu hiyo
ndipo Mwenyezi Mungu akatufanyia hisani na akatulinda na
adhabu ya fukuto la Moto. 28. Hakika sisi zamani (duniani)
tulikuwa tukimwomba Yeye pekee. Hakika Yeye Ndiye
Mwema Mwingi wa huruma.

29. Basi wakumbushe kwamba wewe, kwa neema ya Mola
Wako Mlezi, si mpiga ramli wala mwendawazimu. 30. Au
wanasema: ‘Mtunga mashairi huyu! Acha tungojee limfike
janga la wakati (atuondokee)’. 31. Sema: ‘Nyie ngojeni tu,
nami ni pamoja nanyi katika kungojea’. 32. Au akili zao ndio
zinawaamrisha haya, au wao ni watu wakaidi tu? 33. Au
wanasema: Ameitunga? Hapana, ni vile hawaamini tu! 34. Si
nawalete masimulizi kama haya ikiwa wao wanasema kweli?

35. Au wao wameumbwa pasipo kutokana na chochote;
au wao ndio waumbaji? 36. Au ni wao walioumba mbingu
na ardhi? Ni vile tu hawana yakini! 37. Au wanazo hazina
za Mola Wako Mlezi, au wao ndio wenye madaraka? 38. Au
wanayo ngazi (ya kufika mbinguni) wakawa wanasikiliza
(Malaika) huko? Basi huyo msikilizaji wao na alete hoja
madhubuti! 39. Au Yeye (Mwenyezi Mungu) ana wasichana,
na nyinyi mna wavulana?

40. Au wewe unawaomba ujira, kwa hiyo wanaelemewa
na gharama? 41. Au wanayo elimu ya ghaibu, nao huandika?

42. Au wanataka kukutega kwa njama? Lakini wanaomkana Mwenyezi Mungu ndiyo watakaotegeka. 43. Au wanaye mungu asiye kuwa Mwenyezi Mungu wa haki? Ametakasika Mwenyezi Mungu na hao wanaowashirikisha Naye.

44. Na hata wangeona kipande cha mbingu kimeanguka (juu yao) watasema: 'Ni mawingu tu yaliyobebana'. 45. Basi waache mpaka wakutane na siku yao ambayo watazimia (kwa hofu). 46. Siku ambayo hila zao hazitawafaa kitu, wala wao hawatasaidiwa. 47. Na hakika waliofanya dhuluma watapata adhabu nyingine isiyokuwa hiyo, lakini wengi wao hawajui.

48. Na ingojee kwa subira hukumu ya Mola Wako Mlezi. Kwani wewe hakika uko katika himaya Yetu. Na mtakase kwa kumsifu Mola Wako Mlezi usimamapo. 49. Na usiku pia msabihi, na zinapopotea nyota.

## 53. Surah Al-Najm

# SURA YA NYOTA

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 Naapa kwa nyota inapokwenda chini! 2 Mwenzenu hakupotea, wala hakukosea. 3 Wala hatamki kulingana na matamanio yake (mwenyewe). 4 Hayakuwa haya ila ni ufunuo (wahyi) uliopelekwa kwake. 5 Amemfundisha yeye aliye Mwingi wa nguvu (Jibril). 6 Mwenye hekima, ndipo akadhihiri (katika hali isiyoogofya), 7 Alipokuwa katika upeo wa juu kabisa. 8 Kisha akakaribia na akashuka. 9 Akawa umbali wa pinde mbili, au karibu zaidi. 10 Akamfunulia mja wake yale (aliyotaka) kumfunulia. 11 Moyo haukusema

uwongo uliyoyaona. 12 Je, mnabishana naye juu ya
aliyoyaona? 13 Na hakika alimwona kwa mara nyingine,
14 Penye Mkunazi wa (kivuko cha) mwisho. 15 Karibu yake
pana Bustani ya makazi. 16 Pale ulipoufunikwa mkunazi
huo na hicho kilichoufunika. 17 Jicho halikupepesa wala
halikutazama pengine. 18 Hakika aliona baadhi ya alama
kubwa kabisa za Mola Wake Mlezi.

19 Je, mmemuona Lat na Uzza? 20 Na mungu wao
mwingine wa tatu, Manaat? 21 Ebo! Hivi nyie muwe na jinsi
ya kiume, na Yeye Mwenyezi Mungu anasibishiwe jinsi ya
kike? 22 Huo basi ndiyo ugavi usio wa haki! 23 Hayo si lolote
isipokuwa majina tu mliyowapa hao, nyinyi na baba zenu.
Mwenyezi Mungu hakuleta uthibitisho wowote juu yake.
Hawafuati ila dhana tu na kipendacho nafsi. Na kwa hakika
uwongofu ulikwishawafikia kutoka kwa Mola Wao Mlezi.
24 Kwani mtu ni lazima apate kila anachokitaka? 25 Mwenyezi
Mungu pekee ndiye Mmiliki wa Akhera na Dunia.

26. Na wako Malaika wangapi mbinguni, ambao uombezi
wao hautafaa chochote isipokuwa baada ya Mwenyezi
Mungu kutoa idhini kwa amtakaye na kumridhia? 27. Hakika
wasioamini Akhera wanawaita Malaika kwa majina ya
kike. 28. Nao hawana elimu yoyote juu ya hilo isipokuwa
wanafuata dhana (zao) tu. Na hakika dhana haifai kitu mbele
ya ukweli. 29. Basi mwachilie mbali anayeupa kisogo ujumbe
Wetu, na asitake ila maisha ya dunia. 30. Hicho ndiyo kikomo
cha elimu yao. Hakika Mola Wako Mlezi Ndiye anayemjua
zaidi aliyepotea njia Yake, na Yeye Ndiye anayemjua zaidi
mwenye kuongoka.

31. Ni vya Mwenyezi Mungu vilivyomo mbinguni na
vilivyo katika ardhi, ili awalipe waliotenda ubaya kwa

waliyoyatenda, na waliotenda mema awalipe kwa wema.
[32.] Ambao wanajiepusha na madhambi makubwa na vitendo
vichafu, isipokuwa makosa madogo madogo. Hakika Mola
Wako Mlezi ni Mkunjufu wa msamaha, Naye anawajua sana
nyie tangu alipowaumba kutoka kwenye ardhi, na mlipokuwa
mimba matumboni mwa mama zenu. Basi msijisifie usafi
nyie wenyewe! Yeye anamjua sana mwenye kujikinga na
maovu.

[33.] Je, Umemwona yule aliyegeuza usogo wake? [34.] Na
akatoa kidogo, kisha akajizuia [35.] Je, anayo elimu ya ghaibu,
basi ndio anaona? [36.] Au hakuambiwa yaliyomo katika
Vitabu vya Musa? [37.] Na vya Ibrahim aliyetimiza ahadi?
[38.] Kwamba mbebaji habebi mzigo wa mwingine? [39.] Na
kwamba hatapata mtu ila aliyoyahangaikia? [40.] Na kwamba
(matunda ya) mhangaiko wake yataonekana? [41.] Kisha ndipo
atalipwa malipo yake kwa ukamilifu? [42.] Na kwamba kwa
Mola Wako ndio mwisho (wa yote)? [43.] Na kwamba Yeye
Ndiye anayesababisha kicheko na kilio? [44.] Na kwamba Yeye
Ndiye anayesababisha mauti na uhai? [45.] Na kwamba Yeye
Ndiye aliyeumba jozi, dume na jike? [46.] Kutokana na tone
la manii linapomiminwa?. [47.] Na kwamba ameahidi ufufuo
mwingine? [48.] Na kwamba ni Yeye Ndiye anayetoa utajiri na
anayefanya (mtu) akinai? [49.] Na kwamba Yeye Ndiye Mola
wa Sirius? (Nyota iliyokuwa inaabudiwa na Wapagani wa
Kirabu).

[50.] Na kwamba Yeye Ndiye aliyewaangamiza A'di wa
kwanza. [51.] Na Thamudi hakuwabakisha. [52.] Na kabla
yao watu wa Nuh (Noah). Kwa sababu wao walikuwa
wamebobea katika uovu na ukiukaji wa mipaka yote? [53.] Na
miji iliyopinduliwa juu-chini (ya Sodom na Gomorrah), ni

Yeye aliyeipindua? 54. Ikafunikwa (na vifusi) vilivyoifunika?
55. Basi neema gani ya Mola Wako Mlezi unayoitilia shaka?

56. Hili ni Onyo katika maonyo yale yale ya zamani.
57. Kiyama kimekaribia! 58. Hapana (yeyote) anayeweza
kukifichua (wakati wake) isipokuwa Mwenyezi Mungu.
59. Je, mnayastaajabia maneno haya? 60. Na mnacheka
wala hamlii? 61. Nanyi mmeghafilika? 62. Basi msujudieni
Mwenyezi Mungu, na mumwabudu.

## 54. Sura Al-Qamar

# SURA YA MWEZI

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 Saa (ya hukumu) imekaribia, na mwezi umeshapasuka! 2 Na
wakiona muujiza hugeuka upande na husema: huu ni uchawi
unaoendelea. 3 Na wamekanusha (maonyo) na wakafuata
matamanio yao. Na kila jambo lina wakati maalum. 4 Na bila
ya shaka zimefikia wao habari zenye makaripio. 5 Hekima
kamili, lakini maonyo hayafai tena (kwao). 6 Basi achana nao.
Siku hiyo atakapoita anayeita kuliendea jambo linalochukiza.
7 (huku) Macho yao yakitazama chini, (ndivyo) watatoka
makaburini kana kwamba wao ni nzige waliotawanyika.
8 Wakimkimbilia anayeita; makafiri watasema: ‘Kweli hii ni
siku ngumu’.

9 Kabla yao watu wa Nuh (Noah) pia walikataa, wakamkataa
mtumishi Wetu, na wakasema yeye ni mwendawazimu, na
akakaripiwa. 10 Basi akamwomba Mola Wake Mlezi: ‘Mimi
kwa kweli nimeshindwa, nisaidie’! 11 Basi tukafungua

milango ya mbingu kwa maji yanayomiminika. 12 Na
tukaichimbua ardhi kuwa chemchemi, yakakutana maji kwa
jambo liliokadiriwa. 13 Na tukamchukua kwenye jahazi
iliyotengenezwa kwa mbao na misumari. 14 Inayokwenda
chini ya himaya yetu. Haya yakiwa ni malipo kwa aliyekuwa
amekataliwa (kwa kejeli). 15 Na hakika tuliiacha (jahazi)
iwe ni alama. Basi je, yupo aliyetii maonyo? 16 Namna gani
ilikuwa adhabu na ilani Zangu? 17 Na hakika tumeifanya hii
Qur'an iwe nyepesi kufahamiwa. Jee, yupo anayetii maonyo
(yaliyomo)?

18. A'di pia walikataa. Namna gani ilikuwa adhabu na ilani
Zangu ? 19. Hakika tuliwapelekea upepo mkali wa kimbunga
katika siku ya bahati mbaya mfululizo. 20. Ukiwabwaga watu
kama vigogo vya mitende vilivyong'olewa. 21. Namna gani
ilikuwa adhabu na ilani Zangu? 22. Na hakika tumeifanya hii
Qur'an iwe nyepesi kufahamiwa. Jee, yupo anayetii maonyo
(yaliyomo)?

23. Thamud (pia) waliwakataa waonyaji. 24. Wakasema:
'Hivi kweli itawezekanaje tumfuate mtu mmoja tu kati yetu?
Kwa kweli hapo sisi tutakuwa katika upotevu na dhiki!' 25. Ati
yeye pekee amepewa ujumbe kati yetu sisi (sote)? Hapana!
Yeye mwongo, asiye na aibu! 26. Hivi karibuni watajua ni
nani huyo mwongo, asiye na aibu. 27. Sisi tutawapelekea
ngamia jike ili kuwajaribu. Basi watazame tu (Ewe Saleh)
na usubiri. 28. Na waambie kwamba maji yatagawiwa baina
yao; (haki ya) kila mmoja ya kunywa itahifadhiwa. 29. Ndipo
wakamwita mwenzao, akashika upanga, akamkata miguu.
30. Namna gani ilikuwa adhabu na ilani zangu? 31. Hakika
tuliwapelekea mpasuko mmoja mkubwa, wakawa kama
majani makavu (yaliosagika) katika zizi (la mifugo). 32. Na

hakika tumeifanya Qur’an iwe nyepesi kufahamiwa. Jee,
yupo anayetii maonyo (yaliyomo?)
33. Watu wa Lut (Lot) vilevile waliwakana waonyaji.
34. Nasi tuliwapelekea kimbunga cha kokoto. Isipokuwa
wafuasi wa Lut. Tuliwaokoa mapema alfajiri. 35. Hii ikiwa
ni neema kutoka Kwetu. Namna hii ndivyo tunavyomlipa
anayeshukuru. 36. Na hakika Lut aliwaonya juu ya kamata-
kamata Yetu; lakini wao wakayatilia shaka maonyo hayo.
37. Na wakamtaka awape wageni wake! Tukayapofua macho
yao. Haya, onjeni adhabu na ilani Zangu! 38. Ndipo ikawafikia
asubuhi adhabu mfululizo. 39. Basi onjeni adhabu na Ilani
Zangu! 40. Na hakika tumeifanya hii Qur’an iwe nyepesi
kufahamiwa. Jee, yupo anayetii maonyo (yaliyomo)?
41. Waonyaji pia waliwafikia watu wa Firauni.
42. Wakazikataa Ishara Zetu zote, tukawatia nguvuni kwa
namna afanyavyo Mwenye nguvu, Mwenye uwezo.
43. Je, Makafiri wenu (nyie Maquresh) ni bora kuliko
hao? Au nyie mmepewa hifadhi (iliyorekodiwa) katika
vitabu vitukufu? 44. Au wanasema: ‘Sisi ni wengi, hivyo
tutashinda’? 45. Wingi wao huu utashindwa, na watatoka
mbio. 46. Bali Kiyama ndio miadi yao, na Saa hiyo ni nzito
sana na chungu zaidi. 47. Hakika watenda maovu wao ndiyo
wamo katika upotevu na dhiki. 48. Siku watakapokokotwa
motoni kifudifudi: ‘Onjeni mguso wa Jahannam’!
49. Kwa hakika Sisi tumeumba kila kitu kwa kipimo.
50. Na amri Yetu ni (neno) moja tu (iwe! Na inakuwa), kama
kupepesa kwa kwa jicho. 51. Na bila shaka tumekwisha
waangamiza wenzenu (kama ninyi), Je, yupo anayeonyeka?
52. Na kila kitu walichokifanya kimo katika rekodi (zao).
53. Na kila kidogo na kikubwa kimerekodiwa. 54. Hakika

wachamungu watakuwa katika mabustani na mito. 55. Katika
makao ya heshima mbele ya Mfalme Mwenye uwezo wote.

55. Sura Ar-Rahman

# SURA AR-RAHMAN

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 (Mwenyezi Mungu) Mwingi wa Rehema. 2 Ndiye
aliyefundisha Qur'an. 3 Amemwumba mtu, 4 Akamfundisha
kutamka. 5 Jua na mwezi hufuata hesabu maalum. 6 Na
mimea yenye kutambaa na miti, inanyenyekea. 7 Na mbingu
ameziinua, na ameweka uwiano. 8 Ili msikiuke uwiano
(katika hukumu). 9 Na dumisheni vipimo kwa uadilifu, wala
msipunje katika mizani

10 Na ardhi ameiweka kwa ajili ya viumbe. 11 Humo
yamo matunda na mitende yenye mafumba. 12 Na nafaka
zenye makapi, na mrehani. 13 Basi ni ipi katika neema za
Mola Wenu Mlezi mnayoikanusha (ninyi watu na majinni)?
14 Amemwumba binadamu kwa udongo mkavu kama wa
mfinyazi. 15 Na akawaumba majinni kwa moto usio moshi. 16
Basi ni ipi katika neema za Mola Wenu Mlezi mnayoikanusha
nyinyi wawili? 17 Mola wa mashariki mbili na wa magharibi
mbili. 18 Basi ni ipi katika neema ya Mola Wenu Mlezi
mnayoikanusha nyinyi wawili? 19 Amezifungulia bahari mbili
zikutane; 20 Baina yao kipo kizuizi, haziwezi kukikeuka. 21
Basi ni ipi katika neema ya Mola Wenu Mlezi mnayoikanusha
nyinyi wawili? 22 Zinatoka katika hizo bahari mbili lulu
na matumbawe. 23 Basi ni ipi katika neema ya Mola Wenu

Mlezimnayoikanusha nyinyi wawili? 24 Na ni zake merikebu zilizoinuka baharini kama milima. 25 Basi ni ipi katika neema ya Mola Wenu Mlezi mnayoikanusha nyinyi wawili?

26. Kila kilicho juu ya ardhi kitatoweka. 27. Na itabakia dhati ya Mola Wako Mlezi, Mwenye utukufu na mwingi wa vipawa. 28. Basi ni ipi katika neema ya Mola Wenu Mlezi Mlezi mnayoikanusha nyinyi wawili? 29. Vinamwomba Yeye vilivyo katika mbingu na ardhi. Kila siku Yeye yumo katika jambo jingine. 30. Basi ni ipi katika neema ya Mola Wenu mnayoikanusha nyinyi wawili?

31. Muda mfupi tutamalizana na nyie, enyi viumbe wawili. 32. Basi ni ipi katika neema ya Mola Wenu Mlezi mnayoikanusha nyinyi wawili? 33. Enyi mkusanyiko wa majini na watu! Mkiweza kupenya kwenda nje ya ukanda wa mbingu na ardhi, basi penyeni! Hamtapenya isipokuwa kwa mamlaka (Yetu). 34. Basi ni ipi katika neema ya Mola Wenu Mlezi mnayoikanusha nyinyi wawili? 35. Mtapelekewa miali ya moto na shaba (iliyoyeyuka); hamtashinda. 36. Basi ni ipi katika neema ya Mola Wenu Mlezi mnayoikanusha nyinyi wawili?

37. Pale itakapopasuka mbingu ikawa rangi ya hudhurungi kama ngozi iliyopakwa rangi. 38. Basi ni ipi katika neema ya Mola Wenu Mlezi mnayoikanusha nyinyi wawili? 39. Siku hiyo hataulizwa dhambi zake mtu wala jinni. 40. Basi ni ipi katika neema ya Mola Wenu Mlezi mnayoikanusha nyinyi wawili? 41. Waovu watajulikana kwa alama zao, basi watakamatwa kwa nywele zao za utosi na kwa miguu. 42. Basi ni ipi katika neema ya Mola Wenu Mlezi mnayoikanusha nyinyi wawili? 43. (Wataambiwa): ‘hii ndiyo Jahannam ambayo waovu wanaikanusha’. 44. Watakuwa wakizunguka baina yake na

baina ya maji ya moto yanayochemka. [45.] Basi ni ipi katika neema ya Mola Wenu Mlezi mnayoikanusha nyinyi wawili?

[46.] Na mwenye kuogopa kusimama mbele ya Mola Wake Mlezi atapata Bustani mbili. [47.] Basi ni ipi katika neema ya Mola Wenu Mlezi mnayoikanusha nyinyi wawili? [48.] Zenye matawi yaliyotanda. [49.] Basi ni ipi katika neema ya Mola Wenu Mlezi mnayoikanusha nyinyi wawili? [50.] Ndani yake zimo chemchemi mbili zinazobubujika. [51.] Basi ni ipi katika neema ya Mola Wenu Mlezi mnayoikanusha nyinyi wawili? [52.] Humo kila tunda lina jinsi mbili. [53.] Basi ni ipi katika neema ya Mola Wenu Mlezi mnayoikanusha nyinyi wawili? [54.] Watakuwa wakibembea kwenye vitanda ambavyo foronya za matandiko yake zimechomekewa kwa hariri nzito, huku matunda ya Bustani hizo yakining'inia karibu. [55.] Basi ni ipi katika neema ya Mola Wenu Mlezi mnayoikanusha nyinyi wawili? [56.] Humo watakuwamo wanawake watulizao macho yao; hajawagusa mtu kabla yao wala jinni. [57.] Basi ni ipi katika neema ya Mola Wenu Mlezi mnayoikanusha nyinyi wawili? [58.] Kama kwamba wanawake hao ni yakuti (ruby) na matumbawe. [59.] Basi ni ipi katika neema ya Mola Wenu Mlezi mnayoikanusha nyinyi wawili [60.] Jee, kuna malipo yoyote ya mazuri isipokuwa mazuri vile vile? [61.] Basi ni ipi katika neema ya Mola Wenu Mlezi mnayoikanusha nyinyi wawili?

[62] Zaidi ya hizo mbili ziko Bustani mbili nyingine. [63.] Basi ni ipi katika neema ya Mola Wenu Mlezi mnayoikanusha nyinyi wawili? [64.] Za kijani kibichi. [65.] Basi ni ipi katika neema ya Mola Wenu Mlezi mnayoikanusha nyinyi wawili? [66.] Mna chemchemi mbili zinazofurika. [67.] Basi ni ipi katika neema ya Mola Wenu Mlezi mnayoikanusha nyinyi wawili? [68.] Mna

humo miti ya matunda, mitende na makomamanga. 69. Basi ni
ipi katika neema ya Mola Wenu Mlezi mnayoikanusha nyinyi
wawili? 70. Wamo humo wanawake wema wazuri. 71. Basi
ni ipi katika neema ya Mola Wenu Mlezi mnayoikanusha
nyinyi wawili? 72. Wanawake wazuri wanaotawishwa katika
mahema. 73. Basi ni ipi katika neema ya Mola Wenu Mlezi
mnayoikanusha nyinyi wawili? 74. Hajawagusa mtu kabla
yao wala jinni. 75. Basi ni ipi katika neema ya Mola Wenu
Mlezi mnayoikanusha nyinyi wawili? 76. Wameegemea juu
ya matakia ya kijani na mazulia mazuri. 77. Basi ni ipi katika
neema ya Mola Wenu Mlezi mnayoikanusha nyinyi wawili?
78. Litukuzwe jina la Mola Wako Mlezi, Mwenye utukufu na
ukarimu.

## 56. Sura Al-Waqia

## SURA YA TUKIO MUHIMU

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye Kurehemu.

1 Pindi kitakapotokea Kiyama. 2 Hapana la uwongo juu
kutokea kwake. 3 Kitawashusha (baadhi) (na) kitawanyanyua
(wengine). 4 Pale ardhi itakapotikiswa mtikisiko
mkubwa. 5 Na milima ikatifuliwa kabisa, 6 Iwe mavumbi
yanayopeperushwa. 7 Na nyinyi mtakuwa aina tatu.

8 Watakuwepo wa mkono wa kuume. Ni mema yapi ya
watakaokuwa mkono wa kuume? 9 Na watakuwepo wa
mkono wa kushoto. Ni mabaya yapi ya watakaokuwa mkono
wa kushoto? 10 Na walio mbele (kwa imani, amali) ndio
watatangulia (huko). 11 Hao ndio watakaosogezwa karibu

zaidi. 12 Katika Bustani zenye neema. 13 Fungu kubwa (ni) katika wa mwanzo, 14 Na wachache (ni) katika waliokuja nyuma. 15 Watakuwa juu ya viti vya fahari vilivyodariziwa (kwa dhahabu na vito). 16 Wakibembea juu yake (huku) wakielekeana. 17 Wakihudumiwa na wavulana wa ujana wa milele. 18 Kwa vikombe na mabirika na bilauri za vinywaji safi 19 Hawataumwa kichwa kutokana na vinywaji hivyo wala hawatalewa. 20 Na matunda yoyote wayapendayo, 21 Na nyama ya ndege kama wanavyotamani. 22 Na wenza wasafi, wenye macho makubwa, mazuri (hurul-aini). 23 Walio kama mfano wa lulu zilizohifadhiwa. 24 (Haya) ni malipo kwa waliyokuwa wakiyatenda. 25 Humo hawatasikia upuuzi wala maneno ya dhambi. 26 Isipokuwa maneno ya amani! Amani! (‘Salaam’, ‘salaam’)

27. Na watakaokuwa mkono wa kuume. Ni yapi ya watakaokuwa mkono wa kuume? 28. Katikati ya mikunazi isiyo na miiba, 29. Na migomba iliyosheheni ndizi moja juu ya nyingine, 30. Na kivuli kilichotanda, 31. Na maji yanayomiminika, 32. Na matunda mengi; 33. Yasio ukomo wala hayakatazwi, 34. Na matandiko yaliyonyanyuliwa. 35. Hakika Sisi tumewaumba (wenza wao) kwa maumbile maalum. 36. Na tutawafanya bikira, 37. Wenye mapenzi ya dhati, walio rika sawa. 38. Kwa ajili ya walio mkono wa kuume. 39. Kundi kubwa ni wale waliokuwa wa mwanzo. 40. Na kundi kubwa katika wa mwisho.

41. Na wale watakaokuwa mkono wa kushoto. Ni yapi ya watakaokuwa mkono wa kushoto? 42. Ndani ya upepo wa moto, na maji yanayochemka. 43. Na kivuli cha moshi mweusi. 44. Si cha kuburudisha wala kustarehesha. 45. Hakika hao walikuwa kabla ya haya wakiishi maisha ya anasa.

46. Na walikuwa wakishikilia kwa kiburi kufanya madhambi
makubwa. 47. Na walikuwa wakisema, hivi tutakapokufa
na tukawa mchanga na mifupa, ati ndio tutafufuliwa?
48. (Sisi) na baba zetu wa zamani? 49. Sema: naam! Wa
mwanzo na wa mwisho, 50. Kwa hakika watakusanywa
pamoja kwenye mkutano wa siku maalumu. 51. Kisha nyinyi!
Enyi wapotevu, mnaokataa ukweli… 52. Kwa yakini mtakula
ya mti wa Zaqquum. 53. Na kwa huo mtajaza matumbo
(yenu). 54. Na juu yake mtakunywa maji yanayochemka.
55. Tena mtakunywa kama wanywavyo ngamia wenye kiu.
56. Haya ndiyo mapokezi yao Siku ya Malipo.

57. Sisi ndiyo tumewaumba nyie; si bora mkasadiki? 58. Je,
mnaiona mbegu ya uzazi mnayoimwaga? 59 Je, mnaiumba
nyinyi, au tunaiumba Sisi? 60 Sisi tumewapangia kifo kuwa
majaaliwa yenu. Na Sisi hatushindwi... 61 Kugeuza maumbile
yenu na kuwaumba (tena) katika namna msiyoijua. 62
Na kwa hakika mlikwishajua maumbile ya mwanzo, si
bora mkafikiria? 63 Je, mnaiona mbegu mnayoipanda ?
64 Je, ni nyinyi ndiyo mnayoiotesha au ni Sisi ndio wenye
kuiotesha? 65 Tungetaka tungeifanya iwe mapepe, mkabaki
mnalalamika... 66 Sisi tumeingia gharama (buree)! 67 Bali
sisi tumenyimwa (matunda ya kazi yetu)! 68 Je, mnayaona
maji mnayoyanywa? 69 Je, ni nyinyi mliyoyashusha kutoka
mawinguni au ni Sisi ndio tunaoyashusha? 70 Tungependa
tungeyafanya ya chumvi kali. Si bora mkashukuru?
71 Je, mnauona moto mnaouwasha? 72 Ni ninyi mliouumba
mti wake au Sisi ndio Waumbaji? 73 Sisi tumeufanya uwe
ni ukumbusho na manufaa kwa wasafiri jangwani. 74 Basi
litakase na washirika jina la Mola Wako Mlezi, aliye Mkuu.

75. Naapa kwa sehemu za kutua nyota! 76. Na kwa kweli hiki

ni kiapo kikubwa sana, laiti mngejua... 77. Kwamba hakika
hii ni Qur'an Tukufu, 78. Katika Kitabu kinachohifadhiwa.
79. Wasikiguse ila walio tohara. 80. Ni ufunuo unaotoka kwa
Mola Mlezi wa walimwengu wote 81. Je, maneno kama haya
nyie mnayafanya ni upuuzi? 82. Na mnafanya kula yenu (iwe)
ni kuitangaza kuwa ni uwongo?

83. Yawaje basi inapofika roho kooni (hamwezi kusaidia)?
84. Na nyinyi wakati huo (mpo) mkiangalia tu! 85. Lakini
Sisi tuko karibu zaidi naye kuliko nyinyi, lakini hamuoni tu!
86. Lau (kweli) nyinyi hamumo katika mamlaka (yangu),
87. Kwa nini hamuirudishi, ikiwa nyinyi mnasema kweli?
88. Basi akiwa (huyo anayefariki) miongoni mwa
waliosogezwa karibu, 89. Itakuwa ni mapumziko, starehe na
Bustani zenye neema. 90. Na akiwa katika wale wa mkono wa
kuume, 91. Basi amani ni yako kwa kuwa miongoni mwa wale
wa mkono wa kuume. 92. Na ama akiwa katika wanaoufanya
ukweli ni uwongo, wapotevu, 93. Basi mapokezi yake ni maji
yanayochemka, 94. Na kuungua Motoni. 95. Hakika huu ni
ukweli wa yakini. 96. Basi litakase na washirika jina la Mola
Wako, Mkuu.

## 57. Sura Al-Hadid

## SURA YA CHUMA

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 Vyote vilivyomo katika mbingu na ardhi, vinamtakasa
Mwenyezi Mungu na mshirika. Na Yeye Ndiye Mwenye
nguvu, Mwenye hekima kuu. 2 Ni wake ufalme wa mbingu

na ardhi. Yeye ndiye anayetoa uhai na mauti, na Yeye ni
Mwenye uwezo juu ya kila kitu. 3 Yeye Ndiye wa mwanzo na
ndiye wa mwisho, aliye wazi na aliye siri, Naye Ndiye Mjuzi
wa kila kitu. 4 Yeye Ndiye aliyeziumba mbingu na ardhi
katika siku sita, na Yeye yuko imara juu ya ufalme (wake) wa
enzi. Anayajua yanayoingia ardhini na yanayotoka humo. Na
yanayoshuka kutoka mbinguni, na yanayopanda huko. Naye
yuko pamoja nanyi popote mlipo. Na Mwenyezi Mungu ni
Mwenye kuyaona yote mnayoyatenda. 5 Ni Wake ufalme wa
mbingu na ardhi. Na kwa Mwenyezi Mungu mambo yote
hurejeshwa. 6 Huuingiza usiku katika mchana, na huuingiza
mchana katika usiku. Na Yeye ni Mwenye kuyajua yote
yaliyomo vifuani.

7 Mwaminini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake; na
toeni katika alivyowafanya nyie kuwa warithi wake. Basi
walioamini miongoni mwenu, na wakatoa, wana malipo
makubwa. 8 Na mna nini nyie hata hamumwamini Mwenyezi
Mungu na hali Mtume anawaita mumwamini Mola Wenu
Mlezi? Naye amekwishawapa ahadi, ikiwa nyinyi ni waumini.
9 Yeye Ndiye anayemteremshia mja Wake Aya zinazobainisha
wazi ili awatoe katika giza nene kuapeleka kwenye mwanga.
Na hakika Mwenyezi Mungu kwenu ni Mpole mno, Mwenye
huruma nyingi. 10 Na mna nini nyie hata msitoe katika njia
ya Mwenyezi Mungu, ilhali urithi wa mbingu na ardhi ni wa
Mwenyezi Mungu? Hawalingani katika nyinyi wale waliotoa
kabla ya ushindi na wakapigana vita. Hao wana daraja kubwa
zaidi, kuliko wale waliotoa na wakapigana baadaye. Lakini
wote hao Mwenyezi Mungu amewaahidi (malipo) mema. Na
Mwenyezi Mungu ana habari za mnayoyatenda.

11. Ni nani atakayemkopesha Mwenyezi Mungu mkopo

mzuri, apate kumrudishia maradufu yake, na afaidi ujira
mwema? 12. Siku utakapowaona waumini wanaume na
waumini wanawake, mwanga wao uko mbele yao na
kuume kwao. (Wataambiwa): ‘Habari njema kwenu hii leo
ni Bustani ambazo mito hububujika chini yake, mkakae
humo milele. Huko ndiko kufuzu kukubwa. 13. (Ni) Siku
wanafiki wanaume na wanafiki wanawake watawaambia
walioamini: ‘Tungojeni ili tupate mwangaza kidogo kutoka
kwenye nuru yenu’! Wataambiwa, ‘rudini nyuma yenu
mkautafute mwangaza huko!’ Ndipo ukuta utainuliwa baina
yao (na waumini). (Ukuta) wenye mlango: ndani yake mna
huruma, na upande wake wa nje kuna adhabu. 14. Watawaita:
‘Hivi hatukuwa pamoja nanyi’? Watawajibu: ‘Bila shaka!
Lakini nyie mlijitumbukiza wenyewe kwenye vishawishi,
mkasitasita, na mkatia shaka (ahadi ya Mola) na tamaa
zikawatamalaki, mpaka ikafika amri ya Mwenyezi Mungu,
na Shetani akawadanganya kuhusu Mwenyezi Mungu.
15. Basi leo haitapokelewa kutoka kwenu fidia yeyote, Wala
kutoka kwa wale walio kufuru. Makazi yenu ni Motoni. Huo
ndiyo mahali mnapostahiki. Ni marejeo mabaya yaliyoje!

16. Hivi muda bado haujawadia kwa wale walioamini,
kwamba nyoyo zao ziwe na unyenyekevu zikumbuke
(kumtaja) Mwenyezi Mungu na kwa ajili ya ukweli
uliobainika? Na kwamba wasiwe kama wale waliopewa
Kitabu kabla yao, lakini muda mrefu ukawapitia na hivyo
nyoyo zao zikawa ngumu? Na wengi wao ni watu wapotovu.
17. Jueni kwamba Mwenyezi Mungu huirudisha ardhi kwenye
uhai baada ya kuwa imekufa. Tumewabainishia Ishara ili
mpate kutia akili.

18. Kwa hakika wanaume wanaotoa sadaka, na pia

wanawake wanaotoa sadaka, na wakamkopesha Mwenyezi Mungu mkopo mzuri, watazidishiwa maradufu na watapata ujira mwema. [19.] Na waliomwamini Mwenyezi Mungu na Mitume Wake, hao ndio waumini wa dhati, na ni mashahidi mbele ya Mola Wao, watapata ujira wao na mwangaza wao. Na waliokufuru na wakakadhibisha Ishara Zetu, hao ndio watu wa Motoni.

[20.] Jueni ya kwamba maisha ya duniani ni mchezo, na kipenda roho, na pambo, na kujifaharisha mmoja kwa mwingine, na kushindana kwa wingi wa mali na watoto. Ni kama mfano wa mvua ambayo huwafurahisha wakulima (kukua kwa) mimea yake, kisha hunyauka ukaiona ina rangi ya njano kisha ikawa makapi. Na Akhera kuna adhabu kali na pia maghufira kutoka kwa Mwenyezi Mungu na radhi. Na maisha ya dunia si chochote ila ni starehe ya udanganyifu. [21.] Kuweni wa mbele katika kuomba msamaha wa Mola wenu Mlezi na Pepo ambayo upana wake ni kama upana wa mbingu na ardhi. Imeandaliwa kwa wanaomwamini Mwenyezi Mungu na Mitume Wake. Hiyo ndiyo hisani ya Mwenyezi Mungu anayompa amtakaye. Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa hisani.

[22.] Hakuna maafa yoyote yanayotokea duniani au yawapatayo nyie wenyewe isipokuwa huwa yamekwisharekodiwa katika daftari (hata) kabla ya kuyafanya yatokee. Hakika hayo kwa Mwenyezi Mungu ni mepesi. [23.] Ili msisikitike kwa kile msichokipata, na wala msijigambe kwa alichowazawadia (mwenyezi Mungu). Na Mwenyezi Mungu hampendi yeyote anayejivuna, na kujigamba... [24.] Wale wafanyao ubakhili, na wakawashurutisha watu wafanye ubakhili. Na anayegeuka

(Kuacha amri ya Mola) , basi Mwenyezi Mungu ni Mwenye
kujitosheleza, Mstahiki wa sifa zote njema.
25. Kwa hakika tuliwatuma Mitume Wetu na dalili wazi
wazi, na tukateremsha Kitabu pamoja nao na mizani (ya
mema na mabaya), ili watu wasimamie haki na uadilifu.
Na pia tumeteremsha chuma, ndani yake mna (malighafi
ya kusababisha) madhara makubwa, pia faida nyingi
kwa binadamu. Ili Mwenyezi Mungu awajaribuni nani
atamnusuru Yeye na Mitume Wake (hata) katika mawazo
yake ya faragha. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye
nguvu Mwenye kushinda.
26. Na hakika tulimtuma Nuh (Noah) na Ibrahim (Abraham)
na tukaweka Utume na Kitabu (viwe) katika kizazi chao. Basi
wapo miongoni mwao walioongoka, lakini wengi katika wao
ni wapotofu. 27. Kisha nyuma yao tukawafuatisha Mitume
Wetu. Na tukamfuatisha Isa bin Maryam (Yesu mtoto wa
Maria), na tukampa Injili (Gospel). Na tukatia upole na huruma
katika nyoyo za wafuasi wake. Na utawa walioubuni... Sisi
hatukuwaamrisha hilo; isipokuwa (wameubuni) kutaka radhi
za Mwenyezi Mungu. Lakini hawakuuchunga ipasavyo. Basi
wale walioamini kati yao tuliwapa ujira wao. Lakini wengi
wao ni wapotofu, waasi.
28. Enyi walioamini! Mcheni Mwenyezi Mungu na
mwaminini Mtume Wake, atawapa mara mbili maradufu
katika huruma Yake, na atawapa nuru ya kutembelea (katika
njia yake, msipotee), na atawaghufiria. Na Mwenyezi Mungu
ni Mwingi wa maghufira, Mwingi wa huruma. 29. Ili Wayahudi
na Wakristo (watu wa Kitabu) wajue kwamba wao hawana
uwezo wowote wa (kuzuia) fadhila za Mwenyezi Mungu.
Na kwamba fadhila zote zimo mikononi mwa Mwenyezi

Mungu, humpa amtakaye. Kwani Mwenyezi Mungu Ndiye Mwenye fadhila kubwa.

58. Sura Al-Mujadila

## SURA YA (KISA CHA) MWANAMKE MWENYE MADAI

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 Hakika Mwenyezi Mungu ameyasikia maneno ya
mwanamke anayekufikishia madai yake kuhusu mumewe,
huku akimshitakia Mwenyezi Mungu (Katika Swala). Na
Mwenyezi Mungu anayasikia majibizano yenu wawili.
Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia, Mwenye
kuona.
2 Wale miongoni mwenu wanaowalinganisha wake zao na
mama zao (dhihari), hao si mama zao. Mama zao ni wale tu
waliowazaa. Na hakika hao wanasema maneno machafu na ya
uzushi. Na hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe,
Mwingi wa maghufira. 3 Na wale wanaowalinganisha wake
zao na mama zao, kisha wakajirudia kuachana na yale
walioyasema, basi (hukumu) ni kumwacha huru mtumwa
kabla hawajagusana (jamiiana). Hilo liwe onyo kwenu. Na
Mwenyezi Mungu anayajua mnayoyatenda. 4 Na asiyepata,
basi afunge miezi miwili mfululizo kabla hawajagusana.
Na asiyeweza basi awalishe masikini sitini. Hivyo, ili
mumwamini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake. Na hiyo

ndiyo mipaka ya Mwenyezi Mungu. Na watakaopinga wana
adhabu chungu.

5. Hakika wanaopingana na Mwenyezi Mungu na Mtume
Wake, watadhalilishwa (kwa kufa) kama walivyodhalilishwa
wale waliokuwa kabla yao. Na tulikwishateremsha Ishara
zilizo wazi. Na makafiri watapata adhabu ifedheheshayo.
6. Siku Mwenyezi Mungu atapowafufua wote, na awaambie
yale waliyoyatenda. Mwenyezi Mungu ameyarekodi na wao
wameyasahau! Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kushuhudia
kila kitu.

7. Hivi huoni kwamba Mwenyezi Mungu anajua vilivyo
katika mbingu na vilivyo katika ardhi? Hawanong'oni
(watu) watatu ila Yeye huwa wa nne wao. Wala watano
ila Yeye huwa wa sita wao. Wala wachache kuliko hao au
wengi zaidi, ila Yeye huwa pamoja nao popote pale walipo.
Kisha Siku ya Kiyama atawaambia waliyoyatenda. Hakika
Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu. 8. Kwani huwaoni
wale waliokatazwa kunong'ona, kisha wakayarudia yale
waliyokatazwa, na wakanong'onezana juu ya mambo ya
dhambi na uadui, na ya kumwasi Mtume? Na wanapokuja
kwako hukuamkua kwa namna ambayo Mwenyezi Mungu
hajakuamkua. Na husema katika nafsi zao: Mbona Mwenyezi
Mungu hatuadhibu kwa haya tuyasemayo? Jahannamu
itawatosha. Wataingia humo! Ni mwishio mbaya sana.

9. Enyi walioamini! Mnaponong'onezana msinong'onezane
kwa sababu ya mambo ya madhambi, na uadui, na kumwasi
Mtume. Bali nong'onezaneni kwa kutenda mema na
kumchamungu. Na mcheni Mwenyezi Mungu ambaye
Kwake mtakusanywa. 10. Kwa hakika minong'ono-nong'ono
inaletwa na Shetani ili awatie huzuni wale walioamini. Ila

Shetani hatawadhuru wao chochote isipokuwa kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Juu ya Mwenyezi Mungu pekee ndiyo yawe mategemeo ya waumini.

11. Enyi walioamini! Mkiambiwa toeni nafasi katika vikao, toeni nafasi. Mwenyezi Mungu atawapa nafasi. Na mkiambiwa ondokeni, ondokeni. Mwenyezi Mungu atawainua walioamini miongoni mwenu na waliopewa elimu, daraja za juu. Na Mwenyezi Mungu kwa mnayoyatenda anazo habari.

12. Enyi walioamini! Mkitaka kwenda chemba kwa mazungumzo ya faragha na Mtume, tangulizeni sadaka kabla ya mazungumzo yenu ya siri. Hiyo ni bora kwenu na ina usafi zaidi. Na ikiwa hamkupata cha kutoa, basi Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa maghufira, Mwingi wa huruma. 13. Hivi mnaona ubakhili kutanguliza sadaka kabla ya mazungumzo yenu ya faragha? Ikiwa hamkufanya hivyo, na Mwenyezi Mungu akawasamehe, basi dumisheni Swala, na toeni Zaka, na mtiini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake. Na Mwenyezi Mungu ana habari kwa yale mnayoyatenda.

14. Je, huwaoni wale waliofanya urafiki na watu ambao Mwenyezi Mungu amewakasirikia? Hao si katika nyinyi, wala nyie si katika wao. Na huapa kwa uwongo, na hali ya kuwa wanajua. 15. Mwenyezi Mungu amewaandalia adhabu kali. Kwa hakika waliyokuwa wakiyatenda ni maovu kabisa. 16. Wamefanya viapo vyao kuwa ni ngao ya kuwakinga, wakazuia watu na njia ya Mwenyezi Mungu. Basi watapata adhabu ya kufedhehesha.

17. Hautawafaa chochote utajiri wao, wala watoto wao kwa Mwenyezi Mungu, na wao ndio watu wa motoni. Wao humo watakaa milele. 18. Siku atakayowafufua Mwenyezi

Mungu hao wote; wamwapie Yeye kama wanavyowaapia nyinyi. Watadhani kiapo chao hicho kimewafaa! La hasha! Kwa hakika wao ni waongo. [19.] Shetani amewatamalaki na akawasahaulisha kumkumbuka Mwenyezi Mungu. Hao ndio Hizb-Shaytan, 'kundi la Shetani'. Ndiyo! Hakika kundi la Shetani ndilo litalopata hasara. [20.] Hakika wanaompinga Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, hao ndio miongoni mwa wale watakaodhalilishwa zaidi. [21.] Mwenyezi Mungu amekwisha hukumu: 'Mimi na Mitume Wangu ndiyo tutakaoshinda (njama zote)' Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mwenye kushinda.

[22.] Huwezi kukuta watu wanaomwamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho wakiwapenda wanaompinga Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, hata kama wangekuwa baba zao, au watoto wao, au kaka zao, au ukoo wao. Hao (Mwenyezi Mungu) amethibitisha imani katika nyoyo zao, na amewatia nguvu kwa Roho kutoka Kwake. Na atawaingiza katika mabustani ambayo hububujika mito ya maji chini yake. Humo wataishi. Mwenyezi Mungu yuko radhi nao, na wao wako radhi Naye. Hao ndio Hizbullah, 'kundi la Mwenyezi Mungu'. Ndiyo! Hakika kundi la Mwenyezi Mungu ndilo litakalofaulu.

59. Sura Al-Hashr

# SURA YA MKUSANYIKO

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 Vinamtakasa Mwenyezi Mungu na mshirika (vyote)
vilivyomo mbinguni na vilivyo katika ardhi. Na Yeye Ndiye
Mwenye nguvu, Mwenye hekima. 2 Yeye Ndiye Aliyewatoa
waliokufuru miongoni mwa watu wa Kitabu katika nyumba
zao wakati wa mkusanyiko wa kwanza (wa majeshi).
Hamkudhani kuwa wangetoka; na wao walidhani kuwa
ngome zao zitawalinda dhidi ya Mwenyezi Mungu. Lakini
(ghadhabu ya) Mwenyezi Mungu iliwafikia kutoka mahali
wasipopatazamia, na akatia hofu katika nyoyo zao, wakawa
wanazibomoa nyumba zao kwa mikono yao wenyewe na
mikono ya Waislamu. Basi zingatieni (onyo hili), enyi wenye
macho (muone)!

3 Na laiti si kuwa Mwenyezi Mungu alikwishawahukumia
kuhama, kwa hakika angewaadhibu hapa duniani (kwanza),
na huko Akhera wana adhabu ya Moto. 4 Hayo ni kwa sababu
walimpinga Mwenyezi Mungu na Mtume Wake. Na yeyote
anayempinga Mwenyezi Mungu, basi hakika Mwenyezi
Mungu ni Mkali wa kuadhibu. 5 Mitende (michanga) yoyote
mlioikata au mkaiacha imesimama vile vile juu ya mashina
yake, basi ilikuwa kwa idhini ya Mwenyezi Mungu, ili
kuwafedhehesha hao waasi wapotofu (wa Bani Nadhir).

6. (Mali) aliyoirudisha Mwenyezi Mungu kwa Mtume
Wake kutoka kwao, hamkuikimbilia kwa farasi wala
ngamia (imepatikana bila vita). Lakini Mwenyezi Mungu

huwapa madaraka Mitume wake juu ya yeyote amtakaye.
Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye uwezo juu ya kila kitu.
7. (Mali) aliyoirudisha Mwenyezi Mungu kwa Mtume
Wake kutoka kwa watu wa vijijini (bila vita) ni kwa ajili ya
Mwenyezi Mungu, na Mtume, na jamaa zake, na yatima,
na masikini, na walio safarini; ili isiwe ikizunguka baina ya
matajiri pekee baina yenu. Hivyo, kile alichowapa Mtume
chukueni (hicho), na alichowanyima asiwape kiacheni.
Na mtiini Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni
Mkali wa kuadhibu. 8. (Fungu katika mali hizo) Wapewe
mafukara katika waliohamia (Madina) ambao walifukuzwa
kutoka (Makka, wakaacha) majumba yao na mali zao, kwa
ajili ya kutaka fadhila na radhi za Mwenyezi Mungu, na
wanamnusuru Mwenyezi Mungu na Mtume Wake. Hao ndio
wakweli.

9. Na wale walio na maskani (Madina) na imani kabla ya
hao (kufika), wanawapenda waliohamia kwao, wala hawana
hamu katika vifua vyao ya walivyonavyo (Wahamiaji), bali
wanawapendelea hao zaidi kuliko nafsi zao, ingawa wao
wenyewe ni wahitaji. Na mwenye kuepushwa na uchoyo wa
nafsi yake, basi hao ndio wenye kufaulu. 10. Na waliokuja
baada yao wanasema: Mola Wetu Mlezi! Utughufirie sisi na
ndugu zetu waliotutangulia kwa imani, wala usijaalie ndani
ya nyoyo zetu uhasama na chuki dhidi ya walioamini. Mola
Wetu Mlezi! Hakika Wewe ni Mpole, Mwingi wa huruma.

11. Je, Huwaoni wanaofanya unafiki, wanawaambia ndugu
zao waliokufuru katika Watu wa Kitabu: Mkifukuzwa mji
na sisi hapana budi tutatoka pamoja nanyi, wala hatutamtii
yeyote abadan dhidi yenu. Na mkishambuliwa kwa vita
lazima tutawasaidia. Na Mwenyezi Mungu anashuhudia

kuwa hao hakika ni waongo. [12.] Endapo watafukuzwa mji hawatatoka pamoja nao. Na wakishambuliwa kwa vita hawatawasaidia. Na kama wakiwasaidia basi watageuza migongo yao wakimbie. Hivyo hawatapata msada wowote.

[13.] Hakika nyinyi ni tishio zaidi katika nyoyo zao kuliko Mwenyezi Mungu. Hii ni kwa kuwa hao ni watu wasiofahamu. [14.] Hawatapigana dhidi yenu (hata) wakiwa pamoja, isipokuwa katika vijiji vilivyoimarishwa kwa ngome au nyuma ya kuta. Ugomvi uliopo baina ya wao kwa wao ni mkubwa sana. Utawadhania wako pamoja, kumbe nyoyo zao zimegawanyika. Hivyo ni kwa kuwa wao ni watu wasio na hekima.

[15.] Ni kama mfano wa waliokuwa kabla yao hivi karibuni. Walionja (matokeo) mabaya ya mwenendo wao. Nao watapata adhabu iliyo chungu. [16.] Ni kama mfano wa Shetani pale alipomwambia mwanadamu ‘Mkane Mwenyezi Mungu’ Lakini alipomkana, akamwambia, ‘Aka! Mimi siko nawe. Kwa kweli mimi namwogopa Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa walimwengu wote’. [17.] Basi hatima ya wote wawili itakuwa kuingia Motoni, wadumu humo daima; na hayo ndiyo malipo ya watenda maovu.

[18.] Enyi walioamini! Mtiini Mwenyezi Mungu, na kila mtu aangalie ametanguliza nini kwa ajili ya Kesho. Na mtiini Mwenyezi Mungu. Kwani Mwenyezi Mungu ana habari za mnayoyatenda. [19.] Wala msiwe kama wale waliomsahau Mwenyezi Mungu, na Yeye akawafanya wazisahau nafsi zao. Hao ndio waasi wapotofu. [20.] Hawawi sawa watu wa Motoni na watu wa Peponi. Watu wa Peponi ndio wenye kufuzu.

[21.] Lau tungeliiteremsha hii Qur’an juu ya mlima, basi bila ya shaka ungeliuona ukinyenyekea, ukipasuka kwa hofu

ya Mwenyezi Mungu. Na mifano hiyo tunawapigia watu ili wafikiriye. [22.] Yeye Ndiye Mungu, ambaye hapana mungu wa kweli isipokuwa Yeye tu. Mwenye kuyajua yaliyofichikana na yanayoonekana. Yeye Ndiye Mwingi wa huruma, Mwingi wa kuhurumia. [23.] Yeye Ndiye Mwenyezi Mungu ambaye hapana mungu wa kweli isipokuwa Yeye tu. Mfalme wa vyote, Mtakatifu, Chanzo cha Amani, Mdhamini wa usalama, Mwenye kufunika viumbe wote kwa nguvu, hifadhi na kutamalaki, Mwenye nguvu, Afanyaye alitakalo, Mkuu. Ametakasika Mwenyezi Mungu na hayo wanayomshirikisha nayo. [24.] Yeye Ndiye Mwenyezi Mungu, Muumbaji-Mbunifu, Muumbaji-Mwendelezaji, Mtia sura, Mwenye Majina mazuri kabisa. Mbingu na Ardhi vinatamka sifa na utukufu wake na kumtakasa. Naye ni Mwenye nguvu, Mwenye hekima.

## 60. Sura Al-Mumtahana

## SURA YA (MWANAMKE) KUTATHMINIWA

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

[1] Enyi walioamini! Msiwafanye maadui Wangu na maadui wenu kuwa marafiki, mkiwapa mapenzi, ingawa wao wamekwishaukataa ukweli uliowafikia. Wakamfukuza Mtume na nyinyi pia kwa sababu (tu) mnamwamini Mwenyezi Mungu, Mola Wenu Mlezi. Endapo mmetoka kwenu kwa lengo la kujikakamua kwa bidii kufuata njia Yangu na kutafuta radhi Yangu (msiwafanye marafiki). Mnafanya urafiki nao kwa siri, ilhali Mimi nayajua mnayoyaficha na mnayoyaweka wazi. Na mwenye kufanya hivyo kati yenu

hakika atakuwa amepotea njia ya sawa. 2 Kama wakiweza
kuwatia mikononi basi (watawageukia) kuwa maadui kwenu,
na watawanyooshea mikono yao na ndimi zao kwa uovu.
Wao hutamani nyie pia muwe mnaokana ukweli (kama wao).
3 Si jamaa zenu wala watoto wenu watakuwa na manufaa
yoyote kwenu siku ya Kiyama. Mwenyezi Mungu pekee
atapambanua baina yenu, na Mwenyezi Mungu anayaona
vizuri sana yote mnayoyatenda.

4 Hakika nyinyi mna mfano mzuri wa kufuata kwa Ibrahim
na wale waliokuwa pamoja naye. Pale walipowaambia watu
wao: 'Hakika sisi tumejitenga nanyi na hivyo mnavyoviabudu
kinyume cha Mwenyezi Mungu. Tumewakataa nyie! Na
uadui na chuki tayari zimejitokeza baina yetu na nyie hadi
mumwamini Mwenyezi Mungu peke Yake'. Isipokuwa
(msifuate mfano wa) kauli ya Ibrahim kumwambia baba yake
(aliyemkana Mungu): 'Nitakuombea msamaha; ingawaje
sina madaraka yoyote kwa ajili yako mbele ya Mwenyezi
Mungu'. Mola Wetu Mlezi! Wewe tu tunakutegemea, na
Kwako tu tunaelekea na Kwako tu ndiyo marejeo yetu.
5 Mola Wetu Mlezi! Usitufanye sisi kuwa majaribio kwa wale
waliokufuru, na utusamehe ewe Mola wetu Mlezi! Hakika
Wewe Ndiye Mwenye nguvu, Mwenye hekima. 6 Hakika
umekuwa mfano mzuri kwenu wa kufuata katika mwenendo
wao, kwa anayemtarajia Mwenyezi Mungu na (kuogopa)
Siku ya Mwisho. Na mwenye kugeuka (asifuate) basi hakika
Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujitosheleza, Mstahiki sifa
zote njema. 7 Inawezekana kabisa kwamba Mwenyezi Mungu
akatia mapenzi baina yenu na wale mnawaona maadui. Na
Mwenyezi Mungu ni Muweza, na Mwenyezi Mungu ni
Mwingi wa maghufira Mwingi wa huruma.

8. Mwenyezi Mungu hawakatazi kuwafanyia wema na
uadilifu wale ambao hawakupiga nyinyi vita kwa ajili
ya imani yenu, wala hawakuwatoa makwenu. Hakika
Mwenyezi Mungu huwapenda wafanyao haki na uadilifu.
9. Hakika Mwenyezi Mungu anawakataza (dhidi ya) wale
tu waliowapiga vita kwa ajili ya imani yenu, na wakawatoa
makwenu, na wakasaidia (wengine) katika kufukuzwa
kwenu.... kuwafanya marafiki zenu. Na wanaowafanya hao
marafiki basi hao ndio madhalimu.

10. Enyi walioamini! Wakiwajia wanawake Waumini
waliohama, basi wafanyieni tathmini. Mwenyezi Mungu
Ndiye Mwenye kujua zaidi imani yao. Mkiwa na uhakika
nao kuwa ni waumini, basi msiwarudishe kwa makafiri. Wao
si wake wao wa halali tena, wala wao si waume halali kwa
wanawake hao. Lakini wapeni hao (waume) mahari waliyotoa.
Na haitakuwa vibaya kwenu kuwaoa mkiwapa mahari yao.
Wala msiwaweke wanawake makafiri katika kifungo cha
ndoa zenu. Na ombeni (mrudishiwe) mlichokitoa, na wao
waombe walichokitoa. Hiyo ndiyo hukumu ya Mwenyezi
Mungu, anahukumu baina yenu. Na Mwenyezi Mungu ni
Mwenye kujua, Mwenye hekima. 11. Na akitoroka yeyote
katika wake zenu kwenda kwa makafiri, kisha mkateka nyara
katika vita, basi wapeni waliokimbiwa na wake zao kiasi
cha mahari waliyoyatoa (katika fidia itakayopatikana). Na
mcheni Mwenyezi Mungu ambaye mnamwamini.

12. Ewe Nabii! Watakapokujia wanawake waumini
wakakupa ahadi kwamba hawatamshirikisha Mwenyezi
Mungu na chochote, wala hawataiba, wala hawatazini,
wala hawatawauwa watoto wao, wala hawataleta uzushi wa
makusudi, wala hawatakuasi katika jambo lolote la haki. Basi

kubaliana na kiapo chao cha utiifu, na uwaombee msamaha
kwa Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi
wa maghufira, Mwenye kurehemu.

13. Enyi walioamini! Msiwafanye rafiki watu ambao
Mwenyezi Mungu amewakasirikia. Hao wamekwishakata
tamaa ya Akhera, kama makafiri walivyowakatia tamaa watu
wa makaburini.

61. Sura As-Saf

# SURA YA (UMUHIMU WA) KUPANGA SAFU VITANI

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 Vinamtakasa Mwenyezi Mungu na mshirika yoyote
vilivyomo mbinguni na vilivyo katika ardhi. Na Yeye ni
Mwenye nguvu, Mwingi wa hekima. 2 Enyi walioamini!
Kwa nini mnasema msiyofanya? 3 Ni udhia mkubwa kwa
Mwenyezi Mungu kusema msiyoyafanya. 4 Kwa hakika
Mwenyezi Mungu anawapenda wanaopigana katika Njia
Yake hali wako katika safu kana kwamba wao ni jengo la
saruji lililo wima, imara.

5 Na kumbuka pale Musa (Moses) alipowaambia watu
wake: ‘Enyi watu wangu! Kwa nini mnaniudhi, nanyi mnajua
kuwa mimi ni Mtume wa Mwenyezi Mungu niliyetumwa
kwenu? Walipokwenda kombo, Mwenyezi Mungu naye
aliziachia nyoyo zao ziende kombo. Na Mwenyezi Mungu
hawaongoi watu waasi, wapotevu.

6. Na pale Isa bin Maryam (Yesu mwana Maria)
aliposema: ‘Enyi Wana wa Israeli! Hakika mimi ni Mtume
wa Mwenyezi Mungu kwenu, ninayethibitisha yaliyokuwa
kabla yangu katika Torat, na mwenye kutoa habari njema
za Mtume atakayekuja baada yangu; jina lake ni Ahmad’.
Lakini alipowaletea hoja zilizo wazi, walisema: ‘Huu ni
uchawi dhahiri!’ 7. Na ni nani anayefanya makosa makubwa
zaidi ya yule anayemzulia Mwenyezi Mungu uwongo, ilhali
yeye analinganiwa kwenye Uislamu? Na Mwenyezi Mungu
hawaongoi watu wafanyao mabaya. 8. Wanataka kuuzima
mwangaza wa Mwenyezi Mungu kwa vinywa vyao. Na
Mwenyezi Mungu atakamilisha mwangaza Wake ijapokuwa
makafiri watachukia. 9. Yeye Ndiye Aliyemtuma Mtume
Wake kwa uongofu na dini ya kweli, ili aipe ushindi juu ya
dini zote, ijapokwa wapagani watachukia.

10. Enyi walioamini! Je, niwajulishe biashara itakayowaokoa
na adhabu iliyo chungu? 11. Mumwamini Mwenyezi Mungu
na Mtume Wake, na mfanye juhudi zenu zote katika Njia ya
Mwenyezi Mungu kwa mali zenu na roho zenu. Haya ni bora
kwenu, ikiwa nyinyi mnajua. 12. Atawasamehe dhambi zenu,
na atawaingiza katika Mabustani ambayo hupita mito ya
maji chini yake, na maskani nzuri katika Bustani za milele.
Huko ndio kufuzu kukubwa. 13 Na kinginecho mkipendacho
- nusura itokayo kwa Mwenyezi Mungu na ushindi ulio
karibu. Na wape habari njema waumini!

14. Enyi walioamini! Kuweni wasaidizi wa Mwenyezi
Mungu, kama alivyosema Isa bin Maryam (Yesu mwana
Maria) kuwaambia wanafunzi wake: ‘Nani wasaidizi wangu
kwa Mwenyezi Mungu’? Wanafunzi wakasema: ‘Sisi ni
wasaidizi wa Mwenyezi Mungu’! Basi kundi moja la Wana

wa Israeli likaamini, na kundi jingine likakufuru. Tukawaunga mkono walioamini dhidi ya maadui zao, wakawa wenye kushinda.

## 62. Sura Al-Jum'a

## SURA YA (SIKU YA) IJUMAA

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 Vinamtakasa Mwenyezi Mungu na mshirika yeyote,
vilivyomo katika mbingu na vilivyo katika ardhi. Yeye ni
Mfalme, Mtakatifu, Mwenye nguvu, Mwingi wa hekima.
2 Yeye Ndiye Aliyepeleka kwa watu wasiowahi kupewa
Maandiko Matakatifu, Mtume aliyetokana na wao, awasomee
Aya Zake, na awatakase (na upagani), na awafunze Kitabu
na hekima; japokuwa hapo nyuma walikuwa katika upotofu
ulio dhahiri. 3 Na kwa wengine miongoni mwao ambao bado
hawajaungana nao. Na Yeye Ndiye Mwenye nguvu, Mwingi
wa hekima. 4 Hayo ni fadhila za Mwenyezi Mungu humpa
amtakaye. Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa fadhila.

5 Mfano wa waliopewa jukumu la Torat, kisha
wasiipatilize, ni mfano wa punda anayebeba vitabu
vikubwa (asivyovifahamu). Mfano muovu mno wa watu
waliokadhibisha Ishara za Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi
Mungu hawaongoi watu wafanyao mabaya. 6 Sema: Enyi
walio Mayahudi! Ikiwa nyinyi mnadai kuwa ni vipenzi
vya Mwenyezi Mungu pasipo watu wengine, basi mtamani
mauti ikiwa mnasema kweli. 7 Wala hawatayatamani kamwe,
kwa sababu ya (matendo) ambayo mikono yao imekwisha

yatanguliza. Na Mwenyezi Mungu anawajua wafanya
mabaya. 8 Sema: hakika mauti mnayoyakimbia, bila ya
shaka yatawakuta tu. Kisha mtarudishwa kwa Mjuzi wa
yaliyo siri na yanayoonekana. Hapo atawaambia mliyokuwa
mkiyatenda.

9. Enyi walioamini! Ikinadiwa Swala siku ya Ijumaa,
nendeni upesi kwenye kumtaja ya Mwenyezi Mungu, na
acheni biashara. Hayo ni bora kwenu, kama mnajua. 10. Na
itakapokwisha Swala, tawanyikeni katika ardhi mtafute
hisani za Mwenyezi Mungu; na mkumbukeni Mwenyezi
Mungu kwa wingi ili mpate kufaulu. 11. Na wanapoona
biashara au pumbao wanayakimbilia hayo na wanakuacha
umesimama. Sema: 'Yaliyoko kwa Mwenyezi Mungu ni bora
kuliko pumbao na biashara. Na Mwenyezi Mungu ni bora ya
watoao riziki.

## 63. Sura Al-Munafiqun

## SURA KUHUSU WANAFIKI

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 Wanapokujia wanafiki husema: Tunashuhudia ya kuwa
wewe ni Mtume wa Mwenyezi Mungu. (Si) Mwenyezi
Mungu anajua kuwa wewe ni Mtume Wake! Na Mwenyezi
Mungu anashuhudia ya kuwa hakika wanafiki ni waongo.
2 Wamevifanya viapo vyao kuwa kinga, wakawazuia
(watu) kuifikia Njia ya Mwenyezi Mungu. Ni mabaya
mno wanayoyafanya hao. 3 Hiyo ni kwa sababu ya kuwa

waliamini, kisha wakakanusha imani. Kwa hiyo ukapigwa muhuri juu ya nyoyo zao; ndiyo maana hawafahamu.

[4] Na unapowaona, miili yao inakupendeza. Na wanaposema unasikiza maneno yao. (Lakini) wao ni kama magogo yaliyoegemezwa (Hayawezi kusimama yenyewe). Wao hudhania kila ukelele (unaopigwa) ni kwa ajili yao. Hao ni maadui; jihadhari nao. Mwenyezi Mungu amewalaani! Namna gani wamesalitiwa kuiacha haki? [5] Na wanapoambiwa: Njooni ili Mtume wa Mwenyezi Mungu awaombee msamaha, hugeuza vichwa vyao, na unawaona wanageuka, nao wamejaa kiburi. [6] Ni sawa kwao, ukiwatakia msamaha au usiwatakie msamaha, Mwenyezi Mungu hatawasamehe. Hakika Mwenyezi Mungu hawaongoi watu wafanyao mabaya.

[7.] Hao ndio wanaosema: Msitoe chochote kwa walioko kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu, ili wasambaratike. Na ilhali ni za Mwenyezi Mungu hazina za mbinguni na ardhini. Lakini wanafiki hawalijui hilo. [8.] Wanasema: Endapo tutarejea Madina, basi wenye hadhi na utukufu watawafukuza watwana wanyonge. Na ilhali ni wa Mwenyezi Mungu utukufu wote, na Mtume Wake, na Waumini. Lakini wanafiki hawalijui hilo.

[9.] Enyi walioamini! Zisiwashughulishe mali zenu, wala watoto wenu, kuacha kumkumbuka Mwenyezi Mungu. Na wenye kufanya hivyo hao ndio wenye hasara. [10.] Na toeni baadhi ya vile tulivyowapa, kabla hayajamfikia mmoja wenu mauti, kisha aseme: Mola Wangu Mlezi! Si ungenicheleweshea muda kidogo tu nipate kutoa sadaka, na niwe katika watu wema! [11.] Kamwe Mwenyezi Mungu hataicheleweshea roho

yoyote unapofika muda wake uliokadiriwa. Na Mwenyezi
Mungu ana habari za mnayoyatenda.

## 64. Sura Attaghabun

## SURA YA FAIDA NA HASARA YA PAMOJA

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 Vinamtakasa Mwenyezi Mungu na mshirika yeyote
vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini. Ni Wake Ufalme
na ni Zake sifa njema. Na Yeye ni Mwenye uweza juu ya kila
kitu. 2 Yeye Ndiye Aliyewaumba. Miongoni mwenu yupo
aliye kafiri, na yupo aliye Muumini. Na Mwenyezi Mungu
anayaona mnayoyatenda. 3 Ameziumba mbingu na ardhi
kwa uwiano adilifu, na akawapa sura, akazifanya nzuri sura
zenu. Na marejeo ni Kwake. 4 Anajua vilivyomo mbinguni na
ardhini, na anajua mnayoyafanya siri na mnayoyatangaza. Na
Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa yaliyomo vifuani.

5. Kwani haikuwafikia habari ya waliokufuru hapo zamani,
wakaonja matokeao mabaya ya matendo yao? Na wao wana
adhabu iliyo chungu. 6. Hayo ni kwa kuwa Mitume walikuwa
wakiwajia kwa hoja zilizo wazi, nao wakasema: ‘Hivi
wanadamu ndio watuongoze (isiwe malaika)?’ Wakakufuru,
na wakageuka upande. Na Mwenyezi Mungu si mhitaji. Na
Mwenyezi Mungu ni Mkwasi, naye ni Msifiwa.

7. Waliokufuru wanadai kuwa hawatafufuliwa. Sema:
Ndiyo. Naapa kwa Mola Wangu Mlezi, hapana shaka
mtafufuliwa, na kwa hakika mtaambiwa mliyoyafanya. Na
hilo ni jambo jepesi mno kwa Mwenyezi Mungu. 8. Basi

mumwamini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, na Nuru tuliyoiteremsha. Na Mwenyezi Mungu anazo habari kwa mnayoyatenda. 9. Siku atakayowakusanya kwa ajili ya Siku ya Mkutano. Hiyo ni siku ya faida na hasara. Na anayemwamini Mwenyezi Mungu na akatenda mema, atamfutia madhambi yake, na atamwingiza katika Bustani ambazo hupita mito chini yake, wakae humo milele. Huko ndiko kufuzu kukubwa. 10. Na waliokufuru na wakaona ishara zetu ni uwongo, hao ni watu wa Motoni, watakaa humo milele. Na hayo ndiyo marejeo mabaya.

11. Si msiba wa aina yeyote unaweza kutokea ila kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Na mwenye kumwamini Mwenyezi Mungu, huuongoza moyo wake. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu. 12. Na mtiini Mwenyezi Mungu, na mtiini Mtume. Mkigeuka, basi hakika jukumu la Mtume Wetu ni kufikisha ujumbe kwa uwazi tu. 13. Mwenyezi Mungu. Hapana mungu isipokuwa Yeye. Na juu ya Mwenyezi Mungu ndiyo wategemee Waumini.

14. Enyi walioamini! Hakika miongoni mwa wake zenu na watoto wenu wamo maadui zenu. Basi jihadharini nao. Na mkisamehe, na mkapuuzia, na mkafunika makosa yao, basi hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa msamaha, Mwenye kurehemu. 15. Hakika mali zenu na watoto wenu ni majaribio. Na kwa Mwenyezi Mungu kuna ujira mkubwa. 16. Basi mcheni Mwenyezi Mungu kadri muwezavyo, na sikieni, na mtii, na toeni kwa faida ya roho zenu. Na mwenye kuepushwa na uchoyo wa roho yake, basi hao ndio wenye kufaulu. 17. Mkimkopesha Mwenyezi Mungu mkopo mzuri, atawazidishia maradufu, na atawaghufiria. Na Mwenyezi

Mungu ni Mwingi wa shukrani, Mpole. 18. Mwenye kujua
ghaibu na dhahiri. Mwenye nguvu, Mwingi wa hekima.

## 65. Sura At-Talaq

# SURA YA TALAKA

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 Ewe Nabii! Mtakapowaacha wanawake, basi wapeni talaka
katika muda wao ulioruhusiwa, na hesabuni kwa makini
muda huo. Na mtiini Mwenyezi Mungu, Mola wenu Mlezi.
Msiwatoe katika nyumba zao, wala wasitoke wenyewe, ila
wakifanya tendo la uovu wazi wazi. Hiyo ndiyo mipaka ya
Mwenyezi Mungu, msiikiuke. Na mwenye kuikiuka mipaka
ya Mwenyezi Mungu, ameifanyia ubaya roho yake. Hujui
pengine Mwenyezi Mungu aweza akaleta baada yake hali
nyingine (kubadili uamuzi huo). 2 Basi wanapofikia muda
wao kamili, aidha warejeeni mkae nao kwa wema, au
tenganeni nao kwa wema. Na mshuhudishe mashahidi wawili
waadilifu miongoni mwenu. Na simamisheni ushahidi kwa
ajili ya Mwenyezi Mungu. Hivyo ndivyo anavyoagizwa
anayemwamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho. Na
amchaye Mwenyezi Mungu, daima humtengezea njia ya
kutokea. 3 Na humletea riziki kutoka (vianzio) asivyofikiria.
Na anayemtegemea Mwenyezi Mungu, Yeye humtosha
kabisa. Hakika Mwenyezi Mungu ni mwenye kutimiza jambo
lake. Mwenyezi Mungu amejaalia kila kitu na kipimo chake.

4 Na wale waliokoma kutoka hedhi katika wanawake
wenu, eda yao, ikiwa mna shaka yoyote, ni miezi mitatu. Na

wale ambao hawapati hedhi (pia ni hivyo). Na wenye mimba eda yao ni mpaka watakapojifungua. Na amchaye Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu humfanyia mambo yake yawe mepesi. [5] Hiyo ni amri ya Mwenyezi Mungu amewateremshia. Na anayemcha Mwenyezi Mungu atamfutia maovu yake, na atampa ujira mkubwa.

[6.] Wawekeni (hao walio katika eda) kwa namna ile ile mnavyokaa nyinyi kwa kadiri ya pato lenu. Na msiwanyanyase kwa kuwawekea vizuizi. Na wakiwa waja wazito, wagharamieni mpaka wajifungue. Na wakiwanyonyesha watoto wenu, basi wapeni malipo yao, na shaurianeni (juu ya malipo) kwa busara. Na endapo itawawia vigumu, basi na amnyonyeshee mwanamke mwingine. [7.] Mwenye kipato kizuri agharamie kadri ya kipato chake na ambaye kipato chake ni cha wastani, na atoe kwa kadri ya alivyomruzuku Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu hamkalifishi mtu isipokuwa kwa kadri ya alivyomruzuku. Mwenyezi Mungu atafanya baada ya dhiki faraja.

[8.] Ni wakazi wa miji mingapi chungu nzima waliokana kwa kiburi amri ya Mola Wao Mlezi na Mitume Wake? Ndipo tukaichukulia hatua ngumu miji hiyo na tukaiadhibu vikali. [9.] Wakaonja matokeo mabaya ya mwenendo wao, na mwisho wa mwenendo wao ulikuwa ni kuangamia. [10.] Mwenyezi Mungu amewaandalia adhabu kali. Basi mcheni Mwenyezi Mungu, enyi mliofahamu na mkaamini! Hakika Mwenyezi Mungu amewateremshia ukumbusho. [11.] Mtume anayewasomea Aya za Mwenyezi Mungu zinazobainisha wazi, ili kuwatoa walioamini na wakatenda mema kutoka katika dimbwi la giza, kuwapeleka kwenye mwangaza. Na yeyote anayemwamini Mwenyezi Mungu na akatenda mema,

atamwingiza katika Bustani ambazo hupita mito chini yake, wadumu humo milele. Mwenyezi Mungu amekwishampa riziki nzuri.

12. Mwenyezi Mungu ni Yule ambaye ameziumba mbingu saba, na katika ardhi mfano wa hizo. Amri Zake zinashuka kati yao. Ili mjue kwamba Mwenyezi Mungu ni Mwenye uwezo juu ya kila kitu, na kwamba Mwenyezi Mungu amekizunguka kila kitu kwa elimu yake.

## 66. Surah At-Tahrim

## SURA YA KUKATAZA

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 Ewe Nabii! Kwa nini unakifanya haramu kile ambacho
Mwenyezi Mungu amekifanya halali kwako? Unataka
kuwaridhisha wake zako! Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi
wa maghufira, Mwingi wa huruma. 2 Hakika Mwenyezi
Mungu amekwishawapa Sheria ya kufuta viapo vyenu. Na Mwenyezi Mungu ni Mola Wenu. Na Yeye ni Mwenye kujua, Mwingi wa hekima.

3 Pale Mtume alipomwambia mmoja wa wake zake jambo
la siri. Yule alipolifichua (kwa mwingine), Mwenyezi Mungu akamjulisha Mtume wake, akamjulisha baadhi na akaacha baadhi nyingine. (Mtume) alipomweleza hilo (mkewe aliyefichua), huyu akauliza: Nani aliyekwambia haya? Mtume akasema: Kaniambia Mjuzi Mwenye habari ya kila
kitu. 4 Kama nyinyi wawili mtatubia kwa Mwenyezi Mungu,
basi nyoyo zenu zimekwishaelekea huko. Na mkisaidiana

dhidi yake Mtume, basi hakika Mwenyezi Mungu Ndiye anayemlinda, na Jibrili, na waumini wema, na zaidi ya hayo, Malaika pia watasaidia. 5 Yumkini endapo (Mtume) atawapa nyie takala, Mola wake Mlezi akampa badali yenu wake (wengine) bora zaidi kuliko nyie: watiifu zaidi, waumini zaidi, wachamungu, wanaotubia, washika ibada, watenda kheri, wajane na wanawali.

6. Enyi walioamini! Okoeni nafsi zenu (nyie) na jamaa zenu na Moto ambao kuni zake ni watu na mawe. Wasimamizi wake ni Malaika wakali, wenye nguvu. Hawamuasi Mwenyezi Mungu kwa lolote analowaamrisha. Na wanafanya vile vile walivyoamrishwa. 7. (Watasema): Enyi waliokufuru! Msitoe visingizio leo. Hakika mnalipwa yale tu mliyokuwa mkiyatenda.

8. Enyi walioamini! Tubuni kwa Mwenyezi Mungu toba ya dhati! Asaa Mola Wenu Mlezi akawafutia maovu yenu na akawaingiza katika mabustani ambayo hupita mito chini yake. Siku ambayo Mwenyezi Mungu (hataruhusu) Mtume adhalilishwe, wala wale walioamini pamoja naye. Mwangaza wao utatangulia mbele yao na kuumeni kwao. Watasema, ewe Mola wetu Mlezi! Ufanye mwangaza wetu uwe kamili na utusamehe, hakika Wewe ni Mwenye uwezo juu ya kila kitu.

9. Ewe Nabii! Pambana na makafiri na wanafiki, na uwawekee ngumu! Na makazi yao ni Jahannamu. Mahali pabaya kabisa pa kurejea. 10. Mwenyezi Mungu amewapigia mfano waliokufuru: mke wa Nuhu na mke wa Lut. (Hawa) walikuwa chini ya waja Wetu wema wawili, katika jumla ya waja wetu. Lakini wakawafanyia waume zao uhaini, nao hawakuwafaa kitu kwa (kuwaepusha na adhabu ya)

Mwenyezi Mungu. Na ikasemwa: Ingieni Motoni pamoja na
wanaoingia!
11. Na Mwenyezi Mungu amewapigia mfano wa
walioamini: mke wa Firauni. Pale aliposema: Mola Wangu
Mlezi! Nijengee nyumba kwenye sehemu yako Peponi, na
uniokoe na Firauni na vitendo vyake, na uniokoe na watu
madhalimu. 12. Na Maryam binti Imran (Maria binti ya
Amran), aliyeilinda bikira yake, na tukampulizia ndani ya
mwili wake roho kutoka Kwetu, na akayasadiki maneno ya
Mola Wake Mlezi na Vitabu Vyake, na alikuwa miongoni
mwa (watumishi) watiifu.

## 67. Sura Al-Mulk

# SURA YA UFALME

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 Ametukuka ambaye Ufalme wote uko Mkononi Mwake, na
Yeye ni Muweza juu ya kila kitu. 2 Ambaye ameumba mauti
na uhai, ili awajaribu ni nani miongoni mwenu mwenye
vitendo vizuri zaidi. Na Yeye ni Mwenye nguvu, Mwingi wa
maghufira. 3 Aliyeumba mbingu saba moja baada ya nyingine.
Huwezi kuona ukosefu wowote wa uwiano katika uumbaji
wa Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema. Hebu zungusha
jicho lako! Unaona nyufa zozote? 4 Tena zungusha jicho lako
mara ya pili, litarejea kwako likiwa dhalili lililochoka.
5 Na kwa hakika tumeipamba mbingu ya karibu kwa
mataa, na tumeyafanya kuwa makombora ya kuwafukuzia
mashetani. Wao tumewaandalia adhabu ya Moto uwakao

vikali. 6 Na kwa waliomkufuru Mola Wao Mlezi ni
adhabu ya Jahannamu. Ni marejeo maovu yalioje hayo!
7 Watakapotupwa humo watasikia muungurumo wake ilhali
inafoka. 8 Inakaribia kupasuka kwa hasira. Kila likitupwa
kundi humo walinzi wake huwauliza: Kwani hakuwajia nyinyi
mwonyaji yeyote? 9 Watasema: Ndiyo! Alitujia mwonyaji,
lakini tukamwona mwongo, na tukasema: Mwenyezi Mungu
hakushusha (ujumbe) wowote. Nyinyi si lolote ila mko
katika upotovu mkubwa! 10 Na watasema: Laiti tungesikia
na kutumia akili zetu, tusingekuwa katika jumla ya watu wa
Motoni! 11 Hapo watakiri dhambi zao. Lakini, potelea mbali!
(hakuna msamaha) kwa watu wa Motoni!

12. Hakika wanaomcha na kumtii Mola Wao Mlezi
ingawa hawamwoni kwa macho, wana msamaha na malipo
makubwa. 13. Na mfiche maneno yenu au myaweke wazi
(ni sawa tu), hakika Yeye ni Mjuzi wa yaliyomo nyoyoni.
14. Hivi (mwanadamu) hajui aliyemwumba? Naye ndiye
ajuaye yaliyo siri zaidi, Mwenye habari ya yote.

15. Yeye Ndiye aliyeifanya ardhi muweze kuishi, basi
tembeeni katika pande zake, na kuleni katika riziki zake.
Na Kwake Yeye ndio kufufuliwa. 16. Je, mnadhani mko
salama kwamba Huyo ambaye ufalme wake uko mbinguni
hatawadidimiza ardhini wakati inatikisika? 17. Au mnadhani
mko salama kwamba Huyo ambaye ufalme wake uko
mbinguni hatawapelekea kimbunga chenye kokoto,
mkajua namna gani maonyo Yangu (ni kweli)? 18. Hakika
walikwishakataa (maonyo yangu) wale waliokuwa kabla
yao. Ehe, ilikuwaje ghadhabu yangu?

19. Je, hawawaoni ndege walioko juu yao wakizikunjua
mbawa zao na kuzikunja? Hakuna yeyeto anayewashikilia

huko isipokuwa Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema.
Hakika Yeye ni Mwenye kuona kila kitu. 20. Ni lipi hili
ambalo ni jeshi lenu linaloweza kuwaokoa badala ya
Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema? Makafiri hawako
katika jambo lolote (la maana) isipokuwa kujidanganya tu.
21. Au ni nani huyo ambaye atawapeni riziki kama Yeye
akizuia riziki Yake? Hakuna. Isipokuwa wao wamezama hadi
kina katika kiburi na kuchukia (haki).

22. Je, anayetembea huku akiangalia chini tu ndiye
atakayekwenda sawa sawa barabarani, au ni yule anayetembea
(akitazama) moja-kwa-moja kwenye barabara iliyonyooka?
23. Sema: Yeye Ndiye aliyebuni kuwaumba, na akawapa
masikio na macho, na nyoyo. Ni kidogo tu mnavyoshukuru.
24. Sema: Yeye Ndiye aliyewatawanya katika ardhi, na Kwake
mtakusanywa.

25. Na wanasema: Ni lini basi Ahadi hii? Ikiwa nyinyi ni
wakweli? 26. Sema: Hakika ujuzi wake uko kwa Mwenyezi
Mungu, na hakika mimi ni mwonyaji tu mwenye kubainisha.
27. Hatimaye watakapoiona kwa karibu, nyuso za waliokufuru
zitaingiwa na simanzi, na hapo itasemwa: Hii ndiyo
(ahadi) mliyokuwa mkiiulizia. 28. Sema: Mwaonaje, ikiwa
Mwenyezi Mungu ataniangamiza mimi na walio pamoja
nami, au akituonea huruma, ni nani atakayewalinda makafiri
na adhabu chungu? 29. Sema: Yeye Ndiye Mwenyezi Mungu,
Mwingi wa Rehema; tumemwamini Yeye, na tumeweka
mategemeo yetu juu yake. Ni punde hivi mtajua ni nani
hasa aliye katika upotovu ulio dhahiri. 30. Sema: Mwaonaje,
ikitokea asubuhi moja maji yenu yamedidimia chini! Ni nani
atayeweza kuwaletea maji safi yanayotiririka?

# SURA AL-QALAM

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 *Nun.*

Naapa kwa kalamu na yale waaandikayo! 2 Hukuwa wewe,
kwa neema ya Mola Wako Mlezi, mwendawazimu. 3 Na kwa
hakika wewe una malipo yasiyokatika. 4 Na hakika wewe
uko juu ya tabia tukufu. 5 Punde hivi utaona, na wao wataona.
6 Ni nani kati yenu aliyepandwa wazimu. 7 Hakika Mola
Wako Mlezi Yeye ndiye anayemjua zaidi aliyepotea njia yake
na Yeye Ndiye anayewajua zaidi walioongoka.

8 Basi usiwatii wanaokana ukweli. 9 Wanatamani lau
ungekuwa laini, nao wawe laini kwako. 10 Wala usimtii kila
yeyote mwingi wa kuapa, mtwevu. 11 Mwenye kusingizia
watu, apitae akifitini. 12 Mwenye kuzuia kheri, mchokozi,
mwingi wa kutenda dhambi. 13 Mwenye roho ngumu, juu ya
hayo, ni mwanaharamu. 14 Ati kwa kuwa ana mali na watoto!
15 Anaposomewa Aya Zetu, husema: Hizi ni ngano za watu
wa kale! 16 Tutamtia kovu juu ya pua yake.

17. Hakika Sisi tumewajaribu hao kama tulivyowajaribu
watu wenye shamba. Pale walipoapa kwamba watalivuna
ifikapo asubuhi. 18. Wala wasiseme: Inshaallah!(apendapo
Mwenyezi Mungu) 19. Basi likapitiwa na tukio kutoka
kwa Mola Wako Mlezi, huku wao wamelala! 20. Likawa
kama usiku wa giza. 21. Wakaitana asubuhi. 22. Ya kwamba
raukeni mwende kondeni kwenu ikiwa mnataka kuvuna.

23. Wakaondoka na huku wakinong'onezana.... 24. kwamba
msiruhusu hata maskini mmoja aingie kondeni hii leo!
25. Wakarauka wakidhani wana nguvu za kutimiza azma
yao. 26. Lakini walipoliona, wakasema: ah! Sisi kwa hakika
tumepotea njia! 27. Hasha! Sisi tumenyimwa (matunda
ya kazi yetu) 28. Mmoja wao akasema: Je, Sikuwaambia,
kwa nini hamumtukuzi Mwenyezi Mungu? 29. Wakasema:
Ametakasika Mola Wetu Mlezi! Hakika tulikuwa wakosefu.
30. Basi wakakabiliana huku wakilaumiana wao kwa wao.
31. Wakasema: Ole wetu! Hakika sisi tulikuwa tumekiuka
mipaka! 32. Asaa Mola Wetu akatubadilishia lililo bora kuliko
hili. Hakika sisi ni wenye kurejea kwa Mola Wetu Mlezi.
33. Kama hivyo ndiyo adhabu (hapa duniani), na bila ya shaka
adhabu ya Akhera ni kubwa zaidi, laiti wangejua!

34. Hakika wenye kumchamungu watakuwa na Bustani
za neema kwa Mola wao Mlezi. 35. Hivi tuwachukulie
Waislamu kama (tuwachukuliavyo) wahalifu? 36. Vipi nyie!
Mnahukumu namna gani? 37. Au mnacho kitabu ambacho
ndani yake mnasoma… 38 Kuwa mtapata humo (chochote)
mkichaguacho? 39 Au mna ahadi Nasi za viapo hadi ifikapo
siku ya Kiyama: kuwa mtapata kila mnachotaka? 40 Waulize:
Ni nani miongoni mwao ndiye mdhamini wa hayo? 41Au
wanao washirika? Basi wawalete washirika wao wakiwa
wanasema kweli.

42. Siku utakapofunuliwa muundi, na wakaitwa kusujudu,
wasiweze. 43. Macho yao yatakodolea chini tu, unyonge
utawafunika. Na ilhali walikuwa wakiitwa wasujudu
walipokuwa wazima (wakakataa). 44. Basi niachie Miye na
anayeona maneno haya ni uongo. Tutawavuta kidogo kidogo

kutoka mahali wasipofikiria. 45. Na ninawapa muda; hakika
mipango Yangu ni imara.
46. Au unawaomba malipo, kwa hiyo wanalemewa na
madeni? 47. Au wanayo elimu ya ghaibu, nao wanaandika?
48. Basi ngojea hukumu ya Mola Wako Mlezi, wala usiwe
kama yule wa (kumezwa na) chewa, wakati aliponadi akiwa
amesongwa na dhiki. 49. Kama isingemfikia neema kutoka
kwa Mola Wake Mlezi, bila ya shaka angetupwa ufukweni
naye ni mwenye kulaumiwa. 50. Lakini Mola Wake Mlezi
akamteua (tena) na akamfanya miongoni mwa watu wema.
51. Na kwa hakika waliokufuru hukaribia kukudhuru kwa
macho yao, wanaposikia Qur'an, na wanasema: Hakika yeye
ni mwendawazimu. 52. Ilhali hii si kitu kingine bali ni ujumbe
kwa walimwengu wote.

## 69. Sura Al-Haqqa

## SURA YA UKWELI HALISIA

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 Ukweli halisia (Kiyama)! 2 Nini Ukweli halisia? 3 Na nini
kitachokujulisha Ukweli halisia? 4 Akina Thamudi na A'di
walisema Kiyama ni uongo. 5 Ama Thamudi, waliangamizwa
kwa janga kubwa mno. 6 Na ama A'di, wao waliangamizwa
kwa upepo mkali wenye nguvu za kupita kiasi. 7 Alioufanya
uwakung'ute kwa nyusiku saba na siku nane mfululizo.
Ukawaona watu wamepinduka kana kwamba ni magogo
ya mitende yenye ufa yaliyoyong'olewa. 8 Je, unamwona
yeyote kati yao aliyebaki? 9 Naye Firaun (Pharaoh) na

waliomtangulia na (watu wa) miji iliyopinduliwa juu-chini,
walizoea kufanya madhambi. 10 Wakamwasi Mtume wa Mola
Wao Mlezi, ndipo akawatia nguvuni kwa mshiko wa nguvu
kubwa. 11 Sisi, wakati maji yalipofurika (wakati wa Noah)
tuliwachukua nyie katika Jahazi lililoelea. 12 Ili tulifanye
hilo kuwa ni onyo kwenu na lilizingatie hilo sikio linalotaka
kuzingatia.

13 Pindi itakapopulizwa parapanda mpulizo mmoja. 14 Na
ardhi na milima ikaondolewa, na ikavunjwa-vunjwa mara
moja. 15 Siku hiyo ndiyo Kiyama kimetokea! 16 Na mbingu
zikawa zimepasuka, kwani siku hiyo zitakuwa dhaifu. 17 Na
Malaika watakuwa kandoni mwa mbingu. Na wanane zaidi
ya hao ndiyo siku hiyo wataobeba Taji la Ufalme wa Enzi la
Mola wako Mlezi. 18 Siku hiyo mtaletwa mbele (ya hukumu)
haitafichika siri yenu yoyote.

19. Ama yule atakayepewa kitabu chake kwa mkono wake
wa kuume, atasema: ‘njooni hapa! Someni kitabu changu’!
20. Nilijua kwa yakini kuwa (siku moja) nitapokea rekodi
zangu. 21. Basi yeye atakuwa katika maisha ya kuridhia.
22. Katika Bustani ya juu. 23. Matunda yake (yananing’inia)
karibu. 24. “Kuleni na kunyweni kwa furaha kwa sababu
ya mlivyotanguliza katika siku zilizopita” 25. Na ama
atakayekabidhiwa kitabu chake kwa mkono wake wa
kushoto, atasema: ‘Laiti nisingelipewa kitabu changu!’
26. Wala nisingejua nini hisabu zangu. 27. Ah! Laiti (mauti)
yangekuwa ndiyo mwisho wa yote! 28. Mali yangu haikunifaa
kitu. 29. Madaraka yangu yamenipotea. 30. “Mshikeni na
mumtie pingu”! 31. “Kisha mtupeni Motoni”! 32. “Tena
mfanyeni atembee akiwa katika mnyororo wenye urefu
wa mikono sabini”! 33. “Hakika yeye alikuwa hamwamini

Mwenyezi Mungu Mtukufu”. 34. “Wala hahimizi kuwalisha masikini”. 35. “Basi leo hana hapa rafiki yeyote” 36. “Wala hana chakula ila usaha wa watu wa Motoni”. 37. “Chakula hicho hawakili ila wenye hatia”.

38. Naapa kwa mnavyoviona, 39. Na (kwa) msivyoviona! 40. Hakika hii ni kauli ya Mjumbe mwenye heshima. 41. Wala si kauli ya mshairi. Ni machache mnayoyaamini. 42. Wala si kauli ya kuhani. Ni machache tu mnayoyakumbuka nyie! 43. Ni ufunuo utokao kwa Mola Mlezi wa walimwengu wote. 44. Na lau kama angetuzulia baadhi ya maneno, 45. Hapana shaka tungemkamata kwa mkono wa kulia. 46. Kisha tukamkata mshipa wake mkubwa wa moyo! 47. Na hakuna yeyote katika nyinyi angethubutu kutuzuia naye. 48. Kwa hakika hii Qur’an ni mawaidha kwa wamchao Mwenyezi Mungu. 49. Na Sisi hakika tunajua kwamba miongoni mwenu wapo wanaokataa. 50. Na kwa hakika hii Qur’an itakuwa ni majuto kwa wanaoikana. 51. Na hakika hii bila ya shaka ni ukweli halisia. 52. Basi litukuze, lisifu na ulitakase jina la Mola Wako Mlezi aliye Mkuu.

### 70. Sura Al-Ma’arij

## SURA YA NJIA ZA KUPANDIA MBINGUNI

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 Aliuliza mwulizaji juu ya adhabu itakayowashukia… 2 Wasioamini, hakuna awezaye kuizuia. 3 Kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mwenye Njia za kupandia mbinguni. 4 Watapanda Malaika na Roho kwenda Kwake katika siku

hiyo ambayo kipimo chake ni miaka hamsini elfu (yenu)!
[5] Basi vumilia kuvumilia kwa (angojaye) mema. [6] Hakika
wao wanaiona iko mbali. [7] Na Sisi tunaiona iko karibu.
[8] Siku ambayo mbingu zitakuwa kama shaba iliyoyeyuka.
[9] Na milima ikawa kama sufi. [10] Na rafiki hatamwulizia
rafikiye. [11] (Ingawa) watafanywa waonane. Atatamani
mwovu lau ajikomboe na adhabu ya siku hiyo kwa kuwatoa
fidia wanawe. [12] Na mkewe, na nduguye. [13] Na ukoo wake
uliokuwa ukimpa hifadhi. [14] Na wote waliomo ardhini,
kwamba (hilo) litamwokoa.

[15] La hasha! Hakika huo ni Moto mkali kabisa.
[16] Unaochuna ngozi ya kichwa! [17] Unamwita kila
aliyegeuza mgongo na akageuka (kuacha imani). [18] Na
akakusanya mali, kisha akaificha (asiitumie). [19] Hakika
mtu ameumbwa na papara. [20] Inapomgusa shari hubabaika.
[21] Na inapomgusa kheri huizuia. [22] Isipokuwa wanaoswali,
[23] Ambao wanadumisha Swala zao. [24] Na ambao katika
mali yao iko haki inayojulikana. [25] Kwa mwenye kuomba
na anayejizuia kuomba. [26] Na ambao wanasadiki Siku ya
Malipo. [27] Na ambao wanaogopa adhabu itokayo kwa Mola
Wao Mlezi. [28] Hakika adhabu ya Mola Wao Mlezi si ya
mtu kujiamini kusalimika nayo. [29] Na ambao wanazilinda
tupu zao. [30] Isipokuwa kwa wake zao au kwa iliyowamiliki
mikono yao ya kuume, kwani wao si wenye kulaumiwa.
[31] Lakini anayetaka kinyume cha hayo basi hao ndio
wapetukao mipaka. [32] Na wale ambao wanachunga amana
zao na ahadi zao. [33] Na ambao wanasimama imara katika
ushahidi wao. [34] Na ambao wanazihifadhi Swala zao. [35] Hao
ndio watakuwa Peponi wakiheshimiwa.

[36.] Wana nini wale waliokufuru, mbona wanaelekea upande

wako kwa haraka? 37. Kulia na kushoto, makundi makundi! 38. Hivi kila mmoja wao ana tamaa ya kuingizwa katika Pepo ya neema? 39. La hasha! Hakika Sisi tumewaumba kutokana na wanachokijua.

40. Naapa kwa Mola Mlezi wa mashariki zote na magharibi zote, kwamba Sisi tunaweza.... 41. Kuwabadilisha kwa walio bora kuliko wao; na wala Sisi hatushindwi. 42. Basi waache wapige porojo, wakicheza, mpaka wakutane na hiyo siku yao wanayoahidiwa. 43. Siku watakapotoka makaburini haraka kana kwamba wanakimbilia kitu kilichosimamishwa kwa ajili yao. 44. Macho yao yanaangalia chini tu, wamegubikwa na unyonge. Hiyo ndiyo siku waliyokuwa wakiahidiwa.

## 71. Sura Nuh

# SURA YA NUH/NOAH

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 Hakika Sisi tulimtuma Nuh kwa watu wake, kwamba waonye watu wako kabla ya kuwafikia adhabu chungu. 2 Akawaambia: Enyi watu wangu! Kwa hakika mimi ni mwonyaji wa dhahiri kwenu, 3 Kwamba mwabuduni Mwenyezi Mungu, na mumche, na mnitii mimi. 4 Atawasamehe dhambi zenu, na atawaacha muishi mpaka muda uliowekwa. Hakika muda wa Mwenyezi Mungu utapofika haucheleweshwi. Laiti mngejua. 5 Akasema: Ee Mola Wangu Mlezi! Hakika mimi nimewalingania watu wangu usiku na mchana. 6 Lakini wito wangu haukuwazidisha isipokuwa kuikimbia (haki). 7 Na hakika mimi kila nilipowaita ili upate kuwasamehe, waliziba

masikio yao kwa (ncha za) vidole vyao, na wakajigubika
nguo zao, na wakawa wakaidi na wakazidi jeuri. [8] Tena
niliwalingania kwa uwazi, [9] Kisha nikawatangazia, halafu
nikasema nao kwa siri. [10] Nikawaambia: Mwombeni
msamaha Mola Wenu Mlezi; hakika Yeye daima ni Mwingi
wa kusamehe. [11] Atawaletea mvua nyingi. [12] Na atawapa
mali na wana, na atawapa mabustani na atawafungulia mito
ya maji. [13] Mna nini nyie mkawa hamjali kabisa utukufu wa
Mwenyezi Mungu? [14] Na hali Yeye amewaumba nyie hatua
baada ya hatua? [15] Kwani hamwoni jinsi Mwenyezi Mungu
alivyoziumba mbingu saba, moja baada ya nyingine? [16] Na
akaufanya mwezi ndani yake kuwa mwangaza, na akalifanya
jua kuwa taa? [17] Na Mwenyezi Mungu amewaotesha nyie
katika ardhi kama iotavyo mimea. [18] Kisha atawarudisha
humo na atawatoa tena upya. [19] Na Mwenyezi Mungu
amewaumbia ardhi kama mkeka. [20] Ili mtembee humo katika
njia zilizo pana.

[21.] Nuh akasema: Mola Wangu Mlezi! Hakika hao
wameniasi miye wakamfuata ambaye mali yake na watoto
wake havikumzidishia isipokuwa hasara. [22.] Na wakasuka
hila kubwa: [23.] Wakaambiana: ‘ Kamwe msiiache miungu
yenu, wala msimtupe Wadd, Suwaa, Yaghuth, Ya’uq wala
Nasr (majina ya masanamu) [24.] Na hao waliwapoteza
wengi. Basi usiwazidishie watu hao madhalimu chochote
isipokuwa upotevu tu. [25.] Ndipo kutokana na madhambi
yao waliangamizwa kwa gharika na wakatiwa motoni.
Na hawakupata wengine badala ya Mwenyezi Mungu wa
kuwasaidia.

[26.] Na Nuh akasema: Mola Wangu Mlezi! Usimwache juu
ya ardhi mkazi yeyote miongoni mwa makafiri! [27.] Hakika

ukiwaacha watawapoteza waja Wako, na wao hawatazaa
isipokuwa waovu, makafiri. [28.] Mola Wangu Mlezi! Nisamehe
mimi na wazazi wangu, na kila aliyeingia nyumbani mwangu
akiwa mumini, na waumini wanaume, na waumini wanawake.
Na usiwazidishie waliodhulumu ila maangamizo tu.

72. Sura Al-Jinn

## SURA YA MA-JINNI

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye urehemu.

[1] Sema: Nimefunuliwa kwa Wahyi ya kuwa kundi moja
la majini lilisikiliza, na likasema: Hakika sisi tumeisikia
Qur’an ya ajabu! [2] Inaongoza kwenye uwongofu, kwa
hivyo tumeiamini, wala hatutamshirikisha yeyote na Mola
Wetu Mlezi. [3] Na hakika umetukuka zaidi Ukuu wake
Mola Wetu Mlezi, hakujifanyia mke wala mwana. [4] Na
hakika wapumbavu kati yetu walikuwa wakisema uwongo
wa kupindukia juu ya Mwenyezi Mungu. [5] Lakini sisi
tulionelea kwamba watu na majini wasiseme uwongo juu
ya Mwenyezi Mungu. [6] Na ni kweli kuwa walikuwepo
wanaume miongoni mwa wanadamu waliokuwa wakitaka
hifadhi kwa wanaume miongoni mwa majini; kwa ajili
hiyo wakawazidisha uasi. [7] Na hakika wao walidhani, kama
mlivyodhania nyinyi, kuwa Mwenyezi Mungu hatamfufua
yeyote. [8] Nasi tuliigusa mbingu, tukaikuta imejaa walinzi
wenye nguvu na vimondo. [9] Na hakika tulikuwa tukikaa
humo sehemu za kusikilizia. Lakini sasa anayetaka kusikiliza
atakuta kimondo kinamvizia! [10] Nasi hatufahamu je ni shari

imekusudiwa kwa walio ardhini, au ikiwa Mola wao Mlezi anawatakia uwongofu. 11 Na hakika miongoni mwetu wamo walio wema, na wengine kati yetu ni kinyume na hivyo. Tunafuata njia mbali mbali. 12 Nasi tulijua kuwa hatuwezi kumshinda Mwenyezi Mungu (hapa) duniani, wala hatuwezi kumponyoka kwa kukimbia. 13 Nasi tuliposikia uwongofu tuliuamini. Basi mwenye kumwamini Mola Wake haogopi kupunjwa wala kudhulumiwa. 14 Na hakika wamo katika sisi Waislamu, na wamo katika sisi wachepukao kuacha haki. Ama waliosilimu, hao ndio waliotafuta uwongofu. 15 Na ama waliochepuka kuacha haki, hao ndiyo watakuwa kuni za Jahannamu.

16 Na laiti kama wangelinyooka juu ya njia ya haki, tungewapa maji mengi ya kunywa. 17 Ili tuwajaribu kwa hayo, na anayepuuza kumtaja Mola Wake Mlezi, atampitisha kwenye adhabu inayozidi kupanda. 18 Na hakika misikiti yote ni ya Mwenyezi Mungu, basi msimuombe yoyote pamoja na Mwenyezi Mungu. 19 Na hakika aliposimama mtumishi wa Mwenyezi Mungu akimwomba, wao walikuwa karibu kumzonga! 20 Sema: Hakika mimi namwomba Mola Wangu Mlezi pekee, wala simshirikishi Yeye na yoyote. 21 Sema: Mimi sina mamlaka ya kuwadhuru nyie wala kuwaongoza. 22 Sema: Hakika hakuna yeyote awezaye kuniokoa na (adhabu ya) Mwenyezi Mungu, wala sitapata pa kukimbilia isipokuwa Kwake Yeye tu. 23 Isipokuwa nifikishe Ujumbe utokao kwa Mwenyezi Mungu na risala Zake. Na yeyote anayemwasi Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, hakika kwake yeye ni Moto wa Jahannamu, wakae humo milele.

24. Hadi hapo watapoyaona yale wanayoahidiwa, watajua ni nani mwenye msaidizi dhaifu na mchache wa idadi.

25. Sema sijui kama (adhabu) mnayoahidiwa ipo karibu au
Mola Wangu Mlezi ataiwekea muda mrefu. 26. Yeye ni Mjuzi
wa siri wala hamfunulii yeyote siri Yake, 27. Ila aliyemridhia
katika Mitume wake. Huyo humwekea walinzi mbele yake na
nyuma yake. 28. Ili ahakiki kwamba wao wamefikisha ujumbe
wa Mola Wao Mlezi, Na anajua vyema yote waliyonayo na
amedhibiti idadi ya kila kitu.

73. Sura Al-Muzzamil

## SURA YA MWENYE KUJIZONGAZONGA NGUO

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 Ewe uliyejizongazonga nguo! 2 Simama usiku kucha
(kuswali), ila sehemu ndogo tu. 3 Nusu yake, au ipunguze
kidogo, 4 Au izidishe, na soma Qur’an kwa utuvu na taratibu.
5 Hakika tutakuteremshia ujumbe mzito.

6 Hakika kuamka usiku kuna athari kubwa ya (kuimarisha)
roho, na maneno wakati huo huwa manyoofu zaidi. 7 Hakika
wewe una shughuli nyingi mchana. 8 Basi daima litaje jina
la Mola Wako Mlezi, na jitolee Kwake kwa moyo mkunjufu.
9 Mola wa mashariki na magharibi, hapana mungu (wa kweli)
isipokuwa Yeye, basi mfanye kuwa Msimamizi wa mambo
yako. 10 Na vumilia hayo wayasemayo, na achana nao kwa
njia nzuri. 11 Na niachie Mimi na hao wanaosema huu ni
uwongo, walio na neema , na wape muda kidogo tu! 12 Hakika
Sisi tuna pingu (za kuwafunga) na Moto (wa kuwachoma).
13 Na chakula kinachokwama kooni, na adhabu inayoumiza.

14 Siku ambayo ardhi na milima vitatikisika kwa nguvu, na
milima itakuwa kama tifutifu la mchanga unaopeperushwa.
15. Hakika Sisi tumemtuma kwenu Mtume akiwa shahidi
juu yenu, kama tulivyomtuma Mtume (Musa) kwa Firauni
(Pharaoh). 16. Lakini Firauni alimwasi yule Mtume. Hapo
tukamtia nguvuni kwa mateso mazito. 17. Basi mkimkana
Mwenyezi Mungu mtawezaje kujikinga na Siku ambayo
itawafanya watoto wawe waote ndevu? 18. Mbingu zitapasuka
kwa sababu ya siku hiyo! Ahadi Yake hapana daima budi
itekelezwe. 19. Kwa hakika hili ni onyo. Basi atakaye atashika
njia (sawa sawa) ya kufika kwa Mola Wake Mlezi.
20. Hakika Mola Wako anajua kuwa unasimama kuswali
takriban theluthi mbili za usiku, au nusu yake, au theluthi
yake, wewe na baadhi ya watu walio pamoja nawe. Na
Mwenyezi Mungu anauweka usiku na mchana kwa kipimo
maalum. Anajua kuwa hamwezi kudhibiti kiwango cha
(muda wa kuswali) hivyo amewasamehe. Basi someni
kinachowawia wepesi katika Qur'an. Anajua ya kuwa baadhi
yenu watakuwa wagonjwa, na wengine wanasafiri katika
ardhi wakitafuta fadhila za Mwenyezi Mungu, na wengine
wanapigana vita katika Njia ya Mwenyezi Mungu. Kwa hiyo
someni kinachowawia wepesi katika Qur'an, na dumisheni
kushwali na toeni Zaka. Na mkopesheni Mwenyezi Mungu
mkopo mwema. Na matendo yoyote mema mnayoyatanguliza
kwa ajili ya roho zenu, mtayakuta kwa Mwenyezi Mungu
yamekuwa mema zaidi, na yana malipo makubwa sana. Na
mtakeni maghufira Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi
Mungu ni Mwingi wa maghufira, Mwingi wa huruma.

## 74. Sura Al-Muddathir

# SURA YA MWENYE KUJIGUBIKA SHUKA

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 Ewe mwenye kujigubika nguo! 2 Simama wima uwaonye
watu! 3 Na Mola Wako Mlezi umtukuze! 4 Na nguo zako
zitakase. 5 Na mabaya (yote) achana nayo! 6 Wala usitoe kwa
kutarajia kupata kingi. 7 Na kwa ahadi ya Mola Wako Mlezi,
fanya subira!

8 Hapo litapopulizwa barugumu. 9 Siku hiyo basi
itakuwa siku ngumu kabisa! 10 Kwa makafiri haitakuwa
nyepesi. 11 Niache Mimi mwenyewe (nimshughulikie) yule
niliyemuumba. 12 Nikam utajiri mkubwa..... 13 Na watoto
pembeni mwake.. 14 Na nikamtengenezea maisha yake vizuri
15 Hata ana tamaa nimzidishie! 16 La hasha! Hakika yeye
alikuwa akizifanyia inadi Aya Zetu! 17 Nitamchosha kwa
adhabu inayoondelea kuzidi.

18. Hakika yeye alifikiria na akapanga... 19. Alaaniwe!
Vipi amepanga! 20. Tena alaaniwe! Vipi amepanga! 21. Kisha
akaangalia (kando yake). 22. Kisha akakunja uso na akanuna.
23. Kisha akaipa kisogo, na akapanda kiburi. 24. Akasema:
“Hii si chochote bali ni uchawi wa kufunzwa. 25. Haya si
chochote ila ni maneno ya binadamu.

26. Nitamtia kwenye (moto) Saqar. 27. Na nini kitakujulisha
Saqar ni nini? 28. Haubakishi wala hauachi kitu!
29. Unaochuna ngozi yote hadi kwenye fuvu la kichwa. 30. Juu
yake wapo kumi na tisa. 31. Na hatukuwafanya walinzi wa
Moto isipokuwa Malaika pekee. Na hatukuifanya idadi yao

hiyo ila iwe majaribu kwa wale waliokufuru. Ili waliopewa
Kitabu wawe na yakini, na wazidi imani wale walioamini. Na
ili wasiwe na shaka yoyote (tena) wale waliopewa Kitabu na
pia waumini. Na ili wapate kusema wale walio na maradhi
katika nyoyo zao na makafiri: Mwenyezi Mungu amekusudia
nini kwa mfano huu? Ndio hivyo, Mwenyezi Mungu
humwacha apotee amtakaye na humwongoza amtakaye. Na
hapana ajuae majeshi ya Mola Wako Mlezi isipokuwa Yeye
pekee. Na haya si kingine bali ni ukumbusho kwa watu.

32. La hasha! Naapa kwa mwezi! 33. Na kwa usiku
unapokucha! 34. Na kwa asubuhi inapopambazuka! 35. Hakika
huo (Moto wa Saqar) ni mojawapo ya (mambo) makubwa!
36. Ni onyo kwa watu. 37. Kwa anayetaka miongoni mwenu
kwenda mbele au kurudi nyuma. 38. Kila nafsi ni (itazuiliwa
kama) rehani kwa iliyoyafanya. 39. Isipokuwa watu wa kuliani.
40. Watakuwa katika mabustani, wakiulizana. 41. Juu ya watu
waovu. 42. Ni kipi kilichowapeleka Motoni? 43. Watasema:
Hatukuwa miongoni mwa waliokuwa wakiswali. 44. Wala
hatukuwa tukiwalisha masikini. 45. Na tulikuwa tukibobea
(katika maovu) pamoja na waliokuwa wakibobea. 46. Na
tulikuwa tukisema siku ya hukumu ni uwongo. 47. Mpaka
ikatujia yakini. 48. Hapo hautawafaa uombezi wa waombezi.

49. Basi wana nini hawa kupuuza maonyo haya? 50. Kana
kwamba wao ni punda milia waliotimuliwa. 51. Waliomkimbia
simba! 52. Ati kila mmoja katika wao anataka apewe nyaraka
zake binafsi (za ujumbe) zilizofunuliwa! 53. La hasha! Bali
hawaiogopi Akhera. 54. La hasha! Kwa hakika hii ni ilani. 55.
Basi atakaye ataikumbuka. 56. Na hawatakumbuka isipokuwa
atake Mwenyezi Mungu. Yeye ndiye mstahiki wa kutiiwa na
kuogopwa, na Yeye ndiye mstahiki wa kusamehe.

75. Sura Al-Qiyama

# SURA YA KIYAMA

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 Naapa kwa Siku ya Kiyama! 2 Na naapa kwa nafsi
inayojilaumu! 3 Hivi mwanadamu anadhani kuwa Sisi
hatuwezi kuikusanya mifupa yake? 4 Ndiyo! Sisi tunaweza
kuzirudisha sawa sawa hata tindi za vidole vyake! 5 Lakini
mtu anataka tu kuongopea yaliyo mbele yake. 6 Anauliza:
Lini itakuwa hiyo Siku ya Kiyama? 7 Ni hapo jicho
litakapoduwaa. 8 Na mwezi utapopatwa. 9 Na likakusanywa
jua na mwezi. 10 Siku hiyo mtu atauliza: wapi pa kukimbilia?
11 La! Hapana pa kukimbilia! 12 Ni kwa Mola wako Mlezi
pekee siku hiyo ndiyo pa kutua. 13 Siku hiyo mwanadamu
ataelezwa aliyoyatanguliza na asiyoyafanya. 14 Bali
mwanadamu atakuwa ni hoja juu ya nafsi yake. 15 Ingawa
atatoa visingizio vingi.

16. Usiufuatishie ulimi wako (kwa wahyi) ili ufanye
haraka kusoma Qur'an 17. Hakika ni juu Yetu kuikusanya na
kuisomesha. 18. Hivyo tunapoisoma (kwako), wewe fuatiliza
kisomo chake. 19. Kisha ni juu Yetu kuifafanua.

20. La hasha! Bali nyinyi mnapenda (dunia) ipitayo.
21. Na mnaacha Akhera. 22. Nyuso siku hiyo zitang'ara.
23. Kwa Mola wake Mlezi zitakuwa zenye kutazama. 24. Na
nyuso nyingine siku hiyo zitakunjamana. 25. Kwa kujua kuwa
zitafikwa na janga la kuvunja uti wa mgongo.26. Hapana!
Hapo (roho) itakapofikia mifupa ya mtulinga (ikiwa inatoka)!
27. Na pakaulizwa: 'Nani wa kumganga?' 28. Na akajua kuwa

huko ndiyo kufariki dunia. 29. Na ukajiambatanisha muundi na muundi mwigine. 30. Siku hiyo ndiyo kupelekwa kwa Mola Wako Mlezi.

31. Lakini hakusadiki, wala hakuswali. 32. Bali alikanusha, na akageuka. 33. Kisha akaenda kwa familia yake hali anaringa. 34. Ole wako, tena ole wako! 35. Kisha Ole wako, tena ole wako! 36. Hivi mwanadamu anafikiri ataachwa bure? 37. Je, hakuwa yeye ni tone la manii lililoshushwa? 38. Kisha akawa pande la damu linaloning'inia, akamuumba na akamlinganisha sawa? 39. Akamfanya jinsi mbili, mwanamume na mwanamke? 40. Je! Huyo si mwenye uwezo wa kuwafufua waliokufa?

## 76. Sura Al-Insan

## SURA YA MWANADAMU

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 Hakika kilipita kwa mwanadamu kipindi kirefu cha wakati ambapo hakuwa kitu kinachotajwa. 2 Hakika tumemuumba mwanadamu kutokana na tone la manii yaliyochanganyika. Ili tumtie katika majaribio. Ndipo tukamfanya mwenye kusikia, mwenye kuona. 3 Hakika Sisi tumemwonesha njia; ima awe ni mwenye shukrani, ima awe mtovu wa shukrani.

4 Hakika Sisi tumewaandalia makafiri minyororo ya chuma, na pingu na Moto mkali. 5 Hakika watu wema watakunywa kutoka glasi ya kinywaji kilichochanganywa na kafur. 6 (Kafur) ni chemchemi watakayokunywia hapo waja wa Mwenyezi Mungu, wataifanya ibubujike kwa kadri wapendavyo. 7 Hao ni wale ambao hutimiza nadhiri

zao, na wakaogopa siku ambayo shari yake itaenea kila
mahali. [8] Na huwalisha chakula, pamoja na kuwa wao
wenyewe wanakihitajia, maskini, na yatima, na mateka.
[9] (Wakiwaambia): 'Sisi tunawalisha nyie kwa kutaka radhi
ya Mwenyezi Mungu. Hatutaki kutoka kwenu malipo wala
hata shukrani'. [10] 'Hakika sisi tunaogopa siku nzito ya
shida na dhiki ijayo kutoka kwa Mola wetu Mlezi. [11] Ndipo
Mwenyezi Mungu atawaepusha na shari ya siku hiyo, na
atawapa raha na furaha. [12] Na atawalipa Bustani na (nguo
za) hariri kwa vile walivyosubiri. [13] Humo watabembea
juu ya viti vya enzi, hawahisi humo jua kali wala baridi
kali. [14] Na vivuli vya Bustani hiyo vitakuwa karibu nao, na
mashada ya matunda yake yataning'inia chini chini, rahisi
kuchuma. [15] Na watapitishiwa vyombo vya fedha na bilauri
za vioo. [16] Vioo vitokanavyo na fedha, wamezipima kwa
kadri ya ujazo waupendao. [17] Na humo watanyweshwa
glasi (ya mvinyo) ilichochanganywa na tangawizi. [18] Hiyo
ni chemchemi iliyo humo iitwayo Salsabil. [19] Na pembeni
mwao kuwazunguka watakuwepo wavulana wasiochakaa
(wakiwatumikia), ukiwaona utawadhania ni lulu
zilizotawanywa. [20] Endapo utakuona huko, utaona neema
na ufalme mkubwa. [21] Watavaa nguo za hariri laini za kijani
kibichi, na hariri nzito. Na watavikwa vikuku vya fedha, na
Mola Wao Mlezi atawanywesha kinywaji safi (cha mvinyo).
[22] (Waambiwa): hakika haya ndiyo malipo yenu; na jitihada
zenu zimekubaliwa.

[23.] Hakika Sisi tumekuteremshia hii Qur'an hatua kwa
hatua. [24.] Basi subiri hukumu ya Mola Wako Mlezi, wala
usimtii miongoni mwao mwenye dhambi au mtovu wa
shukrani. [25.] Na litaje jina la Mola Wako Mlezi asubuhi na

jioni. 26 Na usiku msujudie Yeye, na umsabihi usiku mrefu.
27 Hakika watu hawa wanapenda dunia ipitayo, na wanaiacha
nyuma yao siku nzito. 28 Sisi tumewaumba hao, na tukavitia
nguvu viungo vyao. Na tukitaka tunaweza kuwabadilisha kwa
mfano wao wawe badala yao. 29 Hakika haya ni mawaidha;
basi anayetaka atashika Njia ya kwenda kwa Mola Wake
Mlezi. 30 Wala hamtataka hadi apende Mwenyezi Mungu.
Hakika Mwenyezi Mungu daima ni Mwenye elimu, Mwingi
wa hekima. 31 Humwingiza amtakaye ndani ya (Pepo kwa)
huruma Yake. Lakini wafanya mabaya hao amewaandalia
adhabu iliyo chungu.

## 77. Sura Al-Mursalat

# SURA YA PEPO ZITUMWAZO

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 Naapa kwa pepo zitumwazo kwa upole! 2 Na zivumazo
kwa kasi! 3 Na kwa zitawanyazo (mbegu) mbali! 4 Kisha
zikazitenganisha moja na nyingine! 5 Na zinazopeleka ujumbe!
6 Kwa kutoa udhuru au kuonya! 7 Hakika mnayoahidiwa bila
ya shaka yatatokea!

8 Pindi nyota zitakapofutwa (nuru yake). 9 Na mbingu
zitakapopasuliwa. 10 Na pindi milima itakapopeperushwa.
11 Na pindi Mitume watakapowekewa muda wao.
12 Hadi siku gani muda huo uliakhirishwa? 13 Hadi siku
ya upambanuzi! 14 Na nini kitakachokujulisha ni ipi siku
ya upambanuzi? 15 Ole wao siku hiyo wale wanaokataa
ukweli! 16 Je, hatukuwaangamiza waliotangulia? 17 Kisha

tutawafuatilizia na waliokuja nyuma? [18] Ndio kama hivyo tutawafanya wahalifu! [19] Ole wao siku hiyo wanaokataa ukweli!

[20.] Je, hatukuwaumba nyie kutokana na maji duni? [21.] Kisha tukayaweka mahali makini pa utulivu? [22.] Mpaka muda maalumu? [23.] Hilo tumeliweza. Basi Sisi ndiyo bora ya wanaoweza. [24.] Ole wao siku hiyo wanaokataa ukweli! [25.] Je, hatukuifanya ardhi kuwatosha nyie wote? [26.] Walio hai na waliokufa? [27.] Na tukaweka humo milima mirefu yenye kusimama wima, na tukawanywesha maji matamu? [28.] Ole wao siku hiyo wanaokataa ukweli!

[29.] (Wataambiwa) Nendeni kwenye kile mlichokuwa mkikikana. [30.] Nendeni kwenye jivuli lenye ncha tatu! [31.] Halitoi kivuli, wala hakifai kwa kukinga miai ya moto. [32.] Hakika huo moto unarusha cheche (kubwa) kama jumba la ghorofa! [33.] Kana kwamba cheche hizo ni dakawa za rangi ya manjano (Kamba nene inayofungiwa meli). [34.] Ole wao siku hiyo wanaokataa ukweli! [35.] Hii ni siku ambayo hawatatamka kitu. [36.] Wala hawataruhusiwa kuelezea udhuru wao. [37.] Ole wao siku hiyo wanaokataa ukweli! [38.] Hii ndiyo siku ya uamuzi. Tumewakusanya nyinyi na waliotangulia. [39.] Ikiwa mnayo hila, basi nifanyieni! [40.] Ole wao siku hiyo wanaokana ukweli!

[41.] Hakika wenye kumcha Mungu watakuwa katika vivuli na chemchemi. [42.] Na matunda yoyote wanayoyatamani. [43.] Kuleni na kunyweni kwa furaha kwa sababu ya mliyokuwa mkiyatenda. [44.] Sisi namna hii ndivyo tunavyowalipa watendao mema. [45.] Ole wao siku hiyo wanaokana ukweli! [46.] Kuleni na mjifurahishe kidogo tu (hapa duniani). Hakika nyinyi ni wahalifu. [47.] Ole wao siku hiyo wanaokana ukweli!

48. Na wakiambiwa: sujuduni (mswali) hawasujudu. 49. Ole
wao siku hiyo wanaokataa ukweli! 50. Basi ni ujumbe gani
zaidi ya huu watakaouamini?

## 78. Sura An-Nabai

# SURA YA HABARI KUU

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 Juu ya nini wanabishana (hao Maquresh)? 2 Ni kuhusu
habari kubwa? 3 Ambayo hawakubaliani juu yake? 4 La
hasha! Punde tu watajua. 5 Tena la hasha! Punde tu watajua.
6 Kwani hatukuifanya ardhi kuwa tandiko? 7 Na milima
kuwa vigingi? 8 Na tukawaumba nyie wawili wawili?
9 Na tukaufanya usingizi wenu kuwa mapumziko? 10 Na
tukaufanya usiku kuwa (kama) vazi? 11 Na tukaufanya
mchana kuwa wakati wa maisha? 12 Na tukajenga juu
yenu mbingu saba zenye nguvu? 13 Na tukaweka taa yenye
mwangaza mkali na joto? 14 Na tukateremsha kutoka katika
mawingu maji yenye kububujika? 15 Ili tuoteshe kwayo
nafaka na mimea? 16 Na mabustani yaliyomea miti kwa
wingi? 17 Hakika Siku ya uamuzi daima imewekewa muda
wake.

18. Siku itakapopulizwa parapanda nanyi mkaja makundi
makundi. 19. Na zikafunguliwa mbingu zikawa (kama)
milango. 20. Na milima ikaondolewa ikawa (kama) mangati.
21. Hakika Jahannam inawangoja kwa kuwavizia. 22. Kwa
walioasi ndio marejeo. 23. Watakaa humo karne baada ya karne.
24. Hawataonja humo baridi wala kinywaji. 25. Isipokuwa

maji ya moto na usaha. [26.] Ni malipo muwafaka. [27.] Hakika
wao walikuwa hawatarajii kuwajibishwa. [28.] Na wakazikana
Ishara Zetu kwa ujeuri. [29.] Na kila kitu tumekidhibiti kwa
kukiandika [30.] Basi onjeni! Hatutawazidishia isipokuwa
adhabu tu.

[31.] Hakika wachamungu watapata ya kuwaridhisha
[32.] Mabustani na vitalu vya mizabibu. [33.] Na wenza walio rika
moja na wao. [34.] Na bilauri zilizojaa tele. [35.] Hawatasikia humo
upuuzi wala uwongo. [36.] Malipo kutoka kwa Mola Wako
Mlezi, kipawa cha kutosha. [37.] Mola wa mbingu na ardhi na
vilivyomo kati yake, Mwingi wa rehema; hawatamiliki usemi
wowote mbele Yake. [38.] Siku atakaposimama Roho na malaika
kwa safu. Hatasema yeyote isipokuwa yule atayepewa ruhusa
na Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema, na aseme yaliyo
sawa. [39.] Hiyo ndiyo siku ya haki na uhalisia. Basi anayetaka
na ashike njia kurejea kwa Mola Wake Mlezi. [40.] Hakika
tunawaonya na adhabu iliyo karibu. Siku mtu atakapoona
(matendo) ambayo mikono yake imekwishayatanguliza, na
kafiri aseme: ‘Laiti ningekuwa mchanga’.

79. Sura An-Nazia’tt

# SURA YA ‘MALAIKA’ WATOAO ROHO KWA NGUVU

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

[1] Naapa kwa (Malaika) watoao roho za watu waovu kwa
nguvu. [2] Na kwa watoao roho za watu wema kwa upole. [3] Na

wakaelea nazo (mbinguni). 4 Na wakaenda nazo kwa kasi.
5 Na wanaopanga kwa makini kutekeleza (amri za Mola
wao). 6 (Kwamba) Siku kila kitu kitakapotetemeka kwa
nguvu, 7 Likafuatia tetemeko hilo tetemeko jingine, 8 Siku
hiyo nyoyo zitadunda. 9 Macho ya mwenyewe yataangalia
chini tu. 10 Wanasema: Hivi kweli tutarudishwa kwenye
hali ya kwanza? 11 Hata tutakapokuwa mifupa iliyochakaa?
12 Wanasema: Hayo yatakuwa marejeo ya madhara! 13 Kwa
hakika hayo yote ni kwa ukelele mmoja tu. 14 Mara.... tayari
wako juu ya ardhi.

15 Je, kimekufikia kisa cha Musa (Moses)? 16 Wakati
Mola Wake Mlezi alipomwita katika bonde takatifu la
Tuwaa. (Akamwambia): 17 ‘Nenda kwa Firauni. Kwani
yeye amepindukia katika jeuri’. 18 ‘Mwambie, unaonaje
ikiwa utajitakasa (na dhambi)?’ 19 ‘Na nikuongoze kwa
Mola Wako Mlezi upate kumcha?’ 20 Basi akamwonesha
miujiza mikubwa. 21 Lakini alisema ni uongo na akaasi.
22 Kisha akageuza mgongo wake na akafanya jitihada
(kumwasi Mungu). 23 Akakusanya watu wake na akatangaza:
24 Akasema: ‘Mimi ndiye mola wenu mkuu kabisa’. 25 Basi
Mwenyezi Mungu akamtia nguvuni kumwadhibu (kuwa
mfano) Akhera na hapa duniani. 26 Hakika katika hayo kuna
mazingatio kwa wenye kumcha Mungu.

27. Je, ni vigumu zaidi kuwaumba nyinyi au mbingu
aliyoijenga? 28. Akainua kimo chake na akaitengeneza kwa
uwiano sawa. 29. Akautia giza usiku wake na akauchomoza
mwangaza wake. 30. Na baada ya hapo akaitandika ardhi.
31. Akatoa humo maji yake na malisho yake. 32. Na milima
akaikita imara. 33. Kwa manufaa yenu na mifugo yenu.

34. Pindi litakapofika hilo balaa kuu. 35. Siku hiyo

mwanadamu atakumbuka aliyokuwa akihangaika kuyafanya.
36. Na Jahannam itafunuliwa wazi kwa wote waone.
37. Waama yule mwenye kupituka mipaka. 38. Na akapendelea
maisha ya dunia. 39. Basi Jahannam itakuwa ndio makazi
yake. 40. Na ama mwenye kuogopa kusimama mbele ya Mola
Wake Mlezi, na akaizuia nafsi yake na matamanio, 41. Basi
Pepo ndio itakuwa makazi yake! 42. Wanakuuliza kuhusu
Kiyama, kitakuwa lini? 43. Inakuhusu nini wewe hata ukitaje?
44. Ni kwa Mola Wako Mlezi tu mwisho wake. 45. Wewe ni
mwonyaji tu kwa anayekiogopa. 46. Siku watakapokiona,
itakuwa kana kwamba hawakukaa (makaburni) ila jioni moja
au asubuhi ya siku hiyo tu.

80. Sura A'basa

# SURA YA ALIYEKUNJA USO

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 Alikunja uso na akageuka. 2 Kwa sababu alimjia kipofu!
3 Na nini kitakujulisha wewe kwamba yeye huenda
akataka kujitakasa (na dhambi)? 4 Au akasikiza maonyo
yakamfaa maonyo hayo? 5 Ama ajionaye hana haja, 6 Ndio
wewe unamshughulikia? 7 Na si juu yako asipojitakasa.
8 Ama mwenye kukujia mbio mbio. 9 Naye anamwogopa
Mwenyezi Mungu, 10 Ndio wewe unampuuza? 11 La hasha!
Hakika huu ni ujumbe. 12 Atakaye auzingatie. 13 Upo
katika vitabu vinavyoheshimiwa. 14 Vyenye kutukuzwa,
vyenye kutakaswa (na batili). 15 Mikononi mwa Malaika
waandishi. 16 Watukufu, watenda wema. 17 Ameangamia

mwanadamu! Nini kinachomfanya amkane Mungu? 18 Kwa
kitu gani (Mungu) amemuumba? 19 Amemuumba kwa tone
la manii kisha akamsawazisha. 20 Kisha akamfanyia wepesi
njia ya kutokea. 21 Kisha atamfanya afe amweke kaburini.
22 Kisha apendapo atamfufua. 23 La hasha! Bado mwanadamu
hajatekeleza aliloamrishwa. 24 Hebu na atazame mwanadamu
chakula chake: 25 Sisi huyamimina maji kwa wingi. 26 Kisha
tukaipasua ardhi mapande mapande. 27 Humo tukaotesha
nafaka. 28 Na mizabibu na mboga. 29 Na mizaituni na mitende.
30 Na mabustani yenye miti mingi. 31 Na matunda na malisho
ya wanyama. 32 Kwa ajili ya manufaa yenu na ya wanyama
wenu. 33 Hapo utakapokuja ukelele utakaoziba masikio. 34
Siku ambayo mtu atamkimbia nduguye. 35 Na mama yake
na baba yake. 36 Na mkewe na wanawe. 37 Kila mtu katika
wao siku hiyo atakuwa na lake la kumtosha. 38 Siku hiyo
kuna nyuso zitakazonawiri. 39 Zitacheka, zitafurahika.
40 Na nyuso nyingine siku hiyo zitakuwa na mavumbi.
41 Zimefunikwa na giza. 42 Hao ndio makafiri, waovu.

## 81. Sura At-Takwir

## SURA YA KUKUNJWA JUA

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 Pindi jua litakapokunjwa kunjwa, 2 Na pindi nyota
zitakapoanguka, na kukosa mwanga wake. 3 Na pindi
milima itakapoondolewa, 4 Na pindi ngamia wanawake
watakapoachwa (bil kujaliwa). 5 Na pindi wanyama pori
watakapokusanywa, 6 Na pindi bahari zitakapoashwa moto

(zikafurika), 7 Na pindi roho zitakapounganishwa (na miili),
8 Na pindi mtoto wa kike aliyezikwa hai atakapoulizwa,
9 Ni kwa dhambi gani aliuawa? 10Na pindi madaftari
yatakapofunuliwa wazi, 11 Na pindi mbingu itakapoenzuliwa,
12 Na pindi moto utakapochochewa, 13 Na pindi Pepo
itakaposogezwa, 14 Hapo kila nafsi itajua ilichokifanya.
15 Naapa kwa sayari zinazotoweka kidogo kidogo,
16 (Na zile) Zinazokwenda na kujificha, 17 Na kwa usiku
unapoondoka, 18 Na asubuhi inapopumua (kutoa kiza),
19 Hakika hii (Qur'an) ni kauli ya mjumbe mtukufu,
20 Mwenye nguvu na cheo mbele ya Mwenye Ufalme wa
Enzi. 21 Mwenye kutiiwa huko, mwaminifu. 22 Na (huyo)
mwenzenu si mwendawazimu. 23 Na kwa hakika yeye
alimwona (Jibril) kwenye upeo wa mbingu ulio wazi.
24 Wala yeye hafichi chochote juu ya mambo ya ghaibu.
25 Na hii (Quran) si neno la shetani aliyekufukuzwa.
26 Basi mnakwenda wapi? 27 Haikuwa hii ila ni ujumbe
kwa walimwengu wote. 28 Kwa anayetaka katika nyinyi
kushika njia iliyonyooka. 29 Na hamtataka isipokuwa apende
Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa viumbe wote.

## 82. Sura Al-Infitar

# SURA YA MBINGU KUPASUKA

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 Pindi Mbingu itakapopasuka, 2 Na pindi nyota
zitakapopukutika, 3 Na pindi bahari zitakapopasuliwa,
4 Na Makaburi yatakapofukuliwa, 5 Hapo kila nafsi itajua

ilichokifanya na isichokifanya. [6] Ewe mwanadamu! Nini
kilichokudanganya ukamwasi Mola Wako mkarimu? [7] Ambaye
amekuumba, akakusawazisha vizuri, akakulinganisha?
[8] Katika sura yoyote aliyopenda akakutengeneza. [9] La hasha!
Bali mnaikanusha siku ya malipo. [10] Na hakika juu yenu
kuna Malaika wanaowalinda. [11] Watukufu waandishi wenye
heshima, [12] Wanaojua mnayoyafanya. [13] Hakika walio wema
watakuwa katika neema, [14] Na hakika waovu watakuwa
katika moto. [15] Watauingia siku ya malipo. [16] Na hawataacha
kuwa humo. [17] Na nini kitakujulisha ni ipi siku ya malipo? [18]
Kisha ni nini kitakukujulisha ni ipi siku ya malipo? [19] Ni siku
ambayo nafsi haitakuwa na mamlaka juu ya nafsi nyingine;
na amri siku hiyo ni ya Mwenyezi Mungu tu.

## 83. Sura Al-Mutaffifin

# SURA YA WAPUNJAJI VIPIMO

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

[1] Ole wao wanaopunja katika vipimo! [2] Ambao
wanapojipimia kwa watu hutimiza kipimo, [3] Lakini
wanapowapimia watu kwa kipimo au mizani wao hupunguza.
[4] Hivi hawajui kwamba watafufuliwa? [5] Katika siku kuu,
[6] Siku watakaposimama watu mbele ya Mola Mlezi wa
walimwengu wote? [7] La hasha! Hakika maandishi ya waovu
yamo katika Sijiin. [8] Nini kitakujulisha wewe nini Sijiin? [9] Ni
daftari lililokwisha andikwa na kuwekwa namba. [10] Ole wao
siku hiyo wenye kukanusha! [11] Ambao wanaikana siku ya
malipo. [12] Na haikanushi siku hiyo isipokuwa kila mwenye

kupituka mipaka mwenye dhambi. 13 Anaposomewa Aya
Zetu husema: Ni ngano za watu wa kale! 14 La hasha! Lakini
yametia kutu juu ya nyoyo zao waliyokuwa wakiyachuma.
15 La hasha! Hakika wao siku hiyo watawekewa pazia.
16 Kisha hakika Wao watauingia moto. 17 Kisha waambiwe
haya ndiyo mliyokuwa mkiyakanusha.

18 La hasha! Hakika maandishi ya watu wema yako
katika Iliyuun. 19 Ni kipi kitakujulisha wewe ni nini
Iliyuun? 20 Ni daftari lililokwisha andikwa na kuwekwa
namba. 21 Watalishuhudia waliokaribu zaidi kwa Mwenyezi
Mungu. 22 Hakika watu wema watakuwa katika neema.
23 Watakuwa juu ya malili wakitazama. 24 Utatambua katika
nyuso zao mnyiririko wa neema. 25 Watanyweshwa mvinyo
wenye kuzibwa. 26 Kizibo chake ni miski. Na kwa hilo, na
washindane wenye kushindana. 27 Na itachanganywa na kitu
kutoka Tasnim. 28 Hiyo ni chemichemi watakayoinywa walio
karibu zaidi kwa Mwenyezi Mungu. 29 Hakika waliokuwa
wakifanya maovu walikuwa wakiwacheka walioamini. 30 Na
walipokuwa wakiwapitia walikonyezana. 31 Na waliporudi
kwa watu wao walirudi wakishangilia. 32 Na wakiwaona
husema: Hakika hawa wamepotea. 33 Lakini kamwe hao
hawakupelekwa kwao kuwachunga 34 Basi leo walioamini
ndio watakaowacheka makafiri. 35 Watakuwa juu ya malili
wakitazama. 36 Je, makafiri wamelipwa waliyokuwa
wakiyafanya?

84. Sura Al-Inshiqaq

# SURA YA KUCHANIKA MBINGU

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 Pindi mbingu itakapochanika chanika, 2 Na ikatii (amri ya)
Mola Wake Mlezi. Na inabidi ifanye hivyo. 3 Na pindi ardhi
itakaponyooshwa, 4 Na ikavimwaga vilivyo ndani yake na
kuwa tupu, 5 Na ikatii (amri ya) Mola Wake Mlezi. Na inabidi
ifanye hivyo. 6 Ewe mwanadamu! Hakika wewe ni mwenye
kufanya bidii kumwendea Mola Wako Mlezi, bidii kubwa
sana. Basi utakutana Naye. 7 Ama atakayepewa daftari lake
kwa mkono wake wa kulia, 8 Huyo atahesabiwa hesabu
nyepesi, mara moja, 9 Na atarudi kwa watu wake akifurahia.
10 Na ama atakayepewa daftari lake kwa nyuma ya mgongo
wake, 11 Hapo hapo atalia, Oh, ole wangu na maangamizo!
12 Na atauingia moto. 13 Hakika yeye alikuwa baina ya jamaa
zake mwenye furaha. 14 Hakika yeye alidhani hatarejea tena
(kwa Mwenyezi Mungu). 15 Ndiyo! Hakika Mola Wake
Mlezi alikuwa akimwona 16 Naapa kwa mwanga mwekundu
wa jua linapozama! 17 Na kwa usiku na unavyovikusanya!
18 Na kwa mwezi unapopevuka! 19 Bila shaka mtapitia hatua
baada ya hatua (kuumbwa, kuzaliwa,kufa, kufufuliwa…).
20 Wana nini hao hata wasiamini? 21 Na wanaposomewa
Qur’an hawasujudi? 22 Lakini waliokufuru wanakataa tu.
23 Na Mwenyezi Mungu anayajua zaidi wanayoyadhamiria.
24 Basi wape habari ya adhabu chungu! 25 Isipokuwa wale
ambao wameamini na wakafanya mema, hao wana malipo
yasiyokatika milele.

85. Sura Al-Buruj

# SURA YA KITITA CHA SAYARI, ZODIAKI

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 Naapa kwa mbingu yenye kitita cha Sayari kumi na mbili
(Zodiaki) zenye alama: (Upinde, Mshale, Ndoo, Kondoo,
Mashuke, Kaa, Simba, Mizani, Ng’e, Mapacha, Ng’ombe,
Samaki)! 2 Na kwa siku iliyoahidiwa! 3 Na kwa shahidi na
kinachoshuhudiwa! 4 Wemelaaniwa watu waliotengeneza
mahandaki, 5 Yenye moto wenye kuni nyingi, 6 Walipokuwa
wamekaa kando yake, 7 Na wao wakawa wanashuhudia yale
wanayowafanyia waumini. 8 Na hapana lililowachukiza
kwao ila tu ni kwa sababu wao walimwamini Mwenyezi
Mungu Mwenye nguvu, Mwenye kusifiwa. 9 Ambaye ni
Wake ufalme wa mbingu na ardhi, na Mwenyezi Mungu ni
shahidi wa kila kitu. 10 Hakika wale waliowafitini waumini
wanaume na waumini wanawake, kisha wasitubu, watakuwa
ndani ya moto wa Jahannam na watapata adhabu ya kuungua.
11 Hakika waliaomini na wakatenda mema watapata
bustani ambazo hupita mito chini yake. Huko ndiko kufuzu
kukubwa. 12 Hakika mkamato wa Mola Wako Mlezi ni wa
nguvu sana. 13 Hakika Yeye ndiye anayeanzisha (uumbaji)
na anayerejesha tena. 14 Na Yeye ni Mwingi wa maghufira
Mwenye mapenzi na upole. 15 Mtukufu, Mwenye Ufalme
wa Enzi. 16 Mwingi wa kutenda alipendalo. 17 Je imekufikia
habari ya majeshi, 18 Ya Firauni (Pharaoh) na Thamudi?
19 Lakini waliokufuru wanang’an’ania kukataa (ukweli).
20 Na Mwenyezi Mungu amewazunguka kwa nyuma yao.

21 Lakini hii ni Qur'an Tukufu, 22 Iko katika ubao
uliohifadhiwa

## 86. Sura At-Twariq

# SURA YA MGENI WA USIKU

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 Naapa kwa mbingu na kinachokuja usiku! 2 Nini
kitakujulisha wewe ni nini kinachokuja usiku? 3 Ni nyota
yenye mwanga mkali. 4 Hakuna nafsi yoyote ila inayo
mwangalizi. 5 Basi na atajita mwanadamu ameumbwa
kutokana na nini? 6 Ameumbwa kutokana na maji yatokayo
kwa kuruka, 7 Yatokayo baina ya uti wa mgongo na mifupa
ya kifua. 8 Hakika Yeye ni muweza wa kumrejesha (tena).
9 Siku zitakapofunuliwa siri. 10 Hatakuwa na madaraka
wala wa kumsaidia. 11 Naapa kwa mbingu yenye kurudi
(inapozunguka)! 12 Na kwa ardhi yenye mpasuko (kwa kutoa
maji, mimea/ au Bonde la Ufa)! 13 Hakika hii (Quran) ni
kauli yenye kupambanua (kheri na shari). 14 Wala si mzaha.
15 Hakika wao wanapanga njama, 16 Nami nazipindua njama
zao. 17 Basi wape muhula makafiri, wape muhula kidogo.

## 87. Sura Al-Aa'la

# SURA YA MTUKUFU ZAIDI

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema, Mwenye kurehemu.

1 Litukuze jina la Mola Wako Mlezi, Mtukufu zaidi.
2 Ambaye ameumba kisha akaweka uwiano. 3 Na ambaye
amepanga (sheria), na akaweka wazi mwongozo. 4 Na
ambaye ameotesha malisho, 5 Baadaye akayafanya visiki
vikavu. 6 Tutakusomesha hutusahau, 7 Ila akipendacho
Mwenyezi Mungu. Hakika Yeye anayajua yaliyo wazi na
yaliyofichika. 8 Tutakufanyia wepesi (kufuata) njia rahisi.
9 Basi wakumbushe, ikiwa kukumbusha kutafaa.
10 Ataonyeka mwenye kumchamungu. 11 Na atajiepusha
nayo mwovu. 12 Ambaye ataingia moto mkubwa. 13 Kisha
hatokufa humo wala hatakuwa hai. 14 Hakika amekwisha
faulu aliyejitakasa na dhambi. 15 Na akalitaja jina la Mola
Wake Mlezi, na akaswali. 16 Bali nyinyi mnapendelea zaidi
maisha ya duniani! 17 Na ilhali akhera ni bora na yenye
kubakia kuliko vingine. 18 Hakika haya yamo katika vitabu
vya mwanzo, 19 Vitabu vya Ibrahim (Abraham) na Musa
(Moses).

88. Sura Al-Ghashiya

# SURA YA TUKIO LIFUNIKALO MATUKIO YOTE

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 Je, imekujia habari ya tukio linalofunika yote (Kiyama)?
2 Nyuso siku hiyo zitajiinamia, 3 Taabani kwa kazi ngumu!
4 Zitaingia katika moto mkali. 5 Zitanyweshwa katika
chemchemi inayochemka. 6 Hawatakuwa na chakula
isipokuwa cha miiba. 7 Hakinenepeshi wala hakiondoi njaa.
8 Nyuso (nyingine) siku hiyo zitakuwa kunjufu. 9 Zitakuwa
radhi kwa jitihada zao. 10 Katika Bustani ya juu. 11 Hazitasikia
humo upuuzi. 12 Humo mna chemchemi inayotiririka.
13 Mna vitanda vilivyoinuliwa, 14 Na bilauri zilizoandaliwa
tayari, 15 Na mito ya kulalia iliyopangwa, 16 Na mazulia
yaliyotandikwa kila sehemu. 17 Je, hawamtazami ngamia
jinsi alivyoumbwa? 18 Na mbingu jinsi zilivyoinuliwa juu?
19 Na milima jinsi ilivyosimamishwa wima? 20 Na ardhi jinsi
ilivyotandazwa? 21 Basi waonye, hakika wewe ni mwonyaji
tu. 22 Wewe si dikteta juu yao. 23 Lakini anayegeuka nyuma
na akamkana Mwenyezi Mungu, 24 Mwenyezi Mungu
atamwadhibu huyo adhabu kubwa sana! 25 Hakika ni Kwetu
Sisi marejeo yao. 26 Kisha ni juu Yetu Sisi hesabu yao.

# SURA AL-FAJR

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

[1] Naapa kwa alfajiri! [2] Na Kwa nyusiku kumi (za mwezi
Dhul hijja)! [3] Na kwa mbili-mbili na moja-moja! [4] Na kwa
usiku unapopita! [5] Je, hicho si ni kiapo kwa Mwenye akili?
[6] Kwani hujui jinsi gani Mola Wako Mlezi aliwafanya A'd,
[7] Wa (mji wa) Iram wenye maguzo makubwa? [8] Ambayo
mfano wake haukujengwa katika miji yoyote? [9] Na Thamud
waliochonga majabali makubwa katika bonde? [10] Na Firauni
mwenye vigingi? [11] Ambao walifanya ujeuri katika miji?
[12] Wakaeneza uharibifu humo kwa wingi? [13] Basi Mola
Wako akawamiminia janga la adhabu za aina mbali mbali.
[14] Hakika Mola Wako Mlezi daima yuko kwenye doria
(akiwavizia). [15] Waama mwanadamu anapojaribiwa na
Mola wake Mlezi, akamkirimu na akampa neema, husema
(kwa maringo): 'Mola Wangu ameniheshimu!' [16] Na ama
anapomjaribu, akampunguzia riziki yake, husema (kwa
kulalamika): 'Ah! Mola Wangu amenifanya mnyonge!'
[17] La hasha! Bali nyinyi hamuwakirimu yatima, [18] Wala
hamuhimizani juu ya kuwalisha masikini; [19] Na mnakula
mali ya urithi kwa ulafi. [20] Na mnapenda utajiri kupita kiasi.
[21] La hasha! Pindi ardhi itakapopondwa pondwa ikawa
kama poda, [22] Na ikaja (amri) ya Mola Wako Mlezi na
malaika wakipanga safu kwa safu, [23] Na siku hiyo ikaletwa
Jahannam ikawa uso kwa uso. Siku hiyo mwanadamu
(ndipo) atakumbuka, lakini kutamfaa nini kukumbuka!

24 Atasema: laiti ningetanguliza (matendo mema) kwa ajili ya
uhai wangu (huu)! 25 Basi siku hiyo hataadhibu yeyote kama
alivyokuwa akifanya (duniani). 26 Wala hatafunga yeyote
kama alivyokuwa akifunga. 27 (Ndipo roho ya mtu mwema
itaambiwa): ‘Ewe nafsi iliyotua!’ 28 ‘Rejea kwa Mola Wako
Mlezi ukiwa umeridhika na umemridhisha’ 29 ‘Ingia katikati
ya waja Wangu’. 30 ‘Na ingia katika Pepo Yangu’.

## 90. Sura Al-Balad

# SURA YA MJI

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 Naapa kwa mji huu (Makka)! 2 Nawe ni mkazi huru
katika mji huu. 3 Na kwa mzazi na alichokizaa! 4 Hakika
tumemuumba mwanadamu katika shida na taabu. 5 Hivi
anadhani hapana yeyote atakayemuweza? 6 Anasema
(akisikitika): ‘Ah, nimepoteza pesa chungu nzima (kutoa
sadaka, Zaka)! 7 Hivi anadhani kuwa hapana yeyote
anayemwona? 8 Je, hatukumpa macho mawili? 9 Na ulimi
na midomo miwili? 10 Na tukamwonesha njia mbili? 11 Basi
mbona hakuiparamia njia nzito? 12 Nini kitakukujulisha
wewe ni ipi hiyo njia nzito? 13 Kumkomboa mtumwa
14 Au kumlisha siku ya njaa, 15 Yatima aliye na udugu, 16 Au
maskini hohe hahe. 17 Kisha awe miongoni mwa walioamini
na wakatenda mema, wakausiana kusubiri na wakausiana
kuhurumiana. 18 Hao ndio watu wa upande wa kulia. 19 Na
wale waliozikana ishara Zetu, hao ndio watu wa upande wa
kushoto. 20 Juu yao ni moto uliokomewa.

91. Sura As-Shams

# SURA YA JUA

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 Naapa kwa Jua na mwangaza wake! 2 Na kwa mwezi
unapoliandama! 3 Na kwa mchana unapolidhihirisha!
4 Na kwa usiku unapolifunika! 5 Na kwa mbingu na kwa
aliyezijenga! 6 Na kwa ardhi na aliyeitandaza! 7 Na kwa nafsi
na aliyeilinganisha! 8 Akaifahamisha mabaya na mema. 9
Hakika amefaulu aliyeitakasa (nafsi), 10 Na amepata hasara
aliyeifanya kuwa kitu duni. 11 Thamud walimkana (Mtume
wao) kutokana na jeuri yao. 12 Pale walipomteua mwovu
wao zaidi, 13 Hapo Mtume wa Mwenyezi Mungu (Swaleh)
akawaambia: ‘Msimguse ngamia wa Mwenyezi Mungu
na msimzuie na (fungu lake la) kunywa maji’ 14 Lakini
wakamwona mwongo na wakamkata miguu. Mola Wao
akaifunika ardhi juu yao na akaisawazisha, kwa sababu ya
dhambi zao. 15 Wala haogopi matokeo yake ya mwisho.

92. Sura Al-Layl

# SURA YA USIKU

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 Naapa kwa usiku unapofunika (mwangaza)! 2 Na kwa
mchana unapodhihiri (kwa utukufu wake)! 3 Na kwa
aliyeumba dume na jike! 4 Hakika (matokeo ya) jitihada

zenu ni tofauti. 5 Ama mwenye kutoa na akamcha Mwenyezi
Mungu, 6 Na akalisadiki lililo jema (imani ya Mwenyezi
Mungu), 7 Tutamfanyia wepesi (njia) ya Peponi 8 Na ama
mwenye kufanya ubakhili na akajiona anajitosheleza
kwa kila kitu, 9 Na akalikadhibisha lililo jema (imani),
10Basi tutamfanyia wepesi (njia) ya Motoni. 11 Na wala
utajiri wake hautamfaa kitu wakati anaporomoka kuingia
motoni. 12 Hakika ni juu Yetu kuongoza njia ya uongofu.
13 Na hakika ni Yetu Akhera na Dunia. 14 Basi ninawaonya
moto unaowaka! 15 Hatauingia isipokuwa muovu mno.
16 Ambaye amekadhibisha na kuupa mgongo (ukweli).
17 Na ataepushwa nao mchamungu. 18 Ambaye anatoa mali
yake kutaka kujitakasa (na dhambi). 19 Na siyo kwa kuwa
anatarajia kupata manufaa yoyote kutoka kwa yeyote. 20 Ila
tu ni kwa kutaka radhi ya Mola Wake Mlezi, aliye juu kabisa.
21 Na si muda mrefu ujao, atafurahi!

## 93. Sura Ad-Dhuha

## SURA YA MWANGAZA WA ASUBUHI

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 Naapa kwa mwangaza wa asubuhi! 2 Na kwa usiku
unapokuwa bado umetanda! 3 Mola wako hakukuacha, wala
kukukasirikia! 4 Na hakika Akhera ni bora kwako kuliko
Dunia. 5 Na muda mfupi hivi Mola Wako Mlezi atakupa, na
utaridhia. 6 Je, hakukukuta wewe yatima akakupa hifadhi?
7 Na akakukuta umepotea akakuongoza? 8 Na akakukuta
mhitaji akakutosheleza? 9 Basi mtoto yatima usimwonee!

10 Na ama anayeomba usimkaripie! 11 Na waama neema ya
Mola Wako Mlezi, isimulie.

## 94. Sura Al-Inshirah

## SURA YA KUKUNJULIWA KIFUA

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 Je, hatukukukunjulia kifua chako? 2 Na tukakuondolea
mzigo wako, 3 Ambao uliuelemeza mgongo wako? 4 Na
tukakunyanyulia juu jina lako? 5 Basi kwa hakika baada
ya dhiki kuna faraja. 6 Hakika baada ya dhiki kuna faraja.
7 Basi ukishamaliza (kuswali) jitaabishe. 8 Na kwa Mola
Wako Mlezi jipendekeze.

## 95. Sura At-Tin

## SURA YA TIN

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 Naapa kwa tini na zaituni! 2 Na kwa mlima Siniina!
3 Na kwa mji huu wenye amani! 4 Hakika tumemuumba
mwanadamu katika umbile zuri mno. 5 Kisha tutamrudisha
awe chini ya walio chini! 6 Isipokuwa wale walioamini na
wakatenda mema, wao wana ujira usio mwisho. 7 Basi ni
kipi baadaye kinachokufanya ukadhibishe (siku ya) malipo?
8 Kwani Mwenyezi Mungu si mwenye hekima zaidi ya
kuhukumu kuliko mahakimu wote?

## 96. Surat Al-Alaq

# SURA YA KIPANDE CHA DAMU KINING'INIZI

Kwa Jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

[1] Soma kwa jina la Mola Wako Mlezi aliyeumba.
[2] Amemuumba mwanadamu kwa tone linaloning'inia la damu
iliyoganda. [3] Soma! Na hali Mola wako Mlezi ni karimu
mno. [4] Ambaye amemfundisha mwanadamu kuandika kwa
kalamu. [5] Amemfundisha mwanadamu aliyokuwa hayajui.
[6] La hasha! Hakika mwanadamu hupituka mipaka. [7] Kwa
vile anajiona amejitosheleza. [8] Hakika marejeo ni kwa Mola
Wako Mlezi. [9] Je, umemwona yule anayemkataza. [10] Mja
anaposwali? [11] Je, unaonaje kama yuko juu ya uongofu?
[12] Au akiamrisha kumcha Mungu? [13] Je, unaonaje kama
yeye akikadhibisha na kurudi nyuma? [14] Hivi hajui kwamba
Mwenyezi Mungu anaona? [15] La hasha! Kama hatakoma,
tutamburuza kwa nywele za utosi! [16] Utosi mwongo wenye
makosa! [17] Basi na awaite watu wa baraza lake! [18] Nasi
tutawaita Malaika wa kuadhibu (amshughulikie)! [19] La
hasha! Usimtii! Sujudu na jikaribishe kwa Allah.

## 97. Sura Al-Qadr

# USIKU WA HESHIMA

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 Hakika Sisi tumeiteremsha Qur'an katika usiku wa heshima
(Laylatul Qadri). 2 Na nini kitakujulisha wewe ni nini usiku
wa heshima? 3 Usiku wa heshima ni bora kuliko miezi elfu.
4 Hushuka Malaika na Roho kwa idhini ya Mola wao Mlezi
katika usiku huo kwa ajili ya kila jambo. 5 Ni amani tupu
usiku huo mpaka mapambazuko ya alfajiri.

## 98. Sura Al-Bayyina

# SURA YA HOJA YA WAZI

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 Hawakuwa waliokufuru miongoni mwa Watu wa Kitabu na
mapagani wa Kiarabu waaachane na walivyozoea hadi iwajie
hoja: 2 Mtume atokaye kwa Mwenyezi Mungu awasomee
kurasa zilizotakaswa. 3 Ndani yake mna sheria zilizonyooka.
4 Wala hawakufarakana wale waliopewa Kitabu ila baada ya
kuwajia hoja. 5 Na wala hawakuamrishwa (jingine) isipokuwa
wamwabudu Mwenyezi Mungu kwa kumtakasia ibada Yeye
pekee, wawe wanyoofu katika imani, na wadumishe Swala,
na watoe Zaka. Na hiyo ndiyo Dini iliyonyooka. 6 Hakika
waliokufuru katika Watu wa Kitabu na wapagani wa Kiarabu
watakuwa katika Moto wa Jahannam wadumu milele humo.

Hao ndio viumbe waovu. 7 Hakika walioamini na wakatenda
mema hao ndio viumbe bora. 8 Malipo yao kwa Mola Wao
Mlezi ni Bustani za milele, ambazo hupita mito chini yake.
Wakae humo milele. Mwenyezi Mungu yuko radhi nao, na
wao wako radhi Naye. Hayo ni kwa anayemuogopa Mola
Wake Mlezi.

## 99. Sura Al-Zilzal

## SURA YATETEMEKO LA ARDHI

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 Hapo itakapotetemeshwa ardhi kutetemeshwa kwa
nguvu. 2 Na ardhi ikatoa mizigo yake (kutoka ndani). 3 Na
mwanadamu akauliza (kwa wasi wasi) ina nini hiyo? 4 Siku
hiyo (ardhi) itahadithia habari zake. 5 Kwa sababu Mola
Wako Mlezi ameimrisha kufanya hivyo. 6 Siku hiyo watu
watatoka (makaburini) wakiwa tayari wamejipanga makundi
makundi, ili wakaoneshwe matendo yao. 7 Basi anayefanya
hata chembe ya wema, atauona! 8 Na anayetenda hata chembe
ya uovu, atauona!

100. Sura Al-A’diyat

# SURA YA FARASI WATOKAO MBIO

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu

1 Naapa kwa farasi wanaokwenda mbio wakihema,
2 Wanaowasha moto kwa kwato zao, 3 Wanaoshambulia
wakati wa asubuhi, 4 Huku wakatifua vumbi wakati huo,
5 Wakaliingilia kati wakati huo kundi (la maadui).... 6 Hakika
mwanaamu ni mtovu mno wa shukrani kwa Mola Wake
Mlezi! 7 Na hakika yeye bila ya shaka analijua hilo. 8 Na
hakika yeye ana mapenzi makubwa ya utajiri! 9 Kwani hajui
watakapofufuliwa walio makaburini? 10 Na yakadhihirishwa
yaliyomo moyoni? 11 Hakika Mola Wao Mlezi (hata) siku
hiyo, ni mjuzi mno wa hali zao.

101. Sura Al-Qari’a

# SURA YA (SIKU YA) KELELE NA GHASIA/KIYAMA

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye urehemu.

1 Siku ya kelele na ghasia (siku ya Kiyama)! 2 Ni ipi siku
ya kelele na ghasia? 3 Na nini kitakujulisha nini siku ya
kelele na ghasia? 4 Siku ambayo watu watakuwa kama
panzi waliotawanyika 5 Na milima itakuwa kama sufi
zilizochambuliwa. 6 Ama ambaye mizani yake itakuwa nzito,
7 Huyo atakuwa katika maisha ya kuridhisha. 8 Waama yule

ambaye mizani yake itakuwa nyepesi, 9 Basi makazi yake
yatakuwa Hawiya! 10 Na nini kitachokujulisha nini hiyo?
11 Ni Moto mkali!

102. Sura At-Takathur

## SURA YA (WENYE) KULIMBIKIZA UTAJIRI

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 Kumewashughulisha nyinyi kushindana kwa utajiri! 2 Hadi
mwingie makaburini! 3 La hasha! Punde hivi mtajua! 4 Tena
la hasha! Punde hivi mtajua! 5 La hasha! Laiti mngejua ujuzi
wa yakini. 6 Hakika mtauona Moto! 7 Kisha, kwa kweli
mtauona kwa jicho la yakini. 8 Kisha hakika mtaulizwa siku
hiyo juu ya (matumizi ya) neema (mlizopewa).

103. Sura Al-A’sr

## SURA YA WAKATI KUPITIA ZAMA NA ZAMA

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 Naapa kwa zama! 2 Hakika mwanadamu yumo katika
hasara. 3 Ila wale walioamini, na wakatenda mema, Na
wakausiana kutenda haki, na wakausiana kusubiri.

## 104. Sura Al-Humaza

# SURA YA M-MBEA

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu

1 Ole wake! Kila mbea, msengenyaji! 2 Ambaye amekusanya
pesa na akawa anazihesabu-hesabu. 3 Anadhania kuwa
pesa zake zitamwezesha aishi milele! 4 La hasha! Huyo
atasukumiziwa ndani ya kile kinachovunja-vunja. 5 Ni nini
kitakujulisha wewe nini kinachovunja-vunja? 6 Ni Moto wa
Mwenyezi Mungu uliowashwa 7 Ambao unapanda nyoyoni.
8 Hakika huo utatiwa komeo kwa juu yao. 9 Kwenye maguzo
marefu.

## 105. Sura Al-Fil

# SURA YA (KISA CHA) NDOVU

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 Je, hukujua namna gani alivyowafanya Mola Wako Mlezi
wale wenye ndovu? 2 Je, hakuzifanya hila zao zikapotea
bure? 3 Na aliwapelekea ndege makundi makundi.
4 Wakawatupia mawe ya udongo mkavu. 5 Akawafanya kama
majani makavu yaliyoliwa na wadudu!

106. Sura Quraysh

## SURA YA WATU WA KABILA LA QURAYSH

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

[1] Kwa ajili ya kuzoea Maquraysh. [2] Kuzoea kwao msafara wa kusi na kaskazi. [3] Basi na wamwabudu Mola Mlezi wa Nyumba hii. [4] Ambaye amewalisha wasipate njaa, na akawasalimisha na hofu.

107. Sura Al-Mau'n

## SURA YA KUZUIA MSAADA

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu

[1] Je, unamjua akanushaye (siku ya) malipo? [2] Huyo ni ambaye humzuia yatima (na haki yake). [3] Wala hahimizi kumlisha maskini. [4] Ole wao wanaoswali! [5] Ambao wanapuuza Swala zao. [6] Na ambao wanaonesha watu (swala zao). [7] Na wanazuia msaada.

108. Sura Al-Kawthar

## SURA YA KHERI NYINGI

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 Hakika tumekupa wewe (Muhammad) kheri nyingi. 2 Basi swali na uchinje kwa ajili ya Mola Wako. 3 Hakika mwenye kukubughudhi wewe, yeye ndiye mwenye kutindikiwa (na kheri).

109. Sura Al-Kafirun

## SURA YA WANAMKANA MUNGU

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 Sema: Enyi makafiri nyie! 2 Siabudu mnachokiabudu. 3 Wala nyinyi si wenye kuabaudu ninachokiabudu. 4 Wala mimi si mwenye kuabudu mlichokiabudu. 5 Wala nyinyi si wenye kuabudu ninachokiabudu. 6 Mna dini yenu, nami nina dini yangu.

110. Sura An-Nasr

## SURA YA USHINDI

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 Hapo utakapofika msaada wa Mwenyezi Mungu na ushindi.
2 Na ukawaona watu wanaiingia katika dini ya Mwenyezi
Mungu makundi makundi. 3 Basi hapo mtakase Mola Wako
Mlezi kwa kumsifu na umtake msamaha. Hakika Yeye ni
Mwingi wa kukubali toba.

111. Sura Al-Masad

## SURA YA NDIFU

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 Imeangamia mikono ya Abu Lahab na yeye pia ameangamia.
2 Hautamfaa utajiri wake na vile alivyovikusanya. 3 Atauingia
moto wenye miali mikali. 4 Na mkewe (ataingia) hali akibeba
kuni. 5 Shingoni mwake mna kamba ya ndifu.

## 112. Sura Al-Ikhlas

# SURA YA UHALISIA WA IMANI

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 Sema: Yeye Mwenyezi Mungu ni mmoja pekee. 2 Mwenyezi
Mungu ndiye Mwenye kukusudiwa kwa haja zote. 3 Hakuzaa
wala hakuzaliwa. 4 Wala hana anayefanana naye hata mmoja.

## 113. Sura Al-Falaq

# SURA YA MAPAMBAZUKO

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 Sema: Najikinga kwa Mola wa mapambazuko. 2 Na shari
ya alivyoviumba. 3 Na shari ya giza la usiku uingiapo. 4 Na
shari ya wanawake wanaotabana katika mafundo. 5 Na shari
ya hasidi anapohusudu.

## 114. Sura An-Nas

# SURA YA WANADAMU

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.

1 Sema: Najikinga kwa Mola Mlezi wa watu, 2 Mfalme wa
watu, 3 Mungu wa watu, 4 Na shari ya mwenye kutia wasiwasi
na kuondoka, 5 Anayetia wasiwasi katika nyoyo za watu, 6
Miongoni mwa majini na watu.

## REFERENCES

# VITABU VYA MAREJEO

1. The Holy Qur'an Translation and Commentary by A. Yusuf Ali

2. ur-ani Tukufu kwa Lugha ya Kiswahili- Taasisi ya Daarus-salaam

3. Al-Muntakhab- Sheikh Ali Muhsin Al- Barwani

4. Tarjuma ya Tafsir al Kashif- Sheikh Hasan Mwalupa

5. The Holy Qur'an: The Final Testament by S.V. Mi Ahmed Ali

6. The Qr'an by M.H. Shakir: Tahrike Tarsile Qur'an, Inc.

7. The Koran by Mohammed Ahmed- Emere, London.

8. Tafsir al-Tabari online

9. Tafsir Ibn Katheer online

10. Tafsir al Jalalayn online

11. Tafsir al Sha'rawi online